

تَفْسِيرُ الْقُرْآنِ الْعَظِيمِ

للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

Juzuu ya Kumi

Al-Taghabun mpaka An-Nas

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

IBN HAZM MEDIA CENTER
Dar es Salaam, Tanzania

تفسير القرآن العظيم
للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

© Ibn Hazm Media Centre.

Chapa ya Kwanza 2021.

Msimamizi Mkuu wa Mradi:
Yassir Salim Awadh Masoud

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

Kimehaririwa na:
Wanazuoni wa Kiislamu

Usanifu Kurasa:
Ally Said Abdallah
Ibn Hazm Media Center
P.O. Box 22197,
Dar es Salaam
Tanzania.

Kimechapwa:
 Alhuda Publications, New Delhi, India.

Haki Zote Zimehifadhiwa.

Yaliyomo:

Tafsiri ya Suratu At-Taghabun	1
Kumtukuza Allah تعالی na Kutaja Viumbe Vyake na Elimu.....	2
Onyo Lililotolewa Kupitia Kutajwa Hatima ya Mataifa Yaliyokufuru.....	4
Maisha baada ya kufa ni kweli.	7
Siku ya At-Taghabun.....	8
Yote yawapatayo binadamu ni kwa Ridhaa ya Allah تعالی.....	10
Amri ya kumtii Allah تعالی na Mjumbe Wake	11
Tawhiid.....	12
Indhari dhidi ya Fitnah ya Wake na Watoto.....	14
Amri ya Taqwa kwa kadri ya uwezo wa mtu.....	16
Kushajiisha Sadaka.....	17
Tafsiri ya Suratu At-Talaq	19
Kuna kipindi ambacho wanawake waliotalakiwa hubaki Majumbani.....	20
Matumizi na Malazi ni Juu ya Mume katika Kipindi cha Eda.....	23
Hekima ya Kukaa Eda Katika Nyumba ya Mume.....	24
Mwanamke Mwenye Talaka yake Isiyo rejea hana Haki ya Matumizi.....	24
Amri ya Kumtendea Wema Mwanamke Aliyeachwa	27
Amri ya Kuwa na Mashahidi Wakati wa Kurejea.....	27
Allah تعالی Huwaruzuku na kuwapa Mafanikio Thabiti Wanaomcha Yeye.....	28
Eda ya Waliokoma Hedhi na Wale Wasiopata Siku Zao.....	31
Eda ya Mwanamke Mjamzito.....	32
Mwanamke aliye katika Eda ya Talaka Rejea Atahudumiwa.....	36
Imeharamishwa Kuwatendea Vibaya Wanawake Walioachwa.....	36
Mwanamke Mjamzito Aliyeachwa Talaka Isiyo ya Rejea ana Haki.....	37
Mwanamke Aliyeachwa Anaweza Kuchukua Ujira wa Kunyonyesha.....	37
Kisa cha Mwanamke Mchamungu.....	39
Adhabu kwa Kuvunja Amri za Allah تعالی.....	40
Sifa za Mtume.....	42
Ubainifu wa Uwezo Timilifu wa Allah تعالی	43
Tafsiri Suratu At-Tahrim	45
Allah تعالی Anamkosoa Mtume wake.....	46
Kuifundisha Familia Dini na Tabia Njema.....	57
Kuni za Motoni na Sifa za Malaika Wake.....	58

Hakuna Udhuru Utakaokubaliwa Kutoka kwa Wasioamini Siku ya Kiama.....	59
Kushajiisha Toba ya Kweli	59
Amri ya Jihad dhidi ya Makafiri na Wanafiki.....	61
Makafiri Hawatofaidika na Mahusiano ya Kiudugu.....	61
Makafiri Hawawezi Kuwadhuru Waumini.....	63
Tafsiri ya <i>Suratul Mulk</i>.....	67
Fadhila za <i>Suratul Mulk</i>	67
Kumtukuza Allah تعالى na Kubainisha Kuumbwa kwa mauti.....	70
Wasifu wa Moto wa Jahannam na Watakaoingia humo.....	75
Malipo ya Wenye Kumuogopa Mola Asiyekana.....	78
Miongoni mwa Neema za Allah تعالى kwa Waja wake.....	79
Vipi Mtasalimika na Adhabu ya Allah تعالى	81
Ndege Warukao ni kwa Uwezo wa Allah تعالى	83
Hapana Atakayewasaidia Kukupeni Riziki Ispokuwa Allah تعالى	85
Mfano wa Kafiri na Muumini.....	86
Uweza wa Allah تعالى Katika Kuumba	87
Mauti ya Muumini Hayatomuokoa Kafiri.....	90
Allah تعالى Anawakumbusha Neema Zake na Kuwaletea Maji.....	91
Tafsiri ya <i>Suratu Nuun</i>.....	93
Maelezo ya Kalamu.....	94
Kuapa kwa Kalamu Kunaonesha Ukuu wa Mtume.....	95
Maelezo ya Kauli.....	96
Katazo la Kuridhia Shinikizo la Makafiri.....	100
Mfano wa Kuondolewa kipato cha Makafiri.....	108
Malipo kwa Wacha-Mungu na Muamala Wao.....	112
Vitisho vya Siku ya Kiyama.....	115
Karipio Kali kwa Anayepinga Qur'an.....	116
Amri ya kuwa na Subra na Kuacha kufanya pupa.....	118
Athari za Kijicho ni kweli.....	121
Tuhuma za Makafiri na Jibu Lao.....	127
Tafsiri ya <i>Surat Al-Haqqah</i>.....	129
Onyo Kuhusu Ukubwa wa Siku ya Kiyama.....	130
Utajo wa Kuangamizwa kwa Mataifa	131
Ukumbusho Juu ya Neema za Safina.....	135
Kutajwa kwa Vitisho vya Siku ya Kiyama.....	137

Wanadamu Wakiwasilishwa Mbele ya Allah تعالى	139
Furaha ya Mtu Atakayepokea Kitabu Chake kwa Mkono wa Kulia.....	141
Hali Mbaya kwa Atayepewa Kitabu Chake kwa Mkono wa Kushoto.....	145
Qur'an ni Maneno ya Allah تعالى	148
Endapo Mtume Angemzulia Allah تعالى Angeadhibiwa.....	151
Tafsiri ya Surat Al-Maarij.....	155
Ombi la Kutaka Kiyama Kitokee Haraka.....	156
Tafsiri ya "Mola wa Njia za Daraja".....	157
Maana ya "Siku ya Kipimo ambayo Kipimo Chake ni Miaka Elfu Hamsini.....	158
Masimulizi Tofauti ya Hadithi.....	161
Mtume Aaswa Kuvumilia.....	162
Vitisho vya Siku ya Kiyama.....	164
Binadamu Hana Subira.....	169
Kuwatoa Wenye Kusali Sifa Zilizotangulia.....	170
Makaripio na Vitisho vya Makafiri.....	175
Tafsiri ya Surat Nuh عليه السلام	183
Wito wa Nuh عليه السلام kwa Watu Wake.....	184
Malalamiko ya Nuh عليه السلام na Vitimbi vya Watu Wake.....	186
Nuh عليه السلام Anamshitakia Mola Wake Kutokana na Majibu.....	192
Kilichoyasibu Masanamu ya Watu wa Nuh عليه السلام na Matokeo Yake.....	193
Maapizo ya Nuh عليه السلام kwa Watu Wake, na Kuwaombea Waliomuamini.....	195
Tafsiri ya Surat Al-Jinn.....	199
Majini Kusikiliza Qur'an na Kuamini Kwao.....	200
Majini Yanakiri Kwamba Hana Mke Wala Watoto.....	201
Sababu za Majini Kuasi ni Kutokana na Wanadamu Kutaka Kulingwa.....	203
Uibaji wa Majini Habari za Mbinguni Kabla ya Kutumwa Mtume.....	205
Aina za Majini, Kuna Waumini na Makafiri	209
Majini Wanakubali Uwepo wa Kudura ya Allah تعالى Timilifu.....	210
Amri ya Kumuabudu Allah تعالى na Kujiepusha na Ushirikina.....	214
Msongamano wa Majini Katika Kusikiliza Qur'an.....	215
Mtume Hamiliki Madhara Wala Uongofu.....	217
Wajibu wa Mtume ni Ujumbe	218
Mtume Hajui Wakati wa Kutokea Kiama.....	219
Tafsiri ya Surat Muzzammil.....	225
Amri ya Kusimama Usiku.....	227

Njia ya Kusoma Qur'ani.....	228
Utukufu wa Qur'ani.....	230
Utukufu wa Kisimamo cha Usiku.....	231
Amri ya Kusubiri Maudhi ya Makafiri na Kubainishwa Adhabu Yao.....	238
Mtume Wenu ni Kama Mtume Musa عليه السلام kwa Firauni.....	239
Uhofishaji wa Adhabu ya Siku ya Kiama.....	240
Kuondosha Wajibu wa Kusimama Usiku na Kutaja Nyudhuru Zake.....	243
Amri ya Kutoa Sadaka na Kufanya Kheri.....	246
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Mudathir</i>.....	249
Aya za Mwanzo Kushuka Baada ya <i>Iqraa</i>	250
Ukumbusho wa Siku ya Kiyama.....	254
Karipio la Anayesema Qur'an Kuwa ni Uchawi.....	258
Idadi ya Walinzi wa Motoni na Waliyoyasema Makafiri.....	265
Hakuna Anayejua Idadi ya Askari wa Mwenyezi Mungu.....	267
Mjadala Uliopo kati ya Watu Peponi na Watu wa Motoni.....	270
Upuuzi wa Makafiri na Msimamo Wao.....	272
Qur'an ni Ukumbusho.....	274
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Qiyaamah</i>.....	275
Kiapo kwa Watu Kufufuliwa Tena Siku ya Kiyama.....	276
Matendo ya Mtu Yatahudhurishwa Mbele Yake.....	281
Vipi Mtume Alivyokuwa Anapokea Wahyi.....	284
Sababu ya Kukadhibisha Siku ya Kiyama.....	286
Kumuona Allah تعالى.....	286
Nyuso za Watu Waovu Zitakuwa Nyeusi Siku ya Kiyama.....	289
Yakini Itapatikana Wakati wa Kujiwa na Mauti.....	292
Kutajwa kwa Hali ya Mkadhibishaji.....	295
Mwanadamu Hataachwa Hivi hivi tu.....	297
Dua Wakati wa Kuimaliza Sura hii.....	299
Tafsiri ya <i>Suratul Insaan</i>.....	301
Kusomwa kwa <i>Surat Al-Ssajidah</i> na <i>Surat Al-Insaan</i>	301
Allah تعالى Kamuumba Mwanadamu Baada ya Kuwa Hakuwepo.....	303
Mwenyezi Mungu Amemuongoza Mwanadamu Njia.....	304
Malipo ya Makafiri na Watu Wema.....	306
Matendo ya Watu Wema.....	307
Baadhi ya Ufafanuzi wa Malipo ya Watu Wema.....	311

Kutaja Viti vya Enzi.....	314
Kukaribia Vivuli na Matunda.....	315
Vyombo vya Fedha na Bilauri.....	316
Kinywaji cha Tangawizi na Salsabiil.....	317
Vijana na Watumishi.....	318
Mavazi na Mapambo.....	319
Utajo wa Kushushwa Qur'an na Amri ya Kusubiri na Kuleta Dhikri.....	322
Kukosolewa Katika Kupenda Dunia.....	323
Qur'an ni Ukumbusho na Uongofu kwa Tawfiq ya Allah تعالی.....	324
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Mursalaat</i>.....	327
Kushuka kwa Sura Hii na Kusomwa Kwake Katika Sala ya Magharibi.....	327
Allah تعالی Kuapia Juu ya Viumbe Vyake Mbalimbali.....	329
Kutajwa baadhi Yatakatotokea Siku ya Kiama.....	331
Wito wa Kuzingatia Aina Mbalimbali za Qudura.....	335
Waovu Watapelekwa Kwenye Makazi Yao.....	339
Waovu Kushindwa Kusema, Kutoa Udhuru.....	340
Marejeo ya Wachamungu	343
Kutishwa Mwenye Kukanusha Kiyama.....	343
Tafsiri ya <i>Suratu An-Naba'</i>.....	347
Kubainishwa kwa Washirikina Wanaopinga Uwepo wa Kiyama.....	348
Kutaja Mambo Katika Uweza wa Allah تعالی	349
Kuelezea Siku ya Hukumu na Ufafanuzi wa Yaliyomo Ndani Yake.....	355
Kufuzu Kukubwa ni kwa Wenye Kumcha Mwenyezi Mungu.....	361
Hatohubutu Mtu Yeyote Kusema Mbele ya Mwenyezi Mungu.....	364
Kiyama Kiko Karibu	366
Tafsiri ya <i>Suratu An-Naziat</i>.....	369
Kuapiwa Sifa Tano Juu ya Uwepo wa Siku ya Kiyama.....	370
Maelezo ya Kiyama na Sifa za Watu wake.....	371
Kutajwa kwa Kisa cha Mussa عليه السلام.....	376
Kuumbwa kwa Mbingu na Ardhi ni Kugumu.....	381
Siku ya Kiyama na Yaliyomo Ndani Yake	384
Tafsiri ya <i>Suratu Abasa</i>	389
Kukosolewa Mtume kwa Kumkunja Uso Mtu Mnyonge.....	390
Sifa za Qur'an	392
Jibu kwa Anayekanusha Uwepo wa Maisha Mengine.....	395

Kuotesha Tembe za Vyakula na Nyenginezo.....	398
Siku ya Kiyama na Watu Kukimbia Jamaa Zao.....	402
Nyuso za Watu wa Peponi na za Watu wa Motoni.....	404
Tafsiri ya <i>Suratu At-Takwir</i>.....	407
Yatakayotuka Siku ya Kiyama.....	409
Kuporomoka kwa Nyota	410
Kuondoshwa kwa Kuachwa Ngamia Wenye Mimba.....	411
Kuwashwa kwa Bahari	412
Kuchanganywa Nafsi	413
Kuulizwa Mtoto Mwanamke Aliyezikwa Hali Yu Hai.....	414
Kafara ya Kuwazika Mabinti na Hali Wakiwa Hai.....	415
Kufunuliwa kwa Madaftari ya Matendo.....	416
Kuondolewa Mbingu, Kuwashwa Moto na Kusogezwa Pepo.....	416
Kila Mmoja Anajua Siku ya Kiyama.....	416
Tafsiri ya <i>Al-Khunnasi</i> na <i>Al-Kunnasi</i>	418
Qur'an Ameshuka Nayo Jibril عليه السلام	421
Hakuwa Mtume ni Bakhili Katika Kuufikisha Wahy.....	423
Qur'an ni Ukumbusho wa Walimwengu.....	424
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Infitwaar</i>.....	427
Ubora wa <i>Suratu Al-Infitwaar</i>	427
Mambo Yatakayotuka Siku ya Kiyama.....	429
Hatutakikani Kwa Mwanadamu Kumsahau Mwenyezi Mungu.....	430
Sababu ya Mtu Kuhadaika	433
Malipo ya Watu Wema na Waovu.....	434
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Mutwafifiin</i>.....	437
Kuongeza na Kupunguza Katika Kupima.....	438
Kuhofishwa Wapunguzaji Vipimo.....	439
Kumbukumbu za Watu Waovu.....	442
Kitabu cha Kumbukumbu cha Watu Wema.....	449
Uovu wa Wakosefu na Kuwacheza Shere Kwao Waumini.....	453
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Inshiqaq</i>.....	455
Kuna Sijda ya Kisomo katika <i>Surat Al-Inshiqaq</i>	455
Kupasuka kwa Mbingu na Kutanuliwa Ardhi Siku ya Qiyama.....	457
Malipo ya Matendo ni Kweli.....	458
Kuoneshwa na Majadiliano katika Siku ya Hesabu.....	459

Kiapo Juu ya Kupanda Binadamu Kutoka Hali Moja hadi Nyingine.....	462
Ubashiri wa Adhabu kwa Makafiri na Kutokuamini Kwao.....	465
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Buruji</i>.....	468
Tafsiri ya Siku Yenye Kuahidiwa na Shahidi.....	469
Dhulma ya Watu wa Mahandaki dhidi ya Waislamu.....	470
Malipo ya Watu wa Mahandaki.....	477
Malipo ya Watu Wema na Mateso Makali kwa Makafiri.....	479
Tafsiri ya <i>Suratu At-Tariq</i>.....	483
Ubora wa <i>Surat At-Tariq</i>	483
Kiapo Juu ya Kuwa Mwanadamu ni Mwenye Kuzungukwa.....	485
Namna ya Kuumbwa Mwanadamu ni Dalili	486
Siku ya Qiyama Hatakuwa Binadamu na Uwezo Wala Nusra.....	487
Kiapo Juu ya Kuwa Qur'an ni Ukweli na Kufeli kwa Wapinzani Wake.....	489
Tafsiri ya <i>Suratu Al-A'la</i>.....	491
Ubora wa <i>Surat Al-A'la</i>	491
Amri ya Kusabbihi na Majibu Yake.....	494
Kuumba, Kukadiria na Kuotesha Mimea.....	495
Mtume Hasahau Wahy ila Atakapotaka Allah <small>تعالى</small>	496
Amri ya Kukumbusha.....	497
Ubainifu wa Watu wa Mafanikio.....	500
Dunia Haina Thamani kwa Kulinganisha na Akhera.....	501
Vitabu vya Ibrahim <small>عليه السلام</small> na Musa <small>عليه السلام</small>	501
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Ghashiyah</i>.....	505
Kusomwa kwa <i>Surat Al'Aala</i> na <i>Al Ghashiya</i> katika Sala ya Ijumaa.....	505
Qiyama na Hali ya Watu wa Motoni Itakavyokuwa.....	507
Hali ya Watu wa Peponi Siku ya Qiyama.....	509
Mahimizo Juu ya Kuchunguza Kuumbwa kwa Ngamia, Mbingu.....	512
Kisa cha Dwimam Bin Thaalaba.....	513
Kazi ya Mtume ni Kufikisha Ujumbe.....	515
Makemeo kwa Mwenye Kuipa Mgongo Haki.....	516
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Fajr</i>.....	519
Kusomwa Suratul Fajri katika Swala.....	519
Tafsiri ya Sura ya <i>Al-Fajr</i> na Yaliyo Baada Yake.....	521
Tafsiri ya <i>Suratu Allayl (Usiku)</i>.....	522
Kutajwa Kuangamizwa kwa Aadi.....	523

Kutajwa kwa Firauni.....	527
Bwana Yumo Katika Uangalizi.....	528
Utajiri na Ufakiri ni Majaribio na Wala si Kutukuzwa.....	529
Miongoni mwa Maovu Ayafanyayo Mja katika Mali.....	529
Siku ya Qiyama Atalipwa Kila Mtu kwa Yale Aliyoyatenda.....	532
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Balad</i>.....	537
Kiapo kwa Utukufu wa Makkah Juu ya Kuumbwa	538
Mwanadamu Amezungukwa na Allah <small>تعالى</small> na Neema Zake.....	541
Kupambanua Kati ya Kheri na Shari ni Neema.....	542
Kuhimiza Juu ya Kuifuata Njia ya Kheri.....	544
Watu wa Upande wa Kushoto na Malipo Yao.....	548
Tafsiri ya <i>Suratu Ash-Shams</i>.....	551
Kusomwa kwa <i>Washamsi</i> katika Swala ya Isha.....	551
Kuapa kwa Mwenyezi Mungu kwa Viumbe Vyake Juu ya Kufuzu.....	553
Kukadhibisha kwa Thamud na Kuangamiizwa Kwao.....	560
Kisa cha Ngamia wa Swaleh.....	561
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Layl</i>.....	563
Kiapo Juu ya Kutofautiana kwa Watu Katika Juhudi Zao.....	565
Uongofu na Mambo Mengine Vimo Mikononi Mwa Allah <small>تعالى</small>	571
Sababu ya Kushuka Aya Hizi na Ubora wa Abubakar.....	574
Tafsiri ya <i>Suratu Adh-Dhuha</i>.....	577
Sababu ya Kushuka <i>Surat Adh-Dhuha</i>	578
Akhera ni Bora Kuliko Dunia.....	580
Neema Nyingi za Akhera Zinamngojea Mtume <small>ﷺ</small>	581
Kutaja Baadhi ya Neema za Allah <small>تعالى</small> Juu ya Mtume.....	581
Vipi Tutazitukuza Neema Hizi.....	583
Tafsiri ya <i>Suratu Ash-Sharh</i>.....	585
Maana ya Kukunjuliwa Kifua.....	586
Kubainisha Neema za Allah <small>تعالى</small> Juu ya Mtume Wake.....	586
Maana Kunyanyuliwa Utajo wa Mtume <small>ﷺ</small>	587
Wepesi Baada ya Uzito.....	587
Amri ya Kuleta Dhikri Ikipatikana Faragha.....	587
Tafsiri ya <i>Suratu At-Tin</i>.....	589
Tafsiri ya <i>Attini</i> na Yaliyo Baada Yake.....	591
Kusomwa kwa Surat Wattini Katika Sala Ndani ya Safari.....	589

Kuanguka kwa Mwanadamu Chini Zaidi ya Aliye Chini.....	592
Tafsiri ya <i>Suratu Al-'Alaq</i>.....	595
Ndiyo Kitu cha Kwanza Kushuka katika Qur'an.....	595
Kuanza kwa Utume wa Muhammad ﷺ.....	596
Utukufu wa Mwanadamu na Ubora Wake ni kwa Elimu.....	598
Makamio Juu ya Kuvuka Mipaka kwa Mwanadamu.....	600
Kumsema Vibaya Abu-Jahal na Makamio kwa Kumpatiliza.....	600
Kufundishwa kwa Mtume ﷺ.....	603
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Qadr</i>.....	605
Ubora wa Usiku wa Cheo.....	606
Kushuka kwa Malaika na Kuhukumiwa Kila Jambo la Kheri.....	607
Kuuainisha Usiku wa Cheo na Alama Zake.....	609
Maombi ya Usiku wa Cheo.....	613
Tafsiri ya <i>Suratu Lam Yakun (Al-Bayyinah)</i>.....	615
Mtume ﷺ Kumsomea Sura hii Ubayy.....	615
Kutaja Hali ya Makafiri Miongoni Mwa Watu wa Kitabu.....	617
Kulitokea Kotofautiana Baada ya Kuja Elimu.....	618
Lengo la Amri ya Allah تعالى ni Kumtakasia Dini.....	619
Kutajwa Viumbe Waovu na Wema Pamoja na Malipo Yao.....	621
Tafsiri ya <i>Suratu Idha Zulzilati</i>.....	625
Ubora wa <i>Surat Az-Zalzalah</i>	625
Siku ya Qiyama na Mambo Yatakayokuwa Ndani Yake.....	628
Malipo ya Kila Chembe katika Matendo.....	631
Tafsiri ya <i>Suratu Al-'Adiyat</i>.....	635
Kuapiwa Farasi wa Vita Juu ya Ukanushi wa Mwanadamu.....	636
Kukhofisha Kutokana na Siku ya Qiyama.....	638
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Qari'a</i>.....	641
Tafsiri ya <i>Suratu At-Takathur</i>.....	647
Matokeo ya Kuipenda Dunia ni Kughafilika na Akhera.....	648
Karipio la Kuuona Moto na Kuulizwa Juu ya Neema.....	650
Tafsiri ya <i>Suratu Al-'Asr</i>.....	655
Kujua kwa Amri bin Al-Aswi Muujiza wa Qur'ani.....	655
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Humazah</i>.....	659
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Fil</i>.....	663
Kisa cha Watu wa Ndovu kwa Ufupi.....	664

Tafsiri ya <i>Suratu Quraysh</i>	675
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Ma'un</i>	679
Sifa za Wenye Kukanusha Qiyama.....	680
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Kawthar</i>	685
Adui wa Mtume Ndiye Mwenye Kukatikiwa na Kheri Zote.....	689
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Kafirun</i>	691
Kuepukana na Shiriki.....	693
Tafsiri ya <i>Suratu An-Nasr</i>	697
Ubora wa <i>Surat An-Nasr</i>	697
Sura Hii Inaelezea Ukomo wa Muda wa Mjumbe.....	698
Tafsiri ya <i>Suratu Tabbat</i>	703
Sababu ya Kushuka Sura na Upingaji wa Abu Lahb kwa Mtume.....	703
Kutajwa kwa Hatima ya Ummu Jamil Mke wa Abu Lahb.....	706
Kisa cha Maudhi ya Mke wa Abu Lahab kwa Mtume 鸚.....	707
Tafsiri ya <i>Suratu Al-Ikhlās</i>	709
Kutajwa Sababu ya Kushuka Kwake na Ubora Wake.....	709
Hadithi Nyingine katika Ubora Wake.....	710
Hadithi Kuwa Sura Hii Inalingana na Thuluthi ya Qur'ani.....	711
Hadithi Nyingine katika Kukariri Kusoma Kwake	713
Hadithi Nyingine Katika Maombi Ambayo Imekusanya Sura hii.....	713
Hadithi Nyingine Katika Kutaka Kuponya kwa Sura Tatu.....	714
Allah تعالیٰ Ametakasika na Ubaba, Utoto, Uswahiba.....	716
Tafsiri ya Sura Mbili <i>Al-Mu'awwidhatayn</i>	721
Msimamo wa Ibni Masu'di Kuhusu <i>Al-Muawwi dhatayni</i>	721
Ubora wa <i>Al-Muawwidhatayn</i>	721
Kuweka Wazi Kurogwa kwa Mtume 鸚.....	727

Tafsiri ya Suratu Taghabun

Sura ya 64

Iliteremshwa Madinah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ
 الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ۝ هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ
 فَمِنْكُمْ كَافِرٌ وَمِنْكُمْ مُؤْمِنٌ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ۝
 خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ صُوَرَكُمْ
 وَإِلَيْهِ الْمَصِيرُ ۝ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَيَعْلَمُ
 مَا تُسَبِّرُونَ وَمَا تُعْلِنُونَ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِدَاتِ الصُّدُورِ ۝ أَلَمْ
 يَأْتِكُمْ نَبُؤُا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلُ فَدَاقُوا وَبَالَ أَمْرِهِمْ وَهُمْ
 عَدَابٌ أَلِيمٌ ۝ ذَلِكَ بِأَنَّهُ كَانَتْ تَأْتِيهِمْ رُسُلُهُمْ
 بِالْبَيِّنَاتِ فَقَالُوا أَبَشَرٌ يَجْعَدُونَ فَكَفَرُوا وَتَوَلَّوْا ۗ وَاسْتَغْنَى اللَّهُ
 وَاللَّهُ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ۝

يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي
 الْأَرْضِ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ
 عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ۝ هُوَ الَّذِي
 خَلَقَكُمْ فَمِنْكُمْ كَافِرٌ وَمِنْكُمْ مُؤْمِنٌ
 ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ۝ خَلَقَ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ وَصَوَّرَكُمْ
 فَأَحْسَنَ صُوَرَكُمْ ۗ وَإِلَيْهِ الْمَصِيرُ ۝
 يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
 وَيَعْلَمُ مَا تُسَبِّرُونَ وَمَا تُعْلِنُونَ ۗ وَاللَّهُ
 عَلِيمٌ بِدَاتِ الصُّدُورِ ۝

"1. Kinamtakasa Mwenyezi

Mungu kila kilichomo katika mbingu na katika ardhi. Ufalme ni Wake, na Sifa Njema ni Zake. Na Yeye ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.

2. Yeye Ndiye Aliyekuumbeni. Miongoni mwenu yupo aliye kafiri, na yupo aliye Muumini. Na Mwenyezi Mungu Anayaona mnayo yatenda.

3. Ameziumba mbingu na ardhi kwa haki, na Akakupeni sura, na Akazifanya nzuri sura zenu. Na marudio ni Kwake.

4. Anajua viliomo katika mbingu na ardhi, na Anajua mnayoyaficha na mnayoyatangaza. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliomo vifuani.”

Kumtukuza Allah تعالیٰ, Kutaja Viumbe Vyake na Elimu.

Hii ni Surah ya mwisho katika *Al-Musabbihat*. Tulishataja kabla ya kuwa viumbe wote wanamtukuza Allah تعالیٰ, Muumba wao na Mmiliki. Allah تعالیٰ Amesema,

لَهُ الْمَلِكُ وَهُوَ الْحَمْدُ

Ufalme ni Wake, na Sifa Njema ni Zake.

Maana yake: Yeye Ndiye Pekee Anayewadhibiti viumbe wote, Mmoja Anayetukuzwa na vyote Alivyoviumba na Kuvitungia sheria. Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Na Yeye ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu”.

Maana yake: Lolote Alitakalo hutokea bila kipingamizi, na Asilolitaka, halitokei kamwe. Allah تعالیٰ Amesema,

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ فَمِنْكُمْ كَافِرٌ وَمِنْكُمْ مُّؤْمِنٌ

“Yeye Ndiye Aliyekuumbeni. Miongoni mwenu yupo aliye kafiri, na yupo aliye Muumini. (64:2)

Muradi Wake, Allah تعالیٰ Alikuumbeni mkiwa na sifa hizi bainifu na Alikutakieni hayo. Kwa hiyo, watakuwepo waumini na makafiri. Allah تعالیٰ Ndiye Pekee Awaonaye wanaostahili muongozo na wanaostahili upotofu. Yeye ni Shahidi wa matendo ya waja wake na bila shaka Atawalipa. Kwa sababu hiyo Allah تعالیٰ Amesema:

وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٦٤﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyatenda”. (64:2)

Allah تعالیٰ Amesema,

خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ

“Ameziumba mbingu na ardhi kwa haki”.

Kwa ulinganifu na hekima,

وَصَوِّرْكُمْ فَأَحْسَنَ صُورَتِكُمْ ط

“Na Akakupeni sura, na Akazifanya nzuri sura zenu”.

Alikuumbeni katika sura nzuri na maumbile mazuri. Allah تعالى Amesema,

يَتَأْتِيَا الْإِنْسَانَ مَا غَرَّكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيمِ ﴿٦٤﴾ الَّذِي خَلَقَكَ فَسَوَّاكَ فَعَدَلَكَ ﴿٦٣﴾ فِي
أَيِّ صُورَةٍ مَا شَاءَ رَكَّبَكَ ﴿٦٤﴾

“Ewe mwanaadamu! Nini kilicho kughuri ukamuacha Mola wako Mlezi Mtukufu? Aliyekuumba, Akakuweka sawa, Akakunyoosha, Katika sura yoyote Aliyoipenda Akakujenga.” (82:6-8)

Na Kauli Yake,

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ قَرَارًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ صُورَتَكُمْ
وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ ؕ ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ ط فَتَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٤﴾

“Ni Mwenyezi Mungu Aliyekufanyieni ardhi kuwa ni pahala pa kukaa, na mbingu kuwa dari. Na Akakutieni sura, na Akazifanya nzuri sura zenu, na Akakuruzukuni vitu vizuri. Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Basi Ametukuka Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.” (40:64),

Na Kauli Yake,

وَالِيهِ الْمَصِيرُ ﴿٦٤﴾

“...Na marudio ni Kwake...” (64:3)

Maana yake: Marejeo na makazi ya mwisho. Kisha Allah تعالى Awafahamishe juu ya Kufahamu Kwake vyote vilivyopo mbinguni na duniani na nyoyoni.

Amesema:

يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَيَعْلَمُ مَا تُسْتُرُونَ وَمَا تَعْلَمُونَ ؕ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ
﴿٦٤﴾ أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَبُؤُا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلُ فَدَاقُوا وَنَالَ أَمْرِهِمْ وَهُمْ عَدَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٤﴾

﴿ أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَبُؤُا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلُ فَدَاقُوا وَبَالَ أَمْرِهِمْ وَهُمْ عَدَابُ أَلِيمٌ ﴾
 ذَٰلِكَ بِأَنَّهُ كَانَتْ تَأْتِيهِمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَعَالُوا أَكْثَرُٰ مُجْرِمِينَ فَكَفَرُوا وَتَوَلَّوْا ۗ وَأَسْتَغْنَىٰ
 اللَّهُ وَاللَّهُ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿٦﴾

4. *"Anajua viliomo katika mbingu na ardhi, na Anajua mnayo yaficha na mnayo yatangaza. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliomo vifuani."*

5. *"Kwani haikukujieni khabari ya waliokufuru huko zanani, wakaonja matokeo mabaya ya mambo yao? Na wao wana adhabu iliyo chungu."*

6. *"Hayo ni kwa kuwa walikuwa wakiwajia Mitume wao kwa hoja zilizo wazi, nao wakasema: Hivyo binaadamu ndio atuongoe? Basi wakakufuru, na wakageuka upande. Mwenyezi Mungu Akawa hana haja nao. Na Mwenyezi Mungu Ni Mkwasi si Mhitaji, Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujitosha Na Mwenye Kusifiwa."*

Onyo Lililotolewa Kupitia Kutajwa Hatima ya Mataifa Yaliyokufuru

Ikielezea kuhusu mataifa yaliyopita na adhabu na kuadabishwa waliyopewa kwa sababu ya kuwapinga Wajumbe na kukanusha ukweli. Allah تَعَالَى Anasema:

﴿ أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَبُؤُا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلُ ﴾

"...Kwani haikukujieni khabari ya waliokufuru huko zamani..."

Maana yake: Taarifa juu yao na yaliyowapata,

﴿ فَدَاقُوا وَبَالَ أَمْرِهِمْ ﴾

"...wakaonja matokeo mabaya ya mambo yao?..."

Walionja matokeo ya uovu wao na kukataa na matendo mabaya. Na inahusu adhabu na madhila waliyoyapata katika maisha ya dunia,

﴿ وَهُمْ عَدَابُ أَلِيمٌ ﴾

"...Na wao wana adhabu iliyo chungu..."

Siku ya Kiama, ziada ya adhabu walizopata hapa duniani. Allah تعالی Alielezea sababu;

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُ كَانَتْ تَأْتِيهِمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ

“Hayo ni kwa kuwa walikuwa wakiwajia Mitume wao kwa hoja zilizo wazi.”

Wakiunga mkono hoja, ushahidi ulio wazi,

فَقَالُوا أَبَشَرٌ مِّمَّنَّا

“...nao wakasema: Hivyo binaadamu ndio atuongoe?”

Waliona kuwa ni jambo lisilowezekana Utume kupewa Mwanadamu na kuwa muongozo wao upitie kwa mtu kama wao.

فَكَفَرُوا وَتَوَلَّوْا

“...Basi wakakufuru, na wakageuka upande...”

Walikanusha ukweli na wakaupa mgongo,

وَاسْتَعْنَىٰ ٱللَّهُ

“...Mwenyezi Mungu Akawa hana haja nao...”Wao,

وَٱللَّهُ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿٦﴾

“...Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, si mhitaji, naye ni Msifiwa.”

* * *

رَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ لَنْ يُبْعَثُوا قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۗ وَذَلِكَ عَلَىٰ اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧﴾ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَالنُّورِ الَّذِي أَنْزَلْنَا ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٨﴾ يَوْمَ نَجْمَعُكُمْ لِيَوْمِ الْجَمْعِ ۗ ذَلِكَ يَوْمُ التَّغَابُنِ ۗ وَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيَعْمَلْ صَالِحًا يُكْفِرْ عَنَّا سَيِّئَاتِهِ وَيُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرَىٰ مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٩﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٠﴾ مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ يَهْدِ اللَّهُ قَلْبَهُ ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١١﴾ وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ ۗ فَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَإِنَّمَا عَلَىٰ رَسُولِنَا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ ﴿١٢﴾ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ وَعَلَىٰ اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٣﴾

رَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ لَنْ يُبْعَثُوا قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۗ وَذَلِكَ عَلَىٰ اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧﴾ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَالنُّورِ الَّذِي أَنْزَلْنَا ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٨﴾ يَوْمَ نَجْمَعُكُمْ لِيَوْمِ الْجَمْعِ ۗ ذَلِكَ يَوْمُ التَّغَابُنِ ۗ وَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيَعْمَلْ صَالِحًا يُكْفِرْ عَنَّا سَيِّئَاتِهِ وَيُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرَىٰ مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٩﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٠﴾

وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٠﴾

7. Waliokufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa.

Sema: Kwanini? Naapa kwa Mola wangu Mlezi!

Hapana shaka mtafufuliwa, na kisha hapana

shaka mtaambiwa mliyoyatenda. Na hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.

8. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na Nuru Tuliyoiteremsha. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.

9. Siku Atakayokukusanyeni kwa ajili ya Siku ya Mkusanyiko; hiyo ni siku ya faida au hasara. Na anayemuamini Mwenyezi Mungu na akatenda mema, Atamfutia maovu yake, na Atamuingiza katika Mabustani yenye kupitiwa kati yake na mito, watadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

10. Na waliokufuru na wakakadhibisha Ishara Zetu, hao ni watu wa Motoni, watadumu humo milele. Na hayo ndiyo marudio mabaya."

Maisha baada ya kufa ni kweli.

Allah تعالى Anatupa habari juu ya makafiri, washirikina na mapagani kuwa wanadai kuwa hawatafufuliwa,

قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ

“Sema: Kwani? Naapa kwa Mola wangu Mlezi! Hapana shaka mtafufuliwa, na kisha hapana shaka mtaambiwa mliyoyatenda.”

Ina maana: Mtaelezwa kuhusu matendo yenu, yawe makubwa au madogo.

وَذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧﴾

“Na hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.”

Kuwafufua na Kuwarejesha kama mlivyokuwa ni suala jepesi kwa Allah تعالى. Hii ni Ayah ya tatu ambayo kwayo Allah تعالى Anamuamuru Mjumbe Wake ﷺ aape kwa Mola wake, Aliyetukuka na Mwenye cheo kikubwa, kuwa ufufuo utatokea. Ya mwanzo ipo katika *Surat Yunus*,

﴿ وَيَسْتَنْبِئُكَ أَحَقُّ هُوَ قُلْ إِي وَرَبِّي إِنَّهُ لَحَقٌّ وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿١٠﴾ ﴾

“Na wanakuuliza: Je! Ni kweli hayo? Sema: Ehe! Naapa kwa Mola wangu Mlezi! Hakika hayo ni kweli, na wala nyinyi hamshindi!” (10:53)

Ya Pili ni katika *Surat Saba*,

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَأْتِينَا السَّاعَةُ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتَأْتِيَنَّكُمْ

“Na walisema waliokufuru: Haitatufikia Saa (ya Kiyama). Sema: Kwani? Hapana shaka itakufikieni” (34:3)

Na ya Tatu imo katika Aya hii,

رَعِمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ لَنْ يُبْعَثُوا قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ وَذَلِكَ عَلَىٰ

اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧﴾

“Waliokufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: Kwani?”

Naapa kwa Mola wangu Mlezi! Hapana shaka mtafufuliwa, na kisha hapana shaka mtaambiwa mliyoyatenda. Na hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.” (64:7)

Allah تعالى Amesema,

فَقَامُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَالنُّورِ الَّذِي أَنْزَلْنَا

“Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na Nuru Tuliyoiteremsha.” (64:8)

Hiyo ni Qur’ani,

وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٨﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za mnayoyatenda.”

Hapana katika Amali zinazoweza kuepa ufahamu Wake.

Siku ya At-Taghabun

Allah تعالى Amesema,

يَوْمَ تَجْمَعُكُمْ لِيَوْمِ الْجَمْعِ

“Siku Atakayokusanyeni kwa ajili ya Siku ya Mkusanyiko;...”

Ina maana: Siku ya Kiyama. Hii ni Siku ambapo vizazi vya mwanzo na vya baadaye watakusanywa katika eneo moja, munitaji atasikika na wote, na uoni mmoja utaona wote kwa urahisi. Allah تعالى Amesema,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّمَن خَافَ عَذَابَ الْآخِرَةِ ۚ ذَٰلِكَ يَوْمُ تَجْمَعُ لَهُ النَّاسُ وَذَٰلِكَ يَوْمٌ

مَشْهُودٌ ﴿١١﴾

“Hakika katika haya ipo ishara kwa yule anayeogopa adhabu ya Akhera. Hiyo ndiyo Siku itakayokusanyiwa watu, na hiyo ndiyo Siku itakayoshuhudiwa.” (11:103), na,

قُلْ إِنَّ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ ﴿٥٦﴾ لَمَجْمُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿٥٧﴾

“Sema: Hakika wa zamani na wa mwisho. Bila ya shaka watakusanywa kwa wakati wa siku maalumu.” (56:49-50)

Kauli ya Allah تعالى،

ذَلِكَ يَوْمُ التَّغَابُنِ ۗ

“...hiyo ni siku ya kupata faida au hasara...” (64:9)

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Ni moja ya majina ya Siku ya Hukumu na hiyo ni kwa sababu watu wa Peponi watakuwa wamewashinda watu wa Motoni”¹. Qatadah na Mujahid walisema vivyo hivyo².

Muqatil bin Hayyan alisema, “Hapana hasara kubwa na faida kubwa kuliko hali hii ya hawa kuingia Peponi na hawa (wengine) kuingizwa Motoni”

Allah تعالى Ameeleza katika Kauli Yake kwa Kusema;

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَمَنْ يُؤْمِنْ بِاللَّهِ يَهْدِ اللَّهُ قَلْبَهُ ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١١﴾
 وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ ۚ فَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَإِنَّمَا عَلَىٰ رَسُولِنَا الْبَلْغُ الْمُبِينُ ﴿١٢﴾ اللَّهُ
 لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ وَعَلَىٰ اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٣﴾

11. Haufiki msiba wowote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu Huuongoa moyo wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

12. Na mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume. Mkigeuka, basi hakika juu ya Mtume wetu ni kufikisha (Ujumbe wake) kwa uwazi tu.

13. Mwenyezi Mungu, hapana mungu isipo kuwa Yeye. Na juu ya Mwenyezi Mungu nawategemeo Waumini.”

¹ At-Tabari 23:420.

² At-Tabari 23:429, 420.

Yote yawapatayo binadamu ni kwa Ridhaa ya Allah تعالى.

Allah تعالى Anatufahamisha kama Alivyofanya katika *Suratil Al-Hadiyd*,

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَنْ نَبْرَأَهَا ۗ إِنَّ
ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾

“Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.” (57:22)

Allah تعالى Amesema hapa,

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ

“Haufiki msiba wowote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.” (64:11)

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Kwa Amri ya Allah تعالى”, Maana yake: Kwa Kudra Yake na Utashi Wake,

وَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ يَهْدِ اللَّهُ قَلْبَهُ ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١١﴾

“Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu Huuongoa moyo wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.” (64:11)

Maana yake: Yeyote aliyethirika na madhara na akajua kuwa yalijiri kwa Hukumu ya Allah تعالى, na Akaridhia na kusubiri Malipo ya Allah تعالى, basi Allah تعالى Atauongoza moyo wake na Atamfidia aliyoyapoteza katika maisha ya dunia kwa Kumpa mwongozo katika nafsi yake na hasa katika imani. Allah تعالى Atampa mbadala wa chochote alichopoteza kwa ajili Yake au kilicho bora zaidi. Ali bin Abi Talhah alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

وَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ يَهْدِ اللَّهُ قَلْبَهُ ۗ

“Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu Huuongoa moyo wake.”

“Allah تعالى Atauongoza moyo wake katika uhakika. Kwa hiyo, atajua kwamba kilichomfikia kisingelimkosa na kilichomkosa kisingelimfikia”¹.

¹ At-Tabari 23:421.

Kuna makubaliano juu ya Hadith (ambayo Bukhari na Muslim waliipokea) isemayo:

«عَجَبًا لِلْمُؤْمِنِ لَا يَفْضِي اللَّهُ لَهُ قَضَاءَ إِلَّا كَانَ خَيْرًا لَهُ، إِنْ أَصَابَتْهُ ضَرَاءٌ صَبَرَ فَكَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ سَرَاءٌ شَكَرَ فَكَانَ خَيْرًا لَهُ، وَلَيْسَ ذَلِكَ لِأَحَدٍ إِلَّا لِلْمُؤْمِنِ»

“Muumini anastaajabisha: Allah Hamuandikii jambo ila lina kheri kwake. Iwapo atapata madhara, akasubiri ni bora kwake. Iwapo amepewa neema, akashukuru ni bora kwake. Na hayo hayapatikani kwa yeyote isipokuwa kwa muumini.”¹

Amri ya kumtii Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ.

Allah تعالى Amesema,

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ

“Na mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume.”

Allah تعالى Anaamrisha Yeye na Mjumbe Wake ﷺ watiwe. Pia Anaamrisha kutekeleza Aliyoyakataza na kuacha Aliyoyakataza na Kuyakemea.

Allah تعالى Anasema;

فَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَإِنَّمَا عَلَىٰ رَسُولِنَا الْبَلْغُ الْمُبِينُ ﴿٦٤﴾

“Mkigeuka, basi hakika juu ya Mtume wetu ni kufikisha (Ujumbe wake) kwa uwazi tu.”

Maana yake: Endapo utaacha kuamini, basi jukumu la Mtume ni kufikisha na jukumu lenu ni kusikiliza na kutii. Az-Zuhri رحمه الله تعالى alisema, “Ujumbe unatoka kwa Allah تعالى, na kuufikisha ni jukumu la Mtume, na kuufuata ni juu yetu.”²

¹ At-Tabari 23:2295.

² Al-Bukhari, katika kitabu cha *Tawhid*, juzuu ya 16.

Tawhiid

Allah تعالیٰ Anaelezea kuwa Yeye ni Mmoja, ambaye Kwake viumbe wote hupata mahitaji yao, hapana mwingine mwabudiwa (wa kweli).

﴿اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ﴾

“Mwenyezi Mungu, hapana muabudiwa isipokuwa Yeye. Na juu ya Mwenyezi Mungu na wategemee Waumini.” (64:13)

Kwa hiyo Kwanza Anaarifu kuhusu Tawhid na maana yake. Maana iliyokusudiwa ni kumpwekesha na kujisalimisha Kwake, na kumtegemea Yeye, kama Alivyosema;

﴿رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا﴾

“Mola Mlezi wa mashariki na magharibi, hapana muabudiwa isipo kuwa Yeye, basi mfanye kuwa Mtegemewa wako.” (73:9)

* * *

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ مِنْ أَرْوَاجِكُمْ وَأَوْلَادِكُمْ
 عَدُوًّا لَكُمْ فَاحْذَرُوهُمْ ۚ وَإِنْ تَعَفَوْا وَتَصَفَحُوا وَتَغْفِرُوا
 فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٤﴾ إِنَّمَا أَمْوَالُكُمْ وَأَوْلَادُكُمْ
 فِتْنَةٌ ۗ وَاللَّهُ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿١٥﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا
 اسْتَطَعْتُمْ وَأَسْمِعُوا وَأَطِيعُوا وَأَنْفِقُوا خَيْرًا لِّأَنْفُسِكُمْ ۗ
 وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَالِحُونَ ﴿١٦﴾ إِنْ
 تُقْرِضُوا اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا يُّضْعِفْهُ لَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ۗ
 وَاللَّهُ شَكُورٌ حَلِيمٌ ﴿١٧﴾ عَلِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْعَزِيزِ
 الْحَكِيمِ ﴿١٨﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ مِنْ أَرْوَاجِكُمْ وَأَوْلَادِكُمْ
 عَدُوًّا لَكُمْ فَاحْذَرُوهُمْ ۚ وَإِنْ تَعَفَوْا وَتَصَفَحُوا
 وَتَغْفِرُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٤﴾ إِنَّمَا أَمْوَالُكُمْ
 وَأَوْلَادُكُمْ فِتْنَةٌ ۗ وَاللَّهُ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿١٥﴾ فَاتَّقُوا
 اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ وَأَسْمِعُوا وَأَطِيعُوا وَأَنْفِقُوا خَيْرًا
 لِّأَنْفُسِكُمْ ۗ وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ
 الْفَالِحُونَ ﴿١٦﴾ إِنْ تُقْرِضُوا اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا
 يُّضْعِفْهُ لَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ شَكُورٌ حَلِيمٌ
 ﴿١٧﴾ عَلِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْعَزِيزِ
 الْحَكِيمِ ﴿١٨﴾

“14. Enyi mlioamini! Hakika miongoni mwa wake zenu na watoto wenu wamo maadui zenu. Basi tahadharini nao. Na mkiyafuta, na mkapuuzza, na mkasamehe basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

15. Hakika mali zenu na watoto wenu ni mtihani. Na kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa.

16. Basi mcheni Mwenyezi Mungu kwa muezavyo, na sikieni, na t'iini, na toeni, itakuwa kheri kwa nafsi zenu. Na mwenye kuepushwa na uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio waliofanikiwa.

17. Mkimkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mzuri, Atakuzidishieni mara dufu, na Atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa shukrani, Mpole.

18. Mwenye Kujua siri na dhaahiri, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Indhari dhidi ya Fitnah ya Wake na Watoto

Allah تعالی Anaeleza kuwa baadhi ya wake na watoto ni maadui wa waume zao na baba zao, wakawashughulisha badala ya kutumia muda wao kwa kufanya amali njema. Allah تعالی Amesema katika Aya nyingine,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُلْهِكُوا أَمْوَالَكُمْ وَلَا أَوْلَادَكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ ؕ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ

فَأُولَئِكَ هُمُ الْخَسِرُونَ ﴿٦٣﴾

“Enyi mlio amini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio walio khasiri.” (63:9)

Allah تعالی Amesema hapa,

فَاَحْذَرُوهُمْ ؕ

“Basi tahadharini nao...” (64:14)

Kwa Ajili ya Dini Yenu, kwa mujibu wa Zayd. Mujahid alielezea Ayah,

إِنَّ مِنْ أَرْوَاحِكُمْ وَأَوْلَادِكُمْ عَدُوًّا لَكُمْ

“Hakika miongoni mwa wake zenu na watoto wenu wamo maadui zenu.” (64:14)

Kwa kusema, “Wanaweza kumpelekea mtu kuvunja mahusiano au kumuasi Mola wake. Mtu anayependa wakeze na watoto anaweza kuwatii katika hali hii.” Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alimueleza mtu aliyeuliza maana ya Aya hii,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ مِنْ أَرْوَاحِكُمْ وَأَوْلَادِكُمْ عَدُوًّا لَكُمْ فَاَحْذَرُوهُمْ ؕ

“Enyi mlio amini! Hakika miongoni mwa wake zenu na watoto wenu wamo maadui zenu. Basi tahadharini nao.”

“Walikuwepo wanaume waliosilimu Makkah na wakataka kuhajiri kumfuata Mtume ﷺ. Hata hivyo wake zao na watoto wao waliwazuia. Baadaye walipojiunga na Mtume ﷺ, wakawakuta wale waliokuwa naye (Masahaba) wamepata elimu na dini, hivyo walitaka kuwaadhibu wake zao na watoto wao.

Allah تعالى Akashusha Aya hii,

وَإِن تَعْفُوا وَتَصْفَحُوا وَتَغْفِرُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٦٤﴾

“Na mkiyafuta, na mkapuuzwa, na mkasamehe si hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

At Tirmidhi alipokea Hadithi hii na kuipa daraja la *Hassan Sahih*¹. Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّمَا أَمْوَالُكُمْ وَأَوْلَادُكُمْ فِتْنَةٌ وَاللَّهُ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٦٥﴾

“Hakika mali yenu na watoto wenu ni mtihani. Na kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa.” (64:15)

Allah تعالى Anasema kuwa mali na watoto ni mtihani kutoka kwa Allah تعالى kwa waja Wake, ili Awajue wanaomtii na wanaomuasi. Kauli ya Allah تعالى,

وَاللَّهُ عِنْدَهُ

“Na kwa Mwenyezi Mungu upo...” 64:15

Maana yake: Siku ya Kiyama.

أَجْرٌ عَظِيمٌ

“...ujira mkubwa...” (64:15)

Kama Allah تعالى Alivyodhukuru;

زُيِّنَ لِلنَّاسِ حُبُّ الشَّهَوَاتِ مِنَ النِّسَاءِ وَالْبَنِينَ وَالْقَنَاطِيرِ الْمُقَنْطَرَةِ مِنَ الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ وَالْخَيْلِ الْمُسَوَّمَةِ وَالْأَنْعَامِ وَالْحَرْثِ ۗ ذَٰلِكَ مَتَّعُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ۗ وَاللَّهُ عِنْدَهُ حُسْنُ الْمَقَابِ ﴿١٤﴾

“Watu wamepambiwa kupenda matamania ya wanawake, na wana, na mirundi² ya dhahabu na fedha, na farasi asili, na mifugo, na mashamba. Hayo ni starehe ya maisha ya duniani; na kwa Mwenyezi Mungu ndio kwenye marejeo mema.” (3:14) Na Aya baada yake.

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 9:222.

² Angalia Tafsiri ya Surah Al 'Imran (3:14).

Imam Ahmad alipokea kuwa Baraydah alisema, “Mtume ﷺ alikuwa akitoa hotuba na Hasan na Husayn walikuja huku wamevaa kanzu nyekundu, wakitembea na kukimbia. Mtume ﷺ alishuka kwenye *Minbar*, aliwashika na kuwaweka mbele yake. Kisha akasema, “Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ wamesema kweli”

«صَدَقَ اللهُ وَرَسُولُهُ إِنَّمَا أَمْوَالُكُمْ وَأَوْلَادُكُمْ فِتْنَةٌ، نَظَرْتُ إِلَى هَذَيْنِ الصَّيِّبِ يَمْشِيَانِ وَيَعْتُرَانِ، فَلَمْ أَصْبِرْ حَتَّى قَطَعْتُ حَدِيثِي وَرَفَعْتُهُمَا»

“Kwa hakika mali zenu na wana wenu ni mtihani. Niliwaona hawa vijana wawili wakitembea na kukimbia na sikuweza kuvumilia nikaacha kuzungumza na nikawachukua.”¹

Hii ilirekodiwa na wakusanyaji wa Sunan, na At-Tirmidhi aliipa daraja la “*Hasan Gharib*.”²

Amri ya Taqwa kwa kadri ya uwezo wa mtu.

Allah تعالى Anasema,

فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ

“Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama muwezavyo,...” (64:16)

Muradi wake, kama unavyoweza na kudumisha. Sahihi mbili zilirekodi kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا أَمَرْتُكُمْ بِأَمْرٍ فَأْتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ، وَمَا نَهَيْتُكُمْ عَنْهُ فَاجْتَنِبُوهُ»

“Nitakapo kuamuruni kufanya jambo, fanyeni kwa kadri ya uwezo wenu, na chochote ninachokukatazeni, kiacheni.”³

Kauli ya Allah تعالى,

وَأَسْمِعُوا وَأَطِيعُوا

“...na sikieni, na t’iini,...” (64:16)

¹ Ahmad 5:354.

² Abu Dawud 1:663, Tuhfat Al-Ahwadh1i 10:278, An-Nasai 3:108, Ibn Majah 2:1190.

³ Fat’hul Al-Bari 13:264, Muslim 2:975.

Maana yake: Haya uliyoamrisha na Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ na usipotoke kutoka kulia kwenda kushoto. Usitamke kauli au uamuzi kabla Allah تعالى na Mjumbe Wake hawajatoa kauli au uamuzi. Usidharau ulichoamrisha kufanya wala kufanya ulichokatazwa kufanya.

Kushajiisha Sadaka

Allah تعالى Amesema,

وَأَنْفِقُوا خَيْرًا لِّأَنْفُسِكُمْ^٤

“...na toeni, itakuwa kheri kwa nafsi zenu...”

Maana yake: Toeni katika vile Alivyokuruzukuni Allah تعالى, muwape jamaa zenu na masikini, wahitaji na madhalili. Muwatendee wema viumbe wa Allah تعالى, kama vile Allah تعالى Alivyo kwenu na bado Anawatendea wema. Hili litakuwa bora kwenu hapa duniani na Akhera. Vinginevyo, msipofanya hivyo hali itakuwa mbaya hapa duniani na Akhera. Allah تعالى Amesema;

وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَالِحُونَ ﴿٥﴾

“Na mwenye kuepushwa na uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio waliofanikiwa.”

Maneno haya yalielezwa na Aya sawa na hiyo katika Surat Al-Hashr, ambapo pia tulitaja Hadithi¹ muafaka. Kwa hiyo hapana haja ya kuzirejea hapa. Shukrani na Sifa zote Anastahiki Allah تعالى. Allah تعالى Amesema,

إِنْ تُقْرِضُوا اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا يُضْعِفْهُ لَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ^٥

“Mkimkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mzuri, Atakuzidishieni mara dufu, na Atakusameheni.”

Maana yake: Chochote unachotumia, Allah تعالى Atakupa mbadala, na Kwake kuna malipo kwa chochote ulichotoa kwa njia ya sadaka. Allah تعالى Anachukulia kutoa sadaka kama ni mkopo Kwake. Kama Allah تعالى Alivyosema katika Hadithi Qudsi.

¹ Angalia juzuu ya nane Tafsiri ya Surat Hashr (59:9).

«مَنْ يُفْرِضْ غَيْرَ ظُلْمٍ وَلَا عَدِيمٍ»

“Nani atakayemkopesha Ambaye si dhalimu wala masikini?”¹

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema ndani ya Surat Al-Baqarah,

فَيُضَعِّفُهُ لَهُ أضعافًا كَثِيرَةً

“... ili amzidishie mzidisho mwingi,...” (2:245)

Allah تعالى Amesema;

وَيَغْفِرَ لَكُمْ

“...na Atakusameheni.”

Muradi wake ni kuwa Atayafuta makosa yenu.

وَاللَّهُ شَكُورٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa shukrani,...”

Maana yake: Analipa malipo mengi kwa kilicho kichache,

حَلِيمٌ

“...Mpole...”

Maana yake: Anasamehe, Anatoa, Anafunika na Kufuta madhambi, makosa, na udhaifu,

عَلِيمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Mwenye kujua siri na dhahiri, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Maelezo yake jameshatolewa mara kadhaa.

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya Surat At-Taghabun, sifa zote na shukrani zinamstahiki Allah تعالى.

* * *

¹ Muslim 1:522.

Tafsiri ya Suratu Talaq
Sura ya 65
Iliteremshwa Madinah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa Jina la Allah, Mwingi
 wa Rehema, Mwenye
 Kurehemu.**

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ
 فَطَلَّقُوهُنَّ لِعَدَّتِهِنَّ وَأَحْصُوا الْعِدَّةَ
 وَاتَّقُوا اللَّهَ رَبَّكُمْ لَا تَخْرُجُوهُنَّ
 مِنْ بَيْوتِهِنَّ وَلَا تَخْرُجْنَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَنَّ
 بِفَحِشَةٍ مُبَيَّنَةٍ وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ
 وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ فَقَدْ ظَلَمَ
 نَفْسَهُ لَا تَدْرِي لَعَلَّ اللَّهَ يُحْدِثُ بَعْدَ
 ذَلِكَ أَمْرًا ﴿١﴾

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ
 فَطَلَّقُوهُنَّ لِعَدَّتِهِنَّ وَأَحْصُوا الْعِدَّةَ
 وَاتَّقُوا اللَّهَ رَبَّكُمْ لَا تَخْرُجُوهُنَّ
 مِنْ بَيْوتِهِنَّ وَلَا تَخْرُجْنَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَنَّ
 بِفَحِشَةٍ مُبَيَّنَةٍ وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ
 وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ فَقَدْ ظَلَمَ
 نَفْسَهُ لَا تَدْرِي لَعَلَّ اللَّهَ يُحْدِثُ بَعْدَ
 ذَلِكَ أَمْرًا ﴿١﴾

*“Ewe Nabii! Mtakapowapa
 talaka wanawake, basi
 wapeni talaka katika wakati
 wa eda zao. Na fanyeni
 hisabu ya iddah. Na mcheni
 Mwenyezi Mungu, Mola
 Wenu Mlezi. Msiwatoe
 katika nyumba zao, wala*

وَيُعْظَمُ لَهُمْ أَجْرًا ﴿٢﴾

wasitoke wenyewe, ila wakifanya jambo la uchafu uliowazi. Hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu, msiikiuke. Na mwenye kuikiuka mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi amejidhulumu nafsi yake. Hujui; labda Mwenyezi Mungu Ataleta jambo jengine baada ya haya.” (65:1)

Kuna kipindi ambacho wanawake waliotalakiwa hubaki Majumbani mwao. Na huzingatia Eda Yake

Mtume ﷺ alisemeshwa mwanzo katika Ayah hii, ili kumpa heshima, kisha Allah تعالى Akausemesha Ummah wake Akasema,

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَطَلِّقُوهُنَّ لِعَدَّتِهِنَّ.

“Ewe Nabii! Mtakapowapa talaka wanawake, basi wapeni talaka katika wakati wa eda zao.”

Bukhari amenukuu kuwa Abdullah bin Umar رضي الله عنه alimtaliki mkewe, wakati wa uhai wa Mtume ﷺ, mkewe alipokuwa katika hedhi. Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alimuambia hilo Mtume ﷺ. Mtume ﷺ alighadhibika na kusema,

«لِيُرَاجِعَهَا ثُمَّ يُنْسِكُهَا حَتَّى تَطْهَرَ، ثُمَّ تَحْبِضَ فَتَطْهَرَ، فَإِنْ بَدَأَ لَهُ أَنْ يُطَلِّقَهَا، فَلْيُطَلِّقْهَا طَاهِرًا قَبْلَ أَنْ يَمْسَهَا، فَبِئْسَ الْعِدَّةُ الَّتِي أَمَرَ بِهَا اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ»

“Muamrishe amrejee na akae naye mpaka atwahirike, na kisha asubiri mpaka apate hedhi nyingine na atwahirike. Kisha kama atataka kumuacha, anaweza kufanya hivyo atakuwa tohara kutokana na hedhi, kabla hajamuingilia. Hii ndio eda ambayo ameamuru Allah Aliyetukuka.”¹

Bukhari aliiandika Hadithi hii katika sehemu nyingi za Sahihi yake. Muslim amekusanya Hadithi hii na masimulizi yake yanatumia maneno haya,

«فَبِئْسَ الْعِدَّةُ الَّتِي أَمَرَ اللَّهُ أَنْ يُطَلَّقَ لَهَا النِّسَاءُ»

“Hii ndio eda ambayo Allah Ameamrisha kwa wanawake wanaoachwa.”²

¹ Fat’hul Al-Bari 8:521.

² Fat’hul Al-Bari 9:258, 393; Muslim 2:1094, 1095.

Muslim ndani ya Sahihi yake, amenukuu Hadithi ambayo inawiana na mapokezi ya Ibn Jurayji ambaye amesema kuwa Abu Zubayr alimueleza kuwa alimsikia Abdur Rahman bin Ayman, ambaye alipewa uhuru na Azzah, akimsaili Abdullah bin Umar رضي الله عنه. Na Abu Az-Zubayr amemsikia akimuuliza. "Kuna hukumu gani kwa mtu anayemtaliki mkewe huku yumo ndani ya hedhi?" Abdullah رضي الله عنه akajibu, "Wakati wa enzi na uhai wa Mtume ﷺ, Abdullah bin Umar رضي الله عنه alimtaliki mkewe aliyekuwa katika hedhi". Hivyo Mtume ﷺ akasema,

«لِيُرَاجِعَهَا»

"Amrudie" kwa hiyo akamrudia na yeye Mtume ﷺ akasema,

«إِذَا طَهَّرْتَ فَلْيُطَلِّقْ أَوْ يُنِكَ»

"Atakapokuwa tohara, ama amuache au akae naye."

Abdullah bin Umar رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alisoma Aya hii:

(يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَطَلِّقُوهُنَّ فِي قُبُلِ عِدَّتِهِنَّ)

"Ewe Nabii! Mtakapowapa talaka wanawake, basi wapeni talaka katika wakati wa eda zao."¹

Na Abdullah (Ibn Mas'ud) رضي الله عنه ametolea maelezo Kauli ya Allah تعالى,

فَطَلِّقُوهُنَّ لِعَدَّتِهِنَّ

"**Basi wapeni talaka katika wakati wa eda zao,**" Amesema, "kuwa safi bila kuingiliwa."² Hadithi kama hiyo imepokelewa kutoka kwa Ibn Umar, Ata, Mujahid, Al-Hasan, Ibn Sirin, Qatadah, Maymun bin Mihran na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم. Aidha imeripotiwa kutoka kwa Ikrimah na Adh-Dhahaak.³ Ali bin Abi Talhah amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuhusu Aya,

فَطَلِّقُوهُنَّ لِعَدَّتِهِنَّ

"**Basi wapeni talaka katika wakati wa eda zao.**" Amesema hatakiwi kumuacha anapokuwa katika siku zake wala anapokuwa katika tohara ambayo

¹ Muslim 2:1098.

² At-Tabari 23:432.

³ At-Tabari 23:432-434.

amejamiiana naye. Bali awe naye mpaka apate hedhi na baada ya kumalizika hedhi amuache talaka moja.”¹ Na Ikrimah amezungumzia Kauli hii,

فَطَّلِقُوهُنَّ لِإِعْتَابٍ

“...basi wapeni talaka katika wakati wa eda zao...”

Neno “Idda” maana yake ni tohara. Na neno “Qar’u” maana yake ni Hedhi. “Kwa hiyo ampe talaka wakati imedhihirika kuwa ni mja mzito. Na wala asimtaliki hali ya kuwa amemuingilia, au hajui ni mjamzito au la?”

Kwa sababu hii ndio maana wanazuoni wa sharia ya Kiislamu “Fuqahau” wanasema kuwa kuna aina mbili ya talaka, moja kwa mujibu wa Sunnah na nyingine iliyozushwa (Bida’a).

Talaka inayokubalika katika Sunnah ni ile ambayo mume anaitoa kwa mkewe wakati yupo tohara; ambayo hakumuingilia kkatika tohara hiyo, au amuache mke wake ikidhihirika kuwa ni mjamzito. Ama talaka ya uzushi (Bida’a), inatokea wakati mume anamtaliki mkewe akiwa kwenye hedhi, au akiwa katika tohara aliyojamiiana naye, na wala hajui kuwa ni mjamzito au la. Kuna aina ya tatu ya talaka, ambayo si Sunnah wala bida’a ambapo mtu anamtaliki mke aliyekomaa, au kumuacha mke kabla ya kumjamii hata mara moja,

وَأَحْصُوا الْعِدَّةَ

“...Na fanyeni hisabu ya eda.”

Maana yake: Hesabuni ili kujua mwanzo na mwisho ili eda ya mwanamke isirefushwe na kuzuilika kuolewa,

وَأَتَّقُوا اللَّهَ رَبَّكُمْ

“Na mcheni Mwenyezi Mungu, Mola wenu Mlezi.”

Katika jambo hili.

¹ At-Tabari 23:435.

Matumizi na Malazi ni Juu ya Mume katika Kipindi cha Eda ya Talaka Rejea.

Allah تعالى Amesema,

لَا تُخْرِجُوهُنَّ مِنْ بُيُوتِهِنَّ وَلَا يُخْرِجَنَّ

“...Msiwatoe katika nyumba zao, wala wasitoke wenyewe,...”

Maana yake: Wakati wa kipindi cha eda, ana haki ya kuishi kwa mume wake, muda wa kuwa kipindi cha eda kinaendelea. Kwa hiyo, mume hana haki ya kumtoa mke katika nyumba yake, wala haruhusiwi kuihama nyumba, kwani bado yuko kwenye mkataba wa ndoa. Allah تعالى Amesema,

إِلَّا أَنْ يَأْتِيَنَّ بِفِدْحَةٍ مُنِيِنَةٍ

“...ila wakifanya jambo la uchafu ulio wazi...”

Maana yake: Mke aliyeachwa hatakiwi kuihama nyumba ya mume wake isipokuwa kama alitenda uchafu wa wazi, ambapo kwa hali hiyo, ataihama nyumba ya mume wake. Mfano kama kuzini, kwa mujibu wa rai ya Abdullah bin Mas'ud, Ibn Abbas, Said bin Al-Musayyab, Ash-Shabi, Al-Hasan, Ibn Sirin, Mujahid, Ikrimah, Said bin Jubayr, Abuu Kilabi, Abuu Swalehe, Adh-Dhahhak, Zayd bin Aslam, Ata Al-Khurasani, As-Suddi, Said bin Hilal na wengineo رضي الله عنهم¹. “*Fahishah Mubayyinah*” ina maana kumuasi mumewe kwa wazi au anapoikashifu familia ya mume kwa maneno na vitendo, haya maelezo ni kwa mujibu wa Ubay bin Ka'b, Ibn Abbas, Ikrimah na wengineo رضي الله عنهم². Kauli ya Allah تعالى,

وَتَلَكَ حُدُودَ اللَّهِ

“...Hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu, msikiuke...” Maana yake: “Hizi ni kutokana na Sharia Zake na Makatazo Yake.”

وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ

“...Na mwenye kuikiuka mipaka ya Mwenyezi Mungu...” Muradi wake: Yeyote anayechupa mipaka hii, anaivuka na anatekeleza mengine minghairi ya hayo,

فَقَدْ ظَلَمَ نَفْسَهُ

“...basi amejdhulumu nafsi yake...” Kwa kufanya hivyo,

¹ At-Tabari 23:438, Al-Qurtubi 18:156, Ad-Durr Al-Manthur 8:194.

² At-Tabari 23:438.

Hekima ya Kukaa Eda Katika Nyumba ya Mume.

Allah تعالى Amesema,

لَا تَدْرِي لَعَلَّ اللَّهَ تَحْدِثُ بَعْدَ ذَلِكَ أَمْرًا

“...Hujui; labda Mwenyezi Mungu Ataleta jambo jengine baada ya haya...”

Maana yake: Tunaamuru mwanamke aliyetalikiwa abaki kwenye nyumba ya mumewe wakati wa eda, ili mume akiona kuwa alikosea na Allah تعالى Akajaalia ndani ya moyo wa mume kumrejea mkewe. Kwa njia hii itakuwa wepesi kumrejea mkewe. Az-Zuhri amesema kuwa Ubaydullah bin Abdullah رضي الله عنه amesema kuwa Fatimah bint Qays رضي الله عنها alizungumzia Kauli hii ya Allah تعالى.

لَا تَدْرِي لَعَلَّ اللَّهَ تَحْدِثُ بَعْدَ ذَلِكَ أَمْرًا

“...Hujui; labda Mwenyezi Mungu Ataleta jambo jengine baada ya haya...”

Fatma رضي الله عنها amesema: “Huko ni kumrejea mke”¹ Sawa na hayo yalinenwa na Ash-Shabi, Ata, Qatadah. Adh-Dhahhak, Muqatil bin Hayyan na Ath-Thawri.²

Mwanamke Mwenye Talaka yake Isiyo Rejea hana Haki ya Matumizi na Malazi kutoka kwa Mume.

Rai ya wanazuoni wa *Salaf* na wafuasi wao ni kuwa mwanamke aliyepewa talaka isiyo ya rejea hana haki ya kupewa malazi na mume. Wanaegemea katika Hadithi ya Fatimah bint Qays A-Fahriyah رضي الله عنها wakati mumewe Abu Amr bin Hafs رضي الله عنه alipomuacha kwa mara ya tatu na ya mwisho. Wakati huo alikuwa mbali naye huko Yemen, na akamtumia talaka. Pia Mjumbe wake alikuja na Shayiri kwa ajili ya matumizi ya Mkewe, lakini hakuridhia nafaka hiyo. (Abu Amr رضي الله عنه) Akasema, “Wa Llahi sipaswi kukugharamikia.” Fatma رضي الله عنها akamuendea kwa Mtume ﷺ ambaye alisema,

«لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِ نَفَقَةٌ»

“Hana dhima ya kukulisha.” Muslim aliongeza katika masimulizi yake,

¹ At-Tabari 23:441.

² At-Tabari 23:442, Al-Qurtubi 18:157, Ad-Durr Al-Manthur 8:194.

«وَلَا سَكْنِي»

“Wala nyumba” Na akamuamuru aimalizie eda yake kwenye nyumba ya Umm Sharik رضي الله عنها. Kisha akasema,

«بَلَكَ امْرَأَةٌ يَتَشَاهَا أَصْحَابِي، اغْتَدِي عِنْدَ ابْنِ أُمِّ مَكْتُومٍ، فَإِنَّهُ رَجُلٌ أَعْمَى تَصْعِبُ
يَتَابِكَ»

“Mwanamke huyo anatembelewa na Masahaba zangu, kaa eda nyumbani kwa Ibn Umm Maktum, Yeye ni kipofu, hatakuona pindi utakapovua nguo zako.”¹

Imam Ahmad amekusanya Hadithi hii kwa kutumia isnadi tofauti. Katika mapokezi yake, Mtume ﷺ amesema,

«انظري يا بنت آل قيس إنما التَّفَقُّةُ وَالسُّكْنَى لِلْمَرْأَةِ عَلَى زَوْجِهَا، مَا كَانَتْ لَهُ عَلَيْهَا
رَجْعَةٌ، فَإِذَا لَمْ يَكُنْ لَهُ عَلَيْهَا رَجْعَةٌ فَلَا نَفَقَةَ وَلَا سَكْنَى، اخْرُجِي فَأَنْزِلِي عَلَى
فُلَانَةٍ»

“Angalia Ewe binti wa familia ya Qays! Matumizi na makazi yanatakiwa yatolewe na mume anayeweza kumreja mkewe. Kwa hiyo yeye hakuwa na haki ya kumreja, basi hawajibiki kumlisha na kumpa malazi. Kwa hiyo ihame nyumba yake na nenda kwa mwanamke fulani”. Kisha akasema,

«إِنَّهُ يَتَحَدَّثُ إِلَيْهَا، انزِلِي عَلَى ابْنِ أُمِّ مَكْتُومٍ فَإِنَّهُ أَعْمَى لَا يَرَاكَ»

“Yeye anazungumzishwa. Kwa hiyo nenda kwa Ibn Umm Makhtum, kwa kuwa yeye ni kipofu na hatokuona.”²

Abu Al-Qasim At-Tabarani amenukuu kutoka kwa Amir Ash-Shabi kwamba yeye alikwenda kwa Fatimah binti Qays رضي الله عنها, dadake Adh-Dhahhak bin Qays wa kabila la Quraysh. Fatimah رضي الله عنها aliolewa na Abu Amr bin Hafs bin Al-Mughirah رضي الله عنه kutoka Bani Makhzum. Alisema kuwa, “Abu Amir bin Hafs رضي الله عنه alinitaliki alipokuwa kwenye kikosi kilichokuwa Yemen. Niliwataka jamaa zake wanipe chakula na malazi.” Wakanjibu, “Hakututumia chochote

¹ Muslim na. 1480.

² Ahmad 6:373.

wala hakutaka tukusaidie.” Nikaenda kwa Mtume ﷺ na nikamuambia, “Ewe Mjumbe wa Allah! Abu Amr bin Hafs رضي الله عنه amenitaliki, na nikawataka jamaa zake wanipatie matumizi na makazi wakaniambia kuwa hawakupewa chochote.” Mtume ﷺ akasema,

إِنَّمَا السُّكْنَى وَالنَّفَقَةُ لِلْمَرْأَةِ إِذَا كَانَ لِزَوْجِهَا عَلَيْهَا رُجْعَةٌ، فَإِذَا كَانَتْ لَا
نَحْلٌ لَهَا حَتَّى تَنْكِحَ زَوْجًا غَيْرَهُ: فَلَا نَفَقَةَ لَهَا وَلَا سَكْنَى

“Si vinginevyo matumizi na makazi ni jukumu la mume kwa Mwanamke aliyeachwa Talaka rejea. Itakapotokezea kuwa si halali yake kumuoa isipokuwa mpaka kwanza aolewe na mume mwingine, basi hawajibiki kumpa matumizi na makazi.”¹

An-Nasai amenukuu Hadithi hii,²

فَإِذَا بَلَغْنَ أَجْلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ أَوْ فَارِقُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ وَأَشْهِدُوا ذَوَى عَدْلٍ مِّنكُمْ
وَأَقِيمُوا الشَّهَادَةَ لِلَّهِ ذَٰلِكُمْ يُوعَظُ بِهِ مَن كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَن يَتَّقِ
اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ﴿٦﴾ وَيَرْزُقْهُ مِن حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ
حَسْبُهُ إِنَّ اللَّهَ بَلِغٌ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا ﴿٧﴾

2. Basi wanapofikia muda wao, ima warejeeni muwaweke kwa wema, au farikianeni nao kwa wema. Na mshuhudishe mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu. Na simamisheni ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo Anavyoagizwa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na anayemcha Mwenyezi Mungu Humtengezea njia ya kutokea.

3. Na Humruzuku kwa jiha asiyotazamia. Na anayemtegemea Mwenyezi Mungu Yeye Humtosha. Hakika Mwenyezi Mungu Anatimiza Amri Yake. Mwenyezi Mungu Kajaalia kila kitu na kipimo chake.

¹ At-Tabarani in Al-Kabir 24:382.

² An-Nasai 6:144.

Amri ya Kumtendea Wema Mwanamke Aliyeachwa

Allah تعالى Amesema pindi wanawake itakapokaribia kuisha eda yao, mume anatakiwa apatane naye ili ndoa yao isivunjike.

بِمَعْرُوفٍ

“...kwa wema...”

Akimfanyia wema katika mahusiano yao. Vinginevyo aamue kumuacha kwa wema, bila kumnyanyasa, kumtusi au kumdhalilisha. Kinyume chake, amuache kwa hali nzuri, kwa wema na adabu.

Amri ya Kuwa na Mashahidi Wakati wa Kurejea

Allah تعالى Amesema,

وَأَشْهِدُوا ذَوَىٰ عَدْلٍ مِّنكُمْ

“...*Na mshuhudishe mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu...*”

Kwa maana: Unapoamua kumrejea mkeo. Abu Dawud na Ibn Majah wamenukuu kuwa Imran bin Husayn, aliulizwa juu ya mtu aliyemuacha mkewe kisha akajamiiana naye, bila kuwapa habari mashahidi kuhusu siku aliyomuacha na siku ya kumrejea. Imran akasema, “Kuacha na kurejea kwake kunapingana na Sunnah. Wahudhurishe mashahidi wakati wa kuacha na kurejea mke, na usirudie mwenendo wako huo.”¹ Ibn Jurayj amesema kuwa ‘Ata aliitolea maelezo Aya hii kwa kusema,

وَأَشْهِدُوا ذَوَىٰ عَدْلٍ مِّنكُمْ

“...*Na mshuhudishe mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu...*”

Si ruhusa kuo, kuacha au kumrejea mwanamke mpaka wawepo mashahidi wawili waadilifu, kama Alivyosema Allah تعالى, isipokuwa kunapokuwa na udhuru unaokubalika. Kauli ya Allah تعالى,

ذَٰلِكُمْ يُوعَظُ بِهِ مَن كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

“...*Hivyo ndivyo anavyoagizwa anayemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.*”

¹ Abu Dawud 2:637, Ibn Majah 1:652.

Maana yake: “Amri Yetu hii kwenu ya kuwa na mashahidi katika kadhia za namna hiyo, inatekelezwa na wale wanaomuamini Allah تعالى na Siku ya Mwisho.” Amri hii imekusudiwa kuwanufaisha wale wenye kuogopa adhabu ya Allah تعالى kesho Kiyama.

Allah تعالى Huwaruzuku na Kuwapa Mafanikio Thabiti Wanaomcha Yeye

Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ۖ وَيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ ۗ

**“...Na anayemcha Mwenyezi Mungu Humtengezea njia ya kutokea.
Na Humruzuku kwa jiha asiyotazamia...”**

Yeyote mwenye Taqwa ya Allah تعالى katika yale Aliyoyaamrisha na kuacha Aliyoyakataza, basi Allah تعالى Atamuwezesha kutoka katika kila aina ya matatizo na Kumpa mali ambazo hakuzitarajia au kuzifikiria.

Ibn Abi Hatim رضي الله عنه amenukuu kutoka kwa ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه kuwa alisema, “Aya inayojitoshleza ndani ya Quran ni,

❖ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ

**“Hakika Mwenyezi Mungu Anaamrisha kufanya (al-‘Adl) uadilifu,
na (al-Ihsan) hisani,...” (16:90)**

Aya kuu ndani ya Qur’an ambayo ina ujumbe wa kufariji ndani yake ni,

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ۖ

**“...Na anayemcha Mwenyezi Mungu Humtengezea njia ya
kutokea...” (65:2)**

Ikrimah pia ametolea maelezo Aya, “Yeyote anayetaliki kama Allah تعالى Alivyomuamuru, basi Allah تعالى Atamsahilishia njia ya kutoka katika matatizo.”¹ Hadithi sawa na hiyo ilipokelewa kutoka kwa Ibn Abbas na Adh-Dhahhak. ‘Abdullah bin Mas’ud na Masruq رضي الله عنهم wametolea maelezo Aya hii,

¹ At-Tabari 23:446.

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ﴿٦٥﴾

“...Na anayemcha Mwenyezi Mungu Humtengezea njia ya kutokea...” (65:2)

Kuwa inahusu pale mtu anapojua kuwa Allah تعالى Akitaka Hutoa na Akitaka Humnyima,

مِنْ حَيْثُ لَا تَحْتَسِبُ ۗ

“... kwa jiha asiyotazamia...”

Kutokana na mali ambayo hakuitarajia.¹ Oatadah amesema,

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ﴿٦٥﴾

“...Na anayemcha Mwenyezi Mungu Humtengezea njia ya kutokea...”

Maana yake: Kutokana na mashaka na vitisho watavyovipata wakati wa kutolewa roho,

وَيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ ۗ

“...Na Humruzuku kwa jiha asiyotazamia...”

Kutokana na kule asikotarajia.²

وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ ۗ

“Na anayemtegemea Mwenyezi Mungu Yeye humtosha...” (65:3)

Imam Ahmad amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema kuwa alipanda ngamia nyuma ya Mtume ﷺ. Naye akamuambia,

«يَا غُلَامُ! إِنِّي مُعَلِّمُكَ كَلِمَاتٍ: اخْفَظِ اللَّهَ يَحْفَظَكَ، اخْفَظِ اللَّهَ تَجِدْهُ تُجَاهَكَ، وَإِذَا سَأَلَ فَاسْأَلِ اللَّهَ، وَإِذَا اسْتَعْنَيْ فَاسْتَعِنْ بِاللَّهِ، وَاعْلَمْ أَنَّ الْأُمَّةَ لَوِ اجْتَمَعُوا عَلَى أَنْ يَنْفَعُوكَ لَمْ يَنْفَعُوكَ إِلَّا بِشَيْءٍ قَدْ كَتَبَهُ اللَّهُ لَكَ، وَلَوْ اجْتَمَعُوا عَلَى أَنْ يَضُرُّوكَ لَمْ يَضُرُّوكَ إِلَّا بِشَيْءٍ قَدْ كَتَبَهُ اللَّهُ عَلَيْكَ، رُوِيَ فِي الْأَقْلَامِ وَجَعَلَ الصُّحُفُ»

¹ At-Tabari 23:445, 446.

² At-Tabari 23:448.

“Ewe kijana nitakufundisha maneno (ujifunze). Mkumbuke Allah Naye Atakulinda, mkumbuke Allah Naye Atakuwa upande wako. Iwapo unaomba, muombe Allah, na unapotaka msaada, utake kutoka kwa Allah. Tambua kuwa Ummah ukikusanya nguvu ili kukusaidia, hautokunufaisha isipokuwa lile alilokuandikia Allah. Elewa kuwa ukikusanya nguvu ili kukudhuru hautokudhuru isipokuwa kama Allah Alikuandikia. Kalamu zimeshaandika na kurasa zimekauka.”¹

At-Tirmidhi amekusanya Hadithi hii na kuitaja kuwa ni “*Hasan Sahih*”.²

Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّ اللَّهَ بَلِّغُ أَمْرِهِ

“...*Hakika Mwenyezi Mungu Anatimiza Amri Yake...*”

Maana yake: Allah تعالى Atatekeleza Maamuzi na hukumu yake, kwa viumbe wake kwa namna apendavyo،

قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا ﴿٦٥﴾

“...*Mwenyezi Mungu Kajaalia kila kitu na kipimo chake...*”

Ni sawa na Kauli Yake،

وَكُلُّ شَيْءٍ عِنْدَهُ بِمِقْدَارٍ ﴿٦٦﴾

“...*Na kila kitu kwake ni kwa kipimo...*” (13:8)

وَالَّتِي يَبْسُ مِنْ الْمَحِيضِ مِنْ نُسَائِكُمْ إِنْ أَرْبَبْتُمْ فَعِدَّتُهُنَّ ثَلَاثَةُ أَشْهُرٍ وَالَّتِي لَمْ يَحْضَنْ

وَأُولَتْ الْأَحْمَالِ أَجَلُهُنَّ أَنْ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ ۚ وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مِنْ أَمْرِهِ يُسْرًا ﴿٦٧﴾

ذَلِكَ أَمْرُ اللَّهِ أَنْزَلَهُ إِلَيْنَا ۚ وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ سُبُلًا مَخْرُجًا مِنْهُ وَيُؤْتِهِ مِنْ أَمْوَالِهِ مَا يُغْنِيهِ ۚ وَاللَّهُ يُؤْتِي مَن يَشَاءُ ۚ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٦٨﴾

4. “Na wale waliosita hedhi miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka, basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, pamoja na ambao hawapati hedhi. Na wenye mimba eda yao mpaka

¹ Ahmad 1:293.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 7:219.

watakapozaa. Na anayemcha Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu Humfanyia mambo yake kuwa mepesi.

5. “Hiyo ni amri ya Mwenyezi Mungu Amekuteremshieni. Na anayemcha Mwenyezi Mungu Atamfutia maovu yake, na Atampa ujira mkubwa.”

Eda ya Waliokoma Hedhi na Wale Wasiopata Siku Zao

Allah تعالى Anafafanua eda ya mwanamke aliyekoma hedhi. Na huyo ni yule ambaye haoni siku zake zimekoma kutokana na umri wake kuwa mkubwa. Eda yake ni miezi mitatu badala ya mzunguko wa hedhi tatu kwa wanawake wanaoziona siku zao, kama ilivyoielezwa katika Ayah ya *Surat Al-Baqarah* (angalia 2:228). Pia kwa wasichana ambao hawajafikia miaka ya kupata hedhi. Eda yao ni miezi mitatu kama wale waliokoma. Hii ndio maana ya Kauli Yake,

وَأَلَّتِي لَمْ يَحْضَنْ^٤

“...Na wale waliosita hedhi...” (65:4)

Kama ilivyo katika Kauli Yake:

إِنْ أَرَبْتُمْ

“...ikiwa mnayo shaka...”

Kuna rai mbili: Kwanza, ni kauli ya kikundi cha *Salaf*, kama vile Mujahid, Az-Zuhri na Ibn Zayd. Ni kuwa wanapoona damu na wakatia shaka kuwa ilikuwa damu ya hedhi au damu ya ugonjwa¹. Na kama hujui hukumu ya kadhia hii, basi jua kuwa eda yao ni miezi mitatu. Hii ameikubali kutoka kwa Said bin Jubayr na rai yake ilipendelewa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى². Hii ndio maana iliyo sahihi zaidi.

Hadithi inayounga mkono rai hii ni iliyopokelewa³ kutoka kwa Ubay bin Ka'b kuwa amesema, “Ewe Mtume! Baadhi ya wanawake hawakutajwa ndani ya Qur'an, wasichana, ajuza na wenye mimba.” Allah تعالى akateremsha Aya hii,

¹ At-Tabari 23:450.

² At-Tabari 23:452.

³ Hayo na yanayofuata ameyasimulia kutoka kwa 'Amir bin Salim, ambaye imeelezwa kuwa hakuyasikia kutoka kwa Ubay, na masimulizi hayo yakaitwa Mursal.

وَأَلَّتِي يَيْسَنَ مِنَ الْمَحِيضِ مِنْ نِسَائِكُمْ إِنْ أَرْتَبْتُمْ فَعِدَّتُهُنَّ ثَلَاثَةُ أَشْهُرٍ وَالَّتِي لَمْ يَحْضَنْ
وَأُولَتْ الْأَحْمَالِ أَجَلُهُنَّ أَنْ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ^٤

“Na wale waliosita hedhi miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka, basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, pamoja na ambao hawapati hedhi. Na wenye mimba eda yao mpaka watakapozaa.”¹ (65:4)

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu masimulizi mafupi zaidi kuliko haya kutoka kwa Ubay bin Ka'b رضي الله عنه ambaye amesema, “Ewe Mtume! Wakati Aya ndani ya Surat Al-Baqarah iliposhushwa inayoelezea eda ya wanaoachwa, baadhi ya watu wa Madina walisema, “Bado kuna wanawake ambao eda zao hazijaainishwa ndani ya Qur’an. Wapo vigori, ajuza, ambao hedhi yao imekoma, na wajawazito.” Baadaye, Aya hii iliteremshwa,

وَأَلَّتِي يَيْسَنَ مِنَ الْمَحِيضِ مِنْ نِسَائِكُمْ إِنْ أَرْتَبْتُمْ فَعِدَّتُهُنَّ ثَلَاثَةُ أَشْهُرٍ وَالَّتِي لَمْ يَحْضَنْ^٤

“Na wale waliosita hedhi miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka, basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, pamoja na ambao hawapati hedhi.”² (65:4)

Iddah ya Mwanamke Mjamzito.

Kauli ya Allah تعالى،

وَأُولَتْ الْأَحْمَالِ أَجَلُهُنَّ أَنْ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ^٤

“...Na wenye mimba eda yao mpaka watakapozaa...” (65:4)

Allah تعالى Anasema, eda ya mwanamke mjamzito inaisha pale anapojifungua, ima ni kwa kutalikiwa au kufa kwa mumewe, kwa mjibu wa maafikiano ya wanazuoni walio wengi wa mwanzo kabisa (*salafu*) na waliokuja nyuma yao (*khalafu*). Maelezo haya yanaegemea kwenye Aya hii tukufu na katika Sunnah za Mtume ﷺ.

¹ At-Tabari 23:451.

² Al-Hakim 2:492.

Bukhari amenukuu kuwa Abu Salamah amesema, “Mtu mmoja alifika kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما wakati Abu Hurayrah رضي الله عنه alipokuwa pamoja naye na akauliza, “Nipe hukumu inayohusu mwanamke aliyezaa mtoto siku arobaini baada ya kufariki mume wake?” Ibn Abbas رضي الله عنهما akamjibu, “Eda yake inakwisha mpaka mwisho wa kipindi kirefu zaidi kati ya viwili vilivyoelezwa.” Nikasoma,

وَأَوْلَتْ الْأَحْمَالِ أَجْلُهُنَّ أَنْ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ

“...Na wenye mimba eda yao mpaka watakapozaa...”

Abu Hurayrah رضي الله عنه akasema, “Nakubaliana na binamu yangu (Abu Salamah).” Kisha Ibn Abbas رضي الله عنهما alimtuma mjakazi wake Kurayb kwa Umm Salamah رضي الله عنها ili amuulize. Akajibu, “Mume wa Subay’ah Al-Aslamiyyah رضي الله عنه aliuawa alipokuwa mja mzito, na alijifungua siku arobaini baada ya kifo chake. Kisha alipokea posa na Mtume ﷺ alimuozesha kwa mtu fulani. Abu As-Sanabil رضي الله عنه alikuwa mmoja wa waliotuma posa.”¹ Bukhari ameikusanya Hadithi hii kwa ufupi, ambayo Muslim na wanazuoni wengine wa Hadithi waliikusanya kwa urefu wake.²

Imam Ahmad amenukuu kuwa Al-Miswar bin Makhramah amesema, “Ubayah Al-Aslamiyah رضي الله عنهما alijifungua mtoto siku chache baada ya kifo cha mume wake. Alipomaliza nifasi, alichumbiwa. Hivyo aliomba ruksa kutoka kwa Mtume ﷺ ili aolewe, na aliruhusiwa kuolewa, hivyo aliolewa.”³ Bukhari amekusanya Hadithi hii kama walivyofanya Muslim, Abu Dawud, An-Nasai na Ibn Majah⁴ kwa isnadi tofauti kutoka Hadithi ya Subay’ah.

Muslim Al-Hajaj amenukuu kuwa Ubaydullah bin Abdullah bin Utbah amesema kuwa baba yake alimuandikia Umar bin Abdullah bin Al-Arqam Az-Zuhri, akimuomba aende kwa Subay’ah bint Al-Harith Al-Aslamiyah رضي الله عنها kumuuliza juu ya kadhia iliyokuwepo, na alivyojibiwa na Mtume ﷺ alipotaka hukumu ya jambo hilo,

Umar bin Abdullah alimuandikia Ubaydullah bin Abdullah bin Utbah akimpasha habari kuwa Subay’ah رضي الله عنها alimueleza kuwa aliolewa na Said bin Khawlah,

¹ Fat’hul Al-Bari 8:521.

² Fat’hul Al-Bari 9:379, Muslim 2:1123, Tuhfat Al-Ahwadhi 4:375, An-Nasai 6:192.

³ Ahmad 4:327.

⁴ Fat’hul Al-Bari 9:379, 7:360, Abu Dawud 2:728, An-Nasai 6:190, 196, Ibn Majah 1:654.

na alikuwa mmoja wa walioshiriki katika vita vya Badr. Alifariki dunia wakati wa Hija ya Kuaga wakati mkewe akiwa mjamzito. Mara baada ya kifo chake, alijifungua. Alijikwatua kwa wale ambao wanalipenda kumuoa. Abu As Sanabil bin Bakak رضي الله عنه alimuendea na kumuuliza, “Kwa nini amejikwatua? Unataka kuolewa tena? Wallah, huwezi kuolewa mpaka ipite miezi minne na siku kumi.”

Subay’ah رضي الله عنها akasema, “Aliponiambia hivyo, nilivaa mavazi ya jioni na nikaenda kwa Mtume ﷺ nikamuuliza kuhusu hukumu yake. Alinipa hukumu ya kidini kuwa nilikuwa naruhusiwa kuolewa baada ya kujifungua mtoto, akaniambia naweza kuolewa kama nataka.”¹ Haya ni masimulizi yaliyokusanywa na Muslim. Bakhari amekusanya Hadithi hii kwa ufupi.² Kauli ya Allah تعالى:

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ تَجْعَلْ لَهُ مِنْ أَمْرِهِ يُسْرًا ﴿١﴾

“Na anayemcha Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu Humfanyia mambo yake kuwa mepesi.”

Maana yake: Allah تعالى Atayafanya mambo yake mepesi na karibuni Atamletea nafuu na njia nyepesi ya kutoka katika matatizo,

ذَٰلِكَ أَمْرٌ أَلَّهِ أَنْزَلَهُ إِلَيْنَا ﴿٢﴾

“...Hiyo ni Amri ya Mwenyezi Mungu Amekuteremshieni...”

Maana yake: Hii ndiyo Amri Yake na Sharia ambayo Aliyowateremshia kupitia kwa Mjumbe wake ﷺ,

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَكْفِرْ عَنْهُ سَيِّئَاتِهِ وَيُعْظِمْ لَهُ أَجْرًا ﴿٣﴾

“Na anayemcha Mwenyezi Mungu Atamfutia maovu yake, na Atampa ujira mkubwa.”

Maana yake: Allah تعالى Atazuia Anachoogopa na Atazidisha malipo hata kwa kidogo akifanyacho.

* * *

¹ Muslim No. 1122.

² Fat’hul Al-Bari 9:379.

أَسْكِنُوهُمْ مِّنْ حَيْثُ سَكَنْتُمْ مِّنْ وَّجْدِكُمْ وَلَا تَضَارُّوهُمْ
 لِنَصِيْقُوا عَلَيْهِمْ وَإِنْ كُنْ أَوْلَتْ حَمَلٍ فَأَنْفِقُوا عَلَيْهِمْ حَتَّى
 يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ فَإِنْ أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ ۗ
 وَأَتَمِّرُوا بَيْنَكُم بِمَعْرُوفٍ وَإِن تَعَاَسَرْتُمْ فَاسْتَرْضِعْ لَهُ أٰخَرَى
 ۗ لِيُنْفِقَ ذُو سَعَةٍ مِّن سَعَتِهِ ۗ وَمَنْ قَدِرَ عَلَيْهِ رِزْقُهُ
 فَلْيُنْفِقْ مِمَّا آتٰهُ اللهُ لَا يَكْفِ اللهُ نَفْسًا إِلَّا مَا آتٰهَا ۗ
 سَيَجْعَلُ اللهُ بَعْدَ عُسْرٍ يُسْرًا ۝۱۰ وَكَأَيِّن مِّن قَرِيْبٍ عَنَتَ
 عَن أَمْرِ رَبِّهَا وَرُسُلِهِ فَحَاسِبْنَهَا حَسَابًا شَدِيْدًا وَعَدَبْنَهَا
 عَدَابًا نُكْرًا ۝۱۱ فَذَاقَتْ وَبَالَ أَمْرِهَا وَكَانَ عِقَبَةُ أَمْرِهَا
 خُسْرًا ۝۱۲ أَعَدَّ اللهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيْدًا فَاتَّقُوا اللهَ يَتَّقُوا
 اللهُ الَّذِيْنَ ءَامَنُوا ۗ قَدْ أَنْزَلَ اللهُ إِلَيْكُمْ ذِكْرًا ۝۱۳
 رَّسُولًا يَتْلُوا عَلَيْكُمْ ءَايٰتِ اللهِ مُبَيِّنَاتٍ لِّيُخْرِجَ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّٰلِحٰتِ مِنَ الظُّلُمٰتِ إِلَى النُّوْرِ ۗ وَمَنْ
 يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيَعْمَلْ صٰلِحًا يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا
 الْأَنْهَارُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا أَبَدًا ۗ قَدْ أَحْسَنَ اللهُ لَهُ رِزْقًا ۝۱۴
 اللهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمٰوٰتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ يَتَنَزَّلُ
 الْأَمْرُ بَيْنَهُنَّ لِتَعْلَمُوْا أَنَّ اللهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ وَأَنَّ اللهَ قَدْ
 أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا ۝۱۵

أَسْكِنُوهُمْ مِّنْ حَيْثُ سَكَنْتُمْ مِّنْ
 وَّجْدِكُمْ وَلَا تَضَارُّوهُمْ لِنَصِيْقُوا
 عَلَيْهِمْ وَإِنْ كُنْ أَوْلَتْ حَمَلٍ فَأَنْفِقُوا
 عَلَيْهِمْ حَتَّى يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ فَإِنْ
 أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ ۗ
 وَأَتَمِّرُوا بَيْنَكُم بِمَعْرُوفٍ وَإِن تَعَاَسَرْتُمْ
 فَاسْتَرْضِعْ لَهُ أٰخَرَى ۗ لِيُنْفِقَ ذُو
 سَعَةٍ مِّن سَعَتِهِ ۗ وَمَنْ قَدِرَ عَلَيْهِ
 رِزْقُهُ فَلْيُنْفِقْ مِمَّا آتٰهُ اللهُ لَا
 يَكْفِ اللهُ نَفْسًا إِلَّا مَا آتٰهَا ۗ
 سَيَجْعَلُ اللهُ بَعْدَ عُسْرٍ يُسْرًا ۝۱۰

6. "Wawekeni humo humo
 mnamo kaa nyinyi kwa
 kadiri ya pato lenu, wala
 msiwaletee madhara kwa
 kuwadhiki. Na wakiwa wana
 mimba, wagarimieni
 mpaka wajifungue. Na
 wakikunyonyesheeni, basi
 wapeni ujira wao, na
 shaurianeni kwa wema. Na
 mkiona uzito kati yenu, basi
 amnyonyeshe mwanamke
 mwengine.

7. “Mwenye wasaa atoe kadiri ya wasaa wake, na mwenye dhiki atoe katika Alichompa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Hamkalifishi mtu ila kwa kadiri ya Alichompa. Mwenyezi Mungu Atajaalia baada ya dhiki faraji.”

Mwanamke Aliye Katika Eda ya Talaka Rejea Atahudumiwa Kulingana na Kipato cha Mumewe

Allah تعالیٰ Anawaamrisha waja Wake waumini kuwa mmoja wao anapomtaliki mkewe, lazima ampe mahali pa kukaa mpaka kipindi cha eda kimalizike.

أَسْكُنُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ سَكَنْتُمْ

“...Wawekeni humo humo mnamo kaa nyinyi...”

Maana yake: Nawe,

مِنْ وُجَدِكُمْ

“...kwa kadiri ya pato lenu...”

Ibn Abbas رضي الله عنهما, Mujahid na wengineo wengi wamesema, inahusu, “Uwezo wako.”¹ Qatadah amesema, “Kama unamudu kumpa malazi kwenye kona ya nyumba yako basi fanya hivyo.”²

Imeharamishwa Kuwatendea Vibaya Wanawake Walioachwa.

Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَلَا تُضَارُّوهُنَّ لِتُضَيِّقُوا عَلَيْهِنَّ

“...wala msiwaletee madhara kwa kuwadhiki...”

Muqatil bin Hayyan amesema, “Maana yake: Usimkere ili ajikomboe wala usimfukuze kwenye nyumba yako.” Ath-Thawri amepokea kutoka kwa Mansur, kutoka kwa Abu Adh-Dhuha:

وَلَا تُضَارُّوهُنَّ لِتُضَيِّقُوا عَلَيْهِنَّ

“...wala msiwaletee madhara kwa kuwadhiki...”

“Anamtaliki, na siku chache zikibaki, anamrejea.”¹

¹ At-Tabari 23:457.

² Ad-Durr Al-Manthur 8:207.

³ Al-Qurtubi 18:168.

Mwanamke Mjamzito Aliyeachwa Talaka Isiyo ya Rejea ana Haki ya Kutunzwa na Mumewe mpaka Ajifungie.

Allah تعالى Amesema,

وَأَنْتِ كُنْتِ أَوْلَتْ حَمَلٍ فَأَنْفِقُوا عَلَيْهِنَّ حَتَّىٰ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ

“...Na wakiwa wana mimba, wagherimieni mpaka wajifungue...”

Swala hili linamhusu mwanamke aliyeachwa na hatorejewa. Iwapo ni mjamzito, basi ana haki ya kutunzwa mpaka atakapojifungua. Rai hii inaungwa mkono kwa sababu iwapo amepewa talaka rejea, ana haki ya kupewa matunzo bila kujali kuwa ni mjamzito au vinginevyo.

Mwanamke Aliyeachwa Anaweza Kuchukua Ujira wa Kumnyonyesha Mwanaye.

Allah تعالى Anasema,

فَإِنْ أَرْضَعْنَ لَكُمْ

“...Na wakikunyonyesheeni,...”

Maana yake: Wakati watakapojifungua hali ya kuwa wameachwa na kuisha eda zao, basi katika wakati huo wanaweza kunyonyesha mtoto ama hapana. Kwa sababu ni muhimu kwa afya ya mtoto. Kisha kama ataendelea kumnyonyesha atastahiki fidia. Anaruhusiwa kuingia mkataba na baba au mwakilishi wake kwa malipo watakayoridhiana.

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

فَإِنْ أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَكَاتِبْنَ لَهُنَّ أَجُورَهُنَّ

“...Na wakikunyonyesheeni, basi wapeni ujira wao...”

Allah تعالى Amesema,

وَأَتِمُّوا بَيْنَكُمْ بِمَعْرُوفٍ

“...na shaurianeni kwa wema...”

Maana yake: Masuala ya kuachana mume na mke yashughulikiwe kwa uadilifu mkubwa bila kuleta madhara kwa mmoja wao kama Allah تعالى Alivyosema katika Surat Al-Baqarah,

لَا تُضَارَّ وَالِدَةٌ بِوَالِدِهَا وَلَا مَوْلُودٌ لَهُ بِوَالِدِهِ^ع

“...Mama asitiwe taabuni kwa ajili ya mwanawe, wala baba kwa ajili ya mwanawe...” (2:233).

Allah تعالى Amesema,

وَإِنْ تَعَاَسَرْتُم فَاسْتَرْضِعْ لَهُ^ع أٰخْرٰى ﴿٦٥﴾

“...Na mkiona uzito kati yenu, basi amnyonyeshe mwanamke mwingine”

Endapo wawili hao walioachana hawatoafikiana, kwa sababu mwanamke anadai malipo makubwa ya kumnyonyesha mtoto wao, na baba anakataa kulipa kima au anatoa kima kisichoridhisha, anaweza kumtafuta mwanamke mwingine wa kumnyonyesha mtoto wake. Iwapo mama ataridhia malipo ambayo angelilipwa mwanamke mwingine kwa kumnyonyesha mtoto wao, mama ana haki zaidi ya kumnyonyesha mtoto wake.

Kauli ya Allah تعالى,

لِيُنْفِقَ ذُو سَعَةٍ مِّن سَعَتِهِ^ط

“...Mwenye wasaa atoe kadiri ya wasaa wake,...”

Ina maana: Baba mkwasi au muwakilishi wake amtunze mtoto kwa uwezo alionao,

وَمَنْ قُدِرَ عَلَيْهِ رِزْقُهُ فَلْيُنْفِقْ مِمَّا آتَاهُ اللَّهُ لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا مَاءً آتَنَهَا^ع

“Mwenye wasaa atoe kadiri ya wasaa wake, na mwenye dhiki atoe katika Alichompa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Hamkalifishi mtu ila kwa kadiri ya Alichompa.” (65:7)

Kama Allah تعالى Alivyosema,

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا مَاءً آتَنَهَا^ع

“Mwenyezi Mungu Haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri iwezavyo...”. (2:286)

Kisa cha Mwanamke Mchamungu

Kauli ya Allah تعالى،

سَيَجْعَلُ اللَّهُ بَعْدَ عُسْرٍ يُسْرًا ﴿٦﴾

“Mwenyezi Mungu Atajaalia baada ya dhiki faraji.”

Hii ni ahadi isiyo na shaka kutoka Kwake na kwa hakika, ahadi ya Allah تعالى ni ya kweli na Yeye kamwe Haivunji, haya ni Maneno ya Allah تعالى،

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٦﴾ إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٦﴾

“Basi kwa hakika pamoja na uzito upo wepesi. Hakika pamoja na uzito upo wepesi.” (94:5-6)

Kuna Hadithi Sahihi ambayo tutaitaja hapa. Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه، “Kulikuwa mtu na mkewe, masikini, katika vizazi vya mwanzo. Ikatokea siku moja mume aliporejea kutoka safari, na akamuendea mkewe na huku akiwa na njaa na machovu na kumuuliza, ‘Una chochote cha kula?’ Akamjibu, ‘Ndiyo, pokea habari njema za riziki toka kwa Allah تعالى.” Akamuambia tena, “Kama una chochote cha kula niletee!” Akamjibu, ‘Vuta subira.’ Alikuwa anangojea neema za Allah تعالى. Kadhia iliporefushwa, alimuambia, “Simama na uniletee chochote ulicho nacho nile, kwa sababu nina njaa mno na uchovu.” Akamjibu, “Nitakuletea. Karibuni nitafunua mfuniko wa oveni, usiwe na haraka.” Aliposhughulika na akaacha kumhimiza kwa muda, alijisemeza, “Hebu niangalie jiko langu.” Alisimama na kuangalia ndani ya jiko (oveni) na kukuta nyama ya kondoo imejaa na kinu kimejaa nafaka; na kilikuwa kinasaga nafaka chenyewe. Hivyo akachukua kilichokuwemo katika kinu baada ya kukitikisa na kutoa kila kilichokuwemo na pia kuchukua nyama kwenye oveni.” Abu Hurayrah رضي الله عنه aliongeza, ‘Kwa jina la Yule Ambaye maisha ya Abu Al-Qasim yako Mikononi Mwake! Kauli hii ni sawa na aliyosema Muhamad ﷺ،

«لَوْ أَخَذْتُ مَا فِي رَحِيئِهَا وَلَمْ تَنْفُضْهَا [لَطَحَّتْهَا] إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

“Kama angalichukua kilichomo ndani ya kinu chake bila kukitingisha, kingeendelea kusagisha nafaka mpaka Siku ya Kiyama.”¹

¹ Ahmad 2:421. Kuna toleo kama hilo Na. 10663. Isnadi zote mbili zina wapokezi wasio na hadhi.

وَكَايِن مِّن قَرْيَةٍ عَتَتْ عَن أَمْرِ رَبِّهَا وَرُسُلِهِ فَحَاسَبْتَنَهَا حِسَابًا شَدِيدًا وَعَذَّبْنَهَا عَذَابًا
 نُكْرًا ﴿٦﴾ فَذَاقَتْ وَبَالَ أَمْرِهَا وَكَانَ عَنَقِبَهُ أَمْرُهَا خُسْرًا ﴿٧﴾ أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ عَذَابًا
 شَدِيدًا ۖ فَاتَّقُوا اللَّهَ يَا أُولِيَ الْأَلْبَابِ الَّذِينَ ءَامَنُوا ۚ قَدْ أَنزَلَ اللَّهُ إِلَيْكُمْ ذِكْرًا ﴿٨﴾ رُّسُولًا
 يَتْلُوا عَلَيْكُمْ ءَايَاتِ اللَّهِ مَيِّبَتٍ لِّيُخْرِجَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى
 النُّورِ ۗ وَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيَعْمَلْ صَالِحًا يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ
 فِيهَا أَبَدًا ۖ قَدْ أَحْسَنَ اللَّهُ لَهُ رِزْقًا ﴿٩﴾

8. Na miji mingapi iliyovunja amri ya Mola wake Mlezi na Mitume wake, basi Tuliihisabia hisabu ngumu na Tukaiadhibu kwa adhabu kali.

9. Basi ikaunja ubaya wa mambo yake; na mwisho wa mambo yao ilikuwa khasara.

10. Mwenyezi Mungu Aliwaandalia adhabu kali. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, enyi wenye akili, mliaoamini! Hakika Mwenyezi Mungu Amekuteremshieni Ukumbusho,

11. Mtume anayekusomeeni Aya za Mwenyezi Mungu zinazobainisha, ili kuwatoa walioamini na wakatenda mema kutoka gizani kuwapeleka kwenye nuru. Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na akatenda mema, atamuingiza katika Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Mwenyezi Mungu Amekwishampa riziki nzuri.” (65:8-11)

Adhabu kwa Kuvunja Amri za Allah تعالى.

Allah تعالى Anawatisha wale wanaokiuka Amri Zake, kumkanusha Mjumbe Wake ﷺ na wanapinga Sharia Zake, kwa Kuwaeleza hatima ya ummah wa mwanzo uliofanya kama wao,

وَكَايِن مِّن قَرْيَةٍ عَتَتْ عَن أَمْرِ رَبِّهَا وَرُسُلِهِ

“Na miji mingapi iliyovunja amri ya Mola wake Mlezi na Mitume wake.” (65:8)

Maana yake: Waliyasi, walikataa, na kwa kiburi walimuasi Allah تعالى na hawakuwafuata Mitume Wake,

فَحَاسِبْنَهَا حِسَابًا شَدِيدًا وَعَذِّبْنَهَا عَذَابًا نُكْرًا ﴿٦٥﴾

“...basi Tuliihisabia hisabu ngumu na Tukaiadhibu kwa adhabu kali.”Maana yake: Kuogofya na kutisha,

فَذَاقَتْ وَبَالَ أَمْرِهَا

“...Basi ikauonja ubaya wa mambo yake..”

Maana yake: Walionja madhila ya kuasi na walijutia matendo yao wakati hayasaidii,

وَكَانَ عِقَابُهُ أَمْرًا خُسْرًا ﴿٦٦﴾ أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا ط

“...na mwisho wa mambo yao ilikuwa khasara. Mwenyezi Mungu Aliwaandalia adhabu kali...”

Maana: Siku ya Kiyama, wataongezewa adhabu kali zaidi ya walioipata hapa duniani. Allah تعالى Amesema, baada ya kutaja yaliyojiri kwa ummah uliokufuru,

فَاتَّقُوا اللَّهَ يَتَأُولَىٰ آلَآبِئِبٍ

“...Basi mcheni Mwenyezi Mungu, enyi wenye akili,...”

Maana yake: “Enyi wenye akili timamu, msiwe kama wao kwa sababu mkifanya hivyo, mtateseka kama walivyoteseka wao, “Enyi watu wenye kufahamu”,

الَّذِينَ ءَامَنُوا

“...mlio amini!...”Maana yake: Allah تعالى na Wajumbe Wake ﷺ.

قَدْ أَنْزَلَ اللَّهُ إِلَيْنَا ذِكْرًا ﴿٦٧﴾

“...Hakika Mwenyezi Mungu Amekuteremshieni Ukumbusho,...”

Maana yake: Qur’an hii. Aidha Allah تعالى Amesema,

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿٦٨﴾

“Hakika Sisi ndio Tulioteremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio Tutaoulinda.”(15:9)

Sifa za Mtume ﷺ

Kauli ya Allah تعالى

رَسُولًا يَتْلُوا عَلَيْكُمْ آيَاتِ اللَّهِ مُبَيِّنَاتٍ

“Mtume anayekusomeeni Aya za Mwenyezi Mungu zinazo bainisha,...”

Baadhi wamesema kuwa Mjumbe aliyefikisha ukumbusho. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa kilicho sahihi ni kwamba Mjumbe ndiye mchambuzi wa ukumbusho.¹ Allah تعالى Amesema hapa,

رَسُولًا يَتْلُوا عَلَيْكُمْ آيَاتِ اللَّهِ مُبَيِّنَاتٍ

“Mtume anayekusomeeni Aya za Mwenyezi Mungu zinazo bainisha,...”

Maana yake: Wazi na dhahiri. Kauli ya Allah تعالى;

لِيُخْرِجَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ^ع***“...ili kuwatoa walioamini na wakatenda mema kutoka gizani kuwapeleka kwenye nuru.”***

Maneno ya Allah تعالى;

كَتَبْنَا أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ لِتُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ

“Hiki ni Kitabu Tulichokiteremsha kwako ili uwatowe watu kwenye giza uwapeleke kwenye mwangaza,...” (14:1) na,اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ^ط***“Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Huwatoa gizani na Kuwaingiza mwangazani.” (2:257)***

Muradi wake, kutokana na kiza cha ukafiri na ujinga kwenda kwenye mwanga wa Imani na Ilimu. Allah تعالى Ameuita wahyi Aliouteremsha kuwa ni nuru, kwa kuwa ndani yake kunapatikana uongofu. Vile vile ameuita Roho, kwa kuwa, unaleta uhai katika nyoyo,

¹ At-Tabari 23:468.

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا ۗ مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا الْكِتَابُ وَلَا الْإِيمَانُ وَلَٰكِن جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِن عِبَادِنَا ۗ وَإِنَّكَ لَتَهْدَىٰ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٦٥﴾

“Na namna hivi Tumekufunulia Qur’ani kwa Amri Yetu. Ulikuwa hujui Kitabu ni nini, wala Imani. Lakini Tumekifanya kuwa ni Nuru ambayo kwayo Tunamuongoa Tumtakaye katika waja Wetu. Na hakika wewe unaongoa kwenye Njia Iliyonyooka.” (42:52)

Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ يُؤْمِنْ بِاللَّهِ وَيَعْمَلْ صَالِحًا يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ قَدْ أَحْسَنَ اللَّهُ لَهُ رِزْقًا ﴿٦٦﴾

“Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na akatenda mema, Atamuingiza katika Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Mwenyezi Mungu Amekwishampa riziki nzuri.”

Maelezo Yake: Yameshapita zaidi ya Mara moja huko nyuma, na kwa hiyo, hatuhitajii hapa Kuyarejea. Shukrani na sifa zote zinamstahiki Allah تعالى.

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَوَاتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ يَتَنَزَّلُ الْأَمْرُ بَيْنَهُنَّ لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا ﴿٦٧﴾

12. “Mwenyezi Mungu ni Yule ambaye Ameziumba mbingu saba, na ardhi kwa mfano wa hizo. Amri Zake zinashuka baina yao, ili mjue kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu, na kwamba Mwenyezi Mungu Amekizunguka kila kitu Kukijua vilivyo kwa Elimu Yake.” (65:12)

Ubainifu wa Uweza Timilifu wa Allah تعالى

Allah تعالى Anahabarisha kuhusu Uweza Wake na Ukuu usio na kikomo, ili hilo liwe chagizo la kuadhimisha sharia ya Dini Yake nyoofu.

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَوَاتٍ

“Mwenyezi Mungu ni Yule Ambaye Ameziumba mbingu saba...”

Allah تعالى Amesema katika Aya sawa na hizi, kama alivyowaambia Mtume Nuh عليه السلام watu wake,

أَلَمْ تَرَوْا كَيْفَ خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَوَاتٍ طِبَاقًا ﴿٦٥﴾

“Kwani hamuoni jinsi Mwenyezi Mungu Alivyoziumba mbingu saba kwa matabaka?” (71:15) na

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَوَاتُ الْأَسْفَلُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ

“Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vyote viliomo ndani yake.” (17:44) Kauli ya Allah تعالى,

وَمِنَ الْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ

“...na ardhi kwa mfano wa hizo...” (65:12) Maana yake: Aliumba ardhi saba.

Katika Sahihi mbili, kuna Hadithi inayosema,

«مَنْ ظَلَمَ قَيْدَ شَيْءٍ مِنَ الْأَرْضِ طُوقَهُ مِنْ سَبْعِ أَرْضِينَ»

“Mwenye kudhulumu ardhi ya mtu, hata kama ni shubiri, basi shingo yake itazungushiwa kipande hicho mpaka ardhi ya saba.”¹

Na katika Sahihi ya Bukhari maneno yaliyotumika ni;

«خُصِفَ بِهِ إِلَى سَبْعِ أَرْضِينَ»

“...atazamishwa chini mpaka ardhi ya saba.”

Mwanzoni mwa kitabu changu, *Al-Bidayah wan-Nihayah*, nilitaja mapokezi mbalimbali ya Hadithi hii niliposimulia kisa cha kuumbwa kwa dunia. Shukrani zote na sifa zinamstahiki Allah تعالى.

Wale waliyoelezea Hadithi hii kuwa na maana ya mara saba wameleta maelezo yasiyo ya kweli yanayopingana na maandiko ya Qur'an na Hadithi bila kuwapo ushahidi wowote.

Huu ndio mwisho wa Tafsiri ya *Surat At-Talaq*, Shukrani na Sifa zote zinamstahiki Allah تعالى.

¹ *Fat'hul Al-Bari* 5:124, *Muslim* 3:1232.

² *Fat'hul Al-Bari* 5:124.

³ *Al-Bidayah wan-Nihayah* 1:19, 20.

Tafsiri ya Suratu Tahrim Sura ya 66 Iliteremshwa Madinah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

يَتَأْتِيَ النَّبِيَّ لِمَ نَحَرِمُ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكَ ۖ تَتَّبِعِي مَرَضَاتِ
أَزْوَاجِكَ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١﴾ قَدْ فَرَضَ اللَّهُ لَكُمْ تَحِلَّةَ
أَيْمَانِكُمْ ۗ وَاللَّهُ مَوْلَانَا ۖ وَهُوَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٢﴾ وَإِذْ أَسْرَ
النَّبِيُّ إِلَىٰ بَعْضِ أَزْوَاجِهِ حَدِيثًا فَلَمَّا نَبَّأَتْ بِهِ وَأَظْهَرَهُ
اللَّهُ عَلَيْهِ عَرَفَ بَعْضَهُ ۖ وَأَعْرَضَ عَنْ بَعْضٍ فَلَمَّا نَبَّأَهَا
بِهِ قَالَتْ مَنْ أَنْبَأَكَ هَذَا ۗ قَالَ نَبَّأَنِي الْعَلِيمُ الْخَبِيرُ ﴿٣﴾
إِنْ تَتُوبَا إِلَى اللَّهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوبُكُمَا ۗ وَإِنْ تَظَاهَرَا عَلَيْهِ
فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ مَوْلَانَا وَجِبْرِيلُ وَصَلِحُ الْمُؤْمِنِينَ ۗ
وَالْمَلَائِكَةُ بَعْدَ ذَلِكَ ظَهِيرٌ ﴿٤﴾ عَسَىٰ رَبُّهُ إِنْ طَلَّقَكُنَّ
أَنْ يُبَدِّلَهُ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِنْكُنَّ مُسَلِّمَاتٍ مُؤْمِنَاتٍ قَدِيحَاتٍ
تَتَّبِعْنَ عِبْدَاتٍ سَخِيحَاتٍ تَتَّبِعْنَ تَتَّبِعْتَ وَأَبْكَارًا ﴿٥﴾

يَتَأْتِيَ النَّبِيَّ لِمَ نَحَرِمُ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكَ ۖ تَتَّبِعِي مَرَضَاتِ
أَزْوَاجِكَ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١﴾ قَدْ فَرَضَ اللَّهُ لَكُمْ
تَحِلَّةَ أَيْمَانِكُمْ ۗ وَاللَّهُ مَوْلَانَا ۖ وَهُوَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٢﴾
وَإِذْ أَسْرَ النَّبِيُّ إِلَىٰ بَعْضِ أَزْوَاجِهِ حَدِيثًا فَلَمَّا نَبَّأَتْ
بِهِ وَأَظْهَرَهُ اللَّهُ عَلَيْهِ عَرَفَ بَعْضَهُ ۖ وَأَعْرَضَ عَنْ بَعْضٍ
فَلَمَّا نَبَّأَهَا بِهِ قَالَتْ مَنْ أَنْبَأَكَ هَذَا ۗ قَالَ نَبَّأَنِي
الْعَلِيمُ الْخَبِيرُ ﴿٣﴾ إِنْ تَتُوبَا إِلَى اللَّهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوبُكُمَا ۗ
وَإِنْ تَظَاهَرَا عَلَيْهِ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ مَوْلَانَا وَجِبْرِيلُ وَصَلِحُ
الْمُؤْمِنِينَ ۗ وَالْمَلَائِكَةُ بَعْدَ ذَلِكَ ظَهِيرٌ ﴿٤﴾ عَسَىٰ رَبُّهُ
إِنْ طَلَّقَكُنَّ أَنْ يُبَدِّلَهُ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِنْكُنَّ مُسَلِّمَاتٍ
مُؤْمِنَاتٍ قَدِيحَاتٍ تَتَّبِعْنَ تَتَّبِعْتَ وَأَبْكَارًا ﴿٥﴾

عَلَيْهِ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ مَوْلَانَا وَجِبْرِيلُ وَصَلِحُ الْمُؤْمِنِينَ ۗ وَالْمَلَائِكَةُ بَعْدَ ذَلِكَ ظَهِيرٌ ﴿٤﴾ عَسَىٰ رَبُّهُ
إِنْ طَلَّقَكُنَّ أَنْ يُبَدِّلَهُ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِنْكُنَّ مُسَلِّمَاتٍ مُؤْمِنَاتٍ قَدِيحَاتٍ تَتَّبِعْنَ تَتَّبِعْتَ وَأَبْكَارًا ﴿٥﴾

1. Ewe Nabii! Kwa nini unaharimisha Alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu? Unatafuta kuwaridhi wake zako. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.

2. Hakika Mwenyezi Mungu Kakupeni Sharia ya kufungua viapo vyenu, na Mwenyezi Mungu ni Mola wenu. Na Yeye ni Mwenye Kujua, Mwenye Hikima.

3. Na Nabii alipomuambia mmoja wa wake zake jambo la siri. Basi alipolitangaza yule mke, na Mwenyezi Mungu Akamdhihirishia Mtume, Alimjuvya sehemu na Akaacha sehemu nyengine. Alipomuambia hayo, huyo mke akasema: Nani aliyekuambia haya? Mtume akasema: Kaniambia Mjuzi Mwenye khabari zote!

4. Kama nyinyi wawili hamkutubia kwa Mwenyezi Mungu, basi nyoyo zenu zimekwisha elekea huko. Na mkisaidiana dhidi yake (Mtume), basi hakika Mwenyezi Mungu Ndiye kipenzi chake, na Jibrili, na Waumini wema, na zaidi ya hayo Malaika pia watasaidia.

5. Asaa Mola wake Mlezi, akikupeni talaka, akampa wake wengine badala yenu nyinyi, waliobora kuliko nyinyi, wanyenyekevu, Waumini, wat'awa, waliotubu, wenye kushika ibada, wafanyao kheri, wajane na wanawari.

Allah تعالیٰ Anamkosoa Mtume Wake kwa Kuharamisha Halali Pamoja na Kubainisha Kafara Yake, na Kuwaadabisha Wakeze kwa Kumsumbua.

Katika mlango wa Viapo na Nadhiri Bukhari amenukuu kuwa Ubayd bin Umayr amesema kuwa alimsikia Aishah رضي الله عنها akidai kuwa Mtume ﷺ alikuwa akikaa kidogo katika nyumba ya Zaynab binti Jahshi رضي الله عنها na akinywa asali humo (akasema), "Hafsah رضي الله عنها na mimi tulikubaliana kuwa Mtume ﷺ atakapoingia ndani ya moja ya nyumba zetu, tuseme, 'Nasikia unanuka harufu ya *Maghafir*. Je, umekula *Maghafir*?' Alipoingia nyumbani kwa mmoja wetu, alimuambia maneno hayo. Akamjibu:

«لَا، بَلْ شَرِبْتُ عَسَلًا عِنْدَ زَيْنَبَ بِنْتِ جَحْشٍ وَلَنْ أَعُودَ لَهُ»

"Hapana, lakini nilikunywa asali kwa Zaynab bint Jahsh na sitoinywa tena."

Kisha Aya hii iliteremshwa;

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ لِمَ نَحْرِمُ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكَ

“Ewe Nabii! Kwa nini unaharimisha Alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu?” mpaka,

إِنْ تَتُوبَا إِلَى اللَّهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوبُكُمَا

“Kama nyinyi wawili hamkutubia kwa Mwenyezi Mungu, basi nyoyu zenu zimekwishaelekea huko.”

Kwa kuwaambia Aishah na Hafsah رضي الله عنهما.

وَإِذْ أَسْرَأَ النَّبِيُّ إِلَى بَعْضِ أَزْوَاجِهِ حَدِيثًا

“Na Nabii alipomuambia mmoja wa wake zake jambo la siri.”

Ambayo inaturejesha katika kauli hii,

«بَلْ شَرِبْتُ عَسَلًا»

“Lakini nimekunywa asali.”

Ibrahim bin Musa amesema kuwa Hisham amesema kuwa sikuwa na maana ya kauli yake,

«وَلَنْ أَعُودَ لَهُ وَقَدْ حَلَفْتُ فَلَا تُخَيِّرِي بِذَلِكَ أَحَدًا»

“Sitoinywa tena, nimekula kiapo kwa hilo, kwa hiyo msimueleze yeyote jambo hilo.”¹

Bukhari ameandika Hadithi hii pia katika mlango wa Talaka.² Kisha akasema, **“Al-Maghafir ni aina ya maji ya majani na ndani ya Ar-Rimth (aina ya jamii ya mchungwa) ladha yake ni tamu.....”**

Al-Jawhari amesema, **“Urfut ni aina ya mti unaotoa Maghfur.”**

¹ Fat'hul Al-Bari 11:572.

² Fat'hul Al-Bari 9:287.

Muslim alipokea Hadithi hii kutoka kwa Aishah رضي الله عنها katika mlango wa Talaka katika Sahihi yake, na maneno yake ni sawa na ya Bukhari katika mlango wa Viapo na Nadhiri.¹

Katika Kitabu cha Talaka, Bukhari amenukuu kuwa Aishah رضي الله عنها amesema, "Mtume ﷺ alipenda vitu vitamu na asali. Baada ya kusali Asr alikuwa na kawaida ya kuwatembelea wakeze, na kuwa karibu na mmoja wao. Hivyo alikwenda kwa Hafsah رضي الله عنها, binti wa Umar رضي الله عنه, na alikaa naye kwa muda mrefu kinyume na ada. Mimi (Aishah رضي الله عنها) niliona wivu na nikaulizia suala lile. Niliambiwa, "Mwanamke wa familia yake alimpelekea chombo kidogo chenye asali kama zawadi, na alimpa Mtume ﷺ kinywaji cha asali." Nikasema, 'Wallahi, tutaunda njama dhidi yake. 'Nikamuambia Sawdah bint Zam'ah رضي الله عنها, 'Mtume ﷺ atakapotembelea na akikukaribia mwambie, "Je, umekula *Maghafir*? Na atakapokujibu, "Hapana', kisha muulize, "Hii harufu ni ya nini?" Atakuambia, 'Hafsah رضي الله عنها amenipa kinywaji cha asali." Kisha umuambie, "Nyuki huenda wamekula *Urfut*, na mimi nitamuambia vivyo hivyo. Nawe Safiyah رضي الله عنها lazima useme hivyo, "Sawdah رضي الله عنها akasema baadaye, umenilazimisha kusema maneno uliyoniambia; punde kwa uwezo wa Allah تعالى, alikuwa amesimama mlangoni kwangu. Hivyo Mtume ﷺ alipomsogelea, akasema, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Je, umekula *Maghafir*?' Akajibu 'Hapana' Akasema tena, 'Basi hii ni harufu gani?' Akasema,

«سَقَّتْنِي حَفْصَةُ شُرْبَةَ عَسَلٍ»

'Hafsah alinipa asali nikanywa.' Akasema, "Huenda nyuki walikula '*Urfut*'.

Aishah رضي الله عنها akaendelea kusema, "Alipokuja kwangu nilimuambia vivyo hivyo. Kisha alimzuru Safiyah رضي الله عنها, naye alisema maneno yale yale. Alipomtembelea tena Hafsah, akamuambia, 'Ewe Mtume ﷺ, Je, nikupe tena asali?' Akajibu,

«لَا حَاجَةَ لِي فِيهِ»

"Sina haja nayo tena". Sawdah رضي الله عنها akasema, 'Wallah! Tumemzuia asinywe asali." Nikamuambia, "Nyamaza."² Muslim pia amenukuu Hadithi hii³, lakini maneno haya ni kutoka kwa Bukhari.

¹ Muslim 2:1100.

² *Fat'hul Bari*: 9:287.

³ Muslim 2:1101, 1102.

Katika masimulizi ya Muslim, Aishah رضي الله عنها amesema, “Mtume ﷺ alikuwa akichukia harufu mbaya kutoka kinywani mwake.”¹

Ndio maana walimuuliza kama alikula *Maghafir*, kwa sababu inasababisha harufu mbaya. Aliposema,

«بَلْ شَرِبْتُ عَسَلًا»

“Hapana, nimekunywa asali.” Wakasema kuwa nyuki walikula mti unaoitwa *Al-Urfut* ambao una utomvu wa *Maghafir*. Wakiashiria kuwa hiyo ndiyo sababu ya harufu mbaya waliyodai ikitoka kwake.

Masimulizi yaliyopokelewa kupitia kwa Urwah kutoka kwa Aishah رضي الله عنها, yanamtaja Hafsa رضي الله عنها kuwa ndiye aliyempa Mtume ﷺ asali.

Katika mapokezi mengine yaliyopokelewa kutoka kwa Ubayd bin Umayr, kutoka kwa Aishah رضي الله عنها, alikuwa Zainab bint Jahsh رضي الله عنها ndiye aliyempa asali Mtume ﷺ bali Aishah رضي الله عنها na Hafsa رضي الله عنها waliunda njama. Allah تعالى Ndiye Mjuzi wa yote. Baadhi wanaweza kusema kuwa yalikuwa matukio mawili tofauti. Hata hivyo, haiyumkini kuwa wao wawili ndio sababu ya kushushwa aya hii. Allah تعالى Anajua zaidi.

Hadithi ambayo Imam Ahmad aliyoikusanya katika Musnad inataja kuwa Aishah na Hafsa رضي الله عنهما ndio waliopanga njama zile. Imam Ahmad amenukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, “Nilikuwa na pupa ya kumuuliza Umar رضي الله عنه juu ya wake wawili miongoni mwa wakeze Mtume ﷺ ambao Allah تعالى Amesema kuhusu wao,

إِنْ تَتُوبَا إِلَى اللَّهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوبُكُمَا^ط

“Kama nyinyi wawili hamkutubia kwa Mwenyezi Mungu, basi nyoyo zenu zimekwisha elekea huko.”

Kisha nilifanya Hajj pamoja na Umar رضي الله عنه, na wakati wa kurejea kutoka Hajj alikwenda pembeni (kujisaidia). Nami pia nilimfuata nikiwa na birika la maji alipomaliza na kurejea, nilimmiminia maji mikononi akatawadha. Nikamuambia, ‘Ewe Kiongozi wa waumini! Ni wake gani wawili miongoni mwa wakeze Mtume ﷺ ambao Allah تعالى Aliwaambia, kwa kusema;

¹ Muslim 2:1102.

إِن تَتُوبَا إِلَى اللَّهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوبُكُمَا^ط

“Kama nyinyi wawili hamkutubia kwa Mwenyezi Mungu, basi nyoyo zenu zimekwisha elekea huko.”

Umar رضي الله عنه akamjibu, “Nimefadhaishwa na swali lako, Ewe Ibn Abbas.” Az-Zuhri (mpokezi) amesema kuwa Umar رضي الله عنه hakupendezewa na swali lile, lakini alilijibu, akisema kuwa walikuwa Aishah na Hafsa رضي الله عنهما.

Kisha Umar رضي الله عنه akaendelea kusimulia hadithi na akasema, “Sisi Maqureysh, tulikuwa na mamlaka juu ya wake zetu. Lakini tulipoishi na Ansari, tukagundua kuwa wanawake wa Ansari walikuwa na mamlaka kwa wanaume wao, hivyo wanawake zetu wakaanza kuiga tabia za wanawake wa Ansari. Wakati huo nilikuwa nikiishi katika nyumba ya Ummayah bin Zayd sehemu ya Al-Awali.¹ Wakati mmoja nilimkasirikia mke wangu, na akanijibu, nilichukizwa na majibu yake. Amesema, “Kwa nini unachukizwa na kujibiwa nami? Wallah wakeze Mtume ﷺ wanamjibu na baadhi yao wanaweza wasipate kusema naye kwa siku nzima, mpaka usiku.”

Kisha nikaenda kwa Hafsa رضي الله عنها na nikamuuliza, ‘Huwa unamjibu Mtume ﷺ’ Akajibu, ‘Ndiyo’. Nikamuuliza, ‘Kuna mmoja wenu anayemkasirisha Mtume ﷺ siku nzima mpaka usiku?’ Akajibu, ‘Ndiyo’. Nikasema, “Yeyote miongoni mwenu afanyaye hivyo ni mpotofu na ameangamia! Haogopi kuwa Allah تعالى Anaweza kumkasirikia kwa kumkasirisha Mjumbe Wake ﷺ, na hivyo ataangamizwa? Usimuulize Mtume ﷺ mambo mengi, na usibishane naye kwa hali yoyote ile. Niombe utakacho na usijaribu kumuiga jirani yako, kwani yeye ni mrembo kuliko wewe, na anapendwa zaidi na Mtume ﷺ kuliko wewe.” ‘Akimaanisha Bi Aishah رضي الله عنها.

“Mimi na jirani yangu wa Kiansari tulikuwa tukimzuru Mtume ﷺ kwa zamu. Alikuwa akienda siku moja na mimi nyingine. Nilipokwenda nilimletea habari ya yaliyojiri siku ile kuhusu wahyi naye hufanya kama hivyo.

Katika siku hizo kulikuwa na tetesi kuwa ukoo wa Ghassan ulikuwa ukiandaa farasi ili watuvamie. Sahibu wangu alikwenda na akarejea usiku na kubisha hodi. Nilitoka. Akaniambia jambo kubwa limetokea. Nikamuuliza, “ni jambo gani?” Ghassan, “Wamekuja?” Akajibu, “ni jambo baya kuliko hilo.” Na

¹ Sehemu iliyo upande wa kaskazini mashariki mwa Madinah

akaongezea kuwa, "Mtume ﷺ amewaacha wakeze wote." Nikasema, 'Hafsah ameharibikiwa! Nilitaraji hili lingelitokea siku moja.'

Hivyo nilivaa nikasali Subhi. Nikaenda kwa Hafsah رضي الله عنها na nikamkuta analia. Nikamuuliza, "Ati Mtume ﷺ amewataliki nyote?" Akajibu, "sijui." Yuko peke yake chumbani. Nilikwenda chumba kilichopo ghorofani na nikamuambia mtumishi wa Mtume ﷺ amuombe ruhusa ili nimuone, yule mvulana aliingia ndani kisha akatoka huku akisema, 'Nilimtaja jina lako lakini amenyamaza.' Nikatoka nje nikapanda juu ya Minbari nikawakuta watu wengi wameizingira na baadhi yao walikuwa wanalia.

Nilikaa nao kwa muda, lakini sikuweza kuvumilia hali ile. Hivyo nikamuambia yule mvulana, 'Muombe ruhusa Umar ya kuingia.' Akaja akanijibu, 'Nimekutaja lakini hakujibu kitu.' Kwa hiyo nikaenda kwenye Minbar na nikakaa na watu waliokuwa wamekaa karibu na Minbar, lakini sikuimudu hali ilivyo kuwa, hivyo nikaenda tena kwa yule kijana. 'Unaweza kumuomba ruhusa Umar?' Aliingia na akaleta jawabu kama za mwanzo. Nikaondoka na wala sikufika mbali yule kijana akaniita akaniambia ingia amekuruhusu. Hivyo nikaingia na nikamkuta amelala juu ya mkeka bila godoro, na mkeka umeacha alama juu ya mwili wa Mtume ﷺ.

Nikasema, "Umewataliki wakezo, Ewe Mtume?" Aliinua macho yake akanitazama na kujibu, "Hapana." Nikasema, "Allahu Akbar." Ewe Mtume ﷺ! Sisi Maqureysh tulikuwa tukiwadhibiti wanawake wetu. Lakini tulipokuja Madina, tuliwakuta watu ambao wanadhibitiwa na wake zao. Wanawake wetu wakaanza kujifunza tabia hiyo. Kuna wakati nilimkasirikia mke wangu, na alinijibiza. Sikuipeenda tabia ile na alisema, "Kwa nini unachukia nikikujibu? Wallahi, wakeze Mtume ﷺ wanamjibu na mmoja wao anaweza kumpuuza kwa siku nzima mpaka usiku." Nikamuambia, "Yeyote anayetenda hayo miongoni mwao amehasirika na kupotea! Hivi anajisikia salama kwa Allah تعالیٰ Kumkasirikia kwa sababu ya hasira za Mjumbe Wake? Kwa hali hiyo, ataangamia." Kwa hilo Mtume ﷺ alitabasamu.

Kisha nikanena, 'Ewe Mtume ﷺ! Nilikwenda kwa Hafsah na nikamuambia, 'Usijaribu (usishawishike) kumuiga mwenzio (Aishah) kwani yeye ni mrembo kuliko wewe na anapendwa zaidi na Mtume ﷺ.' Mtume ﷺ akatabasamu tena. Nilipomuona anatabasamu, nikasema, 'Hivi Mtume ﷺ unajisikia utulivu?' Akajibu, 'Ndiyo'. Nilikaa nikapiga jicho chumbani mwake kwa Jina la Allah

تعالى، sikuona kitu chochote cha thamani, isipokuwa ngozi tatu. Nikasema, 'Muombe Allah تعالى، Ewe Mtume, umma wako uwe na kipato kizuri, kwani waajemi na warumi ni wenye vipato vizuri na wana mengi katika mapambo ya dunia japokuwa hawamuabudu Allah تعالى.' Mtume ﷺ alikaa kitako na akasema,

«أَفِي سُبُكٍ أَنْتَ يَا ابْنَ الْخَطَّابِ! أَوْلَيْكَ قَوْمٌ عَجَلَتْ لَهُمْ طَيِّبَاتُهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا»

"Ewe Ibn Al-Khattab! Una shaka? Watu hao wameharakishiwa anasa zao hapa duniani tu."

Nilimuomba Mtume ﷺ, "Tafadhali niombe msamaha kwa Allah تعالى، Ewe Mtume ﷺ." Mtume ﷺ aliapa kuwa hatokwenda kwa wake zake kwa kipindi cha mwezi mmoja, kutokana na hasira aliyokuwa nayo dhidi yao, mpaka Allah تعالى Alipomkosoa."¹ Bukhari, Muslim, At-Tirmidhi na An-Nasai pia wameikusanya Hadithi hii kupitia njia tofauti za upokezi.¹¹ Bukhari na Muslim pia wameipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما، aliyesema, "Kwa mwaka mzima, nilikuwa na hamu ya kumuuliza Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه kuhusu Ayah hii. Hata hivyo, nilisita kwa kumheshimu. Mara moja alikwenda Hajj na nilifuatana naye. Wakati wa kurejea, alisimama kujisaidia nyuma ya miti ya Arak. Nilisimama mpaka alipomaliza kisha nikafuatana naye na nikamuuliza, 'Ewe kiongozi wa waumini! Ni wanawake gani wawili waliosaidiana kumfanyia njama Mtume?"² Hii ni Hadithi aliyoikusanya Bukhari, ambapo Muslim ameinukuu kuhusu wanawake wawili ambao Allah تعالى Amesema juu yao;

وَأِنْ تَظْهَرَا عَلَيْهِ

"Na mkisaidiana dhidi yake (Mtume)..."

"Umar رضي الله عنه alijibu, "Aishah na Hafsa رضي الله عنهما."³ Muslim kisha akaitaja sehemu iliyobaki ya Hadith. Pia Muslim amenukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema kuwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alimuambia, "Mtume ﷺ alipojitenga na wakeze. Nilingia Masjid na nikawakuta watu wakipiga ardhi kwa vijjiwe. Wakasema, 'Mtume ﷺ amewataliki wake zake.' Haya yalijiri kabla

¹ Ahmad:1:33,34.

² Fat'hul Al-Bari 9:187, 5:137, Muslim 2:111, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:224, An-Nasai katika Al-Kubra 5:366.

³ Fat'hul Al-Bari 8:525.

ya kufaradhihwa Hijab. Nikajisemea, lazima nichunguze habari hii leo. Kisha alitaja Hadithi ambayo alikwenda kwa Aishah na Hafsa رضي الله عنهما na akawashutumu. Kisha akasema, niliingia nikamkuta Rabah, mtumishi wa Mtume ﷺ amekaa kwenye kuzingiti cha dirisha. Nilimuita, 'Ewe Rabah, nitakie ruhusa kwa Mtume ﷺ."

Alitaja kisa kama tulivyokieleza hapo juu. Umar رضي الله عنه aliendelea, "Nilisema, 'Ewe Mtume, umepata matatizo gani kutoka kwa wakezo? Kama umewaacha, hakika Allah تعالى Yu pamoja nawe, Malaika Wake, Jibril عليه السلام, Mikail عليه السلام, Mimi, Abubakar na waumini wote wako pamoja nawe.'

Kila mara nilipozungumza, "Alhamdulillah", nilitaraji kuwa Allah تعالى Atayasadikisha maneno niliyoyatamka. Na hivyo Aya za kuhiyarishwa¹ zilishushwa. Allah تعالى Amesema,

عَسَىٰ رَبُّهُٖٓ إِن طَلَّقَكُنَّ أَن يُبَدِّلَهُٗٓ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِّنْكَ

"Asaa Mola wake Mlezi, akikupeni talaka, akampa wake wengine badala yenu nyinyi..." na,

وَإِن تَطَّهَّرَا عَلَيْهِ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ مَوْلَاهُ وَجِبْرِيلُ وَصَلِحُ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمَلَائِكَةُ بَعْدَ ذَلِكَ

ظَهْرًا ﴿٥﴾

"Na mkisaidiana dhidi yake (Mtume), basi hakika Mwenyezi Mungu Ndiye kipenzi chake, na Jibrili, na Waumini wema, na zaidi ya hayo Malaika pia watasaidia..."

Nilisema, 'Ewe Mtume, je, umewaacha?' Akajibu 'Hapana.' Nilisimama katika mlango wa Masjid nikasema kwa sauti ya juu kabisa: 'Mtume ﷺ hajawaacha wakeze.' Ilikuwa katika kipindi hiki, Aya hii iliteremshwa.

وَإِذَا جَاءَهُمْ أَمْرٌ مِّنَ الْأَمْنِ أَوْ الْخَوْفِ أَدَّعَوْا بِهٖ ۗ وَلَوْ رَدُّوهُ إِلَى الرَّسُولِ وَإِلَىٰ أُولَىٰ

الْأَمْرِ مِنْهُمْ لَعَلِمَهُ الَّذِينَ يَسْتَنْبِطُونَهُ مِنْهُمْ ۗ

"Na linapowafikia jambo lolote lililokhusu amani au la kitisho wao hulitangaza. Na lau kuwa wangelilipeleka kwa Mtume na kwa

¹ Kwa kumruhusu Mtume ﷺ kuchagua kati ya kuwaacha wakeze ama laa.

wenye mamlaka kati yao, wale wanaochunguza wangelilijua.”
(4:83)

Nilikuwa mimi niliyelielewa suala hili.¹ Habari sawa na hii imesemwa na Said bin Jubayr, Ikrimah, Muqatil bin Hayyan, Adh-Dhahhak na wengine.²

وَصَلِّحُ الْمُؤْمِنِينَ^ط

“...na Waumini wema ...”

Inaturejesha kwa Abubakar na Umar رضي الله عنهما. Al-Hassan Al-Basri رحمه الله تعالى ameongezea na Uthman رضي الله عنه. Layth bin Abi Sulaym amesema kuwa Mujahid anasema,

وَصَلِّحُ الْمُؤْمِنِينَ^ط

“...na Waumini wema ...” akiwemo na Ali bin Abi Talib رضي الله عنه.

Bukhari alinukuu kutoka kwa Anas رضي الله عنه alisema, ‘Umar رضي الله عنه alisema, “Wakeze Mtume ﷺ wote walikuwa na wivu kwa mvuto wake, na niliwaambia,

عَسَىٰ رَبُّهُ إِنْ طَلَّقَكُنَّ أَنْ يُبَدِّلَهُ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِّنْكَ

“Asaa Mola wake Mlezi, akikupeni talaka, akampa wake wengine badala yenu nyinyi...”

Baadaye, Aya hii iliteremshwa.³ Tulitaja kabla ya hapo kuwa Umar رضي الله عنه rai yake iliwafikiana na Qur’an katika kadhia kadhaa. Kwa mfano wahyi juu ya Hijab (angalia 33:53), na mateka wa kishirikina baada ya vita vya Badr (angalia 8:67). Ushauri wa Umar رضي الله عنه kufanya sehemu aliyosimama Ibrahim عليه السلام kuwa pahala pa Sala na Allah تعالى Akashusha Ayah hii,

وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلِّينَ^ط

“...Na alipo kuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia...”
(2:125).

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Anas رضي الله عنه amesema kuwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema, “Nilisikia kuwa Mama wa waumini

¹ Muslim 2:1105.

² At-Tabari 23:486.

³ Fat’hul Al-Bari 8:528.

waligombana na Mtume ﷺ. Hivyo niliwashauri, nikasema, ‘Ama muache kumbughudhi Mtume ﷺ au Allah تعالى Atampa wake bora kuliko nyinyi.’ Nilipokuwa nikizungumza na wa mwisho wao miongoni mwa Mama wa Waumini, aliniambia, ‘Ewe Umar! Ni kuwa Mtume ameshindwa kuwashauri wakeze, ili wewe uingilie kati baina yao?’ Niliacha baada ya kusikia hayo kutoka kwake, lakini Allah تعالى Akateremsha;

عَسَىٰ رَبُّهُ إِنْ طَلَّقَنَّ أَنْ يُبْدِلَهُ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِّنْكَ مِثْلَ مِمَّا مَنَنْتَ قَبْلَ تَبَيَّنَ تَبَيَّنَ

عِبْدَاتٍ سَيِّحَاتٍ تَبَيَّنَ وَأَبْكَارًا ﴿٥﴾

“Asaa Mola wake Mlezi, akikupeni talaka, akampa wake wengine badala yenu nyinyi, walio bora kuliko nyinyi, wanyenyekevu, Waumini, wat’awa, waliotubu, wenye kushika ibada, wafanyao kheri, wajane na wanawari.”¹

Mke aliyetajwa hapa alikuwa Umm Salamah رضي الله عنها na ndiye aliyemshauri Umar رضي الله عنه aache kuingilia kati ya Mtume ﷺ na wake zake, kama ilivyothibitishwa ndani ya Sahihi Al-Bukhari.²

Kauli ya Allah تعالى,

مُسَلِّمَاتٍ مُّؤْمِنَاتٍ قَلْبَتِ تَبَيَّنَ تَبَيَّنَ عِبْدَاتٍ

“Waumini, wat’awa, waliotubu, wenye kushika ibada...”

Ni wazi katika maana yake, ambapo,

سَيِّحَاتٍ

“...wafanyao kheri...”

Ina maana, kufunga, kwa mujibu wa Abu Hurayrah, Aishah, Ibn Abbas, Ikrimah, Mujahid, Said bin Jubayr, Ata, Muhammad bin Ka'b Al-Qurazi, Abu Abdur Rahman As-Sulami, Abu Malik, Ibrahim An-Nakhai, Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahak, Ar-Rabi bin Anas, As Suddi na wengine رضي الله عنهم.³

¹ At-Tabari 23: 488.

² Fat'hul Al-Bari 8:16.

³ At-Tabari 23:490, Al-Qurtubi 18:193, Ad-Dur Al-Manthur 8:224.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قُوًا أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا
النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلَائِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ لَا يَعْصُونَ
اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ﴿٦﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ كَفَرُوا
لَا تَعْتَذِرُوا الْيَوْمَ إِنَّمَا تُجْزَوْنَ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٧﴾ يَتَأْتِيهَا
الَّذِينَ ءَامَنُوا تُوْبُوا إِلَى اللَّهِ تَوْبَةً نَّصُوحًا عَسَىٰ رَبُّكُمْ
أَن يُكَفِّرَ عَنْكُم سَيِّئَاتِكُمْ وَيُدْخِلَكُم جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن
تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ يَوْمَ لَا يُخْزِي اللَّهُ النَّبِيَّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ
تُورُهُمْ يَسْعَىٰ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَيَأْيَمِيهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَنْتُمْ
لَنَا نُورٌ وَآغْفِرٌ لَنَا إِنَّا كُنَّا عَلَىٰ كَلِّ شَيْءٍ قَدِيرِينَ ﴿٨﴾
يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ جَاهِدَ الْكُفَّارَ وَالْمُنَافِقِينَ وَاغْلُظْ عَلَيْهِمْ
وَمَا أُوْنَهُمْ جَاهِدٌ وَبِئْسَ الْأَمِيرُ ﴿٩﴾ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا
لِّلَّذِينَ كَفَرُوا أَمْرَاتٍ نُّوحٍ وَامْرَأَتٍ لُّوطٍ كَاتَتَا تَحْتَ
عِبْدَتَيْنِ مِن عِبَادِنَا صَالِحَيْنِ فَخَانَتَاهُمَا فَلَمَّا بَغْيَانَا فِيهَا
مِنَ اللَّهِ شَيْفًا وَقِيلَ ادْخُلَا النَّارَ مَعَ الدَّاخِلِينَ ﴿١٠﴾
وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا أَمْرَاتٍ فِرْعَوْنَ إِذْ
قَالَتْ رَبِّ ابْنِ لِي عِدَدَكَ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ وَبِخْتِي مِن
فِرْعَوْنَ وَعَمَلِهَا وَبِخْتِي مِن الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿١١﴾
وَمَرْيَمَ ابْنَتَ عِمْرَانَ الَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنفَخْنَا فِيهِ
مِن رُّوحِنَا وَصَدَقْتَ بِكَلِمَاتِ رَبِّهَا وَكُتِبَ عَلَيْهَا مِن
الْقَنِينِ ﴿١٢﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قُوًا أَنفُسَكُمْ
وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا النَّاسُ
وَالْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلَائِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ
لَّا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ
مَا يُؤْمَرُونَ ﴿٦﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ كَفَرُوا
لَا تَعْتَذِرُوا الْيَوْمَ إِنَّمَا تُجْزَوْنَ مَا
كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٧﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ
ءَامَنُوا تُوْبُوا إِلَى اللَّهِ تَوْبَةً نَّصُوحًا
عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يُكَفِّرَ عَنْكُم
سَيِّئَاتِكُمْ وَيُدْخِلَكُم جَنَّاتٍ تَجْرِي
مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ يَوْمَ لَا يُخْزِي اللَّهُ
النَّبِيَّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ تُورُهُمْ
يَسْعَىٰ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَيَأْيَمِيهِمْ
يَقُولُونَ رَبَّنَا أَنْتُمْ لَنَا نُورٌ وَآغْفِرٌ
لَنَا إِنَّا كُنَّا عَلَىٰ كَلِّ شَيْءٍ قَدِيرِينَ ﴿٨﴾

6. Enyi mlioamini! Jilindeni nafi zenu na ahali zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wana-usimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa Anayowaamrisha, na wana-tenda wanayoamrisha.

7. Enyi mliokufuru! Msilete udhuru leo. Hakika mnalipwa mliyokuwa mkiyatenda.

8. Enyi mlio amini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli! Asaa Mola wenu Mlezi Akakufutieni maovu yenu na Akakuingizeni katika Pepo zipitazo mito kati yake, siku ambayo Mwenyezi Mungu Hatamdhalilisha Nabii na walioamini pamoja naye. Nuru yao inakwenda mbele yao na pande zao za kulia, na huku wanasema: Mola wetu Mlezi! Tutimilizie nuru yetu, na Utughufirie! Hakika Wewe ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.

Kuifundisha Familia Dini na Tabia Njema

Ali bin Abi Talhah amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما;

قُوا أَنْفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا

“...Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto...”

Alisema, “Mcheni Allah تعالى, na muepuke kumuasi Allah تعالى na muamrishe familia zenu kumkumbuka Allah تعالى, na Allah تعالى Atakuepusheni na Moto.”¹ Aidha Mujahid akiitolea maelezo.

قُوا أَنْفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا

“...Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto...”

Akisema, “Mcheni Allah تعالى na muwasie watu wenu kumcha Allah تعالى.”² Qatadah amesema, ‘Mnawaamuru utiifu kwa Allah تعالى, na kutomuasi Allah تعالى. Na kuwasimamia kutii amri za Allah تعالى na kuwasaidia kuzitekeleza amri hizo. Mmoja wenu anapona uasi, huuzuia na anawakataza wasiufanye.”³ Maneno kama hayo yamesemwa na Adh-Dhahhak na Muqatil; “Ni wajibu kwa Muislamu kuwafundisha aila yake, na watumwa wa kiume na kike yale Allah تعالى Aliyoyawajibisha kwao na yale Allah تعالى Aliyowaharamishia.”⁴

¹ At-Tabari 23:491.

² At-Tabari 23:492.

³ At-Tabari 23:492.

⁴ Al-Qurtubi 18:196.

Kuna Hadithi inayothibitisha maana ya Ayah hii. Ahmad, Abu Dawud na At-Tirmidhi wamenukuu kuwa Ar-Rabi bin Sabrah amesema kuwa baba yake amesema kuwa Mtume ﷺ amesema;

«مُرُوا الصَّبِيَّ بِالصَّلَاةِ إِذَا بَلَغَ سَبْعَ سِنِينَ، فَإِذَا بَلَغَ عَشْرَ سِنِينَ فَاضْرِبُوهُ عَلَيْهَا»

“Muamrishi ni mtoto kusali anapofikia umri wa miaka saba, na afikiapo miaka kumi wapigeni juu yake kwa kuacha kusali.”

Haya ni masimulizi yaliyokusanywa na Abu Dawud; At-Tirmidhi amesema, *“Hadithi Hasan.”*¹

Kuni za Motoni na Sifa za Malaika Wake

Allah تعالى Amesema;

وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ

“...kuni zake ni watu na mawe...” Inaonesha ya kuwa watoto wa Adam watakuwa kuni za kuwashia Moto,

وَالْحِجَارَةُ

“...na mawe...” Inarejelea kwenye masanamu yaliyokuwa yakiabudiwa, kama Allah تعالى Alivyosema katika Aya nyingine,

إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ

“Hakika nyinyi na hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni kuni za Jahannamu.” (21:98)

Abdullah bin Mas’ud, Mujahid, Abu Jafar Al-Baqir na As-Suddi رضي الله عنهم wamesema kuwa ni ‘mawe ya salfa’. Mujahid ameongeza mawe hayo ni kama, ‘mizoga’.² Kauli ya Allah تعالى

عَلَيْهَا مَلَتِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ

“...Wanausimamia Malaika wakali...”

Maana yake: Wana maumbile ya ukali kwa sababu huruma imetolewa kwenye mioyo yao kwa wale wasiomuamini Allah تعالى,

¹ Ahmah 3:404, Abu Dawud 1:332, Tuhfat Al-Ahwadhi 2:445.

² At-Tabari 1:381.

شِدَادٌ

“...wenye nguvu...” Maana yake: Maumbile yao yana nguvu na yanaogofya,

لَا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ﴿٦٦﴾

“...hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa Anayowaamrisha, na wanatenda wanayoamrisha.”

Maana yake: Chochote wanachoamrisha na Allah تعالى, wanapupia kumtii, bila kuchelewa hata kwa kupepesa jicho. Wanamudu kutekeleza amri; wanaitwa Az-Zabaniyah, yaani watumishi na walinzi wa Motoni. Allah تعالى Atupe hifadhi ya kuepukana nao.

Hakuna Udhuru Utokaokubaliwa Kutoka kwa Wasioamini Siku ya Kiyama.

Allah تعالى Amesema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَعْتَدِرُوا آلَيَوْمَ ۗ إِنَّمَا تُجْزَوْنَ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٦٧﴾

“Enyi mliokufuru! Msilete udhuru leo. Hakika mnalipwa mliyokuwa mkiyatenda.”

Muradi wake ni kuwa Siku ya Kiyama, makafiri wataambiwa, “Msitoe udhuru leo, kwa sababu hamtokubaliwa; mtalipwa kwa yale mliyokuwa mkiyafanya. Leo mtaadhibiwa kwa matendo yenu.”

Kushajiisha Toba ya Kweli.

Allah تعالى Amesema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا تُوْبُوْا إِلَىٰ اللَّهِ تَوْبَةً نَّصُوْحًا

“Enyi mlioamini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli!”

Maana yake: Toba ya kweli na yenye ithibati ambayo inafuta madhambi yaliyotangulia na kurekebisha upungufu wa mtu anayetubia, unamhimiza na kumuongoza kuacha uovu aliokuwa akiufanya. Allah تعالى Amesema,

عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَنْ يُكَفِّرَ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَيُدْخِلَكُم مِّنْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Asaa Mola wenu Mlezi Akakufutieni maovu yenu na Akakingizeni katika Pepo zipitazo mito kati yake...”

Na Allah تعالى Anaposema, **“Inaweza kuwa”**, Ina maana Atafanya.

يَوْمَ لَا تُخْزَىٰ اللَّهُ النَّبِيَّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ

“...siku ambayo Mwenyezi Mungu Hatamdhalilisha Nabii na walioamini pamoja naye...”

Maana yake: Siku ya Kiyama, Allah تعالى Hatowafedhehesha wale waliomuamini Mtume ﷺ.

نُورُهُمْ يَسْعَىٰ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ

“Nuru yao inakwenda mbele yao na pande zao za kulia...”

Kama tulivyoeleza katika Surat Al-Hadid,¹

يُقُولُونَ رَبَّنَا أْتَمَمْنَا نُورَنَا وَأَعْفِرْنَا لَنَا إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“...na huku wanasema: Mola wetu Mlezi! Tutimilizie nuru yetu, na Utughufirie! Hakika Wewe ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.”

Mujahid, Adh-Dhahhak na Al-Hasan Al-Basri na wengine wamesema, “Hii ndio kauli watakayosema waumini Siku ya Kiama, wakishuhudia nuru ya wanafiki ikizimika.”²

Imam Ahmad amenukuu kuwa mtu mmoja kutoka kabila la Banu Kinanah amesema, “Nilisali nyuma ya Mtume ﷺ wakati wa ufunguzi wa mji wa Makkah, na nilimsikia akisema,

اللَّهُمَّ لَا تُخْزِنِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Ewe Allah! Tafadhali usinifedheheshe Siku ya Kufufuliwa.”³

يَتَأْيَأُ النَّبِيُّ جِهْدَ الْكُفَّارِ وَالْمُنَافِقِينَ وَأَعْلَظَ عَلَيْهِمْ وَمَأْوَهُمْ جَهَنَّمُ وَبئسَ الْمَصِيرُ

ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا لِلَّذِينَ كَفَرُوا امْرَأَتَ نُوحٍ وَامْرَأَتَ لُوطٍ كَانَتَا تَحْتَ عَبْدَيْنِ

مِنْ عِبَادِنَا صَالِحِينَ فَحَاتَتْهُمَا فَلَمْ يُغْنِيَا عَنْهُمَا مِنَ اللَّهِ شَيْئًا وَقِيلَ ادْخُلَا النَّارَ مَعَ

الدَّٰخِلِينَ

¹ Angalia Juzuu ya nane, Tafsir ya Surat Al-Hadid (57:12).

² At-Tabari 23:496.

³ Ahmad 4:234.

9. Ewe Nabii! Pambana na makafiri na wanaafiki, na kuwa mgumu kwao! Na makaazi yao ni Jahannamu. Na hayo ni marejeo mabaya.

10. Mwenyezi Mungu Amewapigia mfano waliokufuru: mke wa Nuhu na mke wa Lut'i. Walikuwa chini ya waja wetu wema wawili miongoni mwa waja wetu. Lakini wakawahini waume wao, nao wasiwafae kitumbele ya Mwenyezi Mungu. Na ikasemwa: Ingieni Motoni pamoja na wanaoingia!

Amri ya Jihadi dhidi ya Makafiri na Wanafiki

Allah تعالیٰ Anamuamuru Mjumbe Wake ﷺ kupigana Jihadi dhidi ya makafiri na wanafiki hawa kwa silaha na kwa kusimamisha sheria za Allah تعالیٰ,

وَأَعِظْ عَلَيْهِمْ

"...na kuwa mgumu kwao!" Maana yake: Hapa duniani,

وَمَا لَهُمْ جَهَنَّمَ وَيْسَ الْمَصِيرُ ﴿٦٦﴾

"Na makaazi yao ni Jahannamu. Na hayo ni marejeo mabaya." Maana yake: Kesho Akhera.

Makafiri Hawatofaidika na Mahusiano ya Kindugu na Waumini Siku ya Ufufuo.

ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا لِّلَّذِينَ كَفَرُوا

"Mwenyezi Mungu Amewapigia mfano waliokufuru..."

Muradi wake ni kuwa, makafiri wanaoishi pamoja na Waislamu hapa duniani, kuchanganyika na Waislamu hakutowasaidia makafiri; wala hakutowasaidia kwa Allah تعالیٰ, mpaka hapo watakapokuwa na imani ndani ya nyoyo zao. Kisha Allah تعالیٰ Ametaja mfano kwa Kusema,

أَمْرَاتُ نُوحٍ وَأَمْرَاتُ لُوطٍ ۗ كَانَتَا تَحْتَ عَبْدَيْنِ مِنَّا مِنَّا صَالِحِينَ

"...mke wa Nuhu na mke wa Lut'i. Walikuwa chini ya waja wetu wema wawili miongoni mwa waja wetu..."

Maana yake: Walikuwa wake wa Mitume wawili na walikuwa wasaidizi wao mchana na usiku, wakila nao na kulala nao, kiasi kikubwa kama yalivyo

maingiliano kati ya mume na mke. Hata hivyo.

فَخَاتَّتَاهُمَا

“Lakini waliwahini wao” Kwa Maana: Hawakuafikiana na waume wao: katika Imani, na wala hawakuwasadikisha katika ujumbe wao. Hayo yote hayakuwanufaisha au kuwaondolea madhara. Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالیٰ Amesema:

فَلَمْ يُغْنِيَا عَنْهَا مِنَ اللَّهِ شَيْئًا

“...Nao wasiwafae kitu mbele ya Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Kwa sababu wake zao hawakuwa waumini,

وَقِيلَ

“Na ikasemwa...” Ikiwa na Maana: Kwa hawa wake,

أَدْخَلَا النَّارَ مَعَ الدَّٰخِلِينَ ﴿٦٦﴾

“Ingieni Motoni pamoja na wanao ingia!”

Sehemu ya Aya ambayo inasomeka,

فَخَاتَّتَاهُمَا

“Lakini wakawahini...” Si katika kufanya Zinaa, lakini kukataa kuingia katika dini. Bila shaka, wake wa Mitume walihifadhika kufanya zinaa kwa heshima aliyowapa Mitume Wake, kama tulivyoeleza katika *Surat An-Nur*.¹

Al-Awfi amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, “Waliwasaliti kwa kutofuata dini yao. Mke wa Mtume Nuh عليه السلام alikuwa akitoa siri zake, akiwafahamisha wapinzani wake kila mtu alipoingia katika dini ya Nuh عليه السلام. Ama kuhusu mke wa Mtume Lut عليه السلام, alikuwa akiwaeleza watu wa mji (Sodoma) ambao walifanya vitendo vya liwati, kila mgeni alipokirimiwa na mume wake.”² Adh-Dhahhak alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, alisema, “Hapana mke wa Mtume aliyepata kuzini. Bali waliwasaliti kwa kukataa kufuata dini yao.”³ Habari kama hizo zilinenwa na Ikrimah, Said bin Jubayr, Adh-Dhahhak na wengine.⁴

¹ Hayo yameelezwa kwa kifupi katika *Surat An-Nur* (24:26).

² At-Tabari 23:498.

³ At-Tabari 23:498.

⁴ At-Tabari 23:498.

وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا امْرَأَتَ فِرْعَوْنَ إِذْ قَالَتْ رَبِّ ابْنِ لِي عِنْدَكَ بَيْتًا فِي
الْجَنَّةِ وَنَجِّنِي مِنَ فِرْعَوْنَ وَعَمَلِهِ وَنَجِّنِي مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿١١﴾ وَمَرْيَمَ إِتَتْ
عِمْرَانَ الَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيهِ مِنْ رُوحِنَا وَصَدَّقَتْ بِكَلِمَاتِ رَبِّهَا وَكُتِبَ
وَكَانَتْ مِنَ الْغَابِطِينَ ﴿١٢﴾

11. Na Mwenyezi Mungu Amewapigia mfano walioamini - mkewe Firauni, aliposema: Mola wangu Mlezi! Nijengee Kwako nyumba Peponi, na Uniokoe na Firauni na vitendo vyake, na Uniokoe na watu madhaalimu.

12. Na Mariamu binti wa Imrani, aliyelinda ubikira wake, na Tukampulizia humo kutoka roho Yetu, na akayasadiki Maneno ya Mola Wake Mlezi na Vitabu Vyake, na alikuwa miongoni mwa watiifu.

Makafiri Hawawezi Kuwadhuru Waumini Mbele ya Allah تعالى

Huu ni mfano ambao Allah تعالى Ameumithilisha kwa waumini, kwamba uhusiano wao na makafiri hautowadhuru watawahitajia wao, kama Allah تعالى Alivyosema:

لَا يَتَّخِذِ الْمُؤْمِنُونَ الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ۗ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ فَلَيْسَ مِنَ
اللَّهِ فِي شَيْءٍ ۗ إِلَّا أَنْ تَتَّقُوا مِنْهُمْ تُقَاتًا ۗ

“Waumini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waumini. Na anayefanya hivyo, basi hatakuwa na chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ila ikiwa kwa ajili ya kujilinda na shari zao.”
(3:28)

Qatadah amesema, “Firaun alikuwa katili zaidi miongoni mwa watu wa dunia na kafiri mkubwa. Wa Llah! Mke wake hakuathirika na ukafiri wa mume wake kwa sababu alimtii Mola wake. Ili ipate kufahamika kuwa Allah تعالى ni Hakimu Muadilifu ambaye Hatomuadhibu yeyote isipokuwa kwa madhambi yake.”¹

¹ At-Tabari 23:500.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Sulayman alisema, "Mke wa Firauni aliteswa juani na Firauni alipomaliza kipindi cha kumtesa, malaika walimfunika kwa mbawa zao na alioneshwa nyumba yake ya Peponi."¹

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Al-Qasim bin Abi Bazzah amesema, "Mke wa Firauni alikuwa akiuliza, "Nani mshindi?" Alipoambiwa, Musa عليه السلام na Harun عليه السلام ndio walioshinda, akasema, "Ninamuamini Mola wa Musa عليه السلام na Harun عليه السلام." Firauni aliwapeleka walinzi wake na akawaambia, "Tafuteni jiwe kubwa. Kama ataendelea kuwa na imani yake, mpondeni na jiwe na kama atasita kusema kauli hiyo atabaki kuwa mke wangu. Walipomuendea, aliangalia mbinguni na aliweza kuona nyumba yake Peponi. Alisisitiza kuwa na imani yake. Na akatupiwa jiwe katika mwili usiokuwa na Roho."² Hii ndio maana ya Kauli Yake.

رَبِّ آيِنِ لِي عِنْدَكَ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ وَنَجِّنِي مِنْ فِرْعَوْنَ وَعَمَلِهِ

"...Mola wangu Mlezi! Nijengee kwako nyumba Peponi, na uniokoe na Firauni na vitendo vyake..."

Maana yake: 'Niondoshe kutoka kwake, kwa sababu sina hatia kwake.'

وَنَجِّنِي مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ

"...na uniokoe na watu madhaalimu."

Jina lake ni Asiyah bint Muzahim, Allah تعالى Amuwie radhi. Allah تعالى Amesema,

وَمَرْيَمَ ابْنَتَ عِمْرَانَ الَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا

"...Na Mariamu binti wa Imrani, aliyelinda ubikira wake..."

Kwa maana aliyejihifadhi na machafu.

فَنَفَخْنَا فِيهِ مِنْ رُوحِنَا

"...na Tukampulizia humo kutoka roho Yetu..."

¹ At-Tabari 23:500.

² At-Tabari 23:500. Angalia sehemu zenye masimulizi kama haya na yaliyotangulia katika kitabu hiki.

Maana yake: Kupitia malaika Jibril عليه السلام. Allah تعالى Alimtuma malaika Jibril عليه السلام kwa Maryam, na alifika kwake kwa sura ya mwanaume. Allah تعالى Alimuamrisha apulize kwa mdomo wake katika nguo yake na pumzi ile ilikwenda kwenye mfuko wa uzazi na sehemu zake za siri; hivi ndivyo mimba ya Isa عليه السلام ilivyopatikana. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

فَنَفَخْنَا فِيهِ مِنْ رُوحِنَا وَصَدَقْتَ بِكَلِمَاتِ رَبِّهَا وَكُتُبِهِ

“...na Tukampulizia humo kutoka roho Yetu, na akayasadiki maneno ya Mola Wake Mlezi na Vitabu Vyake ...”

Maana yake: Kwa Amri Yake.

وَكَانَتْ مِنَ الْقَانِتِينَ ﴿٦٦﴾

“...na alikuwa miongoni mwa wat’iifu. ...”

Imam Ahmad amenukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, “Mtume ﷺ alichora mistari minne juu ya ardhi na akasema,

«أَتَذُرُونَ مَا هَذَا؟»

“Je, mnajua mistari hii inawakilisha nini?”

Wakajibu, “Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ wanajua zaidi.” Yeye ﷺ akasema,

«أَفْضَلُ نِسَاءِ أَهْلِ الْجَنَّةِ: خَدِيجَةُ بِنْتُ خُوَيْلِدٍ، وَفَاطِمَةُ بِنْتُ مُحَمَّدٍ، وَمَرْيَمُ ابْنَةُ
عِمْرَانَ، وَأَسِيَّةُ بِنْتُ مُزَاحِمٍ امْرَأَةُ فِرْعَوْنَ»

“Wanawake bora wa Peponi ni Khadijah bint Khuwaylid, Fatimah bint Muhammad, Maryam bint Imran na Asiyah bint Muzahim, mkewe Fir’auni.”¹

Imethibiti katika Sahihi Mbili kutoka kwa Abu Musa Al-Ash’ari رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«كَمُلَ مِنَ الرِّجَالِ كَثِيرٌ وَلَمْ يَكْمُلْ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا أَسِيَّةُ امْرَأَةِ فِرْعَوْنَ، وَمَرْيَمُ ابْنَةُ
عِمْرَانَ، وَخَدِيجَةُ بِنْتُ خُوَيْلِدٍ، وَإِنَّ فَضْلَ عَائِشَةَ عَلَى النِّسَاءِ كَفَضْلِ الثَّرِيدِ عَلَى
سَائِرِ الطَّعَامِ»

¹ Ahmad 1:293.

“Wamekamilika Wanaume wengi na hawakukamilika miongoni mwa wanawake isipokuwa Asiyah mke wa Fir’auni, Maryam binti wa Imran, na Khadijah binti Khuwaylid. Na hapana shaka, ubora wa Aishah kwa wanawake wengine ni kama chakula cha Tharid kwa vyakula vingine.”¹

Katika kitabu changu, *Al-Bidayah wan-Nihayah*,² nilizitaja Hadithi hizi kwa kutumia isnadi tofuati kwa kusimulia kisa cha Mtume Isa عليه السلام na mama yake Maryam, amani iwe juu yao wote.

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu At-Tahrim*, Sifa zote Njema Anastahiki Allah تعالى.



¹ *Fat’h Al-Bari* 6:514, Muslim 4: 1886. *Tharid* ni chakula cha Kiarabu ambacho huandaliwa kwa mchuzi wa nyama na mkate.

² *Al-Bidayah wan-Nihayah* 2:61.

Tafsiri ya Suratul Mulk

Sura ya 67

Iliteremshwa Makkah

Sura hii inaitwa *Suratu Al-Mulk* kutokana na neno *Al-Mulk*, yaani Ufalme, linalotokea katika Aya ya kwanza katika Sura. Makusudio ya Sura hii tukufu ni kuelekeza fikra na nadhari zingatie athari ya Uweza wa Mwenyezi Mungu Uliozagaa katika nafsi za watu na katika viumbe vya Mwenyezi Mungu mnavyoviona katika ardhi na mbingu kwa upeo wa macho yenu, ili hayo yawe ndiyo njia ya kupelekea kumuamini Allah تعالى na Siku ya Mwisho. Na pia Sura hii inabainisha hali ya makafiri ambao watatupwa katika Jahannamu, na watakilizana mikoromo yao, na wataungua katika Moto wake, na wataungama madhambi yao, na watajuta kwa watavyoishia, watapowauliza Malaika kwa kutomuitikia Mtume ﷺ alipowaita na akawahadharisha.

Na ama waliomukhofu Mola wao Mlezi, na wakamuamini, hao watapata maghufira na msamaha kwa makosa yaliyowaporonyoka, na ujira mkubwa kwa mema waliyoyatanguliza na wakayatenda.¹

Fadhila za Suratul Al-Mulk

Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ سُورَةَ فِي الْقُرْآنِ ثَلَاثِينَ آيَةً شَفَعَتْ لِصَاحِبِهَا حَتَّى غُفِرَ لَهُ: ﴿بَبَّرَكَ الَّذِي يَبْدُو
الْمَلِكُ﴾»

“Hakika ndani ya Qur’an kuna sura yenye Aya thelathini itamuombea shufaa msomaji wake mpaka atasamehewa makosa yake. ‘Nayo ni, ‘Ametukuka ambaye Mkononi Mwake Umo Ufalme wote.’”²

Hadithi hii imekusanywa na *At-Tirmidhi* na wakusanyaji wanne wa Sunan. *At-Tirmidhi* ameizungumzia kuwa, “Hii ni Hadithi Hasan.”³

¹ Ahmad 2:321.

² Abuu Dawud 2:119, Tuhfatu Al-Ahwadhi 8:200, An-Nasai in Al-Kubra 6:496, na Ibn Majah 2:1244.

³ At-Tabarani katika Al-Aws 4:391.

At-Tabarani رحمه الله تعالى na Al-Hafiz Ad-Duja Al-Maqdisi رحمه الله تعالى wote waliinukuu kutoka kwa Anas رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«سُورَةُ فِي الْقُرْآنِ خَاصَمَتْ عَنْ صَاحِبِهَا حَتَّى أُدْخِلَتْهُ الْجَنَّةَ: ﴿تَبَرَّكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمَلَكُ﴾»

*“Kuna sura ndani ya Qur’an itamtetea msomaji wake hadi itamuingiza peponi, **‘Ametukuka Ambaye Mkononi Mwake Umo Ufalme wote.’**”¹*

* * *

¹ At-Tabarani katika *Al-Awsat* 4:391.

تَبْرَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمَلِكُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾
 الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۗ
 وَهُوَ الْعَزِيزُ الْغَفُورُ ﴿٢﴾ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقًا ۗ
 مَا تَرَى فِي خَلْقِ الرَّحْمَنِ مِنْ تَفَوُّتٍ ۗ فَارْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ
 تَرَى مِنْ فُطُورٍ ﴿٣﴾ ثُمَّ ارْجِعِ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنْقَلِبْ إِلَيْكَ
 الْبَصَرُ حَاسِمًا ۗ وَهُوَ حَسِيرٌ ﴿٤﴾ وَلَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا
 بِمَصْبِيحٍ ۗ وَجَعَلْنَاهَا رُجُومًا لِلشَّيْطَانِ ۗ وَأَعْتَدْنَا لَهُمْ
 عَذَابَ السَّعِيرِ ﴿٥﴾ وَلِلَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ عَذَابُ جَهَنَّمَ ۗ
 وَيُقَسَّ الْأَمْرُ ﴿٦﴾ إِذَا أُلْقُوا فِيهَا سَمِعُوا لَهَا شَهْقًا وَهِيَ
 تَفُورٌ ﴿٧﴾ تَكَادُ تَمَيَّزُ مِنَ الْغَيْظِ ۗ كُلَّمَا أُلْقِيَ فِيهَا فَوْجٌ
 سَأَلَتْهُمْ خَزَنَتُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَذِيرٌ ﴿٨﴾ قَالُوا بَلَىٰ قَدْ جَاءَنَا
 نَذِيرٌ فَكَذَّبْنَا وَقُلْنَا مَا نَزَّلَ اللَّهُ مِنْ شَيْءٍ إِنْ أَنتُمْ إِلَّا فِي
 ضَلَالٍ كَبِيرٍ ﴿٩﴾ وَقَالُوا لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِي
 أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿١٠﴾ فَأَعْرَفُوا بِذَنبِهِمْ فَسُحْقًا لِأَصْحَابِ
 السَّعِيرِ ﴿١١﴾

تَبْرَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمَلِكُ وَهُوَ عَلَى
 كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾ الَّذِي خَلَقَ
 الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ
 عَمَلًا ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْغَفُورُ ﴿٢﴾
 الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقًا ۗ
 مَا تَرَى فِي خَلْقِ الرَّحْمَنِ مِنْ تَفَوُّتٍ ۗ
 فَارْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ تَرَى مِنْ فُطُورٍ
 ﴿٣﴾ ثُمَّ ارْجِعِ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنْقَلِبْ
 إِلَيْكَ الْبَصَرُ حَاسِمًا وَهُوَ حَسِيرٌ ﴿٤﴾
 وَلَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصْبِيحٍ
 وَجَعَلْنَاهَا رُجُومًا لِلشَّيْطَانِ ۗ
 وَأَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابَ السَّعِيرِ ﴿٥﴾

1. *Ametukuka Ambaye Mkononi Mwake Umo Ufalme wote; na Yeye ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.*

2. *Ambaye Ameumba mauti na uhai ili Kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye Nguvu na Mwenye Msamaha.*

3. *Aliyeumba mbingu saba kwa matabaka. Huoni tafauti yoyote katika Uumbaji wa Mwingi wa Rehema. Hebu rudisha nadhari! Unaona kosa lolote?*

4. *Tena rudisha nadhari mara mbili, nadhari yako itakurejea mwenyewe hali ya kuwa imehizika nayo imechoka.*

5. *Na kwa hakika Tumeipamba mbingu ya karibu kwa mataa, na Tumeyafanya ili kuwapigia mashetani, na Tumewaandalia adhabu ya Moto uwakao kwa nguvu.*

Kumtukuza Allah تعالی na Kubainisha Kuumbwa kwa Mauti, Maisha, Mbingu na Nyota.

Allah تعالی Anajitukuza Mwenyewe na Anaeleza kuwa Utawala uko kwenye Mikono Yake. Hii ina maana kuwa Anashughulika na viumbe Wake namna Atakavyo na hapana awezaye kubadili Amri Yake. Haulizwi kwa yale Ayafanyayo kwa sababu ya Nguvu Zake, Hikima Zake na Uadilifu Wake. Allah تعالی Anasema,

وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٦٧﴾

“...na Yeye ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu...” Kisha Allah تعالی Anasema,

الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ

“...Ambaye Ameumba mauti na uhai...” Wale wanaosema kuwa kifo ni kiumbe kinachoishi wanatumia Ayah hii kwa sababu kimeumbwa. Inaonesha kuwa Allah تعالی Ameumba viumbe ambao hawakuwepo bila kitu ili Apate Kuwatahini viumbe. Anawachunguza ili Kuona yupi kati yao atafanya amali bora zaidi. Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالی,

كَيْفَ تَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَكُنْتُمْ أَمْوَاتًا فَأَحْيَاكُمْ ط

“Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu na hali mlikuwa wafu Akakufufueni!” (2:28)

Katika Aya hii Allah تعالی Ametaja hatua ya mwanzo, ambayo ni kutokuwepo kwa uhai ‘kifo’, na Ameitaja kuwa ni mwanzo wa kuwepo, “uhai”. Kwa ajili hiyo Allah تعالی Anasema,

ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٨﴾

“Kisha Atakufisheni, tena Atakufufueni, kisha Kwake mtarejeshwa?” (2:28). Kuhusu Kauli ya Allah تعالی,

لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ؕ

“...ili Kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi.”

Ina maana mbora wenu katika matendo. Hivi ni kama alivyosema Muhammad bin Ajlan. Inafaa izingatiwe kuwa Allah تعالی Hakusema, “ni nani kati yenu atendaye amali nyingi.” Kisha Allah تعالی Amesema,

وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّغْفُورُ ﴿٦٧﴾

“...Na Yeye ni Mwenye Nguvu na Mwenye Msamaha.”

Hii ina Maana: Yeye ni Mwenyezi, Mkubwa kabisa, Mwenye Nguvu Nyingi na Mtukufu zaidi. Pamoja na hayo, Ana Sifa ya Usamehevu zaidi kwa anayemgeukia Yeye kwa toba na anayeomba msamaha Wake baada ya kumuasi na kupinga Amri Zake. Hata hivyo Allah تعالى ni Muweza, pia Anasemehe, Ana Huruma, Anawia radhi. Kisha Allah تعالى Anasema,

الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَوَاتٍ طِبَاقًا ۗ

“Aliyumba mbingu saba kwa matabaka.”

Maana yake: Amepanga moja juu ya jingine. Je, Mbingu zimeungana, baadhi yao na nyingine?, au zimetenganishwa na kuwa na uwazi kati yao? Kuna rai mbili kuhusu hili, na rai iliyo sahihi zaidi inaelekea ni ya mwisho kwani imethibitishwa na Hadithi ya *Isra* (safari ya usiku ya Mtume) na masimulizi mengine. Kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

مَا تَرَىٰ فِي خَلْقِ الرَّحْمَنِ مِن تَفَوتٍ ۗ

“Huoni tafauti yoyote ya uumbaji wa Mwingi wa Rehema..”

Maana yake: Uumbaji huu umetimia usiokuwa na dosari, au hitilafu au kuachana ndani yake. Kwa sababu hiyo Allah تعالى Anasema,

فَارْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ تَرَىٰ مِن فُطُورٍ ﴿٦٨﴾

“Hebu rudisha nadhari! Unaona kosa lolote?”

Maana yake: Angalia mbingu na uzingatie kwa makini. Je, unaona dosari, upungufu uharibifu ndani yake? Ibn Abbas, Mujahid, Adh-Dhahak, Ath-Thawri na wengineo رضي الله عنهم walizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

فَارْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ تَرَىٰ مِن فُطُورٍ ﴿٦٨﴾

“Hebu rudisha nadhari! Unaona kosa lolote?” Hiyo ina Maana ya Nyufa.¹

¹ Ad-Dur Al-Manthur 8:235, Al-Qurtubi 18:209, na At-Tabari 23:507.

As-Suddi amesema kuwa,

هَلْ تَرَىٰ مِنْ فُطُورٍ ﴿٦٧﴾

“...**Unaona kosa lolote?**” Maana yake: Mipasuko.¹ Qatadah amesema,

هَلْ تَرَىٰ مِنْ فُطُورٍ ﴿٦٧﴾

“...**Unaona kosa lolote?**” Maana yake: Unaona dosari yoyote Ewe mwana wa Adam (binadamu)?

Kwa kurejea Kauli ya Allah تعالى،

ثُمَّ أَرْجِعَ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ

“**Tena rudisha nadhari mara mbili...**”

Qatadah amesema, “Ina maana (Angalia) mara mbili.”

يَنْقَلِبُ إِلَيْكَ الْبَصَرُ خَاسِئًا

“...**nadhari yako itakurejea mwenyewe hali ya kuwa imehizika...**”

Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema kuwa “**Khaasian**” Maana yake: Kufadhaishwa.² Mujahid na Qatadah wamesema ina maana, ‘lililochoka’.³

وَهُوَ حَسِيرٌ ﴿٦٨﴾

“...**nayo imechoka.**”

Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema hii ina maana itakwisha.⁴ Mujahid, Qatadah na As-Suddi wote walisema kuwa ina maana uchovu unaotokana na udhaifu. Hivyo, Aya ina maana kuwa ungeendelea kuangalia kwa muda mrefu uangaliaji wako ungerudi.

خَاسِئًا

“...**hali ya kuwa imehizika...**”

Kutokana na kutoweza kuona dosari (katika Alivyoumba Allah تعالى)،

وَهُوَ حَسِيرٌ ﴿٦٨﴾

“...**nayo imechoka.**”

¹ Al-Qurtubi 18:209.

² At-Tabari 23:507.

³ At-Tabari 23:507.

⁴ Ad-Dur Al-Manthur 8:235.

Maana yake: Amechoka na dhaifu kutokana na kutumia nguvu nyingi kuangalia bila kuona dosari yoyote. Kisha baada ya Allah تعالى Kukanusha kuwa hakuna udhaifu katika Kuumba mbingu, Anaelezea utimilifu na uzuri wake. Anasema,

وَلَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصْبِيحٍ

“Na kwa hakika Tumeipamba mbingu ya karibu kwa mataa...”

Hii inahusu nyota zilizowekwa mbinguni, baadhi zinazunguka na baadhi zimesimama. Katika Kauli ya Allah تعالى,

وَجَعَلْنَاهَا رُجُومًا لِلشَّيْطِينِ

“...na Tumeyafanya ili Kuwapigia mashetani...”

Na aina katika Nyota hizo Tumezifanya kuwa ni vimondo vinavyopigiwa mashetani. Na wala sio Nyota zote zilizo mbinguni hupigiwa mashetani. Na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Kuhusiana na Kauli ya Allah تعالى,

وَأَعْتَدْنَا لَهُم عَذَابَ السَّعِيرِ

“...na Tumewaandalia adhabu ya Moto uwakao kwa nguvu...”

Ina maana: ‘Tumewafedhehesha mashetani hapa duniani, na Tumewaandalia adhabu ya Moto mkali Siku ya Kiyama.’

Hivi ni kama Allah تعالى Alivyosema mwanzoni mwa Surat As-Saffat,

إِنَّا زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِزِينَةِ الْكَوَاكِبِ ۖ وَحِفْظًا مِّنْ كُلِّ شَيْطَانٍ مَّارِدٍ

“Hakika Sisi Tumeipamba mbingu ya karibu kwa pambo la nyota. Na kuihifadhi kwa kuilinda na kila shetani asi.” (37:6-7)

Qatadah amesema, “Nyota hizi ziliumbwa kwa madhumuni matatu: Allah تعالى Aliziumba kama mapambo ya mbingu, kama makombora kwa mashetani na alama ya vyombo vya majini na angani.”

Kwa hiyo, yeyote anayejaribu kutoa tafsiri tofauti na tatu hizi, basi bila shaka amezungumza kwa maoni yake, amepoteza sehemu yake na amejipa mzigo wa kile asichokijua.”

Ibn Jarir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى na Ibn Abi Hatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, wote wameandika kauli hii.¹

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ عَذَابُ جَهَنَّمَ ۖ وَيَبْسُ الْمَصِيرُ ﴿٦٦﴾ إِذَا أُلْقُوا فِيهَا سَمِعُوا لَهَا شَهيقًا
 وَهِيَ تَفُورٌ ﴿٦٧﴾ تَكَادُ تَمَيِّزُ مِنَ الْغَيْظِ ۖ كُلَّمَا أُلْقِيَ فِيهَا فَوْجٌ سَأَلْتُمْ خَزَنَتَهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَذِيرٌ
 ﴿٦٨﴾ قَالُوا بَلَىٰ قَدْ جَاءَنَا نَذِيرٌ فَكَذَّبْنَا وَقُلْنَا مَا نَزَّلَ اللَّهُ مِن شَيْءٍ إِنْ أَنْتُمْ إِلَّا فِي ضَلَالٍ
 كَبِيرٍ ﴿٦٩﴾ وَقَالُوا لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِي أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٧٠﴾ فَأَعْتَرَفُوا بِذَنبِهِمْ
 فَسُحِقًا لِأَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٧١﴾

6. Na kwa waliomkufuru Mola wao Mlezi ipo adhabu ya Jahannamu. Na ni marejeo maovu yalioje hayo!

7. Watakapotupwa humo watausikia mngurumo wake na huku inafoka.

8. Inakaribia kupasuka kwa hasira. Kila mara likitupwa kundi humo walinzi wake huwauliza: Kwani hakukujieni muonyaji?

9. Watasema: Kwani! Ametujia muonyaji, lakini tulimkadhibisha, na tukasema: Mwenyezi Mungu Hakuteremsha chochote. Nyinyi hamumo ila katika upotovu mkubwa!

10. Na watasema: Lau kuwa tungelisikia, au tungelikuwa na akili, tusingelikuwa katika watu wa Motoni!

11. Wakakiri dhambi zao. Basi kuangamia ni kwa watu wa Motoni!

¹ At-Tabari 23:508.

Wasifu wa Moto wa Jahannamu na Watakaolingia Humo

Allah تعالى Amesema,

وَ

“Na...”

Maana yake: Na Tumetayarisha,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ عَذَابُ جَهَنَّمَ وَيُسَّ السَّمِصِيمُ ﴿٦٧﴾

**“...kwa waliomkufuru Mola wao Mlezi ipo adhabu ya Jahannamu.
Na ni marejeo maovu yalioje hayo!”**

Ina maana: Huu utakuwa mwisho mbaya na makazi mabaya.

إِذَا أُلْقُوا فِيهَا سَمِعُوا لَهَا شَهيقًا

“Watakapotupwa humo watausikia mngurumo wake...”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema, “Ina maana sauti za makelele.”¹

وَهِيَ تَفُورُ ﴿٦٨﴾

“...na huku inafoka.”

Ath-Thawri رحمه الله تعالى amesema, “Inawachemsha wao kama vile mbegu inavyochemka ndani ya maji mengi.” Kisha Allah تعالى Anasema,

تَكَادُ تَمَيِّزُ مِنَ الْغَيْظِ ﴿٦٩﴾

“Inakaribia kupasuka kwa hasira.”

Maana yake: Baadhi ya sehemu zake zitavunjika kutokana na ukali wa ghadhabu na kuwakasirikia.

كُلَّمَا أُلْقِيَ فِيهَا فَوْجٌ سَأَلَهُمْ خَزَنَتُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَذِيرٌ ﴿٧٠﴾ قَالُوا بَلَىٰ قَدْ جَاءَنَا نَذِيرٌ

فَكَذَّبْنَا وَقُلْنَا مَا نَزَّلَ اللَّهُ مِن شَيْءٍ إِنْ أَنتُمْ إِلَّا فِي ضَلَالٍ كَبِيرٍ ﴿٧١﴾

¹ At-Tabari 23:508.

“Kila mara likitupwa kundi humo walinzi wake huwauliza: Kwani hakukujieni muonyaji? Watasema: Kwani! Ametujia muonyaji, lakini tulimkadhibisha, na tukasema: Mwenyezi Mungu hakuteremsha chochote. Nyinyi hamumo ila katika upotovu mkubwa!”

Katika Aya hizi Allah تعالى Anatukumbusha Uadilifu Wake Anaawatendea viumbe Wake na kuwa Hamuadhibu yeyote mpaka kuwe na ushahidi juu yao na Mjumbe aliyepelikwa kwao. Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿٦٧﴾

“Wala Sisi Hatuadhibu mpaka Tumpeleke Mtume.” (17:15)

Aidha Allah تعالى Anasema,

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهَا فَتِيحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ يَتْلُونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِ رَبِّكُمْ وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا قَالُوا بَلَىٰ وَلَٰكِن حَقَّتْ كَلِمَةُ الْعَذَابِ عَلَىٰ

الْكَافِرِينَ ﴿٦٨﴾

“...Mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake, na walinzi wake watawaambia: Kwani hawakukujilieni Mitume miongoni mwenu wakikusomeeni Aya za Mola wenu Mlezi na kukuonyeni mkutano wa siku yenu hii? Watasema: Kwani! Lakini limekwisha thibiti neno la adhabu juu ya makafiri.” (39:71)

Hivyo hawana hoja isipokuwa kulaumu nafsi zao na watahisi ukatili wakati majuto hayatowafaa. Watasema,

لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِي أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٦٩﴾

“Lau kuwa tungelisikia, au tungelikuwa na akili, tusingelikuwa katika watu wa Motoni!”

Maana yake: Ingelikuwa tumezitumia ipasavyo akili zetu au tumesikiliza ukweli Aliouteremsha Allah تعالى, tusingalimuasi Allah تعالى na tukapotoshwa kuhusu Yeye. Lakini hatukuwa na uelewa na kuzingatia aliyokuja nayo Mitume, na hatukuwa na maarifa ya kutuongoza kuwafuata. Kisha Allah تعالى Amesema,

فَاعْتَرَفُوا بِذَنبِهِمْ فَسُحِقًا لِأَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿١١﴾

“Wakakiri dhambi zao. Basi kuangamia ni kwa watu wa Motoni!”

Imam Ahmad alipokea, kutoka kwa Abu Bakhtari At-Tai kuwa alisikia kutoka kwa mmoja wa Masahaba kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَنْ يَهْلِكَ النَّاسُ حَتَّى يُعْذِرُوا مِنْ أَنْفُسِهِمْ»

“Watu hawatoangamizwa mpaka wakiri makosa yao.”¹

* * *

¹ Ahmad 5:293.

إِنَّ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿١٢﴾
 وَأَسِرُوا قَوْلَكُمْ أَوْ أَجْهَرُوا بِهِ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١٣﴾
 أَلَا يَعْلَمُ مَنْ خَلَقَ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ ﴿١٤﴾ هُوَ
 الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ ذُلُولًا فَأَمْشُوا فِي مَنَاكِبِهَا وَكُلُوا
 مِنْ رِزْقِهِ ۗ وَإِلَيْهِ النُّشُورُ ﴿١٥﴾ ءَأَمِنْتُمْ مَنْ فِي السَّمَاءِ أَنْ
 يَخْسِفَ بِكُمْ الْأَرْضَ فَإِذَا هِيَ تَمُورُ ﴿١٦﴾ أَمْ أَمِنْتُمْ مَنْ فِي
 السَّمَاءِ أَنْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ۗ فَسَتَعْمُونَ كَيْفَ نَذِيرِ ﴿١٧﴾
 وَلَقَدْ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿١٨﴾
 أَوْلَمْ يَرَوْا إِلَى الْطَّيْرِ فَوْقَهُمْ صَفْتَتْ وَيَقْبِضْنَ ۗ مَا
 يُمَسِّكُهُنَّ إِلَّا الرَّحْمَنُ ۗ إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ بَصِيرٌ ﴿١٩﴾

إِنَّ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ لَهُمْ
 مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿١٢﴾ وَأَسِرُوا
 قَوْلَكُمْ أَوْ أَجْهَرُوا بِهِ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ
 بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١٣﴾ أَلَا يَعْلَمُ مَنْ
 خَلَقَ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ ﴿١٤﴾ هُوَ
 الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ ذُلُولًا
 فَأَمْشُوا فِي مَنَاكِبِهَا وَكُلُوا مِنْ رِزْقِهِ ۗ
 وَإِلَيْهِ النُّشُورُ ﴿١٥﴾

**12. Hakika wanaomugopa
 Mola wao Mlezi kwa
 ghaibu, watapata maghfira
 na ujira mkubwa.**

13. Na ficheni kauli zenu, au zitangazeni; hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.

14. Asijue Aliyeumba, Naye Ndiye Mjua Siri, Mwenye Khabari?

15. Yeye Ndiye Aliyidhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake, na kuleni katika riziki Zake. Na Kwake Yeye ndio kufufuliwa.

Malipo ya Wenye Kumuogopa Mola Asiyeonekana

Allah تعالی Anamueleza mtu ambaye anaogopa kusimama mbele ya Mola Wake. Iwapo atafanya mambo mabaya pindi anapojitenga na macho ya watu. Hivyo anajiepusha na maasi na anafanya vitendo vya utiifu wakati hapana anayemuona isipokuwa Allah تعالی. Allah تعالی Anasema kuwa mtu huyo Atampa, atasamehewa na atapata malipo makubwa. Hii ina maana kuwa dhambi zake zitafutwa na atalipwa kwa wingi. Hii ni sawa na yaliyothibitishwa katika Sahihi Mbili.

«سَبْعَةً يُظْلِمُهُمُ اللَّهُ تَعَالَى فِي ظِلِّ عَرْشِهِ يَوْمَ لَا ظِلَّ إِلَّا ظِلُّهُ»

“Watu saba Allah Mtukufu Atawafunika kwa kivuli cha Arshi Yake Siku ambapo hapatakuwa na kivuli isipokuwa kivuli Chake.”

Kisha Anawataja miongoni mwa watu hao ni:

«دَعَتْهُ امْرَأَةٌ ذَاتُ مَنْصِبٍ وَجَمَالٍ فَقَالَتْ: إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ، وَرَجُلًا تَصَدَّقُ بِصَدَقَةٍ فَأَخْفَاهَا حَتَّى لَا تَعْلَمَ شِمَالَهُ مَا تُنْفِقُ بِمِثْلِهِ»

“Mwanamume aliyetakiwa na mwanamke mwenye hadhi ya juu na uzuri, lakini akasema: Kwa hakika namuogopa Allah. Mtu mwingine ni miongoni mwa watu wenye kutoa sadaka kwa siri kiasi mkono wa kushoto usijue kitolewacho na mkono wa kulia.”¹

Kisha Allah تعالی Akatoa angalizo ya kuwa Yeye Anazijua dhamira na siri sote.

وَأَسِرُّوا قَوْلَكُمْ أَوْ أَجْهَرُوا بِهِ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٦٧﴾

“Na ficheni kauli zenu, au zitangazeni; hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuanii.”

Maana yake: Yanayojiri ndani ya mioyo.

أَلَا يَعْلَمُ مَنْ خَلَقَ

“Asijue Aliyeumba...” Ina maana: ‘Muumbaji hajui?’

وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ ﴿٦٨﴾

“...Naye Ndiye Mjua Siri, Mwenye Khabari?”

Miongoni mwa Neema za Allah تعالی kwa waja wake ni Kudhalilishwa Ardhi Kwao.

Kisha Allah تعالی Ametaja Fadhila Zake kwa viumbe Wake kwa Kuidhalilisha ardhi kwao, na Kuifanya tiifu kwao wao. Kwa Kuifanya ardhi tulivu na thabiti, hainesi wala haitingishiki, kwa kuwa Amejaalia ndani yake Milima na

¹ Fat’hul Al-Bari 2:168, na Muslim 2:715.

chemchemi za mito. Alisawiri njia, na Akaweka vitu vyenye thamani ndani yake na Akaweka mboji kwa ukuaji wa matunda na mazao. Allah تعالى Anasema,

هُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ ذُلُولًا فَأَمْشُوا فِي مَنَاكِبِهَا

“Yeye Ndiye Aliyeidhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake...”

Maana yake: Safirini popote mtakapo katika maeneo yote na nendeni bara na maeneo yote ya utawala katika ziara zenu kwa ajili ya kutafuta riziki na kufanya biashara. Na mfahamu kuwa juhudi zako hazitokunufaisha kabisa mpaka Allah تعالى Akufanyie wepesi. Allah تعالى Anaendelea Kusema,

وَكُلُوا مِنْ رِزْقِهِ

“...na kuleni katika riziki Zake.”

Kuchukua sababu katika kutafuta riziki, hakuondoshi imani ya kumtegemea Allah تعالى. Hii ni sawa na yale aliyonukuu Imam Ahmad kutoka kwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه, kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«لَوْ أَنَّكُمْ تَتَوَكَّلُونَ عَلَى اللَّهِ حَقَّ تَوَكُّلِهِ، لَرَزَقْنَاكُمْ كَمَا يَرْزُقُ الطَّيْرَ، تَخْدُو خِمَاصًا وَتَرُوحُ بِطَانًا»

“Iwapo mtamtegemea kwa dhati kabisa Allah Atawapeni riziki kama Anavyowapa ndege. Wanaruka asubuhi na matumbo matupu, na wanarejea jioni na matumbo yamejaa.”¹

At –Tirmidhi amesema ni, “Hasan Sahihi”². Hivyo hii inathibitisha kuwa ndege wanatafuta asubuhi na jioni riziki huku wakimtegemea Allah تعالى. Kwani Yeye Ndiye Mtoa Haki, Mdhibili, na Msababishi wa kila kitu.

وَالْيَهُ النُّشُورُ

“Na Kwake Yeye ndio kufufuliwa.”

Maana yake: Sehemu ya marejeo Siku ya Kiyama. Ibn Abbas, Mujahid, As-

¹ Ahmad 1:52.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 8:8, An-Nasai katika Al-Kubra, kitabu cha Ar-Raqaiq, Tuhfat Al-Ashraf 8:79, na Ibn Majah 2:1394.

Suddi na Qatadah رضي الله عنهم wote wamesema kuwa *Manakibuha* ina maana ya njia zake mipaka yake ya nje, barabara zake na majimbo yake.¹

ءَأَمِنْتُمْ مَّن فِي السَّمَاءِ أَنْ يَخْسِفَ بِكُمْ الْأَرْضَ فَإِذَا هِيَ تَمُورٌ ﴿١٦﴾ أَمْ أَمِنْتُمْ مَّن فِي السَّمَاءِ أَنْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ۗ فَسَتَعْمُونَ كَيْفَ نَذِيرٍ ﴿١٧﴾ وَلَقَدْ كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿١٨﴾ أَوْلَمْ يَرَوْا إِلَى الطَّيْرِ فَوْقَهُمْ صَفَّتْ وَبَقِيضٌ مَّا يُمْسِكُهُنَّ إِلَّا الرَّحْمَنُ إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ بَصِيرٌ ﴿١٩﴾

16. Mnadhani mko salama kwa Alioko juu kuwa Hataku didimizeni kwenye ardhi, na tahamaki hiyo inatikisika!

17. Au mnadhani mko salama kwa Alioko juu ya kuwa Yeye Hatakupelekeeni kimbunga chenye changarawe? Mtajua vipi maonyo Yangu?

18. Na bila ya shaka walikwishakanusha waliokuwa kabla yao; basi kulikuwaje kukasirika Kwangu?

19. Kwani hawawaoni ndege walioko juu yao namna wanavyo zikunjua mbawa zao, na kuzikunja? Hawawashikilii ila Mwingi wa Rehema. Hakika Yeye ni Mwenye Kuona kila kitu.

Vipi Mtasalimika na Adhabu ya Allah تعالى, Naye Ana Uweza wa Kuwaadhibu Anavyotaka:

Hii ni dalili nyingine ya Uraufu Wake na Huruma Yake kwa viumbe Wake. Ana Uweza wa Kuwaadhibu kwa sababu baadhi yao walimkanusha na waliabudu wengine pamoja Naye, hata hivyo Amewavumilia, Anawasamehe, na Anawapa muda wa kupumua bila Kuwaharakishia adhabu. Hivi ndivyo Anavyosema,

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ بِمَا كَسَبُوا مَا تَرَكَ عَلَى ظَهْرِهَا مِن دَابَّةٍ وَلَكِن يُؤَخِّرُهُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ فَإِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِعِبَادِهِم بَصِيرًا ﴿٢٠﴾

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angeliwachukulia watu kwa

¹ At-Tabari 23:512, na Al-Qurtubi 18:215.

waliyoyachuma, basi Asingelimuacha juu ya ardhi hata mnyama mmoja. Lakini Yeye Anawachukulia mpaka ufike muda maalumu. Basi ukifika muda wao basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwaona waja wake baraabara.” (35:45)

Hapa Allah تعالى Anasema,

ءَأَمِنْتُمْ مِّنْ فِي السَّمَاءِ أَنْ يَخْسِفَ بِكُمْ الْأَرْضَ فَإِذَا هِيَ تَمُورٌ ﴿٦٧﴾

“Mnadhani mko salama kwa Alioko juu kuwa Hatakididimizeni kwenye ardhi, na tahamaki hiyo inatikisika!”

Maana yake: Kuwa itakwenda mbele na nyuma, na kutetemeka.

أَمْ أَمِنْتُمْ مِّنْ فِي السَّمَاءِ أَنْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ۗ

“Au mnadhani mko salama kwa Alioko juu ya kuwa Yeye Hatakupelekeeni kimbunga chenye changarawe?”

Maana yake: Upepo wenye changarawe utawapigeni, kama Allah تعالى Anavyosema katika Aya nyingine,

أَفَأَمِنْتُمْ أَنْ يَخْسِفَ بِكُمْ جَانِبَ الْبَرِّ أَوْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ وُكَيْلًا

“Je! Mmeaminisha ya kuwa Hatakididimizeni upande wowote katika nchi kavu, au kwamba Hatakuleteeni tufani la kokoto? Kisha msipate wa kumtegemea.” (17:68)

Na vivyo hivyo, hapa Allah تعالى Anawatisha kwa,

فَسَتَعْلَمُونَ كَيْفَ نَذِيرٍ ﴿٦٨﴾

“Mtajua vipi maonyo Yangu?”

Maana yake: ‘Adhabu Yangu ilivyo na yatakayowapata waliopuuzi na kukataa.’ Kisha Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ

“Na bila ya shaka walikwisha kanusha waliokuwa kabla yao...”

Ina maana: Katika Ummah uliotangulia na vizazi vya zamani vilivyopita. Kisha Allah تعالى Amesema,

فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٦٧﴾

“...basi kulikuwaje Kukasirika Kwangu?”

Maana yake: ‘Makaripio Yangu na Adhabu zilikuwaje kwao.’ Maana yake: Yalikuwa makubwa na yaumizayo.

Ndege Warukao ni kwa Uwezo wa Allah تعالیٰ, Huu ni Ushahidi kuwa Yeye ni Mjuzi wa Kila Kitu Kidogo na Kikubwa.

Allah تعالیٰ Anasema,

أُولَٰئِكَ يَرَوْنَ إِلَىٰ آلِطَبْرِ فَوْقَهُمْ صَفْتًا وَيَقْبِضُونَ

“Kwani hawawaoni ndege walioko juu yao namna wanavyozikunjua mbawa zao, na kuzikunja?”

Maana yake: Baadhi ya wakati wanatawanya mbawa zao kwenye upepo (kunyiririka) na wakati mwingine wanazikunja na kuzitawanya,

مَا يُمَسِّكُهُنَّ

“...Hawawashikili...” Maana yake: Katika anga,

إِلَّا الرَّحْمَنُ

“...ila Mwingi wa Rehema.” Maana yake: Allah تعالیٰ Amewadhaliishia wao anga kutokana na Huruma Yake na Upole Wake,

إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ بَصِيرٌ ﴿٦٨﴾

“Hakika Yeye ni Mwenye Kuona kila kitu.”

Maana yake: Kila chenye manufaa na faida kwa viumbe vyake vyote. Hii ni sawa na Kauli Yake,

أَلَمْ يَرَوْا إِلَىٰ آلِطَبْرِ مَسْخَرَتٍ فِي جَوِّ السَّمَاءِ مَا يُمَسِّكُهُنَّ إِلَّا اللَّهُ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ

لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٦٩﴾

“Je! Hawawaoni ndege walivyo wat’iifu katika anga la mbingu? Hapana mwenye kuwashika isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanaoamini.” (16:79)

أَمَّنْ هَذَا الَّذِي هُوَ جُنْدٌ لَكُمْ يَنْصُرُكُمْ مِنْ دُونِ الرَّحْمَنِ ۗ
 إِنَّ الْكَافِرُونَ إِلَّا فِي غُرُورٍ ۝ أَمَّنْ هَذَا الَّذِي يَرْزُقُكُمْ
 إِنْ أَمْسَكَ رِزْقَهُ ۗ بَلْ لَجُوا فِي عُتُوٍّ وَنُفُورٍ ۝ أَمَّنْ
 يَمْشِي مَكْبًا عَلَىٰ وَجْهِهِ أَهْدَىٰ أَمَّنْ يَمْشِي سَوِيًّا عَلَىٰ
 صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ۝ قُلْ هُوَ الَّذِي أَنْشَأَكُمْ وَجَعَلَ لَكُمْ
 السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ ۗ قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ۝ قُلْ
 هُوَ الَّذِي ذَرَأَكُمْ فِي الْأَرْضِ وَإِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ۝ وَيَقُولُونَ
 مَتَىٰ هَذَا الْوَعْدُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ۝ قُلْ إِنَّمَا أَلْغَلُمُ
 عِنْدَ اللَّهِ وَإِنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ۝ فَلَمَّا رَأَوْهُ زُلْفَةً سَيِّئَتْ
 وُجُوهُ الَّذِينَ كَفَرُوا وَقِيلَ هَذَا الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ
 تَدْعُونَ ۝ قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَهْلَكَنِيَ اللَّهُ وَمَن مَّعِيَ أَوْ
 رَحِمَنَا فَمَن يُجِيرُ الْكَافِرِينَ مِنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ۝ قُلْ هُوَ
 الرَّحْمَنُ ءَامَنَّا بِهِ وَعَلَيْهِ تَوَكَّلْنَا ۗ فَسْتَعْمُونَ مَن هُوَ فِي
 ضَلَالٍ مُّبِينٍ ۝ قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَصْبَحَ مَاؤُكُمْ غَوْرًا فَمَن
 يَأْتِيكُمْ بِمَاءٍ مَّعِينٍ ۝

أَمَّنْ هَذَا الَّذِي هُوَ جُنْدٌ لَكُمْ
 يَنْصُرُكُمْ مِنْ دُونِ الرَّحْمَنِ ۗ
 إِنَّ الْكَافِرُونَ إِلَّا فِي غُرُورٍ ۝
 أَمَّنْ هَذَا الَّذِي يَرْزُقُكُمْ إِنْ
 أَمْسَكَ رِزْقَهُ ۗ بَلْ لَجُوا فِي
 عُتُوٍّ وَنُفُورٍ ۝ أَمَّنْ
 يَمْشِي مَكْبًا عَلَىٰ وَجْهِهِ
 أَهْدَىٰ أَمَّنْ يَمْشِي سَوِيًّا عَلَىٰ
 صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ۝ قُلْ هُوَ
 الَّذِي أَنْشَأَكُمْ وَجَعَلَ لَكُمْ
 السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ ۗ
 قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ۝ قُلْ
 هُوَ الَّذِي ذَرَأَكُمْ فِي
 الْأَرْضِ وَإِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ۝
 وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَذَا
 الْوَعْدُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ۝
 قُلْ إِنَّمَا أَلْغَلُمُ عِنْدَ اللَّهِ
 وَإِنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ۝
 فَلَمَّا رَأَوْهُ زُلْفَةً

سَيِّئَتْ وُجُوهُ الَّذِينَ كَفَرُوا وَقِيلَ هَذَا الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تَدْعُونَ ۝

20. Au ni lipi hilo jeshi lenu la kukunusuruni badala ya Mwingi wa Rehema? Hakika makafiri hawamo ila katika udanganyifu.

21. Au ni nani huyo ambaye atakupeni riziki kama Yeye Akizuia riziki Yake? Bali wao wanakakamia tu katika jeuri na chuki.

22. Je! Anayekwenda akisinukia juu ya uso wake ni mwongofu zaidi, au yule anayekwenda sawasawa katika Njia Iliyonyooka?

23. Sema: Yeye Ndiye Aliyekuumbeni tangu mwanzo, na Akakupeni masikio na macho, na nyoyo. Ni kidogo kabisa shukrani zenu.

24. Sema: Yeye Ndiye Aliyekutawanyeni katika ardhi, na Kwake mtakusanywa.

25. Na wanasema: Lini ahadi hii, ikiwa mnasema kweli?

26. Sema: Hakika Ujuzi Wake uko kwa Mwenyezi Mungu; na hakika mimi ni mwonyaji tu mwenye kubainisha.

27. Lakini watakapoiona karibu, nyuso za waliokufuru zitahuzunishwa, na itasemwa: Hayo ndiyo mliyokuwa mkiyaomba.

Hapana Atakayewasaidia Kukupeni Riziki Isipokuwa Allah تعالی.

Allah تعالی Anawaeleza mushirikina ambao wanamuabudu asiyekuwa Yeye. Hapana mtu atakayekunusuruni na atakayewapa riziki isipokuwa Allah تعالی. Allah تعالی Anawalingania washirikina ambao wanaabudu viumbe vingine pamoja na Allah تعالی, wanaomba msaada na riziki kutoka kwao. Allah تعالی Anawakemea kwa hayo wanayoabudu, na Anawaeleza kuwa hawatofikia kile wanachotegemea.

Allah تعالی Anasema,

أَمَّنْ هَذَا الَّذِي هُوَ جُنْدٌ لَكُمْ يَنْصُرُكُمْ مِنْ دُونِ الرَّحْمَنِ

“Au ni lipi hilo jeshi lenu la kukunusuruni badala ya Mwingi wa Rehema?”

Maana yake: Hapana muokozi au wa kukusaidieni zaidi ya Yeye. Kwa sababu hiyo Allah تعالی Anasema,

إِنَّ الْكٰفِرُونَ اِلَّا فِيْ غُرُوْرٍ

“Hakika makafiri hawamo ila katika udanganyifu.”

Kisha Allah تعالی Amesema,

أَمَّنْ هَذَا الَّذِي يَرْزُقُكُمْ إِنْ أَمْسَكَ رِزْقَهُ

“Au ni nani huyo ambaye atakupeni riziki kama Yeye Akizuia riziki Yake?”

Maana yake: Ni nani anayeweza kukukimu endapo Allah تعالی Atakukatia riziki? Hapana yeyote anayeweza kuzuia, kuumba, na kusaidia isipokuwa Allah تعالی Pekee, Ambaye Hana mshirika. Hii inathibitisha ya kuwa wanajua lakini bado wanaabudu wengine pamoja Naye. Allah تعالی Anasema,

بَلْ لَّجُوا فِي

“...Bali wao wanakakamia tu...” Maana yake: Wanabobea katika maasi, kuongopa na upotoshaji.

فِي عُنْتٍ وَنُفُورٍ

“...katika jeuri na chuki...” Maana yake: Wanaendelea na ukaidi, ujui na kuukimbia ukweli. Hawausikilizi wala hawaufuati.

Mfano wa Kafiri na Muumini

Kisha Allah تعالی Anasema,

أَفَمَنْ يَمْشِي مُكِبًّا عَلَىٰ وَجْهِهِ أَهْدَىٰ أَمَّنْ يَمْشِي سَوِيًّا عَلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

“Je! Anayekwenda akisinukia juu ya uso wake ni mwongofu zaidi, au yule anayekwenda sawasawa katika njia iliyonyooka?”

Mfano huu Allah تعالی Ameuakisi kwa Muumini na Kafiri. Hivyo hali ya Kafiri ni kama mtu atembeaye kifudufudi. Hivyo ni kama mtu atembeaye huku anainamisha kichwa badala ya kutembea wima. Mtu huyo hajui anakoelekea. Bali, amepotea na amechanganyikiwa. Hivi mtu huyu ameongozwa,

أَمَّنْ يَمْشِي سَوِيًّا

“...au yule anayekwenda sawasawa...” Maana yake: Mtu Huyu anayetembea wima

عَلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

“...katika Njia Iliyonyooka?” Yuko katika njia iliyonyooka, na ya wazi, nafsi yake imesimama sawa na njia yake imenyooka. Haya ndio wayapendayo hapo duniani na yatakuwa vivyo hivyo Siku ya Kiyama. Hivyo Muumini atakusanywa

Siku ya Kiyama huku anasimama wima katika mstari ulionyooka na Pepo kubwa na nzuri itafunguliwa kwa ajili yake. Lakini Makafiri watakusanywa wakiwa wameinamisha nyuso zao kuelekea Motoni.

﴿ أَحْشُرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ وَمَا كَانُوا يَعْبُدُونَ ﴾ ﴿٢٢﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ فَأَهْدُوهُمْ إِلَىٰ صِرَاطِ الْجَحِيمِ ﴿٢٣﴾

“Wakusanyeni waliodhulumu, na Azwa-juhum, na hao waliokuwa wakiwaabudu - Badala ya Mwenyezi Mungu. Waongozeni njia ya Jahannamu!” (37:22-23)

Maana ya: “Azwa-juhum” ni Wanaoashabihiana nao, Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه kuwa ilinenwa, “Ewe Mjumbe wa Allah! Vipi watu watafufuliwa huku wakitembelea nyuso zao?” Mtume ﷺ akasema

«أَلَيْسَ الَّذِي أُنشَاهُمْ عَلَىٰ أَرْجُلِهِمْ قَادِرًا عَلَىٰ أَنْ يُمَشِّئَهُمْ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ»

“Si Yeye Aliyewafanya watembe kwa miguu basi atashindwaje Kuwafanya watembe kwa nyuso zao?”¹ Hadithi hii imenukuliwa pia katika Sahihi Mbili.²

Uweza wa Allah تعالیٰ Katika Kuumba na Ushahidi wa Uwepo wa Siku ya Mwisho.

Allah تعالیٰ Amesema,

قُلْ هُوَ الَّذِي أَنْشَأَكُمْ

“Sema: Yeye Ndiye Aliyekuumbeni tangu mwanzo...”Maana yake: Alianzisha Kuumbwa kwenu wakati hamkuwa chochote.

وَجَعَلَ لَكُمْ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ

“...na Akakupeni masikio na macho, na nyoyo...”Maana yake: Akili na uweza na maarifa.

﴿ قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴾ ﴿٢٤﴾

“Ni kidogo kabisa shukrani zenu.”Maana yake: Ni mara ngapi unautumia uwezo Aliokuruzuku Allah تعالیٰ kumtii Yeye, kutekeleza Amri Zake, na kuacha makatazo Yake.

¹ Ahmad 3:167.

² Fat’hul Al-Bari 6:350, na Muslim 4:2161.

قُلْ هُوَ الَّذِي ذَرَأَكُمْ فِي الْأَرْضِ

“Sema: Yeye Ndiye Aliyekutawanyeni katika ardhi...”

Maana yake: Amewatawanya na Kuwagawa sehemu zote katika nchi mbalimbali na maeneo ya dunia mkiwa na lugha tofauti, rangi, maumbile, sura na muundo.

وَالِيهِ تَحْشُرُونَ ﴿٢٠﴾

“...na Kwake mtakusanywa...”

Maana yake: Nyote mtakuwa pamoja baada ya kutengana na kugawanyika. Atawakusanya nyote kama Alivyowatawanyisha na Atawarejesha kama mlivyokuwa mwanzo. Kisha Atakapokuwa Anawafahamisha makafiri wanaopinga marejeo ya mwisho, na kuwa na mashaka juu ya kutokea kwake, Allah تعالى Anasema,

وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢١﴾

“Na wanasema: Lini ahadi hii, ikiwa mnasema kweli?”

Maana yake: ‘Ni lini mkusanyiko huu utatokea baada kufarakana?’

قُلْ إِنَّمَا أَعْلَمُ عِنْدَ اللَّهِ

“Sema: Hakika ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: ‘Hapana ajuaye muda wa Siku ya Malipo isipokuwa Allah تعالى, lakini ameniamuru niwafahamishe kuwa ni hakika na itatokea, hivyo jihadharini nayo.

وَأِنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٢٢﴾

“...na hakika mimi ni mwenyaji tu mwenye kubainisha.”

Maana yake: “Mimi nimewajibishwa kuwafikishia, na kwa hakika nimetimiza wajibu wangu wa kuwafikishieni.” Kisha Allah تعالى Anasema,

فَلَمَّا رَأَوْهُ زُلْفَةً سَيِّئَتْ وُجُوهُ الَّذِينَ كَفَرُوا

“Lakini watakapoiona karibu, nyuso za waliokufuru zitahuzunishwa...”

Maana yake: Siku ya Kiyama itakapoanza, na makafiri wakashuhudia. Na wakaona mambo yamekaribia, kwa sababu kila lililotarajiwa kutokea litakuwa

linatokea, utawakera kwa sababu watajua kile kinacho wasubiri. Shari kubwa inayo wangojea humo (Motoni).

Hii Ina Maana: Itawazingira na Allah تعالى Atawaamuru yale waliyoshindwa kuya tambua na kuyazingatia,

وَبَدَا لَهُمْ مِنَ اللَّهِ مَا لَمْ يَكُونُوا يَحْتَسِبُونَ ﴿٣٧﴾ وَبَدَا لَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا وَحَاقَ

بِهِمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٣٨﴾

“...Na yatawadhihirikia kwa Mwenyezi Mungu wasiyo kuwa wakiyatarajia. Na utawadhihirikia ubaya wa waliyoyachuma, yatawa zunguka waliyokuwa wakiya fanyia mzaha.” (39:47-48)

Ndiyo sababu itasemwa kwao kwa njia ya kuwakaripia na kuwafedhehesha.

Allah تعالى Anasema,

هَذَا الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تَدْعُونَ ﴿٣٩﴾

“Hayo ndiyo mliyokuwa mkiyaomba.”

Maana yake: Mlikuwa mnataka mfanyiwe haraka.

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَهْلَكْنِي أَلَّهُ وَمَنْ مَعِيَ أَوْ رَحِمَنَا فَمَنْ يُجِيرُ الْكَافِرِينَ مِنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٤٠﴾

قُلْ هُوَ الرَّحْمَنُ ءَامَنَّا بِهِ وَعَلَيْهِ تَوَكَّلْنَا فَسَتَعْمَلُونَ مَنْ هُوَ فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٤١﴾ قُلْ

أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَصْبَحَ مَاؤُكُمْ غَوْرًا فَمَنْ يَأْتِيكُمْ بِمَاءٍ مَعِينٍ ﴿٤٢﴾

28. Sema: Mnaonaje, ikiwa Mwenyezi Mungu Atanihiliki mimi na walio pamoja nami, au Akiturehemu, ni nani atakayewalinda makafiri na adhabu chungu?

29. Sema: Yeye Ndiye Mwingi wa Rehema; tunamuamini Yeye, na juu Yake tunategemea. Mtakuja jua ni nani aliye katika upotovu uliodhaahiri.

30. Sema: Mnaonaje, yakiwa maji yenu yamedidimia chini, nani atakuleteeni maji yanayomiminika?

Mauti ya Muumini Hayatamuokoa Kafiri, Hivyo Atafakari Namna ya Kujiokoa.

قُلْ

“**Sema...**” ‘Ewe Muhammad kuwaambia washirikina wanaomshirikisha Allah تعالى na wanakataa Neema Zake,

أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَهْلَكَنِیَ اللَّهُ وَمَنْ مَعِيَ أَوْ رَحِمَنَا فَمَنْ یُجِیرُ الْکَافِرِینَ مِنْ عَذَابِ أَلِیمٍ ﴿٢٠﴾

“...Mnaonaje, ikiwa Mwenyezi Mungu Atanihiliki mimi na walio pamoja nami, au Akiturehemu, ni nani atakayewalinda makafiri na adhabu chungu?”

Maana yake: ‘Jiokoeni! Kwani kwa hakika, hapana cha kuwaokoa kwa Allah تعالى isipokuwa toba, kurejea Kwake kuomba msamaha, na kurejea katika Dini Yake. Matarajio yenu kuwa mateso na adhabu itatupata sisi, haitokusaidieni. Ima Allah تعالى Atatuadhibu au Atatuhurumia, hapana mwanya wa kukwepa adhabu ya Allah تعالى na adhabu iumizayo itakupateni na hakuna shaka juu ya hilo. Kisha Allah تعالى Anasema,

قُلْ هُوَ الرَّحْمَنُ ءَامَنَّا بِهِ وَعَلَيْهِ تَوَكَّلْنَا

“Sema: Yeye Ndiye Mwingi wa Rehema; tunamuamini Yeye, na juu Yake tunategemea.”

Maana yake: ‘Tunamuamini Mola wa vyote vinavyoishi, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu, na Kwake tunamtegemea kwa kila kitu. Hivi ni kama Allah تعالى Anavyosema,

فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ

“Basi muabudu Yeye na umtegemea Yeye.” (11:123)

Hivyo, Allah تعالى Anaendelea kusema,

فَسَتَعْمَلُونَ مَنْ هُوَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٢١﴾

“Mtakuja jua ni nani aliye katika upotovu ulio dhaahiri.”

Maana yake: ‘Baina Yetu na wewe, mwisho mzuri utakuwa ni wa nani hapa duniani na kesho Akhera!’

Allah تعالیٰ Anawakumbusha Neema Yake ya Kuwaletea Maji; na Kitisho cha Kuyaondosha

Kisha Allah تعالیٰ Akaeleza Huruma Yake kwa viumbe Vyake, Akasema

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَصْبَحَ مَاؤُكُمْ غَوْرًا

“Sema: Mnaonaje, yakiwa maji yenu yamedidimia chini...”

Maana yake: Yamezama chini kabisa ya ardhi. Hayatapatikana kwa nyenzo madhubuti au watu wenye nguvu kubwa. Kwa sababu hii Allah تعالیٰ Amesema,

فَمَنْ يَأْتِيكُمْ بِمَاءٍ مَّعِينٍ ﴿٦٧﴾

“...nani Atakuleteni maji yanayomiminika?”

Maana yake: Kuchimbuka ghafla, kutiririka juu ya ardhi. Ina maana hapana awezaye kufanya hili isipokuwa Allah تعالیٰ. Hivyo ni kutokana na Rehema na Fadhila Zake Anafanya maji yabubujike kwa matumizi yenu, na Anayafanya yaende sehemu mbalimbali za dunia kwa kiasi ambacho kinatosheleza mahitaji ya waja Wake, yawe machache au mengi. Hivyo shukrani zote Anastahiki Allah تعالیٰ.

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu At-Mulk* na Shukrani na Sifa Zote Anastahiki Allah تعالیٰ.

* * *

Tafsiri ya Suratu Nun (Qalam)

Sura ya 68

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْقَلَمِ

تَ وَالْقَلَمِ وَمَا يَسْطُرُونَ ﴿١﴾ مَا أَنْتَ بِعِيمَةٍ رَبِّكَ
بِمَجْنُونٍ ﴿٢﴾ وَإِنَّ لَكَ لَأَجْرًا غَيْرَ مَمْنُونٍ ﴿٣﴾ وَإِنَّكَ
لَعَلَى خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾ فَسَتَبْصُرُ وَيُبْصِرُونَ ﴿٥﴾ بِأَيِّكُمْ
الْمَفْتُونُ ﴿٦﴾ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ
وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿٧﴾ فَلَا تُطِعِ الْمُكَذِّبِينَ ﴿٨﴾
وَدُّوا لَوْ تُدْهِنُ فَيُدْهِنُونَ ﴿٩﴾ وَلَا تُطِعِ كُلَّ حَلَّافٍ
مَّهِينٍ ﴿١٠﴾ هَمَّازٍ مَشَّاءٍ بِنَمِيمٍ ﴿١١﴾ مَنَّاعٍ لِّلْخَبَرِ مُعْتَدٍ
أَثِيمٍ ﴿١٢﴾ عَثَلٍ بَعْدَ ذَلِكَ رَنِيمٍ ﴿١٣﴾ أَنْ كَانَ ذَا مَالٍ
وَبَيْنَ ٱلْأَوَّلِينَ ﴿١٤﴾ إِذَا تَتَلَّى عَلَيْهِ ءَايَاتُنَا قَالَ أَسْطُورٌ
الْأَوَّلِينَ ﴿١٥﴾ سَنَسْمُهُ عَلَى ٱلْخُرطومِ ﴿١٦﴾

تَ وَالْقَلَمِ وَمَا يَسْطُرُونَ ﴿١﴾ مَا أَنْتَ بِعِيمَةٍ رَبِّكَ
بِمَجْنُونٍ ﴿٢﴾ وَإِنَّ لَكَ لَأَجْرًا غَيْرَ مَمْنُونٍ ﴿٣﴾ وَإِنَّكَ
لَعَلَى خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾ فَسَتَبْصُرُ وَيُبْصِرُونَ ﴿٥﴾ بِأَيِّكُمْ
الْمَفْتُونُ ﴿٦﴾ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ
سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿٧﴾

1. Nuun. Naapa kwa kalamu na yale wayaandikayo,

2. Kwa neema ya Mola Wako Mlezi wewe si mwendawazimu.

3. Na kwa hakika wewe una malipo yasiyo katika.

4. Na hakika wewe una tabia tukufu.

5. Karibu utaona, na wao wataona,

6. Ni nani kati yenu aliyepandwa na wazimu.

7. Hakika Mola Wako Mlezi Ndiye Yeye Ajuaye zaidi nani aliye ipotea Njia Yake, na Yeye Ndiye Anayewajua zaidi walioongoka.

Tumekwisha jadili herufi mahsusi za *abjadiya* Kiarabu mwanzoni mwa *Surat Al-Baqarah*. Kwa ajili hiyo Allah تعالی Amesema,

﴿ن﴾

“*Nuun.*” (Nun), kama Kauli ya Allah تعالی,

﴿س﴾

“*(Sad)*”, na Kauli ya Allah تعالی

﴿ق﴾

(*Qaf*), ni sawa na hizo kutoka herufi moja moja zinazojitokeza mwanzoni mwa Sura za Qur’an. Hili lilijadiliwa kwa urefu kabla, hivyo hakuna haja ya kurejea hapa.

Maelezo ya Kalamu

Kuhusiana na Kauli ya Allah تعالی,

وَالْقَلَمِ

“*Naapa kwa kalamu...*” Maana yake: Iliyowazi ni kuwa, inahusu Kalamu hasa itumikayo kuandika. Hii ni kama Kauli ya Allah تعالی,

أَقْرَأُ وَرَبُّكَ الْأَكْرَمُ ﴿٥﴾ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ﴿٤﴾ عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ﴿٣﴾

“Soma! Na Mola wako Mlezi ni Karimu kushinda wote! Ambaye Amefundisha kwa kalamu. Kamfundisha mtu aliyokuwa hayajui.”

(96:3-5)

Kwa hiyo, Kauli hii ya Allah تعالی ya Kuapa na Kuwazindua viumbe Wake kwa yale aliyowapendelea kwayo kwa Kuwafundisha stadi za kuandika, kupitia kwayo wanapata ilimu. Hivyo Allah تعالی Anaendelea kwa Kusema,

وَمَا يَسْطُرُونَ ﴿٦﴾

“*...na yale wayaandikayo,*” Ibn Abbas, Mujahid na Qatadah رضي الله عنهم wote wamesema kuwa hii ina maana, “wanachoandika”¹. As-Suddi amesema,

¹ At-Tabari 23:527, 528.

“Malaika na amali za waja wanazozindika.”

Wengine wamesema, “Bali kinachokusudiwa hapa ni Kalamu ambayo Allah تعالى Alisababisha Kuandika Amri Alipoandika Amri ya maumbile yote, na haya yalijiri miaka elfu hamsini kabla ya Kuumba mbingu na ardhi.” Kwa ajili hiyo wamewasilisha Hadithi zinazozungumzia Kalamu.

Ibn Abi Hatim amenukuu kutoka kwa Al-Walid bin Ubadah bin As-Samit kuwa amesema, “Baba yangu aliagiza niitwe alipokuwa anakaribia kufa na aliniambia: Kwa hakika, “Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«إِنَّ أَوَّلَ مَا خَلَقَ اللهُ الْقَلَمَ فَقَالَ لَهُ: اكْتُبْ، قَالَ: يَا رَبِّ وَمَا أَكْتُبُ؟ قَالَ: اكْتُبِ
الْقَدَرَ وَمَا هُوَ كَائِنٌ إِلَى الْأَبَدِ»

“Hakika kitu cha mwanzo Alichokiumba Allah ni Kalamu, Na Akaiambia: “Andika!’ Kalamu ikanena, “Ewe Mola wangu, niandike nini? Akaiambia” Andika Qadari na chote kitakachotokea katika uhai wa dunia.”¹

Hadithi hii ilinukuliwa na Imam Ahmad kupitia njia nyingi za upokezi.² At-Tirmidhi naye amenukuu Hadithi hii kutoka kwa Abu Dawud At-Tayalisi na yeye (At-Tirmidhi) ametaja kuwa ni: *Hasan Sahih, Gharib.*³

Kuapa kwa Kalamu Kunaonesha Ukuu wa Mtume ﷺ

Allah تعالى Amesema,

مَا أَنْتَ بِنِعْمَةٍ رَبِّكَ بِمَجْنُونٍ ﴿٦٨﴾

“Kwa neema ya Mola Wako Mlezi wewe si mwendawazimu.”

Maana yake: Sifa Zote Zinamstahiki Allah تعالى – wewe si mwandawazimu kama wajinga miongoni mwa watu wako wanavyodai. Ni wale wanaokanusha muongozo na ukweli uliowazi uliokuja nao. Kwa hiyo, wanakuhusisha na wazimu.

¹ At-Tabari 23:317.

² Ahmad 5:317.

³ Tuhfat Al-Ahwadhi 9:232.

وَإِنَّ لَكَ لَأَجْرًا غَيْرَ مَمْنُونٍ ﴿٦٨﴾

“Na kwa hakika wewe una malipo yasiyokatika.”

Maana yake: ‘Utalipwa ujira mkubwa, na neema nyingi ambazo hazitasitishwa au kuisha, kwa sababu ulifikisha Ujumbe wa Mola Wako kwa viumbe, na ulivumilia vitimbi vyao.’ Maana ya:

غَيْرَ مَمْنُونٍ ﴿٦٨﴾

“...malipo yasiyokatika.”

Kuwa haitositishwa. Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى,

عَطَاءٌ غَيْرَ مَجْدُوذٍ ﴿١٠٨﴾

“...Hicho ni kipawa kisio na ukomo.” (11:108)

Na Kauli Yake,

فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٦٩﴾

“...hao watapata ujira usiokwisha.” (95:6)

Mujahid amesema,

غَيْرَ مَمْنُونٍ ﴿٦٩﴾

“...usiokwisha.”

Maana yake: “Usiokatika”¹ Na hili linaturejesha katika yale tuliyosema kabla.

Maelezo ya Kauli, “Na hakika wewe una tabia tukufu.”

Kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٧٠﴾

“Na hakika wewe una tabia tukufu.”

Al-Awf amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, “Kwa hakika uko katika Dini kubwa, nayo ni Uislamu.”² Vivyo hivyo amesema Mujahid, Abu Malik, As-

¹ At-Tabari 23:528.

² At-Tabari 23:529.

Suddi, Ar-Rabi bin Anas.¹ Adh-Dhahhak na Ibn Zayd nao wamesema hivyo.² Said bin Aabi Arubah amepokea kutoka kwa Qatadah amesema kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٦٨﴾

“Na hakika wewe una tabia tukufu.”

“Imeelezwa kwetu kuwa Said bin Hisham alimuuliza Aishah رضي الله عنها kuhusu tabia ya Mtume ﷺ hivyo akajibu: “Hujasoma Qur’an?” Said akajibu, “Bila shaka.” Kisha akasema: “Kwa hakika tabia ya Mtume ﷺ ilikuwa Qur’an.”³ Abdur-Razzaq amepokea sawa na hadithi hii na Imam Muslim ameandika ndani ya Sahihi yake kupitia Hadithi ya Qatadah kwa urefu wake.⁴

Hii ina maana kuwa atatekeleza kwa mujibu wa maamrishi na makatazo yaliyomo kwenye Qur’an. Maumbile na tabia yake vilipambwa kwa mujibu wa Qur’an, na aliacha tamaa za mwili. Kwa hiyo chochote kilichoamriwa na Qur’an, alikifanya, na chochote kilichokatazwa alikiepuka. Pamoja na hayo Allah تعالى Alimpa tabia iliyotukuka, ambayo ni pamoja na upole, ukarimu, ukakamavu, usamehevu, uraifu na kila aina ya mwenendo mzuri.

Hii ni kama ilivyokwisha thibitishwa katika Sahihi Mbili kuwa Anas رضي الله عنه amesema, “Nilimhudumia Mtume ﷺ kwa miaka kumi na hakuwahi kusema neno la kuniudhi (*Uff*) na wala hakuwahi kusema juu ya jambo nililotenda; “Kwa nini ulifanya vile?” Na hakusema lolote kwa kile ambacho sikukifanya. ‘Kwa nini hukufanya hiki?’ Alikuwa na tabia nzuri, na sikuwahi kushika kitu laini au Hariri au kitu kingine laini kama kiganja cha Mtume ﷺ. Na sikuwahi kusikia rihi ya miski au uturi kuliko jasho la Mtume ﷺ.”⁵

Imam Al-Bukhari ameandika kuwa Al- Baraai رضي الله عنه amesema, “Mtume ﷺ alikuwa na sura nzuri kuliko watu wote, na alikuwa na tabia nzuri kuliko watu wote. Na hakuwa mrefu wala mfupi.”⁶

¹ At-Tabari 23:529, na *Ad-Dur Al-Manthur* 8:243.

² At-Tabari 23:530.

³ At-Tabari 23:529.

⁴ Muslim 1:513.

⁵ *Fat’hul Al-Bari* 10:471, na Muslim 4:1814.

⁶ *Fat’hul Al-Bari* 6:652.

Hadithi kuhusu suala hili ziko nyingi. Abu Isa At-Tirmidhi ana mlango mzima kuhusu maudhui uitwao mlango wa *Ash-Shamail*.

Imam Ahmad amenukuu kuwa Bi Aishah رضي الله عنها amesema,

“Mtume ﷺ hakuwahi kumpiga mtumishi wake kwa mkono wake, wala hakuwahi kumpiga mkewe. Hakupata kupiga kitu kwa mkono wake isipokuwa katika kupigana Jihad katika njia ya Allah تعالى. Na hakupata kuharishwa vitu viwili isipokuwa alikiendea kilichokuwa chepesi zaidi madhali hakikuwa chenye kumtia makosani. Na kama kilihusu dhambi alijitenga nacho mbali. Hakulipiza kisasi kwa lolote alilofanyiwa, isipokuwa pale mipaka ya Allah تعالى ilipokiukwa. Kwa hali hiyo angalilipiza kwa ajili ya Allah تعالى.”¹

Imam Ahmad pia amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّمَا بُعِثْتُ لِأَتَمِّمَ صَالِحَ الْأَخْلَاقِ»

“Nimetumwa ili kukamilisha tabia njema.”

Ahmad peke yake ndiye aliyehandika Hadithi hii.² Kwa kurejea Kauli ya Allah تعالى,

فَسْتَبْصِرْ وَتُبْصِرُونَ ﴿٦٨﴾ بِأَيِّكُمْ أَلْمَفْتُونُ ﴿٦٩﴾

“Karibu utaona, na wao wataona, ni nani kati yenu aliyepandwa na wazimu.”

Basi Ina Maana: ‘Ufahamu, Wewe Muhammad – na wale wanaokupinga na kukupuuza – watajua – nani ni mwendawazimu na aliyepotoshwa miongoni mwenu.’

Hii ni kama Kauli ya Allah تعالى,

سَيَعْلَمُونَ غَدًا مِّنَ الْكَذَّابِ الْأَشِيرِ ﴿٥٤﴾

“Kesho watajua ni nani huyo muongo mwenye kiburi.” (54:26)

¹ Ahmad 6:232.

² Ahmad 2:381.

Aidha Allah تعالى Amesema,

وَإِنَّا أَوْ إِيَّاكُمْ لَعَلَىٰ هُدًىٰ أَوْ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٢٤﴾

“Na hakika sisi au nyinyi bila ya shaka tuko kwenye uwongofu au upotofu uliowazi.” (34:24)

Ibn Jurayj amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, ina Maana: “Utajua na watajua Siku ya Kiyama”.¹ Al-Awfi amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.

بِأَيِّكُمْ أَلْمَفْتُونُ ﴿٢٥﴾

“Ni nani kati yenu aliyepandwa na wazimu.”

Maana yake: ‘Nani kati yenu ni majinuni.’² Haya yalisemwa pia na Mujahid na wengineo.³

Maana halisi ya “Maftun” ni mtu aliyerogwa au aliyevutwa mbali kutokana na ukweli na amekwenda kombo.⁴

Hivyo, kauli yote ina Maana: ‘Hivyo utajua na watajua’, au ‘Utafahamishwa na wao watafahamishwa, nani kati yenu ni mwenda wazimu.’ Na Allah تعالى ni Mjuzi wa Yote.

Kisha Allah تعالى Amesema,

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿٢٦﴾

“Hakika Mola Wako Mlezi Ndiye Yeye Ajuaye zaidi nani aliyepotea Njia Yake, na Yeye Ndiye Anayewajua zaidi walioongoka.”

Maana yake: “Anajua ni lipi kati ya makundi mawili lipo sahihi, na Anajua kundi lipi lililopotoka.”

¹ Al-Qurtubi 18:229.

² At-Tabari 23:531.

³ At-Tabari 23:530.

⁴ At-Tabari 23:533.

فَلَا تُطْعِ الْمُكَذِّبِينَ ﴿١٦﴾ وَدُّوْا لَوْ تَدَّهِنُ فَيُدْهِنُوْنَ ﴿١٥﴾ وَلَا تُطْعِ كُلَّ حَلَافٍ مَّهِينٍ
 ﴿١٤﴾ هَمَّازٍ مَّشَاءٍ بِنَمِيمٍ ﴿١٣﴾ مَنَاعٍ لِلْخَيْرِ مُعْتَدٍ أَثِيمٍ ﴿١٢﴾ عَتُلٌ بَعْدَ ذَلِكَ رَنِيمٍ ﴿١١﴾
 أَنْ كَانَ ذَا مَالٍ وَبَنِينَ ﴿١٠﴾ إِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِ ءَايَاتُنَا قَالِ كَسْبَطْنَا الْأَوَّلِينَ ﴿٩﴾
 سَنَسِمُهُ عَلَى الْخُرْطُومِ ﴿٨﴾

8. Basi usiwat'ii wanaokadhibisha.

9. Wanatamani lau unge lainisha ili nao wakulainishie.

10. Wala usimt'ii kila mwingi wa kuapa wa kudharauliwa,

11. Mtapitapi, apitaye akifitini,

12. Mwenye kuzuia kheri, dhaalimu, mwingi wa madhambi,

13. Mkavu, na juu ya hayo, mshari, amejipachika tu.

14. Ati kwa kuwa ana mali na watoto!

15. Anaposomewa Aya zetu, husema: Hizi ni simulizi za uwongo za watu wa zamani!

16. Tutamtia kovu juu ya pua yake.

Katazo la Kuridhia Shinikizo la Makafiri na Mapendekezo yao ya Kuchanganya Imani na Ukafiri.

Allah تعالیٰ Anasema, 'kama Tulivyowapendelea na Tukawapeni sharia iliyonyooka na tabia tukufu.'

فَلَا تُطْعِ الْمُكَذِّبِينَ ﴿١٦﴾ وَدُّوْا لَوْ تَدَّهِنُ فَيُدْهِنُوْنَ ﴿١٥﴾

"Basi usiwatii wanaokadhibisha. Wanatamani lau ungelainisha ili nao wakulainishie."

Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, "Kuwa utawaruhusu wao (ushirikina wao) na wao watakuruhusu (kutekeleza dini yako)."¹ Mujahid amesema,

¹ At-Tabari 23:533.

وَدُّوْا لَوْ تَدَّهِنُ فَيَدَّهِنُوْنَ ﴿١﴾

“Wanatamani lau ungelainisha ili nao wakulainishie.”

Inamaanisha kuwa: Unapaswa unyamaze kuhusu miungu yao na uuache ukweli unaoufuata. Kisha, Allah تعالیٰ Anasema:

وَلَا تُطِيعْ كُلَّ حَلَّافٍ مَّهِينٍ ﴿٢﴾

“Wala usimt’ii kila mwingi wa kuapa wa kudharauliwa.”

“Hii ni kwa sababu ni muongo, kutokana na udhaifu wake na kukata kwake tamaa, anatafuta ulinzi kwa viapo vya uongo ambavyo anaapa kwa kutumia majina ya Allah تعالیٰ, na anayetumia (viapo vya uongo) wakati wote na pasipo husika.” Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, “Al-Mahin maana yake muongo.”¹ Kisha Allah تعالیٰ Amesema,

هَمَّازٍ

“Mtapitapi...”

Ibn Abbas رضي الله عنهما na Qatadah wote wamesema, “Msengenyaji mkubwa.”²

مَشَاءٍ بِنَمِيمٍ ﴿٣﴾

“...apitaye akifitini...” Hii inamhusu Mtu anayewapitia watu akiwachochea kuhamasisha fitna baina yao na akichukua maneno huku na kule ili kuvunja mahusiano yao yaliyokuwa mazuri. Ilihitishwa katika Sahihi Mbili kuwa Mujahid alipokea kutoka kwa Tawus kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, “Mtume ﷺ alipita jirani na makaburi mawili na akasema,

«إِنَّهُمَا لِيُعَذَّبَانِ وَمَا يُعَذَّبَانِ فِي كَبِيرٍ، أَمَّا أَحَدُهُمَا فَكَانَ لَا يَسْتَتِرُ مِنَ
الْبَوْلِ، وَأَمَّا الْآخَرُ فَكَانَ يَمْشِي بِالنَّمِيمَةِ»

“Kwa hakika hawa wawili wanaadhibiwa, na hawaadhibiwi kwa kosa kubwa. Mmoja wao hakuwa makini kujiepusha na mikojo (alipokuwa akijisaidia). Mwingine alikuwa akieneza Fitina.”³

¹ At-Tabari 23:533.

² At-Tabari 23:533.

³ Fat’hul Al-Bari 1:358, na Muslim 1:240.

Hadithi hii imenukuliwa na kikundi cha mapokezi na hadithi katika vitabu vyao kupitia silsila za upokezi ambazo zote ziko chini ya mamlaka ya Mujahid.¹

Imam Ahmad alinukuu kuwa Hudhayfah رضي الله عنه alisema, "Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ قَتَاتٌ

*"Mzushi haingia Peponi."*²

Hadithi hii imeripotwa na kundi la wapokezi wa Hadithi isipokuwa Ibn Majah.³ Kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

مَنَّاعٌ لِلْخَيْرِ مُعْتَدٍ أُثِيمٌ

"Mwenye kuzuia kheri, dhaalimu, mwingi wa madhambi."

Ina maana: Anakataa kutoa na anazuia vizuri alivyo navyo.

مُعْتَدٍ

"...dhaalimu..."

Hii ina Maana: Kwa kufikia kile alichohalalishiwa, anavuka mipaka ya sheria.

أُثِيمٌ

"...mwingi wa madhambi..."

Maana yake: Anajichimbia katika yaliyoharamishwa. Kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

عُتُلٌّ بَعْدَ ذَلِكَ زَنِيمٌ

"Mkavu, na juu ya hayo, mshari, amejipachika tu."

"Utul" ina maana mtu katili, mwenye fujo, mwenye nguvu, mlafi na bahili. Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Al-Harithah bin Wahb رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

¹ Abu Dawud 1:25, Tuhfatu Al-Ahwadhi 1:232, An-Nasai 1:28 na 4:412, Al-Kubra 6:496, na Ibn Majah 1:125.

² Ahmad 5:382.

³ Fat'hul Al-Bari 10:487, Muslim 1:101, Abu Dawud 5:190, Tuhfat Al-Ahwadhi 6:172 na An-Nasai katika Al-Kubra 6:496.

«أَلَا أُنَبِّئُكُمْ بِأَهْلِ الْجَنَّةِ؟ كُلُّ ضَعِيفٍ مُتَّعِفٍ لَوْ أَقْسَمَ عَلَى اللَّهِ لَأَبْرَهُ. أَلَا أُنَبِّئُكُمْ
بِأَهْلِ النَّارِ؟ كُلُّ عَثَلٍ جَوَاطِئِ مُسْتَكْبِرٍ»

“Niwaelezeni juu ya watu wa Peponi? (watakuwa) dhaifu na waliokandamizwa. Anapoapa kwa Jina la Allah, anatekeleza kiapo chake. Niwaelezeni juu ya watu wa Motoni? Kila mtu katili, Jawwaz na mtu mkorofi.”¹

Al-Waki amesema, “Utul”_ni kila mwenye roho mbaya mwenye kiburi, Jozari na mtu mkorofi.” Wote Al-Bukhari na Muslim wameandika kwenye Sahih Mbili, vivyo hivyo wameipokea wapokezi wa Hadithi, isipokuwa Abu Dawud. Silsila zote za upokezi ni kupitia njia ya Sufyan Ath-Thawri na Shu’bah ambao wote walipokea kutoka kwa Said bin Khalid.²

Wanazuoni wa lugha ya Kiarabu wamesema kuwa neno “Jadhar” maana yake ni ‘Katili na fedhuli’, ambapo Jawwaz ina maana mwenye roho mbaya.

Kuhusu neno “Zanim”, Al-Bukhari amerekodi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alitoa maelezo ya Aya,

عَثَلٌ بَعْدَ ذَلِكَ زَنِيمٌ ﴿٦٨﴾

“Mkavu, na juu ya hayo, mshari, amejipachika tu.”

“Mtu mmoja wa kabila la Qurayish aliye mashuhuri miongoni mwao kama mbuzi aliyekatwa sikio.”³ Maana yake: Ni kuwa ni maarufu kwa uovu wake kama mbuzi aliyekatwa sikio huwa maarufu kwa wenzake. Katika lugha ya Kiarabu “Zanim” Ni mtu asiyejulikana nasabu yake. Ibn Jarir رحمه الله تعالى na wengineo miongoni mwa Maimamu wamesema hivi. Kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

أَنْ كَانَ ذَا مَالٍ وَبَنِينَ ﴿٦٩﴾ إِذَا تَتَلَّى عَلَيْهِ ءَايَاتُنَا قَالَ أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٧٠﴾

“Ati kwa kuwa ana mali na watoto! Anaposomewa Aya Zetu, husema: Hizi ni simulizi za uwongo za watu wa zamani!”

Allah تعالى Amesema, “hivi ndivyo wanavyolipa fadhila ambazo Allah تعالى

¹ Ahmad 5:306.

² Fat’hul Al-Bari 8:530, Muslim 4:2190, Tuhfat Al-Ahwadhi 7:331, An-Nasai katika Al-Kubra 6:497, na Ibn Majah 2:1378.

³ Al-Bukhari Na. 4917.

Aliwapa za mali na watoto, kwa kutoamini Aya za Allah تعالى na kuzipa mgongo huku wakidai kuwa ni uongo uliochukuliwa kutoka masimulizi ya kale. Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى.

ذَرْنِي وَمَنْ خَلَقْتُ وَحِيدًا ﴿١﴾ وَجَعَلْتُ لَهُ مَالًا مَمْدُودًا ﴿٢﴾ وَبَيْنَ شُهُودًا ﴿٣﴾
 وَمَهْدُتٌ لَهُ تَمْهِيدًا ﴿٤﴾ ثُمَّ يَطْمَعُ أَنْ أَزِيدَ ﴿٥﴾ كَلَّا إِنَّهُ كَانَ لِآيَاتِنَا عَنِيدًا ﴿٦﴾
 سَأَرْهُقُهُ صَغُودًا ﴿٧﴾ إِنَّهُ فَكَّرَ وَقَدَّرَ ﴿٨﴾ فَقَتَلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿٩﴾ ثُمَّ قَتَلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿١٠﴾
 ثُمَّ نَظَرَ ﴿١١﴾ ثُمَّ عَبَسَ وَسَمَرَ ﴿١٢﴾ ثُمَّ أَدْبَرَ وَاسْتَكْبَرَ ﴿١٣﴾ فَقَالَ إِنَّ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ ﴿١٤﴾
 يُؤْتِرُ ﴿١٥﴾ إِنَّ هَذَا إِلَّا قَوْلُ الْبَشَرِ ﴿١٦﴾ سَأُصْلِيهِ سَقَرَ ﴿١٧﴾ وَمَا أَذْرَكَ مَا سَقَرٌ ﴿١٨﴾
 لَا تُتَّقِي وَلَا تَدْرُ ﴿١٩﴾ لَوْ أَحَاطَ لِلْبَشَرِ ﴿٢٠﴾ عَلَيَّآ نِسْعَةَ عَشَرَ ﴿٢١﴾

“Niache Peke Yangu na Niliyemuumba; Na Nikamjaalia awe na mali mengi, Na wana wanaoonekana, Na Nikamtengenezea mambo vizuri kabisa. Kisha anatumai Nimzidishie! Hasha! Kwani hakika yeye alikuwa akizifanyia inadi Aya Zetu! Nitamtesa kwa mateso yasiowezezana. Kwani hakika yeye alifikiri na akapima. Basi ameangamia! Vipi alivyopima! Tena ameangamia! Vipi alivyo pima! Kisha akatazama, Kisha akakunja kipaji, na akanuna. Kisha akaipa kisogo haki, na akatakabari. Na akasema: Haya si chochote ila ni uchawi ulionukuliwa. Haya si chochote ila kauli ya binaadamu. Nitakuja mtia kwenye Moto wa Saqar. Na nini kitakujuulisha ni nini huo Moto wa Saqar? Haubakishi wala hausazi. Unababua ngozi iwe nyeusi. Juu yake wapo kumi na tisa.” (74:11-30)

Kisha Allah تعالى Alisema hapa,

سَنَسْمُهُ عَلَى الْخُرْطُومِ ﴿٢١﴾

“Tutamtia kovu juu ya pua yake.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema, “Tutalifanya jambo lake wazi na ushahidi wamjue na hatoweza kujificha wasimuone kama vile chapa juu ya pua (ya mnyama).”¹

¹ At-Tabari 23:541.

Wengine wanasema,

سَتَيْمَةٌ

“Tutamtia kovu...”

Hii ni chapa ya watu wa Motoni. Sura yake Tutaitia weusi siku ya Kiyama. Na uso hapa umeelezewa kwa kupewa jina la Mkonga wa Tembo.

* * *

إِنَّا بَلَوْنَهُمْ كَمَا بَلَوْنَا أَصْحَابَ الْجَنَّةِ إِذْ أَقْسَمُوا لَيَصْرِمُنَّهَا
 مُصْبِحِينَ ﴿١٧﴾ وَلَا يَسْتَنْوُونَ ﴿١٨﴾ فَطَافَ عَلَيْهَا طَائِفٌ
 مِّن رَّبِّكَ وَهُمْ نَائِبُونَ ﴿١٩﴾ فَأَصْبَحَتْ كَالصَّرِيمِ ﴿٢٠﴾
 فَتَنَادُوا مُصْبِحِينَ ﴿٢١﴾ أَنْ آغِدُوا عَلَيَّ حَزَنًا إِنْ كُنْتُمْ
 صَٰرِمِينَ ﴿٢٢﴾ فَأَنْطَلَقُوا وَهُمْ يَتَخَفَتُونَ ﴿٢٣﴾ أَنْ لَا
 يَدْخُلَهَا الْيَوْمَ عَلَيْكُمْ مَسْكِينٌ ﴿٢٤﴾ وَغَدُوا عَلَيَّ حَزْدٌ
 قَدِيرٍ ﴿٢٥﴾ فَأَمَّا رَأَوْهَا قَالُوا إِنَّا لَضَالُونَ ﴿٢٦﴾ بَلْ نَحْنُ
 مَحْرُومُونَ ﴿٢٧﴾ قَالَ أَوْسَطُهُمْ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ لَوْلَا تُسْمِعُونَ
 ﴿٢٨﴾ قَالُوا سُبحٰنَ رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٢٩﴾ فَأَقْبَلَ
 بَعْضُهُمْ عَلَيَّ بَعْضٍ يَتَلَوَّمُونَ ﴿٣٠﴾ قَالُوا يَنوِيلُنَا إِنَّا كُنَّا
 طٰغِينَ ﴿٣١﴾ عَسَىٰ رَبِّنَا أَنْ يُبَدِّلَنَا خَيْرًا مِّنْهَا إِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا
 رٰغِبُونَ ﴿٣٢﴾ كَذٰلِكَ الْعَذَابُ ۗ وَالْعَذَابُ الْآخِرَةُ أَكْبَرُ لَوْ
 كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٣٣﴾ إِنَّ لِلْمُتَّقِينَ عِندَ رَبِّهِمْ جَنَّٰتٍ أَلْوَعًا
 ﴿٣٤﴾ أَفَتَجْعَلُ الْمُسْلِمِينَ كَالْجَارِمِينَ ﴿٣٥﴾ مَا لَكُمْ كَيْفَ
 تَحْكُمُونَ ﴿٣٦﴾ أَمْ لَكُمْ كِتٰبٌ فِيهِ تَدْرُسُونَ ﴿٣٧﴾ إِنْ لَكُمْ
 فِيهِ مَا تَحْتَرُونَ ﴿٣٨﴾ أَمْ لَكُمْ أَيْمٰنٌ عَلَيْنَا بَلِغْتُمْ إِلَىٰ يَوْمِ
 الْفِئِمَةِ ۗ إِنْ لَكُمْ مَا تَحْكُمُونَ ﴿٣٩﴾ سَأَلْتُمُوهُم بِذٰلِكَ
 زَعِمٌ ﴿٤٠﴾ أَمْ هُمْ شُرَكَاءُ فَلْيَأْتُوا بِشُرَكَائِهِمْ إِنْ كَانُوا
 صٰدِقِينَ ﴿٤١﴾

إِنَّا بَلَوْنَهُمْ كَمَا بَلَوْنَا أَصْحَابَ الْجَنَّةِ
 إِذْ أَقْسَمُوا لَيَصْرِمُنَّهَا مُصْبِحِينَ ﴿١٧﴾
 وَلَا يَسْتَنْوُونَ ﴿١٨﴾ فَطَافَ عَلَيْهَا
 طَائِفٌ مِّن رَّبِّكَ وَهُمْ نَائِبُونَ ﴿١٩﴾
 فَأَصْبَحَتْ كَالصَّرِيمِ ﴿٢٠﴾ فَتَنَادُوا
 مُصْبِحِينَ ﴿٢١﴾ أَنْ آغِدُوا عَلَيَّ
 حَزَنًا إِنْ كُنْتُمْ صَٰرِمِينَ ﴿٢٢﴾
 فَأَنْطَلَقُوا وَهُمْ يَتَخَفَتُونَ ﴿٢٣﴾
 أَنْ لَا يَدْخُلَهَا الْيَوْمَ عَلَيْكُمْ
 مَسْكِينٌ ﴿٢٤﴾ وَغَدُوا عَلَيَّ حَزْدٌ
 قَدِيرٍ ﴿٢٥﴾ فَأَمَّا رَأَوْهَا قَالُوا
 إِنَّا لَضَالُونَ ﴿٢٦﴾ بَلْ نَحْنُ
 مَحْرُومُونَ ﴿٢٧﴾ قَالَ أَوْسَطُهُمْ
 أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ لَوْلَا تُسْمِعُونَ
 ﴿٢٨﴾ قَالُوا سُبحٰنَ رَبِّنَا إِنَّا
 كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٢٩﴾ فَأَقْبَلَ
 بَعْضُهُمْ عَلَيَّ بَعْضٍ يَتَلَوَّمُونَ
 ﴿٣٠﴾ قَالُوا يَنوِيلُنَا إِنَّا كُنَّا
 طٰغِينَ ﴿٣١﴾ عَسَىٰ رَبِّنَا أَنْ
 يُبَدِّلَنَا خَيْرًا مِّنْهَا إِنَّا إِلَىٰ
 رَبِّنَا رٰغِبُونَ ﴿٣٢﴾ كَذٰلِكَ
 الْعَذَابُ ۗ وَالْعَذَابُ الْآخِرَةُ
 أَكْبَرُ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٣٣﴾

17. Hakika Tumewajaribu hawa kama Tulivyowajaribu wale wenye shamba, walipoapa kwamba watayavuna mazao yake itakapokuwa asubuhi.

18. Wala hawakusema: Mungu Akipenda!

19. Basi lilitokea tukio juu yake kutoka kwa Mola Wako Mlezi, nao wamelala!

20. Likawa kama usiku wa giza.

21. Asubuhi wakaitana.

22. Ya kwamba nendeni kondeni mwenu ikiwa mnataka kuvuna.

23. Basi walikwenda na huku wakinong'onezana,

24. Ya kuwa leo hata masikini mmoja asikuingilieni.

25. Na walikwenda asubuhi, nao wameshikilia azimio hilo.

26. Basi walipoliona, wakasema: Hakika tumepotea!

27. Bali tumenyimwa!

28. Mbora wao akasema: Sikukuambieni, kwa nini hamumtakasi Mwenyezi Mungu?

29. Wakasema: Ametakasika Mola Wetu Mlezi! Hakika sisi tulikuwa wenye kudhulumu.

30. Basi wakakabiliana kulaumiana wao kwa wao.

31. Wakasema: Ole wetu! Tulikuwa tumeikiuka mipaka!

32. Asaa Mola wetu Mlezi Akatubadilishia lililo bora kuliko hili. Hakika sisi ni wenye kurejea kwa Mola Wetu Mlezi.

33. Namna hivi yanakuwa mateso, na bila ya shaka mateso ya Akhera ni makubwa zaidi, laiti wangelijua!

Mfano wa Kuondolewa kipato cha Makafiri.

Huu ni mfano Allah تعالى Aliokasi kwa Makafiri wa Kiqureish kwa huruma kubwa na fadhila nyingi Alizowapa. Huruma na fadhila za Kuwapelekea Muhammad ﷺ lakini walimkataa na kumpinga. Kwa hiyo Allah تعالى Anasema,

إِنَّا بَلَوْنَهُمْ

“Hakika Tumewajaribu hawa...” Maana yake: Tumewatahini.

كَمَا بَلَوْنَا أَصْحَابَ الْجَنَّةِ

“...kama Tulivyowajaribu wale wenye shamba.”

Hii inahusu bustani yenye matunda anuwai na mimea.

إِذْ أَقْسَمُوا لِبَصَرِهَا مُصْبِحِينَ ﴿٧٧﴾

“...walipoapa kwamba watayavuna mazao yake itakapokuwa asubuhi...”

Maana yake: Waliapa usiku miongoni mwao kuwa wangelichuma matunda yote bustanini asubuhi ili masikini na ombaomba wasijue wakifanyacho. Na kwa mtindo huo wangelichukua matunda yote na wasitoe sadaka.

وَلَا يَسْتَنْوِنَ ﴿٧٨﴾

“Wala hawakusema: Mungu Akipenda!” Maana yake: Kiapo walichokula. Kwa hiyo, Allah تعالى Alivunja kiapo chao. Kisha Akasema,

فَطَافَ عَلَيْهَا طَآئِفٌ مِّن رَّبِّكَ وَهُمْ نَائِمُونَ ﴿٧٩﴾

“Basi lilitokea tukio juu yake kutoka kwa Mola Wako Mlezi, nao wamelala!”

Maana yake: Waliangamizwa kwa maangamizo ya mbinguni.

فَأَصْبَحَتْ كَالصَّرِيمِ ﴿٨٠﴾

“Likawa kama usiku wa giza.” Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, “Kama usiku wa kiza.”¹ Ath-Thawri na As-Suddi wote wamesema, “Kama mazao yanapovunwa kunyaukushwa na kukaushwa.”

¹ At-Tabari 23:544.

فَتَنَادُوا مُصْحِحِينَ ﴿١٧﴾

“Asubuhi wakaitana.” Maana yake: Ilipokuwa mapema asubuhi wakaitana ili waende pamoja kuvuna (matunda yake). Kisha Allah تعالى Akasema,

أَنْ أَعْدُوا عَلَيَّ حَرْثَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٨﴾

“Ya kwamba nendeni kondeni mwenu ikiwa mnataka kuvuna.”

Maana yake: ‘Kama mnataka kuchuma matunda’

فَأَنْطَلَقُوا وَهُمْ يَتَخَفَتُونَ ﴿١٩﴾

“Basi walikwenda na huku wakinong’onezana.” Maana yake: Walizungumza kwa siri yale waliyokuwa wakiyafanya ili watu wasisikie waliyokuwa wakiyasema. Akasema,

فَأَنْطَلَقُوا وَهُمْ يَتَخَفَتُونَ ﴿٢٠﴾ أَنْ لَا يَدْخُلَهَا الْيَوْمَ عَلَيْكُمْ مَسْكِينٌ ﴿٢١﴾

“Basi walikwenda na huku wakinong’onezana. Ya kuwa leo hata masikini mmoja asikuingilieni.”

Maana yake: Baadhi yao waliwaambia wenzao, “Msimruhusu masikini yeyote kuingia nanyi (bustanini) leo.” Kisha Allah تعالى Akasema,

وَعَدُوا عَلَيَّ حَرْدٍ ﴿٢٢﴾

“Na walikwenda asubuhi...” Maana yake: Kwa nguvu.

قَدِيرِينَ ﴿٢٣﴾

“...nao wameshikilia azimio hilo.” Maana yake: Walidhani walikuwa na nguvu kufanya waliyodai na waliyoyataka.

فَلَمَّا رَأَوْهَا قَالُوا إِنَّا لَصَّالُونَ ﴿٢٤﴾

“Basi walipoliona, wakasema: Hakika tumepotea!” Maana yake: Walipofika pale, na hali ilikuwa imebadilishwa na Allah تعالى kutoka mng’aro, mwangaza mkali na wingi wa matunda kuwa weusi, iliyofifia na isiyoyote. Waliamini kuwa walikosea njia waliyoifuata kuelekea pale. Kwa sababu hii wamesema,

إِنَّا لَصَّالُونَ ﴿٦٨﴾

“Hakika tumepotea!”. Maana yake: Tunatumia njia nyingine tofauti na ile ambayo ingelitufikisha pale. Haya yamesemwa na Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine. Kisha walibadili msimamo na kutanabahi kuwa ilikuwa njia sahihi. Kisha wakasema,

بَلْ نَحْنُ مُحْرَمُونَ ﴿٦٩﴾

“Bali tumenyimwa!”

Maana yake: Hapana shaka, hii ndiyo, lakini hatuna fungu wala sehemu (ya mavuno).

قَالَ أَوْسَطُهُمْ

“Mbora wao akasema...”. Ibn Abbas, Mujahid, Said bin Jubayr, Ikrimah, Muhammad bin Ka'b, Ar-Rabi bin Anas, Adh-Dhahhak na Qatadah رضي الله عنهم wote wamesema, “Hii ina maana ni haki yao na bora kwao.”¹

أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ لَوْلَا تُسَبِّحُونَ ﴿٧٠﴾

“Sikukuambieni, kwa nini hamumtakasi Mwenyezi Mungu?”

Mujahid, As-Suddi na Ibn Jurayji wote wamesema hivyo,

لَوْلَا تُسَبِّحُونَ ﴿٧١﴾

“...kwa nini hamumtakasi Mwenyezi Mungu?” Ina Maana: “Kwa nini hamkusema, “Allah تعالی Angependa?”² As-Suddi amesema, “Kufanya jambo la mbele kwa sharia ya wakati huo mtu alikuwa anasema, “Subhanallah” kwa maana ya kumtakasa Yeye” Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Ni msemu wa mtu, “Allah تعالی Akipenda.”³ Pia imesemwa kuwa ina maana kuwa wakubwa wao waliwaambia, “Sikuambieni, kwa nini hamumtukuzi Allah تعالی na kumshukuru kwa Alivyowapeni na Kuwaneemesha navyo?”

قَالُوا سُبْحَانَ رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٧٢﴾

“Wakasema: Ametakasika Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tulikuwa wenye kudhulumu.”

¹ At-Tabari 23:550.

² At-Tabari 23:550, na *Ad-Dur Al-Manthur* 8:253

³ At-Tabari 23:550

Ikawa kukiri kwao makosa kujutia na kutubia wakati huo hakusaidii tena chochote. Kisha wakasema,

إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٦٨﴾ فَأَقْبَل بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ يَتَلَؤْمُونَ ﴿٦٩﴾

“Hakika sisi tulikuwa wenye kudhulumu. Basi wakabiliana kulaumiana wao kwa wao.”

Maana yake: Walianza kulaumiana wao kwa wao kutokana na waliyoazimia kufanya, kuwazuia masikini kupokea haki yao ya mavuno ya matunda. Hivyo majibizano kwa kila mmoja wao yalikuwa kukiri makosa na madhambi.

قَالُوا يَوَيْلَنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٦٩﴾

“Wakasema: Ole wetu! Tulikuwa tumekiuka mipaka!” (68:31)

Maana yake: ‘Tulichupa mipaka, tulikiuka maamrishi mpaka tukafikwa na hayo.’

عَسَىٰ رَبُّنَا أَنْ يُبَدِّلَنَا حَيْرًا مِّمَّا إِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا رَاغِبُونَ ﴿٧٠﴾

“Asaa Mola Wetu Mlezi Akatubadilishia lililo bora kuliko hili. Hakika sisi ni wenye kurejea kwa Mola Wetu Mlezi.”

Imeelezwa kuwa, “Walikuwa wakitarajia mambo mazuri badala ya maisha ya dunia.” Pia imenenwa kuwa, “Walikuwa wakitarajia malipo kesho Akhera.” Na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. Baadhi ya Salaf wamesema kuwa watu hao ni kutoka Yemen. Said Bin Jubayr alisema, “Walitoka kijiji kinachoitwa Darawan ambacho hapo ni umbali wa maili sita kutoka Sanaa (Yemeni).” Pia imesemwa, “Walikuwa watu wa Ethiopia ambao waliachiwa bustani hii na baba yao, na walikuwa watu wa Kitabu. Baba yao alikuwa akiitunza vyema bustani hiyo. Chochote alichovuna alikirejesha bustanini ili kuiendeleza yenyewe, na aliweka akiba sehemu kama chakula cha familia yake kwa mwaka mzima, na kiasi kingine alitoa sadaka. Kisha alipofariki dunia, watoto wake walirithi bustani na kusema, ‘Kwa hakika baba yetu alikuwa mpumbavu kwa kuwapa baadhi ya mazao masikini. Iwapo tutawanyima tutakuwa na ziada! Hivyo walipoamua kutekeleza waliadhibiwa kinyume na mipango yao. Allah تعالى Alichukua kila walicho kuwa nacho; utajiri, faida na sadaka. Hawakusaliwa na chochote.” Kisha Allah Amesema,

كَذَٰلِكَ أَلْعَدَابُ ﴿٧١﴾

“Namna hivi yanakuwa mateso...” Maana yake: Hii ni adhabu hapa duniani,

kama ulivyoisikia, na adhabu ya Akhera ni ngumu zaidi.

إِنَّ لِلْمُتَّقِينَ عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنَّاتٍ النَّعِيمِ ﴿١٧﴾ أَفَتَجْعَلُ الْمُسْلِمِينَ كَالْجَرِيمِينَ ﴿١٨﴾ مَا لَكُمْ
 كَيْفَ تَحْكُمُونَ ﴿١٩﴾ أَمْ لَكُمْ كِتَابٌ فِيهِ تَدْرُسُونَ ﴿٢٠﴾ إِنَّ لَكُمْ فِيهِ لَمَا تَخْتَرُونَ ﴿٢١﴾ أَمْ
 لَكُمْ أَيْمَانٌ عَلَيْنَا بَلِغَةٌ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ ۗ إِنَّ لَكُمْ لَمَا تَحْكُمُونَ ﴿٢٢﴾ سَلِّمُوا لَهُمْ بَدَلًا
 زَعِيمٌ ﴿٢٣﴾ أَمْ هُمْ شُرَكَاءُ فَلْيَأْتُوا بِشُرَكَائِهِمْ إِنْ كَانُوا صَادِقِينَ ﴿٢٤﴾

34. Hakika wachamungu watakuwa na Bustani za neema kwa Mola Wao Mlezi.

35. Kwani Tutawafanya Waislamu kama wakosefu?

36. Mna nini? Mnahukumu vipi?

37. Au mnacho kitabu ambacho ndani yake mnasoma?

38. Kuwa mtapata humo mnayoyapenda?

39. Au mnazo ahadi za viapo juu Yetu za kufika Siku ya Kiyama ya kuwa hakika mtapata kila mnayojihukumia?

40. Waulize: Ni nani miongoni mwao mdhamini wa haya?

41. Au wanaowashirika? Basi wawalete washirika wao wakiwa wanasema kweli.

Malipo kwa Wachamungu na Muamala Wao Utakuwa Tofauti na Wakosefu.

Baada ya Allah تعالی kuelezea hali ya watu wa bustani ya duniani na ghadhabu kutoka kwa Allah تعالی walipomuasi na kupinga maamrisha Yake, kisha Anaeleza kuwa wachamungu watapewa bustani zinazopendeza sana Akhera, ambazo hazina mwisho. Bustani zitasalia milele na starehe zake hazitokoma kamwe. Allah تعالی Amesema,

أَفَتَجْعَلُ الْمُسْلِمِينَ كَالْجَرِيمِينَ ﴿١٧﴾

“Kwani Tutawafanya Waislamu kama wakosefu?”Maana yake: Tuwashughulikie sawasawa baina yao katika malipo? siyo, kwa Jina la Mola wa mbinguni na ardhini, hapana! Hivyo Allah تعالی Anasema,

مَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ ﴿٦٨﴾

“Mna nini? Mnahukumu vipi?”

Mnawezaje kufikiria hivyo? Kisha Akasema,

أَمْ لَكُمْ كِتَابٌ فِيهِ تَدْرُسُونَ ﴿٦٩﴾ إِنَّ لَكُمْ فِيهِ لَمَا تَخَيَّرُونَ ﴿٧٠﴾

“Au mnacho kitabu ambacho ndani yake mnasoma? Kuwa mtapata humo mnayoyapenda?”

Allah تعالى Anasema katika hili, ‘Mna Kitabu mikononi mwenu ambacho kiliteremshwa kutoka mbinguni mnachokisoma, kuhifadhi na kuwapa wengine, vizazi vya leo vikapokea kutoka vizazi vilivyopita? Mna Kitabu cha aina hiyo, chenye sheria mahsusi kama mnavyodai?’

إِنَّ لَكُمْ فِيهِ لَمَا تَخَيَّرُونَ ﴿٧٠﴾ أَمْ لَكُمْ أَيْمَانٌ عَلَيْنَا بَلِغَةٌ إِلَى يَوْمِ الْفَيْمَةِ ۚ إِنَّ لَكُمْ لَمَا تَحْكُمُونَ ﴿٦٨﴾

“Kuwa mtapata humo mnayoyapenda? Au mnazo ahadi za viapo juu yetu za kufika Siku ya Kiyama ya kuwa hakika mtapata kila mnayojihukumia?”

Maana yake: Mna ahadi na mikataba Nasi?¹

سَلُّهُمْ أَيُّهُمْ بِذَلِكَ زَعِيمٌ ﴿٧١﴾

“...hakika mtapata kila mnayojihukumia?”

Maana yake: ‘Je wanamiungu – masanamu na miungu washindani (minghari ya Allah تعالى)?’

* * *

¹ At-Tabari 23:554.

يَوْمَ يُكْشَفُ عَن سَاقٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ فَلَا
 يَسْتَطِيعُونَ ﴿٤٢﴾ خَشِيعَةً أَبْصَرُهُمْ تَرَهِقُهُمْ ذَلَّةٌ وَقَدْ
 كَانُوا يُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ وَهُمْ سَلِيمُونَ ﴿٤٣﴾ فَذَرْنِي
 وَمَن يُكَذِّبْ بِهَذَا الْحَدِيثِ ۖ سَنَسْتَدْرِجُهُم مِّن حَيْثُ لَا
 يَعْلَمُونَ ﴿٤٤﴾ وَأُمْلِي لَهُمْ ۖ إِنَّ كَيْدِي مَتِينٌ ﴿٤٥﴾ أَمْ
 تَسْأَلُهُمْ أَجْرًا فَهُمْ مِّن مَّغْرَمٍ مُّثْقَلُونَ ﴿٤٦﴾ أَمْ عِندَهُمُ
 الْغَيْبُ فَهُمْ يَكْتُمُونَ ﴿٤٧﴾ فَأَصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ وَلَا تَكُنْ
 كَصَاحِبِ الْاَحْوَاتِ اِذْ نَادَىٰ وَهُوَ مَكْظُومٌ ﴿٤٨﴾ لَوْلَا اَنْ
 تَدَارَكُہٗ رِجْمًا مِّن رَّبِّہٖ لَنُبَذَ بِالْاَعْرَآءِ وَهُوَ مَذْمُومٌ ﴿٤٩﴾
 فَاجْتَبٰہُ رَبُّہٗ فَجَعَلٰہٗ مِّنَ الصّٰلِحِیْنَ ﴿٥٠﴾ وَاِنْ یَّكَذِّبُ
 الَّذِیْنَ كَفَرُوْا لَنُزَلِّقُوْنَكَ بِاَبْصَرِہِمۡ لَمَّا سَمِعُوْا الذِّكْرَ
 وَیَقُوْلُوْنَ اِنَّہٗ لَمَجْنُوْنٌ ﴿٥١﴾ وَمَا هُوَ اِلَّا ذِكْرٌ لِّلْعٰلَمِیْنَ ﴿٥٢﴾

يَوْمَ يُكْشَفُ عَن سَاقٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى
 السُّجُودِ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٤٢﴾
 خَشِيعَةً أَبْصَرُهُمْ تَرَهِقُهُمْ ذَلَّةٌ وَقَدْ
 كَانُوا يُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ وَهُمْ
 سَلِيمُونَ ﴿٤٣﴾ فَذَرْنِي وَمَن يُكَذِّبْ
 بِهَذَا الْحَدِيثِ ۖ سَنَسْتَدْرِجُهُم مِّن
 حَيْثُ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٤﴾ وَأُمْلِي لَهُمْ
 إِنَّ كَيْدِي مَتِينٌ ﴿٤٥﴾ أَمْ تَسْأَلُهُمْ
 أَجْرًا فَهُمْ مِّن مَّغْرَمٍ مُّثْقَلُونَ ﴿٤٦﴾
 أَمْ عِندَهُمُ الْغَيْبُ فَهُمْ يَكْتُمُونَ ﴿٤٧﴾

42. Siku utakapowekwa
 wazi mudi, na wataitwa
 kusujudu, lakini hawa-
 taweza,

43. Macho yao yatainama chini, fedheha itawafunika. Na hakika walikuwa wakiitwa wasujudu walipokuwa wazima.

44. Basi niache na wanao kadhibisha maneno haya! Tutawavutia kidogo kidogo kwa mahali wasipopajua.

45. Na ninawapururia muhula; hakika hila zangu ni imara.

46. Au unawaomba ujira, na wao wanaemewa na gharama hiyo?

47. Au iko kwao siri, basi wao wanaiandika?

Vitisho vya Siku ya Kiyama

Baada ya Allah تعالى Kutaja kuwa wale wenye uchamungu watapewa bustani zenye neema na Mola Wao, Anaelezea siku ya kutokea haya, na uhakika wake.

Allah تعالى Anasema,

يَوْمَ يُكْشَفُ عَن سَاقٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٤٢﴾

‘Siku utakapowekwa wazi mundi, na wataitwa kusujudu, lakini hawataweza.’

Maana yake: Siku ya Hukumu na Vitisho, Matetemeko ya ardhi, Majaribio, Mitihani na mambo makubwa yatakayojiri.

Al-Bukhari amepokea kutoka kwa Abu Said Al-Khudhri رضي الله عنه amesema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«يُكْشِفُ رَبُّنَا عَن سَاقِهِ، فَيَسْجُدُ لَهُ كُلُّ مُؤْمِنٍ وَمُؤْمِنَةٍ، وَيَتَّقِي مَنْ كَانَ يَسْجُدُ فِي الدُّنْيَا رِيَاءً وَشَمْعَةً، فَيَذْهَبُ لِيَسْجُدَ، فَيَعُودُ ظَهْرُهُ طَبَقًا وَاحِدًا»

“Mola Wetu Ataonesha Muundi Wake, hivyo basi kila muumini mwanaume na mwanamke atamsujudia Yeye. Atabaki amesimama (kwa kutoweza kusujudu) yule aliyesujudu hapa duniani ili aonekane na kusikika (kujionesha). Mtu huyo atajaribu kusujudu wakati huo, lakini mgongo wake utafanywa mgumu (mfupa hautokunjika).”

Hadithi hii imenukuliwa katika Sahihi Mbili na vitabu vingine kutoka isinadi tofuati na kwa maneno tofauti. Ni hadithi ndefu na maarufu.¹ Kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

خَشِيعَةً أَبْصَرُهُمْ تَرَهْقُهُمْ ذَلَّةً

“Macho yao yatainama chini, fedheha itawafunika.”

Maana yake: Katika makazi yao ya mwisho, kutokana na uhalifu na kutakabari kwao hapa duniani. Hivyo wataadhibiwa kwa kutenda kinyume cha walichofanya. Walipoambiwa kusujudu katika maisha ya hapa duniani, walikataa kufanya hivyo japokuwa walikuwa na afya na wako salama. Kwa

¹ Fat'hul Al-Bari 8:531, 532, na Muslim 1:167.

hiyo wataadhibiwa kutokana na kushindwa kufanya hivyo Siku ya Kiyama. Mola Mtukufu Atakapojidhihirisha (mbele ya waumini) waumini wataanguka chini na kumsujudia Yeye, lakini hapana kati ya makafiri na wanafiki watakaoweza kusujudu. Kila mmoja atajaribu kusujudu, atainamisha mgongo wake lakini makafiri hawatoweza kusujudu. Kama ambavyo walikuwa wakifanya hapa duniani, tofauti na waumini wao wataweza.

Karipio Kali kwa Yeyote Anayepinga Qur'an.

Kisha Allah تعالی Amesema,

فَذَرْنِي وَمَنْ يُكَذِّبُ بِهَذَا الْحَدِيثِ ۗ

“Basi niache na wanaokadhibisha maneno haya!”

Maana yake: Qur'an. Huu ni ukaripiaji mkali wenye maana, “Niacheni na mtu huyu; Mimi Namjua na namna Nitakavyomuadhibu taratibu na Kumuongozea upotofu. Ninampumzisha kwa muda, kisha Nitawaadhibu adhabu kali na chungu. ‘Hivyo, Allah تعالی Anasema,

سَنَسْتَدْرِجُهُم مِّنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٤﴾

“Tutawavutia kidogo kidogo kwa mahali wasipopajua.”

Maana yake, na hawatotanabahi. Bali wataamini kuwa hiyo ni rehma kutoka kwa Allah تعالی, lakini kwa hakika suala hilo ni aina ya udhalilishaji kwao. Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالی,

أَحْسَبُونَ أَنَّمَا نُمِدُّهُم بِهِءٍ مِنْ مَّالٍ وَبَيْنَ ۙ نُسَارِعُ لَهُمْ فِي الْخَيْرَاتِ ۗ بَلْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٦﴾

“Je! Wanadhani ya kuwa kwa vile Tunavyowapa mali na watoto. Ndio Tunawahimizia kheri? Lakini wenyewe hawatambui.” (23:55-56)

Aidha, Allah تعالی Amesema,

فَلَمَّا سُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِءٍ فَتَحْنَا عَلَيْهِمَ أَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ حَتَّىٰ إِذَا فَرِحُوا بِمَا أُوتُوا

أَخَذْنَاهُمْ بِغَتَّةٍ فَإِذَا هُمْ مُبْلِسُونَ ﴿٥٧﴾

“Basi waliposahau walivyokumbushwa Tuliwafungulia milango ya kila kitu. Mpaka walipofurahia yale waliyopewa Tuliwashika kwa ghafla, na mara wakawa wenye kukata tamaa.” (6:44)

Kwa hiyo, Allah تعالى Anasema hapa,

وَأْمَلِي هُمْ

“Na Ninawapururia muhula...”

Maana yake: ‘Nitawachelewesha, Kuwapumzisha na Kuwaongezea muda. Hata hivyo huu ni Mpango Wangu, hizi ni njama Zangu kwao.’ Hivyo Allah تعالى Amesema,

إِنَّ كَيْدِي مَتِينٌ

“...hakika Hila Zangu ni imara...”

Maana yake: “Kubwa dhidi ya yeyote anayepinga Amri Yangu, anawakana Mitume Wangu na anadiriki Kuniasi.” Katika Sahihi Mbili imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema,

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى يُبْلِي لِلظَّالِمِ حَتَّىٰ إِذَا أَخَذَهُ لَم يَفْلِتْهُ»

“Hakika Allah Aliyetukuka Anamcheleweshea adhabu mkosaji mpaka Atakapomchukua hatoweza kumtoroka.”

Kisha Akasema,

وَكَذَٰلِكَ أَخَذُ رَبِّكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرَىٰ وَهِيَ ظَالِمَةٌ إِنَّ أَخَذَهُ أَلِيمٌ شَدِيدٌ

“Na ndio kama hivyo ndivyo inavyokuwa Mola Wako Mlezi Anapoikamata miji inapokuwa imedhulumu. Hakika Mkamoto Wake ni Mchungu na Mkali.” (11:102)¹

Kwa kurejea Kauli ya Allah تعالى,

أَمْ تَسْأَلُهُمْ أَجْرًا فَهُمْ مِنْ مَّغْرَمٍ مُّقْتَلُونَ ﴿١١﴾ أَمْ عِنْدَهُمُ الْغَيْبُ فَهُمْ يَكْتُمُونَ ﴿١٢﴾

“Au unawaomba ujira, na wao wanaemewa na gharama hiyo? Au iko kwao siri, basi wao wanaiandika?”

¹ Fat’hul Al-Bari 8:205, na Muslim 4:1997.

Maelezo ya Aya hizi mbili yametangulia katika *Surat At-Tur*. Maana yake: Ewe Muhammad, walinganie kwa Allah تعالى bila kuchukua ujira kutoka kwao, bali, utarajie malipo kutoka kwa Allah تعالى. Pamoja na hayo, wana kanusha ulichowaletea kwa sababu ya ujinga, kukufuru na kususia.

فَأَصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ وَلَا تَكُنْ كَصَاحِبِ الْأُخْتِ إِذْ نَادَىٰ وَهُوَ مَكْظُومٌ ﴿٤٢﴾ لَوْلَا أَن تَدَارَكُهُ نِعْمَةٌ مِّن رَّبِّهِ لَنُبِذَ بِالْعَرَاءِ وَهُوَ مَذْمُومٌ ﴿٤٣﴾ فَاجْتَبِهْ رَبُّهُ فَجَعَلَهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٤٤﴾ وَإِن يَكَادُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَيُزْلِقُونَكَ بِأَبْصَرِهِمْ لَمَّا سَمِعُوا الذِّكْرَ وَيَقُولُونَ إِنَّهُ لَمَجْنُونٌ ﴿٤٥﴾ وَمَا هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿٤٦﴾

48. Basi ingojee hukumu ya Mola wako Mlezi, wala usiwe kama mmezwa na samaki, aliponadi naye kazongwa.

49. Kama isingelimfikia neema kutoka kwa Mola wake Mlezi, bila ya shaka angelitupwa ufukweni naye ni mwenye kulaumiwa.

50. Lakini Mola wake Mlezi alimteua na akamfanya miongoni mwa watu wema.

51. Na waliokufuru hukaribia kukutelezesha kwa macho yao, wanaposikia mawaidha, na wanasema: Hakika yeye ni mwendawazimu.

52. Na hayakuwa haya, ila ni ukumbusho kwa walimwengu wote.

Amri ya kuwa na Subira na Kuacha kufanya pupa Mithili ya Nabii Yunus عليه السلام.

Allah تعالى Amesema,

فَأَصْبِرْ

“Basi ingojee...”

“Ewe Muhammadi, vumilia dhidi ya madhara waliokufanyia watu wako kwa kukukana wewe. Kwani kwa hakika Allah تعالى Atakupa mamlaka juu yao, na Atakupa ushindi wa mwisho pamoja na wafuasi wako hapa duniani na Akhera.”

وَلَا تَكُنْ كَصَاحِبِ الْاَحْوَاتِ

“...wala usiwe kama mmezwa na samaki...”

Maana yake: *Dhan-Nun*, ambaye ni Nabii Yunus bin Matta عليه السلام, alipowakasirikia watu wake. Mambo mengi yalimtokea, kupanda meli baharini, kumezwa na samaki mkubwa, kuchukuliwa na samaki baharini, kuwa katika giza na ndani ya kina cha bahari na akasikia bahari na viumbe viishivyo humo vikimtukuza Aliye Juu. Muweza wa Yote. Kwani Allah تعالى Ndiye Pekee Ambaye Amri Zake za Kiungu Haziwezi kuzuiwa. Baada ya yote Nabii Yunus عليه السلام Alitolewa kutoka matabaka ya giza.

﴿٤٧﴾ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ

“Hapana muabudiwa isipokuwa Wewe Subhanaka - Uliyetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu.” (21:87)

Kisha Allah تعالى Alizungumzia habari zake,

﴿٤٨﴾ فَاسْتَجَبْنَا لَهُ وَوَجَّعْنَاهُ مِنَ الْعَرَّةِ وَكَذَلِكَ نُشَجِّي الْمُؤْمِنِينَ

“Basi Tukamuitikia na Tukamuokoa kutokana na dhiki. Na hivyo ndivyo Tunavyowaokoa Waumini.” (21:88)

Aidha, Allah تعالى Amesema,

﴿٤٩﴾ فَلَوْلَا أَنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُسَبِّحِينَ ﴿٥٠﴾ لَلَّيْتُ فِي بَطْنِهِ إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُونَ

“Na ingelikuwa hakuwa katika wanaomtakasa Mwenyezi Mungu, Bila ya shaka angelikaa ndani yake mpaka siku ya kufufuliwa.” (37:143-144)

Hivyo hapa (katika Surah hii) Allah تعالى Amesema,

﴿٥١﴾ إِذْ نَادَى وَهُوَ مَكْظُومٌ

“...aliponadi naye kazongwa.”

Ibn Abbas, Mujahid na As-Suddi رضي الله عنهم, wote walisema, “alipolemewa”.¹ Kisha Allah تعالى Anaendelea Kusema,

¹ At-Tabari 23:563.

فَاجْتَبَيْهِ رَبُّهُ فَجَعَلَهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٦٨﴾

“Lakini Mola Wake Mlezi Alimteua na Akamfanya miongoni mwa watu wema.”

Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Abdullah رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema:

«لَا يَتَّبِعِي لِأَحَدٍ أَنْ يَقُولَ: أَنَا خَيْرٌ مِنْ يُوسُفَ بْنِ مَتَّى»

“Haifai kwa mmoja wenu kusema kuwa Mimi ni bora kuliko Yunus bin Matta.”¹

Al-Bukhari ameandika Hadithi hii² na imo ndani ya Sahihi Mbili. Imepokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه.³

Kuhusu Kauli ya Allah تعالى

وَأَن يَكَاذَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَيُزْلِقُونَكَ بِأَبْصَرِهِمْ

“Na waliokufuru hukaribia kukutelezesha kwa macho yao.”

Ibn Abbas, Mujahid na wengineo wamesema,

لَيُزْلِقُونَكَ

“...kukutelezesha...” Ili iwe na athari kwenu.⁴

بِأَبْصَرِهِمْ

“...kwa macho yao.”

‘Watawaathirini kwa kuwaangalieni kwa macho yao maovu. Hii ina maana wanakuoneeni wivu kwa kuwa wanakuchukieni, na kama isingelikuwa ulinzi wa Allah تعالى wa kuwahami dhidi yao (kijicho chao kingeliwadhuru).’

¹ Ahmad 1:390.

² Fat’hul Al-Bari 6:519.

³ Fat’hul Al-Bari 8:144, na Muslim 4:1846.

⁴ At-Tabari 23:564, 565.

Athari za Kijicho ni Kweli.

Katika Aya hii kuna ushahidi kuwa athari za kijicho na kudhuru kwake kwa Amri ya Allah تعالى ni uhakika. Hadithi nyingi zimeripotwa kuhusu hili kupitia isnadi tofauti.

Hadithi ya Buraydah bin Al-Husayb رضي الله عنه

Abu Abdullah bin Majah amepokea kutoka kwa Buraydah bin Al-Husayb رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا رُقِيَّةَ إِلَّا مِنْ عَيْنٍ أَوْ حُمَةٍ»

“Hapana Ruqyah ila kwa kuponya kijicho na sumu ya ng’e.”¹

Hivi ndivyo Ibn Majah alivyonukuu Hadithi hii. Aidha Imam Muslim alinukuu Hadithi hii katika Sahihi yake kutoka kwa Buraydah mwenyewe, lakini hakuihusisha na Mtume ﷺ. *Mawqif* kuna kisa kuhusu tukio hili (kama ilivyoripotiwa na Buraydah ndani ya Sahihi Muslim),² At-Tirmidhi amenukuu hadithi hii.³ Hadithi hii pia imenukuliwa na Imam Al-Bukhari, Abu Dawud na At-Tirmidhi kutoka kwa Imran bin Husayn, hata hivyo hakuihusisha na Mtume ﷺ. *“Mawqif”* ni,

«لَا رُقِيَّةَ إِلَّا مِنْ عَيْنٍ أَوْ حُمَةٍ»

“Hapana Ruqyah ila kwa kuponya kijicho na sumu ya ng’e.”⁴

Muslim amenukuu ndani ya Sahihi yake kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema,

«الْعَيْنُ حَقٌّ وَلَوْ كَانَ شَيْءٌ سَابِقَ الْقَدَرِ سَبَقَتْ الْعَيْنُ وَإِذَا اسْتُغْلِبْتُمْ فَاغْلِبُوا»

“Kijicho ni hakika. Na kama kuna kitu kilitaka kuitangulia Qadar (na kubadili), basi ingelikuwa kijicho. Na iwapo mnaoga (ili kuondoa kijicho) basi ogeni sawasawa.”⁵

¹ Ibn Majah 2:1161.

² Muslim 1:199.

³ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:217.

⁴ Ibn Majah 2:1161.

⁵ Muslim 4:1719.

Muslim pekee ndiye aliyeandika Hadithi hii, Al-Bukhari hakuitaja Hadithi hii. Imepokelewa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa amesema, "Mtume ﷺ alikuwa akiomba Ulinzi wa Allah تعالى kwa ajili ya Al-Hassan na Al-Husayn رضي الله عنهما (wajukuu wake) kwa kusema,

«أُعِيدُكُمْ بِكَلِمَاتِ اللَّهِ النَّامَةِ مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ وَهَامَّةٍ، وَمِنْ كُلِّ عَيْنٍ لَامَةٍ»

"Naomba Ulinzi kwa ajili yenu wawili kwa Maneno ya Allah kutokana na kila Shaytan, na viumbe hatari, na jicho ovu"

Kisha akasema:

«هَكَذَا كَانَ إِبْرَاهِيمُ يُعَوِّذُ إِسْحَاقَ وَإِسْمَاعِيلَ عَلَيْهِمَا السَّلَامُ»

"Kama hivi ndivyo Ibrahim alivyokuwa akiomba kinga ya Allah juu ya wanaye, Is'haq na Ismail "

Hadithi imenukuliwa na Al-Bukhari na wakusanyaji wa Sunnah.¹

Hadithi ya Abu Umamah Asad bin Sahl bin Hunayf رضي الله عنه.

Ibn Majah amenukuu kutoka kwa Abu Umamah Asad bin Sahl bin Hunayf رضي الله عنه kuwa Amir bin Rabiah رضي الله عنه alipita kwa Sahl bin Hanayf رضي الله عنه wakati akioga na amesema, "Sijapata kuona ngozi nzuri kama hii ninayoiona leo - maana yake akielezea uzuri wa ngozi ya Sahl." Kwa hiyo hakuondoka kabla ya yeye (Sahl) kuanguka chini. Wakampeleka haraka kwa Mtume ﷺ na kumuambia Sahl رضي الله عنه ameshikwa na kifafa.

Kisha Mtume ﷺ akasema,

«مَنْ تَتَّهَمُونَ بِهِ؟»

"Mnamtuhumu nani kwa hili?"

Watu wakajibu, "Amir bin Rabiah رضي الله عنه." Kisha Mtume ﷺ akasema,

¹ Fat'hul Al-Bari 6:470, Abu Dawud 5:104, Tuhfat Al-Ahwadhi 6:220, An-Nasai katika Al-Kubra 6:250, na Ibn Majah 2:1164.

«غَلَامٌ يَقُولُ أَأَحَاةٌ؟ إِذَا رَأَى أَحَدَكُمْ مِنْ أَحِبِّهِ مَا يُعْجِبُهُ فَلْيَدْعُ لَهُ بِالْبَرَكَاتِ»

“Je, mmoja wenu anaweza kumuua nduguye? Iwapo mmoja wenu ataona kitu kwa nduguye kimpendezacho, basi amuombe rehema na baraka.”

Kisha Mtume ﷺ alitaka aletewe maji na akamuamuru Amir atawadhe kwa maji. Aliosha uso wake, mikono yake mpaka kwenye viwiko viwili, magoti mawili na ndani ya nguo yake. Kisha Mtume ﷺ akamuamuru amwagiwe Sahl رضي الله عنه. Sufyan amesema kuwa Maamar alipokea kutoka kwa Az-Zuhr kuwa amesema, “Mtume ﷺ alimuamuru Sahli رضي الله عنه augeuze mtungi wa maji juu chini (kwa maana ajimwagie).”¹ An-Nasai alipokea Hadithi hii kupitia isnadi tofauti kutoka kwa Abu Umaamah رضي الله عنه kwa maneno haya; “Na akigeuze chombo cha maji upande wa nyuma yake.”²

Hadithi ya Abu Said Al-Khudhri رضي الله عنه

Ibn Majah ameandika kuwa Abu Said Al-Khudhri رضي الله عنه amesema, “Mtume ﷺ amekuwa akijikinga na kijicho cha Majini na Binadamu. Na zilipotemshwa sura mbili za kujikinga,³ ikawa Mtume ﷺ anazisoma hizo, na kuachana na dua za mwanzo.”⁴

Hii imenukuliwa na At-Tirmidhi, na An-Nasai. At-Tirmidhi aliipa daraja la “Hasan.”⁵

Hadithi nyingine kutoka kwa Abu Said رضي الله عنه

Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Said رضي الله عنه kuwa Jibril عليه السلام alikuja kwa Mtume ﷺ na akasema, “Ewe Muhammad!, unaugua maradhi yoyote?” Mtume ﷺ akasema,

«نَعَمْ»

“Ndiyo” Kisha Jibril عليه السلام akasema,

¹ Sunan Ibn Majah Na. 3509.

² An-Nasai katika Al-Kubra na. 7617-7619.

³ Surat Al-Falaq (113) na Surat An-Nas (114).

⁴ Ibn Majah 2:1161.

⁵ Tuhfat ul Al-Ahwadhi 6:218, na An-Nasai 8:271.

«بِسْمِ اللَّهِ أَرْزِقُكَ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ يُؤْذِيكَ، وَمِنْ شَرِّ كُلِّ نَفْسٍ وَعَيْنٍ تَشْفِيكَ، وَاللَّهُ يَشْفِيكَ، بِاسْمِ اللَّهِ أَرْزِقُكَ»

*'Kwa Jina la Allah, nakuombea upone (Ruqyah), kutokana na kile kitu kinachokusumbua, kutokana na uovu wa kila nafsi na kijicho kinachokuchukia, Allah Akuponye, kwa Jina la Allah nakuombea upone.'*¹

Hadithi hii imenukuliwa na Muslim na wakusanyaji wa *Sunnan* isipokuwa Abu Dawud.²

Imam Ahmad pia amepokea kutoka kwa Abu Said رضي الله عنه au Jabir bin Abdullah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alihangaishwa na maradhi, na Jibril عليه السلام akamjia na kumuambia,

«بِسْمِ اللَّهِ أَرْزِقُكَ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ يُؤْذِيكَ، مِنْ كُلِّ حَاسِدٍ وَعَيْنٍ، اللَّهُ يَشْفِيكَ»

*"Kwa Jina la Allah nakuombea upone (Ruqyah) kutokana na kile kinachokusumbua, kutokana na mtu mwenye husuda na kijicho, Allah Akuponye."*³

Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه.

Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Harayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ الْغَيْبَ حَقٌّ»

*"Kwa hakika kijicho ni kweli."*⁴

Wote Al-Bukhari na Muslim wamenukuu hadithi hii pia⁵

Ibn Majah amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

¹ Ahmad 3:28,56.

² Muslim 4:1718, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 4:46, na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:249, na Ibn Majah 2:1164.

³ Ahmad 3:58, 75.

⁴ Ahmad 2:319.

⁵ *Fat'hul Al-Bari* 10:213. na Muslim 4:1719.

«الْعَيْنُ حَقٌّ»

“Kijicho ni hakika”¹

Ibn Majah pekee ndiye aliyenukuu Hadithi hii.

Hadithi ya Asma bint Umays رضي الله عنها.

Imam Ahmad amepokea kutoka kwa Ubayd bin Rifa'ah Az-Zuraqi kuwa Asma رضي الله عنها amesema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Kwa hakika, Bani Jafar walidhuriwa na kijicho, Je niwaombe Dua ya *Ruqyah*?’ Mtume ﷺ akajibu,

«نَعَمْ فَلَوْ كَانَ شَيْءٌ يَسْبِقُ الْقَدَرَ لَسَبَقْتَهُ الْعَيْنُ»

“Ndiyo, kama kuna kitu kitashinda Qadar, kitakuwa kijicho.”²

Hadithi hii imenukuliwa hivi na At-Tirmidhi, Ibn Majah,³ na An-Nasai. Al-Tirmidhi amelezea kuwa ni “*Hasan Sahih*.”⁴

Hadithi ya Aishah رضي الله عنها.

Ibn Majah amenukuu kutoka kwa Aishah رضي الله عنها, kuwa amesema, “Mtume ﷺ amemuamuru kufanya “*Ruqyah*” ili iwe ponyo la kijicho.”⁵ Hadithi hii imeripotiwa na Al-Bukhari na Muslim.⁵

Hadithi ya Sahl bin Hunayf رضي الله عنه.

Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa Abu Umamah bin Sahl bin Hunayf رضي الله عنه kuwa baba yake alimfahamisha kuwa Mtume ﷺ alikwenda safari kuelekea Makkah akifuatana na Masahaba mpaka walipofika katika njia za Kharrar kutoka Al-Juhfah. Walipumzika pale na Sahl رضي الله عنه alikoga. Alikuwa ni mweupe, na ngozi yake iking'aa kwa uzuri. Kwa hiyo kaka wa Bani Adi bin

¹ Ibn Majah 2:1159.

² Ahmad 5: 438.

³ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:219, na Ibn Majah 2:1160.

⁴ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:220.

⁵ Ibn Majah 2:1161.

⁶ *Fat'hul Al-Bari* 10:210, na Muslim 4:1725.

Ka'b, Amir bin Rabiah رضي الله عنه alimuangalia Sahl رضي الله عنه alipokuwa anaoga na akasema, "Sijapata kuona ngozi nzuri yenye kumpendeza kama hii." Ghafla Sahl رضي الله عنه alishikwa na kifafa akaanguka chini. Hivyo akapelekwa kwa Mtume ﷺ! Wakamuambia unaweza kumsaidia Sahl رضي الله عنه? Wallahi, hajanyanyua kichwa chake wala kupata fahamu." Kisha Mtume ﷺ akauliza,

«هَلْ تَتَّهَمُونَ فِيهِ مِنْ أَحَدٍ؟»

"Je, mnamtuhumu mtu yeyote katika hili lililotokea?"

Wakasema, "Amir bin Rabiah رضي الله عنه alimuangalia." Hivyo Mtume ﷺ alimuita Amir رضي الله عنه na akamkasirikia. Akasema,

«عَلَّامٌ يَقْتُلُ أَحَدَكُمْ أَخَاهُ، هَلَّا إِذَا رَأَيْتَ مَا يُعْجِبُكَ بَرَكْتَ؟»

"Je, mmoja wenu anaweza kumuua nduguye huku anajua? Kwa nini hamumuombi Allah Ambariki ndugu yenu mnapomuona ana kitu mkipendacho?"

Kisha Mtume ﷺ akasema,

«اِغْتَسِلْ لَهُ»

"Muogesheni."

Hivyo wakamuosha uso wake, mikono, viwiko, magoti, miguu yake na ndani ya nguo yake, ndani ya chombo cha kunywa maji. Kisha maji yale alimiminiwa Sahl رضي الله عنه. Mtu alimuagia Sahl رضي الله عنه kichwani na mgongoni akiwa nyuma yake. Hili lilifanywa, na baadaye Sahl alipata ahueni na akaondoka na watu akiwa hana shida yoyote."¹

Hadithi ya Amir bin Rabiah رضي الله عنه.

Imam Ahmad ameandika katika kitabu chake cha Musnadi kuwa Ubaydullah bin Amir رضي الله عنه amesema, "Amir bin Rabiah na Sahl bin Hunayf انهما رضي الله عنهما walitoka pamoja kwa azma ya kuoga. Kwa hiyo walioga huku wamejifunika uchi. Amir رضي الله عنه aliondoa joho la sufi alililojihifadhia (sahl رضي الله عنه). Amir رضي الله عنه akasema, "Nilimuangalia na jicho likatua mwilini mwake alipokuwa

¹ Ahmad 3:486.

akijimwagia maji. Kisha nilisikia sauti ya maji kutokea alipokuwa. Hivyo nikaenda alipokuwa nikamuita mara tatu, lakini hakunijibu. Ikabidi niende kwa Mtume ﷺ na kumueleza yaliyojiri. Mtume ﷺ alikuja kwa miguu na akitembea majini. Bado nakumbuka weupe wa maundi yake. Alipokuja kwa Sahl رضي الله عنه aliyepoteza fahamu akakipiga kifua chake kwa mkono wake kisha akasema,

«اللَّهُمَّ اصْرِفْ عَنْهُ حَرَّهَا وَبَرْدَهَا وَوَصَبَهَا»

“Ewe Allah! Muondolee joto lake baridi yake na maumivu yake.”

Sahl رضي الله عنه akasimama wima, na Mtume ﷺ akasema,

«إِذَا رَأَى أَحَدَكُمْ مِنْ أَخِيهِ، أَوْ مِنْ نَفْسِهِ، أَوْ مِنْ مَالِهِ مَا يُعْجِبُهُ، فَلْيَبْرِكْ فَإِنَّ الْعَيْنَ حَقٌّ»

“Iwapo mmoja wenu atamuona nduguye, au mwenyewe, au mali yake ambayo inampendezesha, basi amuombe Allah Aibariki, kwani kijicho ni cha kweli.”¹

Tuhuma za Makafiri na Jibu Lao.

Allah تعالى Amesema,

وَيَقُولُونَ إِنَّهُ لَمَجْنُونٌ ﴿٦٨﴾

“...na wanasema: Hakika yeye ni mwendawazimu.”

Maana yake: Wanamkejeli kwa macho yao na kumshambulia kwa ndimi zao wakisema, “Kwa hakika yeye ni mwenda wazimu.” Wanasema hivi kwa sababu alikuja na Qur’an. Kisha Allah تعالى Amesema,

وَمَا هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿٦٩﴾

“Na hayakuwa haya, ila ni ukumbusho kwa walimwengu wote.”

Huu ni mwisho wa maelezo ya Tafsiri ya *Suratu Nun* (au *Al-Qalam*). Shukrani zote na Rehema zinamstahiki Allah تعالى.

* * *

¹ Ahmad 3:447.

Tafsiri ya Suratul Haqqah

Sura ya 69

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْحَاقَّةِ

الْحَاقَّةُ ﴿١﴾ مَا الْحَاقَّةُ ﴿٢﴾ وَمَا أُذْرِكُ مَا الْحَاقَّةُ ﴿٣﴾
 كَذَّبَتْ ثَمُودُ وَعَادٌ بِالْقَارِعَةِ ﴿٤﴾ فَأَمَّا ثَمُودُ فَأَهْلِكُوا
 بِالطَّاغِيَةِ ﴿٥﴾ وَأَمَّا عَادٌ فَأَهْلِكُوا بِرِيحِ صَرْصَرٍ عَاتِيَةٍ ﴿٦﴾
 سَخَّرَهَا عَلَيْهِمْ سَبْعَ لَيَالٍ وَتَمَنِيَةً أَيَّامٍ حُسُومًا ﴿٧﴾
 فَتَرَى الْقَوْمَ فِيهَا صَرْعَى كَأَنَّهُمْ أُعِجَازٌ مُخْلِ حَاوِيَةٍ ﴿٨﴾
 فَهَلْ تَرَى لَهُمْ مِنْ بَاقِيَةٍ ﴿٩﴾ وَجَاءَ فِرْعَوْنُ وَمَنْ قَبْلَهُ
 وَالْمُؤْتَفِكْتُ بِالْخَاطِئَةِ ﴿١٠﴾ فَعَصَا رَسُولَ رَبِّهِمْ فَأَخَذَهُمْ
 أَخْذَةً رَابِيَةً ﴿١١﴾ إِنَّا لَمَّا طَغَا الْمَاءُ حَمَلْنَاكُمْ فِي الْجَارِيَةِ
 ﴿١٢﴾ لِنَجْعَلَهَا لَكُمْ تَذْكِرَةً وَتَعِيًّا أُذُنٌ وَعِيَّةٌ ﴿١٣﴾ فإِذَا
 نُفِخَ فِي الصُّورِ نَفْخَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿١٤﴾ وَحُمِلَتِ الْأَرْضُ
 وَالْجِبَالُ فَدُكَّتَا دَكَّةً وَاحِدَةً ﴿١٥﴾ فَيَوْمَئِذٍ وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ
 ﴿١٦﴾ وَانْشَقَّتِ السَّمَاءُ فَهِيَ يَوْمَئِذٍ وَاهِيَةٌ ﴿١٧﴾ وَالْمَلَكُ
 عَلَى أَرْجَائِهَا ﴿١٨﴾ وَيَحْمِلُ عَرْشَ رَبِّكَ فَوْقَهُمْ يَوْمَئِذٍ مَنِينٌ ﴿١٩﴾
 يَوْمَئِذٍ تُعْرَضُونَ لَا تَخْفَى مِنْكُمْ خَافِيَةٌ ﴿٢٠﴾

الْحَاقَّةُ ﴿١﴾ مَا الْحَاقَّةُ ﴿٢﴾ وَمَا
 أُذْرِكُ مَا الْحَاقَّةُ ﴿٣﴾ كَذَّبَتْ ثَمُودُ
 وَعَادٌ بِالْقَارِعَةِ ﴿٤﴾ فَأَمَّا ثَمُودُ
 فَأَهْلِكُوا بِالطَّاغِيَةِ ﴿٥﴾ وَأَمَّا عَادٌ
 فَأَهْلِكُوا بِرِيحِ صَرْصَرٍ عَاتِيَةٍ ﴿٦﴾
 سَخَّرَهَا عَلَيْهِمْ سَبْعَ لَيَالٍ وَتَمَنِيَةً
 أَيَّامٍ حُسُومًا فَتَرَى الْقَوْمَ فِيهَا
 صَرْعَى كَأَنَّهُمْ أُعِجَازٌ مُخْلِ حَاوِيَةٍ ﴿٨﴾
 فَهَلْ تَرَى لَهُمْ مِنْ بَاقِيَةٍ ﴿٩﴾ وَجَاءَ
 فِرْعَوْنُ وَمَنْ قَبْلَهُ وَالْمُؤْتَفِكْتُ
 بِالْخَاطِئَةِ ﴿١٠﴾ فَعَصَا رَسُولَ رَبِّهِمْ
 فَأَخَذَهُمْ أَخْذَةً رَابِيَةً ﴿١١﴾ إِنَّا لَمَّا
 طَغَا الْمَاءُ حَمَلْنَاكُمْ فِي الْجَارِيَةِ ﴿١٢﴾
 لِنَجْعَلَهَا لَكُمْ تَذْكِرَةً وَتَعِيًّا أُذُنٌ
 وَعِيَّةٌ ﴿١٣﴾

1. *Tukio la haki.*
2. *Nini hilo Tukio la haki?*
3. *Na nini kitakujuulisha nini hilo Tukio la haki?*
4. *Thamudi na A'di waliukadhibisha Msiba unaositusha.*
5. *Basi Thamudi waliangamizwa kwa balaa kubwa mno.*
6. *Na ama A'di waliangamizwa kwa upepo mkali usiozuilika.*
7. *Aliowapelekea masiku saba, na siku nane, mfululizo bila ya kusita. Utaona watu wamepinduka kama kwamba ni magongo ya mitende yalio wazi ndani.*
8. *Basi je! Unamuona mmoja wao aliyebaki?*
9. *Na Firauni na waliomtangulia, na miji iliyopinduliwa chini juu, walileta khatia.*
10. *Wakamuasi Mtume wa Mola Wao Mlezi, ndipo Yeye Mola Akawakamata kwa Mkamato uliozidi nguvu.*
11. *Maji yalipofurika Sisi Tulikupandisheni katika safina,*
12. *Ili Tuyafanye hayo kuwa ni waadhi kwenu na kila sikio linalo sikia liyahifadhi.*

Onyo Kuhusu Ukubwa wa Siku ya Kiyama

Al-Haqqah ni moja kati ya majina ya Siku ya Kiyama kwa sababu ahadi na vitisho bila shaka vitatokea.

Kwa sababu hii Allah تعالیٰ Ametangaza ukubwa wa jambo hili.

Hivyo Anasema,

وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْحَاقَّةُ

“Na nini kitakujuulisha nini hilo Tukio la haki?”

Utajo wa Kuangamizwa kwa Mataifa.

Kisha Allah تعالی Anataja Kuangamizwa kwa watu waliokana Ufufuo. Anasema,

﴿فَأَمَّا ثَمُودُ فَهَلَكَوْا بِأَلطَاغِيَةِ﴾

“Basi Thamudi waliangamizwa kwa balaa kubwa mno.”

Huo ulikuwa ukelele uliowanyamazisha wao, na tetemeko la ardhi lilowaangamiza. Qatadah amesema maneno kama haya aliposema, “At-Taghiyah” ni ukelele.”¹ Mujahid amesema, “At-Taghiyah” Ina Maana ya madhambi.” Haya yalisemwa pia na Ar-Rabi bin Anas na bin Zayd. Walisema ni kuchupa mipaka. Baada ya kutaja haya, Ibn Zayd alisoma Aya zifuatazo ili kuthibitisha kauli yake.

﴿كَذَّبَتْ ثَمُودُ بِطَغْوَنهَا﴾

“Kina Thamudi walikadhibisha kwa sababu ya upotofu wao.” (91:11)

Kisha Allah تعالی Akasema,

﴿وَأَمَّا آدُ فَهَلَكَوْا بِرِيحٍ صَرْصَرٍ﴾

“Na ama A’di waliangamizwa kwa upepo mkali”

Maana yake: Upepo yabisi. Qatadah, As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas na Ath-Thawri, wote wamesema hivyo,

﴿عَاتِبَةٍ﴾

“...usiozulika.”

Hii maana yake: ‘Upepo mkali uvumao.’ Qatadah amesema, “Unavuma kwa nguvu mpaka unapenya ndani ya mioyo yao.”² Amesema Adh-Dhahak,

﴿صَرْصَرٍ﴾

“...Mkali...” Ina maana baridi, na

﴿عَاتِبَةٍ﴾

“...usiozulika.”

¹ At-Tabari 23:671.

² At-Tabari 23:572.

Maana yake: 'Unawavumia kwa nguvu bila huruma wala baraka.'¹ Amesema Ali na wengine رضي الله عنهم, "Ulivuma kwa nguvu kwenye maghala ya mazao mpaka yakakosa thamani."²

سَخَّرَهَا عَلَيْهِمْ

"Aliowapelekea..."

Maana yake: Alioutuma kwa wao.

سَبْعَ لَيَالٍ وَثَمَنِيَةَ أَيَّامٍ حُسُومًا

"...masiku saba, na siku nane, mfululizo bila ya kusita."

Maana yake: Iliyofuatana kwa ukamilifu. Ibn Mas'ud, Ibn Abbas, Mujahid, Ikrimah, Ath-Thawri na wengine رضي الله عنهم wote wamesema kuwa "Husum" ina maana ya mfululizo.³ Imenukuliwa kuwa Ikrimah na Ar-Rabi bin Khuthaym, wote wamesema, "Kutokana na makosa kwao."

Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى.

فِي أَيَّامٍ نَحْسَاتٍ

"...katika siku za ukorofi." (41:16).

Imesemwa kuwa ni wale watu wasiojimudu kwa lolote kama magogo ya miti. Neno hili hutokana na Kauli ya Allah تعالى,

فَتَرَى الْقَوْمَ فِيهَا صَرْعَى كَأَنَّهُمْ أُعْجَازُ خَلٍ خَاوِيَةٍ ﴿٧﴾

"Utaona watu wamepinduka kama kwamba ni magogo ya mitende yalio wazi ndani."

Ibn Abbas رضي الله عنهما amezungumzia,

خَاوِيَةٍ ﴿٧﴾

"...yalio wazi ndani."

¹ At-Tabari 23:572.

² At-Tabari 23:572.

³ At-Tabari 23:573, 574.

“Ina maana tupu.” Wengine wamesema, “Ina maana chakavu.” Kwa maana kuwa upepo unampiga mmoja wao katika ardhi, huangukia kichwa chake hali ya kuwa amekufa. Kisha kichwa chake kitapondwapondwa na kuwa mzoga uliotulia mithili ya vigogo vya mtende visivyokuwa na matawi juu yake.

Imethibitishwa katika sahihi Mbili kuwa Mtume ﷺ alisema,

«نُصِرْتُ بِالصَّبَاِ وَأُهْلِكَتْ عَادٌ بِالذَّبُورِ»

“Nilisaidiwa na pepo za kusi na watu wa Ad waliangamizwa na pepo za kaskazi.”¹

فَهَلْ تَرَى لَهُم مِّنْ بَاقِيَةٍ ﴿٦٩﴾

“Basi je! Unamuona mmoja wao aliyebaki?”

Maana yake: ‘Je, unamuona aliyesalia kati yao, au mmoja anayejinasibisha nao? Bali wote wameshateketea, kuanzia wa mwanzo mpaka wa mwisho na Allah تعالیٰ Hakuwawekea warithi.”

Kisha Allah تعالیٰ Amesema,

وَجَاءَ فِرْعَوْنُ وَمَنْ قَبْلَهُ

“Na Firauni na waliomtangulia,”

Kwa Maana: Wale aliokuwa nao katika zama zake, ambao walikuwa ni wale makafiri wa Kikoptiki. Wapo wengine waliosema ni katika mataifa yanayoshabihiana na wao.

Kuhusu Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَأَلْمُؤْتِفِكْتُ

“...na miji iliyopinduliwa chini juu...”

Kaumu zilizowakataa Mitume wao,

بِالْحَاطِئَةِ ﴿٧٠﴾

“...walileta khatia.”Ina maana kukanusha kwao ufunuo kutoka kwa Allah تعالیٰ. Ar-Rabi alisema,

¹ Muslim 2:617.

بِالْحَاطِطَةِ ﴿١٧﴾

“... walileta khatia.”

“Kwa Maana ya Uasi.” Mujahid amesema, “Walifanya makosa.”¹ Hivyo Allah تعالی Anasema,

فَعَصَوْا رَسُولَ رَبِّهِمْ

“Wakamuasi Mtume wa Mola wao Mlezi.”

Maana yake: Wote walikuwa na sifa zinazolingana, wote waliwakataa Mitume wa Allah تعالی waliopelekwa kwao. Kama Allah تعالی Anavyosema

كُلٌّ كَذَّبَ الرُّسُلَ فَحَقَّ وَعِيدِ ﴿١٨﴾

“Hao wote waliwakadhibisha Mitume; basi wakastahiki adhabu Yangu.” (50:14).

Kwa hiyo yeyote anayemkanusha Mtume mmoja, basi bila shaka amewakanusha Mitume wote. Hii ni kama Allah تعالی Alivyosema,

كَذَّبَتْ قَوْمُ نُوحٍ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٩﴾

“Kaumu ya Nuhu waliwakadhibisha Mitume”. (26:105)

كَذَّبَتْ عَادُ الْمُرْسَلِينَ ﴿٢٠﴾

“Kina A'd waliwakanusha Mitume.” (26:123)

كَذَّبَتْ ثَمُودُ الْمُرْسَلِينَ ﴿٢١﴾

“Kina Thamud waliwakanusha Mitume.” (26:141)

Hata hivyo, kila Taifa lilipelekewa Mtume mmoja. Hivyo Allah تعالی Anasema

فَعَصَوْا رَسُولَ رَبِّهِمْ فَأَخَذَهُمْ أَخْذَةً رَابِيَةً ﴿٢٢﴾

“Wakamuasi Mtume wa Mola wao Mlezi, ndipo Yeye Mola Akawakamata kwa Mkamato uliozidi nguvu.”

¹ At-Tabari: 23:576.

Kwa maana, kubwa, kali na yenye kuumiza. Mujahid amesema, “*Rabiyah* maana yake kali.”¹ As-Suddi amesema, “Ina maana inayoangamiza.”

Ukumbusho Juu ya Neema za Safina

Kisha Allah تعالى Amesema,

إِنَّا لَمَّا طَغَا آلْمَاءُ

“*Maji yalipofurika...*”.

Maana yake: Yalifurika kwa Idhini ya Allah تعالى na kufunika kila kilichokuwepo. Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine walisema, “Maji yaliongezeka mno² kupita mipaka yake kutokana na dua ya Nuh عليه السلام dhidi ya watu wake walipomkana, kumpinga na wakamuabudu asiyekuwa Allah تعالى.”

Kwa hiyo Allah تعالى Alipokea dua yake na watu wa duniani walifunikwa na mafuriko isipokuwa wale waliokuwa ndani ya safina na Nuh عليه السلام. Hivyo, binadamu wote wanatokana na kizazi cha Nuh عليه السلام na watoto wake. Kwa sababu hii Allah تعالى Anawakumbusha binadamu juu ya Neema Zake,

إِنَّا لَمَّا طَغَا آلْمَاءُ حَمَلْنَاكُمْ فِي الْجَارِيَةِ ﴿١٢﴾

“*Maji yalipofurika Sisi Tulikupandisheni katika safina.*’

Maana yake: Safina inayopita juu ya maji.

لِنَجْعَلَهَا لَكُمْ تَذْكِرَةً

“*Ili Tuyafanye hayo kuwa ni waadhi kwenu...*” (69:12)

Tumekubakishieni jinsi yake miongoni mwa mnavyovipanda juu ya mikondo ya maji baharini.

Hivi ni kama Allah تعالى Alivyosema:

¹ At-Tabari: 23:577.

² At-Tabari: 23:577.

وَالَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا وَجَعَلَ لَكُم مِّنَ الْفُلْكِ وَالْأَنْعَامِ مَا تَرْكَبُونَ ﴿٤٣﴾ لَيْسْتَ تُدْرَأُ عَلَىٰ ظُهُورِهِمْ إِذْ تُدْعَوْنَ بِهِمْ نِعْمَةً رَّبِّكُمْ إِذَا اسْتَوَيْتُمْ عَلَيْهِ وَتَقُولُوا سُبْحٰنَ الَّذِي سَخَّرَ لَنَا هٰذَا وَمَا كُنَّا لَهُ مُقْرِبِينَ ﴿٤٤﴾

“Na Ambaye Ndiye Aliyeumba katika kila kitu jike na dume, na Akakufanyieni marikebu na wanyama mnaowapanda. Ili mkae vizuri migongoni mwao, kisha mkumbuke neema za Mola wenu Mlezi mnapokaa sawasawa juu yao na msem: Ametakasika Aliyemfanya huyu atutumikie, na tusingeliweza kufanya haya wenyewe.” (43:12-13)

Na Allah تعالى Amesema,

وَأَيُّهُم أَنَا حَمَلْنَا ذُرِّيَّتَهُمْ فِي الْفُلْكِ الْمَشْحُونِ ﴿٤١﴾ وَخَلَقْنَا لَهُم مِّن مِّثْلِهِ مَا يَرْكَبُونَ

“Na ni Ishara kwao kwamba Sisi Tuliwapakia dhuriya zao katika jahazi iliosheheni. Na Tukawaumbia kutoka mfano wake wanavyo vipanda.” (36:41-42)

Qatadah amesema, “Allah تعالى Aliibakiza safina hii mpaka wakaidiriki watu wa mwanzo wa Ummah huu.”¹ Pamoja na hayo rai ya mwanzo inafahamika zaidi akilini ya kuwa ni safina zote kwa ujumla. Allah تعالى Anaendelea kusema,

وَتَعْبَأُ أُذُنُ وَاَعْيَةُ ﴿٤٢﴾

“...na kila sikio linalosikia liyahifadhi.”

Maana yake: Sikio linalosikia linaweza kuelewa na kuakisi fadhila hii. Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, “Ina maana sikio lenye kuhifadhi na kusikia.”² Qatadah amesema,

أُذُنٌ وَاَعْيَةُ ﴿٤٣﴾

“...linalosikia...” Maana yake: Sikio ambalo Allah تعالى Amelipa akili, hivyo linafaidika na yale linaloyasikia katika Kitabu cha Allah تعالى. Adh-Dhahak alisema,

¹ At-Tabari: 23:578.

² At-Tabari: 23:579.

وَتَعِيَا أُذُنٌ وَّعِيَةٌ ﴿١٧﴾

“...na kila sikio linalosikia liyahifadhi.”

Maana yake: “Mtu mwenye usikivu na akili timamu.” Na jambo hili linamhusu yeyote anayefahamu na kuzingatia.

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ نَفْخَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿١٨﴾ وَحُمِلَتِ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ فَدُكَّتَا دَكَّةً وَاحِدَةً ﴿١٩﴾
 فَيَوْمَئِذٍ وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ﴿٢٠﴾ وَانْشَقَّتِ السَّمَاءُ فَهِيَ يَوْمَئِذٍ وَاهِيَةٌ ﴿٢١﴾ وَالْمَلَكُ عَلَى
 أَرْجَائِهَا ﴿٢٢﴾ وَيَحْمِلُ عَرْشَ رَبِّكَ فَوْقَهُمْ يَوْمَئِذٍ ثَمَنِيَةٌ ﴿٢٣﴾ يَوْمَئِذٍ تُعْرَضُونَ لَا تَخْفَى مِنْكُمْ
 خَافِيَةٌ ﴿٢٤﴾

13. Na litapopulizwa barugumu mpulizo mmoja tu,

14. Na ardhi na milima ikaondolewa, na ikavunjwa kwa mvunjo mmoja,

15. Siku hiyo ndio Tukio litatukia.

16. Na mbingu zitapasuka, kwani siku hiyo zitakuwa dhaifu kabisa.

17. Na Malaika watakuwa pembezoni mwa mbingu; na wanane juu ya hawa watakuwa wamebeba Kiti cha Enzi cha Mola wako Mlezi.

18. Siku hiyo mtahudhurishwa - haitafichika siri yoyote yenu.

Kutajwa kwa Vitisho vya Siku ya Kiyama

Allah تعالی Anatoa habari ya vitisho vya Siku ya Kiyama. Tukio la mwanzo kabisa ni mpulizo wa kutisha wa Parapanda, ambao utafuatiwa na mpulizo mwingine, ambapo kila mtu aliye mbinguni na ardhini atazirai isipokuwa watakaosalimishwa na Allah تعالی. Kisha, baragumu la tatu ni kusimama mbele ya Mfalme wa kila kitu kinachoishi, na ufufuo, na kukusanywa. Na huu ndio mpulizo uliokusudiwa hapa. Na unasisitizwa kuwa ni mpulizo mmoja tu, kwa sababu Amri ya Allah تعالی haiwezi kupingwa au kuzuiwa, na haihitaji kurudiwa au kutiliwa mkazo. Hivyo, Allah تعالی Anaendelea Kusema,

وَحُمِلَتِ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ فَدُكَّتَا دَكَّةً وَاحِدَةً ﴿٦٩﴾

“Na ardhi na milima ikaondolewa, na ikavunjwa kwa mvunjo mmoja.”

Maana yake: Itasambazwa kwa kiasi ambacho uso wa Ardhi utabadilika kuwa tofauti na ardhi iliyo zoeleka.

فَيَوْمَئِذٍ وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ﴿٧٠﴾

“Siku hiyo ndio Tukio litatukia.”

Maana yake: Siku ya Hukumu,

وَأَنْشَقَّتِ السَّمَاءُ فَهِيَ يَوْمَئِذٍ وَاهِيَةٌ ﴿٧١﴾

“Na mbingu zitapasuka, kwani siku hiyo zitakuwa dhaifu kabisa.”

Ibn Jurayj amesema, “Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى,

وَفُتِحَتِ السَّمَاءُ فَكَانَتْ أَبْوَابًا ﴿٧٢﴾

“Na mbingu zitafunguliwa, ziwe milango.” (78:19)

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mbingu zitararuliwa na Arshi itakuwa karibu yake.”

وَأَلْمَلِكُ عَلَىٰ أَرْجَائِهَا ﴿٧٣﴾

“Na Malaika watakuwa pembezoni mwa mbingu.”

Neno *Malak* hapa inakusudiwa malaika (wote). Maana yake: Malaika kwa ujumla wao watasimama pembezoni mwa mbingu. Ar-Rabi bin Anas amesema katika Kauli ya Allah تعالى,

وَأَلْمَلِكُ عَلَىٰ أَرْجَائِهَا ﴿٧٣﴾

“Na Malaika watakuwa pembezoni mwa mbingu.”

“Hii ina maana kuwa watasimama karibu na mbingu wakiwaangalia watu wa duniani.” Na Kauli ya Allah تعالى,

وَيَحْمِلُ عَرْشَ رَبِّكَ فَوْقَهُمْ يَوْمَئِذٍ ثَمَنِيَةٌ ﴿٧٤﴾

“...na wanane juu ya hawa watakuwa wamebeba Kiti cha Enzi cha Mola Wako Mlezi.”

Maana yake: Siku ya Kiyama, Malaika wanane watabeba Kiti cha Enzi cha Mola. Abu Dawud amenukuu kutoka kwa Jabir bin Abdullah رضى الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَذِنَ لِي أَنْ أُحَدِّثَ عَنْ مَلَكٍ مِنْ مَلَائِكَةِ اللَّهِ تَعَالَى مِنْ حَمَلَةِ الْعَرْشِ: أَنْ مَا بَيْنَ سَحْمَةِ أَذْرِي إِلَى عَاتِقِهِ مَسِيرَةٌ سَبْعِمِائَةٍ عَامٍ»

“Nilipewa idhini kuzungumzia malaika mmoja kati ya wale watakaobeba Arshi ya Allah. Kati ya ndewe yake ya sikio mpaka bega lake ni masafa ya kutembea miaka mia saba.”

Haya ni masimulizi ya Abu Dawud.¹

Wanadamu Wakiwasilishwa Mbele ya Allah تعالى

Kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

يَوْمَئِذٍ تُعْرَضُونَ لَا تَخْفَى مِنْكُمْ خَافِيَةٌ ﴿١٥﴾

“Siku hiyo mtahudhurishwa - haitafichika siri yoyote yenu.”

Maana yake: Mtawasilishwa kwa Mtambuzi wa siri na mambo binafsi. Yeye Ndiye Pekee Ambaye siri zenu hazifichiki. Yeye ni Mtambuzi wa mambo yote yaliyowazi na yaliyofichikana.’ Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

لَا تَخْفَى مِنْكُمْ خَافِيَةٌ ﴿١٥﴾

“...haitafichika siri yoyote yenu.” Imam Ahmad رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Abu Musa رضى الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema

«يُعْرَضُ النَّاسُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ثَلَاثَ عَرَضَاتٍ، فَأَمَّا عَرَضَاتِنِ فَجِدَالٌ وَمَعَاذِيرُ، وَأَمَّا الثَّلَاثَةُ فَعِنْدَ ذَلِكَ تَطِيرُ الصُّحُفُ فِي الْأَيْدِي فَأَخَذَ بِمِيسِهِ وَأَجَذَ بِشِمَالِهِ»

“Watu wataoneshwa mara tatu Siku ya Kiyama. Mahudhurisho mawili ya mwanzo yatakuwa kwa ajili ya kutoa hoja na kutoa nyudhuru. Ya tatu kumbukumbu zitatua kwenye mikono yao. Baadhi yao watapokea rekodi zao kwa mikono ya kulia na baadhi kwa mikono ya kushoto.” Ibn Majah na At-Tirmithi¹ walinukuu Hadith hii.

¹ Abu Dawud 5:96.

فَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ
 فَيَقُولُ هَآؤُمُ اقْرَءُوا كِتَابِيَةَ ﴿١٩﴾ إِنِّي
 ظَنَنْتُ أَنِّي مُلَاقٍ حِسَابِيَةَ ﴿٢٠﴾ فَهُوَ فِي عِيشَةٍ
 رَاضِيَةٍ ﴿٢١﴾ فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ﴿٢٢﴾ قُطُوفُهَا دَانِيَةٌ ﴿٢٣﴾
 كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا أَسْلَفْتُمْ فِي الْأَيَّامِ الْخَالِيَةِ ﴿٢٤﴾
 وَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ بِشِمَالِهِ فَيَقُولُ يَا لَيْتَنِي لَمْ أُوتَ
 كِتَابِيَةَ ﴿٢٥﴾ وَلَمْ أَدْرِ مَا حِسَابِيَةَ ﴿٢٦﴾ يَا لَيْتَنِي كَانَتِ
 الْقَاضِيَةَ ﴿٢٧﴾ مَا أَغْنَىٰ عَنِّي مَالِيَةٌ ﴿٢٨﴾ هَلَكَ عَنِّي
 سُلْطَانِيَةٌ ﴿٢٩﴾ خُذُوهُ فَغُلُّوهُ ﴿٣٠﴾ ثُمَّ الْجَحِيمَ صَلُّوهُ ﴿٣١﴾
 ثُمَّ فِي سِلْسَلَةٍ ذَرْعُهَا سَبْعُونَ ذِرَاعًا فَاسْلُكُوهُ ﴿٣٢﴾ إِنَّهُ
 كَانَ لَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ ﴿٣٣﴾ وَلَا يَحْضُرُ عَلَىٰ طَعَامِ
 الْمَسْكِينِ ﴿٣٤﴾ فَلَيْسَ لَهُ الْيَوْمَ هُنَا حَمِيمٌ ﴿٣٥﴾ وَلَا
 طَعَامٌ إِلَّا مِن غِسْلِينَ ﴿٣٦﴾ لَا يَأْكُلُهُ إِلَّا الْخَنَاطُونَ ﴿٣٧﴾
 فَلَا أُقْسِمُ بِمَا تُبْصَرُونَ ﴿٣٨﴾ وَمَا لَا تُبْصَرُونَ ﴿٣٩﴾ إِنَّهُ
 لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿٤٠﴾ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ قَلِيلًا مَّا
 تُؤْمِنُونَ ﴿٤١﴾ وَلَا بِقَوْلِ كَاهِنٍ قَلِيلًا مَّا تَدَّكُرُونَ ﴿٤٢﴾
 نَزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٣﴾

فَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ
 فَيَقُولُ هَآؤُمُ اقْرَءُوا كِتَابِيَةَ ﴿١٩﴾ إِنِّي
 ظَنَنْتُ أَنِّي مُلَاقٍ حِسَابِيَةَ ﴿٢٠﴾ فَهُوَ
 فِي عِيشَةٍ رَاضِيَةٍ ﴿٢١﴾ فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٍ
 قُطُوفُهَا دَانِيَةٌ ﴿٢٢﴾ كُلُوا
 وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا أَسْلَفْتُمْ فِي
 الْأَيَّامِ الْخَالِيَةِ ﴿٢٤﴾

19. Basi ama atakayepewa
 kitabu chake kwa mkono
 wake wa kulia, atasema:
 Haya someni kitabu changu!

20. Hakika nalijua ya kuwa
 nitapokea hisabu yangu.

21. Basi yeye atakuwa katika
 maisha ya kupendeza,

22. Katika Bustani ya juu,

23. Matunda yake ya karibu.

24. Waambiwe: Kuleni na
 mnywe kwa furaha kwa
 sababu ya mlivyotanguliza
 katika siku zilizopita.

Furaha ya Mtu Atakayepokea Kitabu Chake kwa Mkono wa Kulia na Uzuri wa Hali Yake

Allah تعالى Anatoa habari ya furaha ya wale watakaopokea Kitabu chao kwa mkono wa kulia Siku ya Kiyama na kuwa radhi na hilo. Kutokana na furaha atamuambia kila anayekutana naye,

هَآؤُمُ أَقْرَأُوا كِتَابِيَهٗ ﴿٦٩﴾

“Haya someni kitabu changu!”

Maana yake: ‘Chukua Kitabu changu ukisome.’ Atasema hivyo kwa sababu anajua kuwa kuna mambo mazuri yasiyokuwa na doa. Atakuwa kati ya wale ambao Allah تعالى Amebadilisha amali mbaya yake kuwa nzuri. Abdur-Rahman bin Zayd amesema, “Maana ya,

هَآؤُمُ أَقْرَأُوا كِتَابِيَهٗ ﴿٦٩﴾

“Haya someni kitabu changu!”

Abdurahman bin Zayd amesema: Kwa Maana: Someni kitabu changu hiki.

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu kuwa ‘Abdullah bin Abdullah bin Hanzalah رضي الله عنه – naye (Hanzalah) alikuwa Sahaba aliyekoshwa na Malaika siku ya mazishi yake – alisema, “Bila shaka, Allah تعالى Atamsimamisha mja wake Siku ya Kiyama na Atafanya madhambi yake yaonekane nje ya Kitabu chake cha Rekodi.” Kisha atamuuliza, ‘Je, ulifanya haya? “ Mja atajibu, ‘Ndiyo Mola Wangu.” ‘Kisha Allah تعالى Atamuambia, ‘sitakufichua (au kukuadhiri), kwani kwa kweli, nimekusamehe.’ Binadamu atasema, ‘Hiki hapa (nyote) someni Kitabu changu!’

Allah تعالى Anasema:

إِنِّي ظَنَنْتُ أَنِّي مُلْقٍ حِسَابِيَهٗ ﴿٧٠﴾

“Hakika nalijua ya kuwa nitapokea hisabu yangu.”

¹ Ahmad 4:414, Isnadi yake ni dhaifu, ndani yake kuna Tadhira ya Hasani Basri ambaye hakuweka wazi kuwa alisikia. Ibn Majah 2:1430, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 7:111. Imesimuliwa na Al-Hassan Al-Basri ambaye maulamaa wengi wanasema kuwa hakuisikia kutoka kwa Abu Musa, kwa hivyo kutokana na wengi, ni masimulizi yaliyokatika.

Haya yatajiri wakati mja wa Allah تعالى atakapookolewa kutokana na kudhalilishwa na kudhihirishwa makosa yake Siku ya Kiyama.

Katika Sahihi, imenukuliwa Hadithi kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنه kuwa aliulizwa kuhusu mambo ya siri. Alijibu kwa kusema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«يُذْنِي اللهُ الْعَبْدَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَيَقْرُرُهُ بِذُنُوبِهِ كُلِّهَا، حَتَّى إِذَا رَأَى أَنَّهُ قَدْ هَلَكَ قَالَ اللهُ تَعَالَى: إِنِّي سَتَرْتُهَا عَلَيْكَ فِي الدُّنْيَا وَأَنَا أَعْفِرُهَا لَكَ الْيَوْمَ، ثُمَّ يُعْطِي كِتَابَ حَسَنَاتِهِ بِبَيْمِيهِ. وَأَمَّا الْكَافِرُ وَالْمُنَافِقُ فَيَقُولُ الْأَشْهَادُ هَذَا الَّذِي كَذَبُوا عَلَى رَبِّهِمْ أَلَا لَعْنَةُ اللهِ عَلَى الظَّالِمِينَ»

“Allah Atamsogeza mja karibu Naye Siku ya Hesabu na amfanye atubu madhambi yake yote. Hali hii itaendelea mpaka mja adhanie kuwa ataangamizwa. Kisha Allah Atasema, “Kweli Nimekuhifadhia (kuficha) madhambi yako duniani na leo Nimekusamehe.” Kisha atapewa Kitabu chake chenye amali njema kwa mkono wake wa kulia. Hata hivyo, kuhusu makafiri na wanafiki, mashahidi watasema: ‘Hawa ndio waliomtungia uwongo Mola wao Mlezi. Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate walio dhulumu,’”

Kauli ya Allah تعالى:

إِنِّي ظَنَنْتُ أَنِّي مُلْقٍ حِسَابِيَهٗ ﴿٦٩﴾

“Hakika nalijua ya kuwa nitapokea hisabu yangu.”

Maana yake: “Nilikuwa na uhakika nilipokuwa duniani kuwa bila shaka siku hii itakuja.”

Haya ni sawa kama Allah تعالى Alivyosema,

الَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُمْ مُلْقُوا رَبَّهُمْ

“Ambao wana yakini kuwa hakika watakutana na Mola wao Mlezi.”
(2:46).

Kisha Allah تعالى Amesema,

¹ Ahmad 2:74, Al-Bukhari 4685, na Muslim 1768.

فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَّاضِيَةٍ ﴿٦٩﴾

“Basi yeye atakuwa katika maisha ya kupendeza”,

Ina maana: Yanayoridhisha.

فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ﴿٧٠﴾

“Katika Bustani ya juu,”.

Maana yake: Makasiri ya juu, wanawake wazuri wenye macho makubwa, vyumba vinavyopendeza na furaha ya milele.

Imethibitishwa katika sahih kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ الْجَنَّةَ مِائَةٌ دَرَجَةٍ مَا بَيْنَ كُلِّ دَرَجَتَيْنِ كَمَا بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ»

“Kwa hakika, Pepo ina daraja mia moja na kati ya kila daraja kuna masafa kama umbali kati ya dunia na mbingu.”¹

Kisha Allah تعالى Amesema,

فَطُوفُوهَا دَانِيَةً ﴿٧١﴾

“Matunda yake ya karibu.”

Al-Barau bin Azib amesema, “Ina maana: Yapo karibu kwa mmoja wao (watu wa Peponi) kuyafikia akiwa juu ya kitanda chake.”² Amesema haya zaidi ya mmoja.

Allah تعالى Amesema,

كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا أَسْلَفْتُمْ فِي الْأَيَّامِ الْخَالِيَةِ ﴿٧٢﴾

“Kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya mlivyotanguliza katika siku zilizopita.”

Maana yake: Haya yatasemwa kama mwaliko wa rehema, fadhila na wema. Kwani bila shaka, imethibitishwa ndani ya Sahih kuwa Mtume ﷺ amesema,

¹ Al-Bukhari na. 2790.

² At-Tabari 23:586.

«اعْمَلُوا وَسَدُّوا وَقَارِبُوا، وَاعْلَمُوا أَنَّ أَحَدًا مِنْكُمْ لَنْ يُدْخِلَهُ عَمَلُهُ الْجَنَّةَ»

“Fanyeni amali, mjizatiti, na mpupie kuwa karibu na Allah na mjue kwamba hapana mmoja wenu ambaye amali zake zitamuingiza Peponi.”

Masahaba walisema, “Hata wewe Ewe Mjumbe wa Allah?” Mtume ﷺ akajibu.

«وَلَا أَنَا إِلَّا أَنْ يَتَغَمَّدَنِي اللَّهُ بِرَحْمَةٍ مِنْهُ وَفَضْلٍ»

“Wala mimi, isipokuwa Allah Atakaponifunika kwa Huruma na Fadhila Zake.”¹

وَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِشِمَالِهِ فَيَقُولُ يَلِيَّتَنِي لَمْ أُوتَ كِتَابِيَةَ ﴿٢٥﴾ وَلَمْ أَدْرِ مَا حِسَابِيَةَ ﴿٢٦﴾ يَلِيَّتَهَا كَانَتْ الْقَاضِيَةَ ﴿٢٧﴾ مَا أَغْنَىٰ عَنِّي مَالِيَةَ ﴿٢٨﴾ هَلَكَ عَنِّي سُلْطَانِيَةَ ﴿٢٩﴾ خُدُوهُ فَعُلُوهُ ﴿٣٠﴾ ثُمَّ أَلْحَجِمِ صَلْوَهُ ﴿٣١﴾ ثُمَّ فِي سِلْسِلَةٍ ذَرْعُهَا سَبْعُونَ ذِرَاعًا فَاسْلُكُوهُ ﴿٣٢﴾ إِنَّهُ كَانَ لَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ ﴿٣٣﴾ وَلَا تَحْضُ عَلَىٰ طَعَامِ الْمَسْكِينِ ﴿٣٤﴾ فَلَيْسَ لَهُ الْيَوْمَ هُنَا حَمِيمٌ ﴿٣٥﴾ وَلَا طَعَامٌ إِلَّا مِنْ غِسْلِينٍ ﴿٣٦﴾ لَا يَأْكُلُهُ إِلَّا الْخَنَاطُونَ ﴿٣٧﴾

25. Na ama atakaye pewa kitabu chake katika mkono wake wa kushoto, basi yeye atasema: Laiti nisingelipewa kitabu changu!

26. Wala nisingelijua nini hisabu yangu.

27. Laiti mauti ndiyo yangelikuwa ya kunimaliza kabisa.

28. Mali yangu haikunifaa kitu.

29. Madaraka yangu yamenipotea.

30. (Pasemwe): Mshikeni! Mtieni pingu!

31. Kisha mtupeni Motoni!

32. Tena mtatizeni katika mnyororo wenye urefu wa dhiraa sabiini!

¹ Fat’hul Al-Bari 11:300.

33. Kwani huyo hakika alikuwa hamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu,

34. Wala hahimizi kulisha masikini.

35. Basi leo hapa hana jamaa wa kumuonea uchungu,

36. Wala hana chakula ila usaha wa watu wa Motoni.

37. Chakula hicho hawakili ila wakosefu.

Hali Mbaya kwa Atayepewa Kitabu Chake kwa Mkono wa Kushoto.

Aya hizi zinaeleza kuhusu hali dhalili ya mtu atakayepewa Kitabu chake kwa mkono wa kushoto. Wakati huo atakuwa katika majuto makubwa mbele ya hadhira ya watu.

فَيَقُولُ يَلَيْتَنِي لَمْ أُوتَ كِتَابِيَةَ ۖ وَلَمْ أَدْرِ مَا حِسَابِيَةَ ﴿٦٩﴾

“...atasema: Laiti nisingelipewa kitabu changu! Wala nisingelijua nini hisabu yangu. Laiti mauti ndiyo yangelikuwa ya kunimaliza kabisa.”

Adh-Dhahak amesema, “Ina Maana ya: Kifo kisichofuatiwa na uhai wowote.” Muhammad bin Kaab, Ar-Rabi na As-Suddi wamesema vivyo hivyo. Qatadah amesema, “Atatamani kifo japo alipokuwa duniani alikichukia sana.”¹

مَا أَغْنَىٰ عَنِّي مَالِيَةَ ۖ هَلَكَ عَنِّي سُلْطَانِيَةَ ﴿٧٠﴾

“Mali yangu hayakunifaa kitu. Madaraka yangu yamenipotea.”

Maana yake: ‘Utajiri wangu na hadhi yangu haikuninginga na adhabu ya Allah تعالیٰ na mateso Yake. Sasa yote yamenifika peke yangu na sina msaidizi wala mtu wa kuniokoa.’ Kuhusu hili Allah تعالیٰ Anasema:

خُذُوهُ فَغُلُّوهُ ۖ ثُمَّ الْجَحِيمَ صَلُّوهُ ﴿٧١﴾

“(Pasemwe): Mshikeni! Mtieni pingu! Kisha mtupeni Motoni!”

¹ At-Tabari 23:587.

Maana yake: Atawaamrisha walinzi wa Jahanamu wamuondoe kwa nguvu kutoka katika uwanja wa hukumu, wamfunge mnyororo – yaani kumfungia kola ya chuma shingoni – kisha wambebe na kumtupa Motoni, yaani kumzamisha humo. Allah تعالى Amesema,

ثُمَّ فِي سِلْسِلَةٍ ذَرْعُهَا سَبْعُونَ ذِرَاعًا فَاسْلُكُوهُ ﴿٦٩﴾

“Tena mtatizeni katika mnyororo wenye urefu wa dhiraab sabiini!”

Ka'b Al-Ahbar amesema, “Kila pete itakuwa sawa na chuma chote kilichopo duniani, “Al-Anifi amenukuu kuwa Ibn Abbas na Ibn Jurayj walisema, “Kitakuwa sawa na dhiraab ya Malaika.”¹ Ibn Jurayj رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Abbas رضي الله عنه amesema,

فَاسْلُكُوهُ ﴿٦٩﴾

‘Tena mtatizeni...’

Utaingizwa matakoni na kutolewa mdomoni. Kisha watapangwa katika mnyororo kama nziye waliopangwa kwenye kijiti wakiokwa. Al-Awfi alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Itapitishwa nyuma yake mpaka itolewe kupitia tundu za pua ili asiweze kusimama kwa miguu yake.”² Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Abdullah bin Amr رضي الله عنه Mtume ﷺ amesema:

«لَوْ أَنَّ رِصَاصَةً مِّثْلَ هَذِهِ - وَأَشَارَ إِلَى جُمُوعَةٍ - أُرْسِلَتْ مِنَ السَّمَاءِ إِلَى الْأَرْضِ، وَهِيَ مَسِيرَةٌ خَمْسِمِائَةِ سَنَةٍ، لَبَلَّغَتْ الْأَرْضَ قَبْلَ اللَّيْلِ وَلَوْ أَنَّهَا أُرْسِلَتْ مِنْ رَأْسِ السَّلْسِلَةِ لَسَارَتْ أَرْبَعِينَ خَرِيفًا اللَّيْلِ وَالنَّهَارَ قَبْلَ أَنْ تَبْلُغَ قَعْرَهَا أَوْ أَصْلَهَا»

“Kama tone la risasi kama hili – na akaonesha mfupa wa fuvu – yangeteremshwa kutoka mbinguni mpaka ardhini, na ni masafa ya miaka mia tano, yangefika duniani kabla usiku kuingia. Na kama (tone hilo la risasi) yangetumwa kutoka mnyororo (wa Motoni) yatasafiri misimu arubaini usiku na mchana, kabla ya kufika mvungu wa Jahanamu.”³

¹ At-Tabari 23:589.

² At-Tabari: 23:589.

³ Ahmad 2:197.

At-Tirmidhi amenukuu Hadith hii pia na amesema, "Hadith hii ni Hasan."¹
Kuhusu Kauli ya Allah تعالى

إِنَّهُ كَانَ لَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ ﴿٦٩﴾ وَلَا يَخُصُّ عَلَىٰ طَعَامِ الْمَسْكِينِ ﴿٧٠﴾

"Kwani huyo hakika alikuwa hamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu, wala hahimizi kulisha masikini."

Maana yake: Hakuona kuwa alikuwa na haki ya kumtii Allah تعالى na Kumuabudu. Aidha hakupata faida katika kuwahudumia viumbe wa Allah تعالى wala kuwapa masikini haki zao. Kwa hakika Allah تعالى Ana haki kwa waja kuwa wamuabudu Yeye Peke Yake na wasimshirikishe yeyote Naye. Waja wa Allah تعالى wana haki kwa kila mmoja wao kutendeanana wema na kusaidiana katika mambo mema na uchaji-Mungu. Kwa sababu hiyo Allah Amefaradhisha kusimamisha Sala na kutoa Zaka. Mtume ﷺ alipokaribia kufariki dunia alisema,

«الصَّلَاةُ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ»

*"Shikamaneni na kusali na mnavyovimiliki (yaani watumwa)."*²

Allah تعالى Anasema,

فَلَيْسَ لَهُ الْيَوْمَ هُنَا حَمِيمٌ ﴿٧١﴾ وَلَا طَعَامٌ إِلَّا مِنْ غِسْلِينٍ ﴿٧٢﴾ لَا يَأْكُلُهُ إِلَّا الْخَاطِئُونَ

"Basi leo hapa hana jamaa wa kumuonea chungu. Wala hana chakula ila usaha wa watu wa Motoni. Chakula hicho hawakili ila wakosefu."

Maana yake: Hapana mtu yeyote leo awezaye kumuokoa kutokana na adhabu ya Allah تعالى, wala swahiba au mwombezi ambaye maombi yake yatakubaliwa. Hatakuwa na chakula hapa isipokuwa taka za vidonda. Qatadah alisema, "itakuwa chakula kibaya kwa watu wa Motoni."³ Ar-Rabi na Adh-Dhahak wamesema, "Ghislin" "Ni mti uliopo Motoni." Shabib bin Bishir amenukuu kutoka kwa Ikrimah kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, 'Ghislin' " itakuwa damu na majimaji, itabubujika kutoka katika nyama ya miili yao." Ali bin Abi

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 7:313.

² An-Nasai katika Al-Kubra 4:258.

³ At-Tabari 23:591.

Talhaf amenukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, 'Ghislin' ni usaha wa watu wa Motoni."

فَلَا أُقْسِمُ بِمَا تُبْصِرُونَ ﴿٦٩﴾ وَمَا لَا تُبْصِرُونَ ﴿٧٠﴾ إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿٧١﴾ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ قَلِيلًا مَّا تُؤْمِنُونَ ﴿٧٢﴾ وَلَا بِقَوْلِ كَاهِنٍ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ﴿٧٣﴾ تَنْزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٤﴾

38. Basi naapa kwa mnavyoviona,

39. Na msivyoviona,

40. Kwa hakika hii ni Kauli iliyoletwa na Mjumbe mwenye hishima.

41. Wala si Kauli ya mtunga mashairi. Ni machache sana mnyoyaamini.

42. Wala si Kauli ya kuhani. Ni machache mnyoyakumbuka.

43. Ni uteremsho utokao kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.

Qur'an ni Maneno ya Allah تعالی

Allah تعالی Anaapa kwa viumbe wake kwa yale wanayoyashuhudia miongoni mwa ishara Zake. Viumbe vyake vinaonesha ukamilifu wa Majina Yake na Sifa Zake. Kisha Anaapa kwa vitu visivyoonekana. Hiki ni kiapo kuwa Qur'an ni Maneno Yake, Wahyi Wake kwa mja Wake na Mjumbe Wake, ambaye Amemchagua kufikisha Ujumbe kwa uaminifu mkubwa. Hivyo Allah تعالی Anasema,

فَلَا أُقْسِمُ بِمَا تُبْصِرُونَ ﴿٦٩﴾ وَمَا لَا تُبْصِرُونَ ﴿٧٠﴾ إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿٧١﴾

"Basi naapa kwa mnavyoviona, Na msivyoviona, Kwa hakika hii ni Kauli iliyoletwa na Mjumbe mwenye hishima."

Maana yake: Muhammad ﷺ Allah تعالی Alimpa wasifu - maelezo ambayo yanabeba maana ya kufikisha - kwa sababu kazi ya mjumbe ni kufikisha alilotumwa. Kwa kuzingatia hilo, Allah تعالی Alimpa wasifu huu wa Ujumbe Malaika katika Sura Takwir aliposema,

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿١٩﴾ ذِي قُوَّةٍ عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ ﴿٢٠﴾ مُطَاعٍ ثَمَّ أَمِينٍ ﴿٢١﴾

“Kwamba hakika bila ya shaka hii ni Kauli ya Mjumbe mtukufu, mwenye nguvu na mwenye cheo kwa huyo Mwenye Kiti cha Enzi, Anayetiwa, tena muaminifu.” (81:19-21).

Wasifu huu hapa, unamhusu Malaika Jibril عليه السلام. Kisha Allah تعالى Amesema,

وَمَا صَاحِبُكُمْ بِمَجْنُونٍ ﴿٢٢﴾

“Na wala huyu mwenzenu hana wazimu.” (81:22)

Maana yake: Muhammad ﷺ.

وَلَقَدْ رَءَاهُ بِالْأُفُقِ الْمُبِينِ ﴿٢٣﴾

“Na hakika yeye alimuona kwenye upeo wa macho ulio safi.” (81:23)

Maana yake: Muhammad ﷺ alimuona Jibril عليه السلام kwa umbile lake halisi aliloumbwa nalo na Allah تعالى.

وَمَا هُوَ عَلَى الْغَيْبِ بِضِئِينٍ ﴿٢٤﴾

“Wala yeye si bakhili kwa mambo ya ghaibu.” (81:24)

Maana yake: Shaka.

وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَيْطَانٍ رَجِيمٍ ﴿٢٥﴾

“Wala hii si kauli ya Shetani maluuni.” (81:25)

Ni sawa na linalosemwa hapa:

وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ قَلِيلًا مَّا تُوْمِنُونَ ﴿٢٦﴾ وَلَا بِقَوْلِ كَاهِنٍ قَلِيلًا مَّا تَدْكُرُونَ ﴿٢٧﴾

“Wala si Kauli ya mtunga mashairi. Ni machache sana mnayoyaamini. Wala si kauli ya kuhani. Ni machache mnayo yakumbuka.”

Hivyo, wakati fulani Allah تعالى Analitumia neno Mjumbe kwa Mjumbe wa kimalaika, na wakati mwingine inamhusu Mjumbe wa kibinadamu (Muha mmad

سورة). Hii ni kwa sababu wote wanafikisha kutoka kwa Allah تعالی kile ambacho waliaminiwa nacho, Ufunuo na Maneno ya Allah تعالی. Hivyo Allah تعالی Anasema,

تَنْزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٩﴾

“Ni Uteremsho utokao kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

* * *

وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الْأَقَاوِيلِ ﴿٤٤﴾
 لِأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ﴿٤٥﴾ ثُمَّ لَقَطَعْنَا مِنْهُ الْوَتِينَ ﴿٤٦﴾ فَمَا مِنْكُمْ
 مِنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِزِينَ ﴿٤٧﴾ وَإِنَّهُ لَتَذِكْرٌ لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٤٨﴾
 وَإِنَّا لَنَعْلَمُ أَنَّ مِنْكُمْ مُّكَذِّبِينَ ﴿٤٩﴾ وَإِنَّهُ لَحَسْرَةٌ عَلَى
 الْكٰفِرِينَ ﴿٥٠﴾ وَإِنَّهُ لِحَقِّ الْيَقِينِ ﴿٥١﴾ فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ
 الْعَظِيمِ ﴿٥٢﴾

وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الْأَقَاوِيلِ ﴿٤٤﴾
 لِأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ﴿٤٥﴾ ثُمَّ لَقَطَعْنَا مِنْهُ الْوَتِينَ ﴿٤٦﴾ فَمَا مِنْكُمْ
 مِنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِزِينَ ﴿٤٧﴾ وَإِنَّهُ لَتَذِكْرٌ لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٤٨﴾
 وَإِنَّا لَنَعْلَمُ أَنَّ مِنْكُمْ مُّكَذِّبِينَ ﴿٤٩﴾ وَإِنَّهُ لَحَسْرَةٌ
 عَلَى الْكٰفِرِينَ ﴿٥٠﴾ وَإِنَّهُ لِحَقِّ الْيَقِينِ ﴿٥١﴾ فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ
 الْعَظِيمِ ﴿٥٢﴾

﴿٥١﴾ الْيَقِينِ ﴿٥٢﴾ فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٥٣﴾

- 44. Na lau kama angelituzulia baadhi ya maneno tu.
- 45. Bila ya shaka Tungelimshika kwa mkono wa kulia.
- 46. Kisha kwa hakika Tungelimkata mshipa mkubwa wa moyo!.
- 47. Na hapana yeyote katika nyinyi ambaye angeliweza kutuzuia.
- 48. Kwa hakika hii ni mawaidha kwa wachamungu.
- 49. Na hakika Sisi bila ya shaka Tunajua kwamba miongoni mwenu wapo wanaokadhibisha.
- 50. Na hakika bila ya shaka itakuwa ni majuto kwa wanaokataa.
- 51. Na hakika hii bila ya shaka ni haki ya yakini.
- 52. Basi litakase Jina la Mola Wako Mlezi Mtukufu.

Endapo Mtume ﷺ Angemzulia Allah تعالى Angeadhibiwa.

Allah تعالى Amesema,

وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا

“Na lau kama angelituzulia...”

Maana yake: ‘Kama Muhammad alizua jambo dhidi Yetu, kama wanavyodai, na akaongeza au kupunguza chochote katika Ujumbe au alisema jambo

akalihusisha Nasi, basi bila shaka Tungemuadhibu vikali. Na kwa hakika, Muhammad hakufanya hayo (kama makafiri walivyodai)."

Hivyo Allah تعالى Anasema,

لَأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ﴿٤٤﴾

"Bila ya shaka Tungelimshika kwa mkono wa kulia."

Imesemwa kuwa maana yake, "Tungemshika kwa mkono wa kulia kwa sababu una nguvu za kushika."

ثُمَّ لَفَطَعْنَا مِنْهُ الْوَتِينَ ﴿٤٥﴾

"Kisha kwa hakika Tungelimkata mshipa mkubwa wa moyo!"

Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, "Al-Watin" ina maana mshipa tegemezi katika moyo: Na ni mshipa wa ateri na vena iliyoshikana na moyo.¹ "Haya yamenenwa pia na Ikrimah, Said bin Jubayr, Al-Hakim, Qatadah, Adh-Dhahak, Muslim Al-Batin na Abu Sakhr Hamayd bin Ziyad.² Muhammad bin Ka'b amesema, "Al-Watin" Ni moyo, na kila kinachofanya kazi karibu yake."³

Kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

فَمَا مِنْكُمْ مِّنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِيزٍ ﴿٤٦﴾

"Na hapana yeyote katika nyinyi ambaye angeliweza kutuzuia."

Maana yake: Hapana kati yenu angeweza kuzuia Tulilotaka Kumfanyia. Maana ya yote haya ni kusema kuwa Muhammad ﷺ ni mwaminifu, mcha-Mungu na aliongozwa kwa sababu Allah تعالى Alidhamiria Kufikisha Alichomtuma na Allah تعالى Akamsaidia kwa miujiza na ushahidi uliokamilika."

وَأِنَّهُمْ لَلْمُتَّقِينَ ﴿٤٧﴾

"Kwa hakika hii ni mawaidha kwa wachamungu."

Maana yake: Qur'an. Haya ni kama alivyosema Allah تعالى,

¹ At-Tabari 23:593.

² At-Tabari 23:593, na Ad-Dur Al-Manthur 8:276.

³ Al-Qurtubi 18:276.

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا هُدًى وَشِفَاءً ۗ وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي ءَاذَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى ۗ أُولَٰئِكَ يُنَادَوْنَ مِن مَّكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٤٤﴾

“Sema: Hii (Qur’ani) ni uwongofu na poza kwa wale walioamini, na wasioamini umo uziwi katika masikio yao, nayo kwao imezibwa hawaioni.” (41:44)

Kisha Allah تعالی Akasema,

وَإِنَّا لَنَعْلَمُ أَنَّ مِنكُم مُّكَذِّبِينَ ﴿٤٥﴾

“Na hakika Sisi bila ya shaka Tunajua kwamba miongoni mwenu wapo wanaokadhibisha.”

Maana yake: Kwa maelezo na ufafanuzi huu, bado watakuwapo miongoni mwenu ambao wanakanusha Qur’ani.

Kisha Allah تعالی Anasema,

وَإِنَّهُ لَحَسْرَةٌ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٤٦﴾

“Na hakika bila ya shaka itakuwa ni majuto kwa wanaokataa.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالی amesema, “Na kwa hakika kukataa huko kutakuwa majuto kwa makafiri Siku ya Kiyama.”¹ Pia Ibn Jarir رحمه الله تعالی ametaja kauli sawa na hiyo kutoka kwa Qatadah.² Inawezekana kuwa na maana ya kuikataa Qur’an, kwa hali hiyo Ayah hiyo itakuwa na maana kuwa Qur’an ni kuamini yaliyomo ndio sababu ya majuto ya makafiri.

Sawa na Allah تعالی Anavyosema,

كَذَٰلِكَ سَلَكَنتَهُ فِي قُلُوبِ الْمُجْرِمِينَ ﴿٤٧﴾ لَا يُؤْمِنُونَ بِهِ حَتَّىٰ يَرَوُا الْعَذَابَ
الْأَلِيمَ ﴿٤٨﴾

“Namna hivi Tunaingiza katika nyoyo za wakosefu. Hawataiamini mpaka waione adhabu chungu.” (26:200-201)

¹ At-Tabari 23:595.

² At-Tabari 23:595.

Na Allah تعالی Amesema,

وَحِيلَ بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ مَا يَشْتَهُونَ

“Na watatiliwa kizuizi baina yao na hayo wanayoyatamani.” (34:54)

Kwa hiyo, Allah تعالی Anasema hapa,

وَإِنَّهُمْ لَحَقُّ الْيَقِينِ ﴿٥٥﴾

“Na hakika hii bila ya shaka ni haki ya yakini.”

Maana yake: Taarifa sahihi na za kweli ambazo hazina shaka au zinazokanganya. Kisha Allah تعالی Anasema,

فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٥٦﴾

“Basi Litakase Jina la Mola Wako Mlezi Mtukufu.”

Maana yake: Yule Aliyeteremsha Qur’an Tukufu.

Huu ni mwisho wa maelezo (Tafsiri) ya *Suratu Al-Haqqad*. Na Sifa na Shukrani Zinamstahiki Allah تعالی.

* * *

Tafsiri ya Suratul Maarij¹

Sura ya 70

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْمَاعِرِجِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

سَأَلَ سَائِلٌ بِعَذَابٍ وَاقِعٍ ﴿١﴾ لِلْكَافِرِينَ لَيْسَ لَهُ
 دَافِعٌ ﴿٢﴾ مِنَ اللَّهِ ذِي الْمَعَارِجِ ﴿٣﴾ تَعْرُجُ
 الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ
 أَلْفَ سَنَةٍ ﴿٤﴾ فَأَصْبَرَ صَبْرًا جَمِيلًا ﴿٥﴾ إِنَّهُمْ
 يَرَوْنَهُ بَعِيدًا ﴿٦﴾ وَنَرَنَهُ قَرِيبًا ﴿٧﴾
 وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ ﴿٨﴾ وَلَا يَسْأَلُ حَمِيمًا
 حَمِيمًا ﴿٩﴾ يُبْصِرُونَهُمْ ۖ يَوْمَ الْمُجْرِمِ لَوْ يَفْتَدِي مِنْ عَذَابٍ
 يَوْمِئِذٍ بِبَنِيهِ ﴿١٠﴾ وَصَلْحَتِيهِ وَأَخِيهِ ﴿١١﴾ وَفَصِيلَتِهِ الَّتِي
 تُؤْتِيهِ ﴿١٢﴾ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ يُنْجِيهِ ﴿١٣﴾ كَلَّا
 إِنَّهَا لَطْفٌ ﴿١٤﴾ نَزَاعَةٌ لِلشَّوَى ﴿١٥﴾ تَدْعُوا مَنْ أَدْبَرَ
 وَتَوَلَّى ﴿١٦﴾ وَجَمَعَ فَأَوْعَى ﴿١٧﴾

سَأَلَ سَائِلٌ بِعَذَابٍ وَاقِعٍ ﴿١﴾
 لِلْكَافِرِينَ لَيْسَ لَهُ دَافِعٌ ﴿٢﴾
 مِنَ اللَّهِ ذِي الْمَعَارِجِ ﴿٣﴾ تَعْرُجُ
 الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ
 أَلْفَ سَنَةٍ ﴿٤﴾ فَأَصْبَرَ صَبْرًا جَمِيلًا ﴿٥﴾
 إِنَّهُمْ يَرَوْنَهُ بَعِيدًا ﴿٦﴾ وَنَرَنَهُ قَرِيبًا ﴿٧﴾

1. Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea,
2. Kwa makafiri - ambayo hapana awezaye kuizuia.
3. Kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye mbingu za daraja.
4. Malaika na Jibril hupanda kuendea Kwake katika siku ambayo kadiri yake ni miaka elfu hamsini!

¹ Sura hii inajulikana kwa jina la Al-Maarij.

5. *Basi subiri kwa subira njema.*

6. *Hakika wao wanaiona iko mbali,*

7. *Na Sisi Tunaiona iko karibu.*

Ombi la Kutaka Kiyama Kitokee Haraka.

سَأَلَ سَائِلٌ بِعَذَابٍ وَقِيعٍ ﴿٧٠﴾

“Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea,”

Aya hii ina Maana ya: Kufikiriwa ambayo inadokezwa na herufi “Ba”. Ni kama inasema, muulizaji aliomba kuharakishwa adhabu.

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَدَسْتَعِجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ وَلَنْ يُخْلِفَ اللَّهُ وَعْدَهُ ۗ

“Na wanakuhimiza ulete adhabu, lakini Mwenyezi Mungu hatakwenda kinyume na Ahadi Yake kabisa.” (22:47)

Maana yake: Adhabu Yake itatokea na hapana kuikwepa. Al-Awfi alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuhusu aya hii,

سَأَلَ سَائِلٌ بِعَذَابٍ وَقِيعٍ ﴿٧٠﴾

“Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea.”

“Hilo ni swali la makafiri kuhusu adhabu ya Allah تعالى na itawafika.”¹ Ibn Abi Najih amepokea kutoka kwa Mujahid Kauli ya Allah تعالى,

سَأَلَ سَائِلٌ

“Muulizaji aliuliza...”

“Mtu aliomba adhabu ya akhera itokee hapa duniani.” Kisha akasema, “Hii inafanana na Kauli yao,

¹ At-Tabari 23:599.

اللَّهُمَّ إِنْ كَانَ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَابًا مِنَ السَّمَاءِ أَوْ أُنزِلْ عَلَيْنَا
بِعَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٣٢﴾

“Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo Kwako basi tunyeshee mawe kutoka mbinguni, au tulettee adhabu yoyote iliyochungu”¹ (8:32)

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۚ فِطْرَةَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ لَا تَمَنَّهُ الْمُكْفِرِينَ ﴿١٠٦﴾

“...itakayotokea, kwa makafiri...”

Maana yake: Inawasubiri ikijiandaa na makafiri. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema “Waqi” Maana yake: ‘Itakayokuja.’

لَيْسَ لَهُ دَافِعٌ ﴿١٠٧﴾

“...ambayo hapana awezaye kuizuia ...”

Maana yake: Hapana mtu awezaye kuizuia endapo Allah تعالى Atataka itokee. Hivyo Allah تعالى Anasema,

مِنْ أَلْفِ مَعَارِجٍ ﴿١٠٨﴾

“Kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye mbingu za daraja...”

Tafsiri ya “Mola wa Njia za Kupaa.”

Ali bin Abi Talhah amenukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, “Mola wa njia za kupaa maana yake ubora na wingi.”² Mujahid amesema “Mola wa njia za juu ina maana njia za kupaa kwenda mbinguni.”³ Kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

تَعْرُجُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ إِلَيْهِ ﴿١٠٩﴾

“Malaika na Jibril hupanda kuendea Kwake ...”

¹ At-Tabari 23:599.

² At-Tabari 23:600.

³ At-Tabari 23:600.

Abdur-Razaq amenukuu kutoka kwa Ma'mar kutoka kwa Qatadah kuwa *Taaruju* ina maana kwenda juu. Kwa kurejea kwenye *Ruh*. Abu Salih amesema, "Ni viumbe miongoni mwa viumbe wa Allah تعالى wanafanana na binadamu lakini si binadamu."

Inawezekana kuwa hapa ina maana ya Jibril عليه السلام. Hapa imetumika kanuni ya lugha ya kumtaja mtu au kitu mwenye wadhifa maalumu, ambaye ni sehemu ya kundi hilo. Pia inawezekana kuwa roho za wanadamu. Kwa kuwa roho zinapofishwa zinapandishwa mbinguni, zinapotolewa wakati wa kifo, zinarufaishwa kama isemavyo hadithi ya Al-Bara رضي الله عنه.¹

Maana ya "Siku ya Kipimo ambayo Kipimo chake ni miaka elfu khamsini".

Kuhusu Kauli ya Allah تعالى.

فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ ﴿١٠﴾

"...katika siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu Khamsini!"

Hii inahusu Siku ya Kiyama. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما Maana ya Aya hii,

فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ ﴿١٠﴾

"...katika siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu khamsini!"

"Ni siku ya Kiama." Isnadi yake ni sahihi. Ath-Thawri رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Simak bin Harb kutoka kwa Ikrimah kuwa alisema kuhusu aya hii, "Ni siku ya Kiama." Adh-dhahak na Ibn Zayd, walisema vivyo hivyo. Ali bin Abi Talhah alisimulia kuhusu Aya,

تَعْرُجُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ ﴿١٠﴾

"Malaika na Jibril hupanda kwenda Kwake katika siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu khamsini!"

¹ *At-Tiwal* cha At-Tabarani na. 238.

“Ni Siku ya Kiyama ambayo Allah تعالی Ameifanya kwa makafiri iwe kipimo chake kuwa miaka elfu khamsini.”¹ Hadithi nyingi zimeripotwa kwa maana hii.

Imam Ahmad amepokea kutoka kwa Abu Umar Al-Ghudan kuwa alisema, “Nilikuwa pamoja na Abu Hurayrah رضي الله عنه akapita mtu kutoka kwa Bani Amir bin Sasaah pakasemwa: “Mtu huyu ana mali nyingi kuliko watu wote wa Bani Amir. Hivyo Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, ‘mrejesheni kwangu’. Hivyo wakamrejeshu yule mtu kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه. Kisha Abu Hurayrah رضي الله عنه akasema “Nimefahamishwa kwamba wewe una miliki mali nyingi.’ Yule mtu kutoka Bani Amir alijibu ‘Ndiyo, Naapa kwa Allah تعالی. Nina ngamia wekundu mia moja, wenye rangi ya hudhurungi mia moja...’ Na akaendelea kuwahesabu ngamia wa rangi anuwai, mataifa ya watumwa aliowamiliki na farasi wa vita. Hivyo Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, ‘Jihadhari na kwato za ngamia na kwato za mifugo mingine inayotolewa Zaka!” Akawa akiyarejea maneno hayo mpaka rangi ya bwana yule ikaanza kubadilika. Kisha mtu yule akasema, ‘Ewe Abu Hurayrah maneno gani hayo?’ Abu Hurayrah رضي الله عنه akajibu, ‘nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«مَنْ كَانَتْ لَهُ إِبِلٌ لَا يُعْطِي حَقَّهَا فِي نَجْدَتِهَا وَرَسُولِهَا»

“Mtu yeyote mwenye ngamia na asiwatolee Zakah katika Najdah na Risl (uzito na wepesi wao) zao...”

Tulikatiza kwa kusema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Nini Najdah na Risl zao?’ Alisema,

«فِي عُسْرِهَا وَنُسْرِهَا، فَإِنَّهَا تَأْتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ كَأَعْدَى مَا كَانَتْ وَأَكْثَرِهِ وَأَسْمَهُ وَأَسْرَهُ، ثُمَّ يُطَّحُّ لَهَا بِقَاعٍ قَرَقَرٍ فَتَطْرُقُهُ بِأَخْفَافِهَا، فَإِذَا جَاوَزَتْهُ أُخْرَاَهَا أُعِيدَتْ عَلَيْهِ أَوْلَاَهَا فِي يَوْمٍ كَانَ بِمِقْدَارِهِ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ، حَتَّى يُقْضَى بَيْنَ النَّاسِ قِيَرَى سَيِّئَةٍ. وَإِذَا كَانَتْ لَهُ بَقَرٌ لَا يُعْطِي حَقَّهَا فِي نَجْدَتِهَا وَرَسُولِهَا، فَإِنَّهَا تَأْتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ كَأَعْدَى مَا كَانَتْ وَأَكْثَرِهِ وَأَسْمَهُ وَأَسْرَهُ، ثُمَّ يُطَّحُّ لَهَا بِقَاعٍ قَرَقَرٍ، فَتَطْرُقُهُ كُلُّ ذَاتِ ظَلْفٍ يَطْلِفُهَا وَتَنْطَلِحُهُ كُلُّ ذَاتِ قَرْنٍ بِقَرْنِهَا، لَيْسَ فِيهَا عَفْصَاءٌ وَلَا عُضْبَاءٌ، إِذَا جَاوَزَتْهُ أُخْرَاَهَا

¹ At-Tabari 23:601.

أُعِيدَتْ عَلَيْهِ أَوْلَاهَا، فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ حَتَّى يُفْضَى بَيْنَ النَّاسِ
 قَيْرَى سَبِيلَهُ. وَإِذَا كَانَتْ لَهُ غَنَمٌ لَا يُعْطِي حَقَّهَا فِي نَجْدَتِهَا وَرَسُولُهَا فَإِنَّا تَأْتِي يَوْمَ
 الْقِيَامَةِ كَأَغْذٍ مَا كَانَتْ وَأَسْمِيهِ وَأَسْرِهِ حَتَّى يُبْطِحَ لَهَا بِقَاعٍ قَرَقَرٍ نَقَطُوهُ كُلُّ ذَاتٍ
 ظَلْفٍ بِظَلْفِهَا وَتَنْطَحُهُ كُلُّ ذَاتٍ قَرْنٍ بِقَرْنِهَا، لَيْسَ فِيهَا عَفْصَاءٌ وَلَا عَضْبَاءٌ إِذَا
 جَاوَزَتْهُ أَخْرَاهَا أُعِيدَتْ عَلَيْهِ أَوْلَاهَا، فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ، حَتَّى
 يُفْضَى بَيْنَ النَّاسِ قَيْرَى سَبِيلَهُ»

“Ni uzito wao na wepesi wao, kwani kwa hakika, watakuja Siku ya Kiyama wakiwa na afya zaidi kuliko mwanzo. Idadi yao itakuwa imeongezeka, wanene waliochangamka na wakaidi. Kisha kutatandikwa uwanda laini na watamkanyaga kwa kwato zao. Wa mwisho atakapomaliza kumkanyaga ataanza tena wa mwanzo kumkanyaga kwa siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu khamsini. Hili litaendelea mpaka kadhia ya watu wote itakapoamuliwa. Kisha yule aliyezuia Zakah ataoneshwa njia yake (yaani ama Peponi au Motoni). Endapo alikuwa na ng’ombe ambao hakuwatolea Zakah wakati wa raha na wa matatizo, basi watakuja Siku ya Kiyama wakiwa na afya kuliko walivyokuwa mwanzoni. Idadi yao itaongezeka, wanene, wamechangamka wa wakorofi. Kisha mmoja wao mwenye kwato atamkanyaga kwa kwato zake, na kila mmoja wao mwenye pembe atamchoma kwa pembe zake. Hatakuwepo mnyama asiye na pembe au mwenye pembe zilizopinda. Wa mwisho akishampitia juu yake, yule wa mwanzo atarejea kumkanyaga tena katika siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu khamsini. Zoezi hili litaendelea mpaka kesi za watu wote zimeamuliwa. Kisha yule (aliyezuia Zakah) ataona njia yake (yaani, ama ya Peponi au Motoni). Endapo alikuwa na Kondoo ambao hakuwalipia Zakah katika wakati wa matatizo au raha, basi watakuja Siku ya Hukumu wakiwa na afya kuliko walivyokuwa mwanzoni. Idadi yao itaongezeka, wanene na wamechangamka zaidi. Kisha uwanda mnyofu utatandazwa kwa ajili yao na watamkanyaga. Kila mwenye kwato atamkanyaga kwa kwato zake, hakutakuwa na asiye na pembe au kuwa na pembe zilizopinda miongoni mwao. Wa mwisho akishampitia, yule wa mwanzo atarejea kumkanyaga tena

kwa siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu khamsini. Zoezi hili litaendelea mpaka kesi za watu wote ziwe zimeamuliwa. Kisha yule (aliyezuia Zakah) ataona njia yake (yaani, ama ya Peponi au Motoni)."

Kisha mtu yule kutoka Bani Amir alisema, "Ni ipi haki ya ngamia, Ewe Abu Hurayrah? "Abu Hurairah رضي الله عنه akajibu, 'Ni kile utoacho (katika malipo ya Zakah) katika ngamia wako wenye thamani, unaowapenda, wenye kutoa maziwa wanaofaa kupandwa kwa safari, na wenye kupandisha ngamia jike."¹

Hadithi hii ilirekodiwa pia na Abu Dawud na An-Nasai.²

Masimulizi tofauti ya Hadithi hii.

Imam Ahmad amepokea kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema:

مَا مِنْ صَاحِبٍ كُنْتُ لَا يُؤَدِّي حَقَّهُ إِلَّا جُعِلَ صَنَائِحَ، يُحْمَى عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ،
فَتُكْوَى بِهَا جِبْهُهُ وَجَنْبُهُ وَظَهْرُهُ، حَتَّى يَحْكُمَ اللَّهُ بَيْنَ عِبَادِهِ فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ
خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ مِمَّا تَعُدُّونَ، ثُمَّ يَرَى سَبِيلَهُ إِمَّا إِلَى الْجَنَّةِ وَإِمَّا إِلَى النَّارِ

"Mtu yeyote mwenye mali ambayo hailipii haki yake isipokuwa itafanywa vipande vya chuma vyenye moto na kuwekwa juu yake ndani ya Jahannam. Sehemu ya mbele ya kichwa chake, pembeni na nyuma itachomwa na hivi vipande vya chuma. Hali hii itaendelea mpaka Allah Atakapowahukumu waja wake katika Siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu khamsini kama tunavyohesabu. Kisha ataoneshwa njia yake, ama Peponi au kwenye Moto."

Kishapo yeye (Abu Hurayrah رضي الله عنه) akataja ukamilifu kwa kuanza na Hadithi kuhusu kondoo na ngamia kama ilivyotajwa awali. Katika mapokezi haya (ya Ahmad) Mtume ﷺ pia aliongeza,

¹ Ahmad 2:489.

² Abu Dawud 2:304, na AnNasai 12:5.

«الْخَيْلُ لثَلَاثَةِ: لِرَجُلٍ أُجْرٌ، وَلِرَجُلٍ سِتْرٌ، وَعَلَى رَجُلٍ وَزْرٌ»

“Farasi ni kwa mambo matatu (Siku ya Kiyama): kwa mmoja ni zawadi, kwa mwingine ni ngao (kinga), na kwa mtu mwingine ni mzigo”.

Na Hadithi inaendelea.¹ Aidha Muslim aliinukuu hadithi hii yote japokuwa Al-Bukhari hakuitaja.² Lengo la kuitaja hapa ni kauli ya Mtume ﷺ,

«حَتَّى يَحْكُمَ اللَّهُ بَيْنَ عِبَادِهِ فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ»

“Mpaka Allah Anahukumu kati ya waja wake katika siku yenye urefu wa miaka elfu khamsini.”

Mtume ﷺ Aaswa Kuvumilia

Kisha Allah تعالى Anasema,

فَأَصْبِرْ صَبْرًا جَمِيلًا ﴿٥٠﴾

“Basi subiri kwa subira njema.”

Maana yake: Kuwa na subira, Ewe Muhammad, kwa kukataliwa na watu wako na kwa kutaka kuharakishwa adhabu kwa kuwa wanadhani haitotokea! Allah تعالى Anasema katika Aya nyingine,

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا وَالَّذِينَ آمَنُوا مُشْفِقُونَ مِنْهَا وَيَعْلَمُونَ أَنَّهَا

الْحَقُّ ۗ أَلَا إِنَّ الَّذِينَ يُمَارِؤْنَ فِي السَّاعَةِ لَفِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ﴿٥١﴾

“Wasioamini huihimiza hiyo Saa ifike upesi; lakini wanaoamini wanaiogopa, na wanajua kwamba hakika hiyo ni kweli. Ama kwa hakika hao wanaobishana katika khabari za hiyo Saa wamo katika upotofu wa mbali kabisa.” (42:18)

Kisha Allah تعالى Anasema,

¹ Ahmad 2:262.

² Muslim 2:282.

إِنَّمَا يَرَوْنَهُ بَعِيدًا ﴿١٦﴾

“Hakika wao wanaiona iko mbali.”Maana yake: Adhabu kutokea na kusimama Qiyama (Siku ya Hukumu). Makafiri wanaiona ipo mbali mno kutokea. Kwa maana ni muhali kutokea.

وَتَرَاهُ قَرِيبًا ﴿١٧﴾

“Na Sisi Tunaiona iko karibu.”Maana yake: Waumini wanaamini kuwa kutokea kwake kuko karibu, japokuwa muda wake wa kutokea haufahamiki na hapana ajuaye isipokuwa Allah تعالی. Na yote yanayokaribia ni karibu na bila shaka yatatokea.

يَوْمَ تَكُونُ السَّمَاءُ كَالْهَلِجِ ﴿١٨﴾ وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ ﴿١٩﴾ وَلَا يَسْأَلُ حَمِيمٌ حَمِيمًا ﴿٢٠﴾
 يُبْصِرُونَهُمْ يَوْمَ الْمَجْرِمِ لَوْ يَفْتَدِي مِنْ عَذَابٍ يَوْمِيذٍ بِبَنِيهِ ﴿٢١﴾ وَصَحْبَتِهِمْ وَأَخِيهِ ﴿٢٢﴾
 وَفَصِيلَتِهِ الَّتِي تُؤْوِيهِ ﴿٢٣﴾ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ يُنْجِيهِ ﴿٢٤﴾ كَلَّا إِنَّهَا لَأَطْفَىٰ ﴿٢٥﴾
 نَزَاعَةً لِلشَّوَىٰ ﴿٢٦﴾ تَدْعُوا مَنْ أَدْبَرَ وَتَوَلَّىٰ ﴿٢٧﴾ وَجَمَعَ فَأَوْعَىٰ ﴿٢٨﴾

8. Siku ambayo mbingu zitakapokuwa kama madini yaliyoyayushwa.

9. Na milima itakuwa kama sifi.

10. Wala jamaa hatamuuliza jamaa yake.

11. Ijapo kuwa wataoneshwa waonane. Atatamani mkosefu lau ajikomboe na adhabu ya siku hiyo kwa kuwatoa fidia wanawe,

12. Na mkewe, na nduguye,

13. Na jamaa zake waliokuwa wakimkimu,

14. Na wote waliomo duniani, kisha aokoke yeye.

15. La, hashu! Kwa hakika huo ni Moto mkali kabisa,

16. Unaobabua ngozi ya kichwa!

17. Utamuita kila aliyegeuza mgongo na akageuka.

18. Na akakusanya mali, kisha akayahifadhi.

Vitisho vya Siku ya Kiyama.

Allah تعالى Anasema ya kuwa adhabu itawaangukia makafiri.

يَوْمَ تَكُونُ السَّمَاءُ كَالْهَلِّ ۝

“Siku ambayo mbingu zitakapokuwa kama madini yaliyoyayushwa.”

Ibn Abbas, Mujahid, Ata, Said bin Jubayr, Ikrimah, As-Suddi na wengineo رضي الله عنهم wote wamesema, “Kama mabaki ya mafuta.”

وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ ۝

“Na milima itakuwa kama sufi.”

Maana yake: Kama fungu la sufu. Kauli hii ni ya Mujahid, Qatadah na As-Suddi.¹ Ayah hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى.

وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ الْمَنْفُوشِ ۝

“Na milima itakuwa kama sufi iliyochambuliwa!” (101:5)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَلَا يَسْأَلُ حَمِيمٌ حَمِيمًا ۝ يُبْصِرُونَ ۝

“Wala jamaa hatamuuliza jamaa yake. Ijapokuwa wataoneshwa waonane.”

Kwa maana: Hapana rafiki wa karibu atakayemuuliza jamaa yake wa karibu hali yake, atakapomuona akiwa katika hali mbaya kabisa. Atahofia nafsi yake na kutojali ya wengine. Al-Awfi amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما watatambuana baina yao. Kisha watakaribiana baada ya hapo.

Kama Allah تعالى Anavyosema,

لِكُلِّ أَمْرٍ مِّنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ ۝

“Kila mtu miongoni mwao siku hiyo atakuwa na lake la kumtoshia.” (80:37)²

¹ At-Tabari 23:604.

² At-Tabari 23:605.

Aya hii tukufu inashabihiana na Kauli Yake Allah تعالى

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمْ وَأَخْشَوْا يَوْمًا لَا تَجْزِي وَالِدٌ عَنْ وَلَدِهِ وَلَا مَوْلُودٌ هُوَ جَارٍ
عَنْ وَالِدِهِ شَيْئًا إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ ^ط

“Enyi watu! Mcheni Mola Wenu Mlezi, na iogopeni siku ambayo mzazi hatamfaa mwana, wala mwana hatamfaa mzazi kwa lolote. Hakika Ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli.” (31:33)

Pia Amesema:

وَإِن تَدْعُ مُثْقَلَةٌ إِلَىٰ جَمَلِهَا لَا تُحْمَلُ مِنْهُ شَيْءٌ وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ^ط

“Na mbebaji habebi mzigo wa mwingine. Na aliyetopewa na mzigo wake akiomba uchukuliwe hautachukuliwa hata kidogo, hata kama ni jamaa yake.” (35:18)

Na Anasema,

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ فَلَا أَنْسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَتَسَاءَلُونَ ﴿١٠١﴾

“Basi litapopulizwa baragumu hapo hautakuwapo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana.” (23:101)

Na vivyo hivyo Amesema,

يَوْمَ يَفِرُّ الْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ ﴿٣٤﴾ وَأُمِّهِ وَأَبِيهِ ﴿٣٥﴾ وَصَاحِبَتِهِ وَبَنِيهِ ﴿٣٦﴾ لِكُلِّ أُمَّرٍ يَوْمَئِذٍ يَوْمِئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ ﴿٣٧﴾

“Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye, na mamaye na babaye, na mkewe na wanawe - Kila mtu miongoni mwao siku hiyo atakuwa na lake la kumtoshia.” (80:34-37)

Kisha Allah تعالى Amesema hapa,

يَوْمَ الْمُجْرِمِ لَوْ يَفْتَدِي مِنْ عَذَابِ يَوْمِئِذٍ بِبَنِيهِ ﴿٤٠﴾ وَصَاحِبَتِهِ وَأَخِيهِ ﴿٤١﴾ وَفَصِيلَتِهِ
الَّتِي تُتَوَكَّلُ بِهَا ﴿٤٢﴾ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ يُنَجِّهِ ﴿٤٣﴾ كَلَّا ^ط

“Atatamani mkosefu lau ajikomboe na adhabu ya siku hiyo kwa kuwatoa fidia wanawe, na mkewe, na nduguye, na jamaa zake

waliokuwa wakimkimu, na wote waliomo duniani, kisha aokoke yeye. La..."

Maana yake: Hapana fidia itayokubalika kutoka kwake japo ataleta watu wote wa duniani (kama fidia) na hata alete mali (thamani) zaidi aliyonayo, hata ikiwa ni ardhi iliyosheheni dhahabu. Hata iwe ni mtoto aliyekuwa kipenzi zaidi kwake kuliko pigo la mwisho la moyo wake katika maisha ya dunia. Angependelea kumtoa mtoto kama fidia ili aokoke na adhabu ya Allah تعالی Siku ya Kiyama atakapoona vitisho. Pamoja na hayo, hata huyu mtoto hatokubaliwa kuwa fidia. Mujahid na As-Suddi wamesema,

وَفَصِيلَتِهِ

"Na jamaa zake ..." "Hii ina maana: Kabila lake na ukoo wake."¹ Ikrimah amesema, "Hii ina maana ukoo wa kabila atokalo." Ashhab amepokea kutoka kwa Malik kuwa amesema, "Fasilah maana yake ni mamaye." Allah تعالی Amesema,

إِنَّمَا لَطَىٰ

"Kwa hakika huo ni Moto mkali kabisa." Hapa anaelezea Jahannamu na ukali wa joto lake,

تَرَاعَةَ لِّلشَّوَىٰ

"Unaobabua ngozi ya kichwa!" Ibn Abbas na Mujahid wamesema, "Ni ngozi ya kichwa."² Al-Hasan Al-Basri na Thabit Al-Bunasi walisema,

تَرَاعَةَ لِّلشَّوَىٰ

"Unaobabua ngozi ya kichwa!" "Sehemu za uso zinazoheshimika." Qatadah amesema,

تَرَاعَةَ لِّلشَّوَىٰ

"Unaobabua ngozi ya kichwa!" "Hii Ina Maana: Kuondoa sehemu ya juu katika kichwa chake, sehemu za uso zinazoheshimika, maumbile yake na mikono yake."³ Adh-Dhahak amesema, "Hii ina maana itakwangua nyama na ngozi na kisibaki kitu ila mifupa."⁴ Ibn Zaid amesema, "Shawaa" ni uboho wa mifupa."⁵ Ama kwa,

¹ At-Tabari 23:606.

² At-Tabari 23:608.

³ At-Tabari: 23:609.

⁴ At-Tabari: 23:609.

⁵ At-Tabari: 23:609.

تَزَاعَةٌ

“Unaobabua...”

Ibn Zayd amesema, “Ni kukata mifupa yao na kubadilisha ngozi zao na maumbile yao.” Kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

تَدْعُوا مَنْ أَدْبَرَ وَتَوَلَّىٰ ۖ وَجَمَعَ فَأَوْعَىٰ ۖ

“Utamuita kila aliyegeuza mgongo na akageuka. Na akakusanya mali, kisha akayahifadhi.”

Maana yake: Moto utawaita watu wake ambao Allah تعالى Amewaumba wao, na akawa fanya wao kuwa ni kuni katika moto huo, kwa kutambua kuwa watatenda amali stahiki ya maisha ya kidunia. Itawaita Siku ya Kiyama kwa lugha sahihi fasaha. Kisha utawatoa kwenye kundi la watu kama ndege anavyo donoa nafaka. Kwani wao walikuwa kama Allah تعالى Alivyosema, kwa wale waliogeuza migongo yao na wakawa mbali. Hii ina maana walikana kwa mioyo yao na wakatelekeza kufanya amali kwa mikono yao.

وَجَمَعَ فَأَوْعَىٰ ۖ

“Na akakusanya mali, kisha akayahifadhi.”

Maana yake: Alikusanya mali na kuirundika na kuificha. Maana yake akificha na akikataa kutoa haki ya lazima ya Allah تعالى Ambayo ni wajibu juu yake katika matumizi na kutoa Zakah ya lazima. Ilinukuliwa katika Hadithi ambayo Mtume ﷺ alisema,

«لَا تُوعِي فُيُوعِي اللَّهِ عَلَيْكَ»

“Usiwe bahili katika (mali yako) vinginevyo Allah Atayafanya ya shida maisha yako.”¹

* * *

¹ Muslim 2:713.

* إِنَّ الْإِنْسَانَ خُلِقَ هَلُوعًا ﴿١٩﴾ إِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ جَزُوعًا ﴿٢٠﴾
 وَإِذَا مَسَّهُ الْخَيْرُ مَنُوعًا ﴿٢١﴾ إِلَّا الْمُصَلِّينَ ﴿٢٢﴾
 الَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ دَائِمُونَ ﴿٢٣﴾ وَالَّذِينَ فِي
 أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ ﴿٢٤﴾ لِلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿٢٥﴾
 وَالَّذِينَ يُصَدِّقُونَ بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿٢٦﴾ وَالَّذِينَ هُمْ مِنَ
 عَذَابِ رَبِّهِمْ مُشْفِقُونَ ﴿٢٧﴾ إِنَّ عَذَابَ رَبِّهِمْ غَيْرُ مَأْمُونٍ
 ﴿٢٨﴾ وَالَّذِينَ هُمْ لِأُزْوَاجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٢٩﴾ إِلَّا عَلَى
 أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٣٠﴾
 فَمَنْ آتَبَعْنِي وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْعَادُونَ ﴿٣١﴾ وَالَّذِينَ
 هُمْ لِأَمْسَاتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ﴿٣٢﴾ وَالَّذِينَ هُمْ
 بِشَهَادَاتِهِمْ قَائِمُونَ ﴿٣٣﴾ وَالَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ
 سُحَّافِظُونَ ﴿٣٤﴾ أُولَئِكَ فِي جَنَّتٍ مُّكْرَمُونَ ﴿٣٥﴾ فَمَالِ
 الَّذِينَ كَفَرُوا قِبَلَكَ مُهْطِعِينَ ﴿٣٦﴾ عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ
 الشِّمَالِ عِزِينَ ﴿٣٧﴾ أَبْطَمَعُ كُلِّ امْرِئٍ مِنْهُمْ أَنْ يُدْخَلَ
 جَنَّةَ نَعِيمٍ ﴿٣٨﴾ كَلَّا ۗ إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِمَّا يَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾
 فَلَا أُقْسِمُ بِرَبِّكَ وَالْعَنَبِ ۖ إِنَّا لَقَدِيرُونَ ﴿٤٠﴾ عَلَى
 أَنْ نُبَدِّلَ خَيْرًا مِنْهُمْ وَمَا نَحْنُ بِمَسْبُوقِينَ ﴿٤١﴾ فَذَرَهُمْ
 نَحْوَضُوا وَيَلْعَبُوا حَتَّىٰ يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي يُوعَدُونَ ﴿٤٢﴾
 يَوْمَ نَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ سِرَاعًا ۗ كَأَنَّهُمْ إِلَىٰ نُصُبٍ
 يُوفَّضُونَ ﴿٤٣﴾ حَشِيعَةً أَبْصَرُهُمْ تَرَهِفُهُمْ ذَلَّةٌ ۗ ذَٰلِكَ
 الْيَوْمِ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿٤٤﴾

* إِنَّ الْإِنْسَانَ خُلِقَ هَلُوعًا ﴿١٩﴾ إِذَا
 مَسَّهُ الشَّرُّ جَزُوعًا ﴿٢٠﴾ وَإِذَا مَسَّهُ
 الْخَيْرُ مَنُوعًا ﴿٢١﴾ إِلَّا الْمُصَلِّينَ ﴿٢٢﴾
 الَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ دَائِمُونَ ﴿٢٣﴾
 وَالَّذِينَ فِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ ﴿٢٤﴾
 لِلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿٢٥﴾ وَالَّذِينَ
 يُصَدِّقُونَ بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿٢٦﴾ وَالَّذِينَ
 هُمْ مِنَ عَذَابِ رَبِّهِمْ مُشْفِقُونَ ﴿٢٧﴾
 إِنَّ عَذَابَ رَبِّهِمْ غَيْرُ مَأْمُونٍ ﴿٢٨﴾
 وَالَّذِينَ هُمْ لِأُزْوَاجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٢٩﴾
 إِلَّا عَلَىٰ أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ
 أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٣٠﴾
 فَمَنْ آتَبَعْنِي وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ
 الْعَادُونَ ﴿٣١﴾ وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمْسَاتِهِمْ
 وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ﴿٣٢﴾ وَالَّذِينَ هُمْ
 بِشَهَادَاتِهِمْ قَائِمُونَ ﴿٣٣﴾ وَالَّذِينَ هُمْ
 عَلَى صَلَاتِهِمْ سُحَّافِظُونَ ﴿٣٤﴾ أُولَئِكَ
 فِي جَنَّتٍ مُّكْرَمُونَ ﴿٣٥﴾

19. Hakika mtu ameumbwa na papara.

20. *Inapompata shari hupapatika.*
21. *Na inapomgusa kheri huizuilia.*
22. *Isipokuwa wanaosali,*
23. *Ambao wanadumisha Sala zao,*
24. *Na ambao katika mali yao iko haki maalumu*
25. *Kwa mwenye kuomba na anayejizuilia kuomba;*
26. *Na ambao wanaisadiki Siku ya Malipo,*
27. *Na ambao wanaiogopa adhabu itokayo kwa Mola wao Mlezi.*
28. *Hakika adhabu ya Mola wao Mlezi si ya kuaminika nayo.*
29. *Na ambao wanahifadhi tupu zao.*
30. *Isipokuwa kwa wake zao, au iliyomiliki mikono yao ya kuume, basi hao hawalaumiwi.*
31. *Lakini wanaotaka kinyume ya haya, basi hao ndio wanaoruka mipaka.*
32. *Na ambao wanazichunga amana zao na ahadi zao,*
33. *Na ambao wanasimama imara katika ushahidi wao.*
34. *Na ambao wanazihifadhi Sala zao.*
35. *Hao ndio watakaohishimiwa Peponi.*

Binadamu Hana Subira.

Allah تعالیٰ Anaelezea juu ya binadamu na silka yake duni ambayo Allah تعالیٰ Amemuumba nayo,

﴿ إِنَّ الْإِنْسَانَ خُلِقَ هَلُوعًا ﴾

“Hakika mtu ameumbwa na papara.”

Kisha Allah تعالیٰ Akafasiri tabia yake hiyo,

﴿ إِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ جَزُوعًا ﴾

“Inapompata shari hupapatika.”

Maana yake: Wakati wowote anapopatwa na madhara hubabaika na kufadhaika, na kuwa na hofu na anarejeshwa nyuma kutokana na ukali wa hofu na kukata tamaa kuwa hatolipwa jema.

وَإِذَا مَسَّهُ الْخَيْرُ مَنُوعًا ﴿١٩﴾

“Na anapopatwa na kheri huizuilia.”

Maana yake: Akipata neema kutoka kwa Allah تعالى, anafanya ubahili na kuwanyima watu, na atazuia haki ya Allah تعالى kwa neema hiyo aliyojaaliwa. Imam Ahmad alisema kuwa Abu Abdur-Rahman aliwafahamisha kuwa Musa bin Ali bin Rabah aliwambia kuwa alimsikia baba yake akisimulia kisa alichokipokea kutoka kwa Abdul-Aziz bin Marwan bin Al-Hakim kuwa alimsikia Abu Harayrah رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alisema,

«شَرُّ مَا فِي رَجُلٍ: شُحُّ خَالِعٍ وَجُبْنُ خَالِعٍ»

“Jambo baya kabisa lililoko kwa mtu ni pupa ya ulafi na woga uliokithiri.”¹

Abu Dawud alipokea hadithi hii kutoka kwa Abdullah bin Al-Jarrah kwa amri ya Abu Abdur-Rahman Al-Muqri, na hii ni hadithi pekee kupitia kwa Abdul-Aziz.”²

Kuwatoa Wenye Kusali katika Sifa Zilizotangulia na Ubainifu wa Amali Zao na Sala Zao

Kisha Allah تعالى Amesema,

إِلَّا الْمُصَلِّينَ ﴿٢٠﴾

“Isipokuwa wanaosali.”

Maana yake: Binadamu ameelezewa kwa mwenendo muovu isipokuwa kwa waliohifadhiwa na Allah تعالى, wakasaidiwa na kuongozwa katika mema, na kuwarahisishia wao sababu zake, na hawa ndio wenye kuswali.

¹ Ahmad 2:302.

² Abu Dawud 3:26.

الَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ دَائِمُونَ ﴿١٩﴾

“Ambao wanadumisha Sala zao,”

Imesemwa kuwa wanachunga wakati na mambo yaliyo lazima ndani yake. Haya yamenenwa na Ibn Mas’ud, Masruuq na Ibrahim An-Nakhai.¹ Aidha imesemwa; kwa maana ya unyenyekevu na utiifu katika Sala. Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى،

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٢٠﴾ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ ﴿٢١﴾

“Hakika wamefanikiwa Waumini, ambao ni wanyenyekevu katika Sala zao,” (23:1-2)

Haya yamenenwa na Uqbah bin Amir. Kutokana na maana hiyo kutumika katika istilahi ya kuelezea maji yaliyotuwama (*Al-Ma Ad-Daim*). Inathibitisha wajibu wa kuwa na utulivu ndani ya Sala. Kwa hakika, asiye na utulivu katika rukuu na sijida basi si makini (*Daim*) katika Sala yake. Hii ni kwa sababu hawi mtulivu wa nafsi yake bali anadonoa (haraka) katika Sala yake mithili adonoavyo kunguru. Kwa hiyo, hafaulu katika Sala zake. Aidha imenenwa kuwa maana yake hapa ni wale wanaofanya amali na wakadumu katika amali hizo. Hii ni sawa na hadithi iliyonukuliwa ndani ya Sahih kutoka kwa Aishah رضي الله عنها kuwa Mtume ﷺ alisema،

«أَحَبُّ الْأَعْمَالِ إِلَى اللَّهِ أَدْوَمُهَا وَإِنْ قَلَّ»

“Amali Azipendazo Allah ni zile zinazodumu hata zikiwa chache.”²

Kisha Allah تعالى Amesema،

وَالَّذِينَ فِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ ﴿٢٢﴾ لِلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿٢٣﴾

“Na ambao katika mali zao kuna haki maalumu kwa mwenye kuomba na anayejizulia kuomba.”

¹ At-Tabari 23:612.

² Muslim 1:541.

Maana yake: Katika mali yao kuna sehemu iliyothibitishwa kwa ajili ya wenye haja. Kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

وَالَّذِينَ يُصَدِّقُونَ بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿٦٩﴾

“Na ambao wanaisadiki Siku ya Malipo.”

Maana yake: Wana uhakika wa marejesho ya Mwisho (kwa Allah تعالى). Kuhesabiwa na kulipwa. Kwa hiyo, wanatenda amali za mtu anayetarajia malipo na anachelea adhabu.

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema،

وَالَّذِينَ هُمْ مِّنْ عَذَابِ رَبِّهِمْ مُّشْفِقُونَ ﴿٧٠﴾

“Na ambao wanaiogopa adhabu itokayo kwa Mola wao Mlezi.”

Maana yake: Wenye hofu na mfadhaiko،

إِنَّ عَذَابَ رَبِّهِمْ غَيْرُ مَا مُنُّوا ﴿٧١﴾

“Hakika adhabu ya Mola wao Mlezi si ya kuaminika nayo.”

Maana yake: Hapana atakayesalimika nayo (adhabu ya Allah تعالى) kwa wale waliokataa kutekeleza amri kutoka kwa Allah تعالى، isipokuwa kwa usalama unaotoka kwa Allah تعالى Mwenyewe. Kisha Allah تعالى Anasema،

وَالَّذِينَ هُمْ لِأُزُوجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٧٢﴾

“Na ambao wanahifadhi tupu zao.”

Maana yake: Wanahifadhi tupu zao kutokana na yaliyoharamishwa na wanahifadhi tupu zao kutenda ambayo hayakuruhusiwa na Allah تعالى. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema،

إِلَّا عَلَىٰ أَرْوَاحِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ

“Isipo kuwa kwa wake zao, au iliyomiliki mikono yao ya kuume.”

Maana yake: Katika wajakazi،

﴿فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْعَادُونَ﴾ فَمَنْ آتَىٰ وَرَاءَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْعَادُونَ ﴿١٩﴾

“...basi hao hawalaumiwi. Lakini wanaotaka kinyume ya haya, basi hao ndio wanaoruka mipaka.”

Maelezo haya yamekwisha tangulia katika Surat Al-Muminun, na hapana haja ya kuyarejea hapa.¹ Allah تعالى Anasema,

﴿وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمَسَاتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ﴾

“Na ambao wanazichunga amana zao na ahadi zao.”

Maana yake: Wanapopewa dhamana hawafanyi hiana na wanapoahidi wanatekeleza. Hizi ndio sifa za waumini ambazo ni kinyume na sifa bainifu za wanafiki. Haya ni sawa na yale yaliyoripotiwa katika Hadithi Sahihi.

﴿آيَةُ الْمُنَافِقِ ثَلَاثٌ: إِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا وَعَدَ أَخْلَفَ، وَإِذَا اؤْتُمِنَ خَانَ﴾

“Alama za mnafiki ni tatu, Anapozungumza husema uongo, anapoahidi hatekelezi, na anapoaminiwa hufanya hiana.”²

Katika mapokezi mengine inaelezwa,

﴿إِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا عَاهَدَ غَدَرَ، وَإِذَا خَاصَمَ فَجَرَ﴾

“Anapozungumza huongopa, anapoahidi hatekelezi na anapogombana hutumia lugha chafu.”³

Kuhusu Kauli ya Allah تعالى

﴿وَالَّذِينَ هُمْ بِشَهَادَتِهِمْ قَائِمُونَ﴾

“Na ambao wanasimama imara katika ushahidi wao.”

Hii ina maana wanaozingatia viapo vyao. Hawaongezi au kupunguza katika yale waliyoyashuhudia au kuyaficha. Allah تعالى Anasema katika Ayah nyingine.

¹ Angalia juzu ya sita, Tafsiri ya Suratu Al-Muumin (23:6-7).

² Fat’hul Al-Bari 1:111.

³ Fat’hul Al-Bari 1:111.

وَمَنْ يَكْتُمْهَا فَإِنَّهُ آثِمٌ قَلْبُهُ^٤

“Na atakayeficha basi hakika moyo wake ni wenye kutenda dhambi.” (2:283)

Kisha Allah تعالى Anasema,

وَالَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ سُخَّافُونَ ﴿٦٠﴾

“Na ambao wanazihifadhi Sala zao.”

Maana yake: Wanachunga wakati wake, nguzo zake, masharti yake. Hivyo Allah تعالى Anaanza mjadala huu wa sifa za waumini kwa Sala na Anaujumuisha na Sala na Anahitimisha kwa Sala. Hii inathibitisha umuhimu wake na sifa za hadhi yake tukufu, kama yale yaliyotangulia mwanzoni mwa *Surat Al-Muminun*. Ni mjadala huo huo. Ndio sababu Allah تعالى Amesema pale (katika *Al-Muminun*)

أُولَئِكَ هُمُ الْوَارِثُونَ ﴿٦١﴾ الَّذِينَ يَرِثُونَ الْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٦٢﴾

“Hao ndio warithi, Ambao watairithi Pepo ya Firdausi, wadumu humo.” (23:10-11)

Na Anasema hapa,

أُولَئِكَ فِي جَنَّاتٍ مُّكْرَمُونَ ﴿٦٣﴾

“Hao ndio watakaohishimiwa Peponi.”

Maana yake: Watatunukiwa starehe za aina mbalimbali.

فَمَالِ الَّذِينَ كَفَرُوا قِبَلَكَ مُهْطِعِينَ ﴿٦٤﴾ عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ عِزِينَ ﴿٦٥﴾ أَيُّطْمَعُ كُلُّ امْرِئٍ مِنْهُمْ أَنْ يُدْخَلَ جَنَّةَ نَعِيمٍ ﴿٦٦﴾ كَلَّا^٥ إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِمَّا يَعْلَمُونَ ﴿٦٧﴾ فَلَا أُقْسِمُ بِرَبِّ الْمَشَارِقِ وَالْمَغْرِبِ إِنَّا لَقَدِيرُونَ ﴿٦٨﴾ عَلَىٰ أَنْ تُبَدَّلَ خَيْرًا مِنْهُمْ وَمَا نَحْنُ بِمَسْبُوقِينَ ﴿٦٩﴾ فَذَرَهُمْ سَخِرُوا وَيَلْعَبُوا حَتَّىٰ يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي يُوعَدُونَ ﴿٧٠﴾ يَوْمَ تَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ سِرَاعًا كَأَنَّهُمْ إِلَىٰ نُصْبٍ يُوفِضُونَ ﴿٧١﴾ خَشِيعَةً أَبْصَرُهُمْ تَرَهِقُهُمْ ذِلَّةٌ ذَلِكِ الْيَوْمِ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿٧٢﴾

36. *Wana nini wale waliokufuru wanakutumbulia macho tu?*
37. *Makundi kwa makundi upande wa kulia na upande wa kushoto!*
38. *Kwani kila mmoja wao anatumai kuingizwa katika Pepo ya neema?*
39. *La, hasha! Hakika Sisi Tumewaumba kutokana na wanachokijua.*
40. *Basi naapa kwa Mola Mlezi wa mashariki zote na magharibi zote kwamba Sisi Tunaweza*
41. *Kuwabadili kwa walio bora kuliko wao; na Sisi hatushindwi.*
42. *Basi waache wapige porojo na wacheze, mpaka wakutane na siku yao wanayoahidiwa,*
43. *Siku watakapotoka makaburini haraka kama kwamba wanakimbilia mfundo,*
44. *Macho yao yatainama, fedheha itawafunika. Hiyo ndiyo Siku waliyokuwa wakiahidiwa*

Makaripio na Vitisho kwa Makafiri

Allah تعالی Anawakemea makafiri ambao waliishi pamoja na Mtume ﷺ katika zama zake, huku wakishuhudia uongofu aliopewa. Walishuhudia miujiza ya ajabu aliopewa na Allah تعالی. Hata hivyo, baada ya yote hayo walikimbia na wakajitenga naye. Walikimbia kushoto na kulia, makundi kwa makundi.

فَمَا هُمْ عَنِ التَّذْكَرَةِ مُعْرِضِينَ ﴿٤٩﴾ كَانَهُمْ حُمْرٌ مُّسْتَنْفِرَةٌ ﴿٥٠﴾ فَكَرَّتْ مِنْ قَسْوَرَةٍ ﴿٥١﴾

“Basi wana nini hata wanapuuza onyo hili? Kama kwamba wao ni pundamilia waliotimuliwa. Wanaomkimbia simba!” (74:49-51)

Huu ni mfano wa makafiri.

Na Aya hii ni sawa. Kama Asemavyo Allah تعالی,

فَمَالِ الَّذِينَ كَفَرُوا قِبَلَكَ مُهْطِعِينَ ﴿٦٧﴾

“Wana nini wale waliokufuru kwako wanaharakisha kukukana?”

Maana yake: ‘Wana matatizo gani hawa makafiri pamoja nawe, Ewe Muhammad? Kwa nini ni *Muhtiin*, yaani wanatukimbia? Hii ni kwa mujibu wa Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى na ambao wamesema, “*Muhtiin*” ni kuondoka.”

عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ عِزِينَ ﴿٦٨﴾

“Makundi kwa makundi upande wa kulia na upande wa kushoto!”

Umoja wa *Izwi* ni *Izah*, ambayo ina maaana ya kutenganisha,¹ Maana yake: Katika kutengana kwao na kutofautiana. *Al-Awfi* alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuhusu Aya,

فَمَالِ الَّذِينَ كَفَرُوا قِبَلَكَ مُهْطِعِينَ ﴿٦٧﴾

“Wana nini wale waliokufuru wanaharakisha kukukana?”

Amesema “Wanaangalia upande wako”

عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ عِزِينَ ﴿٦٨﴾

“Makundi kwa makundi upande wa kulia na upande wa kushoto!”

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “*Al-Izin* ni kundi miongoni mwa watu. Upande wa kulia na kushoto maana yake wanageuka (kulia na kushoto), wanampa kisogo Mtume ﷺ na kumdhihaki.’

Jabir bin Samurah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alitoka nje na kuwakuta wamekaa katika duara. Hivyo Mtume ﷺ alisema,

«مَا لِي أَرَاكُمْ عِزِينَ؟»

“Kwa nini nyote mko katika Izin (makundi).”²

Ahmad, Muslim, Abu Dawud, An-Nasai na Ibn Jarir wamenukuu Hadithi³ hii, Kisha, kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

¹ At-Tabari 23:620.

² At-Tabari 23:620.

³ Ahmad 5:93, Muslim 1:322, Abu Dawud 1:561, An-Nasai 3:4, na At-Tabari 23:620.

أَيُّطْمَعُ كُلُّ امْرِئٍ مِّنْهُمْ أَنْ يُدْخَلَ جَنَّةَ نَعِيمٍ ﴿٧٠﴾ كَلَّا

“Kwani kila mmoja wao anatumai kuingizwa katika Pepo ya neema? La, hashaa!”

Ina maana: Huu ni utashi wao, kisha wanamkimbia Mtume ﷺ kwa kuchukua haki? Je, wana matarajio ya kuingizwa ndani ya mabustani yapendezayo sana? La, bali makazi yao ni Motoni. Kisha Allah تعالى Anathibitisha kutokea makazi ya Mwisho na adhabu watakayoipata kwa kukamilisha kuwepo na kudai kuwa ni jambo la kufikirika. Kama ushahidi dhidi yao, Allah تعالى Anadhukuru mwanzo wa maumbile, na kuwa Kurudia mchakato huo ni rahisi kuliko kuanza mwanzo. Hili nalo wanalikubali. Allah تعالى Anasema,

إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِمَّا يَعْلَمُونَ ﴿٧١﴾

“Hakika Sisi Tumewaumba kutokana na wanachokijua.”

Maana yake: Kutokana na manii hakiri. Hivi ni kama Allah تعالى Anavyosema,

أَلَمْ نَخْلُقْكُمْ مِنْ مَّاءٍ مَّهِينٍ ﴿٧٢﴾

“Kwani Hatukukuumbeni kwa maji ya kudharauliwa?” (77:20)

Pia Allah تعالى Amesema,

فَلْيَنْظُرِ الْإِنْسَانُ مِمَّ خُلِقَ ﴿٧٣﴾ خُلِقَ مِنْ مَّاءٍ دَافِقٍ ﴿٧٤﴾ تَخْرُجُ مِنْ بَيْنِ الصُّلْبِ وَالتَّرَائِبِ ﴿٧٥﴾
 إِنَّهُ عَلَىٰ رَجْعِهِ لَقَادِرٌ ﴿٧٦﴾ يَوْمَ تُبْلَى السَّرَائِرُ ﴿٧٧﴾ فَمَا لَهُ مِنْ قُوَّةٍ وَلَا نَاصِرٍ ﴿٧٨﴾

“Hebu na ajitazame mwanaadamu ameumbwa kwa kitu gani? Ameumbwa kwa maji yatokayo kwa kuchupa. Yatokayo baina ya mifupa ya mgongo na mbavu. Hakika Yeye Ana Uweza wa Kumrudisha. Siku zitakapodhihirishwa siri. Basi hatakuwa na nguvu wala msaidizi.” (86:5-10)

Kisha Allah تعالى Anasema;

فَلَا أُقْسِمُ بِرَبِّ الْمَشَارِقِ وَالْمَغْرِبِ

“Basi naapa kwa Mola Mlezi wa Mashariki zote na Magharibi zote.”

Ina maana: Yule Aliyeumba Mbingu na Ardhi na Akajaalia mashariki na magharibi. Ndiye Yeye Aliyezidhalilisha nyota Kuzifanya zionekane upande wa mashariki na kupotelea pande za magharibi (Nukta muhimu hapa ni kwamba jambo hilo si kama wanavyodai Makafiri, kuwa hakuna marejeo ya mwisho, hapana kuhesabiwa, hapana kufufuliwa na hapana kukusanywa. Isipokuwa yote hayo yatatokea na kupita). Hakuna njia ya kuyaepa. Hii ndio sababu Allah تعالی Amekanusha mwanzoni mwa kiapo hiki. Hii inaonesha kuwa Anaapa kwa kukanusha madai yao. Huku ni kukanusha madai yao ya uongo ya kukana Siku ya Hesabu. Tayari wameshashuhudia ukubwa na nguvu za Allah تعالی zinazoshawishi kuamini zaidi ya Siku ya Kiyama, ambako ni Kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na vilivyomo ndani yake miongoni mwa viumbe mbalimbali kama, wanyama, viumbe visivyo na uhai na aina nyingine ya viumbe. Kwa sababu hii Allah تعالی Anasema,

لَخَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾

“Bila ya shaka Kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko Kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.” (40:57)

Aidha Allah تعالی Anasema,

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَكُنْ يَخْلُقْهُنَّ بِقَدْرِ عَلَى أَنْ تُحْيِيَ الْمَوْتَىٰ بَلَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٥٨﴾

“Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, Aliyeziumba mbingu na ardhi, na Hakuchoka kwa Kuziumba, kuwa ni Muweza wa Kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.” (46:33)

Allah تعالی Anasema katika Aya nyingine,

أَوَلَيْسَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدْرِ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۚ بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلَّاقُ الْعَلِيمُ ﴿٨١﴾ إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٨٢﴾

“Kwani aliye ziumba mbingu na ardhi hawezi kuwaumba mfano wao? Kwani! Naye ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi. Hakika Amri Yake Anapotaka kitu ni Kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa.” (36:81-82)

فَلَا أُقْسِمُ بِرَبِّ الْمَشَارِقِ وَالْمَغْرِبِ إِنَّا لَقَدِرُونَ ﴿٤٤﴾ عَلَىٰ أَنْ نُبَدِّلَ خَيْرًا مِنْهُمْ

“Basi naapa kwa Mola Mlezi wa mashariki na magharibi zote kwamba Sisi Tunaweza. Kuwabadili kwa waliobora kuliko wao...”

Maana yake: ‘Siku ya Kiyama Tutawafufua na Kuwapa uhai katika miili iliyo bora kuliko hii mliyo nayo sasa.’ Hakika Allah تعالى Ana Uweza wa Kufanya hayo.

وَمَا نَحْنُ بِمَسْبُوقِينَ ﴿٤٥﴾

“...na Sisi Hatushindwi.” Maana yake: “Sisi Hatushindwi.”

Ni kama Allah تعالى Alivyosema,

أُحْسِبُ الْإِنْسَانَ الْآنَ يُجْمَعُ عِظَامُهُ ﴿٤٦﴾ بَلَىٰ قَدَرِينَ عَلَىٰ أَنْ نُسَوِّيَ بَنَانَهُ ﴿٤٧﴾

“Anadhani mtu kuwa Sisi Hatutaikusanya mifupa yake? Kwani! Sisi Tunaweza hata Kuziweka sawa sawa ncha za vidole vyake!” (75:3-4)

Pia Allah تعالى Anasema,

نَحْنُ قَدَرْنَا بَيْنَكُمْ الْمَوْتَ وَمَا نَحْنُ بِمَسْبُوقِينَ ﴿٤٨﴾ عَلَىٰ أَنْ نُبَدِّلَ أَمْثَلَكُمْ وَنُنشِئَكُمْ فِي

مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٤٩﴾

“Sisi Tumekuwekeeni mauti; na wala Sisi Hatushindwi Kuwaleta wengine badala yenu na Kukuumbeni nyinyi kwa umbo msilolijua.” (56:60-61)

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alipendelea maana iwe, “Ummah utakaotutii na siyo utakaotulasi.” Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameifananisha na Kauli Yake Allah تعالى,

عَلَىٰ أَنْ نُبَدِّلَ خَيْرًا مِنْهُمْ

“Kuwabadili kwa waliobora kuliko wao.” Na,

وَإِن تَوَلَّوْا يَسْتَبَدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا أَمْثَلَكُمْ ﴿٥٠﴾

“Na mkigeuka Atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi.” (47:38).

Hata hivyo, ufafanuzi wa mwanzo ni sahihi zaidi kwa kusapotywa na aya nyingine, na Allah تعالى Aliye Juu zaidi ni Mjuzi zaidi.

Kisha Allah تعالى Anasema,

فَدَرَهُمْ

“Basi waache...” Maana yake: Ewe Muhammad!

تَخُونُوا وَيَلْعَبُوا

“...wapige porojo na wacheze...”

Maana yake: Waache katika ukanushaji na kufuru,

حَتَّىٰ يَلْتَقُوا يَوْمَئِذٍ الَّذِي يُوعَدُونَ ﴿١٧﴾

“...mpaka wakutane na siku yao wanayoahidiwa.”

Maana yake: Watajua matokeo yake na wataonja matokeo ya uovu wao.

يَوْمَ تَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ سِرَاعًا كَأَنَّهُمْ إِلَىٰ نُصُبٍ يُوفِضُونَ ﴿١٨﴾

“Siku watakapotoka makaburini kwa upesi kama kwamba wanakimbilia mfundo.”

Maana yake: Watasema wakiwa nje ya makaburi yao wakati Mola, Mwingi wa Baraka na Aliye Juu, Anawaita katika sehemu ya kuhesabiwa. Watainuka haraka na kwenda mbio kama wanaendea mnara wa makumbusho. Ibn Abbas, Mujahid na Adh-Dhahhak رضي الله عنهم wote wamesema, ‘Kama waliokuwa wakikimbilia bendera.’ Abu Aliyah na Yahya bin Abi Kathir nao wamesema vivyo, “Kana kwamba wanakimbia lengo fulani.’ Wasomaji wengi wamesoma neno hili kama “*Nasb*” (badala ya *nusub*). Hii (*Nasb*) ni kitenzi Nomino – ikiwa ni maana ya kitu kilichosimikwa. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى amesoma “*Nusubin*” hii ina maana ya sanamu. Kwa kisomo hiki, Aya ina maana, kana kwamba haraka yao kupaendea mahali hapo ni kama walivyokuwa wakiyapupia maisha ya dunia na kuyaendea masanamu walipoyaona. Wanayakimbilia haraka ili mtu awe wa mwanzo kuyagusa na kuyabusu. Haya yamenukuliwa kutoka kwa Mujahid, Yahya bin Abi Kathir, Muslim Al-Batin, Qatadah, Adh-Dhahhak, Ar Rabi bin Anas, Abu Salih, Asim bin Bahdalah, Ibn Zayd na wengineo. Kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

خَشِيعَةً أَبْصَرُهُمْ

“Macho yao yatainama...” Maana yake: Wanyenyekevu,

تَرَهْقُهُمْ ذِلَّةٌ

"...fedheha itawafunika."

Maana yake: Kwa malipo ya walivyokuwa wajuvi hapa duniani kwa kukataa kumtii Allah تعالى.

ذَٰلِكَ الْيَوْمِ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿١٩﴾

"Hiyo ndiyo Siku waliyokuwa wakiahidiwa."

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Saala Sail*. Na Shukrani zote Zinamstahiki Allah تعالى.

* * *

Tafsiri ya Suratu Nuh

Sura ya 71

Iliteremshwa Makkah

سُورَةُ نُوحٍ

إِنَّا أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِيهِ أَنْ أَنْذِرْ قَوْمَكَ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١﴾ قَالَ يَنْفَوْرِي لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٢﴾ أَنْ أَعْبُدُوا اللَّهَ وَأَتَّقُوهُ وَأَطِيعُوا ۖ يَغْفِرَ لَكُمْ مِّنْ ذُنُوبِكُمْ وَيُخْرِجَكُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۖ إِنَّ أَجَلَ اللَّهِ إِذَا جَاءَ لَا يُؤَخَّرُ ۗ لَوْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٣﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي دَعَوْتُ قَوْمِي لَيْلًا وَنَهَارًا ﴿٤﴾ فَلَمْ يَزِدْهُمْ دُعَايَ إِلَّا فِرَارًا ﴿٥﴾ وَإِنِّي كُلَّمَا دَعَوْتُهُمْ لِتَغْفِرَ لَهُمْ جَعَلُوا أَصْوَابَهُمْ فِي أَدْبَانِهِمْ وَأَسْتَفْشَوْا بَيْنَهُمْ وَأَصْرُوا وَأَسْتَكْبَرُوا اسْتِكْبَارًا ﴿٦﴾ ثُمَّ إِنِّي دَعَوْتُهُمْ جِهَارًا ﴿٧﴾ ثُمَّ إِنِّي أَعْلَنْتُ لَهُمْ وَأَسْرَرْتُ لَهُمْ إِسْرَارًا ﴿٨﴾ فَقُلْتُ اسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ إِنَّهُ كَانَ غَفَّارًا ﴿٩﴾ يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُمْ مِدْرَارًا ﴿١٠﴾ وَيُمْدِدْكُمْ بِأَمْوَالٍ وَيَبِينْ وَيَجْعَلْ لَكُمْ جَنَّاتٍ وَيَجْعَلْ لَكُمْ أَنْهَارًا ﴿١١﴾ مَا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا ﴿١٢﴾ وَقَدْ خَلَقَكُمْ أَطْوَارًا ﴿١٣﴾ أَلَمْ تَرَوْا كَيْفَ خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقًا ﴿١٤﴾ وَجَعَلَ الْقَمَرَ فِيهِنَّ نُورًا وَجَعَلَ الشَّمْسَ سِرَاجًا ﴿١٥﴾ وَاللَّهُ أُنْتَبِهُكُمْ مِنَ الْأَرْضِ نَبَاتًا ﴿١٦﴾ ثُمَّ يُعِيدْكُمْ فِيهَا وَيُخْرِجْكُمْ مِنْهَا إِخْرَاجًا ﴿١٧﴾ وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ بِسَاطًا ﴿١٨﴾ لِيَتَسَلَّكُوا مِنْهَا سُبُلًا فِجَاجًا ﴿١٩﴾

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

إِنَّا أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِيهِ أَنْ أَنْذِرْ قَوْمَكَ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١﴾ قَالَ يَنْفَوْرِي لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٢﴾ أَنْ أَعْبُدُوا اللَّهَ وَأَتَّقُوهُ وَأَطِيعُوا ۖ يَغْفِرَ لَكُمْ مِّنْ ذُنُوبِكُمْ وَيُخْرِجَكُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۖ إِنَّ أَجَلَ اللَّهِ إِذَا جَاءَ لَا يُؤَخَّرُ ۗ لَوْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٣﴾

1. Hakika Sisi Tulimtuma Nuh'u kwa watu wake: Uwaonye kaumu yako kabla ya kuwafikia adhabu chungu.

2. Akasema: Enyi watu wangu! Kwa hakika mimi ni mwonyaji wa dhaahiri kwenu,

3. Ya kwamba mumuabudu Mwenyezi Mungu, na mumche Yeye, na mnitii mimi.

4. Atakughufirieni madhambi yenu, na Atakuakhirisheni mpaka muda uliowekwa. Hakika muda wa Mwenyezi Mungu utapofika haucheleweshwi. Laiti mngejua!

Wito wa Nuhu عليه السلام kwa Watu Wake.

Allah تعالى Anamzungumzia Nuhu عليه السلام ya kuwa Alimtuma kwa watu wake Akimuamuru awaonye watu wake kabla adhabu ya Allah تعالى haijawajia. Alikuwa awaambie kama watatubia na kurejea kwa Allah تعالى wataondolewa adhabu.

أَنْ أَنْذَرَ قَوْمَكَ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٠﴾ قَالَ يَنْفَوِمِرِّي لَكُمْ نَذِيرٌ مُبِينٌ ﴿١١﴾

“Uwaonye kaumu yako kabla ya kuwafikia adhabu chungu. Akasema: Enyi watu wangu! Kwa hakika mimi ni mwonyaji wa dhaahiri kwenu.”

Maana yake: Maonyo ya wazi na jambo lililokuwa dhahiri kabisa

أَنْ أَعْبُدُوا اللَّهَ وَاتَّقُوهُ

“Ya kwamba mumuabudu Mwenyezi Mungu, na mumche Yeye, na mumtii.”

Kusudio lake, ‘acheni yale Aliyokukatazeni na mjiweke mbali na Aliyoyatangaza kuwa ni makosa.

وَأَطِيعُونَ ﴿١٢﴾

“...na mnitii mimi.” ‘Katika yale ninayokuamrisheni kuyatenda na yale ninayokukanyeni.’

يَغْفِرْ لَكُمْ مِنْ ذُنُوبِكُمْ

“Atakughufirieni madhambi yenu,” Maana yake: Endapo mtafanya ninayokuamrisheni kufanya na mkaamini niliyotumwa kwayo kwenu, basi Allah تعالى Atasamehe madhambi yenu.’

وَيُؤَخِّرْكُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ﴿١٣﴾

“...na Atakuakhirisheni mpaka muda uliowekwa.” Maana yake ni: “Atarefusha umri wenu na Atawahifadhi na mateso ambayo Angeliyaleta kwenu kama hamkujiweka mbali na makatazo Yake. Ayah hii inatumiwa kuwa ushahidi kwa wale wasemao utii kwa (Allah تعالى), uadilifu na kudumisha undugu kwa hakika huongeza umri wa mtu. Kama Hadithi ya Mtume ﷺ inavyoelezea hilo.

«صِلَّة الرَّجْمِ تَزِيدُ فِي الْعُمْرِ»

“Kuendeleza mshikamano wa familia kunaongeza umri.”¹

Na Kauli Yake Allah تعالى،

إِنَّ أَجَلَ اللَّهِ إِذَا جَاءَ لَا يُؤَخَّرُ ۗ لَوْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١﴾

“Hakika muda wa Mwenyezi Mungu utapofika haucheleweshwi. Laiti mngejua!”

Maana yake: Afanye hima kumtii (Allah تعالى) kabla Hajalipa kisasi Chake. Kwani ni dhahiri, endapo Allah تعالى Ataamrisha lolote litokee, Halirudishwi wala halizuiwi. Kwani Yeye Pekee ni Mkuu Ambaye Hushinda kila kitu, Naye ni Muweza Ambaye viumbe wote hawawezi kufanya kinyume.

قَالَ رَبِّ إِنِّي دَعَوْتُ قَوْمِي لَبِلاً وَنَهَارًا ﴿١﴾ فَلَمْ يَزِدْهُمْ دُعَايَ إِلَّا إِفْرَارًا ﴿٢﴾ وَإِنِّي كَلَّمَا دَعَوْتُهُمْ لِيَتَغَفِرَ لَهُمْ جَعَلُوا أَصْدِعُهُمْ فِي آذَانِهِمْ وَأَسْتَعْشَوْا نِيَابَهُمْ وَأَصْرَوْا ﴿٣﴾ وَأَسْتَكْبَرُوا اسْتِكْبَارًا ﴿٤﴾ ثُمَّ إِنِّي دَعَوْتُهُمْ جِهَارًا ﴿٥﴾ ثُمَّ إِنِّي أَعْلَنْتُ لَهُمْ وَأَسْرَرْتُ لَهُمْ إِسْرَارًا ﴿٦﴾ فَقُلْتُ اسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ إِنَّهُ كَانَ غَفَّارًا ﴿٧﴾ يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُمْ مِدْرَارًا ﴿٨﴾ وَيُمْدِدْكُمْ بِأَمْوَالٍ وَيُبَيِّنْ وَيَجْعَلْ لَكُمْ جَنَّاتٍ وَيَجْعَلْ لَكُمْ أَنْهَارًا ﴿٩﴾ مَا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا ﴿١٠﴾ وَقَدْ خَلَقَكُمْ أَطْوَارًا ﴿١١﴾ أَلَمْ تَرَ كَيْفَ خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَوَاتٍ طِبَاقًا ﴿١٢﴾ وَجَعَلَ الْقَمَرَ فِيهِنَّ نُورًا وَجَعَلَ الشَّمْسَ سِرَاجًا ﴿١٣﴾ وَاللَّهُ أَنْبَتَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ نَبَاتًا ﴿١٤﴾ ثُمَّ يُعِيدْكُمْ فِيهَا وَيُخْرِجْكُمْ إِخْرَاجًا ﴿١٥﴾ وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ بِسَاطًا ﴿١٦﴾ لِتَسْلُكُوا مِنْهَا سُبُلًا فِجَاجًا ﴿١٧﴾

5. Akasema: Ee Mola Wangu Mlezi! Hakika mimi nimewaita watu wangu usiku na mchana,

6. Lakini wito wangu haukuwazidishia wao ila kukimbia.

¹ Ibn Shihab 1:93. Angalia As-Sahihain cha Al-Baani na. 1908.

7. Na hakika mimi kila nilipowaita ili Upate Kuwaghufiria, waliziba masikio yao kwa vidole vyao, na wakafunika nguo zao, na wakakamia, na wakatakabari vikubwa mno!

8. Tena niliwaita kwa uwazi,

9. Kisha nikawatangazia kwa kelele, tena nikasema nao kwa siri.

10. Nikasema: Ombeni msamaha kwa Mola Wenu Mlezi; hakika Yeye ni Mwingi wa Kusamehe.

11. Atakuleteeni mvua inyeshe mfululizo.

12. Na Atakupeni mali na wana, na Atakupeni bustani na Atakufanyieni mito.

13. Mna nini hamueki heshima ya Mwenyezi Mungu?

14. Na hali Yeye Kakuumbeni hali baada ya hali?

15. Kwani hamuoni jinsi Mwenyezi Mungu Alivyoziumba mbingu saba kwa matabaka?

16. Na Akaufanya mwezi ndani yake uwe nuru, na Akalifanya jua kuwa taa?

17. Na Mwenyezi Mungu Amekuotesheni katika ardhi kama mimea.

18. Kisha Atakurudsheni humo na Atakutoeni tena.

19. Na Mwenyezi Mungu Amekukunjulieni ardhi kama busati.

20. Ili mtembee humo katika njia zilizo pana.

Malalamiko ya Nuhu عليه السلام na Vitimbi vya Watu Wake

Allah تعالیٰ Anadhukuru kuhusu mja na Mjumbe Wake, Nuhu عليه السلام, na kuwa alimlalamikia Mola Wake kuhusu majibu aliyopewa na watu wake, na uvumilivu aliouonesha kwao kwa kipindi kirefu, ambacho ni miaka mia tisa na khamsini. Alilalamika kutokana na kuwaeleza na kuwafafanulia mambo na kuwalingania katika uongofu na njia iliyonyooka. Hivyo Nuhu عليه السلام, akasema,

رَبِّ إِنِّي دَعَوْتُ قَوْمِي لَيْلًا وَنَهَارًا ﴿٦١﴾

“Ee Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimewalingania watu wangu usiku na mchana.”

Maana yake: Sikuacha kuwalingania usiku na mchana, nikitekeleza amri Yako na nikikutii Wewe!

فَلَمْ يَزِدْهُمْ دُعَاؤِي إِلَّا فِرَارًا ﴿٦٢﴾

“Lakini wito wangu haukuwazidisha ila kukimbia.”

Maana yake: ‘Nilivyozidi kuwalingania kuja katika ukweli, ndivyo walivyozidi kuukimbia na kuuepuka.’

وَإِنِّي كُلَّمَا دَعَوْتُهُمْ لِتَغْفِرَ لَهُمْ جَعَلُوا أَصْبَعَهُمْ فِي آذَانِهِمْ وَأَسْتَغْشَوْا ثِيَابَهُمْ ﴿٦٣﴾

“Na hakika mimi kila nilipowaita ili Upate Kuwaghufiria, waliziba masikio yao kwa vidole vyao, na wakajifunika nguo zao.”

Maana yake: Waliziba masikio yao ili wasisikie wito wangu. Haya ni sawa na yale Allah تعالی Aliyoyazungumzia kuhusu makafiri wa Kikurayshi.

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَسْمَعُوا هَذَا الْقُرْآنَ وَالْغَوْا فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٦٤﴾

“Na waliokufuru walisema: Msiisikilize Qur’ani hii, na timueni zogo, huenda mkashinda.” (41:26)

وَأَسْتَغْشَوْا ثِيَابَهُمْ ﴿٦٥﴾

“...na wakajifunika nguo zao!...”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Walijificha ili asiweze kuwatambua.” Said bin Jubair na Suddi walisema, “Walifunika vichwa vyao ili wasisikie alichokuwa akisema.”

وَأَصْرُوا ﴿٦٦﴾

“...na wakakamia...” Maana yake: Waliendelea na waliyokuwa wakiyafanya, wakimshirikisha Allah تعالی na kufanya ukafiri mkubwa na kuwatisha.

وَأَسْتَكْبَرُوا اسْتِكْبَارًا ﴿٦٧﴾

“...na wakatakabari vikubwa mno.”

Maana yake: Wakiupa mgongo ukweli na kujisalimisha kwayo.

ثُمَّ إِنِّي دَعَوْتُهُمْ جِهَارًا ﴿١٤﴾

“Tena niliwaita kwa uwazi.” Maana yake: Wazi miongoni mwa watu.

ثُمَّ إِنِّي أَعْلَنْتُ لَهُمْ

“Kisha nikawatangazia kwa kelele...” Maana yake: Kwa kujadiliana nao. Hivyo alijaribu njia mbalimbali za *Daawah* ili afahamike vizuri.

وَأَسْرَرْتُ لَهُمْ إِسْرَارًا ﴿١٥﴾

“...tena nikasema nao kwa siri.” Maana yake: Katika kujadiliana nao, alitumia mbinu nyingi za *da'awa* (kuwaita) ili afahamike vizuri kwao.

Nabii Nuh عليه السلام Alichosema Alipowalingania Watu Wake kwa Allah تعالى

فَقُلْتُ اسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ إِنَّهُ كَانَ غَفَّارًا ﴿١٦﴾

“Nikasema: Ombeni msamaha kwa Mola Wenu Mlezi; hakika Yeye ni Mwingi wa Kusamehe.”

Maana yake: ‘Rejeeni Kwake na myape mgongo mliyokuwa mkiyafanya. Ombeni toba haraka, kwani kwa hakika, Allah تعالى ni Mpokeaji wa Toba hata kama madhambi ni makubwa, hata kama ni ukafiri na ushirikina. Hivyo akasema,

فَقُلْتُ اسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ إِنَّهُ كَانَ غَفَّارًا ﴿١٦﴾ يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُمْ مِدْرَارًا ﴿١٧﴾

“Nikasema: Ombeni msamaha kwa Mola wenu Mlezi; hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe. Atakuleteni mvua inyeshe mfululizo.”

Maana yake: Mvua mfululizo. Hivyo inapendekezwa kusoma sura hii wakati wa Sala ya kuomba mvua kutokana na aya hii. Hili limepokelewa kutoka kwa Kamanda wa Waumini, Umar bin Al Khattab رضي الله عنه. Alipanda juu ya Minbar kusali Sala ya kuomba mvua, na hakufanya zaidi ya kumuomba Allah تعالى maghufira na kusoma Ayat zinazotaja kutaka Maghufira kwa Allah تعالى. Miongoni mwa aya hizo ni:-

فَقُلْتُ اسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ إِنَّهُ كَانَ غَفَّارًا ﴿٦٠﴾ يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُمْ مِدْرَارًا ﴿٦١﴾

“Nikasema: Ombeni msamaha kwa Mola Wenu Mlezi; hakika Yeye ni Mwingi wa Kusamehe. Atakuleteni mvua inyeshe mfululizo.”

Kisha Umar رضي الله عنه alisema, “Kwa hakika, ‘Nimeitaka mvua kwa mchanganyiko wa mawingu yanayoteremsha mvua.’ Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine walisema, “Midrar maana yake mvua inayofuatiwa na nyingine.” Kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

وَيُمَدِّدْكُمْ بِأَمْوَالٍ وَبَيْنَ وَبَيْنَ وَبِجَعَلْ لَكُمْ جَنَّاتٍ وَبِجَعَلْ لَكُمْ أَنْهَارًا ﴿٦٢﴾

“Na Atakupeni mali na wana, na Atakupeni bustani na Atakufanyieni mito.”

Maana yake: Unapotubia kwa Allah تعالى، omba msamaha na mtii Yeye. Atakuongezea riziki yako na Atakuteremshia maji kutoka katika mbingu zilizobarikiwa. Atasababisha neema katika ardhi na mimea kuongezeka. Atakuongezea wanyama na Atakuongezea mali na watoto. Hii ina maana Atakupa mali zaidi, watoto zaidi na bustani zenye matunda anuwai. Atasababisha mito kupita katika hizo bustani. Huu ni wito wenye kushajiisha. Kisha akawalingania kwa wito wa kuhofisha. Akasema،

مَا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا ﴿٦٣﴾

“Mna nini hamweki heshima ya Mwenyezi Mungu?”

Maana yake: Ukuu wa Enzi. Hii ni tafsiri ya Ibn Abbas, Mujahid na Adh-Dhahhak رضي الله عنهم.¹ Na Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, “Nyie nyote hamumtukuzi Allah تعالى kama inavyostahili kutukuzwa. Maana, hamuogopi adhabu Yake na kisasi Chake.”²

وَقَدْ خَلَقَكُمْ أَطْوَارًا ﴿٦٤﴾

“Na hali Yeye Kakuumbeni hali baada ya hali?”

Imesemwa kuwa hii ina maana kutoka tone la manii, kisha pande la damu, kisha pande la nyama. Ibn Abbas, Ikrimah, Qatadah, Yahya bin Rafi, As-Suddi na Ibn Zaid رضي الله عنهم، wote wamesema hivyo. Kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

¹ At-Tabari 23:634.

² At-Tabari 23:634.

أَلَمْ تَرَوْا كَيْفَ خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَوَاتٍ طِبَاقًا ﴿٥﴾

“Kwani hamuoni jinsi Mwenyezi Mungu Alivyoziumba mbingu saba kwa matabaka?”

Maana yake: Moja juu ya nyengine. Je hili nalo linahitaji kuhadithiwa au ni masuala ambayo yanafahamika kwa kutumia milango ya fahamu ambayo inajua mizunguuko ya maumbile na kupatwa kwa jua?

Kusudio hapa ni kuwa Allah تعالى:

خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَوَاتٍ طِبَاقًا ﴿٥﴾ وَجَعَلَ الْقَمَرَ فِيهِنَّ نُورًا وَجَعَلَ الشَّمْسَ سِرَاجًا ﴿٦﴾

“...Alivyoziumba mbingu saba kwa matabaka? Na Akaufanya mwezi ndani yake uwe nuru, na Akalifanya jua kuwa taa?”

Maana yake: Alifanya tofauti kati ya viwili hivyo (jua na mwezi) kwa kuzingatia kuangaza kwao Alijaalia sifa ya upekee ili mchana na usiku ufahamike kwa mawio na machweo ya jua. Aidha Aliujaalia mwezi uwe na vituo na mashukio ya nyota na Akafanya nuru yake iwe tofauti, ili wakati mwingine izidi kufikia ukomo, kisha inapungua mpaka inapotea. Hii inaonesha hisabu ya miezi na miaka.

Hivi ni kama Allah تعالى Alivyoosema,

هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَاءً وَالْقَمَرَ نُورًا وَقَدَرَهُ مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ

وَالْحِسَابَ ۗ مَا خَلَقَ اللَّهُ ذَلِكَ إِلَّا بِالْحَقِّ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٥﴾

“Yeye Ndiye Aliyelijaalia jua kuwa na mwangaza, na mwezi ukawa na nuru, na Akaupimia vituo ili mjue idadi ya miaka na hisabu. Mwenyezi Mungu Hakuviumba hivyo ila kwa Haki. Anazipambanua Ishara kwa watu wanaojua.” (10:5)

Kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

وَاللَّهُ أَنْبَتَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ نَبَاتًا ﴿٥﴾

“Na Mwenyezi Mungu Amekuotesheni katika ardhi kama mimea.”

ثُمَّ يُعِيدُكُمْ فِيهَا

“Kisha Atakurudisheni humo.” (71:18)

Maana yake: Mtakapo kufa.

وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ بِسَاطًا ﴿١٨﴾

“Na Mwenyezi Mungu Amekukunjulieni ardhi kama busati.”

Maana yake: Siku ya Kiyama Atawarejesha tena kama Alivyowaumba mwanzo.

وَيُخْرِجُكُمْ إِخْرَاجًا ﴿١٩﴾

“..na Atakutoeni tena.”

Maana yake: Aliwakunjulia, Akaisawazisha Akaifanya makazi na Akaiimarisha kwa milima imara na mirefu.

لَتَسْلُكُوا مِنْهَا سُبُلًا فِجَاجًا ﴿٢٠﴾

“Ili mtembee humo katika njia zilizokuwa pana.”

Maana yake: Aliiumba ardhi ili muweze kuishi humo, na kusafiri popote mpendapo, kutoka pande na maeneo tofauti. Haya yote ni katika ambayo Nuhu عليه السلام aliwaambia watu wake juu ya Nguvu za Allah تعالى kwa Uumbaji wa mbingu na ardhi, na neema Alizowa jaalia wao miongoni mwa manufaa ya mbinguni na duniani. Aya inaonesha kuwa Allah تعالى Ndiye Muumba Aliyeumba mbingu kama jengo na ardhi kama kitanda na Akakuza vyakula kwa ajili ya viumbe vyake. Kwa hiyo ni lazima kumuabudu Yeye Pekee na kumkubali kuwa ni Mungu Mmoja. Hapana apasaye kuabudiwa na kupwekeshwa wala asishirikishwe na chochote, kwa sababu Hana aliye sawa na Yeye, awe mkuu, mshindani, rafiki, mwana, waziri au mshauri, bali Yeye Ana Hadhi ya juu, na Mkuu wa viumbe wote.

* * *

قَالَ نُوحٌ رَبِّ إِنَّهُمْ عَصَوْنِي وَأَتَّبَعُوا مَالَهُ
 وَمَنْ لَمْ يَزِدْهُ مَالَهُ وَّوَلَدَهُ إِلَّا خَسَارًا ﴿٢١﴾
 وَمَكَرُوا مَكْرًا كَبِيرًا ﴿٢٢﴾
 وَقَالُوا لَا تَنْزُلْ ۖ الْهَاتِكُمْ وَلَا تَنْزُلْ ۖ وَدَا وَلَا سَوَاعَا وَلَا
 يَغُوتَ وَيَعُوقَ وَنَسْرًا ﴿٢٣﴾ وَقَدْ أَضَلُّوا كَثِيرًا ۗ وَلَا تَرِدْ
 الظَّالِمِينَ إِلَّا ضَلَالًا ﴿٢٤﴾ مِمَّا خَطَبْتَهُمْ أُعْرِقُوا فَأُدْخِلُوا
 نَارًا فَلَمْ يَجِدُوا لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْصَارًا ﴿٢٥﴾ وَقَالَ نُوحٌ
 رَبِّ لَا تَذَرْنِي عَلَى الْأَرْضِ مِنَ الْكَافِرِينَ دَيَّارًا ﴿٢٦﴾ إِنَّكَ
 إِن تَذَرَهُمْ يُضِلُّوا عِبَادَكَ وَلَا يَلِدُوا إِلَّا فَاجِرًا كَفَّارًا
 ﴿٢٧﴾ رَبِّ آغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِمَنْ دَخَلَ بَيْتِيَ مُؤْمِنًا
 وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَلَا تَرِدِ الظَّالِمِينَ إِلَّا تَبَارًا ﴿٢٨﴾

قَالَ نُوحٌ رَبِّ إِنَّهُمْ عَصَوْنِي وَأَتَّبَعُوا
 مَنْ لَمْ يَزِدْهُ مَالَهُ وَّوَلَدَهُ إِلَّا خَسَارًا
 ﴿٢١﴾ وَمَكَرُوا مَكْرًا كَبِيرًا ﴿٢٢﴾
 وَقَالُوا لَا تَنْزُلْ ۖ الْهَاتِكُمْ وَلَا تَنْزُلْ ۖ
 وَدَا وَلَا سَوَاعَا وَلَا يَغُوتَ وَيَعُوقَ
 وَنَسْرًا ﴿٢٣﴾ وَقَدْ أَضَلُّوا كَثِيرًا ۗ وَلَا
 تَرِدِ الظَّالِمِينَ إِلَّا ضَلَالًا ﴿٢٤﴾

21. Nuhu akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika hao wameniasi, na wamemfuata yule ambaye mali yake na wanawe hawakumzidishia ila khasara.

22. Na wakapanga vitimbi vikubwa.

23. Na wakasema: Msiwaache miungu yenu, wala msimuache Wadda wala Suwaa' wala Yaghutha, wala Yau'qa, wala Nasra.

24. Na hao walikwisha wapoteza wengi, wala usiwazidishie walio dhulumu ila kupotea.

Nuhu عليه السلام Anamshitakia Mola Wake Kutokana na Majibu.

Nuhu عليه السلام alimgeukia Allah تعالى kumueleza – Ajuaye yote na hapana limpatalo – kuwa aliwafikishia ulinganio ulio wazi kama tulivyotaja awali, na wito uliyotumia njia anuwai. Aliwalingania wao baadhi ya wakati kwa kuwapa mawaidha mazuri na wakati mwingine mawaidha ya kuhofisha. Pamoja na haya yote walimuasi, walimpinga, walimkataa na wakawafuata wanadamu. Walikana Amri za Allah تعالى, na kujifaharisha kwa mali na watoto. Hata hivyo,

vitu hivi (manufaa ya kidunia) vilikuwa ni kuwapa muda tu sio takrima. Hivyo Allah تعالى Amesema,

وَاتَّبِعُوا مَنْ لَمْ يَزِدْهُ مَالَهُ وَوَلَدَهُ إِلَّا خَسَارًا ﴿٢١﴾

“...na wamemfuata yule ambaye mali yake na wanawe hawakumzidishia ila khasara.”

Maana ya Kauli ya Allah تعالى,

وَمَكْرُوا مَكْرًا كُبْرًا ﴿٢٢﴾

“Na wakapanga vitimbi vikubwa.”

Ni kuwa walipanga njama zilizoshindwa kwa wafuasi wao wakiwafanyia hila wakiamini kuwa walikuwa wakifuata ukweli na muongozo sahihi. Hivi ni kama watakavyowaambia Siku ya Kiyama,

بَلْ مَكْرُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ إِذْ تَأْمُرُونَنَا أَنْ نَكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُ أَندَادًا ﴿٢٣﴾

“...Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana, mlipokuwa mkituamrisha tumkufuru Mwenyezi Mungu, na tumfanyie washirika...” (34:33)

Kwa kuzingatia hilo ndio maana amesema hivyo hapa.

Kilicho Yasibu Masanamu ya Watu wa Nuh عليه السلام.

وَمَكْرُوا مَكْرًا كُبْرًا ﴿٢٤﴾ وَقَالُوا لَا تَذَرُنَّ آلِهَتَكُمْ وَلَا تَذَرُنَّ وَدًّا وَلَا سُوَاعًا وَلَا

يَغُوثَ وَيَعُوقَ وَنَسْرًا ﴿٢٥﴾

“Na wakapanga vitimbi vikubwa. Na wakasema: Msiwaache miungu yenu, wala msimuache Wadda wala Suwaa’ wala Yaghutha, wala Yau’qa, wala Nasra.”

Haya ni majina ya masanamu waliyokuwa wakiyaabudu na kuacha kumuamudu Allah تعالى.

Bukhari kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema: “Masanamu yaliyokuwepo katika kaumu Nuhu عليه السلام baadaye yakawa kwa Waarabu. Ama Sanamu la *Wadd*, lilikuwa sanamu la watu wa Kalb katika eneo la Dawmat Al-Jandal. *Suwa* alikuwa sanamu wa watu wa Hudhayli. *Yaghutha* alikuwa sanamu la watu wa Murad, kisha watu wa bani Ghutayfi katika Al-Juruf katika eneo la Saba. *Yauq* alikuwa sanamu la watu wa Hamdan. *Nasr* alikuwa sanamu la watu wa Himyar kwa familia ya Dhu Kala. Masanamu hayo yote yalipewa majina ya watu, wamo miongoni mwa watu wa Nuhu عليه السلام. Watu hao walipofariki dunia, shetani aliwatia msukumo watu wa Nuhu عليه السلام kujenga sanamu kwa heshima yao katika eneo walilokuwa wakitumia kukutaniana kuyapa majina hayo masanamu. Kwa hiyo walifanya kama walivyoshauriwa na shetani, lakini masanamu hayo hayakuabudiwa mpaka watu walipoyajenga walipofariki dunia na habari zao kusahaulika. Kisha hayo masanamu yalianza kuabudiwa baadaye.”¹

Maelezo sawa na haya yalinukuliwa kutoka kwa Ikrimah, Adh-Dhahhak, Qatadah na Ibn Ishaq. Ali bin Abi Talhah alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Haya ni masanamu yakiabudiwa zama za Nuh عليه السلام.”² Ibn Jarir رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Muhammad bin Qays kuwa alisema kuhusu *Yaghuth*, *Yauq* na *Nasr*, “Walikuwa watu wema kati ya zama za Adam عليه السلام na Nuh عليه السلام, na walikuwa na wafuasi waliokuwa wakishikamana na muongozo wao. Na wakati walipokufa, wafuasi wao waliokuwa wakiwafuata walisema, “Endapo tutatengeneza sura zao, itaongeza hamu yetu ya kufanya ibada tunapo wakumbuka.’ Hivyo walitengeneza taswira zao. Kisha hao watu walipofariki dunia na wengine wakaja baada yao, Iblis aliwaendea na kusema, “Watangulizi wenu walikuwa wakiyaabudu masanamu haya na walipata mvua kwa kuabudu masanamu ya watu hawa.’ Hivyo, wakayaabudu.”

¹ *Fat’hul Al-Bari* 8:535.

² *At-Tabari* 23:640.

Maapizo ya Nuh عليه السلام kwa Watu wake, na Kuwaomba Waliomuamini Yeye.

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَقَدْ أَضَلُّوا كَثِيرًا

“Na hao walikwisha wapoteza wengi.”

Maana yake: Kwa masanamu waliyoabudia, waliwapoteza watu wengi. Kwa hakika, ibada ya masanamu iliendelea kwa karne nyingi mpaka zama zetu leo, miongoni mwa Waarabu na Mataifa mbalimbali.

Na Mtume Ibrahim عليه السلام alisema katika dua yake.

وَأَجُنَّبُنِي وَبَنِيَّ أَنْ نَعْبُدَ الْأَصْنَامَ ﴿٣٥﴾ رَبِّ إِنِّي أَخْلَلْتُ كَثِيرًا مِنَ النَّاسِ

“...na Uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu. Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika hayo yamewapoteza watu wengi” (14:35-36)

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَلَا تَزِدِ الظَّالِمِينَ إِلَّا ضَلَالًا ﴿٣٦﴾

“...wala usiwazidishie waliodhulumu ila kupotea.”

Hii ni dua ya Nuhu عليه السلام dhidi ya watu wake kutokana na kuasi kwao, ukafiri na ukaidi. Hivi ni kama Musa عليه السلام alivyomuapiza Fir'aun na wasaidizi wake.

Katika kauli yake,

رَبَّنَا أَطْمَسَ عَلَىٰ أَمْوَالِهِمْ وَأَشَدُّدَ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُوا حَتَّىٰ يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٨٨﴾

“Mola wetu Mlezi! Yafutilie mbali mali yao na zifunge nyoyo zao, wasiamini mpaka waione adhabu chungu.” (10:88)

Kwa hakika Allah تعالى Alijibu dua za Mitume wake hao wawili kuhusu upingaji wa watu wao. Aligharikisha mataifa yao kutokana na kukana yaliyoletwa na Mtume عليه السلام.

مِمَّا خَطِيئَتِهِمْ أُغْرِقُوا فَأَدْخَلُوا نَارًا فَلَمْ يَجِدُوا لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْصَارًا ﴿٢٥﴾ وَقَالَ
 نُوحٌ رَبِّ لَا تَذَرْنِي عَلَى الْأَرْضِ مِنَ الْكَافِرِينَ دَيَّارًا ﴿٢٦﴾ إِنَّكَ إِنْ تَذَرَهُمْ يُضِلُّوا عِبَادَكَ
 وَلَا يَلِدُوا إِلَّا فَاجِرًا كَفَّارًا ﴿٢٧﴾ رَبِّ آغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِمَنْ دَخَلَ بَيْتِيَ مُؤْمِنًا
 وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَلَا تَزِدِ الظَّالِمِينَ إِلَّا تَبَارًا ﴿٢٨﴾

25. Kwa sababu ya makosa yao waligharikishwa kisha wakaingizwa Motoni, wala hawakuwapata wa kuwanusuru badala ya Mwenyezi Mungu.

26. Na Nuh'u akasema: Mola Wangu Mlezi! Usimuache juu ya ardhi mkaazi wake yeyote katika makafiri!

27. Hakika ukiwaacha watawapoteza waja Wako, wala wao hawatazaa ila waovu makafiri.

28. Mola wangu Mlezi! Nighufirie mimi na wazazi wangu, na kila aliyeingia nyumbani mwangu kuwa ni mwenye kuamini, na Waumini wote wanaume, na wanawake. Na wala Usiwazidishie waliodhulumu ila kupotea.

Allah تعالى Amesema,

مِمَّا خَطِيئَتِهِمْ

“Basi kwa ajili ya makosa yao...”

Pia imesemwa kama,

(خَطَايَاهُمْ)

(Khatwaayaahum)

أُغْرِقُوا

“...Waligharikishwa...”

Maana yake: Kutokana na wingi wa madhambi, uasi, kubobea katika ukafiri na kuwapinga Mitume wao.

أُغْرِقُوا فَأَدْخِلُوا نَارًا

“...waligharikishwa, wakaingizwa Motoni...”

Maana yake: Watachukuliwa kutoka kwenye mafuriko ya bahari kwenda kwenye joto la Moto.

فَلَمْ يَجِدُوا لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْصَارًا ﴿٦٦﴾

“...wala hawakuwapata wa kuwanusuru badala ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Hawatakuwa na msaidizi au muokozi atakayewaokoa na adhabu ya Allah تعالى. Kauli hii ni sawa na maneno ya Allah تعالى,

لَا عَاصِمَ الْيَوْمَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ إِلَّا مَنْ رَحِمَ ۗ

“Leo hapana wa kulindwa na Amri ya Mwenyezi Mungu ila aliye mrehemu mwenyewe.” (11:43)

وَقَالَ نُوحٌ رَبِّ لَا تَذَرْ عَلَيَّ الْأَرْضَ مِنَ الْكَافِرِينَ دَيَّارًا ﴿٦٧﴾

“Na Nuh’u akasema: Mola wangu Mlezi! Usimuache juu ya ardhi mkaazi wake yeyote katika makafiri!”

Maana yake: Usimuache yeyote kati yao juu ya uso wa ardhi, wala mtu mmoja. Hii ni njia ya mazungumzo inayotilia mkazo ukanushaji. Adh-Dhahhak alisema, “Dayyar ina maana moja” As-Suddi alisema, ‘Dayyar ni yule anayekaa nyumbani.’ Hivyo Allah تعالى Alijibu maombi yake na Akawaangamiza wote waliokuwa juu ya uso wa ardhi ambao walikuwa makafiri. Allah تعالى Alimuangamiza pia mtoto wa Nuh عليه السلام wa kuzaa, ambaye alijitenga na baba yake (Nuhu عليه السلام). Yeye (Mtoto wa Nuh عليه السلام) alisema,

سَأَوَىٰ إِلَىٰ جَبَلٍ يَعْصِمُنِي مِنَ الْمَاءِ ۚ قَالَ لَا عَاصِمَ الْيَوْمَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ إِلَّا مَنْ رَحِمَ ۗ

وَحَالَ بَيْنَهُمَا الْمَوْجُ فَكَانَ مِنَ الْمُغْرَقِينَ ﴿٦٨﴾

“Nitakimbilia mlimani unilinde na maji. (Nuh) akasema: Leo hapana wa kulindwa na Amri ya Mwenyezi Mungu ila aliyemrehemu Mwenyewe. Na wimbi likawatenganisha, akawa katika walio zama.” (11:43)

Allah تعالى Aliwaokoa watu wa safina waliomuamini Nuh عليه السلام, na ni wale ambao Allah تعالى Alimuamrisha Nuh عليه السلام awachukue. Allah تعالى Amesema, Yaani, endapo utamuacha mmoja wao watawapotosha waja wako.' Hii inahusu wale utakaowaumba baada yao.

وَلَا يَلِدُوا إِلَّا فَاجِرًا كَفَّارًا ﴿٢٧﴾

“Wala wao hawatazaa ila waovu makafiri.” Maana yake: Waovu katika matendo yao na wanakanusha katika mioyo yao. Yeye (Nuhu عليه السلام) alisema kutokana na aliyoyajua juu yao kwani alikuwa nao kwa miaka mia tisa na khamsini. Kisha akasema,

إِنَّكَ إِن تَذَرَهُمْ يُضِلُّوا عِبَادَكَ

“Hakika Ukiwaacha watawapoteza waja wako...”

رَبِّ أَغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِمَن دَخَلَ بَيْتِيَ مُؤْمِنًا

“Nighufirie mimi na wazazi wangu, na kila aliyeingia nyumbani mwangu kuwa ni mwenye kuamini...”

Adh-Dhahhak alisema, “Hii ina maana, Masjid yangu.’ Hata hivyo hapana ubaya kuelewa Ayah kwa maana iliyo wazi, ambayo itakuwa (Nuh عليه السلام) aliomba kwa kila mtu aliyeingia nyumbani kwake ambaye ni muumini. Kisha alisema,

وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ

“...na Waumini wote wanaume, na Waumini wanawake.” Aliwaombea wote, waumini wanawake na wanaume, na hiyo iliwajumuisha waliokuwa hai na waliokufa. Kwa sababu hii, imependekesha kuomba kama hivi, kwa kufuata mfano wa Nuhu عليه السلام, na yale yaliyopokelewa katika hadithi na dua zilizofaradhiwa ambazo ni maarufu. Kisha alisema,

وَلَا تَزِدِ الظَّالِمِينَ إِلَّا تَبَارًا ﴿٢٨﴾

“Na wala Usiwazidishie walio dhulumu ila kupotea.” As-Suddi alisema, “Lakini uharibifu” Mujahid alisema “Lakini hasara.” Ina maana katika maisha ya duniani na akhera. Huu ni mwisho wa Tafsiri ya Surat Nuhu na Shukrani na Sifa Zinamstahiki Allah تعالى .

Tafsiri ya Suratul Jinn

Sura ya 72

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْجِنِّ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قُلْ أُوحِيَ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْتَمَعَ نَفَرٌ مِّنَ الْجِنِّ فَقَالُوا إِنَّا سَمِعْنَا قُرْءَانًا عَجَبًا ﴿١﴾ يَهْدِي إِلَى الرُّشْدِ فَآمَنَّا بِهِ ۗ وَلَنْ نُشْرِكَ بِرَبِّنَا أَحَدًا ﴿٢﴾ وَأَنَّهُ تَعَلَّى جَدُّ رَبِّنَا مَا اتَّخَذَ صَاحِبَةً وَلَا وَلَدًا ﴿٣﴾ وَأَنَّهُ كَانَ يَقُولُ سَفِيهُنَا عَلَى اللَّهِ شَطَطًا ﴿٤﴾ وَأَنَا ظَنَنَّا أَن لَّن نَقُولَ الْإِنسُ وَالْجِنُّ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ﴿٥﴾ وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِّنَ الْإِنسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِّنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا ﴿٦﴾ وَأَنَا لَمَسْنَا السَّمَاءَ فَوَجَدْنَهَا مَلْفَتٌ حَرَسًا شَدِيدًا وَشُهُبًا ﴿٧﴾ وَأَنَا كُنَّا نَقْعُدُ مِنهَا مَقْعِدًا لِلسَّمْعِ ۖ فَمِنَ اسْتَمْعِ الْآنَ يَنجِدُ لَهُمْ شُهَابًا رَّصَدًا ﴿٨﴾ وَأَنَا لَا تَدْرِي أَشْرُّ أَرِيدَ بِمَن فِي الْأَرْضِ أَم أَرَادَ بِهِمْ رَبُّهُمْ رَشَدًا ﴿٩﴾

قُلْ أُوحِيَ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْتَمَعَ نَفَرٌ مِّنَ الْجِنِّ فَقَالُوا إِنَّا سَمِعْنَا قُرْءَانًا عَجَبًا ﴿١﴾ يَهْدِي إِلَى الرُّشْدِ فَآمَنَّا بِهِ ۗ وَلَنْ نُشْرِكَ بِرَبِّنَا أَحَدًا ﴿٢﴾ وَأَنَّهُ تَعَلَّى جَدُّ رَبِّنَا مَا اتَّخَذَ صَاحِبَةً وَلَا وَلَدًا ﴿٣﴾ وَأَنَّهُ كَانَ يَقُولُ سَفِيهُنَا عَلَى اللَّهِ شَطَطًا ﴿٤﴾ وَأَنَا ظَنَنَّا أَن لَّن نَقُولَ الْإِنسُ وَالْجِنُّ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ﴿٥﴾ وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِّنَ الْإِنسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِّنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا ﴿٦﴾ وَأَنَا لَمَسْنَا السَّمَاءَ فَوَجَدْنَهَا مَلْفَتٌ حَرَسًا شَدِيدًا وَشُهُبًا ﴿٧﴾ وَأَنَا كُنَّا نَقْعُدُ مِنهَا مَقْعِدًا لِلسَّمْعِ ۖ فَمِنَ اسْتَمْعِ الْآنَ يَنجِدُ لَهُمْ شُهَابًا رَّصَدًا ﴿٨﴾ وَأَنَا لَا تَدْرِي أَشْرُّ أَرِيدَ بِمَن فِي الْأَرْضِ أَم أَرَادَ بِهِمْ رَبُّهُمْ رَشَدًا ﴿٩﴾

1. Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikiliza, na likasema: Hakika sisi tumeisikia Qur'ani ya ajabu!

2. Inaongoza kwenye uwongofu, kwa hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha yeyote na Mola wetu Mlezi.

3. Na kwa hakika Utukufu wa Mola Wetu Mlezi Umetukuka kabisa; hana mke wala mwana.

4. Na kwa hakika wapumbavu miongoni mwetu walikuwa wakisema uwongo uliopindukia mipaka juu ya Mwenyezi Mungu.

5. Nasi tulidhani kuwa watu na majini hawamzulii uwongo Mwenyezi Mungu.

6. Na hakika walikuwako wanaume katika watu waliokuwa wakitafuta kujikinga kwa wanaume wa kijini; kwa hivyo wakawazidisha madhambi.

7. Na kwa hakika wao walidhani, kama mlivyodhani nyinyi, ya kuwa Mwenyezi Mungu hatamleta Mtume.

Majini Kusikiliza Qur'ani na Kuiamini Kwao

Allah تعالیٰ Anasema Akimuamuru Mtume wake ﷺ kuwapa habari watu wake kuwa majini walisikiliza Qur'ani wakaiamini na kuisadiki na wakaongozeka kwa sababu ya Qur'an. Allah تعالیٰ Akasema:

قُلْ أَوْحَىٰ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْتَمَعَ نَفَرٌ مِّنَ الْجِنِّ فَقَالُوا إِنَّا سَمِعْنَا قُرْءَانًا عَجَبًا ﴿١﴾ يَهْدِي إِلَى
الرُّشْدِ

“Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikiliza, na likasema: Hakika sisi tumeisikia Qur'ani ya ajabu!, Inaongoza kwenye uwongofu.” (72:1-2)

Maana yake: Kwenye usawa na uokovu

فَقَامْنَا بِهِ ^ع وَلَكِنْ نُّشْرِكُ بِرَبِّنَا أَحَدًا ﴿٢﴾

“kwa hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha yeyote na Mola Wetu Mlezi.” (72:2).

Mnasaba huu unashabihiana na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

وَإِذْ صَرَفْنَا إِلَيْكَ نَفَرًا مِّنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ

“Na wakati Tulipowaleta kundi la majini kuja kwako kusikiliza Qur’ani.” (46:29)

Tumeshabainisha Hadithi zilizoelezea suala hilo, kwa namna inayotosha hakuna haja ya kuirudia tena hapa.¹ Na Kauli Yake تعالى

وَأَنَّهُ تَعَلَّى جَدُّ رَبِّنَا

“Na kwa hakika Utukufu wa Mola Wetu.” (72:3)

Ali bin Abi Twalhah رضي الله عنهما amesema toka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما katika Kauli Yake تعالى

جَدُّ رَبِّنَا

“Utukufu wa Mola wetu”. (72:3)

Maana yake: Utendaji Wake, Amri na Kudura Yake,² Adh-Dhahaak amesema: toka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما: *Jaddullaahi* Utukufu wa Allah تعالى: Fadhila, Kudura na Neema Zake kwa viumbe wake. Imepokewa toka kwa Mujaahid na Ikrimah: Utukufu wa mola Wetu, Qatadah amesema: Umetukuka Utukufu Wake, ukuu Wake na Amri Yake. Sudi amesema: Imetukuka Amri ya Mola Wetu, na kutoka kwa Abi Dardaai, Mujahid na vilevile Ibn Juraij: Umetukuka Utajo Wake,

Majini Yanakiri Kwamba Allah تعالى Hana Mke Wala Watoto

Kauli Yake تعالى:

مَا آتَخَذَ صَنِيعَةً وَلَا وَلَدًا ﴿٢٤﴾

“Hana mke wala mwana.” Maana yake: Ametakasika Hana mke wala watoto. Maana yake: Majini walisema: Ametakasika Mola Mtukufu, wakati waliposilimu wakaiamini Qur’ani, walikiri Kutakasika Kwake Allah تعالى kuwa Hana mke na mtoto, kisha wakasema:

وَأَنَّهُ كَانَ يَفُولُ سَفِيهًا عَلَى اللَّهِ شَطَطًا ﴿٢٤﴾

“Na kwa hakika wapumbavu miongoni mwetu walikuwa wakisema uwongo uliopindukia mipaka juu ya Mwenyezi Mungu.” (72:4)

¹ Angalia juzuu ya Tisa, *Tafsir ya Surat Al-Ahqaf* (46:29).

² At-Tabari 23:648.

Mujaahid, Ikrimah, Qatadah na Sudi,

سَفِيهُنَا

“Wapumbavu miongoni mwetu.” (72:4)

Wanakusudia Ibilisi.

شَطَطًا

“Uwongo uliopindukia mipaka.” (72:4)

Maana yake: Uovu. Na Ibn Zaid amesema: Maana yake: Dhuluma kubwa. Inawezekana kuwa muradi wa Kauli yao: (*safiihunaa*) kila aliyedai kuwa Allah تعالى Ana mke au mtoto. Na kwa ajili hii wamesema:

وَأَنَّهُ كَانَ يَاقُولُ سَفِيهُنَا

“Na kwa hakika wapumbavu miongoni mwetu walikuwa wakisema.” (72:4)

Maana yake: Kabla ya kusilimu kwake,

عَلَى اللَّهِ شَطَطًا

“Uongo uliopindukia mipaka juu ya Mwenyezi Mungu.” (72:4)

Maana yake: Batili na uongo. Na kwa ajili hii Amesema:

وَأَنَا ظَنَنْتَ أَن لَّنْ نَقُولَ الْإِنْسُ وَأَجْنُ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا

“Nasi tulidhani kuwa watu na majini hawamzulii uwongo Mwenyezi Mungu.” (72:5)

Maana yake: Hatukudhani kabisa kuwa wanadamu na majini watamsingizia Allah تعالى uongo katika kumnasibishia mke na watoto, basi tuliposikia hii Qur’ani na kuiamini, tulijua kuwa walikuwa wakimsingizia Allah تعالى katika hilo.

Sababu za Majini Kuasi ni Kutokana na Wanadamu Kutaka Kulingwa na Majini

Kauli Yake:

وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِّنَ الْإِنسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِّنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا ﴿٦﴾

“Na hakika walikuwako wanaume katika watu waliokuwa wakitafuta kujikinga kwa wanaume wa kijini; kwa hivyo wakawazidisha madhambi.” (72:6)

Tulikuwa tunaona kuwa sisi ni bora, kuliko watu, kwa kuwa wao walikuwa wakitutaka sisi uokovu kwetu wanapopita kwenye wangwa au mahali panapotisha katika nchi kavu na kwingine. Kama ilivyokuwa ada ya waarabu katika kipindi cha jahiliya walikuwa wakijikinga kwa mkubwa wa mahali hapo miongoni mwa majini, ili wasifikwe na kitu kitakachowadhuru wao. Kama ilivyokuwa mmoja wao anaingia mji wa adui zake, akijiweka katika ulinzi wa mtu mkubwa na dhima yake. Kwa hiyo majini walipoona kuwa watu wanajikinga kwao kutokana na hofu yao kwao, waliwazidishia hofu, uoga na mfazaiko hadi wakabakia na hofu kali zaidi na kuendelea kuwataka wao uokovu, kama alivyosema Qatadah:

فَزَادُوهُمْ رَهَقًا ﴿٦﴾

“Hivyo wakawazidisha madhambi.” (72:6)

“Maana yake: Dhambi, na majini wakazidisha jeuri juu yao.”¹

Thauri amesema: Kutoka kwa Mansuur kutoka kwa Ibrahimu,

فَزَادُوهُمْ رَهَقًا ﴿٦﴾

“Hivyo wakawazidisha madhambi.” (72:6)

Maana yake: Majini walizidisha jeuri.

Suddi amesema: Mtu alikuwa anatoka na familia yake kwenda sehemu anasema: Najikinga na bwana wa Jangwa hili katika majini wasinidhuru mimi, au mali yangu au watoto wangu au mifugo yangu, Qatadah anasema: Na anapowataka wao uokovu na wakaacha kuomba kwa Allah تعالی, majini huacha

¹ At-Tabari 23:655.

kuwapa maudhi. Ibi Abi Hatim amepokea toka kwa Ikrimah amesema: majini walikuwa wakiwaogopa watu, kama ambavyo watu walikuwa wakiwaogopa majini maradufu yake. Na ilikuwa watu wakipita jangwani majini hukimbia, na bwana wa kaumu husema: tunajilinda na bwana wa jangwa hili, na Jini atasema: tunawaona wanatuogopa kama sisi tunavyowaogopa wao, kwa hiyo watu wakajikurubisha kwa majini wakawatia upunguani na ukichaa. Kauli Yake,

وَأَنَّهُمْ كَانُوا رِجَالًا مِّنَ الْإِنسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِّنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا ﴿٦﴾

“Na hakika walikuwako wanaume katika watu waliokuwa wakitafuta kujikinga kwa wanaume wa kijini; kwa hivyo wakawazidisha madhambi.” (72:6).

Maana yake: Dhambi. Abul Aaliyah Ar Rabii na Zaid bin Aslam wamesema:

رَهَقًا ﴿٦﴾

“Madhambi.” (72:6).

Maana yake: Hofu. Na Mujahid amesema: Makafiri wakazidisha uasi. Kauli Yake:

وَأَنَّهُمْ ظَنُّوا كَمَا ظَنَنْتُمْ أَن لَّنْ يَبْعَثَ اللَّهُ أَحَدًا ﴿٦﴾

“Na kwa hakika wao walidhani, kama mlivyodhani nyinyi, ya kuwa Mwenyezi Mungu Hatamleta (Mtume) yeyote.” (72:6).

Maana yake: Allah تعالى Hatatuma baada ya muda huu Mtume yeyote, hilo amelisema Al-Kalb na Ibn Jariir رحمه الله تعالى .

وَأَنَا لَمَسْنَا السَّمَاءَ فَوَجَدْنَاهَا مُلْتَأَةً فَخَشَا شَدِيدًا وَشُهَبًا ﴿٦﴾ وَأَنَا كُنَّا نَقْعُدُ مِنْهَا مَقْعِدًا لِلسَّمْعِ فَمَنْ يَسْتَمِعِ الْآنَ يَحْدِثْ لَكُمْ شُهَابًا رَّصَدًا ﴿٦﴾ وَأَنَا لَا نَدْرِي أَشَرُّ أَرِيدَ يَمَنَ فِي الْأَرْضِ أَمْ أَرَادَ بِهِمْ رَبُّهُمْ رَشَدًا ﴿٦﴾

8. Nasi tulizigusa mbingu, na tukazona zimejaa walenzi wenye nguvu na vimondo.

9. Na hakika tulikuwa tukikaa humo katika baadhi ya makao ili kusikiliza; lakini sasa anayetaka kusikiliza atakuta kimondo kinamvizia!.

10. Nasi hatujui kama wanatakiwa shari wale wanaokaa kwenye ardhi au Mola wao Mlezi anawatakiwa uwongofu.

Uibaji wa Majini Habari za Mbinguni Kabla ya Kutumwa Mtume ﷺ na Kuvurumushiwa kwao Vimondo Baada ya Kutumwa

Allah ﷻ Anatoa habari kuhusu majini wakati Alipomtuma Mtume wake ﷺ, na akamteremshia Qur'ani, na katika njia ya kuhifadhi Qur'an Yake kwake, na kwamba mbingu imejazwa walinzi wakali, na kulindwa katika pande zake, na mashetani wakafukuzwa toka kwenye makazi yao, ambayo walikuwa wakikaa kabla ya hapo, wafanye udakuzi japo kidogo katika Qur'ani, na kuwaambia makuhani, kwa hiyo uwepo utatanishi, wala asijulikane yupi mkweli, na hii ni katika Upole wa Allah ﷻ kwa viumbe Wake na Rehema Yake kwa waja Wake na Kuhifadhi Kitabu Chake.

Na kwa ajili hiyo Allah ﷻ Amesema:

وَأَنَا لَمَسْنَا السَّمَاءَ فَوَجَدْنَاهَا مُلَمَّتًا حَرَسًا شَدِيدًا وَشُهَبًا ﴿١٠﴾ وَأَنَا كُنَّا نَقْعُدُ مِنْهَا مَقْعِدًا لِلسَّمْعِ فَمَنْ يَسْتَمِعِ الْآنَ يَسْمِعِ لهُ شَهَابًا رَّصَدًا ﴿١١﴾

“Nasi tulizigusa mbingu, na tukazona zimejaa walinzi wenye nguvu na vimondo. Na hakika tulikuwa tukikaa humo katika baadhi ya makao ili kusikiliza; lakini sasa anayetaka kusikiliza atakuta kimondo kinamvizia!” (72:10).

Maana yake: Mwenye kutaka kufanya udakuzi wa kusikiliza siku hizi leo anakutana na kimondo kikumvizia, na hakimkosi isipokuwa kitamtafuta na kumwangamiza,

وَأَنَا لَا نَدْرِي أَشَرٌّ أُرِيدَ بِمَنْ فِي الْأَرْضِ أَمْ أَرَادَ بِهِمْ رَبُّهُمْ رَشَدًا ﴿١٢﴾

“Nasi hatujui kama wanatakiwa shari wale wanaokaa kwenye ardhi au Mola Wao Mlezi Anawatakiwa uwongofu.” (72:10).

Maana yake: Hatujui jambo hili ambalo limetokea mbinguni. Hii ni adabu yao katika kuzungumza, kwa jinsi ambayo wametegemeza shari kwa asiyejulikana, na kheri wameitegemeza kwa Allah ﷻ, Imekuja katika sahihi:

«وَالشَّرُّ لَيْسَ إِلَيْكَ»

“Na shari sio Yako”¹

Nyota zilikuwa kabla ya hapo zikitumiwa kama vimondo, lakini sio kwa wingi sana bali baadhi ya nyakati, kama katika hadithi ya Ibn Abbaas رضي الله عنهما: Siku moja tulipokuwa tumekaa pamoja na Mtume ﷺ ghafla nyota ikavurumishwa, na kung’aa, Mtume ﷺ akasema:

«مَا كُنتُمْ تَقُولُونَ فِي هَذَا؟»

“Mlikuwa mnasema nini katika hili?”

Tukasema: Tulikuwa tukisema anazaliwa mtukufu na anakufa mtukufu, akasema:

«لَيْسَ كَذَلِكَ، وَلَكِنَّ اللَّهَ إِذَا قَضَى الْأَمْرَ فِي السَّمَاءِ»

“Sio hivyo, lakini ni wakati Allah Anapohukumu jambo mbinguni”

Akataja ukamilifu wa Hadithi,² Tumeileta Hadithi hiyo katika Surat Saba³ kwa ukamilifu wake, na hii ndio sababu ambayo imewafanya kutafuta njia katika hilo, wakawa wanatembea mashariki ya ardhi na magharibi yake, wakamkuta Mtume ﷺ anawasomea masahaba wake katika Sala, wakajua kuwa huyu ndiye ambaye mbingu imehifadhiwa kwa ajili yake, kwa hiyo wakaamini walioamini miongoni mwao, na wengine wakaasi, kama ilivyotangulia kutaja hilo Hadithi ya Ibn Abbas رضي الله عنهما. Katika Kauli Yake Allah تعالى katika Surat Ahqaaf:

وَإِذْ صَرَفْنَا إِلَيْكَ نَفَرًا مِّنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ

“Na wakati Tulipowaleta kundi la majini kuja kwako kusikiliza Qur’ani.” (46:29)⁴

¹ Muslim 1:535.

² Muslim 4:1750.

³ Angalia juzuu ya nane, Tafsir ya Surat Saba’ (34:22-23). Masimulizi halisi yaliondolewa kwenye toleo lililofupishwa; lakini maelezo yamebakia, pamoja na masimulizi yanayofanana yaliyoandikwa na Al-Bukhari na wengine.

⁴ Fat’hul Al-Bari 8:537. Angalia maelezo ya (46:29) katika juzuu ya tisa.

Hakuna shaka kuwa jambo hili lilitokea, na jambo hilo ni kukithiri kwa vimondo mbinguni na kupigwa navyo liliwatisha majini na watu wakababaika, wakajua kuwa hilo ni kwa ajili ya kuibomoa dunia, kama alivyosema Sudi: Mbingu haikuwa ikilindwa isipokuwa ardhini awepo Mtume, au Dini ya Allah تعالی imedhihiri, na mashetani kabla ya ujio wa Muhammad ﷺ walikuwa wakifanya makazi yao katika mbingu ya dunia. Mtume Muhammad ﷺ alipotumwa na Allah تعالی kuwa Nabii na Mtume, kuna usiku mmoja walivurumishiwa vimondo.

Watu wa Twaaf wakafazaika kwa hilo wakasema: watu wa mbinguni wameangamia kwa sababu ya ukali wa moto waliouona mbinguni na kupishana vimondo, wakawa wanaacha huru watumwa wao na kutoa kafara wanyama wao, mtumwa mmoja Yalaylu bin Amri bin Umayr akawaambia: “Ole wenu enyi watu wa Twaaf, zuieni mali zenu na angalieni alama za nyota, iwapo mtaziona zimetulia mahali pake, basi watu wa mbinguni hawajaangamia, hakika hii ni kwa ajili ya Ibn Abi Kabshah, anamkusudia Muhammad ﷺ, na mkziangalia na msizone basi watu wa mbinguni wameangamia. Basi wakaangalia wakazona, wakazuia mali zao, kwa hiyo mashetani wakafazaika katika usiku huo, wakamfuata Ibilisi wakamhadithia ambayo yametokea, akasema: nileteeni kila ardhi kifumba cha mchanga nikinuse, wakamletea akainusa akasema: Mtu wenu yuko Makkah, kwa hiyo wakatuma watu saba wa majini wakaja Makkah wakamkuta Mtume ﷺ amesimama anasali katika *Almasjid Alharaam* anasoma Qur’ani wakamsogelea kwa pupa yao ya kusikiliza Qur’ani, mpaka msugvano wao ulikaribia kumpata, kisha wakasilimu, Allah تعالی Akateremsha jambo lao kwa Mtume ﷺ.

Tumetaja kipambanuzi hiki kwa urefu katika mwanzo wa utume katika kitabu cha seera, ndefu.¹

Na Allah تعالی ni Mjuzi zaidi, na ni Zake Sifa Njema.



¹ Kuna masimulizi sawa na hayo kutoka kwa Abbas عنهما الله yaliyosimuliwa na At-Tabari. Angalia juzuu ya nane, Tafsiiri ya *Surat As-Saffat*.

وَأَنَا مِنَّا الصَّالِحُونَ وَمِنَّا دُونَ ذَلِكَ ۖ كُنَّا طَرَائِقَ قَدَدًا ﴿١١﴾
وَأَنَا ظَنَنَّا أَنْ لَنْ نُعْجِزَ اللَّهَ فِي الْأَرْضِ وَلَنْ نُعْجِزَهُ هَرَبًا
﴿١٢﴾ وَأَنَا لَمَّا سَمِعْنَا آهْدَىٰ ءَامِنَّا بِهِ ۖ فَمَنْ يُؤْمِنُ
بِرَبِّهِ فَلَا يَخَافُ كَخَسَا وَلَا رَهَقًا ﴿١٣﴾ وَأَنَا مِنَّا الْمُسْلِمُونَ
وَمِنَّا الْقَاسِطُونَ ۖ فَمَنْ أَسْلَمَ فَأُولَٰئِكَ تَحَرَّوْا رَشَدًا ﴿١٤﴾
وَأَمَّا الْقَاسِطُونَ فَكَانُوا لِجَهَنَّمَ حَطَبًا ﴿١٥﴾ وَالْوَالِدُوا
اَلَّذِينَ اسْتَفْتَمُوا عَلَى الطَّرِيقَةِ لِأَسْقَيْنَهُمْ مَاءً غَدَقًا ﴿١٦﴾
لِنَفْتِنَهُمْ فِيهِ ۖ وَمَنْ يُعْرِضْ عَنْ ذِكْرِ رَبِّهِ يَسْلُكُهُ عَذَابًا
صَعَدًا ﴿١٧﴾ وَأَنْ اَلْمَسْجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا
﴿١٨﴾ وَأَنْتُمْ كَمَا قَامَ عَبْدُ اللَّهِ يَدْعُوهُ كَادُوا يَكُونُونَ عَلَيْهِ
لِبَدًا ﴿١٩﴾ قُلْ إِنَّمَا أَدْعُوا رَبِّي وَلَا أُشْرِكُ بِهِ أَحَدًا ﴿٢٠﴾
قُلْ إِنِّي لَا أَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَلَا رَشَدًا ﴿٢١﴾ قُلْ إِنِّي لَنْ
نُجِيرَكَ مِنَ اللَّهِ أَحَدٌ وَلَنْ أَجِدَ مِنْ دُونِهِ مُلْتَحَدًا ﴿٢٢﴾
إِلَّا بَلَاغًا مِنَ اللَّهِ وَرِسَالَاتِهِ ۖ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنَّ
لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ﴿٢٣﴾ حَتَّىٰ إِذَا رَأَوْا مَا
يُوعَدُونَ فَسِعِلْمُونَ مَنْ أضعف ناصبرًا وأقل عدداً ﴿٢٤﴾
قُلْ إِنْ أَدْرَيْتَ أَقْرَبُ مَا تُوعَدُونَ أَمْ يَجْعَلُ لَهُ رَبِّي أَمَدًا
﴿٢٥﴾ عَلِيمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا ﴿٢٦﴾ إِلَّا
مَنْ أَرْتَضَىٰ مِنْ رَسُولٍ فَإِنَّهُ يَسْلُكُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ
خَلْفِهِ رَصَدًا ﴿٢٧﴾ لِيَعْلَمَ أَنْ قَدْ أُبْلِغُوا رِسَالَاتِ رَبِّهِمْ
وَأَحَاطَ بِمَا لَدَيْهِمْ وَأَحْصَىٰ كُلَّ شَيْءٍ عَدَدًا ﴿٢٨﴾

وَأَنَا مِنَّا الصَّالِحُونَ وَمِنَّا دُونَ ذَلِكَ ۖ
كُنَّا طَرَائِقَ قَدَدًا ﴿١١﴾ وَأَنَا ظَنَنَّا أَنْ
لَنْ نُعْجِزَ اللَّهَ فِي الْأَرْضِ وَلَنْ نُعْجِزَهُ
هَرَبًا ﴿١٢﴾ وَأَنَا لَمَّا سَمِعْنَا آهْدَىٰ
ءَامِنَّا بِهِ ۖ فَمَنْ يُؤْمِنُ بِرَبِّهِ فَلَا
يَخَافُ كَخَسَا وَلَا رَهَقًا ﴿١٣﴾ وَأَنَا مِنَّا
الْمُسْلِمُونَ وَمِنَّا الْقَاسِطُونَ ۖ فَمَنْ
أَسْلَمَ فَأُولَٰئِكَ تَحَرَّوْا رَشَدًا ﴿١٤﴾
وَأَمَّا الْقَاسِطُونَ فَكَانُوا لِجَهَنَّمَ
حَطَبًا ﴿١٥﴾ وَالْوَالِدُوا
اَلَّذِينَ اسْتَفْتَمُوا عَلَى الطَّرِيقَةِ
لِأَسْقَيْنَهُمْ مَاءً غَدَقًا ﴿١٦﴾
لِنَفْتِنَهُمْ فِيهِ ۖ وَمَنْ يُعْرِضْ عَنْ ذِكْرِ
رَبِّهِ يَسْلُكُهُ عَذَابًا صَعَدًا ﴿١٧﴾

11. Na hakika katika sisi wamo walio wema, na wengine wetu ni kinyume na hivyo. Tumekuwa njia mbalimbali.

12. Nasi tulijua kuwa hatutomshinda Mwenyezi Mungu duniani, wala hatuwezi kumponyoka kwa kukimbia.

13. Nasi tuliposikia uwongofu tuliuamini. Basi mwenye kumuamini Mola wake Mlezi basi haogopi kupunjwa wala kudhulumiwa.

14. Na hakika wamo katika sisi Waislamu, na wamo kati yetu wanaoacha haki. Basi waliosilimu, hao ndio waliotafuta uwongofu.

15. Na ama wanaoacha haki, hao watakuwa kuni za Jahannamu.

16. Na lau kama wangelisimama sawasawa juu ya njia Tungeliwanyweshaji kwa wingi,

17. Ili Tuwajaribu kwa hayo. Na anayepuuza kumkumbuka Mola Wake Mlezi Atamsukuma kwenye adhabu ngumu.

Aina za Majini, Kuna Waumini na Makafiri, Wapotevu na Waongofu.

Allah تعالیٰ Anasema Akielezea majini kuwa wao wenyewe wamesema:

وَأَنَا مِنَّا الصَّالِحُونَ وَمِنَّا دُونَ ذَلِكَ^ط

“Na hakika katika sisi wamo walio wema, na wengine wetu ni kinyume na hivyo.” (72:11)

Maana yake: Wasiokuwa wema.

كُنَّا طَرَائِقَ قَدَدًا

“Tumekuwa njia mbalimbali.” (72:11)

Maana yake: Njia nyingi tofauti, na mitazamo tofauti, Ibn Abbaas, Mujaahid na wengine wamesema:

كُنَّا طَرَائِقَ قَدَدًا

“Tumekuwa njia mbalimbali.” (72:11)

Maana yake: Katika sisi wapo waumini na makafiri.¹

Ahmad bin Sulaimaan Najaad amesimulia katika kitabu chake: Kuwa nimemsikia A'amash akisema: 'Alikuwa kwetu jinni nikamuambia': Ni chakula

¹ At-Tabari 23:659.

gani kinapendwa zaidi kwenu? ' Akasema: 'mchele', akasema: "tukampelekea (mchele) tukaona matonge yakipelekwa mdomoni lakini hatuoni yoyote." Nikasema: "Je katika nyinyi kuna ambao hufuata utashi wao wa nafsi kama, tulivyo sisi?' Akasema: 'ndio', Nikasema: 'Ni nani mpingaji katika nyinyi?', Akasema: 'muovu wetu' Isinadi hii imeoneshwa kwa shekhe wetu Haafidh Abi Al Hajjaaj {Almizzi} رحمه الله تعالى akasema: Isinadi hii ni sahihi kwa A'amash.

Majini Wanakubali Uwepo wa Kudura ya Allah تعالى Timilifu

وَأَنَا ظَنَنَّا أَنْ لَنْ نُعْجِزَ اللَّهَ فِي الْأَرْضِ وَلَنْ نُعْجِزَهُ هَرَبًا ﴿١٢﴾

***"Nasi tulijua kuwa hatutomshinda Mwenyezi Mungu duniani, wala hatuwezi kumponyoka kwa kukimbia."* (72:12).**

Maana yake: Tunajua kuwa kudura ya Allah تعالى juu yetu ina hekima kubwa na kuwa sisi hatuwezi kuishinda katika ardhi, na hata tukiweza kukimbia hakika Yeye Allah تعالى juu yetu ni Mwenye Nguvu hakuna yeyote atakayemshinda,

وَأَنَا لَمَّا سَمِعْنَا آهْدَىٰءَ آمَنَّا بِهِ ۗ

***"Nasi tuliposikia uwongofu tuliuamini."* (72:13)**

Wanajifakharisha kwa hilo, hiyo ni fakhari yao, na sharafu kubwa pamoja na sifa nzuri, na kauli yao,

فَمَنْ يُؤْمِنُ بِرَبِّهِ فَلَا يَخَافُ بَخْسًا وَلَا رَهَقًا ﴿١٣﴾

***"Basi mwenye kumuamini Mola wake Mlezi basi haogopi kupunjwa wala kudhulumiwa."* (72:13).**

Ibn Abbaas, Qatadah, na wengine رضي الله عنهم wamesema: Hahofii kupunguzwa katika mema yake, au kubebeshwa makosa yasiyokuwa yake,¹ Kama Alivyosema Allah تعالى:

فَلَا يَخَافُ ظُلْمًا وَلَا هَضْمًا ﴿١٣﴾

***"Basi haogopi kudhulumiwa wala kupunjwa."* (20:112)**

¹ At-Tabari 23:660.

Maana yake: Katika sisi kuna Muislamu na kuna waovu naye ni yule anayeipindisha haki na kuikandamiza. Katika lugha ya kiarabu kuna tofauti ya matumizi kati ya neno "Alqaasitu" yenye maana ya mtu muovu. Na neno "Muqsitu" yenye maana ya mtu muadilifu.

وَأَنَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ وَمِنَّا الْقَاسِطُونَ

"Na hakika wamo katika sisi Waislamu, na wamo kati yetu wanaoacha haki."

فَمَنْ أَسْلَمَ فَأُولَئِكَ تَحَرَّوْا رَشَدًا

"Basi waliosilimu, hao ndio waliotafuta uwongofu." (72:14)

Maana yake: Wametafuta uokovu wa nafsi zao

وَأَمَّا الْقَاسِطُونَ فَكَانُوا لِجَهَنَّمَ حَطَبًا

"Na ama wanaoacha haki, hao watakuwa kuni za Jahannamu."

Maana yake: Kuni zitakazowaka. Kauli Yake تعالی:

وَأَلَوْ اسْتَقَمْتُمْ عَلَى الطَّرِيقَةِ لَأَسْقَيْنَهُمْ مَاءً غَدَقًا ﴿١٦﴾ لِنَفْسِهِمْ فِيهِ

"Na lau kama wangelisimama sawasawa juu ya njia Tungeli-wanyweshaji maji kwa wingi, Ili Tuwajaribu." (72:16-17)

Wafasiri wametofautiana katika maana hii kwa kauli mbili:

Mosi:

Na lau waovu watashikamana na mafundisho ya Uislamu wakawa waadilifu na wakadumu katika hali hiyo.

لَأَسْقَيْنَهُمْ مَاءً غَدَقًا ﴿١٦﴾

"Tungeliwanyweshaji maji kwa wingi."

Maana yake: Mengi, na muradi wa hilo ni kuzidishiwa riziki, kwa kuzingatia hilo, inakuwa maana ya Kauli Yake تعالی,

لَتَفْتِنَهُمْ فِيهِ

“Ili Tuwajaribu.” (72:17)

Maana yake: Ili Tuwajaribu wao, kama alivyosema Maalik toka kwa Zaid bin Aslam: ili tuwape mtihani na majaribu tujue anaebaki katika uongofu na mwenye kutenda uovu.

Watu wenye mtazamo huu; Aafi amepokea mfano wake toka kwa Ibn Abbaas, na kadhalika amesema Mujaahid, Saiid bin Jubair, Saiid bin Musayyib, Atwaa, Sudi, Muhammad bin Ka'ab Quradhi, Qatadah, na Adh-Dhahaak رضي الله عنهم. Muqaatil amesema: Imeshuka kwa makafiri wa kuraishi wakati walipozuiwa mvua miaka saba.

Pili:

وَالْوِاسْتَقْمُوا عَلَى الطَّرِيقَةِ

“Na lau kama wangelisimama sawasawa juu ya njia.” (72:16)

Maana yake: Wapotevu.

لَأَسْقِيَنَّهُمْ مَاءً غَدَقًا

“Tungeliwanyesha maji kwa wingi.” (72:16)

Kwa maana: Tungewakunjulia riziki polepole. Kama Allah تعالى Alivyosema:

فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِ فَتَحْنَا عَلَيْهِمْ أَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ حَتَّى إِذَا فَرِحُوا بِمَا أُوتُوا

أَخَذْنَاهُمْ بَغْتَةً فِإِذَا هُمْ مُبْلِسُونَ

“Basi waliposahau waliyokumbushwa Tuliwafungulia milango ya kila kitu. Mpaka walipofurahia yale waliyopewa Tuliwaadhibu wao kwa ghafla, na mara wakawa wenye kukata tamaa.” (6:44).

Kama Kauli Yake:

أَتَحْسَبُونَ أَنَّمَا نُمِدُّهُم بِهِ مِنْ مَّالٍ وَبَيْنَ ۖ نُسَارِعُ لَهُمْ فِي الْآخِرَاتِ ۗ بَلْ لَا يَشْعُرُونَ

“Je! Wanadhani ya kuwa kwa vile Tunavyowapa mali na watoto, Ndio Tunawahimizia kheri? Lakini wenyewe hawatambui.” (23:55-56)

Na huu ni mtazamo wa Abuu Mijilazi Lakiji bin Humaid. Hakika amesema katika Kauli Yake Allah تعالى،

وَأَلِّوْا أَسْتَقْنُمُوا عَلَى الطَّرِيقَةِ

“Na lau kama wangelisimama sawasawa juu ya njia.” (72:16)

Maana yake: Njia ya upotovu, ameipokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى، Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى¹ Ameihadithia Baghawi رحمه الله تعالى toka kwa Rabii bin Anas na Zayd bin Aslam, Kalb na Ibn Kaysaan.²

Mtazamo wake huu una mashiko na hupewa nguvu na Kauli Yake تعالى ili Tuwafitini ndani yake.

Na Kauli Yake تعالى:

وَمَنْ يُعْرِضْ عَن ذِكْرِ رَبِّهِ يَسْلُكْهُ عَذَابًا صَعَدًا ﴿١٧﴾

“Na anayepuza kumku mbuka Mola Wake Mlezi Atamsukuma kwenye adhabu ngumu.” (72:17)

Maana yake: Adhabu ngumu iumizayo na kutia uchungu. Ibn Abbas, Mujaahid, Ikrimah, Qatadah na Ibn Zayd رضي الله عنهم wamesema:

عَذَابًا صَعَدًا ﴿١٧﴾

“Adhabu ngumu.” (72:17)

Maana yake: Ni tabu isiyokuwa na kupumzika.³

Na kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema: ni jabali katika Jahannam.⁴

Na kutoka kwa Saiid bin Jubair: Kisima ndani yake (Maana: Ndani ya Jahannam).

¹ At-Tabari 23:663.

² Al-Baghawi 4:404.

³ At-Tabari 23:664.

⁴ At-Tabari 23:664.

وَأَنَّ الْمَسْجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا ﴿١٨﴾ وَأَنْتُمْ لِمَا قَامَ عَبْدُ اللَّهِ يَدْعُوهُ كَادُوا
يَكُونُونَ عَلَيْهِ لِبَدًا ﴿١٩﴾ قُلْ إِنَّمَا أَدْعُوا رَبِّي وَلَا أُشْرِكُ بِهِ أَحَدًا ﴿٢٠﴾ قُلْ إِنِّي لَا أَمْلِكُ
لَكُمْ ضَرًّا وَلَا رَشَدًا ﴿٢١﴾ قُلْ إِنِّي لَنْ يُجِيرَنِي مِنَ اللَّهِ أَحَدٌ وَلَنْ أَجِدَ مِنْ دُونِهِ مُلْتَحَدًا
﴿٢٢﴾ إِلَّا بَلَاغًا مِنَ اللَّهِ وَرِسَالَاتِهِ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدًا
فِيهَا أَبَدًا ﴿٢٣﴾ حَتَّىٰ إِذَا رَأَوْا مَا يُوعَدُونَ فَسَيَعْلَمُونَ مَنْ أَضَعُفٌ نَاصِرًا وَأَقَلُّ عَدَدًا ﴿٢٤﴾

18. Na hakika misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimuabudu yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu.

19. Na hakika Mja wa Mwenyezi Mungu aliposimama kumuomba, wao walikuwa karibu kumzonga!

20. Sema: Hakika mimi namuomba Mola Wangu Mlezi, wala simshirikishi Yeye na yeyote.

21. Sema: Mimi sina mamlaka ya kukudhuruni wala kukuongozeni.

22. Sema: Hakika hapana yeyote awezae kunilinda na Mwenyezi Mungu, wala sitapata pa kukimbilia isipokuwa Kwake Yeye tu.

23. Ili nifikishe Ujumbe utokao kwa Mwenyezi Mungu na risala Zake. Na wenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, basi hakika hao watapata Moto wa Jahannamu wadumu humo milele.

24. Hata watakapoyaona wanayoahidiwa, ndipo watakapojua ni nani mwenye msaidizi dhaifu, na mchache wa idadi.

Amri ya Kumuabudu Allah تعالی na Kujiepusha na Ushirikina

Allah تعالی Anasema Akiwaamrisha waja Wake kumpwekesha katika mahali pa ibada Yake, wala asiombwe pamoja Nae yoyote, wala asishirikishwe na kitu kingine. Kama alivyosema Qatadah katika Kauli Yake تعالی:

وَأَنَّ الْمَسْجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا ﴿١٨﴾

“Na hakika misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimuabudu yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu.” (72:18)

Amesema: Mayahudi na Manaswara walikuwa waingiapo makanisani mwao na katika masinagogi yao humshirikisha Allah تعالى. Hivyo Allah تعالى Akamuamrisha Mtume Wake ﷺ, kumpwekesha Yeye Peke Yake,¹ Ibn Jariir رحمه الله تعالى amepokea toka kwa Saiid bin Jubair,

وَأَنَّ الْمَسْجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا ﴿١٨﴾

“Na hakika misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimuabudu yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu.” (72:18).

Amesema: Majini walimwambia Mtume ﷺ: ‘Vipi sisi kuja msikitini, na hali ya kuwa sisi tutakuwa mbali na wewe?, na vipi tutahudhuria Sala hali ya kuwa tuko mbali na wewe?’ Icashuka,

وَأَنَّ الْمَسْجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا ﴿١٨﴾

“Na hakika misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimuabudu yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu.” (72:18)²

Msongamano wa Majini Katika Kusikiliza Qurani

Kauli Yake تعالى:

وَأَنَّهُ لَمَّا قَامَ عَبْدُ اللَّهِ يَدْعُوهُ كَادُوا يَكُونُونَ عَلَيْهِ لِبَدًا ﴿١٩﴾

“Na hakika Mja wa Mwenyezi Mungu aliposimama kumuomba, wao walikuwa karibu kumzonga!” (72:19)

Aufi amesema toka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما anasema: Walipomsikia Mtume ﷺ anasoma Qur’ani walikaribia kumpanda kwa shauku na wakamsogelea, hakuwajua mpaka alipomjia Jibril عليه السلام ikawa anamsomea:

قُلْ أَوْحَىٰ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْتَمَعَ نَفَرٌ مِّنَ الْجِنِّ

“Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikiliza.” (72:1)

¹ At-Tabari 23:665.

² At-Tabari 23:665. Haya ni masimulizi ambayo ni Mursal

Wanasikiliza Qur'ani, huu ni mtazamo mmoja, na mtazamo huu umepokewa toka kwa Zubairi bin Awwaam رضي الله عنه, na amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى toka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما, amesema: Majini wamesema kuwaambia kaumu yao,

لَمَّا قَامَ عَبْدُ اللَّهِ يَدْعُوهُ كَادُوا يَكُونُونَ عَلَيْهِ لِبَدًا ﴿١٩﴾

“Mja wa Mwenyezi Mungu aliposimama kumuomba, wao walikuwa karibu kumzonga!” (72:19)

Amesema: walipomuona anasali na sahaba wake, wanarukuu anaporukuu na wanasujudu anaposujudu. Amesema: walistajabu kutokana na utii wa swahaba wake kwake. Akasema: wakasema kuwaambia jamaa zao,

لَمَّا قَامَ عَبْدُ اللَّهِ يَدْعُوهُ كَادُوا يَكُونُونَ عَلَيْهِ لِبَدًا ﴿١٩﴾

“Mja wa Mwenyezi Mungu aliposimama kumuomba, wao walikuwa karibu kumzonga!” (72:19)¹

Huu ni mtazamo wa pili, na huo pia umepokewa na Saidi bin Jubair.² Hasan amesema: Mtume ﷺ aliposimama anasema: *“Laa ilaaha illa Ilaah”* na akiwalingania watu kwa Mola Wao, waarabu wote walikaribia kumzonga.³ Qatadah amesema katika Kauli Yake:

وَأَنَّهُ لَمَّا قَامَ عَبْدُ اللَّهِ يَدْعُوهُ كَادُوا يَكُونُونَ عَلَيْهِ لِبَدًا ﴿١٩﴾

“Na hakika Mja wa Mwenyezi Mungu aliposimama kumuomba, wao walikuwa karibu kumzonga!” (72:19)

Amesema: Majini na watu walimzonga kuhusu jambo hili ili walizime. Allah تعالى Akakataa isipokuwa kumnusuru, kulipa msukumo na kulidhihirisha juu ya wale waliokuwa wakimpinga.⁴ Na hii ni Kauli inayofuata:

قُلْ إِنَّمَا أَدْعُوا رَبِّي وَلَا أُشْرِكُ بِمِثْلِهِ أَحَدًا ﴿٢٠﴾

“Sema: Hakika mimi namuomba Mola Wangu Mlezi, wala simshirikishi Yeye na yeyote.” (72:20)

¹ At-Tabari 23:667.

² At-Tabari 23:667.

³ At-Tabari 23:668.

⁴ At-Tabari 23:667.

Maana yake: Mtume ﷺ aliwaambia hayo, walipomuudhi, wakamkhalifu, kumkadhibisha na kumfanyia uadui ili wabatilishe haki aliokuja nayo, wakakusanyika juu ya kumfanyia uadui.

إِنَّمَا أَدْعُوا رَبِّي

“Hakika mimi namuomba Mola Wangu.” (72:20)

Si vingine namuabudu Mola Wangu Peke Yake asiye na mshirika, na nataka hifadhi Yake, na nategemea Kwake.

وَلَا أُشْرِكُ بِهِ أَحَدًا ﴿٢٠﴾

“Wala simshirikishi Yeye na yeyote.” (72:20)

Mtume ﷺ Hamiliki Madhara wala Uongofu

Kauli Yake تعالى:

قُلْ إِنِّي لَا أَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَلَا رَشَدًا ﴿٢١﴾

“Sema: Mimi sina mamlaka ya kukudhuruni wala kukuongozeni.” (72:21)

Maana yake: Hakika mimi ni binadamu mfano wenu, ninapewa ufunuo na Allah تعالى, na ni mja katika waja Wake, mimi sina amri yoyote katika uongofu wenu wala upotevu wenu, bali marejeo katika hayo yote ni kwa Allah تعالى Peke Yake.

Kisha akahabarisha ya kuwa hakuna yeyote angelimuokoa yeye kama angelimuasi Allah تعالى, basi hakuna yoyote angeweza kuniokoa kutokana na adhabu Yake:

وَلَنْ أَجِدَ مِنْ دُونِهِ مُلْتَحَدًا ﴿٢٢﴾

“Wala sitapata pa kukimbilia isipokuwa Kwake Yeye tu.” (72:22)

Mujahid, Qatadah na Sudi wamesema, “hakuna kimbilio.”¹

¹ At-Tabari 23:669.

Wajibu wa Mtume ﷺ ni Ujumbe

Kauli Yake تعالى:

إِلَّا بَلَاغًا مِّنَ اللَّهِ وَرِسَالَاتٍ

“Ila nifikishe Ujumbe utokao kwa Mwenyezi Mungu na risala Zake.” (72:23)

Kujivua kutoka Kauli Yake تعالى:

لَن يُجِيرَنِي مِنَ اللَّهِ أَحَدٌ

“Hapana yeyote awezae kunilinda na Mwenyezi Mungu.” (72:22)

Maana yake: hakitanihifadhi chochote na kuniokoa isipokuwa kufikisha ujumbe ambao Amelazimisha juu yangu kuufikisha. Kama Allah تعالى Alivyosema,

* يَتَأْتِيهَا الرُّسُولُ يَلْفِغُ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ وَإِن لَّمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَغْتَ رِسَالَتَهُ ؕ وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ

“Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe Wake. Na Mwenyezi Mungu Atakulinda na watu...” (5:67)

Na Kauli Yake تعالى:

وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدًا فِيهَا أَبَدًا

“Na wenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, basi hakika hao watapata Moto wa Jahannamu wadumu humo milele.” (72:23)

Maana yake: Mimi nakufikishieni ujumbe wa Allah تعالى, kwa hiyo atakayeasi baada ya hapo huyo malipo yake juu ya hilo ni moto wa jahannamu milele.

Maana yake: Hana kimbilio, wala kutoka humo. Na Kauli Yake تعالى:

حَتَّىٰ إِذَا رَأَوْا مَا يُوعَدُونَ فَسَيَعْلَمُونَ مَنْ أَضْعَفُ نَاصِرًا وَأَقَلُّ عَدَدًا

“Hata watakapoyaona wanayoahidiwa, ndipo watakapojua ni nani mwenye msaidizi dhaifu, na mchache wa idadi.” (72:24)

Maana yake: Mpaka watakapoona hao washirikina wa kijini, na watu wanayoahidiwa siku ya kiama, basi siku hiyo watajua ni nani mwenye wasaidizi dhaifu na wachache zaidi, Je, ni wao au waumini wanaomuabudu Allah تعالى Peke Yake. Inamaanisha kuwa washirikina hawana mwenye kuwanusuru kabisa, na wao ni wachache wa idadi, ukilinganisha na jeshi la Allah تعالى.

قُلْ إِنْ أَدْرِي أَقْرَبُ مَا تُوعَدُونَ أَمْ يَجْعَلُ لَهُ رَبِّي أَمَدًا ﴿٢٥﴾ عَلِيمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ
عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا ﴿٢٦﴾ إِلَّا مَنِ ارْتَضَىٰ مِنْ رَسُولٍ فَإِنَّهُ يَسْلُكُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَيَمْنِ
خَلْفِهِ رَصَدًا ﴿٢٧﴾ لِيَعْلَمَ أَنْ قَدْ أَبْلَغُوا رَسُولَاتِ رَبِّهِمْ وَأَحَاطَ بِمَا لَدَيْهِمْ وَأَحْصَىٰ كُلَّ
شَيْءٍ عَدَدًا ﴿٢٨﴾

25. Sema: Sijui kama yapo karibu hayo mnayoahidiwa, au Mola Wangu Mlezi atayawekea muda mrefu.

26. Yeye Ndiye Mwenye Kujua ya siri, wala hamdhihirishii yeyote siri Yake,

27. Isipokuwa Mtume Wake aliyemridhia. Naye huyo Humuekea walinzi mbele yake na nyuma yake.

28. Ili Yeye ajue kwamba wao wamefikisha ujumbe wa Mola Wao Mlezi, na Yeye Anayajua vyema yote walio nayo, na Amedhibiti idadi ya kila kitu.

Mtume ﷺ Hajui Wakati wa Kutokea Kiama

Allah تعالى Anasema Akimuamuru Mtume Wake ﷺ, kuwaambia watu kuwa yeye hajui siku ya kutokea kiama wala hajui wakati wake upo karibu au mbali,

قُلْ إِنْ أَدْرِي أَقْرَبُ مَا تُوعَدُونَ أَمْ يَجْعَلُ لَهُ رَبِّي أَمَدًا ﴿٢٥﴾

“Sema: Sijui kama yapo karibu hayo mnayoahidiwa, au Mola wangu Mlezi Atayawekea muda mrefu.” (72:25)

Maana yake: Muda mrefu. Na katika aya hii tukufu kuna ushahidi wa wazi ya kwamba Hadithi wanayoitumia wajinga wengi kuwa Mtume ﷺ katika kaburi lake hatofikisha miaka elfu moja isipokuwa kiama kikubwa kitatokea ni uongo

haina asili yoyote, na hatujaiona katika kitabu chochote. Na Mtume ﷺ alipokuwa akiulizwa kuhusu kiama kitatokea lini alikuwa hajibu kitu. Na Jibrili عليه السلام alipomtokea katika sura ya bedui katika aliyomuuliza alisema: “Ewe Muhammad ﷺ niambie kuhusu habari ya kiama. Akasema:

«مَا الْمَسْئُولُ عَنْهَا بِأَعْلَمَ مِنَ السَّائِلِ»

“Mwenye kuulizwa si mjuzi kuliko mwenye kuuliza.”

Na wakati Bedui alipomuita kwa sauti ya wazi akasema: ‘Ewe Muhammad ni lini kiama?’

Mtume ﷺ akamjibu:

«وَبِحَاكِ إِتْنَاهَا كَاتِبَتُهُ، فَمَا أَغَدَدْتَ لَهَا؟»

“Ole wako kwa hakika hicho kitatokea, basi umekiandalia nini?”

Akasema: ‘Ama mimi sikukiandalia Sala nyingi wala Saumu lakini mimi nampenda Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ,’ Mtume ﷺ akasema:

«فَأَنْتَ مَعَ مَنْ أُخِيَّتْ»

“Basi wewe uko pamoja na uliyempenda”

Anas رضي الله عنه amesema: ‘Hawajafurahi waislamu kwa jambo lolote, kama furaha yao kwa mazungumzo haya.’¹ Kauli Yake تعالى،

عَلِمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا ﴿٦٥﴾ إِلَّا مَنِ ارْتَضَىٰ مِنْ رَسُولٍ

“Yeye Ndiye Mwenye Kujua ya siri, wala hamdhihirishii yeyote Siri Yake, isipokuwa Mtume Wake aliyemridhia.”

Hii ni Kama Kauli Yake تعالى:

وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ

“Wala wao hawajui chochote katika Ujuzi Wake, ila kwa Atakalo Mwenyewe.” (2:255)

¹ Fat’hul Al-Bari 1:140. Vile vile angalia Al-Bukhari 6167.

Kama hivi Amesema hapa kuwa Yeye Anajua vyenye kuonekana na visivyoonekana hakuna yoyote katika viumbe Wake anayejua chochote katika elimu Yake, isipokuwa ile aliyomuonesha Allah تعالى. Kwa ajili hii Amesema:

عَلِمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا ﴿٦٧﴾ إِلَّا مَن أَرْتَضَىٰ مِن رَّسُولٍ

“Yeye Ndiye Mwenye Kujua ya siri, wala hamdhihirishii yeyote siri Yake. Isipokuwa Mtume Wake Aliyemridhia.”

Hili linaenea kwa Mtume wa kimalaika na wa kibinadamu.

Kisha Akasema Allah تعالى:

فَإِنَّهُ يَسْأَلُكُم مِّن بَيْن يَدَيْهِ وَمَن خَلْفِهِمْ رَصَدًا ﴿٦٨﴾

“Naye huyo humuekea walinzi mbele yake na nyuma yake.”

Maana yake: Humuhusisha kwa kumzidishia malaika wanaofuatana kumhifadhi kutokana na amri ya Allah تعالى, na humsindikiza kwa kuwa amebeba wahyi wa Allah تعالى. Kwa ajili hii Amesema:

لَيَعْلَمَنَّ أَن قَدْ أَبْلَغُوا رِسَالَاتِ رَبِّهِمْ وَأَحَاطَ بِمَا لَدَيْهِمْ وَأَحْصَىٰ كُلَّ شَيْءٍ عَدَدًا ﴿٦٩﴾

“Ili Yeye ajue kwamba wao wamefikisha ujumbe wa Mola Wao Mlezi, na Yeye Anayajua vyema yote walio nayo, na Amedhibiti idadi ya kila kitu.”

Katika Kauli Yake:

لَيَعْلَمَنَّ

“Ili Yeye ajue.”

Kinarudi kwa Mtume ﷺ, Ibn Jariir رحمه الله تعالى amepokea toka kwa Saiid bin Jubayr katika Kauli Yake تعالى:

عَلِمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا ﴿٦٧﴾ إِلَّا مَن أَرْتَضَىٰ مِن رَّسُولٍ فَإِنَّهُ يَسْأَلُكُم

مِّن بَيْن يَدَيْهِ وَمَن خَلْفِهِمْ رَصَدًا ﴿٦٨﴾

“Yeye Ndiye Mwenye Kujua ya siri, wala hamdhihirishii yeyote Siri Yake, Isipo kuwa Mtume Wake Aliyemridhia. Naye huyo humuekea walinzi mbele yake na nyuma yake.” (72:26-27)

Akasema: ni walinzi wane wa kimalaika pamoja na Jibrili عليه السلام,

لَيَعْلَمَنَّ

“Ili Yeye ajue.” (72:28)

Maana yake: Muhammad ﷺ.

أَنْ قَدْ أُبْلَغُوا رِسَالَتِ رَبِّهِمْ وَأَحَاطَ بِمَا لَدَيْهِمْ وَأَحْصَى كُلَّ شَيْءٍ عَدَدًا ﴿٢٨﴾

“Kwamba wao wamefikisha ujumbe wa Mola Wao Mlezi, na Yeye Anayajua vyema yote walionayo, na Amedhibiti idadi ya kila kitu.”¹

Ameipokea Ibn Abi Haatim na kadhalika amepokea kama hivyo Adh-Dhahaak, Sudi na Yazid bin Abi Hubaib. Abdur Razzaak, Ma’amar toka kwa Qatadah.

لَيَعْلَمَنَّ أَنْ قَدْ أُبْلَغُوا رِسَالَتِ رَبِّهِمْ

“Ili Yeye ajue kwamba wao wamefikisha ujumbe wa Mola Wao.”

Amesema: Ili Mtume ﷺ ajue kuwa Mitume wamefikisha toka kwa Allah تعالى, na kuwa malaika waliwalinda na kuwatetea.² Na kama hivyo amepokea Saiid bin Abi Arubah toka kwa Qatadah, na kauli hiyo ameikubali Ibn Jariir رحمه الله تعالى.³ Baghawi رحمه الله تعالى amesema: Ya’aquub amesoma:

(لَيُعْلَمَنَّ)

“Ilyu’lama”,

Kwa *dhuma*, Maana yake: Ili watu wajue kuwa Mitume wamefikisha.⁴ Na inawezekana kuwa dhamiri (kiwakilishi hapa) inarudi kwa Allah تعالى, na hiyo ni kauli alioisimulia Ibn Jawzy katika kitabu ‘*Zaadul Masiir*’. Na maana yake itakuwa: Kwamba Yeye Anawalinda Mitume Wake kwa Kuwapa malaika ili waweze kufikisha ujumbe Wake, na kuhifadhi wahyi unaowashukia, ili ajue kuwa wamefikisha ujumbe wa Mola wao. Kama katika Kauli ya Allah تعالى:

¹ At-Tabari 23:673.

² Abdur-Razzaq 3:323.

³ At-Tabari 23:673.

⁴ Al-Baghawi 4:406.

وَمَا جَعَلْنَا الْقِبْلَةَ الَّتِي كُنْتَ عَلَيْهَا إِلَّا لِنَعْلَمَ مَنْ يَتَّبِعُ الرَّسُولَ مِمَّنْ يَنْقَلِبُ عَلَيَّ عَاقِبِيهِ ۗ

“Na hatukukifanya kibla ulicho kuwa nacho ila Tupate kumjua yule anayemfuata Mtume na yule anayegeuka akarejea nyuma.”
(2:143).

Aidha kama Kauli Yake Allah تعالی:

وَلْيَعْلَمَنَّ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَلْيَعْلَمَنَّ الْمُنَافِقِينَ ﴿١١﴾

“Na hapana shaka Mwenyezi Mungu Anawajua walioamini, na Anawajua wanafiki.” (29:11)

Mifano mingi kama hiyo ya kuwa Allah تعالی Anajua vitu kabla ya kutokea, bila kizuizi. Na kwa ajili hii Amesema baada ya hapa:

وَأَحَاطَ بِمَا لَدَيْهِمْ وَأَحْصَىٰ كُلَّ شَيْءٍ عَدَدًا ﴿١٢﴾

“Na Yeye Anajua vyema yote walionayo na Amedhibiti idadi ya kila kitu.”

Mwisho wa suratu *Aljinni*. Kuhimidiwa ni kwa Allah تعالی na Kuneemesha.

* * *

Tafsiri ya Suratul Muzzammil

Sura ya 73

Iliteremshwa Makkah

Sababu ya Kushuka Sura Mbili, *Al-Muzzammil* na *Al-Muddathir*:

Haafidh Abu Bakr Ahmad Al-Bazaar رحمه الله تعالى amepokea toka kwa Jaabir amesema: Makureishi walikusanyika katika ukumbi: - *An-Nadwah* wakasema: Mtu huyu mpeni jina baya litakalowafanya watu wasimkubali. Wakasema: 'tumuite kuhani'. Wakasema: 'sio kuhani'. Wakasema basi tumuite: 'Mwenda wazimu'. Wakasema: 'sio mwenda wazimu'. Wakasema tumuite: 'mchawi.' Wakasema hapana: 'sio mchawi.' Washirikina wakatofautiana juu ya hilo, habari hiyo ikamfikia Mtume ﷺ, akajifunika nguo zake, Jibril عليه السلام akamjia Mtume ﷺ, akamuambia,

يَا أَيُّهَا الْمُزَّمِّلُ

"Ewe uliye jifunika!"

يَا أَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ

"Ewe uliye jifunika nguo!"

* * *

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْمُزَّمِّلِ

يَتَأْتِيَ الْمُزْمِلُ ﴿١﴾ قُمْ أَلَيْلَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢﴾ نِصْفَهُ أَوْ
 أَنْقُصْ مِنْهُ قَلِيلًا ﴿٣﴾ أَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلًا
 ﴿٤﴾ إِنَّا سَنُلْقِي عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيلًا ﴿٥﴾ إِنَّ نَاشِئَةَ اللَّيْلِ
 هِيَ أَشَدُّ وَطْأًا وَأَقْوَمُ قِيلًا ﴿٦﴾ إِنَّ لَكَ فِي النَّهَارِ سَبْحًا
 طَوِيلًا ﴿٧﴾ وَادْكُرْ اسْمَ رَبِّكَ وَتَبَتَّلْ إِلَيْهِ تَتْتِيلًا ﴿٨﴾ رَبُّ
 الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿٩﴾ وَأَصْبِرْ
 عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَاهْجُرْهُمْ هَجْرًا حَمِيلًا ﴿١٠﴾ وَذَرِنِي
 وَالْكَذِبِينَ أُولَىٰ النِّعْمَةِ وَمَهْلَهْرٍ قَلِيلًا ﴿١١﴾ إِنَّ لَدَيْنَا
 أَنْكَالًا وَحِمِيمًا ﴿١٢﴾ وَطَعَامًا ذَا غُصَّةٍ وَعَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٣﴾
 يَوْمَ تَرْجُفُ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ وَكَانَتِ الْجِبَالُ كَثِيبًا مَهِيلًا
 ﴿١٤﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَا أَرْسَلْنَا
 إِلَىٰ فِرْعَوْنَ رَسُولًا ﴿١٥﴾ فَعَصَىٰ فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ
 فَأَخَذْنَاهُ أَخْذًا وَبِيلًا ﴿١٦﴾ فَكَيْفَ تَتَّقُونَ إِنْ كَفَرْتُمْ يَوْمًا
 يَجْعَلُ الْوِلْدَانَ شِيبًا ﴿١٧﴾ الْأَسْمَاءُ مُنْفِطِرَةٌ بِهِ ؕ كَانَ وَعْدُهُ
 مَفْعُولًا ﴿١٨﴾

يَتَأْتِيَ الْمُزْمِلُ ﴿١﴾ قُمْ أَلَيْلَ إِلَّا
 قَلِيلًا ﴿٢﴾ نِصْفَهُ أَوْ أَنْقُصْ مِنْهُ
 قَلِيلًا ﴿٣﴾ أَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَتِّلِ
 الْقُرْآنَ تَرْتِيلًا ﴿٤﴾ إِنَّا سَنُلْقِي
 عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيلًا ﴿٥﴾ إِنَّ نَاشِئَةَ
 اللَّيْلِ هِيَ أَشَدُّ وَطْأًا وَأَقْوَمُ قِيلًا ﴿٦﴾
 إِنَّ لَكَ فِي النَّهَارِ سَبْحًا طَوِيلًا ﴿٧﴾
 وَادْكُرْ اسْمَ رَبِّكَ وَتَبَتَّلْ إِلَيْهِ تَتْتِيلًا
 ﴿٨﴾ رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ
 إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿٩﴾

1. Ewe uliyejifunika nguo!
2. Simama usiku kucha, ila kidogo tu!
3. Nusu yake, au ipunguze kidogo.
4. Au izidishe - na soma Qur'ani kwa utaratibu na utungo.
5. Hakika Sisi Tutakute-remshia kauli nzito.

6. Hakika kuamka usiku kunawafikiana zaidi na moyo, na maneno yake yanatua zaidi.

7. Kwani hakika mchana una shughuli nyingi.

8. Na lidhukuru jina la Mola Wako Mlezi, na ujitolee Kwake kwa ukamilifu.

9. Mola Mlezi wa mashariki na magharibi, hapana muabudiwa isipokuwa Yeye, basi mfanye kuwa Mtegemewa Wako.

Amri ya Kusimama Usiku Kufanya Ibada.

Allah تعالیٰ Anamuamrisha Mtume Wake ﷺ kuacha kujifunika usiku na kuinuka kwa ajili ya Mola Wake Mtukufu. Kama Alivyosema:

تَتَجَافَى جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ خَوْفًا وَطَمَعًا وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿١٦﴾

“Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumuabudu Mola Wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na Tulivyowaruzuku.” (32:16)

Kadhalika Mtume ﷺ alikuwa akitii amri ya Allah تعالیٰ katika kisimamo cha usiku, na ilikuwa ni wajibu kwake peke yake Kama Allah تعالیٰ Alivyosema:

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٧٩﴾

“Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya sunna khasa kwako wewe. Huenda Mola Wako Mlezi Akakunyanyua cheo kinacho sifika.” (17:79)

Hapa Amebainisha kiasi anachotakiwa kusimama (Usiku) akasema:

يَتَأْتِيَ الْمُرْمِلُ ﴿٧٩﴾ قُمْ أَلَيْسَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٨٠﴾

“Ewe uliyejifunika nguo!, Kesho usiku kucha, ila kidogo tu!”

Ibn Abbaas, adh-Dhahaak, na Sudi رضي الله عنهم wamesema:

يَتَأْتِيَ الْمُرْمِلُ ﴿٧٩﴾

“Ewe uliyejifunika!” Maana yake: Ewe mwenye kulala, Qatadah amesema: Mwenye kujifunika nguo zake, na Kauli Yake تعالیٰ:

نُصِّفَهُ

“Nusu yake.” (73:3)

Ni sehemu ya usiku.

أَوْ أَنْقُصَ مِنْهُ قَلِيلاً ﴿٣﴾ أَوْ زِدَ عَلَيْهِ

“Au ipunguze kidogo. Au izidishe”.

Maana yake: Tumekuamuru kusimama nusu ya usiku kwa kuzidisha kidogo au kupunguza kidogo hakuna ubaya wowote katika hilo.

Njia ya Kusoma Qur’ani

Kauli Yake Allah تعالیٰ:

وَرَتَّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلاً ﴿١٠﴾

“Na soma Qur’ani kwa utaratibu na utungo.”

Maana yake: Soma kwa utulivu kwani kufanya hivyo itakusaidia kufahamu Qur’ani na kuizingatia.

Hivyo, ndivyo alivyokuwa Mtume ﷺ akisoma. Aishah رضي الله عنها amesema: ‘Mtume ﷺ alikuwa akisoma sura moja na huisoma vizuri kwa *tartili* (utungo) mpaka inakuwa ndefu kuliko urefu wake.’¹

Na imekuja katika Sahihi Bukhari kutoka kwa Anas رضي الله عنه aliulizwa kuhusu kisomo cha Mtume ﷺ, akasema: Alikuwa akivuta, kisha akasoma:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

“Bismillaahir Rahmanir Rahiim.” (1:1)

‘Anavuta *Bismilaahi*, anavuta *Ar Rahmaani*, na anavuta *Ar Rahiim*.² Ibn Juraij anasema: Imetoka kwa Abu Mulaikah kutoka kwa Ummu Salamah رضي الله عنها aliulizwa kuhusu usomaji wa Mtume ﷺ akasema: ‘Katika usomaji wake alikuwa akisoma aya moja moja.’

¹ Muslim 1:507.

² *Fat’h Al-Bari* 8:709.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿١﴾ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٢﴾ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٣﴾
مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٤﴾

***“Bismillaahir Rahmanir Rahiim, Alhamdulillah rabbil ‘aalamiin,
ar Rahmanir ar Rahiim, Maaliki yawmid’diin.” (1:1-4)***

Ameipokea Ahmad, Abuu Dawud na Tirmidhi.³ Tumetanguliza mwanzoni mwa tafsiri, Hadithi zinazofahamisha upendekezaji wa kuisoma Qur’an vizuri kwa sauti nzuri kama ilivyokuja katika Hadithi:

«زَيُّتُوا الْقُرْآنَ بِأَصْوَاتِكُمْ»

“Ipambeni Qur’an kwa sauti zenu.”¹

Na katika Hadithi nyingine,

«لَيْسَ مِنَّا مَنْ لَمْ يَتَعَنَّ بِالْقُرْآنِ»

“Si katika sisi asiyeghani Qur’an.”²

Na katika Hadithi,

«لَقَدْ أُوتِيَ هَذَا مِزْمَارًا مِنْ مَزَامِيرِ آلِ دَاوُدَ»

“Hakika huyu amepewa zumari miongoni mwa zumari za watu wa Daudi.”³

Maana yake: Abu Musa akasema, ‘Lau ningejua kuwa wewe ulikuwa unanisikiliza kisomo changu, ningekifanya vizuri kwa ajili yako’. Na nimeipokea kutoka kwa Ibn Masuud رضى الله عنه amesema: ‘Msiisome Qur’an ovyo ovyo, na wala msimbe mfano wa utenzi, simameni mfikapo katika mambo yenye kushangaza, na nyoyo zisisimkwe kwa Qur’an, na wala hamu ya mmoja wenu isiwe ni (kufika) mwisho wa sura.’ Ameipokea Baghawi رحمه الله تعالى.⁵ Al-Bukhari

¹ Ahmad 6:302, Abu Dawud 4:294, na *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:241.

² *Fat’h Al-Bari* 13:527.

³ *Fat’h Al-Bari* 8:510.

⁴ *Fat’h Al-Bari* 8:710.

⁵ *Ma’alim At-Tanzil* 8:215.

رحمته الله تعالى amenukuu kutoka kwa Abi Wail kuwa alisema: Alikuwa mtu mmoja kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه na akasema, "Nimesoma sura za *Mufasswal* (kuanzia *Qaf* mpaka *An-Nas*) usiku uliopita katika rakaa moja. Ibn Mas'ud رضي الله عنه akasema, 'huko ni kuharakisha kama haraka ya usomaji mashairi. Kwa hakika, ninazijua jozi (za sura) alizokuwa akisoma Mtume ﷺ katika Sala.' Kisha akataja sura ishirini katika *Mufasswal* na kusema kuwa, 'Mtume alikuwa akizisoma sura mbili katika rakaa moja.'¹

Utukufu wa Qur'ani

Kauli Yake تعالى:

إِنَّا سَنُلْقِي عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيلًا ﴿٥﴾

"Hakika Sisi Tutakuteremshia kauli nzito." (73:5)

Hasan na Qatadah wamesema: Maana yake: Kuitumia. Imesemwa: Nzito wakati wa kushuka kwake kutokana na utukufu wake. Kama alivyosema Zayd bin Thaabit, 'Imeshushwa Qur'an kwa Mtume ﷺ na paja lake likiwa juu ya paja langu, basi paja langu likatikiswa kwa nguvu.'²

Imamu Ahmad رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Abdillaahi bin Umar رضي الله عنه amesema: Nilimuuliza Mtume ﷺ: 'Ewe Mtume je unapata hisia gani wahyi unaposhuka?' Mtume ﷺ akasema:

«أَسْمَعُ صَلَاحٍ لِّمَنْ أَتَيْتُهُ مِنْ مَّرَّةٍ يُوحَىٰ إِلَيَّ إِلَّا ظَنَنْتُ أَنْ تَنْبِئَنِي
تَنْبِئَنِي»

*"Nasikia kishindo kikubwa, kisha hunyamaza. Na si mara moja wahyi unapoteremshwa juu yangu ila nahisi kama natolewa roho."*³

Ameipokea Ahmad peke yake. Na katika mwanzo wa Sahihi Bukhari, kutoka kwa Aishah رضي الله عنها kuwa Haarithah bin Hishaam رضي الله عنه alimuuliza Mtume ﷺ: 'Wahyi unakuja katika taswira gani?' Akasema:

¹ *Fat'hul Al-Bari* 2:298.

² *Fat'hul Al-Bari* 8:108.

³ Ahmad 2:222.

«أَخْيَانًا يَأْتِي فِي بَيْتِ صَلَٰةِ الْجَرَسِ وَهُوَ أَشَدُّ عَلَيَّ، فَيَقْضِمُ عَنِّي وَقَدْ وَعَيْتُ عَنْهُ
مَا قَالَ، وَأَخْيَانًا يَتَمَثَّلُ لِي الْمَلَكُ رَجُلًا فَيَكَلِّمُنِي فَأَعْبِي مَا يَقُولُ»

“Mara nyingine unakuja mfano wa mlio wa kengele na taswira hiyo ndio kali zaidi, na hiyo huniumiza na huwa nimezingatia aliyoyasema, na mara nyingine hunijia malaika kwa mfano wa mtu hunizungumzisha, kwa hiyo ninazingatia anayosema.”

Aishah رضي الله عنها anasema: ‘Nilimuona Mtume ﷺ akijiwa na wahyi katika siku ya baridi kali inamuumiza na huku paji lake la uso likaloo jasho’ na huu ni upokezi wa Al-Bukhari رحمه الله تعالى.¹ Imamu Ahmad رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Aishah رضي الله عنها kuwa amesema: ‘Mtume alikuwa akijiwa na wahyi, na hali ya kuwa yuko juu ya mnyama wake basi hapo hujipiga mnyama huyo na shingo yake’.² Na hili amelichagua Ibn Jariir رحمه الله تعالى, kuwa ni nzito, katika hali zote mbili, kama alivyosema Abdur Rahman bin Zayd bin Aslam: Kama ilivyokuwa nzito katika dunia itakuwa nzito akherah katika mizani.

Utukufu wa Kisimamo cha Usiku

Kauli Yake تعالى:

إِنَّ نَاشِئَةَ اللَّيْلِ هِيَ أَشَدُّ وَطْأًا وَأَقْوَمُ قِيْلًا ﴿٦﴾

“Hakika kuamka usiku kunawafikiana zaidi na moyo, na maneno yake yanatua zaidi.”

Umar, Ibn Abbaas na Ibn Zubair رضي الله عنهم wamesema: Usiku wote ni kisimamo (*Naashiah*)³. Kadhalika amesema Mujaahid na wengine.⁴ Katika lugha ya kiarabu husemwa, ‘*Nashi-a*’ kwa mtu aliyesimama usiku, na katika riwaya nyingine toka kwa Mujaahid: ‘Ni baada ya Isha’.⁵ Kadhalika amesema Abu Mijlaz, Qatadah, Salim, Abu Haazim na Muhammad bin Munkadir;⁶ “Lengo la kisimamo cha usiku ni saa na nyakati zake.”

Na kila muda katika usiku huo huitwa, ‘*Naashiatah*’, na hizo ni nyakati, Na Kusudio ni kuwa kisimamo cha usiku kinathibiti vizuri katika moyo na ulimi. Hujumuisha usomaji mzuri na wa makini. Kwa ajili hii Allah تعالى Amesema:

¹ *Fat’hul Al-Bari* 1:25.

² Ahmad 6:118.

³ At-Tabari 23:683.

⁴ At-Tabari 23:682.

⁵ At-Tabari 23:682.

⁶ At-Tabari 23:683.

هِيَ أَشَدُّ وَطَقًا وَأَقْوَمُ قِيلاً ﴿٦﴾

“Kunawafikiana zaidi na moyo, na maneno yake yanafahamika zaidi.”

Maana yake: Akili inakubali kusoma vizuri na kufahamu kinachosomwa kuliko kisimamo cha mchana, kwa sababu mchana ni wakati wa kutawanyika watu na mchanganyiko wa sauti pamoja na kutafuta maisha. Haafidh Abu Ya’alaa Mauswily رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Al-Aamashi kwamba: Anas bin Maalik رضي الله عنه amesoma aya hii:

إِنَّ نَاشِئَةَ اللَّيْلِ هِيَ أَشَدُّ وَطَقًا وَأَقْوَمُ قِيلاً ﴿٦﴾

“Hakika kuamka usiku kunawafikiana zaidi na moyo, na maneno yake yanafahamika.”

Mtu mmoja akamuambia: sisi tunaisoma:

وَأَقْوَمُ قِيلاً ﴿٦﴾

“Maneno yake yanapatia zaidi.” (73:6) Akasema: Hakika: Aswwaba (kupatia), Aqwama (Kunyooka), Ahyaa (Kusahihika) na mfano wake yote hayo yana maana moja.¹ Kwa hili Allah تعالى Amesema;

إِنَّ لَكَ فِي النَّهَارِ سَبْحًا طَوِيلًا ﴿٦﴾

“Kwani hakika mchana una shughuli nyingi.” Ibn Abbaas, Ikrimah, na Atwaa bin Abu Muslim رضي الله عنهم wamesema: Faragha na kulala.² Abul ‘Aaliyah, Mujaahid, Abu Maalik, Adh-Dhahak, Hasan, Qatadah, Rabii bin Anas na Sufiyaan Thaury wamesema: Faragha ndefu. Qatadah amesema; faragha, mahitaji, na mizunguko. Abdur Rahmaan bin Zaid bin Aslam amesema katika Kauli Yake تعالى:

إِنَّ لَكَ فِي النَّهَارِ سَبْحًا طَوِيلًا ﴿٦﴾

“Kwani hakika mchana una shughuli nyingi.” (73:6)

Amesema: Kwa ajili ya haja zako basi utumie usiku kwa ajili ya Dini yako. Amesema; Na Hili ni wakati Sala ya usiku ilipokuwa lazima. Kisha Allah تعالى

¹ Musnad Abu Ya’ala 7:88.

² At-Tabari 23:686, na Al-Qurtubi 19:42.

Akaneemesha kwa waja Wake kwa kufanya tahafifu na kuiondoa, akasoma:

﴿قُمِ اللَّيْلَ إِلَّا قَلِيلًا﴾

“Kesha usiku kucha, ila kidogo tu!”

Hadi mwisho wa aya, kisha akasoma,

﴿إِنَّ رَبَّكَ يَعْلَمُ أَنَّكَ تَقُومُ أَدْنَىٰ مِن ثُلُثِي اللَّيْلِ وَنِصْفَهُ﴾

“Hakika Mola Wako Mlezi Anajua ya kuwa hakika wewe unakesha karibu na thuluthi mbili za usiku, na nusu yake.” (73:20)

Mpaka akafika,

﴿فَأَقْرءُوا مَا تَيَسَّرَ مِنْهُ﴾

“Basi someni kilicho chepesi katika Qur’ani.”¹ (73:20)

Akasema تعالى:

﴿وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَن يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا﴾

“Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya sunnah khasa kwako wewe. Huenda Mola Wako Mlezi Akakunyanyua cheo kinachosifika.”² (17:79)

Hili ambalo amelisema ni kama alivyosema (Abdur Rahmaan). Na ushahidi juu ya hilo ni Hadithi aliyoipokea Imamu Ahmad katika Musnadi wake kutoka kwa Saiid bin Hishaam kwamba yeye alimuacha mke wake, kisha akasafiri kwenda Madina ili auze ardhi yake, na fedha (za ardhi hiyo) anunulie wanyama na silaha kisha aende kupigana jihadi dhidi ya Warumi mpaka atakapokufa, Akakutana na kikundi katika watu wake wakamuambia kuwa watu sita katika jamaa zake wametaka kufanya hilo hilo, katika wakati wa Mtume ﷺ akasema:

﴿أَلَيْسَ لَكُمْ فِي آسْوَةِ حَسَنَةٍ؟﴾

“Kwani nyie kutoka kwangu hamna kiigizo chema?”

Akawakataza hilo akawashuhudisha juu ya kurejea kwake, kisha akarudi kwetu akatuambia kuwa alimuendea Ibn Abbaas رضي الله عنهما akamuuliza kuhusu Sala

¹ At-Tabari 23:686

² Angalia maelezo ua juzuu ya sita.

ya Witri akasema: 'Nikufahamishe mjuzi zaidi wa watu katika ardhi kwa witri ya Mtume?' Akamjibu: 'Ndio.' Akasema, 'Muendee Aisha رضي الله عنها muulize, kisha rudi tena kwangu uniambie majibu yake kwako.' Akasema: 'Nimemuendea Hakim bin Aflah nikamuomba twende naye kwake, akasema, 'Sitaki kumkaribia, nilimkataza kusema chochote kuhusu makundi hayo mawili (la Ali na la Muawiyah رضي الله عنهما), akakataa na akaendelea kujihusisha nayo (katika ugomvi wao). Nikamuapia, basi tukaenda naye, na tukaingia (kwa Aisha رضي الله عنها). Aisha رضي الله عنها akauliza lakini anamjua. Akasema (Aisha رضي الله عنها): 'Ni nani huyu uliyekuja naye?' Akamjibu: 'Ni Saidi bin Hishaam'. Akauliza: 'ni nani Hishaam?' 'Akajibu, 'Ibn Aamir.' Akasema: Akamuomba rehema. Kisha akasema: 'Aamir alikuwa mtu bora.' Nikauliza: 'Ewe Mama wa waumini niambie kuhusu tabia ya Mtume ﷺ.' Akasema: 'kwani wewe husomi Qur'ani.' Nikajibu: 'kwanini?'. Akasema: 'Kwa hakika tabia za Mtume ﷺ ilikuwa ni Qur'ani.' Nikataka kuondoka nikakumbuka kisimamo cha Mtume ﷺ, nikauliza: 'Ewe Mama wa waumini niambie kuhusu kisimamo cha Mtume?' Akasema: 'Kwani wewe husomi Sura Hii:

بَيِّنَاتٍ آتَمَّتْ

"Ewe uliyejifunika!" (73:1) Nikasema: "Kwanini, ninasoma.' Akasema: 'Hakika Allah تعالى Alifaradhisha kisimamo cha usiku mwanzoni mwa sura hii. Kwa hiyo Mtume ﷺ akasimama kusali na Sahaba wake mwaka mzima mpaka miguu yao ikavimba. Allah تعالى Akazuia hitimisho lake kwake mbinguni kwa miezi kumi na mbili. Kisha Allah تعالى Akateremsha unafuu mwisho wa sura hii, kwa hiyo kisimamo cha usiku kikawa ni hiari baada ya kuwa faradhi."

Nikataka kuondoka, kisha likanijia swali la Witri ya Mtume ﷺ, nikauliza: "Ewe mama wa waumini nihabarishe kuhusu Sala ya Witri ya Mtume?' Akasema: 'Tulikuwa tukimuandalia mswaki wake na maji yake, kisha Allah تعالى humpeleka kwa namna atakayo kumpeleka usiku, kwa hiyo atapiga mswaki, atatawadha kisha anasali rakaa nane, na wala hakai katika hizo isipokuwa katika rakaa ya nane, atakaa na kumtaja Mola Wake, na anaomba na anainuka na hatoi salamu, kisha anasimama kwa ajili ya rakaa ya tisa, kisha anakaa anamtaja Allah تعالى Peke Yake, kisha anamuomba kisha anatoa salamu tunayoisikia, kisha anasali rakaa mbili akiwa amekaa baada ya kutoa salamu, hizo ni rakaa kumi na moja. Ewe mwanangu, Mtume ﷺ alipokuwa mzee na akawa mnene, alisali Witri rakaa saba, kisha anasali rakaa mbili, akiwa anakaa baada ya kutoa salamu, hizo ni rakaa tisa. Ewe mwanangu, na Mtume ﷺ, alikuwa akisali Sala alipenda

kudumu juu yake, na alikuwa akishughulishwa na kisimamo cha usiku, kwa kulala au maradhi basi huisali mchana rakaa kumi na mbili, na wala sijui kwamba Mtume ﷺ alisoma Qur’ani usiku wote mpaka kukicha, wala kufunga mwezi kamili zaidi ya Ramadhani.” Nikamuendea Ibn Abbaas رضي الله عنهما nikamhadithia mazungumzo yake (Aishah رضي الله عنها), akasema, ‘amesema kweli, ama mimi lau ningekuwa naingia kwake ningemuendea anihadithie kwa mdomo wake.’¹ Hivi ndivyo alivyoipokea Ahmad, kwa ukamilifu wake, Muslimu ameitoa katika sahihi yake kwa mfano huo huo.² Ibn Jariir رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Abi Abdir Rahman amesema: iliposhuka,

يَتَأْتِيَا الْمُرْمِلُ ﴿١﴾

“Ewe uliyejifunika nguo!” (73:1)

Walisimama mwaka mmoja hadi miguu yao ikavimba mpaka iliposhuka,

فَأَقْرَهُوْا مَا تَيَسَّرَ مِنْهُ

“Basi someni kilicho chepesi katika Qur’ani.” (73:20).

Amesema: ‘Watu wakapumzika.’³ Kama hivi amesema: Hasan Baswiry na Sudy⁴, Ali bin Abi Twalha amesema kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما katika Kauli Yake تعالى:

قُرِ الْيَلَّ إِلَّا قَلِيلاً ﴿٢﴾ نَضَفَهُ أَوْ أَنْقَصَ مِنْهُ قَلِيلاً ﴿٣﴾

“Ewe uliye jifunika nguo! Kesho usiku kucha, ila kidogo tu!” (73:1-2)

Hilo likawasumbua waumini. Kisha Allah تعالى Akawahafifishia, na Kuwahurumia. Akateremsha baada ya hapa:

عَلِمَ أَنْ سَيَكُونُ مِنْكُمْ مَرْضًى ۖ وَأَآخِرُونَ يَضْرِبُونَ فِي الْأَرْضِ يَبْتَغُونَ مِنْ فَضْلِ اللَّهِ ۖ

“Anajua ya kuwa baadhi yenu watakuwa wagonjwa, na wengine wanasafiri katika ardhi wakitafuta Fadhila ya Mwenyezi Mungu,”.

Mpaka Kauli Yake,

¹ Ahmad 6:53.

² Muslim 1:512.

³ At-Tabari 23:679.

⁴ At-Tabari 23:680.

فَأَقْرءُوا مَا تَيَسَّرَ مِنْهُ

“Basi someni kilicho chepesi katika Qur’ani.” (73:20)

Allah تعالى ni Zake Sifa Njema Akafanya wepesi na wala hakuwafanya wawe katika tabu.¹ Na Kauli Yake تعالى:

وَأَذْكُرِ اسْمَ رَبِّكَ وَتَبَتَّلْ إِلَيْهِ تَتَبِيلًا ﴿٨﴾

“Na lidhukuru Jina la Mola Wako Mlezi, na ujitolee kwake kwa ukamilifu.” (73:8)

Maana yake: Zidisha kumtaja ujibidiishe Kwake na utenge muda wa ibada pindi unapomaliza shughuli zako na unayoyahitaji katika mambo yako ya dunia. Kama Alivyosema Allah تعالى:

فَإِذَا فَرَغْتَ فَانصَبْ ﴿٧﴾

“Na ukipata faragha, fanya juhudi.” (94:7)

Maana yake: Ukishamaliza shughuli zako jipinde katika kumtii yeye ili uwe mtulivu wa akili. Amelisema Ibn Zaid kwa maana yake au karibu na hivyo.² Ibn Abbaas Mujaahid, Abu Swaalih, Atwiyah, Adh-Dhahaak na Sudy رضي الله عنهم wamesema:

وَتَبَتَّلْ إِلَيْهِ تَتَبِيلًا ﴿٨﴾

“Na ujitolee Kwake kwa ukamilifu.” Maana yake: Mtakasie Yeye ibada.³ Hasan amesema: Jitahidi na isabilie kwako nafsi yako.⁴ Ibn Jariir رحمه الله تعالى amesema: Mwenye kushikamana na ibada anaitwa *mutabattil*. Na kwa kuzingatia hilo imepokewa Hadithi: ‘Mtume ﷺ Amekataza *tabattul*.’ Yaani kuacha kuoa kwa sababu ya kushughulika na ibada.⁶ Na Kauli Yake:

رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿٥﴾

“Mola Mlezi wa mashariki na magharibi, hapana Mola isipokuwa Yeye, basi mfanye kuwa Mtegemewa wako.”

¹ At-Tabari 23:679.

² At-Tabari 6:689.

³ At-Tabari 23:688.

⁴ At-Tabari 23:688.

⁵ At-Tabari 23:687.

Maana yake: Yeye Ndie Mfalme Mwenye Kuendesha mashariki na magharibi, ambaye hapana mola isipokuwa Yeye, na kama ulivyompwekesha katika ibada hivyo hivyo mpwekeshe katika kumtegemea Yeye, na kumfanya Mlinzi. Kama Alivyosema katika aya nyingine:

فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ

“Basi muabudu na umtegemea Yeye.” (11:123)

Kama Kauli Yake تعالى

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

“Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada.” (1:5)

Aya zinazoelezea maana hii zipo nyingi, ndani yake kuna amri ya Kumpwekesha kwa ibada, Kumtii Mwenyezi Mungu na Kumhusisha katika ibada na Kumtegemea Yeye Pekee.

وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَاهْجُرْهُمْ هَجْرًا حَسِيلًا ﴿١٠﴾ وَذَرْنِي وَالْمُكَذِّبِينَ أُولِي النَّعْمَةِ
 وَمَهْلُومٍ قَلِيلًا ﴿١١﴾ إِنَّ لَدَيْنَا أَنكَالًا وَحَصِيمًا ﴿١٢﴾ وَطَعَامًا ذَا غُصَّةٍ وَعَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٣﴾
 يَوْمَ تَرْجُفُ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ وَكَانَتِ الْجِبَالُ كَثِيبًا مَّهِيلًا ﴿١٤﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا
 شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَا أَرْسَلْنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ رَسُولًا ﴿١٥﴾ فَعَصَىٰ فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ فَأَخَذْنَاهُ
 أَخْذًا وَبِيلًا ﴿١٦﴾ فَكَيْفَ تَتَّقُونَ إِن كَفَرْتُمْ يَوْمًا يَجْعَلُ الْوِلْدَانَ شِيبًا ﴿١٧﴾ السَّمَاءُ مُنْفَطِرٌ
 بِهِ ؕ كَانَ وَعْدُهُ مَفْعُولًا ﴿١٨﴾

10. Na vumilia hayo wayasemayo, na jitenge nao kwa vizuri.

11. Na niache Mimi na hao wanaokanusha, walioneemeka; na wape muhula kidogo!

12. Hakika Sisi Tunazo pingu nzito na Moto unaowaka kwa ukali kabisa!

13. Na chakula kinacho kwama kooni, na adhabu inayoumiza.

14. Siku ambayo ardhi itatikiswa na milima pia, na milima itakuwa kama tifutifu la mchanga!

15. Hakika Sisi Tumemtuma kwenu Mtume aliye shahidi juu yenu, kama Tulivyomtuma Mtume kwa Firauni.

16. Lakini Firauni alimuasi huyo Mtume, basi Tukamshika mshiko wa mateso.

17. Basi nyinyi mkikufuru, mtawezaje kujikinga na Siku ambayo itawafanya watoto wadogo waote mvi?

18. Hapo mbingu zitapasuka! Ahadi Yake itakuwa imetekelezwa.

Amri ya Kusubiri Maudhi ya Makafiri na Ubainifu wa Adhabu Yao.

Allah تعالى Anasema Akimuamrisha Mtume Wake ﷺ kusubiri juu upingaji unaofanywa na wapumbavu katika watu wake. Na awahame kwa kutumia njia nzuri nayo ni ile ambayo haitamletea usumbufu yeye. Na kuwatisha kuwa Allah ni Mkuu Ambaye Akighadhibika hakibaki chochote.

وَذَرْنِي وَالْمُكَذِّبِينَ أُولَى النَّعْمَةِ

“Na Niache Mimi na hao wanaokanusha, walioneemeka.”

Maana yake: Niache na wakadhibishaji matajiri wenye mali, kwani wao juu ya utii wa Mola wao wanaweza zaidi kuliko wengine, na wao wanatakiwa kutekeleza haki ambayo hawaimiliki wengine.

وَمَهْلَهْمُ قَلِيلاً

“Na wape muhula kidogo!” Maana yake: Kidogo kidogo,

Kama Alivyosema Allah تعالى:

نُمَتِّعُهُمْ قَلِيلاً ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ

“Tunawastarehesha kwa uchache, kisha Tutawasukuma kwenye adhabu ngumu.” (31:24)

Kwa Ajili ya hii Amesema hapa:

إِنَّ لَدَيْنَا أَنْكَالًا

“Hakika Sisi Tunazo pingu nzito.” Nazo ni pingu. Kauli hiyo ni ya Ibn Abbaas, Ikrimah, Twaawuus, Muhammad bin Ka’ab, Abdullaahi bin Buraydah, Abuu Mijlaz, Adh-Dhahaak, Hammaad bin Abi Sulaimaan, Imraani Juwain, Qatadah, Sudi, Ibnul Mubaarak, Thauri na wengine رضي الله عنهم.¹

¹ At-Tabari 23:690, 691, na Ad-Durr Al-Manthur 8:319.

وَحِيمًا ﴿١٧﴾

“na Moto.” Huo ni moto wenye kutoa miale,

وَطَعَامًا ذَا غُصَّةٍ ﴿١٨﴾

“Na chakula kinacho kwama kooni.”

Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, ‘Kinakwama kooni hakiingii wala hakitoki’.¹

وَعَدَابًا أَلِيمًا ﴿١٩﴾ يَوْمَ تَرْجُفُ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ

“Na adhabu inayoumiza siku ambayo ardhi itatikiswa na milima pia.”

Maana yake: Itatetemeshwa,

وَكَانَتْ الْجِبَالُ كَثِيبًا مَّهِيلًا ﴿٢٠﴾

“Na milima itakuwa kama tufufu la mchanga.” Maana yake: Itakuwa kama kichuguu cha mchanga, baada ya kuwa ilikuwa mawe magumu. Kisha itasagwa sagwa hakubakii humo chochote isipokuwa kimeondoka, hadi ardhi ibakie uwanja tambarare, huoni humo bonde wala konakona. Maana yake: Kichuguu wala chochote, hakuna mwinuko wala mporomoko.

Mtume Wenu ﷺ ni Kama Mtume Musa عليه السلام kwa Firauni na Matokeo ya Firauni Mnayajua

Kisha Allah تعالى Anasema Akiwahutubia makafiri wa Kikureishi, na kusudio hapa, ni watu wote,

إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ

“Hakika Sisi Tumemtuma kwenu Mtume aliye shahidi juu yenu.”

Maana yake: Matendo yenu,

كَمَا أَرْسَلْنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ رَسُولًا ﴿٢١﴾ فَعَصَىٰ فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ فَأَخَذْنَاهُ أَخْذًا وَبِيلاً ﴿٢٢﴾

“Kama Tulivyomtuma Mtume kwa Firauni. Lakini Firauni alimuasi Mtume huyo, basi Tukamuadhibu adhabu kali.”

Ibn Abbaas, Mujaahid, Qatadah, Sudi, na Thaury رضي الله عنهم wamesema:

¹ At-Tabari 23:691.

أَخَذًا وَبَيْلًا ﴿٧٣﴾

“Adhabu kali.”

Maana yake: Chungu.¹ Maana yake ingine: Jihadharisheni nyinyi kumkadhibisha Mtume huyu msije mkapatwa na yaliompata Firauni. Allah تعالی Alivyomuadhibu kwa Adhabu Yake. Naye ni Mwenye Nguvu na Uwezo. Kama Alivyosema Allah تعالی,

فَأَخَذَهُ اللَّهُ نَكَالَ الْأَخْزَرَةِ وَالْأُولَىٰ ﴿٧٩﴾

“Basi hapo Mwenyezi Mungu Akamuadhibu adhabu ya mwisho na ya mwanzo.” (79:25).

Nyinyi ni aula wa kuangamia kama mkimkadhibisha Mtume wenu, kwa kuwa Mtume wenu ni mtukufu na adhimu mno, kuliko Musa bin Imraan عليه السلام. Haya yamepokewa toka kwa Ibn Abbaas na Mujaahid رضي الله عنهما.

Uhofishaji wa Adhabu ya Siku ya Kiama

Kauli Yake تعالی,

فَكَيْفَ تَتَّقُونَ إِنْ كَفَرْتُمْ يَوْمًا يَجْعَلُ الْوِلْدَانَ شِيبًا ﴿٧٤﴾

“Basi nyinyi mkikufuru, mtawezaje kujikinga na Siku ambayo itawafanya watoto wadogo waote mvi?”

Ibn Jariir رحمه الله تعالی amesimulia kutoka kwenye kisomo cha Ibn Mas’ud عنه رضي الله عنه, “Basi vipi mnahofia enyi watu siku itakayo wafanya watoto kuwa na mvi kama mkimkufuru Allah تعالی na hamkumuamini Yeye?”²

Aidha inawezekana Maana Ikawa: ‘Vipi itapatikana amani kutokana na siku hii kama mkikufuru, au vipi utapatikana kwenu uchamungu kama mkikufuru siku ya Kiama.’ Na maana zote hizo ni sahihi, lakini maana ya kwanza ni aula, na Allah تعالی ni Mjuzi zaidi. Na Maana ya Kauli Yake:

يَوْمًا يَجْعَلُ الْوِلْدَانَ شِيبًا ﴿٧٤﴾

“Siku ambayo itawafanya watoto wadogo waote mvi?”

¹ At-Tabari 23:693.

² At-Tabari 23:694.

Maana yake: Kutokana na ukali wa vituko, balaa, tetemeko, na kelele zake. Na hilo ni wakati Allah تعالى Atakapomuambia Adam عليه السلام: "Peleka watu wa motoni." Atasema: 'Kuanzia wangapi?' Atasema: 'kila elfu moja, mia tisa tisini na tisa ni motoni, na mmoja tu ndio wa peponi.'" Na Kauli Yake,

أَلْسَمَاءُ مُنْفَطِرٌ بِهِ

"Hapo mbingu zitapasuka!"

Amesema Al-Hasan na Qatadah: Kwa maana: Kupasuka huko ni kutokana na shida na kitisho cha siku hiyo.

كَانَ وَعْدُهُ مَفْعُولًا

"Ahadi Yake itakuwa imetekelezwa." (73:18)

Maana yake: Miadi ya siku hii itatekelezwa. Maana yake: Itatokea bila shaka na itakuwa bila kipingamizi.

* * *

إِنَّ هَدِيمَهُ تَذَكِيرَةٌ ۖ فَمَنْ شَاءَ اتَّخَذْ إِلَىٰ رَبِّهِ سَبِيلًا ﴿١٩﴾
 * إِنَّ رَبَّكَ يَعْلَمُ أَنَّكَ تَقُومُ أَدْنَىٰ مِنْ ثُلُثِي اللَّيْلِ وَنِصْفَهُ ۖ
 وَثُلُثَهُ وَطَآئِفَةٌ مِّنَ الَّذِينَ مَعَكَ ۗ وَاللَّهُ يُقَدِّرُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ ۗ
 عَلِمَ أَن لَّنْ نَّحْصُوهُ فَتَابَ عَلَيْكُمْ ۖ فَاقْرَءُوا مَا تَيَسَّرَ مِنَ
 الْقُرْآنِ ۗ عَلِمَ أَن سَيَكُونُ مِنكُم مَّرْضَىٰ ۙ وَآخَرُونَ
 يَضْرِبُونَ فِي الْأَرْضِ يَبْتَغُونَ مِن فَضْلِ اللَّهِ ۙ وَآخَرُونَ
 يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۖ فَاقْرَءُوا مَا تَيَسَّرَ مِنْهُ ۗ وَأَقِيمُوا
 الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَأَقْرِضُوا اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا ۗ وَمَا
 تُقَدِّمُوا لِأَنفُسِكُمْ مِّنْ خَيْرٍ يَّجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ هُوَ خَيْرًا
 وَأَعْظَمَ أَجْرًا ۗ وَاسْتَغْفِرُوا اللَّهَ ۖ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٠﴾

إِنَّ هَدِيمَهُ تَذَكِيرَةٌ ۖ فَمَنْ شَاءَ
 اتَّخَذْ إِلَىٰ رَبِّهِ سَبِيلًا ﴿١٩﴾ * إِنَّ
 رَبَّكَ يَعْلَمُ أَنَّكَ تَقُومُ أَدْنَىٰ مِنْ ثُلُثِي
 اللَّيْلِ وَنِصْفَهُ ۖ وَثُلُثَهُ وَطَآئِفَةٌ مِّنَ
 الَّذِينَ مَعَكَ ۗ وَاللَّهُ يُقَدِّرُ اللَّيْلَ
 وَالنَّهَارَ ۗ عَلِمَ أَن لَّنْ نَّحْصُوهُ فَتَابَ
 عَلَيْكُمْ ۖ فَاقْرَءُوا مَا تَيَسَّرَ مِنَ الْقُرْآنِ
 ۗ عَلِمَ أَن سَيَكُونُ مِنكُم مَّرْضَىٰ ۙ
 وَآخَرُونَ يَضْرِبُونَ فِي الْأَرْضِ
 يَبْتَغُونَ مِن فَضْلِ اللَّهِ ۙ وَآخَرُونَ
 يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۖ فَاقْرَءُوا مَا
 تَيَسَّرَ مِنْهُ ۗ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا
 الزَّكَاةَ وَأَقْرِضُوا اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا ۗ
 وَمَا تُقَدِّمُوا لِأَنفُسِكُمْ مِّنْ خَيْرٍ
 يَّجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ هُوَ خَيْرًا وَأَعْظَمَ
 أَجْرًا ۗ وَاسْتَغْفِرُوا اللَّهَ ۖ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ
 رَّحِيمٌ ﴿٢٠﴾

19. Kwa hakika hili ni kumbusho. Mwenye kutaka atashika njia ya kwendea kwa Mola Wake Mlezi.

20. Hakika Mola wako Mlezi Anajua ya kuwa hakika wewe unakesha karibu na thuluthi mbili za usiku, na nusu yake, na thuluthi yake. Na baadhi ya watu walio pamoja nawe kadhaalika. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Anaye ukadiria usiku na mchana. Anajua kuwa hamuezi kuswali (faradhi hiyo), basi Amekusameheni. Basi someni kilicho chepesi katika Qur'ani. Anajua ya kuwa baadhi yenu watakuwa wagonjwa, na wengine wanasafiri katika ardhi wakitafuta fadhila ya Mwenyezi Mungu, na wengine wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo someni kilicho chepesi humo, na simamisheni Sala, na toeni Zaka, na mkopesheni

Mwenyezi Mungu mkopo mwema. Na kheri yoyote mnayo itanguliza kwa ajili ya nafsi zenu mtaikuta kwa Mwenyezi Mungu, imekuwa bora zaidi, na ina thawabu kubwa sana. Na mtakeni msamaha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.

Sura Hii ni Ukumbusho kwa Wenye Akili Wanapata Onyo na Kunasihiwa

Allah تعالیٰ Anasema:

إِنَّ هٰذِهِ

“Kwa hakika (sura) hii.” Maana yake: Sura.

تَذَكُّرًا

“Ni ukumbusho.” Maana yake: Wanajikumbusha nayo wenye akili, Na kwa ajili hii Amesema Allah تعالیٰ:

فَمَنْ شَاءَ اتَّخَذْ إِلَىٰ رَبِّهِ سَبِيلًا ﴿١٩﴾

“Mwenye kutaka atashika njia ya kuendea kwa Mola Wake Mlezi.”
(73:19).

Maana yake: Miongoni mwa Awatakao Allah تعالیٰ Kuwaongoa Kwake, kama Alivyoliwekea mpaka hilo katika sura nyingine,

وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٣٠﴾

“Wala hamuezi kutaka ila Atakapo Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Ilimu, Mwenye Hikima.” (76:30).

Kuondosha Wajibu wa Kusimama Usiku¹ na Kutaja Nyudhuru Zake

Kisha Allah تعالیٰ Anasema:

﴿ إِنَّ رَبَّنَا يَعْلَمُ أَنَّكَ تَقُومُ أَدْنَىٰ مِنْ ثُلُثِي اللَّيْلِ وَنِصْفَهُ وَثُلُثَهُ وَطَائِفَةٌ مِنَ الَّذِينَ مَعَكَ ﴾

“Hakika Mola wako Mlezi Anajua ya kuwa hakika wewe unakesha karibu na theluthi mbili za usiku, na nusu yake, na theluthi yake. Na baadhi ya watu walio pamoja nawe.”

¹ Kama ilivyotajwa awali, hii inarejea kwenye *Qiyam Al-layl* au kila kinachoitwa *Tahajjud*.

Maana yake: Mara nyingine inakuwa hivi na mara nyingine inakuwa hivi, na hayo yote bila makusudio toka kwenu, lakini hamuwezi kudumu juu ya yale aliyokuamrisheni, katika kusimama usiku kwa kuwa hayo yanakupeni tabu. Na kwa ajili hii Amesema:

وَاللَّهُ يُقَدِّرُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ^٤

“Na Mwenyezi Mungu Ndiye Anayeukadiria usiku na mchana.”

Maana yake: Mara nyingine hulingana na wakati mwingine huzidiana,

عَلِمَ أَنْ لَنْ تُحْصُوهُ

“Anajua kuwa hamuwezi kuisali (faradhi hiyo).”

Maana yake: Faradhi ambayo Ameiwajibisha kwenu.

فَأَقْرَأُوا مَا تيسَّرَ مِنَ الْقُرْآنِ^٥

“Basi someni kilicho chepesi katika Qur’ani.”

Maana yake: Bila kuainisha wakati. Kwa maana: Lakini simameni usiku kadiri muwezavyo. Na Sala imetajwa hapa kwa tamko la kusoma kama Allah تعالى Alivyosema katika Surat Subhaana:

وَلَا تَجْهَرُ بِصَلَاتِكَ

“Wala usitangaze Sala yako kwa sauti kubwa.” (17:110)

Maana yake: Kwa kisomo chako.

وَلَا تُخَافِتْ بِهَا

“Wala usiifiche kwa sauti ndogo.”

Kauli Yake تعالى،

عَلِمَ أَنْ سَيَكُونُ مِنْكُمْ مَّرْضَىٰ^٦ وَءَاخَرُونَ يَضْرِبُونَ فِي الْأَرْضِ يَبْتَغُونَ مِنْ فَضْلِ اللَّهِ^٧
وَأَخَرُونَ يُقْتَلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ^٨

“Anajua ya kuwa baadhi yenu watakuwa wagonjwa, na wengine wanasafiri katika ardhi wakitafuta Fadhila ya Mwenyezi Mungu, na wengine wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Amejua kuwa katika umma huu kutakuwa na wenye udhuru kwa kuacha kusimama usiku hawawezi wajibu huo, kutokana na maradhi, wenye kusafiri katika ardhi, wanatafuta Fadhila za Allah تعالى katika kuchuma na kutafuta biashara. Na wengine wanashughulika kwa yale yalio muhimu zaidi katika haki zao kama vile kupigana vita katika njia ya Allah تعالى. Na aya hii bali sura hii yote imeshuka Makkah. Wakati huo sheria ya kupigana vita haikuwa tayari na hiyo ni dalili kubwa zaidi ya utume, kwa sababu hiyo iko katika mlango wa kutoa habari za ghaibu katika wakati ujao.

Kwa ajili hii Allah تعالى Anasema:

فَأَقْرَهُوا مَا تَيَسَّرَ مِنْهُ

“Kwa hivyo someni kilicho chepesi humo.”

Maana yake: Simameni kiasi mtakavyoona kuwa kuna wepesi juu yenu. Kauli Yake:

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ

“Na Simamisheni Sala, na toeni Zaka.”

Maana yake: Simamisheni Sala zenu za wajibu juu yenu, na toeni Zaka za faradhi. Aya hii ni ushahidi kwa yule ambaye amesema kuwa Zaka imefaradhiwa Makkah, lakini viwango na vipimo vyake vilikuja kubainika katika mji wa Madinah. Na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

Ibn Abbaas Ikrimah, Qatadah Mujaahid, Hasan, na wengine katika *salaf* رضي الله عنهم wamesema: Kwa hakika aya hii imefuta hukumu ambayo Allah تعالى Alikuwa Amewawajibishia Waislamu mwanzoni kusimama usiku.¹ Imethibitika katika sahihi ya Bukhari na Muslim kuwa Mtume ﷺ alimuambia mtu mmoja aliyemuuliza:

«خَمْسُ صَلَوَاتٍ فِي الْيَوْمِ وَاللَّيْلَةِ»

“Sala tano katika mchana na usiku.”

Akasema: ‘Je mimi ninao wajibu mwingine?’ Mtume ﷺ akasema:

¹ At-Tabari 23:679, 680, na A-Durr Al-Manthur 8:322.

«لَا، إِلَّا أَنْ نَطْرَعُ»

“Hapana isipokuwa Sala za Sunna.”¹

Amri ya Kutoa Sadaka na Kufanya Kheri

Kauli Yake تعالى:

وَأَقْرِضُوا اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا

“Na mkopesheni Mwenyezi Mungu mkopo mwema.”

Maana yake: Sadaka, kwa kuwa Allah تعالى Analipa juu ya hilo malipo mazuri mno, na nyongeza zaidi. Kama alivyosema katika Kauli Yake تعالى:

مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضْعِفُهُ لَهُ أَمْعَافًا كَثِيرًا

“Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema ili Amzidishie mzdisho mwingi.” (2:245).

Kisha Allah تعالى Akasema tena:

وَمَا تَقْدِمُوا لِأَنْفُسِكُمْ مِّنْ خَيْرٍ تَجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ هُوَ خَيْرًا وَأَعْظَمَ أَجْرًا

“Na kheri yoyote mnayoitanguliza kwa ajili ya nafsi zenu mtaikuta kwa Mwenyezi Mungu, imekuwa bora zaidi, na ina thawabu kubwa sana.”

Maana yake: Yote mtakayoyatanguliza mbele yenu mtakutana nayo, hilo ni bora kuliko mlivyobakisha kwa ajili ya nafsi zenu katika dunia. Haafidh Abu Ya’alaa Mauswil amepokea toka kwa Haarith bin Suway amesema: Abdullaahi amesema: Mtume ﷺ amesema:

«أَيُّكُمْ مَأْلُهُ أَحَبُّ إِلَيْهِ مِنْ مَالِ وَارِثِهِ؟»

“Ni yupi kati yenu mali yake anaipenda zaidi kuliko mali ya warithi wake?”

Wakasema: ‘Ewe Mtume ﷺ hakuna yoyote kati yetu isipokuwa mali yake anaipenda zaidi kuliko mali ya warithi wake.’ Akasema:

¹Fat’hul Al-Bari 1:130, na Muslim 1:41.

«اعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ»

“Jueni mnayoyasema.”

Wakasema: ‘Hatujui isipokuwa hivyo ewe Mtume ﷺ.’ Akasema:

«إِنَّمَا مَالٌ أَحَدِكُمْ مَا قَدَّمَ، وَمَالٌ وَارِثِهِ مَا آخَرَهُ»

“Hakika mali ya mmoja wenu ni ile alioitanguliza, na mali ya warithi wake ni ile alioichelewesha.”¹

Ameipokea Bukhari.² Kisha Allah تعالى Akasema:

وَأَسْتَغْفِرُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“Na mtakeni msamaha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.”

Maana yake: Zidisheni Utajo Wake, na mumtake maghfira katika mambo yenu yote, hakika Yeye ni Msamehevu, Mwenye Huruma kwa anayemuomba msamaha.

Mwisho wa tafsiri ya *Suratu Muzzammil*, Shukrani ni za Allah تعالى na Kuneemesha ni Kwake.

* * *

¹ Musnad Abu Ya'ala 9:97.

² Fat'hul Al-Bari 11:24, na An-Nasai 6:237.

Tafsiri ya Suratul Muddaththir

Sura ya 74

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْمُذْثِّرِ

يَتَأَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ ﴿١﴾ قُمْ فَأَنْذِرْ ﴿٢﴾ وَرَبِّكَ فَكَبِّرْ ﴿٣﴾
 وَتِيَابِكَ فَطَهِّرْ ﴿٤﴾ وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ ﴿٥﴾ وَلَا تَمَنَّ
 تَسْتَكْبِرُ ﴿٦﴾ وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ ﴿٧﴾ فَإِذَا نُفِرَ فِي الْأَقْوَ
 رِ ﴿٨﴾ فَذَلِكَ يَوْمَئِذٍ يَوْمٌ عَسِيرٌ ﴿٩﴾ عَلَى الْكَافِرِينَ غَيْرُ
 يَسِيرٍ ﴿١٠﴾ ذَرْنِي وَمَنْ خَلَقْتُ وَحِيدًا ﴿١١﴾ وَجَعَلْتُ لَهُ
 مَالًا مَمْدُودًا ﴿١٢﴾ وَبَيْنَ يَدَيْهِ شُهُودًا ﴿١٣﴾ وَمَهَّدْتُ لَهُ
 تَمْهِيدًا ﴿١٤﴾ ثُمَّ يَطْمَعُ أَنْ أَزِيدَ ﴿١٥﴾ كَلَّا إِنَّهُ كَانَ
 لِآيَاتِنَا عَنِيدًا ﴿١٦﴾ سَأَرْهُقُهُ صُعُودًا ﴿١٧﴾ إِنَّهُ فَكَّرَ
 وَقَدَّرَ ﴿١٨﴾ فَقَتَلَ كَيْفَ قَدَرَ ﴿١٩﴾ ثُمَّ قَتَلَ كَيْفَ قَدَرَ ﴿٢٠﴾
 ثُمَّ نَظَرَ ﴿٢١﴾ ثُمَّ عَبَسَ وَسَرَ ﴿٢٢﴾ ثُمَّ أَدْبَرَ ﴿٢٣﴾
 وَأَسْتَكْبَرَ ﴿٢٤﴾ فَقَالَ إِنْ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ يُؤْتَى ﴿٢٥﴾ إِنْ
 هَذَا إِلَّا قَوْلُ الْبَشَرِ ﴿٢٦﴾ سَأُصَلِّهِ سَقَرًا ﴿٢٧﴾ وَمَا
 أَدْرَاكَ مَا سَقَرٌ ﴿٢٨﴾ لَا تُتَّبَعِي وَلَا تَذُرِّي ﴿٢٩﴾ لَوْ آخَاةٌ
 لِلْبَشَرِ ﴿٣٠﴾ عَلَيْهَا تِسْعَةَ عَشَرَ ﴿٣١﴾

يَتَأَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ ﴿١﴾ قُمْ فَأَنْذِرْ ﴿٢﴾ وَرَبِّكَ فَكَبِّرْ ﴿٣﴾
 وَتِيَابِكَ فَطَهِّرْ ﴿٤﴾ وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ ﴿٥﴾ وَلَا تَمَنَّ
 تَسْتَكْبِرُ ﴿٦﴾ وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ ﴿٧﴾ فَإِذَا نُفِرَ فِي الْأَقْوَ
 رِ ﴿٨﴾ فَذَلِكَ يَوْمَئِذٍ يَوْمٌ عَسِيرٌ ﴿٩﴾ عَلَى
 الْكَافِرِينَ غَيْرُ يَسِيرٍ ﴿١٠﴾

1. Ewe uliyejifunika nguo!
2. Simama uonye watu!
3. Na Mola Wako Mlezi mtukuze!
4. Na nguo zako, zisafishe.
5. Na usiabudu masanamu!
6. Wala usitoe kwa kutaraji kuzidishiwa.
7. Na kwa ajili ya Mola Wako Mlezi, subiri!
8. Basi litapo pulizwa barugumu.

9. Siku hiyo, basi, itakuwa siku nzito.

10. Kwa makafiri haitakuwa nyepesi.

Aya za Mwanzo Kushuka Baada ya Iqraa'

Imethibitika katika Sahihi Bukhari na Muslim toka kwa Abii Salamah amesema, Jabir bin Abdillah رضي الله عنه ameniambia kuwa amemsikia Mtume ﷺ akihadithia kipindi cha wahyi akasema:

«قَبِينَا أَنَا أَمْشِي إِذْ سَمِعْتُ صَوْتًا مِنَ السَّمَاءِ فَرَفَعْتُ بَصْرِي قِبَلَ السَّمَاءِ، فَإِذَا الْمَلَكُ الَّذِي جَاءَنِي بِحِرَاءَ، قَاعِدٌ عَلَى كُرْسِيِّ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ، فَجِئْتُ مِنْهُ حَتَّى هَوَيْتُ إِلَى الْأَرْضِ، فَجِئْتُ إِلَى أَهْلِي قُلْتُ: زَمَلُونِي زَمَلُونِي فَزَمَلُونِي. فَأَنْزَلَ [اللهُ تَعَالَى]: ﴿بِأَيِّ آيَاتِنَا أَتَى الْكَافِرُونَ ۚ﴾ وَفَإِذَا نَزَلَ ﴿إِلَى الْفَاهِجِ﴾ ثُمَّ حَمِيَ الْوَحْيُ وَتَتَابَعُ»

“Wakati ninatembea mara nikasikia sauti kutoka mbinguni nikanyanyua macho yangu mbinguni, ghafla nikamuona Malaika aliyenijia katika pango la Jabal Hiraam amekaa katika kiti kati ya mbingu na ardhi nikafazaika kutokana naye mpaka nikaanguka chini, nikaenda kwa mke wangu nikasema: Nifunikeneni nifunikeneni, wakanifunika, Mwenyezi Mungu Mtukufu Akateremsha, “Ewe uliyejifunika nguo! Simama uonye watu! Na Mola Wako Mlezi Mtukuze!” Mpaka Kauli Yake: “Na kwa Mola Wako Mlezi usubiri” Amesema Abu Salama: ‘Ar’rajzu’ ni masanamu, kisha wahyi ukapamba moto na kufuatana.”

Tamko hili ni la Bukhari.¹ Na mtiririko huu wa maneno unapelekea kuwa wahyi ulishuka kabla ya maneno haya, kwa sababu za kusema kwake Mtume ﷺ,

«فَإِذَا الْمَلَكُ الَّذِي جَاءَنِي بِحِرَاءَ»

“Ghafla malaika ambaye alinijia katika pango la Jabali la Hiraam.”

Na huyo ni Jibrili عليه السلام wakati alipomjia na Kauli Yake تعالى:

أَقْرَأُ بِأَسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ﴿١﴾ خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ﴿٢﴾ أَلَمْ يَكُنْ الْأَكْرَمُ ﴿٣﴾
الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ﴿٤﴾ عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ﴿٥﴾

¹ Fat'hul Al-Bari 6:361, na Muslim 1:143.

“Soma kwa Jina la Mola Wako Mlezi Aliyeumba, Amemuumba binaadamu kwa tone la damu, Soma! Na Mola Wako Mlezi ni Karimu kushinda wote! Ambaye Amefundisha kwa kalamu. Kamfundisha mtu aliyokuwa hayajui.” (96:1-5)

Hali ilivyo ni kwamba, baada ya hapa wahyi ulisimama kipindi kisha baada ya hapo malaika Jibril عليه السلام akashuka tena.

Imamu Ahmad amepokea kutokana na hadithi ya Az-Zuhri kutoka kwa Abi Salamah bin Abdu Rahmaan amesema: Jabir bin Abdullah رضى الله عنه amenieleza kwamba yeye alimsikia Mtume ﷺ anasema:

ثُمَّ فَتَرَ الْوَحْيَ عَنِّي فَتْرَةً، فَبَيْنَمَا أَنَا أَمْشِي سَمِعْتُ صَوْتًا مِنَ السَّمَاءِ، فَرَفَعْتُ بَصْرِي قِبَلَ السَّمَاءِ، فَإِذَا الْمَلَكُ الَّذِي جَاءَنِي، قَاعِدٌ عَلَى كُرْسِيِّ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ، فَجِئْتُ مِنْهُ فَرَقًا حَتَّى هَوَيْتُ إِلَى الْأَرْضِ، فَجِئْتُ أَهْلِي فَقُلْتُ لَهُمْ: زَمَلُونِي زَمَلُونِي فَرَمَلُونِي، فَأَنْزَلَ اللَّهُ تَعَالَى: ﴿بِأَنبَاءِ السُّورِ ۝ قُرْ فَأَنْزِلْ ۝ وَرَبِّكَ تَكْوِينًا ۝ وَبِأَنبَاءِ ظَفِيرًا ۝ وَالْأَجْرَ مَا فَجَّرَ ۝﴾ ثُمَّ حَمِي الْوَحْيُ وَتَتَابَعُ

*“Kisha Wahyi ulikatika kwangu kwa muda, wakati ninatembea nilisikia sauti kutoka mbinguni, nikanyanyua macho upande wa mbinguni ghafla malaika ambaye alinijia amekaa katika kiti baina ya mbingu na ardhi nikafazaika kutokana naye kufazaika kukubwa, nikaanguka ardhini, nikamuendea mke wangu nikamuambia nifuniken nifuniken akanifunika, Mwenyezi Mungu Mtukufu Akateremsha: **“Ewe uliye jifunika nguo! Simama uonye watu! Na Mola Wako Mlezi Mtukuze! Na nguo zako zisafishe. Na masanamu usiabudu!”** Kisha wahyi ukapamba moto na kufuatana.”¹*

Wameitoa kupitia hadithi ya Az-Zuhri²

At-Tabarani amepokea kutoka kwa Ibni Abbas رضى الله عنهما amesema: Al-Waliid bin Al-Mughira alitengeneza chakula kwa ajili ya makureshi walipokwisha kula akasema: ‘Mnasema nini kuhusu mtu huyu?’ Baadhi yao wakasema, ‘Mtu huyu ni mchawi.’ Baadhi yao wakasema, ‘siyo mchawi.’ Na wengine wakasema,

¹ Ahmad 3:325.

² FAT’hul Al-Bari 1:37 na Muslim 1:143.

'ni kuhani.' Na wengine wakasema, 'siyo kuhani.' Wakasema baadhi yao, 'Mtu huyo ni mshairi.' Wengine wakasema, 'sio mshairi.' Baadhi yao wakasema, 'ni uchawi unaopokewa.. Wakakubaliana kuwa ni uchawi unaopokewa. Hivyo habari hiyo ikamfikia Mtume ﷺ. Akahuzunika na akainamisha kichwa chake na akajifunika nguo. Allah تعالى Akateremsha.

يٰٓأَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ ﴿١﴾ قُمْ فَأَنْذِرْ ﴿٢﴾ وَرَبِّكَ فَكَبِّرْ ﴿٣﴾ وَتِيَابَكَ فَطَهِّرْ ﴿٤﴾ وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ ﴿٥﴾
 وَلَا تَمَنَّ أَنْ تَمُنَّ تَسْتَكْبِرُ ﴿٦﴾ وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ ﴿٧﴾

“Ewe uliyejifunika nguo!, Simama uonye watu!. Na Mola Wako Mlezi Mtukuze!. Na nguo zako, zisafishe. Na usiabudu masanamu!. Wala usitoe kwa kutaraji kuzidishiwa. Na kwa ajili ya Mola Wako Mlezi, subiri!”¹ (74:1-7)

Na Kauli Yake تعالى:

قُمْ فَأَنْذِرْ ﴿٢﴾

“Simama uonye watu!”

Maana yake: Jizatiti katika hilo na uwaonye watu. Na hii ndio aya iliyomfanya awe ni Mtume. Kama ambavyo aya ya kwanza ilimfanya awe na wadhifa wa unabii.

وَرَبِّكَ فَكَبِّرْ ﴿٣﴾

“Na Mola Wako Mlezi Mtukuze!”

Maana yake: Adhimisha. Al-Aufi amesema kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما:

وَتِيَابَكَ فَطَهِّرْ ﴿٤﴾

“Na nguo zako, zisafishe.”

Maana yake: Nguo zako unazozivaa, zisitokane na chumo ambalo lisilo halali. Na husemwa, na panasemwa usivae nguo zako kwa Maasi.² Amesema Muhammad bin Siriin رحمه الله تعالى.³

¹ At-Tabarani 11:125. Katika mnyororo wa silsila ya mapokezi ni dhaifu. Kuna mapokezi mengine yanayoweza kuunga mkono. Angalia majadiliano yanayofuata baada ya aya ya 25.

² At-Tabari 24:11.

³ At-Tabari 24:12.

وَتِيَابَكَ فَطَهَّرَ ﴿١٠﴾

“Na nguo zako, zisafishe.”

Maana yake: Zisafishe kwa maji.¹ Na amesema Ibn Zaid: washirikina walikuwa hawajisafishi. Kwa hiyo Allah تعالى Akamuamrisha kujisafisha na kusafisha nguo zake.² Na kauli hii ameichagua Ibn Jariir رحمه الله تعالى.³

Said Bin Jubair amesema:

وَتِيَابَكَ فَطَهَّرَ ﴿١٠﴾

“Na nguo zako, zisafishe.”

Na moyo wako na nia yako vitakase. Na amesema Muhammad bin Ka’ab Al-Quradhi na Al-Hassan Al-Basry, maana yake, ‘Na tabia yako iifanye njema.’ Na Kauli Yake تعالى:

وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ ﴿١١﴾

“Na yaliyo machafu yahame!.”

Amesema Ali bin Abi Twalha kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما, **Ar’Rujz-** na masanamu yahame;⁴ kama hivyo amesema Mujahid, Ikrima, Qatadah, Az-Zuhri, na Ibn Zaid: ‘Kwamba hayo ni masanamu.’⁵ Kama katika Kauli Yake Allah تعالى:.

يَتَأْتِيَ النَّبِيَّ اتَّقِ اللَّهَ وَلَا تُطِيعِ الْكٰفِرِينَ وَالْمُنٰفِقِينَ ﴿١٢﴾

“Ewe Nabii! Mche Mwenyezi Mungu wala usiwatii makafiri na wanaafiki.” (33:1)

وَقَالَ مُوسَىٰ لِأَخِيهِ هَارُونَ أَخْلِفْنِي فِي قَوْمِي وَأَصْلِحْ وَلَا تَتَّبِعْ سَبِيلَ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٤٢﴾

“Na Musa akamuambia nduguye Haarun: Shika mahala pangu kwa watu wangu na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu.” (7:142)

¹ At-Tabari 24:12.

² At-Tabari 24:12.

³ At-Tabari 24:12.

⁴ At-Tabari 24:13.

⁵ At-Tabari 24:13.

Kauli Yake Allah تعالى:

وَلَا تَمَنَّوْا نَسْتَكْتِكُمْ

“Wala usitoe kwa kutaraji kuzidishiwa.”

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما: Usitoe kichache kwa kutaka kingi. Khuswaif amesema kutoka kwa Mujaahid katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَلَا تَمَنَّوْا نَسْتَكْتِكُمْ

“Wala usitoe kwa kutaraji kuzidishiwa.”

Amesema, ‘Usidhoofike katika kuzidisha kheri.’ Amesema, ‘*Tamnun*,’ katika maneno ya waarabu ina maana ya - kudhoofika.¹ Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ

“Na kwa ajili ya Mola Wako Mlezi, subiri!”

Maana yake: Ifanye subira yako juu ya maudhi yao ni kwa ajili ya Dhati ya Mola Wako Mwenye Kushinda na Mtukufu. Ameyasema hayo Mujahid.² Ibrahimu Al-Nakhai amesema, ‘Vumilia kipawa chako kwa ajili ya Allah تعالى.’³

Ukumbusho wa Siku ya Qiyama

Kauli Yake Allah تعالى:

فَإِذَا نُفِرَ فِي النَّاقُورِ ۖ فَذَلِكَ يَوْمَئِذٍ يَوْمٌ عَسِيرٌ ۖ عَلَى الْكَافِرِينَ غَيْرُ يَسِيرٍ

“Basi litapopulizwa barugumu. Siku hiyo, basi, itakuwa siku nzito. Kwa makafiri haitakuwa nyepesi.”

Ibn Abbaas, Mujaahid, Al-Sha’abi, Zaid Bin Aslam, Al-Hassan, Qatadah, Adh-Dhahaak, Ar-Rabi Ibn Anas na Al-Sudi na Ibn Zaid رضي الله عنهم wamesema;

النَّاقُورِ

(Annaaquur)

¹ At-Tabari 24:16.

² At-Tabari 24:16.

³ At-Baghawi 4:414.

Ni baragumu.¹ Mujaahid amesema, 'na baragumu ni kama umbile la pembe.'² Na amesema Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى ametuzungumzia Abu Said Al-Ash'shaj ametuzungumzia Asbaati bin Muhammad kutoka kwa Mutwarrif kutoka kwa Atwiyah–Al–Awfi kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما.

فَإِذَا تُقْرِفَى الْفَأَقُورِ ﴿٢٦﴾

"Basi litapopulizwa barugumu,"

Amesema: Amesema Mtume ﷺ,

«كَيْفَ أَنْعَمُ وَصَاحِبُ الْقَرْنِ قَدِ التَّمَّ الْقَرْنَ وَحَسَىٰ جِبْهَتُهُ يَتَّظِرُ مِنِّي يُؤْمَرُ فَيَنْفُخُ؟»

"Vipi nitastarehe na hali ya kuwa mwenye parapanda amekwisha kulitia mdomoni parapanda na ameinamisha paji lake la uso anangojea lini ataamrisha apulizie?"

Masahaba wa Mtume ﷺ wakasema, 'Nini unachotuamrisha, Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?' Mtume ﷺ akasema:

«قُولُوا: حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ، عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا»

"Semeni tosha yetu ni Mwenyezi Mungu na bora ya kutegemewa ni Yeye tu. Juu ya Mwenyezi Mungu tumetegemea"

Na kama hivyo amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Al'Asbaat¹. Na Kauli ya Allah تعالى:

فَذَلِكَ يَوْمَئِذٍ يَوْمٌ عَسِيرٌ ﴿٢٧﴾

"Siku hiyo, basi, itakuwa siku nzito."

Maana yake: Ngumu, ya shida na mashaka.

عَلَى الْكٰفِرِينَ عَذَابٌ عَسِيرٌ ﴿٢٨﴾

"Kwa makafiri haitakuwa nyepesi."

Maana yake: Si rahisi juu yao, kama alivyosema Allah تعالى:

¹ At-Tabari 24:18.

² At-Tabari 24:18.

³ Ahmad 326.

يَقُولُ الْكَافِرُونَ هَذَا يَوْمٌ عَسِيرٌ ﴿١﴾

“Watasema makafiri hii ni siku nzito sana.” (54:8)

Na tumesimuliwa kwamba Zurarah bin Aufa - Kadhi wa Basra رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى alisalisha watu Sala ya Asubuhi akasoma sura hii alipofika katika Kauli ya Allah تَعَالَى:

فَإِذَا نُقِرَ فِي النَّاقُورِ ﴿٢﴾ فَذَلِكَ يَوْمَئِذٍ يَوْمٌ عَسِيرٌ ﴿٣﴾ عَلَى الْكَافِرِينَ غَيْرُ يَسِيرٍ ﴿٤﴾

**“Basi litapopulizwa barugumu, Siku hiyo, basi, itakuwa siku nzito.
Kwa makafiri haitakuwa nyepesi.”**

Alipiga yowe moja tu, kisha akaanguka akiwa amekufa.¹

* * *

¹ Al-Hakim 2:507.

ذَرْنِي وَمَنْ خَلَقْتُ وَحِيدًا ﴿١١﴾ وَجَعَلْتُ لَهُ مَالًا
 مَمْدُودًا ﴿١٢﴾ وَبَيْنَ شُهُودًا ﴿١٣﴾ وَمَهَّدْتُ لَهُ تَمْهِيدًا ﴿١٤﴾
 ثُمَّ يَطْمَعُ أَنْ أَزِيدَ ﴿١٥﴾ كَلَّا إِنَّهُ كَانَ لِآيَاتِنَا
 عِينِدًا ﴿١٦﴾ سَأْهِقَهُ صَعُودًا ﴿١٧﴾ إِنَّهُ فَكَّرَ وَقَدَّرَ ﴿١٨﴾
 فَقَتِلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿١٩﴾ ثُمَّ قَاتَلَ كَيْفَ فَدَرَّ ﴿٢٠﴾
 ثُمَّ نَظَرَ ﴿٢١﴾ ثُمَّ عَبَسَ وَسَكَرَ ﴿٢٢﴾ ثُمَّ أَدْبَرَ وَاسْتَكْبَرَ ﴿٢٣﴾
 فَقَالَ إِنَّ هَذَا إِلَهٌ سِحْرٌ يُؤْتِرُ ﴿٢٤﴾ إِنَّ هَذَا إِلَهٌ
 قَوْلُ الْبَشَرِ ﴿٢٥﴾ سَأُصْلِيهِ سَقَرَ ﴿٢٦﴾ وَمَا أَذْرَكَ مَا
 سَقَرُ ﴿٢٧﴾ لَا تُتَّبِعِي وَلَا تَنْذُرِي ﴿٢٨﴾ لَوْ أَحَاطَ لِلْبَشَرِ ﴿٢٩﴾
 عَلَيْهَا تِسْعَةَ عَشَرَ ﴿٣٠﴾ وَمَا جَعَلْنَا أَصْحَابَ النَّارِ إِلَّا
 مَلَائِكَةً ۖ وَمَا جَعَلْنَا عِدَّتَهُمْ إِلَّا فِتْنَةً لِلَّذِينَ كَفَرُوا
 لِيَسْتَيَقِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَزَادَ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِيمَانًا
 ۗ وَلَا يَرْتَابَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَالْمُؤْمِنُونَ ۗ وَلِيَقُولَ
 الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ وَالْكَافِرُونَ مَاذَا أَرَادَ اللَّهُ بِهَذَا
 مَثَلًا ۗ كَذَلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ مَن يَشَاءُ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ ۗ وَمَا
 يَعْلَمُ جُنُودَ رَبِّكَ إِلَّا هُوَ ۗ وَمَا هِيَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْبَشَرِ ﴿٣١﴾
 كَلَّا وَالْقَبْرِ ﴿٣٢﴾ وَاللَّيْلِ إِذْ أَدْبَرَ ﴿٣٣﴾ وَالصُّبْحِ إِذَا
 أَسْفَرَ ﴿٣٤﴾ إِنَّهَا لِإِلْحَادِي الْكُبْرَى ﴿٣٥﴾ نَذِيرًا لِلْبَشَرِ ﴿٣٦﴾
 لِمَن شَاءَ مِنْكُمْ أَنْ يَتَقَدَّمَ أَوْ يَتَأَخَّرَ ﴿٣٧﴾

ذَرْنِي وَمَنْ خَلَقْتُ وَحِيدًا ﴿١١﴾
 وَجَعَلْتُ لَهُ مَالًا مَمْدُودًا ﴿١٢﴾
 وَبَيْنَ شُهُودًا ﴿١٣﴾ وَمَهَّدْتُ لَهُ
 تَمْهِيدًا ﴿١٤﴾ ثُمَّ يَطْمَعُ أَنْ أَزِيدَ
 ﴿١٥﴾ كَلَّا إِنَّهُ كَانَ لِآيَاتِنَا
 عِينِدًا ﴿١٦﴾ سَأْهِقَهُ صَعُودًا ﴿١٧﴾
 إِنَّهُ فَكَّرَ وَقَدَّرَ ﴿١٨﴾
 فَقَتِلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿١٩﴾ ثُمَّ قَاتَلَ
 كَيْفَ فَدَرَّ ﴿٢٠﴾ ثُمَّ نَظَرَ ﴿٢١﴾
 ثُمَّ عَبَسَ وَسَكَرَ ﴿٢٢﴾ ثُمَّ أَدْبَرَ
 وَاسْتَكْبَرَ ﴿٢٣﴾ فَقَالَ إِنَّ هَذَا
 إِلَهٌ سِحْرٌ يُؤْتِرُ ﴿٢٤﴾ إِنَّ هَذَا
 إِلَهٌ قَوْلُ الْبَشَرِ ﴿٢٥﴾ سَأُصْلِيهِ
 سَقَرَ ﴿٢٦﴾ وَمَا أَذْرَكَ مَا
 سَقَرُ ﴿٢٧﴾ لَا تُتَّبِعِي وَلَا تَنْذُرِي
 ﴿٢٨﴾ لَوْ أَحَاطَ لِلْبَشَرِ ﴿٢٩﴾
 عَلَيْهَا تِسْعَةَ عَشَرَ ﴿٣٠﴾

11. Niache na Niliye-muumba akiwa pekee;

12. Na Nikamjaalia awe na mali nyingi,

13. Na wana wanao-onekana,

14. Na Nikamtengenezea mambo vizuri kabisa.

15. ***Kisha anatumai nimzidishie!***
16. ***Hasha! Kwani hakika yeye alikuwa akizifanyia inadi Aya Zetu!***
17. ***Nitamtesa kwa mateso yasiyowezezana.***
18. ***Kwani hakika yeye alifikiri na akapima.***
19. ***Basi amelaaniwa kwa namna alivyofikiri!***
20. ***Tena amelaaniwa namna alivyofikiri!***
21. ***Kisha akatazama,***
22. ***Kisha akakunja paji la uso, na akanuna.***
23. ***Kisha akaipa kisogo haki, na akatakabari.***
24. ***Na akasema: Haya si chochote ila ni uchawi ulionukuliwa.***
25. ***Haya si chochote ila ni maneno ya binaadamu.***
26. ***Nitakuja mtia kwenye Moto wa Saqar.***
27. ***Na nini kitakujulisha wewe kuhusu Moto huo wa Saqar?***
28. ***Haubakishi wala hausazi.***
29. ***Unababua ngozi iwe nyeusi.***
30. ***Juu yake wapo (walinzi) kumi na tisa.***

Karipio kwa Anayesema Qur'ani kuwa ni Uchawi

Allah تعالی Anasema hali ya Kumkemea mtu huyu muovu ambaye Allah تعالی Amemneemesha neema za duniani akazikufuru badala ya kushukuru. Na akazikabili kwa kuzikanusha aya za Mwenyezi Mungu na kuzusha juu yake na akazifanya ni katika maneno ya watu. Na Allah تعالی Ameorodhesha neema Zake juu yake Alizomneemesha. Pale Aliposema Allah تعالی:

ذَرْنِي وَمَنْ خَلَقْتُ وَحِيدًا

“Niache na Niliyemuumba akiwa pekee.”

Maana yake: Amemtoa tumboni mwa mama yake peke yake, hana mali wala watoto, kisha Allah تعالی Akamruzuku:

﴿١١﴾ مَالًا مَّمدُودًا

“Mali nyingi.” (74:12).

Maana yake: Nyingi kunjufu. Na Amemfanyia,

﴿١٢﴾ وَنِينَ شُهُودًا

“Na wana wanaoonekana.”

Mujahidi amesema hawakosekani.¹ Maana yake: wako mbele yake hawasafiri kwa ajili ya biashara, bali watumwa wao na wafanyakazi wao wanasimamia hayo kwa niaba yao na hali ya kuwa wao wamekaa mbele ya baba yao huku akiliwazika.

As-Sudi, Abu Maalik na Qaasim bin ‘Umar, bin Qatadah wametaja kwamba walikuwa kumi na watatu.² Na amesema Ibnu Abbaas na Mujaahid رضي الله عنهما walikuwa watoto kumi na watatu.³ Hii neema kubwa sana ya kuishi pamoja nao.

﴿١٣﴾ وَمَهَّدتُّ لَهُ تَمْهيدًا

“Na nikamtengenezea mambo vizuri kabisa.”

Maana yake: Nimemmakinisha kwa kumpa mali mbali mbali, kama samani na visivyo kuwa hivyo.

﴿١٤﴾ ثُمَّ يَطْمَعُ أَنْ أَزِيدَ ﴿١٥﴾ كَلَّا إِنَّهُ كَانَ لِآيَاتِنَا عَنِيدًا

“Kisha anatumai Nimzidishie!, Hasha! Kwani hakika yeye alikuwa akizifanyia inadi Aya Zetu!”

Maana yake: ‘Ni mpinzani, na hilo ni juu ya kukufuru neema Zake, baada ya kujua.’ Allah تعالیٰ Amesema.

﴿١٦﴾ سَأَرْهُقُهُ صَعُودًا

“Nitamtesa kwa mateso yasiowezezana.”

¹ Al-Baghawi 4:414.

² Ad-Durr Al-Manthur 8:329.

³ Al-Tabari 24:21.

Amesema Qatadah kutoka kwa Ibni Abbaas رضي الله عنهما 'Swa'uuda' ni jiwe la motoni litawekwa juu ya uso wa kafiri na kulikokota. As-suddi amesema: 'Swa'uuda' - ni jabali la jiwe lenye kuteleza lililo katika moto wa Jahannamu atalazimishwa kulipanda. Na Mujaahid amesema:

سَأْزَهُقُهُ صَعُودًا ﴿٧٤﴾

"Nitamtesa kwa mateso yasiyowezezana."

Maana yake: Uzito wa adhabu.¹ Na Qatadah رضي الله عنه amesema adhabu ambayo hamna mapumziko ndani yake.²

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّهُ فَكَّرَ وَقَدَّرَ ﴿٧٥﴾

"Kwani hakika yeye alifikiri na akapima."

Maana yake: Kwa hakika tumemlazimisha adhabu ngumu. Maana yake: tumemsogeza kwenye adhabu ngumu kwa sababu ya kuwa kwake mbali na imani kwa sababu yeye amefikiri na akakadiria. Maana yake: Alifikiri kwa umakini wakati alipoulizwa kuhusu Qur'ani. Hivyo, akaona aizushie maneno ya uongo,

وَقَدَّرَ ﴿٧٦﴾

"Na akapima." (74:18)

Maana yake: Alifikiri vizuri.

فَقْتَلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿٧٧﴾ ثُمَّ قَتَلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿٧٨﴾

"Basi amelaaniwa kwa namna alivyofikiri! Tena amelaaniwa namna alivyofikiri!" (74:19-20).

Maana yake: Alimuapiza.

ثُمَّ نَظَرَ ﴿٧٩﴾

"Kisha akatazama."

Akarudia kuangalia na kutafakari.

¹ At-Tabari 24:21.

² Ad-Durr Al-Muthur 8:331.

ثُمَّ عَبَسَ

“Kisha akakunja paji la uso.”

Maana yake: Alifumba macho yake na kukunja uso.

وَسَرَ

“Na akanuna.” (74:22).

Maana yake: Aliukunja uso na kuchukia. Na Kauli Yake,

ثُمَّ أَدْبَرَ وَأَسْتَكْبَرَ

“Kisha akaipa kisogo haki, na akatakabari.” (74:23).

Maana yake: Aliupa kisogo ukweli na akarudi nyuma hali ya kuwa anaonesha kibri akiacha kunyenyekea Qur’ani.

فَقَالَ إِنَّ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ يُؤْتَرُ

“Na akasema: Haya si chochote ila ni uchawi ulionukuliwa.” (74:24).

Maana yake: Huu ni uchawi ambao Muhammad anaunakili – kutoka kwa watu wengine waliokuwa kabla yake na anasimulia kutoka kwao. Na kwa sababu hii amesema:

إِنَّ هَذَا إِلَّا قَوْلُ الْبَشَرِ

“Haya si chochote ila maneno ya binaadamu.” Maana yake: Sio maneno ya Allah تعالى.

Na huyu aliyetajwa katika mtiririko wa maneno haya ni Al-Waliid bin Al-Mughira Al-Makhzuumi mmoja wa viongozi wa Kikureishi Mwenyezi Mungu Amemlaani. Na kuhusu habari yake bwana huyu ni simulizi iliyopokelewa na Al-Aufi kutoka kwa Ibni Abbaas رضي الله عنهما amesema:

“Al-Waliid bin Al-Mughira aliingia kwa Abu Bakri bin Abu Quhafah, akamuuliza kuhusu Qur’ani, alipomueleza alitoka kwa Makureishi akasema, ‘Ee ajabu kwa yale asemayo Ibnu Abu Kabshah.¹ Naapa kwa Mwenyezi Mungu hayakuwa maneno hayo ni mashairi wala uchawi wala haropoki kutokana na ukichaa,

¹ At-Tabari 24:16

kwa hakika maneno yake ni katika maneno ya Mwenyezi Mungu.’ Kundi katika Makureishi liliposikia maneno hayo lilifanya mkutano, likasema, tunaapa kwa Mwenyezi Mungu iwapo Al-Walid atatoka katika dini yetu basi Makureishi wote watatoka. Alipoyasikia maneno hayo Abu Jahl bin Hishaam – alisema: Mimi ninaapa kwa Mwenyezi Mungu nitamtuliza, akaondoka mpaka akaingia nyumbani kwake akamuambia Al-Waliid: ‘Hivi huwaoni jamaa zako wamekukusanyia sadaka?’ Akasema: ‘Hivi sikuwa mimi mwingi wao kwa mali na watoto?’ Abu Jahl akamuambia: ‘Wanazungumza kwamba wewe unaingia kwa Ibni Abi Quhafah ili upate chakula kutoka kwake.’ Al-Walid akasema, ‘Hivi wamelizungumza hilo jamaa zangu? Hapana naapa kwa Mwenyezi Mungu sitamkaribia Ibni Abi Kuhafah, ‘Umar wala Ibn Abi Kabshah na hayakuwa maneno yake, isipokua ni uchawi unaopokewa.’ Allah تعالی Akateremsha juu ya Mjumbe Wake ﷻ,

﴿١١﴾ ذَرْنِي وَمَنْ خَلَقْتُ وَحِيدًا

“Niache na Niliyemuumba akiwa pekee.” Mpaka aliposema:

﴿١٢﴾ لَا تُتَّبِعِي وَلَا تَتَذَرِّي

“Haubakishi wala hausazi.”¹

Qatadah amesema: Wamedai kwamba yeye kabla ya maneno hayo mabaya alisema: ‘Naapa kwa Mwenyezi Mungu kwa hakika niliyachunguza yale aliyoyasema yule mtu nimegundua kuwa si mashairi kwa hakika ayasemayo yana ladha na uzuri, Kwa Hakika – Maneno hayo yanakaa juu na hapana kitu kitakachoyakalia juu yake, na siyashuku kuwa hayo ni uchawi.”

Allah تعالی Akateremsha:

﴿١٣﴾ فَكَيْفَ قَدَّرَ

“Basi amelaaniwa namna alivyofikiri!” Mpaka Mwisho wa Aya hiyo.

﴿١٤﴾ ثُمَّ عَبَسَ وَسَكَرَ

“Kisha akakunja paji la uso, na akanuna.”

¹ At-Tabari 24:24. Angalia vile vile Al-Hakim 2:507, ambaye aliipa hadhi ya *sahih* na Adh-Dhahabi akakubaliana nayo. Katika *Dalail An-Nubuwwah* cha Al-Bayhaqi 2:198, 199. Wanazuoni wengi wa *Hadith* wanaichukulia kuwa ni katika silsila nzuri na ni *Mursal*.

Akakunja baina ya macho yake na kukasirika.¹ Allah تعالى Amesema.

سَأُصَلِّيَةَ سَقَرٍ

“Nitakuja mtia kwenye Moto wa Saqar.”

Maana yake: Nitamzamisha katika moto kwa pande zake zote.

Kisha Allah تعالى Anasema,

وَمَا أَدْرَاكَ مَا سَقَرٌ

“Na nini kitakujuulisha wewe kuhusu Moto huo wa Saqar?”

Hii ni staili ya kukuza jambo la moto huo kisha amelifasiri neno ‘Saqar’ kwa Kauli Yake Allah تعالى:

لَا تُتَقَى وَلَا تَنْذَرُ

“Haubakishi wala hausazi.”

Maana yake: Unakula nyama zao, mifupa yao, mishipa yao na ngozi zao, kisha zitabadilishwa, katika hali zote hizo hawatakufa na hawatakuwa wazima. Ameyasema hayo Ibn Buraidah na Abu Sinaani na wengine.²

Na Kauli Yake Allah تعالى:

لَوْاحَةٌ لِلْبَشَرِ

“Unababua ngozi iwe nyeusi.”

Mujaahid amesema: Maana yake: Ngozi ya juu ya mwil. Na Qatadah amesema,

لَوْاحَةٌ لِلْبَشَرِ

“Unababua ngozi iwe nyeusi.” (74:29).

Maana yake: ‘Unachoma Ngozi.’³

Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema: ‘Unachoma ngozi ya mwanadamu.’⁴

¹ At-Tabari 24:25.

² Ad-Durr Al-Muthur 8:332.

³ At-Tabari 24:27.

⁴ At-Tabari 24:28.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

عَلَيْهَا تِسْعَةَ عَشَرَ ﴿١٣﴾

“Juu yake wapo (walinzi) kumi na tisa.”

Maana yake: Katika uangalizi kuna walinzi wa moto wenye maumbo makubwa na wakatili.

وَمَا جَعَلْنَا أَصْحَابَ النَّارِ إِلَّا مَلَائِكَةً ۖ وَمَا جَعَلْنَا عِدَّتَهُمْ إِلَّا فِتْنَةً لِلَّذِينَ كَفَرُوا لِيَسْتَيْقِنَ
الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَيَزْدَادَ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِيمَانًا ۖ وَلَا يَرْتَابَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ
وَالْمُؤْمِنُونَ ۚ وَيَقُولَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ وَالْكَافِرُونَ مَاذَا أَرَادَ اللَّهُ بِهَذَا مَثَلًا ۗ كَذَلِكَ
يُضِلُّ اللَّهُ مَن يَشَاءُ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ ۗ وَمَا يَعْلَمُ جُنُودَ رَبِّكَ إِلَّا هُوَ ۗ وَمَا هِيَ إِلَّا ذِكْرَى
لِلْبَشَرِ ﴿١٤﴾ كَلَّا وَالْقَمَرِ ﴿١٥﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا أَدْبَرَ ﴿١٦﴾ وَالصُّبْحِ إِذَا أَسْفَرَ ﴿١٧﴾ إِنَّهَا لَإِحْدَى
الْكُبَرِ ﴿١٨﴾ نَذِيرًا لِلْبَشَرِ ﴿١٩﴾ لِمَن شَاءَ مِنكُمْ أَن يَتَقَدَّمَ أَوْ يَتَأَخَّرَ ﴿٢٠﴾

31. Na hatukuwafanya walinzi wa Motoni ila ni Malaika, wala hatukuifanya idadi yao hiyo ila kuwapa mtihani waliokufuru, wapate kuwa na yakini waliopewa Kitabu, na wazidi Imani wale walioamini, wala wasiwe na shaka walio pewa Kitabu na Waumini, na wapate kusema wenye maradhi katika nyoyo zao na makafiri: Mwenyezi Mungu Amekusudia nini kwa mfano huu? Ndio kama hivyo Mwenyezi Mungu Humuacha apotee Amtakaye, na Humuongoa Amtakaye. Na hapana yeyote anayejua majeshi ya Mola Wako Mlezi ila Yeye tu. Na huu (moto) si chochote ila ni ukumbusho kwa binaadamu.

32. Hasha! Naapa kwa mwezi!

33. Na kwa usiku unapokucha!

34. Na kwa asubuhi inapopambazuka!

35. Hakika huo Moto katika mambo yaliyo makubwa kabisa!

36. Ni onyo kwa binaadamu,

37. Kwa anayetaka miongoni mwenu kutangulia au kuchelewa.

Idadi ya Walinzi wa Motoni na Waliyoyasema Makafiri Kuhusiana na Idadi Hiyo:

Allah تعالی Anasema:

وَمَا جَعَلْنَا أَصْحَابَ النَّارِ

“Na hatukuwafanya walinzi wa Motoni.” (74:31)

Maana yake: Watumishi wake.

إِلَّا مَلَائِكَةً

“Ila ni Malaika.”

Ma-Zabania shupavu wenye nguvu walio wakali. Na hayo ni majibu juu ya washirikina wa Kikureishi wakati ilipotajwa idadi ya walinzi wa moto. Abu Jahli akasema: Enyi kongamano la Makureishi: Hivi kila watu kumi kati yenu hawawezi kumdhibiti mmoja miongoni mwao na kuwashinda.

Allah تعالی Akasema:

وَمَا جَعَلْنَا أَصْحَابَ النَّارِ إِلَّا مَلَائِكَةً

“Na hatukuwafanya walinzi wa Motoni ila ni Malaika.”

Maana wenye maumbile yenye nguvu, mtu yeyote hawezi kupambana nao na hawashindwi. Na pamesemwa kuwa: Aba Al-Ashadain na jina halisi ni Kaladah bin Usaid Bin Khalaf, amesema: ‘Enyi jamaa wa kikureshi mimi niachieni wawili na nitawachieni katika wao kumi na saba.’ Alisema hivyo kutokana na kujiona nafsi yake, kwa sababu alikuwa na nguvu kubwa, kwa kudai kwamba yeye alikuwa akisimama juu ya ngozi ya ng’ombe wanavutana naye watu kumi ili waichomoe ngozi hiyo chini ya nyayo zake. Ngozi hiyo huchanika na bila ya yeye kutetereka hata kidogo.

Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَمَا جَعَلْنَا عِدَّتَهُمْ إِلَّا فِتْنَةً لِلَّذِينَ كَفَرُوا

“Wala hatukuifanya idadi yao hiyo ila kuwatahini waliokufuru.”

Maana yake: Kwa Hakika tumetaja idadi yao, kuwa wao wako kumi na tisa. Kwa ajili ya kuwajaribu watu.

لَيْسَتَيْنِ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ

“Wapate kuwa na yakini waliopewa Kitabu.” (74:31)

Maana wajue kwamba Mtume huyu ni wa kweli na kwamba yeye anayoyasema yanalingana na yale yaliyomo ndani ya vitabu vyao vilivyoteremshwa kutoka mbinguni, juu ya Mitume waliokuwa kabla yake.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَيَزِدَادَ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِيمَانًا

“Na wazidi Imani wale walioamini.” (74:31)

Maana: longezeke imani yao, kwa yale wanayoyashuhudia miongoni mwa ukweli wa habari za Mtume wao Muhammad ﷺ.

وَلَا يَرْتَابَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَالْمُؤْمِنُونَ وَلَيَقُولَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ

“Wala wasiwe na shaka waliopewa Kitabu na Waumini, na wapate kusema wenye maradhi katika nyoyo zao.”

Maana yake: Miongoni mwa wanafiki.

وَالْكَافِرُونَ مَاذَا أَرَادَ اللَّهُ بِهِذَا مَثَلًا

“Na makafiri: Mwenyezi Mungu Amekusudia nini kwa mfano huu?” (74:31)

Maana yake: “Wanasema kuna hekima gani kulitaja jambo hili hapa.”

Allah تعالى Amesema.

كَذَلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ مَن يَشَاءُ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ

“Ndio kama hivyo Mwenyezi Mungu Humuacha apotee amtakaye, na Humuongoa amtakaye.”

Maana yake: Kutokana na mfano huu na unaofanana na huu, imani inapata nguvu katika nyoyo za watu, na inayumba kwa wengine na Allah تعالى Ana Hekima kubwa sana na hoja yenye nguvu sana.

Hakuna Anayejua Idadi ya Askari wa Allah تعالی Isipokuwa Yeye Tu.

Kauli Yake Allah تعالی:

وَمَا يَعْلَمُ جُنُودَ رَبِّكَ إِلَّا هُوَ

“Na hapana yeyote anayejua majeshi ya Mola Wako Mlezi ila Yeye tu.”

Maana: Hajui idadi yao na wingi wao, isipokuwa Yeye Allah تعالی, ili mtu asije akadhani kuwa wao ni kumi na tisa tu. Imethibitika katika Hadithi ya Israa iliyopokewa katika sahihi mbili na vitabu vya Hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ katika kuisifu *Al-Bayt Al-Ma’amuur* ambayo iko katika mbingu ya saba amesema:

«فَإِذَا هُوَ بِدُخُلِهِ فِي كُلِّ يَوْمٍ سَبْعُونَ أَلْفَ مَلَكٍ لَا يُعُودُونَ إِلَيْهِ آخِرَ مَا عَلَيْهِمْ»

*“Malaika elfu sabini huingia humo ‘Al-Baytul Maamur’ kila siku na wala hawarajei tena.”*¹

Kauli Yake Allah تعالی:

وَمَا هِيَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْبَشَرِ ﴿٣١﴾

“Na huu (moto) si chochote ila ni ukumbusho kwa binaadamu.” (74:31)

Mujaahid na wengine wamesema:

وَمَا هِيَ

“Na huu (moto) si chochote.”

Maana yake: Moto uliosifiwa.²

إِلَّا ذِكْرٌ لِلْبَشَرِ ﴿٣٢﴾

“ila ni ukumbusho kwa binaadamu.”

Kisha Akasema Allah تعالی:

¹ *Fat’hul Al-Bari* 6:348, na *Muslim* 1:146.

² *At-Tabari* 24:32.

كَلَّا وَالْقَمَرَ ﴿١١﴾ وَاللَّيْلِ إِذْ أَدْبَرَ ﴿١٢﴾

“Hasha! Naapa kwa mwezi! Na kwa usiku unapokucha!”

Maana yake: Unapoondoka.

وَالصُّبْحِ إِذَا أَسْفَرَ ﴿١٣﴾

“Na kwa asubuhi inapo pambazuka!” (74:34)

Maana yake: Inapochomoza.

إِنهَا لِأَحَدَى الْأَكْبَرِ ﴿١٤﴾

“Hakika huo Moto ni katika mambo yaliyo makubwa kabisa!”

Maana yake: Makubwa anakusudia moto, ameyasema hayo Ibn Abbaas, Mujaahid, Qatadah na Ad-Dhahak na wengine katika *Salaf* (watu wema waliotangulia) رضي الله عنهم.¹

نَذِيرًا لِلْبَشَرِ ﴿١٥﴾ لِمَنْ شَاءَ مِنْكُمْ أَنْ يَتَقَدَّمَ أَوْ يَتَأَخَّرَ ﴿١٦﴾

“Ni onyo kwa binaadamu, kwa anayetaka miongoni mwenu kutangulia au kuchelewa.”

Maana yake: Kwa mwenye kutaka kukubali maonyo na kuongoka kwenye kufuata haki au mwenye kukataa haki hiyo na kuipinga.

* * *

¹ At-Tabari 24:33.

كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ﴿٣٨﴾ إِلَّا أَصْحَابَ الْإِيمَانِ
 فِي جَنَّاتٍ يَتَسَاءَلُونَ ﴿٣٩﴾ عَنِ الْمُجْرِمِينَ ﴿٤٠﴾
 مَا سَلَكَكُمْ فِي سَقَرٍ ﴿٤١﴾ قَالُوا لَمْ نَكُ مِنْ
 الْمُصَلِّينَ ﴿٤٢﴾ وَلَمْ نَكُ نَطْعُمُ الْمَسْكِينِ ﴿٤٣﴾ وَكُنَّا
 نَخُوضُ مَعَ الْخَائِضِينَ ﴿٤٤﴾ وَكُنَّا نَكْذِبُ بِيَوْمِ
 الدِّينِ ﴿٤٥﴾ حَتَّىٰ أَتَانَا الْيَقِينُ ﴿٤٦﴾ فَمَا تَنْفَعُهُمْ
 شَفَعَةُ الشَّفِيعِينَ ﴿٤٧﴾ فَمَا هُمْ عَنِ التَّذْكِيرِ مُعْرِضِينَ ﴿٤٨﴾
 كَانَهُمْ حُمُرٌ مُسْتَنْفِرَةٌ ﴿٤٩﴾ فَرَّتْ مِنْ قَسْوَرَةٍ ﴿٥٠﴾ بَلْ
 يُرِيدُ كُلُّ امْرِيٍّ مِنْهُمْ أَنْ يُوْتِيَ صُحُفًا مُنَشَّرَةً ﴿٥١﴾ كَلَّا
 بَلْ لَا يَخَافُونَ الْآخِرَةَ ﴿٥٢﴾ كَلَّا إِنَّهُ تَذَكُّرٌ ﴿٥٣﴾
 فَمَنْ شَاءَ ذَكَرْهُ ﴿٥٤﴾ وَمَا يَذْكُرُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ
 هُوَ أَهْلُ التَّقْوَىٰ وَأَهْلُ الْغَفْرِ ﴿٥٥﴾

كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ﴿٣٨﴾
 إِلَّا أَصْحَابَ الْإِيمَانِ ﴿٣٩﴾ فِي جَنَّاتٍ
 يَتَسَاءَلُونَ ﴿٤٠﴾ عَنِ الْمُجْرِمِينَ ﴿٤١﴾
 مَا سَلَكَكُمْ فِي سَقَرٍ ﴿٤٢﴾ قَالُوا لَمْ
 نَكُ مِنْ الْمُصَلِّينَ ﴿٤٣﴾ وَلَمْ نَكُ
 نَطْعُمُ الْمَسْكِينِ ﴿٤٤﴾ وَكُنَّا
 نَخُوضُ مَعَ الْخَائِضِينَ ﴿٤٥﴾ وَكُنَّا
 نَكْذِبُ بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿٤٦﴾ حَتَّىٰ أَتَانَا
 الْيَقِينُ ﴿٤٧﴾ فَمَا تَنْفَعُهُمْ شَفَعَةُ
 الشَّفِيعِينَ ﴿٤٨﴾ فَمَا هُمْ عَنِ
 التَّذْكِيرِ مُعْرِضِينَ ﴿٤٩﴾ كَانَهُمْ
 حُمُرٌ مُسْتَنْفِرَةٌ ﴿٥٠﴾ فَرَّتْ مِنْ قَسْوَرَةٍ ﴿٥١﴾
 بَلْ يُرِيدُ كُلُّ امْرِيٍّ مِنْهُمْ أَنْ يُوْتِيَ

صُحُفًا مُنَشَّرَةً ﴿٥٢﴾ كَلَّا بَلْ لَا يَخَافُونَ الْآخِرَةَ ﴿٥٣﴾ كَلَّا إِنَّهُ تَذَكُّرٌ ﴿٥٤﴾ فَمَنْ شَاءَ ذَكَرْهُ ﴿٥٥﴾ وَمَا يَذْكُرُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ هُوَ أَهْلُ التَّقْوَىٰ وَأَهْلُ الْغَفْرِ ﴿٥٥﴾

38. Kila nafsi imo rahanini kwa mabaya iliyoyachuma.

39. Isipo kuwa watu wa kuliani.

40. Hao watakuwa katika Mabustani, wawe wanaulizana

41. Khabari za wakosefu:

42. Ni nini kilichokupelekeni Motoni?

43. *Watasema: Hatukuwa miongoni mwa waliokuwa wakisali.*
44. *Wala hatukuwa tukiwalisha masikini.*
45. *Na tulikuwa tukizungumza (maneno ya kuchukiza) pamoja na walio zama katika maovu.*
46. *Na tulikuwa tukiikanusha siku ya malipo.*
47. *Mpaka yakini (mauti) ilipotufikia.*
48. *Basi hautawafaa kitu uombezi wa waombezi.*
49. *Basi wana nini hata wanapuza onyo hili?*
50. *Kama kwamba wao ni pundamilia waliotimuliwa,*
51. *Wanaomkimbia simba!*
52. *Ati kila mmoja katika wao anataka apewe nyaraka zilizo funuliwa.*
53. *Hasha! Kwani wao hawaiogopi Akhera?*
54. *Hasha! Kwa hakika (Qur'an) huu ni ukumbusho!*
55. *Basi anayetaka atakumbuka.*
56. *Na hawatakumbuka isipokuwa Mwenyezi Mungu Atake. Yeye Ndie Anayestahiki Kuogopwa, na msamaha ni Wake Yeye.*

Mjadala Uliopo Kati ya Watu wa Peponi na Watu wa Motoni

Allah تعالیٰ Anasema hali ya Kueleza kwamba,

كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ﴿٧٤﴾

“Kila nafsi imo rahanini kwa mabaya iliyoyachuma.”

Maana yake: Itadhibitiwa na matendo yake Siku ya Qiyama. Ameyasema hayo Ibn Abbaas رضي الله عنهما na wengine.

إِلَّا أَصْحَابَ الْيَمِينِ ﴿٧٥﴾

“Isipokuwa watu wa kuliani.” Kwa Hakika wao,

فِي جَنَّاتٍ يَتَسَاءَلُونَ ﴿٤٤﴾ عَنِ الْمُجْرِمِينَ ﴿٤٣﴾

“Hao watakuwa katika Mabustani, wawe wanaulizana Khabari za wakosefu.”

Maana yake: Watawauliza watu waovu hali ya kuwa wao wamo katika vyumba, na hao wamo katika vidato vya chini vya moto wakiwa wanawaambia:

مَا سَأَلَكُمْ فِي سَقَرٍ ﴿٤٢﴾ قَالُوا لَمْ نَكُ مِنَ الْمُصَلِّينَ ﴿٤١﴾ وَلَمْ نَكُ نُطْعِمُ
الْمَسْكِينِ ﴿٤٠﴾

“Ni nini kilicho kupelekeni Motoni? Watasema: Hatukuwa miongoni mwa walio kuwa wakisali. Wala hatukuwa tukiwalisha masikini.”

Maana yake: Hatukumuabudu Mola Wetu na hatukuwatendea wema viumbe wake kama sisi.

وَكُنَّا نَخُوضُ مَعَ الْخَائِضِينَ ﴿٤٥﴾

“Na Tulikuwa tukizungumza (maneno ya kuchukiza) pamoja na waliozama katika maovu.”

Maana yake: Tunazungumza katika mambo tusiyoyajua, Qatadah amesema: ‘Kila anapopotoka mpotovu hupotoka naye.’¹

وَكُنَّا نَكْذِبُ بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿٤٦﴾ حَتَّىٰ أَتْنَا الْيَقِينَ ﴿٤٧﴾

“Tukiikanusha siku ya malipo, mpaka yakini (mauti) ilipotufikia.”
(74:44-45)

Anakusudia, mauti. Kama ilivyo Kauli Yake,

وَأَعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ ﴿٩٩﴾

“Na muabudu Mola Wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini (mauti).”
(15:99)

¹ At-Tabari 24:37.

Mtume ﷺ amesema,

«أَمَّا هُوَ - يعني عثمان بن مظعون - فَقَدْ جَاءَهُ الْيَقِينُ مِنْ رَبِّهِ»

“Ama huyo ni Uthmaan bin Madh`uun, kwa hakika yeye amejiwa na yakini (mauti) kutoka kwa Mola Wake Mlezi”¹

Allah عزوجل Amesema:

﴿فَمَا تَنْفَعُهُمْ شَفَاعَةُ الشَّافِعِينَ﴾

“Basi hautawafaa kitu uombezi wa waombezi.” (74:48)

Maana yake: Mtu aliyekuwa na sifa hizi hakika huyo siku ya Qiyama hautamfaa uombezi wowote katika siku hiyo, kwa sababu uombezi unafaa pakiwa pale mahali pana kubali kuombewa. Ama yule atakaye muendea Allah تعالي hali ya kuwa ni kafiri Siku ya Qiyama hakika huyo moto ni wake na hapana budi kuishi humo milele.

Upuuzaji wa Makafiri na Msimamo Wao

Kisha Allah عزوجل Amesema:

﴿فَمَا لَهُمْ عَنِ التَّذْكَرَةِ مُعْرِضِينَ﴾

“Basi wana nini hata wanapuuza onyo hili?”

Maana yake: Wana nini hawa makafiri –ambao wako mbele yako wanapinga lile ambalo unawalingania, na kuwaonya?

﴿كَأَنَّهُمْ حُمُرٌ مُسْتَنْفِرَةٌ﴾ ﴿فَكَرَّتْ مِنْ قَسْوَرَةٍ﴾

“Kama kwamba wao ni pundamilia waliotimuliwa, wanaomkimbia simba!”

Maana yake: Kama kwamba wao kutokana na kukimbia kwao ukweli na kuupinga ni pundamilia wakati wanapomkimbia Simba anayetaka kuwawinda. Ameyasema hayo Abu Hurairah رضي الله عنه.² Na amesema Hamd bin Salama

¹ Al-Bayhaqi 3:406.

² At-Tabari 24:42. Isnadi yake ni dhaifu.

kutoka kwa Ali bin Zaid kutoka kwa Yuusuf bin (Mahraani) kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما. 'Al-Asad' kwa lugha ya Kiarabu ni Simba, na wahabeshi humuita 'Qas-wara' na wafursi humuita 'Shairu' na kwa lugha ya kianbati ni 'Auba'.¹ Kauli Yake Allah تعالى،

بَلْ يُرِيدُ كُلُّ امْرِئٍ مِّنْهُمْ أَنْ يُؤْتَىٰ صُحُفًا مُّنشَرَةً ﴿٥٦﴾

“Ati kila mmoja katika wao anataka apewe nyaraka zilizo funuliwa.”

Maana yake: Bali kila mmoja katika hawa washirikina anataka ateremshiwe kitabu kama Allah تعالى Alivyomteremshia Mtume Muhammad ﷺ. Ameyasema hayo Mujahidi na wengine.²

Kama Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذَا جَاءَتْهُمْ آيَةٌ قَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ حَتَّىٰ نُؤْتَىٰ مِثْلَ مَا أُوتِيَ رُسُلُ اللَّهِ ۗ اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ ۗ

“Na inapowajia Ishara, wao husema: Hatutoamini mpaka tupewe mfano wa waliopewa Mitume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi kuliko wote Hujua wapi Anaweka ujumbe wake.” (6:124)

Na katika upokezi mwingine kutoka kwa Qatadah: Wanataka kupewa utakaso pasi na matendo yoyote.³ Kwa hiyo Kauli Yake Allah عزوجل Amesema,

كَلَّا ۗ بَلْ لَا تَخَافُونَ ٱلْآخِرَةَ ﴿٧٤﴾

“Hasha! Kwani wao hawaiogopi Akhera?” (74:53)

Maana yake: Hakika kilichowaharibu ni kutoamini kwao Akhera na kukadhibisha kwao uwepo wake.

¹ At-Tabari 24:42.

² Al-Qurtubi 19:90.

³ At-Tabari 24:43.

Qur'ani ni Ukumbusho

Kisha Allah تعالى Amesema:

كَلَّا إِنَّهُ تَذَكُّرٌ ﴿٣٨﴾

“Hasha! Kwa hakika huu (Qur'an) ni ukumbusho!”

Maana yake: Kwa hakika Qur'an hii ni ukumbusho,

فَمَنْ شَاءَ ذَكَرْهُ ﴿٣٩﴾ وَمَا يَذْكُرُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ

“Basi anayetaka atakumbuka. Na hawatakumbuka isipokuwa Mwenyezi Mungu Atake.” (74:55-56)

Kama Kauli Yake تعالى:

وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٠﴾

“Wala hamuezi kutaka ila Atakapo Mwenyezi Mungu.” (81:29).

Na Kauli Yake Allah تعالى:

هُوَ أَهْلُ التَّقْوَىٰ وَأَهْلُ الْغَفْرِ ﴿٤١﴾

“Yeye Ndie Anayestahiki Kuogopwa, na Msamaha ni Wake Yeye.”

Maana yake: Yeye Ndiye Anayestahiki Kuogopwa na Yeye Ndiye Anayesamehe dhambi ya mwenye kutubia Kwake, na akarejea. Hayo ameyasema Qatadah.¹

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Al-Muddaththir* na Kusifiwa na Kuneemesha ni kwa Allah تعالى tu.

* * *

¹ At-Tabari 24:44.

Tafsiri ya Suratul Qiyamah

Sura ya 75

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْقِيَامَةِ

لَا أُقْسِمُ بِيَوْمِ الْقِيَامَةِ ❶ وَلَا أُقْسِمُ بِالنَّفْسِ اللَّوَّامَةِ ❷
 ❸ أَحْسَبُ الْإِنْسَانَ أَلَّنْ نَجْمَعُ عِظَامَهُ ❹ بَلَىٰ
 قَدَرِينٌ عَلَىٰ أَنْ نُسَوِّيَ بَنَانَهُ ❺ بَلْ يُرِيدُ الْإِنْسَانُ
 لِيَفْجُرَ أَمَامَهُ ❻ يَسْأَلُ أَيَّانَ يَوْمِ الْقِيَامَةِ ❼ فَإِذَا
 بَرَاقَ الْبَصُرُ ❽ وَخَسَفَ الْقَمَرُ ❾ وَجُمِعَ الشَّمْسُ
 وَالْقَمَرُ ❿ يَقُولُ الْإِنْسَانُ يَوْمَئِذٍ أَيْنَ الْمَفْرُ ❶
 وَذَرَّ ❷ إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمُسْتَقَرُّ ❸ يُتَّبِعُوا الْإِنْسَانَ
 يَوْمَئِذٍ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ ❹ بَلِ الْإِنْسَانُ عَلَىٰ نَفْسِهِ
 بَصِيرَةٌ ❺ وَلَوْ أَلْقَىٰ مَعَاذِيرَهُ ❻ لَا تُحْرَكُ بِهِ
 لِسَانُكَ لِتَتَعَجَّلَ بِهِ ❼ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ❽
 فَإِذَا قَرَأْنَاهُ فَاتَّبِعْ قُرْآنَهُ ❾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ❿
 كَلَّا بَلْ تُحِبُّونَ الْعَاجِلَةَ ❶ وَتَذَرُونَ الْآخِرَةَ ❷ وَجُوهٌ
 يَوْمَئِذٍ نَاضِرَةٌ ❸ إِلَىٰ رَبِّهَا نَاطِرَةٌ ❹ وَوُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ
 بَاسِرَةٌ ❺ تَنْظُرُونَ أَنْ يُفْعَلَ بِهَا فَاقِرَةٌ ❻

لَا أُقْسِمُ بِيَوْمِ الْقِيَامَةِ ❶ وَلَا
 أُقْسِمُ بِالنَّفْسِ اللَّوَّامَةِ ❷ أَحْسَبُ
 الْإِنْسَانَ أَلَّنْ نَجْمَعُ عِظَامَهُ ❸
 بَلَىٰ قَدَرِينٌ عَلَىٰ أَنْ نُسَوِّيَ بَنَانَهُ
 ❹ بَلْ يُرِيدُ الْإِنْسَانُ لِيَفْجُرَ
 أَمَامَهُ ❺ يَسْأَلُ أَيَّانَ يَوْمِ الْقِيَامَةِ
 ❻ فَإِذَا بَرَاقَ الْبَصُرُ ❼ وَخَسَفَ
 الْقَمَرُ ❽ وَجُمِعَ الشَّمْسُ وَالْقَمَرُ
 ❿ يَقُولُ الْإِنْسَانُ يَوْمَئِذٍ أَيْنَ الْمَفْرُ
 وَذَرَّ ❶ إِلَىٰ رَبِّكَ ❷ يَوْمَئِذٍ
 الْمُسْتَقَرُّ ❸ يُتَّبِعُوا الْإِنْسَانَ
 يَوْمَئِذٍ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ ❹ بَلِ
 الْإِنْسَانُ عَلَىٰ نَفْسِهِ بَصِيرَةٌ ❺
 وَلَوْ أَلْقَىٰ مَعَاذِيرَهُ ❻

1. ***Ninaapa kwa Siku ya Kiyama!***
2. ***Na Ninaapa kwa nafsi inayo jilaumu!***
3. ***Anadhani mtu kuwa Sisi Hatutaikusanya mifupa yake?***
4. ***Kwani! Sisi Tunaweza hata Kuziweka sawa sawa ncha za vidole vyake!***
5. ***Lakini mtu anataka tu kuendelea na maasi kwa siku zilioko mbele yake***
6. ***Anauliza: Lini itakuwa hiyo Siku ya Kiyama?***
7. ***Basi jicho litakapoduwaa,***
8. ***Na mwezi utakapopatwa,***
9. ***Na likakusanywa jua na mwezi,***
10. ***Siku hiyo mtu atasema: Yako wapi makimbilio?***
11. ***La! Hapana pa kukimbilia!***
12. ***Siku hiyo pa kutua ni kwa Mola Wako Mlezi tu.***
13. ***Siku hiyo ataambiwa mtu aliyoyatanguliza na aliyoyaakhirisha.***
14. ***Bali mtu anaitambua zaidi nafsi yake.***
15. ***Na hata kama atatoa udhuru chungu nzima***

Kiapo Juu ya Watu Kufufuliwa Tena Siku ya Kiama na Majibu ya Hoja za Wanaopinga Fikra Zao

Kwa hakika imetangulia sio mara moja kwamba ikiwa kinachoapiwa ni chenye kukanushwa inafaa kuleta tamko la 'Laa' kabla ya kuapa kwa ajili ya kutilia mkazo kanusho (hilo), na kinachoapiwa hapa ni kuthibitisha uwepo wa siku ya kiama na kujibu hoja za wajinga wanaopinga kufufuliwa viwiliwili. Na kwa ajili hii Allah تعالیٰ Anasema:

لَا أُقْسِمُ بِيَوْمِ الْقِيَامَةِ ۖ وَلَا أُقْسِمُ بِالنَّفْسِ اللَّوَّامَةِ ۖ

“Ninaapa kwa Siku ya Kiyama!. Na ninaapa kwa nafsi inayojilaumu!”

Qatadah amesema: Ameviapia vyote viwili.¹ Na kauli hiyo ndiyo iliyopokewa kutoka kwa Ibni Abbaas na Saiid Bin Jubair رضي الله عنهما² Ama Siku ya Qiyama inajulikana. Na ama nafsi yenye kujilaumu amesema Qurrah bin Khaalid kutoka kwa Al-Hassan Al-Bassry رحمه الله تعالى, katika ufafanuzi wa aya hii. Hakika muumini siku zote huilaumu nafsi yake. Huwa akijiuliza mara kwa mara, 'Nimekusudia nini katika maneno yangu, nimekusudia nini kwa chakula changu, nimekusudia nini katika mazungumzo ya nafsi yangu?. Ama muovu hana muda wa kuilaumu nafsi yake, anafanya kila linalokuja mbele yake.'³ Amepokea Ibnu Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa Said Bin Jubair رضي الله عنه katika Kauli Yake:

وَلَا أُقْسِمُ بِالنَّفْسِ اللَّوَّامَةِ ﴿٧٥﴾

“Na Ninaapa kwa nafsi inayojilaumu!”

Amesema, inalaumu juu ya kheri na shari. Yamepokewa maneno mfano wa hayo kutokana na Ikrimah. Anasema Ali Bin Abi Najih kutoka kwa Mujaahid: Inajuta kwa mambo iliyoyakosa na inajilaumu.⁴ Na Kauli Yake Allah تعالى:

أَلْحَسِبُ الْإِنْسَانَ أَنْ يُجْمَعَ عِظَامُهُ ﴿٧٦﴾

“Anadhani mtu kuwa Sisi Hatutaikusanya mifupa yake?”

Maana yake: Siku ya Qiyama. Hivi anadhani kwamba Sisi hatuwezi kurudisha mifupa yake na kuikusanya kutoka sehemu zake zilizotengana

بَلَىٰ قَدَرِينَ عَلَىٰ أَنْ تُسَوَّىٰ بِنَانِهِ ﴿٧٧﴾

“Kwani! Sisi Tunaweza hata Kuziweka sawa sawa ncha za vidole vyake!”

Maana yake: Hivi mtu anadhani kwamba Sisi Hatutaikusanya mifupa yake? Kwa nini? Tutaikusanya na Tunaweza Kuzisawazisha zaidi ya tindi za vidole vyake. Yaani, Tunaweza kuvikusanya, na lau Tungetaka tungemfufua hali ya

¹ At-Tabari 24:48.

² Ad-Durr Al-Muthur 8:47, na Al-Qurtubi 19:91.

³ Al-Qurtubi 19:93.

⁴ At-Tabari 24:50.

kuwa amezidi kuliko alivyokuwa na Tukazifanya tindi za vidole vyake kwa maana, nazo ni ncha za vidole vyake zikilingana sawa. Na Kauli Yake تعالى:

بَلْ يُرِيدُ الْإِنْسَانُ لِيَفْجُرَ أَمَامَهُ ﴿٧٥﴾

“Lakini mtu anataka tu kuendelea na maasi kwa siku zilioko mbele yake.”

Maana yake: Kwa Kujipa Matarajio. Mtu husema: Ninafanya makosa kisha nitatubu kabla ya siku ya Kiama. Na husemwa kuwa ni kuipinga haki katikati ya ishara zote za uwepo wa Kiama. Amesema Said kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما anakusudia kwamba anakwenda mbele tu. Na Mujaahid amesema:

لِيَفْجُرَ أَمَامَهُ ﴿٧٥﴾

“Kuendelea kufanya maasi kwa siku zilioko mbele yake.”

Ili aendelee kufuata matamano yake. Na amesema Ali Bin Abi Twalha, kutoka kwa Ibni Abbaas رضي الله عنهما kuwa huyo ni kafiri anaikadhibisha Siku ya Kiama. Siku ya kuhesabiwa.¹ Na kama hivyo amesema Ibn Zayd. Kwa sababu hiyo, Allah تعالى Amesema baadaye:

يَسْأَلُ أَيَّانَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ﴿٧٦﴾

“Anauliza: Lini itakuwa hiyo Siku ya Kiyama?”

Maana yake: Anasema, lini itakuwa Siku ya kiyama. Na hakika swali lake ni la kukifanya Kiama kiko mbali mno kutokea kwake. Na kukadhibisha uwepo wake. Kama Allah تعالى Alivyosema:

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٧٦﴾ قُلْ لَكُمْ مِيعَادُ يَوْمٍ لَا

تَسْتَفْخِرُونَ عَنْهُ سَاعَةً وَلَا تَسْتَغْدِمُونَ ﴿٧٧﴾

“Na wanasema: Ahadi hii itakuwa lini, ikiwa nyinyi mnasema kweli?, Sema: Nyinyi mnayo miadi ya Siku ambayo hamtachelewa nayo kwa saa moja, wala hamtaitangulia.” (34:29-30)

¹ At-Tabari 24:54.

Allah تعالى Amesema hapa:

فَإِذَا بَرِقَ الْبَصَرُ ﴿١٠﴾

“Basi jicho litapo duwaa.”

Abu Amri Bin Al-Alaa Amesoma, ‘Bariqa’ kwa kasri ya ree.¹ Maana yake: Litakapoduwazwa jicho na haya aliyoyasema yanafanana na Kauli Yake Allah تعالى:

لَا يَرْتَدُّ إِلَيْهِمْ طَرْفُهُمْ ﴿١١﴾

“Na macho yao hayapepesi.” (14:43)

Maana yake: Bali watatazama huku na kule kutokana na fazaa hayatatulizana kwao macho juu ya kitu chochote kutokana na khofu.

Wengine wamesoma: ‘Baraqa’ kwa fat’ha na kisomo hicho kiko karibu kwa maana na kisomo cha kwanza, na makusudio ni kwamba macho yatafazaika siku ya Qiyama na yatadhaliika na kunyenyekea, Na yataduwa kutokana na ukubwa wa vituko na vishindo. Na kutokana na ukubwa wa yale ambayo macho yanayashuhudia Siku ya Qiyama – miongoni mwa mambo mbali mbali.

Kauli Yake Allah تعالى:

وَحَسَفَ الْقَمَرُ ﴿١٢﴾

“Na mwezi utapopatwa.”

Maana yake: Mwangaza wake utaondoka.

وَجُمِعَ الشَّمْسُ وَالْقَمَرُ ﴿١٣﴾

“Na likakusanywa jua na mwezi.”

Mujaahid amesema: Vitakunjwa vyote viwili. Ibnu Zaid alisoma wakati wa kuifasiri Aya hii.

إِذَا الشَّمْسُ كُوِّرَتْ ﴿١٤﴾ وَإِذَا النُّجُومُ انْكَدَرَتْ ﴿١٥﴾

“Jua litakapokunjwa, na nyota zikazimwa.” (81:1-2).

Imepokewa kutoka kwa Ibni Mas’uud رضي الله عنه, kwamba yeye alisoma:

(وَجُمِعَ بَيْنَ الشَّمْسِ وَالْقَمَرِ)

“Pakakusanywa baina ya jua na mwezi.”

Na Kauli Yake Allah تعالى:

يَقُولُ الْإِنْسَانُ يَوْمَئِذٍ أَيْنَ الْمَفْرُجُ ﴿١٠﴾

“Siku hiyo mtu atasema: Yako wapi makimbilio?”

Maana yake: Mwanaadamu atakapoyaona haya mambo ya kutisha Siku ya kياما wakati huo atataka kukimbia na atasema: ni wapi mahali pa kukimbilia? Maana yake, Je kuna mahali pa kujihifadhi?

Allah تعالى Amesema:

كَلَّا لَا وَزَرَ ﴿١١﴾ إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمُسْتَقَرُّ ﴿١٢﴾

“La! Hapana pa kukimbilia! Siku hiyo pa kutua ni kwa Mola Wako Mlezi tu.” (75:11-12).

Bin Mas’uud, bin Abbaas na Said Bin Jubair na wengi katika wanazuoni waliotangulia رضي الله عنهم wamesema, maana yake, hakuna kuokoka. Na aya hii ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

مَا لَكُمْ مِّنْ مَّلْجَأٍ يَوْمَئِذٍ وَمَا لَكُمْ مِّنْ نَّكِيرٍ ﴿٤٧﴾

“Siku hiyo hamtakuwa pa kukimbilia wala hamtakuwa na cha kujikingia.” (42:47)

Maana yake: Hamna nyinyi mahali ambapo mtajificha ndani yake, kadhalika amesema hapa:

لَا وَزَرَ ﴿٤٨﴾

“Hapana pa kukimbilia!”

Maana yake: Hamna nyinyi mahali mtakapojikinga. Na kwa ajili hiyo amesema hapa:

إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمُسْتَقَرُّ ﴿٤٩﴾

“Siku hiyo pa kutua ni kwa Mola wako Mlezi tu.”

Maana yake: Marejeo na maishio.

Matendo ya Mtu Yatahudhurishwa Mbele Yake Siku ya Qiyamah

Kisha Allah تعالى Amesema:

يُنَبِّئُوا الْإِنْسَانَ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ ﴿٧٥﴾

“Siku hiyo ataambiwa aliyoyatanguliza na aliyoyaakhirisha.”

Maana yake: Ataelezwa matendo yake yote ya zamani, ya sasa, ya mwanzo, ya mwisho, madogo na makubwa. Kama Allah تعالى Alivyosema:

وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا ۗ وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ أَحَدًا ﴿٧٦﴾

“Na watayakuta yote waliyoyatenda yamehudhuria hapo. Na Mola wako Mlezi Hamdhulumu yeyote.” (18:49).

Kadhalika Amesema hapa:

بَلِ الْإِنْسَانُ عَلَىٰ نَفْسِهِ بَصِيرَةٌ ﴿٧٧﴾ وَلَوْ أَلْقَىٰ مَعَاذِيرَهُ ﴿٧٨﴾

“Bali mtu ni hoja juu ya nafsi yake. Na hata kama atatoa chungu ya udhuru.”

Maana yake: Yeye ni shahidi juu ya nafsi yake anajua aliyoyatenda japokuwa atatoa udhuru na kukanusha. Kama Allah تعالى Alivyosema,

أَقْرَأُ كِتَابَكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا ﴿٧٩﴾

“Soma kitabu chako! Nafsi yako inakutosha leo kukuhisabu.”

Ali Bin Abi Twalha amesema, kutoka kwa Ibni Abbaas رضي الله عنهما

بَلِ الْإِنْسَانُ عَلَىٰ نَفْسِهِ بَصِيرَةٌ ﴿٨٠﴾

“Bali mtu ni hoja juu ya nafsi yake.”

Anasema, usikivu wake, uoni wake, mikono yake, miguu yake na viungo vyake.¹

Qatadah amesema ni shahidi juu ya nafsi yake. Na katika upokezi mwingine amesema, “Ukitaka naapa kwa Mwenyezi Mungu utamuona ni mwenye kuona

¹ At-Tabari 24:62.

sana aibu za watu wengine na dhambi zao, huku anaghafulika na dhambi zake.” Na husemwa: ‘Hakika katika Injili kumeandikwa: Ewe binadamu unaona kibanzi katika jicho la ndugu yako na unaacha kuona boriti katika jicho lako.’ Mujahid amesema:

﴿وَلَوْ أَلْقَىٰ مَعَاذِيرَهُ﴾

“Na ingawa atatoa udhuru mwingi.”

Hata kama atajadiliana na nafsi atatambua jambo hilo.¹ Na amesema Qatadah:

﴿وَلَوْ أَلْقَىٰ مَعَاذِيرَهُ﴾

“Na ingawa atatoa udhuru mwingi.”

Japokuwa siku hiyo atatoa sababu za kujitetea za batili hazitakubaliwa kwake.² As-Sudiy amesema:

﴿وَلَوْ أَلْقَىٰ مَعَاذِيرَهُ﴾

“Na ingawa atatoa udhuru mwingi.”

Hoja yake kama Kauli Yake Allah تعالى.

﴿ثُمَّ لَمْ تَكُنْ فِتْنَتُهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا وَاللَّهِ رَبَّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ﴾

“Kisha hautakuwa udhuru wao ila ni kusema: Wallahi! Mola Wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina.” (6:23)

Kama Kauli Yake Allah تعالى:

﴿يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا فَيَحْلِفُونَ لَهُ كَمَا يَحْلِفُونَ لَكُمْ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ أَلَّا إِنَّهُمْ هُمُ الْكَاذِبُونَ﴾

“Siku ambayo Mwenyezi Mungu Atawafufua watu wote watamuapia kama wanavyowaapia nyinyi na wanadhani kwamba wao wako juu ya jambo, Ehee hakika wao hao ndiyo waongo.” (58:18)

¹ At-Tabari 24:64.

² At-Tabari 24:65.

Al-Awfi amesema kutoka kwa Ibni Abbaas رضي الله عنهما:

وَلَوْ أَلْقَىٰ مَعَاذِيرَهُ ﴿٥١﴾

“...Na ingawa atatoa udhuru mwingi.”

Hizo ni nyudhuru. Hivi husikii kwamba Yeye Amesema

لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذِرَتُهُمْ ﴿٥٢﴾

“Hautawafaa madhaalimu udhuru wao.” (40:52)

Amesema:

وَأَلْقُوا إِلَى اللَّهِ يَوْمَئِذٍ السَّلَامَ ﴿١٦٨٧﴾

“Na siku hiyo watasalimu amri mbele ya Mwenyezi Mungu.” (16:87)

Amesema:

فَأَلْقُوا السَّلَامَ مَا كُنَّا نَعْمَلُ مِنْ سُوءٍ ﴿١٦٢٨﴾

“Basi watasalimu amri, waseme: Hatukuwa tukifanya uovu wowote.” (16:28)

Na kauli yao:

وَاللَّهُ رَبَّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ ﴿٦٢٣﴾

“Tunaapa kwa Mwenyezi Mungu Bwana Wetu hatukuwa wenye kushirikisha.” (6:23)¹

لَا تُحْرِكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ﴿٦٢٣﴾ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ﴿٦٢٤﴾ فَإِذَا قَرَأْتَهُ فَاتَّبِعْ

قُرْآنَهُ ﴿٦٢٥﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ﴿٦٢٦﴾ كَلَّا بَلْ تُحِبُّونَ الْعَاجِلَةَ ﴿٦٢٧﴾ وَتَذَرُونَ الْآخِرَةَ

﴿٦٢٨﴾ وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ ﴿٦٢٩﴾ إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ ﴿٦٣٠﴾ وَوُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ بَاسِرَةٌ ﴿٦٣١﴾ تَنْظُرُ

أَنْ يُفْعَلَ بِهَا فَاقِرَةٌ ﴿٦٣٢﴾

16. Usitukisie huu wahyi ulimi wako kwa kuufanyia haraka.

17. Hakika ni juu Yetu Kuukusanya na Kuusomesha.

18. Tunapousoma, basi nawe fuatiliza kusoma kwake.

¹ At-Tabari 24:64.

19. *Kisha ni juu Yetu Kuubainisha.*
20. *Hasha! Bali nyinyi mnapenda maisha ya duniani,*
21. *Na mnaacha maisha ya Akhera.*
22. *Zipo nyuso siku hiyo zitakazong'ara,*
23. *Zinamuangalia Mola Wao Mlezi.*
24. *Na zipo nyuso siku hiyo zitakazosinyaa.*
25. *Zitajua ya kuwa zitafikiwa na livunjalo uti wa mgongo.*

Vipi Mtume ﷺ Alivyokuwa Anapokea Wahyi

Haya ni mafunzo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye Kushinda Mwenye Kutukuka kwa Mjumbe Wake ﷺ katika namna ya kupokea Wahyi kutoka kwa Malaika kwani yeye Mtume ﷺ alikuwa anafanya haraka katika kupokea wahyi na alikuwa anamtangulia Malaika katika kusoma kwake. Mwenyezi Mungu Mwenye Kushinda Mwenye Kutukuka Akamuamrisha atakapojiwa na Malaika na wahyi amsikilize, kwani Mwenyezi Mungu Amechukua Dhamana ya kuikusanya hiyo Qur'ani kifuani mwake na Atarahisisha kuifikisha kwa njia ambayo malaika ameileta kwake, na kuibainisha kwake, kuifasiri kwake na kuiweka wazi.

Kwa hiyo hali ya kwanza ni kuikusanya kifuani mwake, na hali ya pili ni kuisoma, na hali ya tatu ni kuifasiri na kuweka wazi maana yake.

Na kwa sababu hiyo Allah تعالیٰ Amesema:

لَا تُحْرِكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ﴿١٦﴾

“Usiutikisie huu wahyi ulimi wako kwa kuufanyia haraka.” (75:16)

Maana yake: Kwa Qur'ani. Kama Allah تعالیٰ Alivyosema:

وَلَا تَعْجَلْ بِالْقُرْآنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يُقْضَىٰ إِلَيْكَ وَحْيُهُ ۗ وَقُل رَّبِّ زِدْنِي عِلْمًا ﴿١٦﴾

“Wala usiifanyie haraka hii Qur'ani, kabla haujamalizika ufunuo wake. Na sema: Mola Wangu Mlezi! Nizidishie elimu.” (20:114)

Kisha Allah تعالیٰ Amesema:

إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ

“Hakika ni juu Yetu Kuukusanya.” (75:17) Maana yake: Kifuani kwako.

وَقُرْءَانَهُ

“Na Kuusomesha.” (75:17) Maana yake: Kuisoma kwako.

فَإِذَا قَرَأْتَهُ

“Tunapo usoma.” (75:18) Maana yake: Atakapoisoma kwako Malaika kutoka kwa Allah تعالى.

فَاتَّبِعْ قُرْءَانَهُ

“Basi nawe fuatiliza kusoma kwake.” (75:18) Maana yake: Msikilize kisha isome kama alivyokusomesha.

ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ

“Kisha ni juu yetu kuubainisha.” Maana yake: Baada ya kuihifadhi na kuisoma Tutaiweka wazi kwako, Tutaifafanua na Tutakufahamisha maana yake juu ya vile Tulivyotaka na Tulivyopanga.

Al-Imamu Ahmad amepokea kutoka kwa Ibni Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: Mtume ﷺ alikuwa anapata shida katika kupokea uteremsho wa wahyi kwa hiyo alikuwa anatikisa midomo yake. Amesema: Ibni Abbaas رضي الله عنهما akaniambia mimi: ‘Mimi ninatikisa midomo yangu kama alivyokuwa Mtume ﷺ akiitikisa midomo yake.’ Na Said aliniambia, ‘Na mimi ninatikisa midomo yangu’ kama nilivyomuona Ibni Abbaas رضي الله عنهما anatikisa midomo yake.’ Allah تعالى Akateremsha:

لَا تُحْرِكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ۚ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْءَانَهُ

“Usiutikisie huu wahyi ulimi wako kwa kuufanyia haraka. Hakika ni juu Yetu Kuukusanya na Kuusomesha.”

Amesema: Kuikusanya kifuani mwako kisha unaisoma.

فَإِذَا قَرَأْتَهُ فَاتَّبِعْ قُرْءَانَهُ

“Tunapo usoma, basi nawe fuatiliza kusoma kwake.” Maana yake: Isikilize na unyamaze.

ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ﴿١٩﴾

“Kisha ni juu Yetu Kuubainisha.” (75:19)

Kwa hiyo baada ya hapo akawa anapoondoka Jibril عليه السلام anaisoma Qur’ani kama alivyomsomesha.¹

Ameyapokea hayo Al-Bukhari. Akawa wakati Jibril عليه السلام anapomjia huinamisha kichwa na pindi anapoondoka huisoma Qur’ani kama alivyomuahidi Allah تعالى.²

Sababu ya Kukadhibisha Siku ya Qiyama ni Kupenda Dunia na Kughafilika na Akhera

Kauli Yake Allah تعالى.

كَلَّا بَلْ تُحِبُّونَ الْعَاجِلَةَ ﴿٢٠﴾ وَتَذَرُونَ الْآخِرَةَ ﴿٢١﴾

“Hasha! Bali nyinyi mnapenda maisha ya duniani, na mnaacha maisha ya Akhera.”

Maana yake: Jambo pekee lililosababisha wakanushe siku ya Kiama na kupinga Wahyi wa kweli na Qur’an Tukufu ambayo Allah تعالى Alimteremshia Mjumbe wake, ni kuwa wao wamezama katika maisha ya mpito ya kidunia. Wameyapuuza maisha ya Akhera.

Kumuona Allah تعالى

Kisha Allah تعالى Anasema:

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ ﴿٢٢﴾

“Zipo nyuso siku hiyo zitakazong’ara.” (75:22)

Maana yake: Nzuri zenye kuvutia na zenye furaha.

إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ ﴿٢٣﴾

“Zinamuangallia Mola Wao Mlezi.”

¹ Ahmad 1:343.

² Fat’h Al-Bari 1:39, 8:547, 549, 550, 707, na 13:508, na Muslim 1:330.

Maana yake: Zitamuona kwa macho, kama alivyopokea hilo Al-Bukhari katika sahihi yake:

«إِنَّكُمْ سَتَرُونَ رَبَّكُمْ عَيْنًا»

“Hakika nyinyi mtamuona Mola Wenu Mlezi kwa macho”.¹

Imethibitika waumini kumuona Allah عزوجل Akhera, katika hadithi nyingi sahihi, zilizopokewa kwa wingi na maimamu wa hadithi kwa namna ambayo ni vigumu kuzikataa Hadithi hizo. Kama vile Hadithi ya Abi Said na Abu Hurayrah رضي الله عنهما na Hadithi hizo zimo katika sahihi Al-Bukhari na Muslim, kwamba kuna watu walisema, ‘Ee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Je tutamuona Bwana wetu Siku ya Qiyama?’ Mtume ﷺ akasema:

«هَلْ تَفَارُونَ فِي رُؤْيَةِ الشَّمْسِ وَالْقَمَرِ لَيْسَ دُونَهُمَا سَحَابٌ؟»

“Jee mnadhuriwa katika kuona jua na mwezi pasipokuwa na mawingu mbele yake”

Wakasema: ‘Hapana.’ Akasema:

«فَإِنَّكُمْ تَرُونَ رَبَّكُمْ كَذَلِكَ»

“Kwa hakika nyinyi mtamuona Bwana Wenu kama hivyo”.²

Imekuja katika sahihi ya Al-Bukhari na Muslim kutoka kwa Jarir رحمه الله تعالى amesema: Mtume ﷺ alitazama mwezi katika usiku wa mbala mwezi, akasema:

«إِنَّكُمْ تَرُونَ رَبَّكُمْ كَمَا تَرُونَ هَذَا الْقَمَرَ، فَإِنْ اسْتَطَعْتُمْ أَنْ لَا تُغْلِبُوا عَلَى صَلَاةٍ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَلَا قَبْلَ غُرُوبِهَا، فَافْعَلُوا»

“Hakika nyinyi mtamuona Mola Wenu kama mnavyoona mwezi huu, na iwapo mtaweza kutoshindwa juu ya Sala kabla ya kuchomoza jua, wala kabla ya kuzama kwake fanyeni”.³

Muslim amepokea peke yake kutoka kwa Suhaib kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

¹ Fat'h Al-Bari 13:430.

² Fat'h Al-Bari 13:430, 431 na Muslim 1:163, 162.

³ Fat'h Al-Bari 13:429, na Muslim 1:439.

«إِذَا دَخَلَ أَهْلُ الْجَنَّةِ الْجَنَّةَ - قَالَ - يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: تُرِيدُونَ شَيْئًا أَزِيدُكُمْ؟ فَيَقُولُونَ: أَلَمْ نُبَيِّضْ وُجُوهَنَا؟ أَلَمْ نُدْخِلْكَ الْجَنَّةَ وَنُجِّنَا مِنَ النَّارِ؟ قَالَ: فَيَكْتُمُ الْجَنَابَ، فَمَا أُعْطُوا شَيْئًا أَحَبَّ إِلَيْهِمْ مِنَ النَّظَرِ إِلَى رَبِّهِمْ، وَهِيَ الزِّيَادَةُ»

“Watu wa Peponi watakapoingia Peponi, Mtume amesema,; Atasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ‘Jee mnataka kitu chochote niwaongezezi?’ Watasema: ‘kwani hukuzifanya nyeupe nyuso zetu? kwani hukutuingiza Peponi na ukatuepusha na moto?’ Amesema: ‘Hapo litafunuliwa pazia hawatakuwa wamepewa kitu chochote kinachopendeza sana kwao kuliko kumuona Mola Wao, na hiyo ndiyo nyongeza.”

Kisha akasoma aya hii:

﴿لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا أَحْسَنُ زِيَادَةً﴾

“Kwa wafanyao wema ni wema na zaidi.” (10:26).¹

Muslim amepokea kutoka kwa Jaabir رضي الله عنه katika hadithi yake,

﴿إِنَّ اللَّهَ يَتَجَلَّى لِلْمُؤْمِنِينَ بِضَحْكَ﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Atadhihiri kwa waumini hali ya kuwa Anacheka.”²

Anakusudia katika viwanja vya Qiyama. Katika hadithi hizi, ni kwamba waumini watamuona Mwenye Kushinda na Kutukuka katika viwanja vya Qiyama na katika mabustani ya Peponi. Na lau si kuogopa kurefusha tungezileta hadithi hizo kwa njia zake, na matamko yake, *Sahihi, Hassan, Musnad na Sunan*.

Isipokuwa tumezitaja hadithi hizi mahali pengi kwa kuzitawanya katika tafsiri hii. Taufiki ni kwa Mwenyezi Mungu tu.

Na hili kwa Himidi za Allah تعالى limekubaliwa kati ya Masahaba na Taabiina, na watangulizi wa ummah huu, kama ambavyo jambo hill limekubaliwa kwa pamoja kati ya maimamu wa Uislamu na waongozi wa watu.

¹ Muslim 1:163.

² Muslim 1:178.

Nyuso za Watu Waovu Zitakuwa Nyeusi Siku ya Qiyama

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَوُجُوهُ يَوْمَئِذٍ بِآسِرَةٍ ﴿٢٥﴾ تَنْظُنُّ أَنْ يُفْعَلَ بِهَا فَاقِرَةٌ ﴿٢٦﴾

“Na zipo nyuso siku hiyo zitakazokunjana. Zitajua ya kuwa zitafikiwa na livunjalo uti wa mgongo.”

Nyuso za watu waovu Siku ya Qiyama zitakuwa nyeusi. Amesema Qatadah: Zitakunjika.¹ Na As-Suddi amesema: zitabadilika rangi zake.²

تَنْظُنُّ

“Zitajua” (75:25). Maana yake: Zitayakinisha

أَنْ يُفْعَلَ بِهَا فَاقِرَةٌ ﴿٢٦﴾

“Zitafikiwa na livunjalo uti wa mgongo.”

Mujahid amesema: ‘Balaa.’³ Qatadah amesema: ‘Shari.’ Na amesema As-Sudy zitakuwa na uhakika kwamba zitaangamia. Amesema Ibnu Zaid, Zitakuwa na uhakika kwamba zitaingia motoni. Maneno haya ni kama Maneno Yake Allah تعالى.

يَوْمَ تَبْيَضُّ وُجُوهٌُ وَتَسْوَدُّ وُجُوهٌُ

“Siku ambayo nyuso zitanawiri na nyuso zitasawijika.” (3:106).

Kama Kauli Yake Allah تعالى.

وَوُجُوهُ يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرَةٌ ﴿٣٨﴾ ضَاحِكَةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ ﴿٣٩﴾ وَوُجُوهُ يَوْمَئِذٍ عَلَيْهَا غَبَرَةٌ ﴿٤٠﴾

تَرَاهُهَا قَتَرَةٌ ﴿٤١﴾ أُولَئِكَ هُمُ الْكٰفِرَةُ الْفٰجِرَةُ ﴿٤٢﴾

“Siku hiyo ziko nyuso zitakazonawiri, zitacheka, zitachangamka; na nyuso siku hiyo zitakuwa na mavumbi, giza toloro litazifunika, Hao ndio makafiri watenda maovu.” (80:38-42).

Kama Kauli Yake Allah تعالى.

¹ At-Tabari 24:74.

² Al-Qurtubi 19:110.

³ At-Tabari 24:74.

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ خَشِيعَةٌ ﴿٢٤﴾ عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿٢٥﴾ تَصَلَّىٰ نَارًا حَامِيَةً ﴿٢٦﴾

“Siku hiyo nyuso zitainama, zikifanya kazi, nazo taabani. Ziingie katika Moto unao waka.” (88:2-4).

Mpaka Aliposema:

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاعِمَةٌ ﴿٨﴾ لِّسَعْيِهَا رَاضِيَةٌ ﴿٩﴾ فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ﴿١٠﴾

“Siku hiyo nyuso nyengine zitakuwa kunjufu. Zitakuwa radhi kwa juhudi yao, katika Bustani ya juu.” (88:8-10).

Na mfano wa hizo katika aya mbali mbali na mtiririko wake.

* * *

كَلَّا إِذَا بَلَغَتِ التَّرَاقِيَ ﴿٢٦﴾ وَقِيلَ مَنْ رَاقٍ ﴿٢٧﴾ وَظَنُّهُ أَنَّهُ
 الْفِرَاقُ ﴿٢٨﴾ وَالْتَفَتِ إِلَى السَّاقِ بِالسَّاقِ ﴿٢٩﴾ إِلَى رَبِّكَ
 يَوْمَئِذٍ الْمَسَاقُ ﴿٣٠﴾ فَلَا صَدَقَ وَلَا صَلَّى ﴿٣١﴾ وَلَكِنْ
 كَذَّبَ وَتَوَلَّى ﴿٣٢﴾ ثُمَّ ذَهَبَ إِلَىٰ أَهْلِهِ يَتَمَطَّى ﴿٣٣﴾ أَوْلَىٰ
 لَكَ فَأَوْلَىٰ ﴿٣٤﴾ ثُمَّ أَوْلَىٰ لَكَ فَأَوْلَىٰ ﴿٣٥﴾ أَتُحَسِبُ الْإِنْسَانَ
 أَن يُتْرَكَ سُدًى ﴿٣٦﴾ أَلَمْ يَكُ نُطْفَةً مِن مَّنِيِّ يُمْنَىٰ ﴿٣٧﴾
 ثُمَّ كَانَ عِلْقَةً فَطَلَقَ فَسَوَىٰ ﴿٣٨﴾ فَجَعَلَ مِنْهُ الزَّوْجَيْنِ
 الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ ﴿٣٩﴾ أَلَيْسَ ذَلِكَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَن نُّحْيِيَ
 الْمَوْتَىٰ ﴿٤٠﴾

كَلَّا إِذَا بَلَغَتِ التَّرَاقِيَ ﴿٢٦﴾ وَقِيلَ مَنْ رَاقٍ ﴿٢٧﴾ وَظَنُّهُ أَنَّهُ الْفِرَاقُ ﴿٢٨﴾
 وَالْتَفَتِ إِلَى السَّاقِ بِالسَّاقِ ﴿٢٩﴾ إِلَى رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمَسَاقُ ﴿٣٠﴾ فَلَا
 صَدَقَ وَلَا صَلَّى ﴿٣١﴾ وَلَكِنْ كَذَّبَ وَتَوَلَّى ﴿٣٢﴾ ثُمَّ ذَهَبَ إِلَىٰ أَهْلِهِ
 يَتَمَطَّى ﴿٣٣﴾ أَوْلَىٰ لَكَ فَأَوْلَىٰ ﴿٣٤﴾ ثُمَّ أَوْلَىٰ لَكَ فَأَوْلَىٰ ﴿٣٥﴾
 أَتُحَسِبُ الْإِنْسَانَ أَن يُتْرَكَ سُدًى ﴿٣٦﴾ أَلَمْ يَكُ نُطْفَةً مِن مَّنِيِّ يُمْنَىٰ ﴿٣٧﴾
 ثُمَّ كَانَ عِلْقَةً فَطَلَقَ فَسَوَىٰ ﴿٣٨﴾ فَجَعَلَ مِنْهُ الزَّوْجَيْنِ
 الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ ﴿٣٩﴾ أَلَيْسَ ذَلِكَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَن نُّحْيِيَ
 الْمَوْتَىٰ ﴿٤٠﴾

كَانَ عِلْقَةً فَطَلَقَ فَسَوَىٰ ﴿٣٨﴾ فَجَعَلَ مِنْهُ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ ﴿٣٩﴾ أَلَيْسَ ذَلِكَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَن نُّحْيِيَ الْمَوْتَىٰ ﴿٤٠﴾

26. La, hash! (Roho) itakapofikia kwenye mishipa ya koo,

27. Na pakasemwa: Nani wa kumganga?

28. Na mwenyewe akajua kwa hakika kuwa huko ndiko kufariki;

29. Na utapo ambatishwa muundi kwa muundi,

30. Siku hiyo ndiyo kuchungwa kupelekwa kwa Mola Wako Mlezi!

31. Kwa sababu hakusadiki, wala hakusali.

32. Bali alikanusha, na akageuka.

33. Kisha akenda kwa ahali zake kwa matao.

34. Ole wako, ole wako!

35. *Kisha Ole wako, ole wako!*

36. *Ati anadhani binaadamu kuwa ataachwa bure?*

37. *Kwani hakuwa yeye tone ya manii lilio shushwa?*

38. *Kisha akawa kidonge cha damu, tena Mwenyezi Mungu Akamuumba na Akamtengeneza vilivyo.*

39. *Kisha Akamfanya namna mbili, mwanamume na mwanamke.*

40. *Je! Huyu aliyeyafanya yote hayo hakuwa ni Muweza wa kufufua wafu?*

Yakini Itapatikana Wakati wa Kujiwa na Mauti

Allah تعالى Anaeleza, Kuhusiana na hali ya kufikwa na mauti na yaliyo mbele yake miongoni mwa vitisho, Tunamuomba Allah تعالى Atuthibitisha huko kwa kauli thabiti. Allah تعالى Amesema.

كَلَّا إِذَا بَلَغَتِ الرَّاقِيَ ﴿٦٦﴾

“La, hash! (Roho) itakapofikia kwenye mifupa ya koo.”

‘Kallaa’ ni tamko la makemeo. Maana yake: Ewe Mwanadamu huko hatakadhibisha yale ambayo umeelezwa, bali mambo hayo yatakuwa bayana kwako. Na tukilifanya neno ‘Kallaa’ kwa maana ya kweli, basi maana yake itakuwa dhahiri. Maana yake: Ni kweli pindi roho itakapofikia katika mitulinga. Maana yake: Itakapotolewa roho yako katika mwili wako na ikafikia katika mitulinga, na hiyo ni mifupa ya Mtulinga. Kama Kauli Yake Allah تعالى.

فَلَوْلَا إِذَا بَلَغَتِ الْحُلُقُومَ ﴿٦٧﴾ وَأَنْتُمْ حِينِيذٍ تَنْظُرُونَ ﴿٦٨﴾ وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْكُمْ وَلَكِنْ

لَا تَبْصُرُونَ ﴿٦٩﴾ فَلَوْلَا إِنْ كُنْتُمْ غَيْرَ مَدِينِينَ ﴿٧٠﴾ نَرْجِعُونَهَا إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٧١﴾

“Yawaje basi itakapofika roho kwenye koo, Na nyinyi wakati huo mnatazama! Na Sisi Tuko karibu zaidi naye kuliko nyinyi. Na lakini nyinyi hamumo katika mamlaka Yangu? Kwanini hamuirudishi hiyo roho, ikiwa nyinyi mnasema kweli?” (56:83-87).

Kama Hivyo Amesema Hapa.

كَلَّا إِذَا بَلَغَتِ التَّرَاقِيَ ﴿٦٦﴾ وَقِيلَ مَنْ رَاقٍ ﴿٦٧﴾

“La, hashah! (Roho) itakapofikia kwenye mifupa ya koo, na pakasemwa: Nani wa kumganga.”

Amesema Ikrima kutoka kwa Ibni Abbas رضي الله عنهما. Maana yake: ‘Ni nani mganga atakayetibu?’¹ Na kama hivyo amesema Abu Qilabah,

وَقِيلَ مَنْ رَاقٍ ﴿٦٧﴾

“Na pakasemwa: Nani wa kumganga.”

Maana yake: “Ni nani tabibu atakayemponya.”² Na kama hivyo amesema Qatadah na Adh-Dhahaak na Ibni Zayd.³ Ali Bin Abi Twalha amesema kutoka kwa Ibni Abbas رضي الله عنهما,

وَأَلْتَفَّتْ السَّاقُ بِالسَّاقِ ﴿٦٨﴾

“Na utapoambatishwa muundi kwa muundi.”

Anasema: Hiyo itakuwa mwisho wa siku katika siku za dunia, na mwanzo wa siku katika siku za akhera, hapo atakutana na shida juu ya shida isipokuwa mtu aliyerehemewa na Allah تعالى.⁴ Ikrima amesema:

وَأَلْتَفَّتْ السَّاقُ بِالسَّاقِ ﴿٦٨﴾

“Na utapoambatishwa muundi kwa muundi.”

Jambo kubwa kwa jambo kubwa. Amesema Mujaahid: Litakutana balaa kwa balaa. Al-Hasan Al-Basry amesema katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَلْتَفَّتْ السَّاقُ بِالسَّاقِ ﴿٦٨﴾

“Na utapo ambatishwa muundi kwa muundi.”

¹ At-Tabari 24:75.

² At-Tabari 24:75.

³ At-Tabari 24:75.

⁴ At-Tabari 24:76.

Hiyo ni miundi yako miwili itakapokutana.¹ Na katika upokezi mwingine kutokana na yeye: miguu itakufa na haitaweza kumchukua na alikuwa juu ya miguu miwili hiyo mwenye kuzunguka.²

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمَسَاقُ ﴿٦٢﴾

“Siku hiyo ndiye kuchungwa kupelekwa kwa Mola Wako Mlezi!”

Maana yake: Marejeo na kurejea huko, Ni kwamba roho itanyanyuliwa hadi mbinguni. Mwenyezi Mungu, Mwenye Kushinda na Kutukuka Atasema: Mrudisheni mja Wangu ardhini kwani Mimi kutokana na hiyo ardhi Nimemuumba na katika hiyo ardhi Nitamrudisha na katika hiyo ardhi Nitamtoa mara nyingine, kama ilivyokuja katika hadithi ndefu ya Al-Baraa.³

Kwa hakika Allah تعالى Amesema.

وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ ۖ وَيُرْسِلُ عَلَيْكُمْ حَفَظَةً حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ تَوَفَّتْهُ
رُسُلُنَا وَهُمْ لَا يُفِرُّونَ ﴿٦١﴾ ثُمَّ رُدُّوْا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمْ الْحَقَّ ۚ لَا لَهُ الْحُكْمُ وَهُوَ أَسْرَعُ
الْحُسْبَيْنِ ﴿٦٢﴾

“Naye ndiye Mwenye Nguvu za Kushinda, Aliye juu ya waja wake. Na Hukupelekeeni waangalizi, mpaka mmoja wenu yakimjia mauti wajumbe Wetu Humfisha, nao hawafanyi taksiri. Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa Haki. Hakika, Hukumu ni Yake. Naye ni Mwepesi kuliko wote wanao hisabu.”
(6:61-62).

¹ At-Tabari 24:78.

² Al-Qurtubi 19:112.

³ At-Tiwal na At-Tabarani namba 238.

Kutajwa kwa Hali ya Mkadhibishaji

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَلَا صَدَقَ وَلَا صَلَّى ﴿٣١﴾ وَلٰكِنْ كَذَّبَ وَتَوَلَّى ﴿٣٢﴾

“Kwa sababu hakusadiki, wala hakusali. Bali alikanusha, na akageuka.” (75:30-31)

Kutajwa huku kunamuhusu kafiri ambaye alikuwa duniani akikadhibisha ukweli kwa moyo wake, na kufuatishia kwa vitendo vyake. Kwa hiyo hana kheri yoyote ya ndani wala ya nje, na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى.

فَلَا صَدَقَ وَلَا صَلَّى ﴿٣٣﴾ وَلٰكِنْ كَذَّبَ وَتَوَلَّى ﴿٣٤﴾ ثُمَّ ذَهَبَ إِلَىٰ أَهْلِهِ يَتَمَطَّى ﴿٣٥﴾

“Kwa sababu hakusadiki, wala hakusali. Bali alikanusha, na akageuka. Kisha akenda kwa ahali zake kwa matao.” (75:31-33).

Maana yake: Akiwa na furaha, kujiona, kiburi na mvivu hana hima yoyote ya kazi. Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَإِذَا أُنْقَلَبُوا إِلَىٰ أَهْلِهِمْ أُنْقَلَبُوا فٰكِهِينَ ﴿٨٣﴾

“Na wanapo rudi kwa watu wao hurudi nao wamefurahi.” (83:31).

Amesema Allah تعالى:

إِنَّهُمْ كَانُوا فِيْ أَهْلِهِمْ مُّسْتُرُوْرًا ﴿٨٤﴾ إِنَّهُمْ ظَنُّوا أَن لَّنْ نَّحْوَرَ ﴿٨٥﴾

“Hakika alikuwa furahani kati ya jamaa zake. Huyu hakika alidhani kuwa hatarejea tena.” (84:13-14).

Maana: Hatarejea.

بَلَىٰ إِنَّ رَبَّهُ كَانَ بِمُبْصِرًا ﴿٨٦﴾

“Kwani? Hakika Mola Wake Mlezi Alikuwa Akimuona!” (84:15).

Amesema Adh-Dhahaak kutoka kwa Ibni Abbaas رضي الله عنهما

ثُمَّ ذَهَبَ إِلَىٰ أَهْلِهِ يَتَمَطَّى ﴿٨٧﴾

“Kisha akenda kwa ahali zake kwa matao.”

Maana: Anajivuna.¹ Na amesema Qatadah na Zaid Bin Aslam: Anajifaharisha.²
Amesema Allah تعالى:

أَوَّلِي لَكَ فَأَوَّلِي ۝ ثُمَّ أَوَّلِي لَكَ فَأَوَّلِي ۝

“Ole wako, ole wako! Kisha Ole wako, ole wako!”

Hivi ni vitisho na makamio ya nguvu kutoka kwa Allah تعالى kwa yule anaye mkufuru, anayetembea kwa kujiona. Maana: Unayo haki ya kwenda mwendo huu na hali ya kuwa umemkufuru Mola Wako na Muumba Wako?. Kama ambavyo husemwa katika mfano wa hili kwa njia ya kumkejeli na kumtisha. Kama Kauli Yake Allah تعالى:

ذُقْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ۝

“Onja! Ati wewe ndiye mwenye nguvu, mtukufu!” (44:49).

Kama Kauli Yake Allah تعالى:

كُلُوا وَتَمَتَّعُوا قَلِيلًا إِنَّكُمْ تُجْرِمُونَ ۝

“Kuleni na mjifurahishe kidogo tu. Hakika nyinyi ni wakosefu!” (77:46).

Kauli Yake Allah تعالى:

فَاعْبُدُوا مَا شِئْتُمْ مِنْ دُونِهِ ۝

“Basi nyinyi abuduni mpendacho badala Yake Yeye.” (39:15)

Kama Kauli Yake Allah تعالى:

اعْمَلُوا مَا شِئْتُمْ ۝

“Tendeni mpendavyo.” (41:40) Na aya nyinginezo.

Abu Abdirahmaan An-Nasai amepokea kutoka kwa Said Bin Jubair amesema:
Nilimuambia Ibni Abbaas رضي الله عنهما:

¹ Ad-Dur Al-Mansur 8:363.

² At-Tabari 24:81.

أُولَىٰ لَكَ فَأُولَىٰ ۖ ثُمَّ أُولَىٰ لَكَ فَأُولَىٰ ۖ

“Ole wako, ole wako! Kisha Ole wako, ole wako!”

Akasema: aliyasema hayo Mtume ﷺ kumuambia Abu Jahli kisha Allah تعالى Akateremsha maneno hayo.¹

Amepokea Ibnu Abi Hatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Qatadah Kauli Yake,

أُولَىٰ لَكَ فَأُولَىٰ ۖ ثُمَّ أُولَىٰ لَكَ فَأُولَىٰ ۖ

“Ole wako, ole wako! Kisha Ole wako, ole wako!”

Hayo ni makamio juu ya makamio, ‘Ole wako, kisha Ole wako’ mnavyosikia. Na wamedai kwamba Mtume ﷺ alizikamata nguo za adui wa Allah Abu Jahli, kisha akamuambia: “Adui wa Mwenyezi Mungu.” Abu Jahli akasema, ‘Hivi unanikaripia ewe Muhammad? Naapa kwa Mwenyezi Mungu hutaweza wewe wala Bwana wako kufanya chochote, na kwa hakika mimi ni Mtukufu sana kuliko yoyote mwenye kwenda kati ya majabali mawili ya Makkah.’

Mwanadamu Hataachwa Hivi Hivi Tu

Kauli Yake Allah تعالى،

أَلَيْسَ الْإِنْسَانُ أَنْ يُتْرَكَ سُدًى ۖ

“Ati anadhani binaadamu kuwa ataachwa bure?”

As-Suddi amesema: Anakusudia: hatafufuliwa? hataamrisha wala kukatazwa. Amesema Mujaahid, As-Shaafii na Abdurrahmaan bin Zaid bin Aslam, anakusudia, haamrishi wala hakatazwi? Lili lowazi ni kwamba aya inajumuisha hali zote mbili. Maana yake, aidha, hatoachwa hivi hivi tu bila ya kufufuliwa. Bali ni kwamba yeye ataamrisha na kukatazwa. Kaburini kwake hapa duniani atakusanywa. Kwa Mwenyezi Mungu katika nyumba ya akhera atarejea. Na makusudio hapa ni kuthibitisha suala la kurejea akhera na kuwapinga wale wenye kukanusha hilo katika watu waovu, wajinga, na wapingaji.

¹ An-Nasai katika Al-Kubra 6:504.

Kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema hali ya kutoa hoja ya Kuwarejesha viumbe huko akhera. Kwa kuwa Aliweza Kuwaumba wao kwa mara ya kwanza. Allah تعالى Amesema:

أَلَمْ يَكُنْ نُطْفَةً مِّنْ مَّنِيِّ يُمْنَىٰ ﴿٧٥﴾

“Kwani hakuwa yeye tone ya manii lilio shushwa?”

Maana yake: Kwani mwanadamu hakuwa tone la manii dhaifu – kutokana na maji manyonge?. Yanamwagwa kutoka katika uti wa mgongo katika mifuko ya uzazi.

ثُمَّ كَانَ عَلَقَةً فَخَلَقَ فَسَوَّىٰ ﴿٧٦﴾

“Kisha akawa kidonge cha damu, tena Mwenyezi Mungu Akamuumba na Akamtengeneza vilivyo.”

Akawa pande la damu, kisha pande la nyama kisha Akatengeneza na Akapulizia ndani yake roho. Akawa kiumbe mwingine aliye sawa, aliyesalimika viungo, mwanamume au mwanamke kwa idhini ya Allah تعالى na makadirio Yake. Na kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema:

فَجَعَلَ مِنْهُ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ ﴿٧٧﴾

“Kisha Akamfanya namna mbili, mwanamume na mwanamke.”

Kisha Allah تعالى Akasema:

أَلَيْسَ ذَٰلِكَ بِقَدِيرٍ عَلَيَّ أَنْ تُحْيِيَ الْمَوْتَىٰ ﴿٧٨﴾

“Je! Huyu hakuwa ni Muweza wa Kufufua wafu?” (75:40).

Maana yake: Hivi Huyu Aliyeliumba hili umbo lililo sawa sawa kutokana na hili tone la manii lililonyongea hakuwa ni Mwenye Kuweza Kulirudisha kama alivyolianzisha? Na uwezo wa kurejesha upo ama kwa njia bora zaidi kwa mnasaba wa kuanzisha, au kulinganisha juu ya kauli mbili, kama ilivyokuja Kauli Yake Allah تعالى:

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ ﴿٧٩﴾

“Na Yeye Ndiye Anayeanzisha Uumbaji, kisha Ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake.” (30:27)

Kauli ya kwanza ni mashuhuri sana kama ilivyotangulia katika *Suratu Ar-Ruum*, ubainifu wake na uthibitisho wake. Na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Dua Wakati wa Kuimaliza Sura Hii

Amepokea Abu Dawuud رضي الله عنه kutoka kwa Musa bin Abi Aishah amesema: Mtu mmoja alikuwa anasali juu ya nyumba yake, na kila aliposoma,

أَلَيْسَ ذَٰلِكَ بِقَدِيرٍ عَلَيَّ أَنْ تُجِئَنِي الْمَوْتُ ﴿٤٠﴾

“Je! Huyu hakuwa ni Muweza wa kufufua wafu?” (75:40).

Alisema: “Utakatifu ni Wako, hakuna shaka.” Wakamuuliza kuhusiana na maneno yake hayo akasema: ‘Nimeyasikia maneno haya kutoka kwa Mtume ﷺ.¹ Ameipokea Abuu Dawuud peke yake, na hakumtaja swahaba huyu, na hilo halidhuru chochote.

Mwisho wa tafsiri ya *Suratu Al-Qiyamah*. Kuhimidiwa pamoja na Kusifiwa ni kwa Allah تعالى tu.

* * *

¹ Abu Dawud 1:549.

Tafsiri ya Suratul Insan¹

Sura ya 76

Iliteremshwa Makkah

Kusomwa kwa Suratu *Al-Ssajdah na Surat Al-Insan* katika Sala Siku ya Ijumaa.

Imetangulia katika sahihi Muslim, kutoka kwa Ibni Abbaas رضي الله عنهما kwamba Mtume ﷺ alikuwa anasoma katika Sala ya Asubuhi siku ya Ijumaa

الْمُرُوءَاتُ تَنْزِيلُ

“Alif – Laam Miim Tanzil.” (32) Na:

هَلْ أُنِى عَلَى الْإِنْسَانِ

“Hal-ataa ‘alal’insaan.” (76)¹

* * *

¹ Muslim 2:599.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْإِنْسَانِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

هَلْ أَتَى عَلَى الْإِنْسَانِ حِينٌ مِّنَ الدَّهْرِ لَمْ يَكُن شَيْئًا مَّذْكُورًا ﴿١﴾
 إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِن نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٢﴾
 إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾
 إِنَّا أَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ سَلَاسِلًا وَأَغْلَلْنَا وَسْعِيرًا ﴿٤﴾
 إِنَّ الْأَبْرَارَ يَشْرَبُونَ مِن كَأْسٍ كَانَ مِزَاجُهَا كَافُورًا ﴿٥﴾
 عَيْنًا يُفَرِّبُهَا عِبَادُ اللَّهِ يُفَجِّرُونَهَا تَفْجِيرًا ﴿٦﴾
 يُوفُونَ بِالْأَنْذَرِ وَيَخَافُونَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهُ مُسْتَطِيرًا ﴿٧﴾
 وَيُطْعَمُونَ الطَّعَامَ عَلَى حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٨﴾
 إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكْرًا ﴿٩﴾
 إِنَّا نَخَافُ مِن رَّبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا ﴿١٠﴾
 فَوَقَدْنَاهُمْ اللَّهُ شَرَّ ذَلِكَ الْيَوْمِ وَلَقَّاهُمْ نَضْرَةً وَسُرُورًا ﴿١١﴾
 وَجَزَّاهُمْ بِمَا صَبَرُوا جَنَّةً وَحَرِيرًا ﴿١٢﴾

هَلْ أَتَى عَلَى الْإِنْسَانِ حِينٌ مِّنَ الدَّهْرِ لَمْ يَكُن شَيْئًا مَّذْكُورًا ﴿١﴾
 إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِن نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٢﴾
 إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾

1. Hakika kilimpitia binaadamu kipindi katika zama ambacho kwamba hakuwa kitu kinachotajwa.

2. Hakika Sisi Tume-muumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyo changanyika. Tumfanyie mtihani. Kwa hivyo Tukamfanya mwenye kusikia, mwenye kuona.

3. Hakika Sisi Tume-mbainishia Njia. Ama ni mwenye kushukuru, au mwenye kukufuru.

Allah تعالی Kumuumba Mwanadamu Baada ya Kuwa Hakuwepo

Allah تعالی Anasema Akielezea kuhusu mwanadamu kwamba Yeye Amempatisha baada ya kutokuwepo wala kuwa ni kitu chenye kutajwa kutokana na uduni na unyonge wake. Allah تعالی Amesema:

هَلْ أَتَى عَلَى الْإِنْسَانِ حِينٌ مِّنَ الدَّهْرِ لَمْ يَكُنْ شَيْئًا مَّذْكُورًا ﴿١﴾

“Hakika kilimpitia binaadamu kipindi katika zama ambacho kwamba hakuwa kitu kinachotajwa.” (76:1)

Kisha Akaliweka wazi hilo. Allah تعالی Akasema:

إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِن نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ

“Hakika Sisi Tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyo changanyika.” (76:2)

Maana yake: Mchanganyiko wa baadhi ya vitu. Amesema Ibnu Abbaas رضي الله عنهما katika Kauli Yake Allah تعالی:

مِن نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ

“Kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika.” (76:2).

Anakusudia: Maji ya mwanamume na maji ya mwanamke yatakapokutana na kuchanganyika.¹ Kisha yanahama baada ya hapo kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine, na hali moja hadi hali nyingine, na rangi moja kwenda rangi nyingine. Na kama hivyo amesema Ikrimah, Mujaahid, Al-Hassan na Ar-Rabi'i Bin Anas: 'Al-Amshaaj': ni mchanganyiko wa maji ya mwanamume na maji ya Mwanamke.² Kauli Yake Allah تعالی:

نَّبْتَلِيهِ

“Tumfanyie mtihani.” (76:2) Maana yake: Tunamjaribu. Kama Kauli Yake Allah تعالی:

لِيَبْلُوكُم بِأَكْبَرِ أَحْسَنُ عَمَلًا

“Ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi.” (67:2)

¹ At-Tabari 24:89.

² At-Tabari 24:89, 90.

Kisha Allah تعالى Anasema:

فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٦﴾

“Kwa hivyo Tukamfanya mwenye kusikia, mwenye kuona.”

Maana yake: Tumempa usikivu na uoni, kwa viwili hivyo anaweza kutii na kuasi.

Mwenyezi Mungu Amemuongoza Mwanadamu Njia, kwa Hiyo Ima Atashukuru Ama Atakufuru

Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ

“Hakika Sisi Tumembainishia njia.” Maana yake: Tumembainishia, Tumemfafanulia na Tumemuonesha. Kama Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَاهُمْ فَاسْتَحَبُّوا الْعَمَىٰ عَلَىٰ الْهُدَىٰ

“Na ama Thamudi Tuliwaongoza, lakini walipenda upofu kuliko uwongofu.” (41:17)

Kama Kauli Yake Allah تعالى:

وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ ﴿١٠﴾

“Na Tukambainishia njia zote mbili?” (90:10).

Maana yake: Tumemuekea wazi njia ya kheri na ya shari. Na hii ni kauli ya Ikrimah na Atiyyah, Ibni Zaid na Mujaahid katika kauli iliyo mashuhuri kwake na kwa jopo kubwa la wanazuoni.

Kauli Yake Allah تعالى:

إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٦﴾

“Ama ni mwenye kushukuru, au mwenye kukufuru.”

Makadirio yake: Yeye katika hilo ima awe muovu au mwema. Kama ilivyokuja katika hadithi ambayo ameipokea Muslim kutoka kwa Aby Maalik Al-Ash’ari amesema: Mtume ﷺ amesema :

«كُلُّ النَّاسِ يَغْدُو فَبَائِعٌ نَفْسَهُ، فَمُؤَيِّقُهَا أَوْ مُعْتِقُهَا»

“Kila mtu anapodamka asubuhi nafsi yake huiweka mnadani, kuna

anayeitia nafsi yake katika maangamizi na ambae huiepusha na maangamizi".¹

إِنَّا أَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ سَلَاسِلًا وَأَغْلَالًا وَسَعِيرًا ﴿١﴾ إِنَّ الْأَبْرَارَ يَشْرَبُونَ مِنْ نَأْسٍ
كَانَ مِزَاجُهَا كَافُورًا ﴿٢﴾ عَيْنًا يَشْرَبُ بِهَا عِبَادُ اللَّهِ يُفَجِّرُونَهَا تَفْجِيرًا ﴿٣﴾ يُوفُونَ
بِالنَّذْرِ وَيَخَافُونَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهُ مُسْتَطِيرًا ﴿٤﴾ وَيُطْعَمُونَ أَلْطَعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِ مِسْكِينًا
وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٥﴾ إِنَّمَا نَطْعَمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكُورًا ﴿٦﴾ إِنَّا
نَخَافُ مِنْ رَبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا ﴿٧﴾ فَوَقْنَهُمْ اللَّهُ شَرَّ ذَٰلِكَ الْيَوْمِ وَلَقَّيْنَهُمْ نَصْرَةً
وَسُرُورًا ﴿٨﴾ وَجَزَيْنَهُمْ بِمَا صَبَرُوا جَنَّةً وَحَرِيرًا ﴿٩﴾

4. Hakika Sisi Tumewaandalia makafiri minyororo na pingu na Moto mkali.

5. Hakika watu wema watakunywa katika vinywaji vilivyo changanyika na kafuri,

6. Ni chemchem watakaoinywa waja wa Mwenyezi Mungu, wakiifanya imiminike kwa wingi.

7. Wanatimiza ahadi, na wanaiogopa siku ambayo shari yake inaenea sana,

8. Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, nayatima, na wafungwa.

9. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani.

10. Hakika sisi tunaiogopa kwa Mola Wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na taabu.

11. Basi Mwenyezi Mungu Atawalinda na shari ya siku hiyo, na Atawakutanisha na raha na furaha.

12. Na Awajazi Bustani za Peponi na maguo ya hariri kwa vile walivyo subiri.

¹ Muslim 1:203.

Malipo ya makafiri na watu wema

Allah تعالى Anaeleza, Kuhusu Aliyowaandalia makafiri katika viumbe wake, kama vile minyororo, pingu na moto, nao ni miale ya moto wa Jahannam. Kama Allah تعالى Alivyosema:

إِذِ الْأَعْلَىٰ فِي أَعْنَاقِهِمْ وَالسَّلْسِلُ يُسْحَبُونَ ﴿٧٦﴾ فِي الْحَمِيمِ ثُمَّ فِي النَّارِ يُسْجَرُونَ ﴿٧٧﴾

“Zitakapokuwa pingu shingoni mwao na minyororo, huku wanabururwa, katika maji ya moto, kisha wanaunguzwa Motoni.”
(40:71:72)

Alipotaja yale Aliyowaandalia hawa waovu kama vile moto wa Sa’iir. Amesema baada ya hapo:

إِنَّ الْأَبْرَارَ يَشْرَبُونَ مِنْ كَأْسٍ كَانَ مِزَاجُهَا كَافُورًا ﴿٧٦﴾

“Hakika watu wema watakunywa katika vinywaji vilivyo changanyika na kafuri.”

Hakika yamejulikana yaliyomo katika *Kafuur*, miongoni mwa ubaridi na harufu nzuri, pamoja na nyongeza ya ladha nyinginezo humo peponi. Amesema Al-Hassani, kupoa kwa Kafuri, ni katika uzuri wa tangawizi. Kwa ajili hii amesema:

عَيْنًا يَشْرَبُ بِهَا عِبَادُ اللَّهِ يُفَجِّرُونَهَا تَفْجِيرًا ﴿٧٦﴾

“Ni chemchemi watakaoinywa waja wa Mwenyezi Mungu, wakiifanya imiminike kwa wingi.”

Maana yake: Hiki ambacho kimechanganywa kwa ajili ya watu hawa wema miongoni mwa *kafuur*, ni chemchem watakayoinywa waliokurubishwa katika waja wa Mwenyezi Mungu, hali ya kuwa safi pasina kuchanganywa na chochote na watakata kiu. Na kwa sababu hiyo, neno kunywa limebeba maana ya unywaji unaokata kiu. Kauli Yake Allah تعالى:

يُفَجِّرُونَهَا تَفْجِيرًا ﴿٧٦﴾

“Wakiifanya imiminike kwa wingi.” Maana yake: Watatumia watakavyo katika chemchemi kwa kuipeleka mahali popote watakapo katika kasri zao na sehemu zao. Na neno *Tafjiir* ni kububujisha kama Allah تعالى Alivyosema;

وَقَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ بِكَ حَتَّىٰ تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَنْبُوعًا ۝١٧

“Na walisema: Hatutakuamini mpaka ututimbulie chemchemi katika ardhi hii.” (17:90),

Akasema:

وَفَجَّرْنَا خِلْفَهُمَا نَهْرًا ۝١٨

“Na ndani yake Tukapasua mito.” (18:33)

Mujahid amesema:

يُفَجِّرُونَهَا تَفْجِيرًا ۝١٩

“Wakiifanya imiminike kwa wingi.” (76:6)

Wataikokota kokote watakako.¹ na kama hivyo amesema Ikrimah na Qatadah.² At-Thaury amesema: “Wataipeleka chemchemi hiyo wanakotaka.”³

Matendo ya watu wema

Na Kauli Yake Allah تعالى:

يُوفُونَ بِالنَّذْرِ وَيَخَافُونَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهُ مُسْتَطِيرًا ۝٢٠

“Wanatimiza ahadi, na wanaiogopa siku ambayo shari yake inaenea sana.”

Maana yake: Wanamuabudu Allah تعالى katika yale ambayo Ameyawajibisha juu yao katika kufanya utii wa wajibu kwa msingi wa sheria, Na yale ambayo yamewajibishwa juu ya nafsi zao kwa njia ya kuweka nadhiri. Imam Maalik amepokea kutoka kwa Twalha Bin Abdi Al-Malik Al-Aylaa, kutoka kwa Al-Qasim Bin Malik kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kwamba Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ نَذَرَ أَنْ يُطِيعَ اللَّهَ فَلْيُطِيعْهُ، وَمَنْ نَذَرَ أَنْ يُعْصِيَ اللَّهَ فَلَا يُعْصِهِ»

“Atakayeweka nadhiri juu ya kumtii Mwenyezi Mungu na amtii na atakayeweka nadhiri juu ya kumuasi Mwenyezi Mungu, asimuasi.”⁴

¹ At-Tabari 24:94.

² Ad-Durr Al-Manthur 8:369.

³ At-Tabari 24:95.

⁴ Muwatta' 2:476.

Ameipokea Bukhari kutokana na hadithi ya Maaliki.¹

Na wanaacha mambo ambayo Ameyaharamisha. Ambayo Amewakataza kwa kuogopea hesabu mbaya siku ya kiama, Nayo ni siku ambayo shari yake itaenea. Kwa maana ni yenye kuwaenea watu wote isipokuwa wale ambao Allah تعالی Amewarehemu. Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema: ni yenye kuenea. Qatadah amesema: Shari ya siku hiyo itaenea mpaka ijaze mbingu na ardhi.² Kauli Yake Allah تعالی:

وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَى حُبِّهِ

“Na hulisha chakula, juu ya kukipenda kwake.”

Aidha imesemwa: kufanya hivyo kwa maana ya kumpenda Allah تعالی kwa sababu mtiririko wa maneno umefahamisha juu ya maana hayo. Hata hivyo kauli yenye nguvu ni kwamba wanalisha chakula hali ya kukipenda na kukitamani. Mtazamo huu ni wa Mujaahid na Muqaatil, na ameukubali Ibnu Jariir رحمه الله تعالی.³

Kama Kauli Yake Allah تعالی:

وَأَتَى الْمَالَ عَلَى حُبِّهِ

“...na Anawapa mali, kwa kupenda kwake.” (2:177)

Kama Kauli Yake Allah تعالی:

لَنْ نَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّىٰ تُنْفِقُوا مِمَّا حُبُّونَ^٤

“Kabisa Hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda.” (3:92).

Imekuja katika hadithi sahihi.

«أَفْضَلُ الصَّدَقَةِ أَنْ تَصَدَّقَ وَأَنْتَ صَاحِبٌ شَجِيحٌ، تَأْمُلُ الْغِنَىٰ وَتَخْشَى الْفَقْرَ»

“Bora ya sadaka ni kutoa hali ya kuwa wewe ni mzima mwenye uchu, unatarajia utajiri na unaogopa ufukara.”⁴

¹ Fat'hul Al-Bari 11:589.

² At-Tabari 24:96.

³ At-Tabari 24:96.

⁴ Fat'hul Al-Bari 3:334.

Maana yake: Katika hali ya kupenda mali hiyo, kuipupia na kuihitajia. Kwa ajili hiyo Amesema Allah تعالى:

﴿ وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴾

“Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa.” (76:8)

Ama maskini na yatima ufafanuzi wa sifa zao umekwisha tangulia. Ama kuhusu mateka: Saidi Bin Jubair, Hassan na Adh-Dhahak wamesema: Mateka katika watu wa *Kibla*¹– Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema: Mateka wao siku hiyo walikuwa ni washirikina.² Na mtazamo huu unapata nguvu kwa Mtume ﷺ alipowaamrisha masahaba wake siku ya Badri kuheshimu mateka. Kwa hiyo walikuwa wanawatanguliza kuliko nafsi zao wakati wa chakula. Ikrimah amesema: Hao ni watumwa,³ na kauli hii ameichagua Ibnu Jariir رحمه الله تعالى. Kwa sababu aya imejumlisha Muislamu na Mshirikina.⁴ Kama hivyo amesema Said Bin Jubair, Atwaa, Al-Hassan na Qatadah. Mtume ﷺ aliusia kuwatendea wema watumwa katika hadithi nyingi, mpaka wasia wake wa mwisho akawa anasema:

«الصَّلَاةُ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ»

“Shikamaneni na Sala na mliowamiliki katika watumwa”⁵

Mujaahid amesema: “Huyo ni mfungwa.”⁶ Maana: wanawalisha chakula hali watu hawa wenyewe wanakitamani na wanakipenda, huku vitendo vyao vikisema.

﴿ إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ ﴾

“Hakika sisi tunakulisheni kwa wajahi wa Mwenyezi Mungu.” (76:9)

Maana yake: Kwa kutaka malipo kutoka kwa Allah تعالى na Radhi Yake.

﴿ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكْرًا ﴾

“Hatutaki kwenu malipo wala shukrani.”

¹ At-Tabari 24:97.

² Abdu-Razzaq 3:337.

³ Al-Qurtubi 19:129.

⁴ At-Tabari 24:98.

⁵ An-Nasai in *Al-Kubra* 4:258.

⁶ At-Tabari 24:98.

Maana yake: ‘Hatutaki kutoka kwenu malipo ambayo mtatulipa na kutushukuru mbele za watu’.

Mujaahid na Saiid Bin Jubair wamesema: Kwa hakika naapa kwa Allah تعالى hawakuyasema hayo kwa ndimi zao, isipokuwa Allah تعالى Aliyajua hayo kutokana na nyoyo zao, hivyo Akawasifu kutokana na jambo hilo, ili avutike katika kufanya hivyo mwenye kuvutika.¹

إِنَّا نَخَافُ مِنْ رَبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا ﴿١٠﴾

“Hakika sisi tunaigopa kwa Mola Wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na taabu.” (76:10)

Maana yake: Hakika si vingine tunafanya haya huenda Allah تعالى Akaturehemu na Akatupokea kwa upole wake katika siku ngumu yenye tabu. Ali Bin Aby Twalha amesema kutoka kwa Ibni Abbas رضي الله عنهما ‘Abuusaa: ni Dhiki. Qamtwariira: Ndefu.²

Ikrimah na wengine wamesema kutoka kwake, katika Kauli Yake Allah تعالى:

يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا ﴿١٠﴾

“Siku yenye shida na taabu.”

Amesema: Kafiri atakunja uso siku hiyo mpaka jasho litachirizika kati ya macho yake mfano wa lami.³

Na Mujaahid amesema: ‘Abuusaa: Ni mwenye kukunja midomo miwili. Qamtwariira: Amesema: ni kukunja uso kutokana na ugumu. Na Said bin Jubair na Qatadah wamesema: Nyuso zitakunjika siku hiyo kutokana na vitisho. Qamtwariira: Kukunjika bapa la uso na baina ya macho kutokana na vituko. Ibnu Zaid amesema. Al-Abuus, ni shari. Na Al-Qamtwarir, ni nzito.

¹ At-Tabari 24:98.

² At-Tabari 24:100.

³ At-Tabari 24:99.

Baadhi ya Ufafanuzi wa Malipo ya Watu Wema Peponi na Yaliyomo Ndani yake Miongoni mwa Neema

Amesema Allah تعالى:

فَوَقَّهْمُ اللَّهُ شَرَّ ذَلِكَ الْيَوْمِ وَلَقَّهْمَ نَصْرَةً وَسُرُورًا ﴿١١﴾

“Basi Mwenyezi Mungu Atawalinda na shari ya siku hiyo, na Atawakutanisha na raha na furaha.”

Huu ni katika mlango wa uwiano wenye maana kubwa.

فَوَقَّهْمُ اللَّهُ شَرَّ ذَلِكَ الْيَوْمِ

“Atawalinda na shari ya siku hiyo.” (76:11)

Maana yake: Amewapa amani kwa yale wanayoyaogopa.

وَلَقَّهْمَ نَصْرَةً وَسُرُورًا ﴿١٢﴾

“Na Atawakutanisha na raha na furaha.”

Maana yake: Katika nyuso zao.

وَسُرُورًا ﴿١٣﴾

“Na furaha.” (76:11).

Maana yake: Katika nyoyo zao. Al-Hasan Al-Basry, Qatadah, Abu Al-'Aliyah na Ar-Rabi'i Bin Anas wamesema hivyo.¹ Na hii ni kama Kauli Yake Allah تعالى.

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرَةٌ ﴿٣٨﴾ ضَاحِكَةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ ﴿٣٩﴾

“Siku hiyo ziko nyuso zitazonawiri, zitacheka, zitachangamka.” (80:38-39).

Na hilo ni kwamba moyo ukifurahi uso huonesha nuru. Ka'ab Bin Maalik رضي الله عنه katika hadithi yake ndefu amesema: Mtume ﷺ pindi anapofurahishwa na jambo uso wake hunawiri mpaka unakuwa kana kwamba ni kipande cha mwezi.²

¹ At-Tabari 24:101.

² Fat'hul Al-Bari 6:653.

Aisha رضي الله عنها amesema: Mtume ﷺ aliingia kwangu hali ya kuwa amefurahi huku mikunjuo ya uso wake ikimeremeta. Isome hadithi hiyo.¹

Kauli Yake Allah تعالى:

وَجَزَّئُهُمْ بِمَا صَبَرُوا

“Na Amewalipa kwa sababu ya kusubiri.”

Maana yake: Kwa sababu ya kusubiri kwao, Amewatunuku wao kwa kuwaingiza peponi, na Amewavalisha hariri. Kwa maana: Amewaingiza mahali pazuri penye mashukio mapana na maisha ya nafasi na mavazi mazuri. Na amepokea Al-Haafidhi Bin Asaakir رحمه الله تعالى katika kumuelezea Hisham Bin Sulaiman Al-Darani. Amesema: Aby Sulaimaan Ad-Darani alisomewa *Surat Ad-Dahr*, Msomaji alipofika katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَجَزَّئُهُمْ بِمَا صَبَرُوا جَنَّةً وَحَرِيرًا

“Na Atawajazi Bustani za Peponi na maguo ya hariri kwa vile walivyosubiri.”

Alisema: Kwa sababu ya kusubiri juu ya kuacha matamaniao duniani.

* * *

¹ *Fat'h Al-Bari* 6:653.

مُتَّكِبِينَ فِيهَا عَلَى الْأَرَائِكِ ۗ لَا يَرَوْنَ فِيهَا شَمْسًا وَلَا
 زَمَهْرِيرًا ﴿١٣﴾ وَذَانِبَةً عَلَيْهِمْ ظِلَالُهَا وَذُلَّتْ أَقْطُوبُهَا تَذَلِيلًا
 ﴿١٤﴾ وَيُطَافُ عَلَيْهِمْ بِبَاقِيَةٍ مِّنْ فِضَّةٍ وَأَكْوَابٍ كَانَتْ قَوَارِيرًا
 ﴿١٥﴾ قَوَارِيرًا مِّنْ فِضَّةٍ قَدَّرُوهَا تَقْدِيرًا ﴿١٦﴾ وَنُسَقُونَ فِيهَا
 كَأْسًا كَانَ مِزَاجُهَا زَجْجِيلًا ﴿١٧﴾ عَيْنًا فِيهَا تُسَمَّى
 سَلْسَبِيلًا ﴿١٨﴾ * وَيَطُوفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُّخَلَّدُونَ إِذَا رَأَيْتَهُمْ
 حَسِبْتَهُمْ لُؤْلُؤًا مَّنثُورًا ﴿١٩﴾ وَإِذَا رَأَيْتَ ثَمَّ رَأَيْتَ نَعِيمًا
 وَمُلْكًا كَبِيرًا ﴿٢٠﴾ عَلَيْهِمْ ثِيَابٌ سُنْدُسٍ خُضْرٍ وَإِسْتَبْرَقٍ ۗ
 وَخُلُوعًا أُسَاوِرَ مِّنْ فِضَّةٍ وَسَقَنَهُمْ رُبَّمَا شَرَابًا طَهُورًا ﴿٢١﴾
 إِنَّ هَذَا كَانَ لَكُرْمًا جَزَاءً وَكَانَ سَعْيُكُمْ مَّشْكُورًا ﴿٢٢﴾ إِنَّا
 نَحْنُ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ تَنْزِيلًا ﴿٢٣﴾ فَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ
 وَلَا تَطِعْ مِمَّنْ ءِثْمًا أَوْ كُفُورًا ﴿٢٤﴾ وَأَذْكُرِ اسْمَ رَبِّكَ بُكْرَةً
 وَأَصِيلًا ﴿٢٥﴾ وَمِنَ اللَّيْلِ فَاسْجُدْ لَهُ وَسَبِّحْهُ لَيْلًا
 طَوِيلًا ﴿٢٦﴾ إِنَّ هَؤُلَاءِ لَشُجْبُونَ الْعَاجِلَةَ وَيَذَرُونَ
 وَرَاءَهُمْ يَوْمًا ثَقِيلًا ﴿٢٧﴾ نَحْنُ خَلَقْنَاهُمْ وَشَدَدْنَا أَسْرَهُمْ ۗ
 وَإِذَا شِئْنَا بَدَّلْنَا أَمْثَلَهُمْ تَبْدِيلًا ﴿٢٨﴾ إِنَّ هُنْدِيهَ تَذَكُّرَةٌ
 فَمَنْ شَاءَ انْتَحِذْ إِلَىٰ رَبِّهِ سَبِيلًا ﴿٢٩﴾ وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ
 يَشَاءَ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٣٠﴾ يُدْخِلُ مَنْ

يَشَاءُ فِي رَحْمَتِهِ ۗ وَالظَّالِمِينَ أَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٣١﴾

مُتَّكِبِينَ فِيهَا عَلَى الْأَرَائِكِ ۗ لَا يَرَوْنَ
 فِيهَا شَمْسًا وَلَا زَمَهْرِيرًا ﴿١٣﴾
 وَذَانِبَةً عَلَيْهِمْ ظِلَالُهَا وَذُلَّتْ أَقْطُوبُهَا
 تَذَلِيلًا ﴿١٤﴾ وَيُطَافُ عَلَيْهِمْ بِبَاقِيَةٍ
 مِّنْ فِضَّةٍ وَأَكْوَابٍ كَانَتْ قَوَارِيرًا
 ﴿١٥﴾ قَوَارِيرًا مِّنْ فِضَّةٍ قَدَّرُوهَا تَقْدِيرًا
 ﴿١٦﴾ وَنُسَقُونَ فِيهَا كَأْسًا كَانَ
 مِزَاجُهَا زَجْجِيلًا ﴿١٧﴾ عَيْنًا فِيهَا
 تُسَمَّى سَلْسَبِيلًا ﴿١٨﴾ * وَيَطُوفُ
 عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُّخَلَّدُونَ إِذَا رَأَيْتَهُمْ
 حَسِبْتَهُمْ لُؤْلُؤًا مَّنثُورًا ﴿١٩﴾ وَإِذَا
 رَأَيْتَ ثَمَّ رَأَيْتَ نَعِيمًا وَمُلْكًا كَبِيرًا
 ﴿٢٠﴾ عَلَيْهِمْ ثِيَابٌ سُنْدُسٍ خُضْرٍ
 وَإِسْتَبْرَقٍ ۗ وَخُلُوعًا أُسَاوِرَ مِّنْ فِضَّةٍ
 وَسَقَنَهُمْ رُبَّمَا شَرَابًا طَهُورًا ﴿٢١﴾
 إِنَّ هَذَا كَانَ لَكُرْمًا جَزَاءً وَكَانَ
 سَعْيُكُمْ مَّشْكُورًا ﴿٢٢﴾

13. Humo wataegemea juu
 ya viti vya enzi, hawa-
 taona humo jua kali wala
 baridi kali.

14. *Na vivuli vyake vitakuwa karibu yao, na mashada ya matunda yataning'inia mpaka chini.*
15. *Na watapitishiwa vyombo vya fedha na vikombe vya vigae,*
16. *Vya fedha safi kama kiyoo, wamevipima kwa vipimo.*
17. *Na humo watanyweshwa kinywaji kilichochanganyika na tangawizi.*
18. *Hiyo ni chemchem iliyo humo inaitwa Salsabil.*
19. *Na watawazungukia (kuwatumikia) wavulana wasiochakaa. Ukiwaona utawafikiri ni lulu zilizotawanywa.*
20. *Na utakapoyaona, utakuwa umeona neema na ufalme mkubwa.*
21. *Juu yao zipo nguo za hariri laini za kijani kibichi, na hariri nzito ya at'ilasi. Na watavikwa vikuku vya fedha, na Mola wao Mlezi Atawanyweshwa kinywaji safi kabisa.*
22. *Hakika haya ni malipo yenu; na juhudi zenu zimekubaliwa*

Kutaja Viti vya Enzi, Bila ya Shaka Peponi Hakuna Joto Wala Baridi

Allah تعالی Anaeleza kuhusu maisha ya watu wa Peponi na yale ambayo watayapata ndani yake miongoni mwa neema za kudumu na fadhila tukufu. Kwa hiyo Allah تعالی Amesema:

مُتَّكِّينَ فِيهَا عَلَى الْأَرْبَابِ ط

"Humo wataegemea juu ya viti vya enzi."

Maelezo yake jameshabainishwa katika *Surat As'swaafaat*, na kutaja tofauti katika kuegemea huko, jee ni kujilaza, au kuegemea kwa kuegemeza fundo za mikono au kuambatanisha makalio katika ardhi na kuikunja miguu au kujimakinisha katika kukaa, na kuwa *Al'araaik* ni vitanda chini ya mabesela. Kauli Yake Allah تعالی:

لَا يَرَوْنَ فِيهَا شَمْسًا وَلَا زَمَهْرِيرًا ﴿١٣﴾

"Hawataona humo jua kali wala baridi kali." (76:13)

Maana yake: Kwao hakuna joto lenye kuchukiza wala baridi yenye kuumiza, bali Peponi kuna hali moja ya kudumu na ya milele, na hawatataka kubadilishiwa Peponi.

Kukaribia Vivuli na Matunda

Allah تعالیٰ Anasema:

وَدَانِيَةً عَلَيْهِمْ ظِلُّهَا

“Na vivuli vyake vitakuwa karibu yao.”

Maana yake: Matawi yake yatakuwa karibu nao.

وَذُلِّلَتْ قُطُوفُهَا تَذْلِيلًا ﴿٢١﴾

“Na mashada ya matunda yataning’inia mpaka chini.”

Maana yake: Wakati wowote atakapotaka kuyachuma matunda yatasogea kwake na yataning’inia kutoka juu ya matawi yake kana kwamba matunda na matawi hayo yanasikia na yanatii.

Kama Allah تعالیٰ Alivyosema katika aya nyingine:

وَجَنَى الْجَنَّتَيْنِ دَانٍ ﴿٥٤﴾

“Na matunda ya Bustani hizo yapo karibu.” (55:54)

Amesema Allah تعالیٰ:

قُطُوفُهَا دَانِيَةٌ ﴿٢٣﴾

“...Na mashada ya matunda yataning’inia mpaka chini.” (69:23).

Mujaahid amesema:

وَذُلِّلَتْ قُطُوفُهَا تَذْلِيلًا ﴿٢١﴾

“Na mashada ya matunda yataning’inia mpaka chini.”

Akisimama huinuka pamoja naye matunda hayo kwa kiasi chake na akikaa hujisogea kwake yeye mpaka ayapate, na hivyo hivyo akijilaza.

Kama isemavyo Kauli Yake Allah تعالیٰ:

تَذَلُّيلًا

“Kusogezwa sana.”¹

Qatadah رضي الله عنه amesema: mikono yao hairudishwi dhidi ya matunda hayo, kwa mwiba au umbali.²

Vyombo vya Fedha na Bilauri

Kauli Yake Allah تعالى:

وَيُطَافُ عَلَيْهِمْ بِبَائِنَةٍ مِّنْ فَضَّةٍ وَأَكْوَابٍ

“Na watapitishiwa vyombo vya fedha na vikombe vya vigae.”

Maana yake: Watazungukiwa na watumishi – wakiwa na vyombo vya chakula, na vyombo hivyo ni vya fedha. Na bilauri za kunywa ni bilauri ambazo hazina mikono wala vishikio. Na Kauli Yake Allah تعالى:

قَوَارِيرًا ﴿١٥﴾ قَوَارِيرًا مِّنْ فَضَّةٍ

“Vigae, vigae vya fedha.” (76:15-16)

Ibnu Abbaas, Mujahid, Al-Hassan Al-Basry na wengine رضي الله عنهم wamesema: Weupe wa fedha ni katika usafi wa kioo,³ na chupa hizo haziwi isipokuwa kutokana na vioo. Kwa hiyo bilauri hizi ni za fedha na zaidi ya hivyo kioo chake ni chembamba kilichomo ndani yake huonekana kwa nje yake, na haya ni katika yale yasiyokuwa na mfanano katika dunia. Kauli Yake Allah تعالى:

قَدَّرُوهَا تَقْدِيرًا ﴿١٦﴾

“Wamevipima kwa vipimo.”

Maana yake: Kulingana na kiu chao, haipungui wala haizidi juu ya hapo, bali hizo bilauri zimeandaliwa kwa ajili hiyo zimekadiriwa kufuatana na kiu cha wahusika, na hii ndiyo maana ya kauli ya Ibni Abbaas, Mujaahid, Said Bin Jubair, Aby Swaleh, Qatadah, Ibni Abzaa, Abdillahi Bin Ubaidi Ibn Umayr, Qatadah, As-Sha’aby’ na Ibni Zayd رضي الله عنهم. Ibnu Jariri رحمه الله تعالى amekubali

¹ At-Tabari 24:103.

² At-Tabari 24:103.

³ At-Tabari 24:105, 106.

maana hiyo na wengine.¹ Na hii ni maana kubwa katika kuwaenzi na kuwapa utukufu.

Kinywaji cha Tangawizi na *Salsabiil*

Kauli Yake Allah تعالیٰ:

وَيُسْقَوْنَ فِيهَا كَأْسًا كَانَ مِزَاجُهَا زَجْجِيلًا ﴿١٧﴾

“Na humo watanyweshwa kinywaji kilichochanganyika na tangawizi.” (76:17)

Maana yake: Anakusudia watu wema vile vile watanyeshwa katika bilauri hizi.

كَأْسًا

“Kinywaji.” (76:17) Maana yake: Pombe.

كَانَ مِزَاجُهَا زَجْجِيلًا ﴿١٧﴾

“Mchanganyiko wake ulikuwa ni tangawizi.” (76:17) Mara watachanganyiwa wao katika kinywaji hicho na *kafuur* hali ya kuwa ni baridi. Na mara nyingine kwa tangawizi, hali ya kuwa ipo moto, na watu hawa mara watachanganyiwa katika aina hii na katika wakati mwingine aina nyingine. Ama wale wenye kukurubishwa hao watakunywa katika kila moja katika hizo ikiwa safi kama alivyoyasema hayo Qatadah na wengine.² Na Kauli Yake Allah تعالیٰ imetangulia

عَيْنًا يَشْرَبُ بِهَا عِبَادُ اللَّهِ

“Ni chemchemi watakaoinywa waja wa Mwenyezi Mungu.” (76:6)

Akasema hapa,

عَيْنًا فِيهَا تُسْمَىٰ سَلْسَبِيلًا ﴿١٨﴾

“Hiyo ni chemchemi iliyo humo inaitwa Salsabiil.” (76:18)

Maana yake: *Zanjabiil*, ni Chemchemi iliyo Peponi na inaitwa *Salsabiil*. Ikrima amesema: ni jina la chemchemi ndani ya Pepo. Mujahidi amesema imeitwa kwa hivyo kwa sababu ya wepesi wa mapito yake na kasi ya kupita kwake.³

¹ At-Tabari 24:106, 107, na Al-Qurtubi 19:141.

² At-Tabari 24:107.

³ At-Tabari 24:108.

Vijana na Watumishi

Kauli Yake Allah تعالى.

﴿ وَيَطُوفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُّخَلَّدُونَ إِذَا رَأَيْتَهُمْ حَسِبْتَهُمْ لُؤْلُؤًا مَّنشُورًا ﴾

“Na watawazungukia kuwatumikia wavulana wasiopevuka, ukiwaona utawafikiri ni lulu zilizo tawanywa.”

Maana yake: Wavulana wa Peponi watawazungukia watu wa peponi kwa ajili ya kuwahudumia.

مُخَلَّدُونَ

“Wasio pevuka.” (76:20)

Maana yake: Watakuwa katika hali moja ya wasiopevuka milele hawatabadilika katika hali nyingine. Hautazidi umri wao juu ya miaka hiyo. Walioeleza sifa zao kuwa wamevaa hereni masikioni mwao wameeleza hivyo kwa sababu mtoto hufaa zaidi kwa sifa hiyo na si mtu mzima. Kauli ya Allah تعالى.

﴿ إِذَا رَأَيْتَهُمْ حَسِبْتَهُمْ لُؤْلُؤًا مَّنشُورًا ﴾

“Ukiwaona utawafikiri ni lulu zilizo tawanywa.” (76:19)

Maana yake: Utakapowaona katika kutawanyika kwao kwa ajili ya kuhudumia mahitaji ya mabwana, wingi wao, weupe wa nyuso zao, uzuri wa rangi zao, nguo zao na vipambo vyao utawadhania kuwa ni lulu zilizotawanywa. Hakuna katika kufananisha kuzuri kuliko huku wala katika mandhari nzuri kuliko lulu iliyotawanywa. Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذَا رَأَيْتَ

“Na utakapo yaona.” (76:20)

Maana yake: Ni pindi utakapoona Ee Muhammad,

ثُمَّ

“Huko.” (76:20)

Maana yake: Huko, anakusudia Peponi, neema zake, upana wake, utukufu wake na yaliyomo ndani yake miongoni mwa uzuri na furaha.

رَأَيْتَ نَعِيمًا وَمُلْكًا كَبِيرًا ﴿٧٦﴾

“Utakuwa umeona neema na ufalme mkubwa.”

Maana yake: Mamlaka ya Allah تعالى huko ni makubwa mno, na ni ufalme uliyo mkubwa zaidi. Imethibitika katika hadithi sahihi kwamba Allah تعالى Atamuambia mtu wa mwisho kutoka motoni na mtu wa mwisho kuingia Peponi,

«إِنَّ لَكَ مِثْلَ الدُّنْيَا وَعَشْرَةَ أَمْثَالِهَا»

“Hakika wewe mgao wako ni zaidi ya dunia mara kumi yake.”¹

Itakapokuwa huu ndio mgao wake Allah تعالى kwa mtu wa chini kabisa katika watu wa Peponi, unafikiri hali inakuwaje kwa mtu mwenye daraja na hadhi ya juu mbele ya Allah?

Mavazi na Mapambo

Na Kauli Yake Allah تعالى:

عَلَيْهِمْ ثِيَابٌ سُنْدُسٍ خُضْرٌ وَإِسْتَبْرَقٌ

“Juu yao zipo nguo za hariri laini za kijani kibichi, na hariri nzito ya at’ilasi.”

Maana yake: Vazi la watu wa Peponi. Humo kuna hariri na katika hiyo hariri ni hariri nyembamba na hiyo ni hariri ya hali ya juu, kama vile kanzu na mfano wake katika nguo inayoandamia viwili wili vyao. Na *Al-Istabraq*, ni ile ambayo ina mng’ao na weupe ambayo huonekanwa kwa umbo la nje, kama inavyofahamika kwa walio wengi.

وَحُلُوا أَسَاوِرَ مِنْ فِضَّةٍ

“Na watavikwa vikuku vya fedha.”

Na hii ni sifa ya watu wema. Ama wale wenye kukurubishwa hao ni kama Alivyosema Allah تعالى:

¹ Muslim 1:173.

مُخَلَّوْنَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا مِطَّ وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ ﴿٢٣﴾

“Watapambwa humo kwa mapambo ya mikononi ya dhahabu na lulu. Na mavazi yao humo ni hariri.” (22:23)

Allah تعالی Alipotaja mapambo ya muonekano wa nje wa hariri na vito. Amesema baada ya hapo,

وَسَقَلْنَهُمْ رِئْمًا شَرَابًا طَهُورًا ﴿٢٤﴾

“na Mola Wao Mlezi Atawanyweshwa kinywaji safi kabisa.”

Maana yake: Nafsi zao Anazisafisha kutokana na husda, mfundo, maudhi na tabia zote mbaya kama tulivyosimuliwa na Amiri Al-Muuminina Ali Bin Aby Twaalib رضي الله عنه kwamba yeye amesema: “Watu wa Peponi watakapofika kwenye mlango wa Pepo watakuta huko chemchemi mbili, kana kwamba wamefahamishwa jambo hilo, watakunywa katika chemchemi moja. Allah تعالی Ataondosha uchafu uliomo ndani mwao, kisha wataoga katika chemchemi nyingine, watapitiwa juu yao na mng’ao wa neema. Kwa hiyo Allah تعالی Ameielezea hali yao ya taswira ya nje na uzuri wao wa ndani.”¹ Na Kauli Yake تعالی:

إِنَّ هَذَا كَانَ لَكُمْ جَزَاءً وَكَانَ سَعْيُكُمْ مَشْكُورًا ﴿٢٥﴾

“Hakika haya ni malipo yenu; na juhudi zenu zimekubaliwa.” (76:21)

Maana yake: Wataambiwa hivyo kwa kukirimiwa na kufanyiwa hisani. Kama Alivyosema تعالی:

كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا أَسْلَفْتُمْ فِي الْأَيَّامِ الْخَالِيَةِ ﴿٢٦﴾

“Waambiwe: Kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya mlivyo tanguliza katika siku zilizo pita.” (69:24)

Kama Kauli Yake تعالی:

وَنُودُوا أَنْ تِلْكَمُ الْجَنَّةُ أَوْرَثْتُمُوهَا بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾

“Na watanadiwa (wataambiwa) ya kwamba, “Hii ndio pepo mliyorthishwa kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyafanya.” (7:43)

¹ Al-Qurtubi 19:47.

Kisha Allah تعالى Akasema:

وَكَانَ سَعْيُكُمْ مَشْكُورًا ﴿٧٦﴾

“Na juhudi zenu zimekubaliwa.” (76:22).

Maana yake: Allah تعالى Amekulipeni kingi kwa kichache,

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ تَنْزِيلًا ﴿٧٦﴾ فَأَصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ وَلَا تُطِعْ مِنْهُمْ ءَاثِمًا أَوْ كَفُورًا ﴿٧٧﴾ وَأَذْكُرِ اسْمَ رَبِّكَ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٧٨﴾ وَمِنَ اللَّيْلِ فَاسْجُدْ لَهُ وَسَبِّحْهُ لَيْلًا طَوِيلًا ﴿٧٩﴾ إِنَّ هَتُولَاءِ يُحِبُّونَ الْعَاجِلَةَ وَيَذَرُونَ وَرَاءَهُمْ يَوْمًا ثَقِيلًا ﴿٨٠﴾ نَحْنُ خَلَقْنَاهُمْ وَشَدَدْنَا أَسْرَهُمْ ﴿٨١﴾ وَإِذَا شِئْنَا بَدَلْنَا أَمْثَلَهُمْ تَبْدِيلًا ﴿٨٢﴾ إِنَّ هَذِهِ تَذَكُّرَةٌ ﴿٨٣﴾ فَمَنْ شَاءَ اتَّخَذْ إِلَىٰ رَبِّهِ سَبِيلًا ﴿٨٤﴾ وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٨٥﴾ يُدْخِلُ مَنْ يَشَاءُ فِي رَحْمَتِهِ وَالظَّالِمِينَ أَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٨٦﴾

23. Hakika Sisi Tumeku teremshia Qur'ani kidogo kidogo.

24. Basi ngojea hukumu ya Mola Wako Mlezi wala usimt'ii miongoni mwao mwenye dhambi au mwenye kufuru.

25. Na likumbuke jina la Mola Wako Mlezi asubuhi na jioni;

26. Na usiku msujudie Yeye, na umtakase usiku, wakati mrefu.

27. Kwa hakika watu hawa wanapenda maisha ya kidunia, na wanaicha nyuma yao siku nzito.

28. Sisi Tumewaumba, na Tukavitia nguvu viungo vyao. Na Tukitaka Tutawabadilisha mfano wao wawe badala yao.

29. Hakika haya ni mawaidha; basi anayetaka atashika Njia ya kwenda kwa Mola Wake Mlezi.

30. Wala hamuezi kutaka ila Atakapo Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Ilimu, Mwenye Hikima.

31. Humuingiza amtakaye katika rehema Yake. Na wenye kudhulumu Amewawekea adhabu iliyo chungu.

Utajo wa Kushushwa Qur'ani, na Amri ya Kusubiri na Kuleta Dhikri

Allah تعالى Anasema kwa Kumkumbusha Mtume Wake ﷺ juu ya neema Aliyompa ya kumteremshia Qur'ani Tukufu.

فَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ

“Basi subiri hukumu ya Mola Wako Mlezi.”

Maana yake: Kama Nilivyokukirimu kwa Nilichokuteremshia, basi subiri juu ya Hukumu na Qadari Yake, na ujue kuwa Atakuwekea wewe mikakati mizuri,

وَلَا تُطِعْ مِنْهُمْ ءَاثِمًا أَوْ كَفُورًا ﴿٢٤﴾

“Wala usimtii miongoni mwao mwenye dhambi au mwenye kufuru.” (76:24)

Maana yake: Usiwatii makafiri na wanafiki kama wakitaka kukuzuia kufikisha kile ulichoteremshiwa juu yako na Allah تعالى, bali fikisha ulichoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako na umtegemee Allah تعالى, kwa kuwa Allah تعالى Atakuhifadhi na watu. Na mwenye dhambi ni mtu muovu katika vitendo vyake na kupinga ni kukataa kwa moyo,

وَأَذْكُرِ اسْمَ رَبِّكَ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٢٥﴾

“Na litaje Jina la Mola wako Mlezi asubuhi na jioni.”

Maana yake: Mwanzo wa mchana na mwisho wake.

وَمِنَ اللَّيْلِ فَاسْجُدْ لَهُ وَسَبِّحْهُ لَيْلًا طَوِيلًا ﴿٢٦﴾

“Na usiku msjudie Yeye, na Umtakase usiku, wakati mrefu.”

Kama Kauli Yake تعالى:

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٢٧﴾

“Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya sunna khasa kwako wewe. Huenda Mola Wako Mlezi Akakunyanyua cheo kinachosifika.” (17:79)

Hii ni kama Kauli Yake تعالى،

يَتَأْتِيَا الْمُرْمِلُ ﴿١﴾ قُمْ أَلَيْلَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢﴾ بَصَفَهُ أَوْ أَنْقَصَ مِنْهُ قَلِيلًا ﴿٣﴾ أَوْ زِدَ عَلَيْهِ وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلًا ﴿٤﴾

“Ewe uliyejifunika!, Kesha usiku kucha, ila kidogo tu!, Nusu yake, au ipunguze kidogo. Au izidishe - na soma Qur’ani kwa utaratibu na utungo.” (73:1-4)

Kukosolewa Katika Kupenda Dunia na Kutoa Angalizo Juu ya Siku ya Marejeo

Kisha Allah تعالى Anasema kwa Kuwakanusha makafiri na mfano wao, katika kupenda kwao dunia na kuacha kwao nyumba ya akhera nyuma ya migongo yao.

إِنَّ هَتُوْلًا تَحِبُّونَ الْعَاجِلَةَ وَيَذْرُونَ وِرَاءَهُمْ يَوْمًا ثَقِيلًا ﴿١٧﴾

“Kwa hakika watu hawa wanapenda maisha ya kidunia, na wanaicha nyuma yao siku nzito.”

Maana yake: Siku ya kiama. Kisha Allah تعالى Akasema:

فَخُنْ خَلْقَنَّهُمْ وَشَدَدْنَا أَسْرَهُمْ ﴿٢٨﴾

“Sisi Tumewaumba, na Tukavitia nguvu viungo vyao.” (76:28)

Ibn Abbaas, Mujaahid na wengine wamesema: Maana yake: “Umbo lao”¹

وَإِذَا شِئْنَا بَدَلْنَا أَمْثَلَهُمْ تَبْدِيلًا ﴿٢٩﴾

“Na Tukitaka Tutawabadilisha mfano wao wawe badala yao.” (76:28)

Maana yake: Tukitaka Tutawafufua siku ya kiama na Tutawabadilisha na Kuwafanyia umbo jingine, na kubadilisha huku ni kwa kuanza kuumbwa upya. Ibn Zayd na Ibn Jariir رحمه الله تعالى wamesema:

¹ At-Tabari 24:118.

وَإِذَا شِئْنَا بَدَّلْنَا أَمْثَلَهُمْ تَبْدِيلًا ﴿٧٦﴾

“Na Tukitaka Tutawabadilisha mfano wao wawe badala yao.”

Maana yake: Tungetaka Tungeleta viumbe wengine wasiokuwa wao.¹ Kama Kauli Yake:

إِنْ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ أَيُّهَا النَّاسُ وَيَأْتِ بِآخَرِينَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ قَدِيرًا ﴿١٣٣﴾

“Akitaka Atakuondoeni, enyi watu! Na Awalete wengineo. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa hayo.” (4:133).

Kama Kauli Yake تعالیٰ،

إِنْ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٩﴾ وَمَا ذَٰلِكُمْ عَلَىٰ اللَّهِ بِعَزِيزٍ ﴿٢٠﴾

“Akitaka Atakuondoeni na Alete viumbe wapya!, na hilo kwa Mwenyezi Mungu si jambo gumu.” (14:19-20)

Qur’ani ni Ukumbusho na Uongofu kwa Taufiki ya Allah تعالیٰ

Kisha Allah تعالیٰ Anasema:

إِنَّ هَٰذِهِ تَذَكُّرٌ ﴿١٠٠﴾

“Hakika haya ni mawaidha.”

Maana yake: Ukumbusho.

فَمَنْ شَاءَ اتَّخِذْ إِلَىٰ رَبِّهِ سَبِيلًا ﴿١٠١﴾

“Basi anayetaka atashika Njia ya kwenda kwa Mola Wake Mlezi.”

Maana yake: Njia na mfumo. Maana yake: Anayetaka ataongoka kwa Qur’ani. Kama ilivyo katika Kauli Yake:

وَمَا ذَا عَلَيْهِمْ لَوْ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

“Na ingeliwadhuru nini wao lau wangelimuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.” (4:39)

¹ At-Tabari 24:118, 119

Kisha Allah تعالى Anasema:

وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ

“Wala hamuezi kutaka ila Atakapo Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Hawezi yeyote kuiongoa nafsi yake, wala kuingia katika imani au kuiletea nafsi yake manufaa,

إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٢٦﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Ilimu, Mwenye Hikima.”

Maana yake: Anamjua mtu anayetaka, hivyo Anamrahisishia yeye hivyo au Anamuunganisha na sababu zake. Na Anamjua mtu anayestahiki upotevu hivyo Humpondoa na uongofu, na Yeye Ana Hikima ya juu, na hoja yenye kushinda. Na kwa ajili hii Amesema Allah تعالى:

إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٢٧﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Elimu, Mwenye Hikima.”

Kisha Akasema,

يُدْخِلُ مَنْ يَشَاءُ فِي رَحْمَتِهِ وَالظَّالِمِينَ أَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٢٨﴾

“Humuingiza Amtakaye katika rehema Yake. Na wenye kudhulumu Amewawekea adhabu iliyo chungu.”

Maana yake: Anamuongoa Amtakaye na Humpoteza Amtakae, na Anayemuongoa hapana wa kumpotoa na mwenye Kumpotoa hakuna wa kumuongoa.

Mwisho wa Suratu Al-Insan. Kuhimidiwa ni kwa Allah تعالى na Kuneemesha.

* * *

Tafsiri ya Suratul Mursalat Sura ya 77

Iliteremshwa Makkah

Kushuka kwa Sura hii na Kusomwa Kwake katika Sala ya Magharibi

Bukhari amepokea kutoka kwa Abdullaahi, na huyo ni Ibn Mas'ud رضي الله عنه amesema: Tukiwa pamoja na Mtume ﷺ katika pango huko Mina ikashuka:

وَأَلْمُرْسَلَاتِ

“*Wal mursalaat.*” Alikuwa anaisoma na mimi ninaipokea toka kinywani mwake. Mtume akiwa katika hali hiyo ghafla nyoka alitokea juu yetu. Mtume ﷺ akasema:

«اِقْتُلُوهَا»

“*Muueni.*” Tukamkimbilia, akaenda zake. Mtume ﷺ akasema:

«وَيَبِثْ شَرُّكُمْ، كَمَا وَيَبِثُمْ شَرُّهَا»

“*Mmekingwa na shari yake kama yeye alivyokingwa na shari yenu.*”¹

Muslim vile vile ameitaja Hadithi hii kupitia njia ya A'amash². Imam Ahmad amepokea kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما toka kwa mama yake alimsikia Mtume ﷺ anasoma katika wakati wa magharibi:

وَأَلْمُرْسَلَاتِ عُرْفًا

“*Wal Mursalaat `Urfaa.*”³ Katika riwaya ya Maalik toka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما kwamba Ummul Fadhl رضي الله عنها alimsikia anasoma:

وَأَلْمُرْسَلَاتِ عُرْفًا

“*Wal Mursalaat `Urfaa.*” (77:1) Akasema (Ummul Fadhl رضي الله عنها): ‘Ewe mwanangu usomaji wako wa sura hii umenifanya nikumbuke kisomo cha mwisho nilichokisikia Mtume ﷺ akikisoma katika magharibi.’⁴ Wameipokea Bukhari na Muslim katika sahihi zao kupitia njia ya Maalik رضي الله عنه.⁵

¹ Fat'hul Al-Bari 4:42.

² Muslim 4:1755.

³ Ahmad 6:338.

⁴ Muwatta' 1:78 .

⁵ Fat'hul Al-Bari 2:287, na Muslim 1:338.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْمُرْسَلَاتِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَأَلْمُرْسَلَاتِ عُرْفًا ﴿١﴾ فَأَلْعِصْفَا ۝
 وَالنَّشِيطَاتِ نَشْرًا ﴿٢﴾ فَأَلْمَلَقَاتِ
 ذِكْرًا ﴿٣﴾ عَذْرًا أَوْ تَنْذَرًا ﴿٤﴾ إِنَّمَا
 تُوعَدُونَ لَوَاقِعٌ ﴿٥﴾ فَإِذَا الْتَجُومُ
 طُمِسَتْ ﴿٦﴾ وَإِذَا السَّمَاءُ فُرِجَتْ ﴿٧﴾
 وَإِذَا الْجِبَالُ سُيِّفَتْ ﴿٨﴾ وَإِذَا
 الرُّسُلُ أُنزِلَتْ ﴿٩﴾ لِأَيِّ يَوْمٍ أُجِّلَتْ
 لِيَوْمِ الْفَصْلِ ﴿١٠﴾ وَمَا
 أَذْرَكَ مَا يَوْمَ الْفَصْلِ ﴿١١﴾ وَيَلٌ
 يَوْمِئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٢﴾
 بِالْمُجْرِمِينَ ﴿١٣﴾ وَيَلٌ يَوْمِئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٤﴾
 أَلَمْ تَجْعَلْنَا فِي قَرَارٍ مَكِينٍ ﴿١٥﴾
 إِلَى قَدَرٍ مَعْلُومٍ ﴿١٦﴾ فَقَدَرْنَا فَنِعْمَ الْقَادِرُونَ ﴿١٧﴾ وَيَلٌ
 يَوْمِئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٨﴾ أَلَمْ تَجْعَلِ الْأَرْضَ كِهَاتَا ﴿١٩﴾
 أَحْيَاءَ وَأَمْوَاتًا ﴿٢٠﴾ وَجَعَلْنَا فِيهَا رَوَاسِيَ شَامِخَاتٍ
 وَأَسْقَيْنَكُم مَّاءً فُرَاتًا ﴿٢١﴾ وَيَلٌ يَوْمِئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٢٢﴾

وَأَلْمُرْسَلَاتِ عُرْفًا ﴿١﴾ فَأَلْعِصْفَا ۝
 وَالنَّشِيطَاتِ نَشْرًا ﴿٢﴾ فَأَلْمَلَقَاتِ
 ذِكْرًا ﴿٣﴾ عَذْرًا أَوْ تَنْذَرًا ﴿٤﴾ إِنَّمَا
 تُوعَدُونَ لَوَاقِعٌ ﴿٥﴾ فَإِذَا الْتَجُومُ
 طُمِسَتْ ﴿٦﴾ وَإِذَا السَّمَاءُ فُرِجَتْ ﴿٧﴾
 وَإِذَا الْجِبَالُ سُيِّفَتْ ﴿٨﴾ وَإِذَا
 الرُّسُلُ أُنزِلَتْ ﴿٩﴾ لِأَيِّ يَوْمٍ أُجِّلَتْ
 لِيَوْمِ الْفَصْلِ ﴿١٠﴾ وَمَا
 أَذْرَكَ مَا يَوْمَ الْفَصْلِ ﴿١١﴾ وَيَلٌ
 يَوْمِئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٢﴾

1. Naapa kwa zinazotumwa kwa upole!
2. Na zinazovuma kwa kasi!
3. Na zikaeneza maeneo yote!
4. Na zinazofarikisha zikatawanya!
5. Na zinazopeleka mawa-idha!

6. Kwa kuudhuru au kuonya,

7. Hakika mnayoahidiwa bila ya shaka yatakuwa!

8. *Wakati nyota zitakapofutwa,*
9. *Na mbingu zitakapopasuliwa,*
10. *Na milima itakapopeperushwa,*
11. *Na Mitume watakapowekewa wakati wao,*
12. *Kwa siku gani hiyo wamewekewa muda huo?*
13. *Kwa siku ya kupambanua!*
14. *Na nini kitakachokujulisha siku ya kupambanua ni nini?*
15. *Ole wao, siku hiyo hao wanaokanusha!*

Allah تعالیٰ Kuapia juu ya Viumbe Vyake Mbalimbali Kuhusu Ukweli wa Kutokea Kiama

Ibn Abi Haatim رضي الله عنه amesimulia kutoka kwa Abu Hurairah رحمه الله تعالى:

وَأَلْمُرْسَلَاتِ عُرْفًا

“Naapa kwa zinazotumwa kwa upole!”

Amesema: Ni Malaika. Aidha Imepokewa toka kwa Masruuq, Abu Ad-Dhuhaa, na Mujaahid katika moja ya riwaya mbili, Na Sudi na Rabi'i bin Anas mfano wa hivyo. Na imepokewa toka kwa Aby Swaalih kuwa amesema: Hao ni Mitume. Na katika riwaya nyingine toka kwake: Hao ni Malaika. Vile vile kama hivi amesema Abuu Swaalih katika: *“Wal'aaswifaat, wannaashiraat, walfaariqaat, walmulqiyaat”* Kuwa hao ni Malaika.

Thaury رحمه الله تعالى amesema toka kwa Salamah bin Kuhail toka kwa Muslim Bitwiin toka kwa Aby Al'Abiidain amesema: Nilimuuliza Ibn Mas'uud رضي الله عنه kuhusu *'Almursalaat Urfaa?'* Akasema: 'Ni upepo'¹ Na kadhalika wamesema hivyo Ibn Abbaas, Mujaahid na Qatadah.²

Na Ibn Jariir رحمه الله تعالى amekata shauri kwa kusema: *'Al'aswifaat'* ni pepo zinazovuma kama alivyosema Ibnu Mas'uud رضي الله عنه na waliomfuata, na akasita

¹ At-Tabari 24:124, 125.

² At-Tabari 24:123, 124, 125, 126.

kusema katika *Annaashiraat nashraa*, kuwa Je hao ni malaika au pepo kama ilivyotangulia? Na Abu Swaalih yeye amesema: '*Annaashiraat nashraa* hizo ni mvua. Na dhahiri ni kama alivyosema Allah تعالى:

وَأَرْسَلْنَا الرِّيحَ لَوَاقِحَ

"Na Tunazipeleka pepo za kupandishia." (15:22)

Allah تعالى Amesema:

وَهُوَ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهِ

"Na Yeye Ndiye Anayepeleka pepo (za kuvuma) kuwa ni bishara kabla ya kufika Rehema Yake." (7:57)

Kama hivi, *Al'aswifaat* hizo ni pepo, husemwa hivyo pindi pepo zinapovuma zinavuma kwa sauti. Kadhalika '*Annashiraat*' hizo ni pepo ambazo hutawanya mawingu katika anga za mbingu kama atakavyo Mola. Na Kauli Yake تعالى:

فَالْفَرْقَتِ فَزَقًا ۝ فَالْمَلَقَتِ ذِكْرًا ۝ عُذْرًا أَوْ تُذْرًا ۝

"Na zinazofarikisha zikatawanya! Na zinazopeleka mawaidha! Kwa kudhuru au kuonya."

Maana yake: Malaika, amelisema hilo Ibn Mas'ud, Ibn Abbaas, Masruuq, Mujaahid, Qataadah, Rabii bin Anas, Sudy na Thauri رضي الله عنهم¹. Na wala hapa hakuna upinzani kuwa hao wanashuka kwa amri ya Allah تعالى kwa mitume wakipambanua baina ya haki na batili, Na uongofu na upotevu, Halali na haramu, na wakawapa mitume wahyi wenye uadilifu kwa viumbe na kuwaonya na adhabu ya Allah تعالى iwapo watakalifu amri Yake. Na Kauli Yake تعالى:

إِنَّمَا تُوعَدُونَ لَوَاقِعٌ

"Hakika mnayohidiwa bila ya shaka yatakuwa!"

Hili ndio jambo linalosisitizwa kwa kutumia viapo hivi. Maana yake: Mlioahidiwa kama kusimama kiama, Kupulizwa parapanda, Kufufuliwa miili, na Kukusanywa wa mwanzo na wa mwisho katika uwanja mmoja, Kulipwa

¹ At-Tabari 24:128,129.

kila mtu kwa alilofanya, ikiwa ni kheri basi atalipwa kheri na ikiwa ni shari basi atalipwa shari. Kwa hakika haya yote yatatokea. Maana yake: Yatakuwa bila kizuizi.

Kutajwa baadhi ya yatakayotokea Siku ya Kiama

Kisha Allah تعالی Anasema:

﴿١٧﴾ فَإِذَا النُّجُومُ طُمِسَتْ

“Wakati nyota zitakapofutwa.”

Maana yake: Mwanga wake utaondoka. Kama Kauli Yake تعالی:

﴿١٨﴾ وَإِذَا النُّجُومُ أَنْكَدَرَتْ

“Na nyota zikazimwa.” (81:2)

Kama katika Kauli Yake تعالی:

﴿١٩﴾ وَإِذَا الْكَوَاكِبُ انْتَبَرَتْ

“Na nyota zitapotawanyika.” (82:2)

Kisha Allah تعالی Anasema:

﴿٢٠﴾ وَإِذَا السَّمَاءُ فُرِجَتْ

“Na mbingu zitakapopasuliwa.”

Maana yake: Zitafura na kupasuka, pande zake zitaporomoka, pambizo zake kuwa dhaifu. Allah تعالی Anasema:

﴿٢١﴾ وَإِذَا الْجِبَالُ نُسِفَتْ

“Na milima itakapopeperushwa.” (77:10)

Maana yake: Itaondoshwa wala haitabaki athari yake yoyote. Kama katika Kauli Yake تعالی:

﴿٢٢﴾ وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الْجِبَالِ فَقُلْ يَنْسِفُهَا رَبِّي نَسْفًا

“Na wanakuuliza khabari za milima. Waambie: Mola Wangu Mlezi ataivurugavuruga.” (20:105)

Allah تعالى Anasema:

﴿٤٧﴾ وَيَوْمَ نُسَيِّرُ الْجِبَالَ وَتَرَى الْأَرْضَ بَارِزَةً وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا

“Na siku Tutapoiondoa milima na ukaiona ardhi iwazi, na Tukawafufua - wala hatutamuacha hata mmoja kati yao.” (18:47).

Kauli Yake تعالى:

﴿١١﴾ وَإِذَا الرُّسُلُ أُقْتَتِ

“Na Mitume watakapowekewa wakati wao” (77:11)

Al'Awfi amesema toka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: watakapokusanywa.¹ Ibn Zayd amesema: Hii ni kama Kauli Yake:

﴿١٠﴾ يَوْمَ يَجْمَعُ اللَّهُ الرُّسُلَ

“...Ile siku ambayo Mwenyezi Mungu Atapowakusanya Mitume...” (5:109).²

Mujaahid amesema:

﴿١١﴾ أُقْتَتِ

“Watakapowekewa wakati wao.” (77:11).

Maana yake: Watakapoekewa muda.³ Thaury anasema toka kwa Mansuur kutoka kwa Ibrahimu:

﴿١١﴾ أُقْتَتِ

“Watakapowekewa wakati wao.”

Watakapopewa miadi yao,¹ ni kana kwamba anaijaalia miadi hiyo. Kama katika Kauli Yake:

﴿٣٦﴾ وَأَشْرَقَتِ الْأَرْضُ بِنُورِ رَبِّهَا وَوُضِعَ الْكِتَابُ وَجِئَتْ بِالنَّبِيِّينَ وَالشُّهَدَاءِ وَقُضِيَ بَيْنَهُمْ

﴿٣٦﴾ بِالْحَقِّ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

“Na ardhi itang'ara kwa Nuru ya Mola Wake Mlezi, na Kitabu

¹ At-Tabari 24:129.

² At-Tabari 24:130.

³ At-Tabari 24:130.

kitawekwa, na wataletwa Manabii na mashahidi, na patahukumiwa baina yao kwa haki, wala hawatadhulumiwa.” (39:69).

Kisha Allah تعالى Akasema:

لَأَيَّ يَوْمٍ أُجِّلَتْ ﴿٦٩﴾ لِيَوْمِ الْفَصْلِ ﴿٧٠﴾ وَمَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمَ الْفَصْلِ ﴿٧١﴾ وَيَلَّ يَوْمَئِذٍ ﴿٧٢﴾
لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٧٣﴾

“Kwa siku gani hiyo wamewekewa muda huo?. Kwa siku ya kupambanua!. Na nini kitakachokujulisha siku ya kupambanua ni nini?. Ole wao, siku hiyo hao wanaokanusha!”

Allah تعالى Anasema, kwa siku gani hiyo ambayo mitume wamewekewa na kucheleweshwa jambo lao ili kisimame kiama. Kama Allah تعالى Anavyosema:

فَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ مُحَلِّفًا وَعَدِيهٖ زُسْلَهُۥٓ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ ذُو انْتِقَامٍ ﴿٧٤﴾ يَوْمَ تُبَدَّلُ الْأَرْضُ ﴿٧٥﴾
غَيْرَ الْأَرْضِ وَالسَّمَوٰتُ ۖ وَبُرُزُوا۟ لِلَّهِ الْوٰحِدِ الْقَهَّارِ ﴿٧٦﴾

“Basi usimdhania Mwenyezi Mungu kuwa ni Mwenye Kuwavunjia ahadi Yake Mitume Wake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushinda, na ni Mwenye Kulipiza. Siku itapogeuzwa ardhi iwe ardhi nyengine, na mbingu pia. Nao watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu Mmoja, Mwenye Nguvu.”

Hiyo ni siku ya upambanuzi. Kama Allah تعالى Anavyosema:

لِيَوْمِ الْفَصْلِ ﴿٧٧﴾

“Kwa siku ya kupambanua!”

Kisha Allah تعالى Anasema kuonesha uzito wa jambo hilo:

وَمَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمَ الْفَصْلِ ﴿٧٨﴾ وَيَلَّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٧٩﴾

“Na nini kitakachokujulisha siku ya kupambanua ni nini? Ole wao, siku hiyo hao wanaokanusha!”

¹ At-Tabari 24:130.

Maana yake: Ole wao kutokana na adhabu ya Allah تعالى kesho.

أَلَمْ يُلْهِكَ الْأُولَىٰ ۖ ثُمَّ نَسَّيَهُمُ الْآخِرِينَ ۚ ۝ كَذَٰلِكَ نَفْعَلُ بِالْمُجْرِمِينَ ۝
 وَيَلُومُ يَوْمَئِذٍ الْمُكَذِّبِينَ ۝ أَلَمْ نَخْلُقْكُمْ مِّنْ مَّاءٍ مَّهِينٍ ۝ فَجَعَلْنَاهُ فِي قَرَارٍ مَّكِينٍ ۝
 إِلَىٰ قَدَرٍ مَّعْلُومٍ ۝ فَقَدَرْنَا فَنِعْمَ الْقَادِرُونَ ۝ وَيَلُومُ يَوْمَئِذٍ الْمُكَذِّبِينَ ۝ أَلَمْ
 نَجْعَلِ الْأَرْضَ كِفَاتًا ۝ أَحْيَاءَ وَأَمْوَاتًا ۝ وَجَعَلْنَا فِيهَا رِوْاسِيَ شَامِخَاتٍ وَأَسْقَيْنَاكُمْ
 مَّاءً فَرَاتًا ۝ وَيَلُومُ يَوْمَئِذٍ الْمُكَذِّبِينَ ۝

16. Kwani hatukuwaangamiza walio tangulia?
17. Kisha Tukawafuutilizia waliofuatia?
18. Ndio kama hivi Tuwatendavyo wakosefu!
19. Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!
20. Kwani hatukukuumbeni kwa maji ya kudharauliwa?
21. Kisha Tukayaweka mahali pa utulivu madhubuti?
22. Mpaka muda maalumu?
23. Tukakadiria na Sisi ni wabora wa kukadiria.
24. Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!
25. Kwani hatukuifanya ardhi yenye kukusanya
26. Walio hai na maiti?
27. Na ndani yake Tukaweka milima mirefu yenye kuthibiti, na Tunakunywesheni maji matamu?
28. Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!

Wito wa Kuzingatia aina Mbalimbali za Qudura na Uwezo wa Allah تعالی

Allah تعالی Anasema:

أَلَمْ يَهْدِكَ الْأَوَّلِينَ ﴿١٦﴾

“Kwani hatukuwaangamiza waliotangulia?”

Maana yake: Miongoni mwa wakadhibishaji Mitume, wenye kuhalifu waliokuja nayo. Allah تعالی Anasema:

ثُمَّ تَتَّبِعُهُمُ الْآخِرِينَ ﴿١٧﴾

“Kisha Tukawafuutilizia waliofuatia?” (77:17)

Maana yake: Miongoni mwa wanaofanana na hao, na kwa kuzingatia hilo, Allah تعالی Anasema:

كَذَلِكَ نَفْعَلُ بِالْمُجْرِمِينَ ﴿١٨﴾ وَيَلُومُنَّ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٩﴾

“Ndio kama hivi Tuwatendavyo wakosefu!. Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!”

Amelisema hilo Ibn Jariir رحمه الله تعالی¹ kisha Allah تعالی Akasema Akiwakumbusha waja Wake neema Alizowapa, akijenga hoja ya kuwakumbusha mwanzo wa kuumbwa jinsi ulivyokuwa:

أَلَمْ نَخْلُقْكُمْ مِّن مَّاءٍ مَّهِينٍ ﴿٢٠﴾

“Kwani hatukukuumbeni kwa maji ya kudharauliwa?”

Maana yake: Dhaifu, duni kwa mnasaba wa kudura ya Allah تعالی kama ilivyokuja katika hadithi ya (Busri) bin Jihaash:

«إِنَّ أَدَمَ أَنَّى تُعْجِزُنِي وَقَدْ خَلَقْتَنكَ مِن مِّثْلِي هَذِهِ؟»

“Ewe mwanadamu utanishinda vipi, na hali ya kuwa Nimekuumba kutokana na mfano huu?”²

¹ At-Tabari 24:131.

² Ahmad 4:210.

فَجَعَلْنَاهُ فِي قَرَارٍ مَّكِينٍ ﴿١٣٤﴾

“Kisha Tukayaweka mahali pa utulivu madhubuti?”

Maana yake: Tumeyaweka katika kifuko cha Uzazi, na mahali hapo ni madhubuti kwa maji yatokanayo kwa mwanamume na mwanamke, na kifuko cha uzazi kimeandaliwa kwa ajili hiyo ili kuhifadhi maji yaliowekwa ndani yake. Na Kauli Yake تعالى:

إِلَى قَدَرٍ مَّعْلُومٍ ﴿١٣٥﴾

“Mpaka muda maalumu?”

Maana yake: Muda maalumu, uliyoainishwa kuanzia miezi sita hadi miezi tisa. Na kwa ajili hii Allah تعالى Anasema:

فَقَدَرْنَا فَنِعْمَ الْقَادِرُونَ ﴿١٣٦﴾ وَيَلَّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٣٧﴾

“Tukakadiria na Sisi ni wabora wa kukadiria. Ole wao siku hiyo hao wanao kanusha!”

Kisha Allah تعالى Anasema:

أَلَمْ نَجْعَلِ الْأَرْضَ كِفَاتًا ﴿١٣٨﴾ أَحْيَاءً وَأَمْوَاتًا ﴿١٣٩﴾

“Kwani hatukuifanya ardhi yenye kukusanya. Walio hai na maiti?”

Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Kifat” Ni mahali pa kujihifadhi. Mujaahid amesema: Inamfunika maiti wala hakionekani kitu chochote kwake na juu ya mgongo wake.¹

Sha’aby amesema: Ndani yake ni kwa ajili ya maiti wenu na ni kwa ajili ya watu walio hai wenu.²

Na hivyo hivyo amesema Mujaahid na Qatadah.³

¹ At-Tabari 24:134.

² At-Tabari 24:138.

³ At-Tabari 24:134, 139-141.

⁴ Fat-hul Bari 8:556.

وَجَعَلْنَا فِيهَا رَوْيِيَ شَمِخَاتٍ

“Na ndani yake Tukaweka milima mirefu yenye kuthibiti.” (77:27)

Maana yake: Milima, Ameshikizia Ardhi ili isitikisike na kutetemeka:

وَأَسْقَيْنَكُم مَّاءٍ فُرَاتًا

“Na Tunakunywesheni maji matamu?” (77:27)

Maana yake: Matamu yaliyopoa kutoka juu mawinguni au Aliyokuchimbulieni kutoka chemchemi za ardhini.

وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ

“Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!”

Maana yake: Ole wake ambaye amezingatia viumbe hivi vyenye kuonesha ukubwa wa Aliyeviumba na Utukufu Wake. Kisha baada ya hapo akaendelea kukadhibisha na kukufuru kwake.

* * *

أَنْطَلِقُوا إِلَىٰ مَا كُنْتُمْ بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿٢٩﴾ أَنْطَلِقُوا إِلَىٰ ظِلِّ
 ذِي ثَلَاثِ شُعَبٍ ﴿٣٠﴾ لَا ظَلِيلٍ وَلَا يُغْنِي مِنَ اللَّهِبِ ﴿٣١﴾
 إِنَّهَا تَرْمِي بِشَرَرٍ كَالْقَصْرِ ﴿٣٢﴾ كَأَنَّهُ جَمَلٌ صُفْرٌ ﴿٣٣﴾
 وَبَلِّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٤﴾ هَذَا يَوْمٌ لَا يَنْطِقُونَ ﴿٣٥﴾
 وَلَا يُؤْذَنُ لَهُمْ فَيَعْتَذِرُونَ ﴿٣٦﴾ وَبَلِّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ
 ﴿٣٧﴾ هَذَا يَوْمٌ الْفَصْلِ ط جَمَعْنَاكَ وَالْأُولَىٰ ﴿٣٨﴾ فَإِن
 كَانَ لَكُمْ كَيْدٌ فَكِيدُوا ﴿٣٩﴾ وَبَلِّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٠﴾
 إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي ظِلَالٍ وَعُيُونٍ ﴿٤١﴾ وَقَوَاكِبٍ مِّمَّا يَشْتَبُونَ
 ﴿٤٢﴾ كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٤٣﴾ إِنَّا
 كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٤٤﴾ وَبَلِّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ
 ﴿٤٥﴾ كُلُوا وَتَمَتَّعُوا قَلِيلًا إِنَّكُمْ تُجْرِمُونَ ﴿٤٦﴾ وَبَلِّ يَوْمَئِذٍ
 لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٧﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ ارْكَعُوا لَا يَرْكَعُونَ
 ﴿٤٨﴾ وَبَلِّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٩﴾ فَبِأَيِّ حَدِيثٍ بَعْدَهُ
 يُؤْمِنُونَ ﴿٥٠﴾

أَنْطَلِقُوا إِلَىٰ مَا كُنْتُمْ بِهِ تُكَذِّبُونَ
 ﴿٢٩﴾ أَنْطَلِقُوا إِلَىٰ ظِلِّ ذِي ثَلَاثِ
 شُعَبٍ ﴿٣٠﴾ لَا ظَلِيلٍ وَلَا يُغْنِي مِنَ
 اللَّهِبِ ﴿٣١﴾ إِنَّهَا تَرْمِي بِشَرَرٍ كَالْقَصْرِ
 ﴿٣٢﴾ كَأَنَّهُ جَمَلٌ صُفْرٌ ﴿٣٣﴾
 وَبَلِّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٤﴾ هَذَا
 يَوْمٌ لَا يَنْطِقُونَ ﴿٣٥﴾ وَلَا يُؤْذَنُ لَهُمْ
 فَيَعْتَذِرُونَ ﴿٣٦﴾ وَبَلِّ يَوْمَئِذٍ
 لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٧﴾ هَذَا يَوْمٌ الْفَصْلِ ط
 جَمَعْنَاكَ وَالْأُولَىٰ ﴿٣٨﴾ فَإِن كَانَ
 لَكُمْ كَيْدٌ فَكِيدُوا ﴿٣٩﴾ وَبَلِّ يَوْمَئِذٍ
 لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٠﴾

29. Nendeni kwenye adhabu mliyokuwa mkiikanusha!

30. Nendeni kwenye kivuli chenye mapande matatu!
31. Hakikingi moto, wala hakiwaepushi na mwako.
32. Hakika Moto huo unatoa macheche kama majumba!
33. Kama kwamba ni ngamia wa rangi ya manjano!
34. Ole wao siku hiyo hao wanao kanusha!
35. Hii ni siku ambayo hawatatamka kitu,
36. Wala hawataruhusiwa kutoa udhuru.

37. Ole wao siku hiyo hao waliokanusha!

38. Hii ndiyo siku ya kupambanua. Tumekukusanyeni nyinyi na waliotangulia.

39. Ikiwa mnayo hila, nifanyieni hila Mimi!

40. Ole wao siku hiyo hao waliokanusha!

Waovu Watapelekwa kwenye makazi yao ya Jahannamu na Kupata Wanachostahiki

Allah تعالى Anasema kuhusu makafiri wakadhibishaji wa kufufuliwa malipo, pepo na moto, kuwa wao wataambiwa siku ya kiama:

أَنْطَلِقُوا إِلَىٰ مَا كُنْتُمْ بِهِ تَكْذِبُونَ ﴿٢٩﴾ أَنْطَلِقُوا إِلَىٰ ظِلٍّ ذِي ثَلَاثِ شُعَبٍ ﴿٣٠﴾

“Nendeni kwenye adhabu mliyokuwa mkiikanusha!, Nendeni kwenye kivuli chenye mapande matatu!”

Maana yake: Miale ya moto inayopanda na moshi pamoja. Kwa hiyo, kutokana na ukali na nguvu yake unakuwa na pande tatu:

لَا ظَلِيلٍ وَلَا يُغْنِي مِنَ الْلَّهَبِ ﴿٣١﴾

“Hakikingi moto, wala hakiwaepushi na mwako.”

Maana yake: Kivuli cha moshi chenye kuambatana na miale ya moto, hicho chenyewe si kivuli halisi wala hakitoshi kujikinga na miale ya moto, wala hakiwakingi wao na joto la miale ya moto huo. Na Kauli Yake تعالى:

إِنَّمَا تَرَىٰ بِشَرِّهِ كَالْفَصْرِ ﴿٣٢﴾

“Hakika Moto huo unatoa macheche kama majumba!”

Maana yake: Cheche zake zinaruka kutokana na miale yake kama nyumba. Ibn Mas'ud رضي الله عنه amesema: kama ngome.¹ Ibn Abbaas, Mujaahid, Qatadah, na Maalik رضي الله عنهم, wamesema toka kwa Zaid bin Aslam na wengine: Maana yake: Kama mashina ya miti.²

¹ At-Tabari 24:163.

² At-Tabari 24:163.

كَأَنَّهُ جُمِلَتْ صُفْرًا ﴿٣٣﴾

“Kama kwamba ni ngamia wa rangi ya manjano!” (77:33).

Maana yake: Kama ngamia weusi. Kauli hii ameisema Mujaahid Hasan, Qatadah, na Adh-Dhahaak, na ameikubali Ibn Jariir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى³. Na kutoka kwa Ibn Abbaas, Mujaahid, na Saiid bin Jubayr رضي الله عنهم:

جُمِلَتْ صُفْرًا ﴿٣٣﴾

“Ni ngamia wa rangi ya manjano!” (77:33).

Maana yake: Kamba za meli.

إِنهَا تَرَى بِشَرِّرٍ كَالْقَصْرِ ﴿٣٤﴾

“Hakika Moto huo unatoa macheche kama majumba!”

Amesema: Tulikuwa tunatumia mbao dhiraatatu na zaidi ya hapo, na tunazijenga kwa kuzienua juu, kwa kufanya hivyo tunaziita nyumba.

كَأَنَّهُ جُمِلَتْ صُفْرًا ﴿٣٥﴾

“Kama kwamba ni ngamia wa rangi ya manjano!”

Kamba za meli, zinakusanywa hadi zinakuwa kama matumbo ya watu.¹

وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٦﴾

“Ole wao siku hiyo hao waliokanusha!”

Waovu Kushindwa Kusema, Kutoa Udhuru, na Kusimamisha Hoja Siku ya Kiama

Kisha Allah تَعَالَى Anasema:

هَذَا يَوْمٌ لَا يَنْطِقُونَ ﴿٣٧﴾

“Hii ni siku ambayo hawatatamka kitu,” Maana yake: Hawatasema.

وَلَا يُؤْذَنُ لَهُمْ فَيَعْتَذِرُونَ ﴿٣٨﴾

“Wala hawataruhusiwa kutoa udhuru.”

¹ Fat'hul Al-Bari 8:556.

Maana yake: Hawataweza kusema, wala hawataruhusiwa kutoa udhuru, bali ushahidi dhidi yao upo wazi. Na kauli ya kudhulumu kwao, imeshathibiti, hivyo wao hawatazungumza. Na viwanja vya kiama vina hali nyingi. Mola Mtukufu Anaeleza kuhusu hali hizo, kwa kutumia taswira mbalimbali, ili kujulisha ukali wa vituko na matetemeko ya siku hiyo. Na kwa ajili hii anasema baada ya kila kipambanuzi:

وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٧٧﴾

“Ole wao siku hiyo hao waliokanusha!”

Na Kauli Yake تعالی:

هَذَا يَوْمُ الْفَصْلِ ط جَمَعْنَاكُمْ وَالْأُولَىٰ ﴿٧٨﴾ فَإِنْ كَانَ لَكُمْ كَيْدٌ فَكِيدُونِ ﴿٧٩﴾

“Hii ndiyo siku ya kupambanua. Tumekukusanyeni nyinyi na walio tangulia, ikiwa mnayo hila, nifanyieni hila Mimi”

Huu ni ulinganu wa Muumba kwa waja Wake. Anawaambia:

هَذَا يَوْمُ الْفَصْلِ ط جَمَعْنَاكُمْ وَالْأُولَىٰ ﴿٨٠﴾

“Hii ndiyo siku ya kupambanua. Tumekukusanyeni nyinyi na walio tangulia.”

Maana yake: Amewakusanya kwa Kudura Yake katika uwanja mmoja, wakisikia wito Wake na huku wakiwachunga wao.

إِنْ كَانَ لَكُمْ كَيْدٌ فَكِيدُونِ ﴿٨١﴾

“Ikiwa mnayo hila, nifanyieni hila Mimi!”

Hii ni kauli nzito yenye kitisho na kemeo kali. Maana yake: Ni kuwa, iwapo mtaweza kutoroka Mikononi Mwangu na mkaokoka na Hukumu Yangu basi fanyeni. Na wala hamtaweza hilo kama Alivyosema تعالی.

يَمَعَّشَرَ آلِجِنِّ وَالْإِنْسِ إِنَّ اسْتَعْطَعْتُمْ أَنْ تَنْفُذُوا مِنْ أَقْطَارِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ فَانْفُذُوا

لَا تَنْفُذُونَ إِلَّا بِسُلْطَانٍ ﴿٨٢﴾

“Enyi makundi ya majini na watu! Mkiweza kupenya kwenye mbingu na ardhi, basi penyeni! Hamtapenya ila kwa kupewa madaraka.” (55:33)

Allah تعالیٰ Amesema:

وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئًا

“Wala nyinyi hamumdhuru kitu Yeye.” (11:57)

Katika hadithi Qudsi Allah تعالیٰ Anasema:

«يَا عِبَادِي، إِنَّكُمْ لَنْ تَبْلُغُوا نَفْعِي فَتَنْفَعُونِي، وَلَنْ تَبْلُغُوا ضَرْيَ فَتَضُرُّونِي»

“Enyi waja Wangu hakika nyinyi hamuwezi mkaniletea manufaa au kunisababishia madhara”¹

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي ظِلِّهِ وَعُيُونٍ ﴿١١﴾ وَفَوَاكِهِ مِمَّا يَشْتَهُونَ ﴿١٢﴾ كُلُّوْا وَأَشْرَبُوا هَيْئًا بِمَا
 كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٣﴾ إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٤﴾ وَيَلُومِيزُ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٥﴾ كُلُّوْا
 وَتَمَتَّعُوا قَلِيلًا إِنَّكُمْ مُجْرِمُونَ ﴿١٦﴾ وَيَلُومِيزُ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٧﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ ارْكَعُوا
 لَا يَرْكَعُونَ ﴿١٨﴾ وَيَلُومِيزُ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٩﴾ فَبِأَيِّ حَدِيثٍ بَعْدَهُ يُؤْمِنُونَ ﴿٢٠﴾

41. Hakika wachamngu watakuwa katika vivuli na chemchem,

42. Na matunda wanayoyapenda,

43. Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa yale mliyo kuwa mkiyatenda.

44. Hakika ndio kama hivyo Tunavyowalipa watendao mema.

45. Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!

46. Kuleni na mjifurahishe kidogo tu. Hakika nyinyi ni wakosefu!

47. Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!

48. Na wakiambiwa: Inameni! Hawainami.

49. Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!

50. Basi maneno gani baada ya haya watayaamini?

¹ Muslim 4:1994.

Marejeo ya wachamungu

Allah تعالیٰ Anasema Akielezea kuhusu waja Wake wema ambao wamemuabudu kwa kutekeleza wajibu na kuacha yaliyoharamishwa, na kuwa wao siku ya kياما watakuwa katika pepo na chemchemi. Kwa maana: Kinyume cha hao waovu watakaokuwa katika vivuli vya moshi mweusi wa uvundo. Na Kauli Yake تعالیٰ:

﴿فَوَاكِهَ مِمَّا يَشْتَبُونَ﴾

“Na matunda wanayoyapenda.” Maana yake: Na katika aina nyingine mbalimbali za matunda, vyovyote watakavyotaka watapata.

﴿كُلُوا وَأَشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ﴾

“Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa yale mliyokuwa mkiyatenda.”

Maana yake: Wataambiwa hivyo kwa njia ya hisani. Kisha Allah تعالیٰ Anasema habari mpya:

﴿إِنَّا كَذَّابِكُمْ جَزَى الْمُحْسِنِينَ﴾

“Hakika ndio kama hivyo Tunavyowalipa watendao mema.”

Maana yake: Haya ni malipo Yetu kwa ajili ya aliyefanya amali njema.

﴿وَيَلُّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ﴾

“Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!”

Kutishwa Mwenye Kukanusha Kiama

Kauli Yake تعالیٰ:

﴿كُلُوا وَتَمَتُّعُوا قَلِيلًا إِنَّكُمْ تُجْرَمُونَ﴾

“Kuleni na mjifurahishe kidogo tu. Hakika nyinyi ni wakosefu!”

Tamko hili ni kwa wanaopinga siku ya malipo, na amri hii juu yao ni ya kuonya, na kukemea. Allah تعالیٰ Anasema:

﴿كُلُوا وَتَمَتُّعُوا قَلِيلًا﴾

“Kuleni na mjifurahishe kidogo tu.” Maana yake: Muda mchache na mfupi mno.

إِنكُمْ تُجْرِمُونَ ﴿٤٩﴾

“Hakika nyinyi ni wakosefu!”

Maana yake: Kisha wataswagwa kwenye moto wa Jahanamu ambao tumeshatangulia kuutaja.

وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٥٠﴾

“Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!”

Kama Allah تعالى Alivyosema:

نُمَتِّعُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٣١﴾

“Tunawastarehesha kwa uchache, kisha Tutawasukuma kwenye adhabu ngumu.” (31:24)

Allah تعالى Anasema:

إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿٦٩﴾ مَتَّعٌ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُذِيقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٧٠﴾

“Hao wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa. Hiyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha marejeo yao ni Kwetu. Tena Tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao.” (10:69-70)

Kauli Yake تعالى:

وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ ارْكَعُوا لَا يَرْكَعُونَ ﴿٨٠﴾

“Na wakiambiwa: Inameni! Hawainami.”

Maana yake: Wanapoamriwa hao majahili wa kikafiri wawe miongoni mwa wanaosali pamoja na waislamu, hujizuia kwa hilo, na kufanya majivuno.

Na kwa ajili hii Allah تعالى Anasema:

وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٨١﴾

“Ole wao siku hiyo hao wanaokanusha!”

Kisha Akasema تعالى:

فَبِأَيِّ حَدِيثٍ بَعْدَهُ يُؤْمِنُونَ ﴿٤٥﴾

“Basi maneno gani baada ya haya watayaamini?”

فَبِأَيِّ حَدِيثٍ بَعْدَ اللَّهِ وَءَايَاتِهِ يُؤْمِنُونَ ﴿٤٦﴾

“Basi hadithi gani watakayoiamini baada ya Mwenyezi Mungu na Aya Zake?” (45:6)

Mwisho wa Tafsiri ya surat Al-Mursalat

* * *

Tafsiri ya Suratun Naba'

Sura ya 78

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ النَّبَاِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

عَمَّ يَتَسَاءَلُونَ ﴿١﴾ عَنِ النَّبِيِّ الْعَظِيمِ ﴿٢﴾ الَّذِي هُوَ فِيهِ
 مُخْتَلِفُونَ ﴿٣﴾ كَلَّا سَيَعْمُونَ ﴿٤﴾ ثُمَّ كَلَّا سَيَعْمُونَ ﴿٥﴾
 أَلَمْ نَجْعَلِ الْأَرْضَ مِهْدًا ﴿٦﴾ وَالْجِبَالَ أَوْتَادًا ﴿٧﴾
 وَخَلَقْنَاهُكُمْ أَزْوَاجًا ﴿٨﴾ وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتًا ﴿٩﴾ وَجَعَلْنَا
 اللَّيْلَ لِبَاسًا ﴿١٠﴾ وَجَعَلْنَا النَّهَارَ مَعَاشًا ﴿١١﴾ وَبَنَيْنَا فَوْقَكُمْ
 سَبْعًا شِدَادًا ﴿١٢﴾ وَجَعَلْنَا سِرَاجًا وَهَاجًا ﴿١٣﴾ وَأَنْزَلْنَا
 مِنَ الْمُعْصِرَاتِ مَاءً ثَجَّاجًا ﴿١٤﴾ لِنُخْرِجَ بِهِ حَبًّا وَنَبَاتًا ﴿١٥﴾
 وَجَنَّاتٍ أَلْفَافًا ﴿١٦﴾

عَمَّ يَتَسَاءَلُونَ ﴿١﴾ عَنِ النَّبِيِّ
 الْعَظِيمِ ﴿٢﴾ الَّذِي هُوَ فِيهِ
 مُخْتَلِفُونَ ﴿٣﴾ كَلَّا سَيَعْمُونَ ﴿٤﴾
 ثُمَّ كَلَّا
 سَيَعْمُونَ ﴿٥﴾ أَلَمْ نَجْعَلِ
 الْأَرْضَ
 مِهْدًا ﴿٦﴾ وَالْجِبَالَ
 أَوْتَادًا ﴿٧﴾ وَخَلَقْنَاهُكُمْ
 أَزْوَاجًا ﴿٨﴾ وَجَعَلْنَا
 نَوْمَكُمْ
 سُبَاتًا ﴿٩﴾ وَجَعَلْنَا
 اللَّيْلَ
 لِبَاسًا ﴿١٠﴾ وَجَعَلْنَا
 النَّهَارَ
 مَعَاشًا ﴿١١﴾ وَبَنَيْنَا
 فَوْقَكُمْ
 سَبْعًا شِدَادًا ﴿١٢﴾
 وَجَعَلْنَا
 سِرَاجًا
 وَهَاجًا ﴿١٣﴾ وَأَنْزَلْنَا
 مِنَ
 الْمُعْصِرَاتِ
 مَاءً ثَجَّاجًا ﴿١٤﴾
 لِنُخْرِجَ
 بِهِ حَبًّا
 وَنَبَاتًا ﴿١٥﴾
 وَجَنَّاتٍ
 أَلْفَافًا ﴿١٦﴾

1. Wanaulizana nini?
2. Ile khabari kuu,
3. Ambayo kwayo wanakhitalifiana.
4. La! Karibu watakuja jua.
5. Tena la! Karibu watakuja jua.

6. Kwani hatukuifanya ardhi kama tandiko?
7. Na milima kama vigingi?
8. Na Tukakuumbeni kwa jozi?
9. Na Tukakufanya kulala kwenu ni mapumziko?
10. Na Tukaufanya usiku ni nguo?
11. Na Tukaufanya mchana ni wa kuchumia maisha?
12. Na Tukajenga juu yenu mbingu saba zenye nguvu?
13. Na Tukaifanya taa yenye mwanga na joto,
14. Na Tukateremsha maji yanayoanguka kwa kasi kutoka mawinguni,
15. Ili Tutoe kwayo nafaka na mimea,
16. Na mabustani yenye miti iliyokamatana.

Kubainishwa kwa Washirikina Wanaopinga Uwepo wa Kiama.

Allah تعالیٰ Anasema kuhusu washirikina katika kuulizana kwao kuhusu siku ya kiyama ambayo wanaikanusha uwepo wake,

عَمَّ يَتَسَاءَلُونَ ﴿١٠٠﴾ عَنِ النَّبِئِ الْعَظِيمِ ﴿١٠١﴾

“Wanaulizana nini? Ile khabari kuu...”

Maana yake: Ni kutokana na jambo gani wanaulizana? Kuhusu jambo la kiyama! Hiyo ndiyo khabari kubwa. Allah تعالیٰ Anakusudia khabari kubwa sana yenye kutisha yenye kufadhaisha yenye kuogofya,

الَّذِي هُمْ فِيهِ مُخْتَلِفُونَ ﴿١٠٢﴾

“Ambayo kwayo wanakhitalifiana.”

Kwa maana: Watu kuhusu suala la Kiyama wako katika mapote mawili; kuna wenye kukiamini na wenye kukikufuru. Kisha Amesema Allah تعالیٰ hali ya kuwakemea wakanushaji Kiyama,

كَلَّا سَيَعْمُونَ ﴿١٠﴾ ثُمَّ كَلَّا سَيَعْمُونَ ﴿١١﴾

“La! Karibu watakuja jua. Tena la! Karibu watakuja jua.”

Na hivyo ni vitisho vikubwa sana na makemeo yenye kutiliwa mkazo.

Kutaja Mambo katika Uwezo wa Allah تعالى kama Dalili Juu ya Uwezo Wake wa Kufufua Baada ya Kufa.

Kisha Allah تعالى Akaanza Kubainisha na Kuweka wazi Uwezo Wake mkubwa juu ya Kuviumba vitu vya ajabu na mambo ya ajabu yenye kufahamisha juu ya Uwezo Wake katika yale Ayatakayo miongoni mwa mambo ya kurejea viumbe Kwake na mengineyo. Anasema:

أَلَمْ نَجْعَلِ الْأَرْضَ مَهْدًا ﴿١٢﴾

“Kwani hatukuifanya ardhi kama tandiko?”

Maana yake: Imetandikwa kwa ajili ya viumbe na imeidhinishwa kwa ajili yao, hali ya kuwa ni tulivu na imara.

وَالْجِبَالَ أَوْتَادًا ﴿١٣﴾

“Na milima kama vigingi?” Maana yake: Ameifanyia vigingi. Ameithibitisha kwa vigingi hivyo na Ameituliza mpaka imetulia na haikutikisika na vilivyo juu yake. Kisha Amesema Allah تعالى:

وَخَلَقْنَاكُمْ أَزْوَاجًا ﴿١٤﴾

“Na Tukakuumbeni kwa jozi?”

Anakusudia mume na mke anastarehe kila mmoja na mwenzie na kunapatikana kuzaana kwa njia hiyo. Kama Kauli Yake Allah تعالى:

وَمِنْ آيَاتِنَا أَنْ خَلَقْنَا لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلْنَا بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً
وَرَحْمَةً ﴿١٥﴾

“Na katika Ishara Zake ni kuwa Amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye Amejaalia mapenzi na huruma baina yenu.” (30:21)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتًا ﴿١١﴾

“Na Tukakufanya kulala kwenu ni mapumziko?”

Maana yake: Ni kukata harakati ili yapatikane mapumziko kutokana na uwingi wa mizunguko na kuyahangakia maisha katikati ya mchana, na hakika umetangulia mfano wa aya hii katika *Surat Al-Furqan*.

وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ لِبَاسًا ﴿١٢﴾

“Na Tukaufanya usiku ni nguo?”

Maana yake: Kinawafunika watu kiza chake na weusi wake kama Alivyosema Allah تعالى:

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَاهَا ﴿١٣﴾

“Na kwa usiku unapolifunika!” (91:4)

Na amesema Qatadah katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَجَعَلْنَا النَّهَارَ مَعَاشًا ﴿١٤﴾

“Na Tukaufanya mchana ni wa kuchumia maisha?”

Maana yake: Tumeufanya ni wenye kuangaza wenye nuru ili watu waweze kufanya mambo yao ndani yake na kwenda na kurudi kwa ajili ya maisha na kuchuma na kufanya biashara na yasiyo kuwa hayo.¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَنَبِّئْنَا فَوْقَكُمْ سَبْعًا شِدَادًا ﴿١٥﴾

“Na Tukajenga juu yenu mbingu saba zenye nguvu?”

Anakusudia mbingu saba katika upana wake na kunyanyuka kwake na kutandazwa vizuri na kwa umadhubuti wake na kuzipamba kwa nyota zenye kudhibiti na zenye kwenda. Na kwa sababu hii Amesema Allah تعالى:

¹ At-Tabari 24:152.

وَجَعَلْنَا سِرَاجًا وَهَاجًا ﴿٣٠﴾

“Na Tukaifanya taa yenye mwanga na joto.”

Analikusudia jua lenye kutoa mwangaza katika ulimwengu wote. Jua ambalo unaangaza mwangaza wake kwa watu wote wa ardhini.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَنْزَلْنَا مِنَ الْمُعْصِرَاتِ مَاءً مُّجَبَّاجًا ﴿٣١﴾

“Na Tukateremsha maji yanayoanguka kwa kasi kutoka mawinguni...”

Na amesema Ali bin Twalha kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما, “Al-Muuswirat.” Kwa Maana ya mawingu.¹

Na kama hivyo amesema Ikrima vile vile na Abu Al-'Alia, Adh-Dhahak na Al-Hasan na Ar-Rabi na kauli hii ameichagua Ibnu Jarir رحمه الله تعالى.² Amesema, ‘Faraa’: Nayo ni mawingu ambayo yanajikamua kwa mvua na ambayo hayajaanza kunyesha mvua. Kama ambavyo husemwa mwanamke, “muuswir” utakapokaribia wakati wake wa kutokwa na hedhi na akawa hakutokwa na hedhi hiyo.³

Na maneno haya ni kama Alivyosema Allah تعالى,

اللَّهُ الَّذِي يُرْسِلُ الرِّيحَ فَتُثِيرُ سَحَابًا فَيَبْسُطُهُ فِي السَّمَاءِ كَيْفَ يَشَاءُ وَيَجْعَلُهُ كِسْفًا
فَتَرَى الْوَدَّاقَ يَخْرُجُ مِنْ خَلِيلِهِ ۗ

“Mwenyezi Mungu Ndiye Anayezituma pepo zikayatimua mawingu, kisha Akayatandaza mbinguni kama Apendavyo. Na Akayafanya mapande mapande, basi ukaiona mvua inatoka ndani yake...” (30:48).

Kwa Maana: Katikati Yake.

¹ At-Tabari 24:154.

² At-Tabari 24:153, 154, na Al-Baghawi 4:437.

³ Al-Baghawi 4:437.

Kauli Yake Allah تعالیٰ:

مَاءٌ حَاجًا ﴿١٠﴾

“Maji yanayoanguka kwa kasi kutoka mawinguni.”

Amesema Mujahid na Qatadah na Ar-Rabi bin Anasi kuwa, “*Thajjaj*” yenye ‘kumiminika.’¹ Na amesema Ath-Thauri رحمه الله تعالى yenye ‘kufuatana’² na amesema Ibnu Zaid ‘nyingi.’³ Imekuja katika Hadithi ya mwanamke mwenye damu ya ugonjwa wakati alipomuambia Mtume ﷺ,

«أَنْتُ لَكَ الْكُرْسُفُ»

“Ninakueleza kuhusu pamba.”

Anakusudia uingize pamba mahali hapo. Akasema, ‘Ewe, Mtume, Damu ni nyingi kuliko, hivyo si vyengine inamiminika sana.’ Ndani ya maneno haya pana dalili juu ya kutumiwa kwa tamko, “*Thajjaj*”⁴ katika kumiminika kwenye kufuatana. Na Allah تعالیٰ Ndie Mjuzi sana.

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

لِنُخْرِجَ بِهِ حَبًّا وَنَبَاتًا ﴿١١﴾ وَجَنَّاتٍ أَلْفَافًا ﴿١٢﴾

“Ili Tutoe kwayo nafaka na mimea, na mabustani yenye miti iliyokamatana.”

Maana yake: Ili Tuoteshe kwa maji haya mengi mazuri yenye manufaa yenye kubarikiwa.

حَبًّا

“nafaka.”

Ambazo huhifadhiwa kwa ajili ya watu na wanyama

وَنَبَاتًا ﴿١٣﴾

“Na mimea.” Maana: Mimea inayoliwa hali ya kuwa mibichi.

¹ At-Tabari 24:155.

² At-Tabari 24:155.

³ At-Tabari 24:155.

⁴ Abu Dawud 1:199.

وَجَنَّتٍ

“Na mabustani.”

Maana yake: Bustani za matunda mbali mbali na rangi tofauti na ladha na harufu tofauti japokuwa hayo yapo katika eneo moja la ardhi hali ya kuwa yamechanganyika pamoja. Na kwa sababu hiyo amesema:

وَجَنَّتٍ أَلْفَافًا ﴿١٣﴾

“Na mabustani yenye miti iliyokamatana.”

Amesema Ibn Abass رضي الله عنهما na wengineo, maneno haya, “Alfaf’ Yaani iliyokusanyika pamoja.”¹ Ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

وَفِي الْأَرْضِ قِطْعٌ مُتَجَبَّرَاتٌ وَجَنَّاتٌ مِّنْ أَعْنَابٍ وَزُرْعٌ وَنَخِيلٌ صِنَوَانٌ وَعَيْرٌ صِنَوَانٍ
يُسْقَى بِمَاءٍ وَاحِدٍ وَنُفِضَلُ بَعْضُهَا عَلَىٰ بَعْضٍ فِي الْأَكْلِ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ

يَعْقِلُونَ ﴿١٤﴾

“Na katika ardhi vimo vipande vilivyokaribiana, na zipo bustani za mizabibu, na mimea mingine, na mitende yenye kuchipua kwenye shina moja na isiochipua kwenye shina moja, nayo inatiliwa maji yale yale. Na Tunaifanya baadhi yao bora kuliko mengine katika kula. Hakika katika hayo zimo ishara kwa watu wanaotia mambo akilini.” (13:4)

* * *

¹ At-Tabari 24:156.

إِنَّ يَوْمَ الْفَاضِلِ كَانَ مِيقَتَنَا ﴿٧٧﴾ يَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ
 فَتَأْتُونَ أَفْوَاجًا ﴿٧٨﴾ وَفُتِحَتِ السَّمَاءُ فَكَانَتْ أَبْوَابًا ﴿٧٩﴾
 وَسُيِّرَتِ الْجِبَالُ فَكَانَتْ سَرَابًا ﴿٨٠﴾ إِنَّ جَهَنَّمَ كَانَتْ
 مِرْصَادًا ﴿٨١﴾ لِلطَّغْيِينِ مَقَابًا ﴿٨٢﴾ لَيْسِيْنَ فِيهَا أَحْقَابًا ﴿٨٣﴾
 لَا يَذُوقُونَ فِيهَا بَرْدًا وَلَا شَرَابًا ﴿٨٤﴾ إِلَّا حَمِيمًا وَعَسَاقًا
 جِرَاءً وَفَاقًا ﴿٨٥﴾ إِنَّهُمْ كَانُوا لَا يَرْجُونَ حِسَابًا ﴿٨٦﴾
 وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا كِذَابًا ﴿٨٧﴾ وَكُلَّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ
 كِتَابًا ﴿٨٨﴾ فَذُوقُوا فَلَنْ نَزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا ﴿٨٩﴾ إِنَّ
 لِلْمُتَّقِينَ مَفَازًا ﴿٩٠﴾ حَدَائِقَ وَأَعْنَابًا ﴿٩١﴾ وَكَوَاعِبَ أَتْرَابًا ﴿٩٢﴾
 وَكَأْسًا دِهَاقًا ﴿٩٣﴾ لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا كِذَابًا ﴿٩٤﴾
 جِرَاءً مِنْ رَبِّكَ عَطَاءً حِسَابًا ﴿٩٥﴾ رَبِّ السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا الرَّحْمَنِ لَا يَلْجَأُونَ مِنْهُ خِطَابًا ﴿٩٦﴾
 يَوْمَ يَقُومُ الرُّوحُ وَالْمَلَائِكَةُ صَفًّا ﴿٩٧﴾ لَا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ
 أُذِنَ لَهُ مِنَ الرَّحْمَنِ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٩٨﴾ ذَلِكَ الْيَوْمَ الْحَقُّ ﴿٩٩﴾ فَمَنْ
 شَاءَ اتَّخَذْ إِلَىٰ رَبِّهِ مَقَابًا ﴿١٠٠﴾ إِنَّا أَنْذَرْنَاكُمْ عَذَابًا قَرِيبًا
 يَوْمَ يَنْظُرُ الْمَرْءُ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ وَيَقُولُ الْكَافِرُ يَا لَيْتَنِي
 كُنْتُ تُرَابًا ﴿١٠١﴾

إِنَّ يَوْمَ الْفَاضِلِ كَانَ مِيقَتَنَا ﴿٧٧﴾
 يَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ فَتَأْتُونَ
 أَفْوَاجًا ﴿٧٨﴾ وَفُتِحَتِ السَّمَاءُ
 فَكَانَتْ أَبْوَابًا ﴿٧٩﴾ وَسُيِّرَتِ
 الْجِبَالُ فَكَانَتْ سَرَابًا ﴿٨٠﴾ إِنَّ
 جَهَنَّمَ كَانَتْ مِرْصَادًا ﴿٨١﴾
 لِلطَّغْيِينِ مَقَابًا ﴿٨٢﴾ لَيْسِيْنَ
 فِيهَا أَحْقَابًا ﴿٨٣﴾ لَا يَذُوقُونَ
 فِيهَا بَرْدًا وَلَا شَرَابًا ﴿٨٤﴾
 إِلَّا حَمِيمًا وَعَسَاقًا جِرَاءً
 وَفَاقًا ﴿٨٥﴾ إِنَّهُمْ كَانُوا لَا
 يَرْجُونَ حِسَابًا ﴿٨٦﴾ وَكَذَّبُوا
 بِآيَاتِنَا كِذَابًا ﴿٨٧﴾ وَكُلَّ
 شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ كِتَابًا ﴿٨٨﴾
 فَذُوقُوا فَلَنْ نَزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا ﴿٨٩﴾

17. Hakika siku ya uamuzi imewekewa wakati wake.

18. Siku litapopulizwa baragumu, nanyi mtakuja kwa makundi.

19. Na mbingu zitafunguliwa, ziwe milango.

20. Na milima itaondolewa na itakuwa kama sarabi.

21. Hakika Jahannamu inangojea!

22. Kwa walioasi ndio makazi yao,

23. *Wakae humo karne baada ya karne,*
24. *Hawataonja humo chochote kibaridi wala kinywaji,*
25. *Ila maji ya moto sana na usaha,*
26. *Ndio jaza muwafaka.*
27. *Hakika hao hawakuwa wakitaraji kuwa kuna hisabu.*
28. *Na wakikanusha Aya Zetu kwa nguvu.*
29. *Na kila kitu Sisi Tumekidhibiti kwa kukiandika.*
30. *Basi onjeni! Nasi hatutakuzidishieni ila adhabu!*

Kuelezea Siku ya Hukumu na Ufafanuzi wa Yaliyomo Ndani Yake:

Allah تعالى Anasema Akielezea kuhusu siku ya hukumu, hiyo ni siku ya kiyama. Kwamba siku hiyo imewekewa wakati na muda wenye kuhesabika, hapataongezwa katika muda huo na hapatapunguzwa na hawajui wakati wake kwa hakika isipokuwa Allah تعالى kama Alivyosema,

وَمَا نُؤَخِّرُهُ إِلَّا لِأَجَلٍ مَّعْدُودٍ ﴿١٠٤﴾

“Na Sisi hatuiakhirishi ila kwa muda unaohisabiwa.” (11:104)

يَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ فَتَأْتُونَ أَفْوَاجًا ﴿٧١﴾

“Siku litapopulizwa baragumu, nanyi mtakuja kwa makundi.”

Amesema Mujahidi ni makundi makundi.¹ Amesema Ibn Jarir رحمه الله تعالى anakusudia kuwa kila umma utakuja pamoja na mjumbe wake kama Alivyosema Allah تعالى ,

يَوْمَ نَدْعُوا كُلَّ أُنَاسٍ بِإِٰمَنِهِمْ ﴿٧١﴾

“Siku Tutapowaita kila kikundi cha watu kwa mujibu wa Mtume wao...” (17:71)²

¹ At-Tabari 24:158.

² At-Tabari 24:158.

Amepokea Al- Bukhari katika tafsiri ya Kauli Yake,

يَوْمَ يَنْفُخُ فِي الصُّورِ فَتَأْتُونَ أَفْوَاجًا ﴿٧٨﴾

“Siku litapopulizwa baragumu, nanyi mtakuja kwa makundi.”

Kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه amesema, “Amesema Mtume ﷺ,

«مَا بَيْنَ النَّفْخَتَيْنِ أَرْبَعُونَ»

“Kati ya mipulizo miwili ya baragumu kunapita Arubaini,

Masahaba wakauliza, ‘Je, ni siku arubaini?’ Abu Hurayrah رضي الله عنه akakataa. Wakauliza tena, ‘Je ni miezi arubaini?’ Pia akakataa. Wakauliza tena, ‘Je ni miaka arobaini?’ Pia akakataa. Kisha Mtume ﷺ akasema,

«ثُمَّ يُنَزَّلُ اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَيَنْبُتُونَ كَمَا يَنْبُتُ النَّبْتُ، لَيْسَ مِنَ الْإِنْسَانِ شَيْءٌ إِلَّا يَنْلَى، إِلَّا عَظْمًا وَاحِدًا، وَهُوَ عَجْبُ الذَّنْبِ، وَمِنْهُ يُرَكَّبُ الْخَلْقُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

“Baada ya hapo Mwenyezi Mungu Atateremsha toka mbinguni mvua na hapo wanaadamu watachipua kama vile mimea ichipuavyo. Hapana kwa mwanaadamu kitakachobakia baada ya kuzikwa isipokuwa mfupa mmoja tu, nao ni, ‘Ajbu Ddhanab, Mfupa huu upo chini ya mgongo karibu na kiuno, na kutokana na mfupa huo litatengenezwa tena umbo la mwanaadamu siku ya Kiyama.”¹

وَفُتِحَتْ السَّمَاءُ فَكَانَتْ أَبْوَابًا ﴿٧٩﴾

“Na mbingu zitafunguliwa, ziwe milango.”

Maana yake: Zitakuwa njia na mapito ya kuteremka Malaika.

وَسُيِّرَتِ الْجِبَالُ فَكَانَتْ سَرَابًا ﴿٨٠﴾

“Na milima itaondolewa na itakuwa kama sarabi.”

Kwa Kauli Yake Allah تعالى:

¹ Fat’hul Al-Bari 8:558.

وَتَرَى الْجِبَالَ تَحْسِبُهَا جَمِدَةً وَهِيَ تَمُرُّ مَرَّ السَّحَابِ ۗ

“Na unaiona milima imetulia; nayo inakwenda kama mwendo wa mawingu...”

Kwa Kauli Yake Allah تعالى:

وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ الْمَنْفُوشِ ﴿٥﴾

“Na milima itakuwa kama sufi zilizochambuliwa!” (101:5)

Na Amesema hapa:

فَكَانَتْ سَرَابًا ﴿٦﴾

“Itakuwa kama sarabi.”

Maana yake: ‘Panadhanishwa kwa mwenye kutazama kwamba majabali hayo yapo kisha yanaondoka yote hapana kitu wala alama inayoonesha uwepo wa majabali hayo.’

Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَدَسَّلُونَاكَ عَنِ الْجِبَالِ فَقُلْ يَنْسِفُهَا رَبِّي نَسْفًا ﴿٧﴾ فَيَذَرُهَا قَاعًا صَفْصَفًا ﴿٨﴾ لَا تَرَى فِيهَا عِوَجًا وَلَا أَمْتًا ﴿٩﴾

“Na wanakuuliza khabari za milima. Waambie: Mola Wangu Mlezi Ataiwurugavuruga. Na Ataiacha tambarare, uwanda. Hutaona humo mdidimio wala muinuko.” (20:105-107)

Na Amesema Allah تعالى:

وَيَوْمَ نُسَيِّرُ الْجِبَالَ وَتَرَى الْأَرْضَ بَارِزَةً

“Na siku Tutapoiondoa milima na ukaiona ardhi iwazi...” (18:47)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّ جَهَنَّمَ كَانَتْ مِرْصَادًا ﴿١٠﴾

“Hakika Jahannamu inangojea!”

Maana yake: Imewekwa imetayarishwa.

لَلطَّغِينِ مَعَابًا ﴿١٧﴾

“Kwa walio asi”

Nao ni wale wenye kuvuka mpaka wenye kuasi wenye kuwapinga Mitume,

مَعَابًا ﴿١٧﴾

“...ndio makaazi yao,...”

Maana yake: Marejeo mageukio, mafikio na mashukio.

Kwa Kauli Yake Allah تعالى:

لَيْسَ فِيهَا أَحْقَابًا ﴿١٨﴾

“Wakae humo karne baada ya karne...”

Maana yake: Watakaa humo muda mrefu katika zama “*Ahqaba*” ni wingi wa “*Hiqb*” nao ni muda katika zama.

Na amesema Khalid bin Madaan aya hii na Kauli Yake Allah تعالى:

إِلَّا مَا شَاءَ رَبُّكَ ﴿١٩﴾

“...isipokuwa Apendavyo Mola wako Mlezi.” (11:107).

Kwa watu wa *Tawhiid*.¹ Ameyapokea hayo Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Salim. Nilimsikia Al-Hassan akiuliza kuhusu Kauli Yake Allah تعالى:

لَيْسَ فِيهَا أَحْقَابًا ﴿١٨﴾

“Wakae humo karne baada ya karne,...”

Amesema ama *Ahqab* hazina muda isipokuwa ni kuishi milele motoni. Wapo waliosema kwamba “*Hiqb*” ni miaka sabini kila siku moja katika hiyo miaka sabini ni kama miaka elfu kwa hesabu ya duniani.¹ Na amesema Said toka kwa Qatada: Allah تعالى Amesema:

لَيْسَ فِيهَا أَحْقَابًا ﴿١٨﴾

“Wakae humo karne baada ya karne...”

¹ At-Tabari 24:162.

Huu ni muda usiyo na mwisho kila utakapopita muda utakuja muda mwingine baada yake. Na tumeambiwa kwamba, “*Al-Hiqb*” ni miaka thamanini.² Na amesema Al-Rabii Bin Anas,

لَيْشِينَ فِيهَا أَحْقَابًا ﴿٧٨﴾

“Wakae humo karne baada ya karne...”

Hajuwi hesabu ya “*Ahqab*” isipokuwa Allah تعالى Mwenye Kushinda na Mwenye Utukufu na tumeambiwa kwamba “*Hiqb*” moja ni miaka thamanini, na mwaka ni siku mia tatu na sitini. Na siku moja tu ni kama miaka elfu moja katika mnayo hesabu. Mitazamo yote hii miwili ni ya Ibn Jarir رحمه الله تعالى.³

Na Kauli Yake Allah تعالى:

لَا يَذُوقُونَ فِيهَا بَرْدًا وَلَا شَرَابًا ﴿٧٩﴾

“Hawataonja humo chochote kibaridi wala kinywaji.”

Maana yake: Hawatapata ndani ya moto wa Jahannamu baridi ya kupozea nyoyo zao, wala kinywaji kizuri ambacho watajilisha nacho.

Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى:

إِلَّا حَمِيمًا وَغَسَّاقًا ﴿٨٠﴾

“Ila maji ya moto sana na usaha.”

Amesema Abu Aaliyah na vile vile amesema Ar Rabii bin Anas, “Imevuliwa kutoka kwenye barafu, maji ya moto, na kwenye kinywaji cha usaha.”⁴ Ama, “*Hamim*” Ni maji ya moto mno na “*Ghassaq*” ni mkusanyiko wa usaha wa watu wa motoni na jasho lao, machozi yao na majeraha yao. Mkusanyiko huo ni baridi hauwezekani kutokana na ubaridi wake na wala haukabiliki kutokana na uvundo wake. Tunamuomba Allah تعالى Atuepushe na hayo kwa neema Zake na ukarimu Wake. Na Kauli Yake Allah تعالى

¹ At-Tabari 24:162.

² At-Tabari 24:162.

³ At-Tabari 24:162.

⁴ At-Tabari 24:165.

جَزَاءٌ وِفَاقًا ﴿٧٨﴾

"...Ndio jaza muwafaka."

Maana yake: Hili ambalo wamelifikia kutokana na adhabu hizi ni kwa kuafikiana na matendo yao maovu ambayo walikuwa wanayatenda katika dunia. Amesema hayo Mujahid na Qatadah na zaidi yao. Kisha Amesema Allah تعالیٰ,

إِنَّمْ كَانُوا لَا يُرْجُونَ حِسَابًا ﴿٧٩﴾

"...hakika wao walikuwa hawakuwa wanaamini kuwa kuna kuhesabiwa." (78:27)

Maana yake: Hawakuwa wakiitakidi kuwa kuna siku watahesabiwa na watalipwa humo,

وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا كِذَابًا ﴿٨٠﴾

"Kwa hiyo wakazikadhibisha aya Zetu kuzikadhibisha kukubwa sana."

Maana yake: Walikuwa wanakadhibisha hoja za Allah تعالیٰ na dalili Zake juu ya Kuumba Kwake, ambazo wakawa wanazikabili kwa kukadhibisha na kupinga.

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

كِذَابًا ﴿٨١﴾

"Kiddhaba." Maana yake: Kukadhibisha kukubwa sana.

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

وَكُلُّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ كِتَابًا ﴿٨٢﴾

"Na kila kitu Tumekidhibiti kwa Kukiandika."

Maana yake: Tunayajua matendo ya waja wote na Tumeyaandika juu yao, Tutawalipa kutokana na matendo hayo, yakiwa matendo ni mema watalipwa mema na yakiwa maovu watalipwa uovu. Kauli Yake Allah تعالیٰ.

فَذُوقُوا فَلَنْ نَزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا ﴿٨٣﴾

"Onjeni adhabu hatutawaongezea isipokuwa adhabu."

Maana yake: Wataambiwa watu wa motoni lionjeni lile ambalo mumo ndani yake hatutawaongezea isipokuwa adhabu kulingana na matendo yenu. Amesema Qatadah kutoka kwa Abdilah bin Amri amesema, 'Haijashuka kwa watu waovu ya nzito kwa wao kama hii."

فَذُوقُوا فَلَنْ نَزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا ﴿٧٨﴾

"Onjeni adhabu hatutawaongezeeni isipokuwa adhabu."

Kwa hiyo wao watakuwa katika nyongeza ya adhabu milele.¹

إِنَّ لِلْمُتَّقِينَ مَفَازًا ﴿٧٩﴾ حَدَائِقَ وَأَعْنَابًا ﴿٨٠﴾ وَكَوَاعِبَ أَتْرَابًا ﴿٨١﴾ وَكَأْسًا دِهَاقًا ﴿٨٢﴾
لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا كِدًّا بَابًا ﴿٨٣﴾ جَزَاءً مِّن رَّبِّكَ عَطَاءً حِسَابًا ﴿٨٤﴾

31. Hakika wachamungu wanastahiki kufuzu.

32. Mabustani na mizabibu.

33. Na wake waliolingana nao.

34. Na bilauri zilizo jaa.

35. Hawatasikia humo upuuzi wala uwongo.

36. Malipo kutoka kwa Mola Wako Mlezi, kipawa cha kutosha.

Kufuzu Kukubwa ni kwa Wenye Kumcha Mwenyezi Mungu

Allah تعالى Akiwahabarisha watu wema yale Aliyowaandalia wao miongoni mwa utukufu na neema za kudumu. Allah تعالى Amesema,

إِنَّ لِلْمُتَّقِينَ مَفَازًا ﴿٨٥﴾

"Hakika wana wenye kumcha Mwenyezi Mungu mahali pa kufuzu."

Amesema Ibnu Abbas na Adh-Dhahaak mahali pa mapumziko.² Na amesema Mujahid na Qatada wamefuzu wakaokoka na moto.³ Na kauli yenye nguvu hapa ni kauli ya Ibni Abbas رضي الله عنهما kwa sababu Allah تعالى Amesema baada ya hapo,

¹ At-Tabari 24:169.

² At-Tabari 24:170, na Al-Baghawi 4:439.

³ At-Tabari 24:169, 170.

حَدَائِقَ

"Mabustani."

Bustani za mitende na miti mingine,

وَأَعْنَبًا ۝ وَكَوَاعِبَ أَتْرَابًا ۝

"Na mizabibu. Na wanawari waliyo marika."

Maana yake: Wanawake wa peponi waliyo katika rika moja. Amesema Ibnu Abbas na Mujahid na watu wengine رضي الله عنهم:

كَوَاعِبَ

"Kawaib."

Wenye matiti yaliyosimama. Wanakusudia kwamba matiti yao yamesimama hayakuning'inia kwa sababu wao ni wari wenye kuwapenda wanaume wao na wamo katika rika moja.¹ Kama yalivyotangulia maelezo yake katika *Surat Al Waqia*.² Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَكَأْسًا دِهَاقًا ۝

"Na bilauli yenye kujaa kinywani."

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما Imejazwa kujazwa³ kwenye kufuatana. Na amesema Mujahid na Al-Hassan na Qatada na Ibni Zaid,

دِهَاقًا ۝

"Yenye kujaa."

Iliyojazwa.⁴ Na Kauli Yake Allah تعالى:

لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا كِدَابًا ۝

"Hawatasikia humo upuuzi wala kukadhibishana."

¹ At-Tabari 24:170, na *Ad-Durr Al-Manthur* 8:398.

² Angalia juzuu ya tisa, *Tafsiri ya Surat Al-Waqi'ah* (56:37).

³ At-Tabari 24:173.

⁴ At-Tabari 24:172.

Kama Alivyosema:

لَا لَعُوًّا فِيهَا وَلَا تَأْتِيُمُ ﴿١٧﴾

“Hapana upuuzi ndani yake wala kutiana katika madhambi.”

Maana yake: Hamna ndani yake maneno ya upuuzi yasiyo na faida yoyote na hapana madhambi ya uongo, bali hiyo ni nyumba ya amani na yote yaliyomo ndani yake ni yenye kuepukana na upungufu na kasoro yoyote. Kauli Yake,

جَزَاءَ مِّن رَّبِّكَ عَطَاءٌ حِسَابًا ﴿١٨﴾

“Malipo kutoka kwa Mola Wako Mlezi, kipawa chenye kutosha.”

Maana yake: Kwa hayo tuliyoyataja Amewalipa Allah تعالى kwayo na Amelipa hayo kwa fadhila Zake na wema Wake na rehema Yake, *“kipawa chenye kutosha.”* Maana: Kingi. Wanasema waarabu: “Amenipa akanitosheleza.” Maana: “Ametosheleza.” Na katika matumizi ya neno hilo ni Allah تعالى ndio tosha yangu; Maana: “Ananitosheleza.”

رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا الرَّحْمَنُ ۗ لَا يَمْلِكُونَ مِنْهُ خِطَابًا ﴿١٩﴾ يَوْمَ يَقُومُ
الرُّوحُ وَالْمَلَائِكَةُ صَفًّا ۗ لَا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أُذِنَ لَهُ الرَّحْمَنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٢٠﴾ ذَلِكَ
الْيَوْمَ الْحَقُّ ۗ فَمَنْ شَاءَ اتَّخَذْ إِلَىٰ رَبِّهِ مَآبًا ﴿٢١﴾ إِنَّا أَنْذَرْنَاكُمْ عَذَابًا قَرِيبًا يَوْمَ يَنْظُرُ
الْمَرْءُ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ وَيَقُولُ الْكَافِرُ يَلَيْتَنِي كُنْتُ تُرَابًا ﴿٢٢﴾

37. Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilivyo baina yao, Arrahman, Mwingi wa rehema; hawamiliki usemi mbele Yake!

38. Siku atakapo simama Roho na Malaika kwa safu. Hawatasema ila Mwingi wa rehema Aliyemruhusu, na atasema yaliyo sawa tu.

39. Hiyo ndiyo Siku ya haki. Basi anayetaka na ashike njia arejee kwa Mola Wake Mlezi.

40. Hakika Tumekuhadharisheni adhabu iliyo karibu kufika; siku ambayo mtu atakapoona yaliyotangulizwa na mikono yake; na kafiri atasema: Laiti ningelikuwa udongo!

Hatothubutu Mtu Yeyote Kusema Mbele ya Mwenyezi Mungu Hata Malaika, Isipokuwa Baada ya Kuruhusiwa

Anaeleza Allah تعالى kuhusu Ukubwa na Utukufu Wake na kwamba Yeye ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilivyo kati yao na ndani yao, kwamba Yeye ni Mwingi wa Kurehemu Ambaye Rehema Yake imekienea kila kitu.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

لَا يَمْلِكُونَ مِنْهُ خِطَابًا ﴿٣٧﴾

“Hawataweza kwa Mwenyezi Mungu kumsemesha.”

Maana yake: Hatoweza mtu yeyote kuanza kumsemesha, isipokuwa kwa ruhusa Yake. Hii ni kama Kauli ya Allah تعالى:

مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ ﴿٣٨﴾

“Ni nani huyo atakayeomba mbele isipokuwa kwa ruhusa Yake.”
(2:225).

Na ni Kama Kauli Yake Allah تعالى:

يَوْمَ يَأْتِ لَا تَكَلِّمُ نَفْسٌ إِلَّا بِإِذْنِهِ ﴿٣٩﴾

“Siku hiyo itakapofika, hatosema hata mtu mmoja ila kwa idhini Yake Mwenyezi Mungu.” (11:105)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

يَوْمَ يَقُومُ الرُّوحُ وَالْمَلَائِكَةُ صَفًّا ﴿٤٠﴾

“Siku ambayo atasimama Jibril na malaika hali ya kupanga safu.”
(78:38)

Neno *Ruh* hapa linarejea kwa Malaika Jibril عليه السلام. Hayo yamesemwa na Al Shaabi na Saed Bin Jubair na Ad-Dhahaak.¹

Kama Alivyosema Allah تعالى:

¹ At-Tabari 24:176, na Al-Qurtubi 19:186.

عَلَىٰ قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿١٧﴾ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ ﴿١٨﴾

“Alishuka na hii Qur’ani Rouh Mwaminifu, juu ya moyo wako ili uwe katika wenye kukhofisha.” (26:193-194)

Na amesema Muqatil bin Hayaan kuwa *Ar-Ruuh* ni malaika mwenye hadhi tukufu zaidi na ndie aliye karibu zaidi na Allah تعالى na ndie mshusha wahyi.¹ Kuhusu Kauli Yake Allah تعالى:

إِلَّا مَنْ أَدْرَأَهُ الرَّحْمَنُ

“Isipokuwa yule aliyeruhusiwa na Mwenyez Mungu Mwenye Huruma sana.”

Kama Alivyosema:

يَوْمَ يَأْتِ لَا تَكَلِّمُ نَفْسٌ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۗ

“Siku hiyo itakapofika, hatosema hata mtu mmoja ila kwa Idhini Yake Mwenyezi Mungu.” (11:105)

Na kama ilivyothibiti katika sahihi,

وَلَا يَتَكَلَّمُ يَوْمَئِذٍ إِلَّا الرُّسُلُ ۗ

“Wala hawatasema siku hiyo ila Mitume tu.”²

Ama Kauli Yake:

وَقَالَ صَوَابًا ﴿٢٤﴾

“Na akasema ukweli.”

Maana yake: Ukweli na katika haki ni tamko la *“Laa ilaaha illallah”* kama alivyosema Abuu Swaleh na Ikrima.³ Na Kauli Yake Allah تعالى

ذَٰلِكَ أَلْيَوْمَ الْحَقُّ ط

“Hiyo ndiyo siku ambayo itakuwa haina budi ni kweli.”

Itatokea tu na haikwepeki.

¹ *Ad-Durr Al-Manthur* 8:400.

² *Fat’hul Al-Bari* 13:430.

³ *At-Tabari* 24:178.

فَمَنْ شَاءَ اتَّخَذْ إِلَىٰ رَبِّهِ مَآبًا ﴿٧٨﴾

“Basi anayetaka na ashike njia arejee kwa Mola Wake Mlezi.”

Maana yake: Marejeo na njia ambayo ataongoka kuelekea Kwake na utaratibu ambao atapitia kuelekea Kwake.

Qiyama Kiko Karibu:

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّا أَنْذَرْنَاكُمْ عَذَابًا قَرِيبًا

“Kwa hakika sisi Tumewahofisheni adhabu iliyo karibu.”

Anakusudia siku ya Qiyama kwa kukokoteza kutokea kwake. Imekuwa siku hiyo karibu kwa sababu kila chenye kuja kipo karibu,

يَوْمَ يَنْظُرُ الْمَرْءُ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ

“Siku ambayo ataona kila mtu yale yaliyotangulizwa na mikono yake.”

Maana yake: Yataoneshwa kwake matendo yake yote miongoni mwa kheri na shari ya zamani na ya sasa. Kama Alivyosema Allah تعالى,

وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا

“Ataelezwa mtu siku hiyo yale aliyoyatanguliza na yale aliyoyachelewesha.” (18:49)

Kama Kauli Yake Allah تعالى:

يُنَبِّئُوا الْإِنْسَانَ بِوَمَعِدِ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ ﴿٧٩﴾

“Siku hiyo ataambiwa aliyoyatanguliza na aliyoyaakhirisha.” (75:13)

وَيَقُولُ الْكَافِرُ يُلَيْتَنِي كُنْتُ تُرَابًا ﴿٨٠﴾

“Atasema kafiri najitamania ningekuwa mchanga.”

Maana yake: Atatamania kafiri siku hiyo angekuwa katika nyumba za Dunia ni mchanga na asingekuwa ameumbwa na kutokea katika ulimwengu. Atatamani

hayo wakati atakapoona kwa macho yake adhabu ya Allah تعالی na akayaona matendo yake maovu yameandikwa dhidi yake kwa mikono ya malaika wajumbe watukufu wema. Na pamesemwa hakika si vingine atayatamani hayo wakati atakapohukumu Allah تعالی wanyama ambao walikuwa Duniani. Atahukumu kati yao kwa hukumu Yake ya Uadilifu ambayo haidhulumu. Na husemwa kwamba Kafiri atatamani hali hiyo, pale atakapoona kisasi cha mnyama asiyekuwa na pembe kulipiza kwa mwenye pembe. Atakapomaliza katika Kuwahukumu Atawaambia kuweni mchanga kwa hiyo watakuwa mchanga. Wakati huo atasema kafiri,

يَلِيَّتِي كُنْتُ تُرَابًا ﴿٣٧﴾

“Ee najitania ningekuwa mchanga.”

Maana yake: Ningekuwa mnyama nikarejea kwenye mchanga. Yamekuja Maana ya Maelezo haya katika hadithi ya Baragumu inayojulikana. Na yamekuja kuhusiana na hilo maelezo kutoka kwa Abu Huraira na Abdillahi Bin Amr na wengine رضي الله عنهم.

Huu ni Mwisho wa Tafsiri ya *Surat Annaba*. Na sifa Njema ni za Allah تعالی na Kwake tu Kuwezesha na Kuhifadhiwa.

* * *

Tafsiri ya Suratun Nazi'at

Sura ya 79

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُوْرَةُ النَّازِعَاتِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالنَّازِعَاتِ غَرْقًا ۝ وَالنَّشِيطَاتِ نَشْطًا ۝ وَالسَّيِّحَاتِ

سَبْحًا ۝ فَالْمُدَبِّرَاتِ أَمْرًا ۝ فَالْمُدَبِّرَاتِ أَمْرًا ۝

يَوْمَ تَرْجُفُ الرَّاجِفَةُ ۝ تَتَّبِعُنَّ الرَّادِفَةَ ۝ قُلُوبٌ

يَوْمِئِذٍ وَاجِفَةٌ ۝ أَبْصُرُهَا خَشِيعَةٌ ۝ يَقُولُونَ أَيْنَا

لَمَرْدُودُونَ فِي الْحَافِرَةِ ۝ أَيْدَا كُنَّا عِظْمًا نَجْرَةً ۝

قَالُوا تِلْكَ إِذًا كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ ۝ فإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ

۝ فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ۝ هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ مُوسَىٰ

۝ إِذْ نَادَاهُ رَبُّهُ بِاللَّوَادِ الْأَقْدَاسِ طُوى ۝ أَذْهَبَ

إِلَىٰ قِرْعَوْنَ إِنَّهُ طَغَىٰ ۝ فَقلْ هَلْ لَكَ إِلَٰهٌ إِلَّا أَن تَرْكَبُنَا

وَأَهْدِيكَ إِلَىٰ رَبِّكَ فَتَخْشَىٰ ۝ فَأَرْسَلْنَا إِلَيْكَ الْكُتُبَ ۝

فَكَذَّبَ وَعَصَىٰ ۝ ثُمَّ أَدْبَرَ يَسْعَىٰ ۝ فَحَشَرَ فَنَادَىٰ

۝ فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَىٰ ۝ فَأَحْذَهُ اللَّهُ نَكَالَ

الْآخِرَةِ وَالْأُولَىٰ ۝ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَعِبْرَةً لِّمَن يَخْشَىٰ ۝

وَالنَّازِعَاتِ غَرْقًا ۝ وَالنَّشِيطَاتِ

نَشْطًا ۝ وَالسَّيِّحَاتِ سَبْحًا ۝

فَالْمُدَبِّرَاتِ أَمْرًا ۝ فَالْمُدَبِّرَاتِ

أَمْرًا ۝ يَوْمَ تَرْجُفُ الرَّاجِفَةُ ۝

تَتَّبِعُنَّ الرَّادِفَةَ ۝ قُلُوبٌ

وَاجِفَةٌ ۝ أَبْصُرُهَا خَشِيعَةٌ ۝

يَقُولُونَ أَيْنَا لَمَرْدُودُونَ فِي الْحَافِرَةِ

۝ أَيْدَا كُنَّا عِظْمًا نَجْرَةً ۝

قَالُوا تِلْكَ إِذًا كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ ۝

1. Naapa kwa wanaochomoa kwa guvu.

2. Na kwa wanaotoa kwa upole.

3. Na wanaoogelea.

4. Wakishindana mbio.

5. Wakidabiri mambo.

6. Siku kitapotetemeka cha kutetemeka.

7. Kifuate cha kufuatia.

8. Siku hiyo nyoyo zitapigapiga.

9. Macho yatainama chini.

10. Sasa wanasema: Ati kweli tutarudishwa kwenye hali ya kwanza?

11. Hata tukiwa mifupa iliyobunguliwa?

12. Wanasema: Basi marejeo hayo ni yenye khasara!

13. Kwa hakika huo ni ukelele mmoja tu,

14. Mara watakuwa kwenye uwanda wa mkutano!

Kuapiwa kwa Sifa Tano Juu ya Uwepo wa Siku ya Qiyama

Ibnu Mas'ud, Ibnu Abbas, Masruq, Said bin Jubair, Abu Swaleh, Abu Adh-Dhuha na Al-Ssudiy رضي الله عنهم wamesema:

وَالنَّزَعَتِ عَرْقًا

“Naapa kwa wanaochomoa kwa nguvu.”

Wakimaanisha Malaika wakati wa kuzitoa roho za wanadamu.¹ Katika wao kuna wale ambao wanaochukua roho ya mwanadamu kwa nguvu. Wanapitiliza, wanaopitiliza katika kuing'oa kwake. Na katika wao kuna yule ambaye anaichukua roho ya mwanadamu kwa wepesi kana kwamba wameifungua kutoka katika fundo. Na hiyo ndiyo Kauli Yake:

وَالنَّشِطَتِ نَشْطًا

“Na kwa wanaotoa kwa upole.”

Ameyasema hayo Ibnu Abbas رضي الله عنهما.² Na ama Kauli Yake Allah تعالى:

وَالسَّيْحَتِ سَيْحًا

“Na wanaoogelea”

¹ At-Tabari 24:185 na Al-Qurtubi 19:190 na Ad-Durr Al-Manthur 8:404.

² At-Tabari 24:178.

Ibnu Mas'ud رضي الله عنهما amesema hao ni malaika.¹ Na pamepokewa kutoka kwa Ali, Mujahid, Abu Swaleh na Said bin Jubair رضي الله عنهم mfano wa hayo.²

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَالسَّيِّئَاتِ سَبَقًا ﴿١﴾

“Wakishindana mbio.”

Pamepokewa kutoka kwa Ali, Masrouq, Mujahid, Abu Swaleh, Al-Hassan Al-Basry رضي الله عنهم kuwa anakusudia Malaika³. Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَالْمُدَبِّرَاتِ أَمْرًا ﴿٢﴾

“Wakidabiri mambo.”

Amesema Ali, Mujahid, Atwa, Abu Swaleh, Al-Hassan, Qatada, Al-Rabi bin Anas na Al-Ssudi kuwa hao ni Malaika.⁴ Ameongeza Al-Hasan, “Wanayapanga mambo kutoka mbinguni kuja ardhini yaani kwa amri ya Bwana wao Mwenye Kushinda, Mwenye Utukufu.

Maelezo ya Qiyama, Sifa za Watu Wake na Maneno Yao ndani Yake.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

يَوْمَ تَرُجُّفُ الرَّاحِفَةُ ﴿٣﴾ تَتَّبِعُهَا الرَّاادِفَةُ ﴿٤﴾

“Siku kitapotetemeka cha kutetemeka, kifuate cha kufuatia.”

Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema hiyo ni mipulizo miwili wa kwanza na wa pili.⁵ Na kama hivyo amesema Mujahid, Al-Hassan, Qatada, Adh-Dhahaak na wengine.⁶ Imepokewa kutoka kwa Mujahid kuwa, ama mpulizo wa kwanza nao ni Kauli Yake Allah تعالى:

¹ Ad-Durr Al-Manthur 8:404.

² At-Tabari 24:190 na Al-Qurtubi 19:193.

³ Al-Qurtubi 19:93 na Ad-Durr Al-Manthur 8:404.

⁴ At-Tabari 24:190 na Al-Qurtubi:19:194 na Ad-Durr Al-Manthur 8:403-405.

⁵ At-Tabari 24:190.

⁶ At-Tabari 24:191,192.

يَوْمَ تَرْجُفُ الرَّاجِفَةُ ﴿٧٣﴾

“Siku kitapotetemeka cha kutetemeka.”

Kauli hiyo ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

يَوْمَ تَرْجُفُ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ

“Siku itakapotetemeka ardhi na majabali.” (73:14)

Na mpulizo wa pili ni ule wenye kuufuatia huo nao ni kama isemavyo Kauli Yake Allah تعالى:

وَحُمِلَتِ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ فَدُكَّتَا دَكَّةً وَاحِدَةً ﴿٦٩﴾

“Na ardhi na milima ikaondolewa, na ikavunjwa kwa mvunjo mmoja.” (69:14)¹

Na Kauli Yake Allah تعالى,

أَبْصَرُهَا يَوْمَئِذٍ وَاحِفَةً ﴿٧٩﴾

“Siku hiyo nyoyo zitapigapiga...”

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما anakusudia ni zenye kuogopa.² Na kama hivyo amesema Mujahid na Qatada.³

أَبْصَرُهَا حَسِيعَةً ﴿٨١﴾

“Macho yatainama chini.”

Maana yake: Macho ya wenye nyoyo hizo. Yamehusishwa macho na nyoyo kwa sababu ya kuhusiana. Maana: ‘Ni manyonge yakiwa duni, kutokana na yale ambayo yameyaona miongoni mwa vitisho.’ Na Kauli Yake Allah تعالى,

يَقُولُونَ أَءِنَّا لَمَرْدُودُونَ فِي الْحَافِرَةِ ﴿٨٤﴾

“Sasa wanasema: Ati kweli tutarudishwa kwenye hali ya kwanza?”

¹ At-Tabari 24:192.

² At-Tabari 24:193.

³ At-Tabari 24:193 na Al-Baghawi 4:443.

Anawakusudia washirikina wa Kikureishi wanaosema kama wanavyosema katika kupinga kwao marejeo. Kufufuliwa (Akhera) wanaona kuwa ni jambo ambalo haliwezekani baada ya kuwa kwao makaburini. Ameyasema hayo Mujahid.¹ Na baada ya kuchanika chanika viwiliwili vyao na kutawanyika mifupa yao na kuchakaa. Kwa sababu hiyo wamesema,

أءَذَا كُنَّا عِظْمًا خِزَّةً ﴿١١﴾

“Hivi tutakapokuwa mifupa iliyochakaa?”

Na imesomwa,

(نَاخِرَةً)

(Na-khira).

bnu Abbas, Mujahid na Qatada رضي الله عنهم wamesema: Maana yake: “Iliyooza iliyochakaa.”²

Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema : Huo ni mfupa pindi unapochakaa na ukaingia upepo ndani yake. Ama kauli yao:

قَالُوا تِلْكَ إِذًا كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ ﴿١٢﴾

“Huko wakati huo ni kurejea kwenye hasara.” (79:12).

Muhammad bin Kaab amesema kuwa, Makureishi wamesema, ‘Iwapo Atatufufua Allah تعالى baada ya kufa kwa hakika tutapata hasara.”³

Allah تعالى Amesema:

فَأِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿١٣﴾ فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿١٤﴾

“Kwa hakika huo ni ukelele mmoja tu. Mara watakuwa kwenye uwanda wa mkutano!”

Maana yake: Kwa hakika hii ni amri ya Allah تعالى hapana shaka juu yake. Kitakachotokea hapo ni kuwa wakati watu wakiwa katika taharuki

¹ At-Tabari 24:195.

² At-Tabari 24:195.

³ Al-Qurtubi 19:198.

wamesimama wakiwa wanaangalia, Ghafila Allah تعالی Atamuamrisha malaika wake Israfil kupuliza parapanda, nae atapuliza mpulizo wa ufufuo, hapo watu wote; wa mwanzo na wa mwisho, watakuwa wamesimama mbele ya Mola Mlezi Mwenye Kushinda na Kutukuka hali ya kuwa wanaangalia.

Kama ilivyosema Kauli Yake Allah تعالی:

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ وَتَظُنُّونَ إِن لَّبِئْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٥٢﴾

“Siku Atakapokuiteni, na nyinyi mkamuitikia kwa kumshukuru, na mkadhani kuwa hamkukaa ila muda mdogo tu.” (17:52)

Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَّمَجِّ بِالْبَصَرِ ﴿٥٤﴾

“Na Amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.” (54:50)

Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَمَا أَمْرُ السَّاعَةِ إِلَّا كَلَّمَجِّ الْبَصَرِ أَوْ هُوَ أَقْرَبُ ﴿٧٧﴾

“Wala halikuwa jambo la Saa (ya Kiyama) ila kama kupepesa kwa jicho, au akali ya hivyo...” (16:77),

فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿٧٩﴾

“Kwa hakika hayo ni ukelele mmoja tu...”.

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما, “Sahira” ni ardhi yote.¹ Na kama hivyo amesema Said bin Jubair, Qatada, Abu Swaleh na amesema Ikrima, Hassan na Adh-Dhahak na Ibnu Zaid, “Assahira” ni uso wa ardhi.² Amesema Mujahid walikuwa chini yake wakatolewa kuletwa juu yake. Amesema, “Sahira” ni mahali palipo tambarare.³

¹ At-Tabari 24:198.

² At-Tabari 24:198.

³ At-Tabari 24:198 na Ad-Durr Al-Manthur 8:408.

Na amesema Ar-Rabi bin Anas,

فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿٧٩﴾

“Kwa hakika hayo ni ukelele mmoja tu.”

Kauli Yake Allah تعالى:

يَوْمَ تُبَدَّلُ الْأَرْضُ غَيْرَ الْأَرْضِ وَالسَّمَوَاتُ ۗ وَرَزَوُا لِلَّهِ الْوَحِيدِ الْقَهَّارِ ﴿١٤﴾

“Siku itapogeuzwa ardhi iwe ardhi nyengine, na mbingu pia. Nao watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu Mmoja, Mwenye Nguvu.” (14:48)

Kauli Yake Allah تعالى:

وَسَتَلُونَكُمْ عَنِ الْجِبَالِ فَقُلْ يَنْسِفُهَا رَبِّي نَسْفًا ﴿١٠٦﴾ فَيَذَرُهَا قَاعًا صَفْصَفًا ﴿١٠٧﴾ لَا تَرَى فِيهَا عِوَجًا وَلَا أَمْتًا ﴿١٠٨﴾

“Na wanakuuliza khabari za milima. Waambie: Mola Wangu Mlezi Ataiwurugavuruga. Na Ataiacha tambarare, uwanda. Hutaona humo mdidimio wala muinuko.” (20:105-107)

Kauli Yake Allah تعالى:

وَيَوْمَ نُسَيِّرُ الْجِبَالَ وَتَرَى الْأَرْضَ بَارِزَةً

“Na siku Tutapoiondoa milima na ukaiona ardhi iwazi, na Tukawafufua...” (18:47)

Na itaonekana ardhi ambayo juu yake palikuwa na majabali. Na ardhi hizo haihesabiwi kuwa ni ardhi hii. Hiyo ni ardhi ambayo hayakufanywa juu yake makosa yoyote na haikumwagwa juu yake damu.

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ مُوسَى ﴿٦١﴾ إِذْ نَادَاهُ رَبُّهُ بِالْوَادِ الْأَقْدَسِ طُوًى ﴿٦٢﴾ أَذْهَبَ إِلَى فِرْعَوْنَ
 إِنَّهُ طَغَى ﴿٦٣﴾ فَقُلْ هَلْ لَكَ إِلَى أَنْ تَزَكَّى ﴿٦٤﴾ وَأَهْدِيكَ إِلَى رَبِّكَ فَتَخْشَى ﴿٦٥﴾ فَأَرَاهُ الْآيَةَ
 الْكُبْرَى ﴿٦٦﴾ فَكَذَّبَ وَعَصَى ﴿٦٧﴾ ثُمَّ أَدْبَرَ يَسْعَى ﴿٦٨﴾ فَحَشَرَ فَنَادَى ﴿٦٩﴾ فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ
 الْأَعْلَى ﴿٧٠﴾ فَأَخَذَهُ اللَّهُ نَكَالَ الْآخِرَةِ وَالْأُولَى ﴿٧١﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِمَنْ يَخْشَى ﴿٧٢﴾

15. *Je! Imekufikia hadithi ya Musa?*
16. *Mola Wake Mlezi alipomuita katika bonde takatifu la T'uwaa, Akamuambia:*
17. *Nenda kwa Firauni. Hakika yeye amezidi jeuri.*
18. *Umuambie: Je! Unapenda kujitakasa?*
19. *Nami nitakuongoa ufike kwa Mola Wako Mlezi, upate kumcha.*
20. *Basi alimuonesha Ishara kubwa.*
21. *Lakini alikadhibisha na akaasi.*
22. *Kisha alirudi nyuma, akaingia kufanya juhudi.*
23. *Akakusanya watu akanadi.*
24. *Akasema: Mimi ndiye mola wenu mlezi mkuu kabisa.*
25. *Basi hapo Mwenyezi Mungu Akamshika Kumuadhibu kwa la mwisho na la mwanzo.*
26. *Kwa hakika katika haya yapo mazingatio kwa wanaoogopa.*

Kutajwa kwa Kisa cha Musa عليه السلام na Kwamba Kisa Hicho ni Mazingatio kwa Mwenye Kumuogopa cha Mwenyezi Mungu:

Anamueleza Allah تعالى, Mtume ﷺ kuhusu Mja Wake na Mjumbe Wake Musa عليه السلام kwamba Yeye Alimtuma kwa Firauni na Akamtia nguvu kwa miujiza na pamoja na hayo Firauni aliendelea juu ya ukafiri wake na kuvuka kwake mipaka hadi pale Mwenyezi Mungu Alipomkamata kwa kamato la Mwenye Kushinda, Mwenye Uwezo Mkubwa. Na hivyo hivyo utakuwa mwisho wa wale watakaokupinga na wakakadhibisha yale uliyokuja nayo. Na kwa sababu hiyo Amesema mwishoni mwa kisa,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِّمَن يَخْشَى ﴿٧٩﴾

“Kwa hakika katika haya yapo mazingatio kwa wanaoogopa.”

Kauli Yake Allah تعالى:

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ مُوسَى ﴿٧٩﴾

“Je! Imekufikia hadithi ya Musa?”

Maana yake: "Jee umeisikia habari yake?"

إِذْ نَادَاهُ رَبُّهُ

"Mola Wake Mlezi Alipomuita."

Maana yake: Alimsemesha kwa kumuita,

بِالْوَادِ الْمُقَدَّسِ

"katika bonde takatifu."

Maana yake: Lenye kutakaswa,

طُوًى

"Tuwaa" Ni jina la jangwa, juu ya kauli sahihi kama yalivyotangulia maelezo haya katika *Surat Twaha*. Akamuambia,

أَذْهَبَ إِلَى فِرْعَوْنَ إِنَّهُ طَغَى

"Nenda kwa Firauni. Hakika yeye amezidi jeuri."

Maana yake: Amejifanya jabari, ameasi na ametakabari,

فَقُلْ هَلْ لَكَ إِلَهٌ إِلَّا أَنْ تَرْكَبُوا

"Umuambie: Je! Unapenda kujitakasa?"

Maana yake: Muambie jee uko tayari kuitika kuelekea kwenye njia ambayo kwayo utatakasika. Maana: "Utasalimika na utatii?"

وَأَهْدِيكَ إِلَى رَبِّكَ

"Nami nitakuongoa ufike kwa Mola Wako Mlezi,..."

Maana yake: "Nikuoneshe kwenye kumuabudu Bwana Wako."

فَتَخَشَى

"Upate kumcha." Maana yake: "Ili moyo wako uwe ni wenye kunyenyekea Kwake, wenye Kumtii, wenye Kumuogopa baada ya kuwa ulikuwa mgumu, muovu, uko mbali na kheri.

فَأَرْنَهُ الْآيَةَ الْكُبْرَى ﴿٧٩﴾

“Basi alimuonesha Ishara kubwa.”

Anakusudia kuwa Alimdhahirishia Musa عليه السلام baada ya wito huu wa ukweli wa hoja yenye nguvu na dalili iliyo wazi juu ya ukweli wa ule ambalo amekuja nalo, kutoka kwa Allah تعالى.

فَكَذَّبَ وَعَصَى ﴿٨٠﴾

“Lakini aliikadhibisha na akaasi...”

Maana yake: Akaukadhibisha ukweli na akayapinga yale aliyomuamrisha kwayo miongoni mwa kumtii Allah تعالى. Matokeo yake ni kwamba ulikufuru moyo wake na hakuathirika na wito wa Musa عليه السلام kwa siri na dhahiri yake. Na Musa عليه السلام akamfahamisha kwamba yale aliyokuja nayo ni ukweli, na wala hailazimu kuamini ukweli huo. Kwa sababu maarifa ni elimu ya moyo, na kuamini ni matendo yake, nako ni kufuata ukweli na kuunyenyeka.

Na Kauli Yake Allah تعالى,

ثُمَّ أَدْبَرَ يَسْعَى ﴿٨١﴾

“Kisha alirudi nyuma, akaingia kufanya juhudi.”

Maana yake: Katika kupinga haki kuikumbatia batili nako ni kuwakusanya wachawi ili wakabiliane na yale ambayo amekuja nayo Musa عليه السلام miongoni mwa miujiza ya wazi.

فَحَشَرَ فَنَادَى ﴿٨٢﴾

“Akakusanya watu akanadi.”

Maana yake: Katika watu wake.

فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَى ﴿٨٣﴾

“Akasema: Mimi ndiye mola wenu mlezi mkuu kabisa.”

Amesema Ibnu Abbas na Mujahid kuwa tamko hili amelisema Firauni baada ya kauli yake.

مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرِي

“Sijui kama mnaye mungu asiyekuwa mimi.” (28:38)

Kwa muda wa miaka arubaini.¹ Allah تعالى Amesema:

فَأَحَدَهُ اللَّهُ نَكَالَ الْأَخِرَةِ وَالْأُولَى ﴿٧٩﴾

“Basi hapo Mwenyezi Mungu Akamshika Kumuadhibu kwa la mwisho na la mwanzo.”

Maana yake: Allah تعالى Alimlipiza kwa kisasi kikali na Akamfanya awe mfano kwa waovu duniani walio kama yeye.

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ بِئْسَ الرِّفْدُ الْمَرْفُودُ

“Nao wamefuatishiwa laana hapa duniani na Siku ya Kiyama. Ni mabaya yalioje watakayo pewa!” (11:99)

Kama Allah تعالى Alivyosema,

وَجَعَلْنَاهُمْ أَيْمَةً يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ لَا يُنصَرُونَ ﴿٢٨﴾

“Na Tuliwafanya ni waongozi waitao kwenye Moto. Na Siku ya Kiyama hawatanusuriwa.” (28:41).

Allah تعالى Akasema,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِّمَن تَخْشَى ﴿٨٠﴾

“Kwa hakika katika haya yapo mazingatio kwa wanaoogopa.”

Maana yake: ‘Kwa wenye kuonyeka na wenye kukatazika’.

* * *

¹ Al-Qurtubi 19:202.

ءَأَنْتُمْ أَشَدُّ خَلْقًا أَمِ السَّمَاءُ بَنَّا ۖ ۝٧ رَفَعَ سَمَكَهَا
 فَسَوَّيْنَاهَا ۝٨ وَأَغْطَشَ لَيْلَهَا وَأَخْرَجَ ضُحَاهَا ۝٩
 وَالْأَرْضَ بَعْدَ ذَلِكَ دَحَاهَا ۝١٠ أَخْرَجَ مِنْهَا مَاءَهَا
 وَمَرْعَاهَا ۝١١ وَالْجِبَالَ أَرْسَاهَا ۝١٢ مَتَاعًا لَكُمْ
 وَلِاتِّعِمِكُمْ ۝١٣ فَإِذَا جَاءَتِ الطَّامَةُ الْكُبْرَى ۝١٤ يَوْمَ
 يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ مَا سَعَى ۝١٥ وَبُرِزَتِ الْجَحِيمُ لِمَنْ يَرَى
 ۝١٦ فَأَمَّا مَنْ طَفَى ۝١٧ وَءَاثَرَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ۝١٨ فَإِنَّ
 الْجَحِيمَ هِيَ الْمَأْوَى ۝١٩ وَأَمَّا مَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ
 وَنَهَى النَّفْسَ عَنِ الْهَوَى ۝٢٠ فَإِنَّ الْجَنَّةَ هِيَ الْمَأْوَى ۝٢١
 ۝٢٢ يَسْأَلُونَكَ عَنِ السَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسِلُهَا ۝٢٣ فِيمَ أَنْتَ
 مِنْ ذِكْرِهَا ۝٢٤ إِلَىٰ رَبِّكَ مُنْتَهَاهَا ۝٢٥ إِنَّمَا أَنْتَ مُنذِرٌ
 مَنْ يَخْشَاهَا ۝٢٦ كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبَثُوا إِلَّا عَشِيَّةً أَوْ
 ضُحَاهَا ۝٢٧

ءَأَنْتُمْ أَشَدُّ خَلْقًا أَمِ السَّمَاءُ بَنَّا ۖ ۝٧ رَفَعَ سَمَكَهَا فَسَوَّيْنَاهَا ۝٨
 وَأَغْطَشَ لَيْلَهَا وَأَخْرَجَ ضُحَاهَا ۝٩ وَالْأَرْضَ بَعْدَ ذَلِكَ دَحَاهَا ۝١٠
 أَخْرَجَ مِنْهَا مَاءَهَا وَمَرْعَاهَا ۝١١ وَالْجِبَالَ أَرْسَاهَا ۝١٢ مَتَاعًا لَكُمْ
 وَلِاتِّعِمِكُمْ ۝١٣

27. Je! Ni vigumu zaidi kukuumbeni nyinyi au mbingu? Yeye ndiye Aliye-ijenga!

28. Akainua kimo chake, na Akaitengeneza vizuri.

29. Na Akautia giza usiku wake, na Akautokeza mchana wake.

30. Na juu ya hivyo Ameitandaza ardhi.

31. Akatoa ndani yake maji yake na malisho yake.

32. Na milima Akaisimamisha.

33. Kwa nafuu yenu na mifugo yenu.

Kuumbwa kwa Mbingu na Ardhi ni Kugumu Zaidi kuliko Kurejeshwa tena Viumbe

Allah تعالى Amesema hali akitoa hoja juu ya wale wanaokanusha kufufuliwa katika kuumba viumbe tena baada ya uumbaji wa kwanza.

ءَأَنْتُمْ

“Je, nyinyi?” Enyi watu,

أَشَدُّ خَلْقًا أَمِ السَّمَاءِ

“Ni vigumu zaidi Kukuumbeni nyinyi au mbingu?”

Anakusudia kwamba mbingu ni imara sana na ngumu kwa umbile kuliko nyinyi. Kama Allah تعالى Alivyosema,

لَخَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ

“Bila ya shaka Kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko Kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui”(40:57),

Ameyatafsiri maneno hayo kwa Kauli Yake Allah تعالى,

أَوَلَيْسَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۚ بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلَّاقُ

الْعَلِيمُ ﴿٥٨﴾

“Kwani Aliyeziumba mbingu na ardhi hawezi Kuwaumba mfano wao? Kwani! Naye Ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi.”(36:81)

Kauli Yake Allah تعالى,

بَنَيْهَا ﴿٥٩﴾

“...Yeye Ndiye Aliyeijenga.”

Amefasiri hilo kwa Kauli Yake,

رَفَعَ سَمَكَهَا فَسَوَّاهَا ﴿٦٠﴾

“Akainua kimo chake, na Akaitengeneza vizuri.”

Maana yake: Amelifanya ni la juu jengo lake, liko mbali eneo lake, zimelingana sawa pande zake, zimepambwa kwa nyota katika usiku wenye kiza.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَغْطَشَ لَيْلَهَا وَأَخْرَجَ ضُحَاهَا ﴿٧٩﴾

“Na Akautia giza usiku wake, na Akautokeza mchana wake.”

Maana: ‘Ameufanya usiku wake ni wenye kiza cheusi totoro na mchana wake unaangaza na uko wazi sana.’ Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما ‘Ameufunika usiku wake’¹ na kama hivyo amesema Mujahid, Ikrima, Said bin Jubair na watu wengine wengi²

وَأَخْرَجَ ضُحَاهَا ﴿٨٠﴾

“na Akautokeza mchana wake.”

Kwa maana: Ameutia mwangaza mchana wake. Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَالْأَرْضَ بَعْدَ ذَلِكَ دَحَاهَا ﴿٨١﴾

“Na juu ya hivyo Ameitandaza ardhi.”

Ameyatafsiri maneno hayo kwa Kauli Yake Allah تعالى,

أَخْرَجَ مِنْهَا مَاءَهَا وَمَرْعَاهَا ﴿٨٢﴾

“Akatoa ndani yake maji yake na malisho yake...”

Maelezo Yake Yametangulia katika Surat Hamim Al-Ssajda³ kwamba ardhi iliumbwa kabla ya Kuumbwa kwa mbingu, isipokuwa ni kwamba ilitandikwa baada ya kuumbwa kwa mbingu. Kwa maana ya kwamba, yalitolewa yaliyokuwa ndani yake kutoka katika makadirio kwenda kwenye utekelezaji na haya ndiyo maana ya maneno ya Ibni Abbas رضي الله عنهما na wengine. Ameyaridhia maelezo hayo Ibnu Jarir رحمه الله تعالى.⁴

¹ At-Tabari 24:306.

² At-Tabari 24:207 na Ad-Durr Al-Manthur 8:411.

³ Angalia juzuu ya nane, Tafsiri ya Surat Fussilat (41:9-12).

⁴ At-Tabari 24:308.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَلْجِبَالَ أَرْسَنَهَا ﴿٢٧﴾

“Na milima Akaisimamisha.” Maana yake: Ameikita na Kuithibitisha na Kuisimika katika sehemu zake na Yeye ni Mwingi wa Hekima, Mwingi wa Ujuzi, Mwingi wa Upole kwa viumbe Wake na Mwingi wa Rehema.

Na Kauli Yake Allah تعالى,

مَتَعًا لَكُمْ وَلَا تَعْمِرُنَّ ﴿٢٨﴾

“Kwa nafuu yenu na mifugo yenu.”

Maana yake: Ameitandika ardhi Akabubujisha chemchemu zake, Akadhihirisha siri zake, Akaipitisha mito yake, Akaotesha mimea yake, na miti yake na matunda yake na Ameyathibitisha majabali yake ili itulizane kwa ajili ya watu wake; na utulivu wake uwe utulivu mkubwa sana. Yote hayo ni kwa ajili ya manufaa ya viumbe wake na kwa vile wanavyovihitajia miongoni mwa wanyama ambao wanawala na wanawapanda muda wote wa mahitaji yao katika hii nyumba ya dunia, mpaka utakapokoma muda na kumalizika maisha ya dunia.

فَإِذَا جَاءَتِ الطَّامَةُ الْكُبْرَىٰ ﴿٢٩﴾ يَوْمَ يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ مَا سَعَىٰ ﴿٣٠﴾ وَبُرْزَتِ الْجَحِيمُ لِمَن يَرَىٰ ﴿٣١﴾ فَأَمَّا مَنْ طَغَىٰ ﴿٣٢﴾ وَءَاثَرَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ﴿٣٣﴾ فَإِنَّ الْجَحِيمَ هِيَ الْمَأْوَىٰ ﴿٣٤﴾ وَأَمَّا مَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ وَنَهَىٰ النَّفْسَ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٣٥﴾ فَإِنَّ الْجَنَّةَ هِيَ الْمَأْوَىٰ ﴿٣٦﴾ يَسْأَلُونَكَ عَنِ السَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسَلُهَا ﴿٣٧﴾ فِيمَ أَنْتَ مِنْ ذِكْرِهَا ﴿٣٨﴾ إِلَىٰ رَبِّكَ مُنْتَهَىٰ ﴿٣٩﴾ إِنَّمَا أَنْتَ مُنذِرٌ مَّن نَّحْشُهَا ﴿٤٠﴾ كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبِتُوا إِلَّا عَشِيَّةً أَوْ ضُحًىٰ ﴿٤١﴾

34. Basi itakapofika hiyo balaa kubwa,

35. Siku ambayo mtu atakumbuka aliyoyafanya,

36. Na Jahannamu itadhihirishwa kwa mwenye kuona,

37. Basi ama yule aliyezidi ujeuri,

38. Na akakhiari maisha ya dunia,

39. *Kwa hakika Jahannamu ndiyo makaazi yake!*
40. *Na ama yule anayeogopa kusimamishwa mbele ya Mola Wake Mlezi, na akajizuilia nafsi yake na matamania,*
41. *Basi huyo, Pepo itakuwa ndiyo makaazi yake!*
42. *Wanakuuliza Saa (ya Kiyama) itakuwa lini?*
43. *Una nini wewe hata uitaje?*
44. *Kwa Mola Wako Mlezi ndio mwisho wake.*
45. *Kwa hakika wewe ni mwonyaji tu kwa mwenye kuikhofu.*
46. *Ni kama kwamba wao siku watapoiona (hiyo Saa) hawakukaa ila jioni moja tu, au mchana wake.*

Siku ya Qiyama na Yaliyomo Ndani Yake Miongoni mwa Neema na Moto na Kwamba Wakati Wake Haujulikani

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَإِذَا جَاءَتِ الطَّامَّةُ الْكُبْرَىٰ ﴿٧٩﴾

“Basi itakapofika hiyo balaa kubwa.”

Nayo ni siku ya Qiyama ameyasema hayo Ibnu Abbas رضي الله عنهما¹ Qiyama kimeitwa kwa jina hilo, kwa sababu kitasheheni jambo lenye kutisha na kufadhaisha. Kama Allah تعالى Alivyosema,

وَالسَّاعَةَ أَذْهَىٰ وَأَمْرٌ ﴿٨٠﴾

“Bali Saa ya Kiyama ndio miadi yao, na Saa hiyo ni nzito zaidi na chungu zaidi.” (54:46) Kama Alivyosema Allah تعالى:

يَوْمَ يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ مَا سَعَىٰ ﴿٨١﴾

“Siku ambayo mtu atakumbuka aliyoyafanya,”

Maana yake: Siku hiyo atakumbuka mtu matendo yake yote mema na maovu,

¹ At-Tabari 24:211.

Kama Alivyosema Allah تعالى،

يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ وَأَنَّى لَهُ الذِّكْرَى ﴿٢٣﴾

“Siku hiyo mtu atakumbuka! Lakini kukumbuka huko kutamfaa nini?” (89:23)

Kama Allah تعالى Alivyosema،

وَبُرِّزَتِ الْجَحِيمُ لِمَن يَرَى ﴿٢٤﴾

“Na Jahannamu itadhihirishwa kwa mwenye kuona.”

Maana yake: Itadhihirishwa kwa wenye kutazama watauona watu waziwazi.

فَأَمَّا مَنْ طَغَى ﴿٢٥﴾

“Basi ama yule aliyezidi ujeuri.”

Maana yake: Atakayeasi na akatakabari.

وَأَنزَلَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿٢٦﴾

“Na akakhiari maisha ya dunia.”

Maana yake: Akayatanguliza maisha hayo kuliko mambo ya Dini yake na akhera yake.

فَإِنَّ الْجَحِيمَ هِيَ الْمَأْوَىٰ ﴿٢٧﴾

“Kwa hakika Jahannamu ndiyo makaazi yake!”

Maana yake: “Kwa hakika marejeo yake ni kwenda motoni na kwamba chakula chake ni katika miti ya miba na kinywaji chake ni katika maji ya moto.

وَأَمَّا مَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ وَنَهَى النَّفْسَ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٢٨﴾

“Na ama yule anayeogopa kusimamishwa mbele ya Mola Wake Mlezi, na akajizuilia nafsi yake na matamaniao.”

Maana yake: “Ameogopa kusimama mbele ya Allah تعالى Mwenye Kushinda, Mwenye Kutukuka na akaiogopa hukumu ya Allah تعالى na akaikataza nafsi yake na mapenzi yake na akairudisha kwenye utii wa Mola Wake:

فَإِنَّ الْجَنَّةَ هِيَ الْمَأْوَىٰ ﴿١٤﴾

“Basi huyo, Pepo itakuwa ndiyo makaazi yake!”

Maana yake: Marejeo yake na makazi yake ni katika Pepo. Kisha Amesema Allah تعالى،

يَسْأَلُونَكَ عَنِ السَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسَلُهَا ﴿١٥﴾ فِيمَ أَنْتَ مِنْ ذِكْرِهَا ﴿١٦﴾ إِلَىٰ رَبِّكَ مُنْتَهَىٰ ﴿١٧﴾

“Wanakuuliza Saa (ya Kiyama) itakuwa lini?, Una nini wewe hata uitaje? Kwa Mola Wako Mlezi ndio mwisho wake.”

Maana yake: Wewe huna ujuzi wa Kiama wala mtu yeyote miongoni mwa viumbe, bali marejeo ya jambo hilo ni kwa Allah تعالى، Mwenye Kushinda na Kutukuka. Kwani, Yeye Pekee Ndiye Anayejua wakati wake kwa uhakika.

ثُقُلْتُ فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۚ لَا تَأْتِيكُمْ إِلَّا بَغْتَةً ۚ يَسْأَلُونَكَ كَأَنَّكَ حَفِيٌّ عَنْهَا ۗ قُلْ إِنَّمَا عَلَّمَهَا عِنْدَ اللَّهِ

“Ni nzito katika mbingu na ardhi. Haikujiini ila kwa ghafla tu. Wanakuuliza kama kwamba wewe una pupa ya kujua. Sema: Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu.” (7:187).

Na amesema hapa،

إِلَىٰ رَبِّكَ مُنْتَهَىٰ ﴿١٧﴾

“Kwa Mola Wako Mlezi ndio mwisho wake.”

Na kwa sababu hiyo wakati Jibril عليه السلام alipomuuliza Mtume ﷺ kuhusu Qiyama Mtume ﷺ alisema،

«مَا الْمَسْئُولُ عَنْهَا بِأَعْلَمَ مِنَ السَّائِلِ»

“Hakuwa mwenye kuulizwa kuhusu Qiyama ni mjuzi zaidi kuliko mwenye kuuliza.”¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

¹ Fat'hul Bari 1:140.

إِنَّمَا أَنْتَ مُنذِرٌ مَّنْ نَّحْشُهَا ﴿٢٧﴾

“Kwa hakika wewe ni mwoyaji tu kwa mwenye kuikhofu.”

Maana yake: Hakika hapana jambo lolote nimekupeleka uwaonye watu na uwatahadharishe na nguvu ya Allah تعالى na adhabu Zake. Atakayemcha Allah تعالى na akaogopa kusimama mbele yake na akayaogopa makamio yake, huyo atakuwa amefaulu na kufuzu. Na ama kuruka patupu na kupata hasara ni kwa Mwenye Kukukadhibisha na akakupinga. Na Kauli Yake Allah تعالى:

كَلِّمْتُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبَثُوا إِلَّا عَشِيَّةً أَوْ ضُحًىهَا ﴿٢٨﴾

“Ni kama kwamba wao siku watapoiona (hiyo Saa) hawakukaa ila jioni moja tu, au mchana wake.”

Maana yake: Watakaposimama kutoka makaburini mwao kuelekea kwenye mkusanyiko, watauona ni mfupi muda wa maisha ya dunia, mpaka wataona kana kwamba maisha hayo kwao yalikuwa ni jioni ya siku au asubuhi ya siku. Na amesema Juwaibir kutoka kwa Adh-Dhahaak kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما

كَلِّمْتُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبَثُوا إِلَّا عَشِيَّةً أَوْ ضُحًىهَا ﴿٢٨﴾

“Ni kama kwamba wao siku watapoiona (hiyo Saa) hawakukaa ila jioni moja tu, au mchana wake.”

Ama jioni ni muda uliopo kati ya Adhuhuri na kuzama kwa jua.

أَوْ ضُحًىهَا ﴿٢٩﴾

“Au mchana wake.”

Ni muda uliopo kati ya kuchomoza kwa jua mpaka nusu ya mchana.¹ Na amesema Qatadah, ‘Wakati wa dunia machoni mwa watu pindi watakapoiona akhera kwa macho.”

Huu ni Mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Annaziati* na Kuhimidiwa ni kwa Allah تعالى na Kuneemesha.

* * *

¹Ad-Durr Al-Manthuur 8:413.

Tafsiri ya Surah 'Abasa

Sura ya 80

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ عَبَسَ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

عَبَسَ وَتَوَلَّى ۝ أَنْ جَاءَهُ الْأَعْمَى ۝ وَمَا يُدْرِيكَ
لَعَلَّهُ يَزْكِي ۝ أَوْ يَذَّكَّرُ فَتَنْفَعَهُ الذِّكْرَى ۝ أَمَا مِنْ
أَسْتَغْفَى ۝ فَأَنْتَ لَهُ تَصَدَّى ۝ وَمَا عَلَيْكَ أَلَّا يَزْكِي ۝
وَأَمَا مِنْ جَاءَكَ يَسْعَى ۝ وَهُوَ يَخْشَى ۝ فَأَنْتَ
عَنْهُ تَلْهَى ۝ كَلَّا إِنَّهَا تَذْكِرَةٌ ۝ فَمَنْ شَاءَ ذَكَرْهُ ۝
فِي صُحُفٍ مُكَرَّمَةٍ ۝ مُرْفُوعَةٍ مُطَهَّرَةٍ ۝ بِأَيْدِي سَفَرَةٍ ۝
كِرَامٍ بَرَرَةٍ ۝ قَبِيلَ الْإِنْسَانِ مَا أَكْفَرُهُ ۝ مِنْ
أَيِّ شَيْءٍ خَلَقَهُ ۝ مِنْ نُطْفَةٍ خَلَقَهُ فَقَدَّرَهُ ۝ ثُمَّ
السَّبِيلَ يَسْرَهُ ۝ ثُمَّ أَمَاتَهُ فَأَقْبَرَهُ ۝ ثُمَّ إِذَا شَاءَ
أَنْشُرَهُ ۝ كَلَّا لَمَّا يَقْضِ مَا أَمَرَهُ ۝ فَلْيَنْظُرِ
الْإِنْسَانُ إِلَى طَعَامِهِ ۝ أَنَا صَبَبْنَا الْمَاءَ صَبًّا ۝
ثُمَّ شَقَقْنَا الْأَرْضَ شَقًّا ۝ فَأَنْبَتْنَا فِيهَا حَبًّا ۝
وَعَبَبْنَا وَقَضَبًّا ۝ وَزَيَّنَّوْنَا وَخَلَّلَّا ۝ وَحَدَّاقْنَا غُلْبًا ۝
وَفَلَكْنَاهُ وَأَبَّا ۝ مَتَعْنَا لَهُمْ وَلَا تَجْمَعُهُمُ ۝

عَبَسَ وَتَوَلَّى ۝ أَنْ جَاءَهُ الْأَعْمَى ۝
وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّهُ يَزْكِي ۝
أَوْ يَذَّكَّرُ فَتَنْفَعَهُ الذِّكْرَى ۝ أَمَا
مِنْ أَسْتَغْفَى ۝ فَأَنْتَ لَهُ تَصَدَّى ۝
وَمَا عَلَيْكَ أَلَّا يَزْكِي ۝ وَأَمَا
مِنْ جَاءَكَ يَسْعَى ۝ وَهُوَ يَخْشَى ۝
فَأَنْتَ عَنْهُ تَلْهَى ۝ كَلَّا إِنَّهَا
تَذْكِرَةٌ ۝ فَمَنْ شَاءَ ذَكَرْهُ ۝
فِي صُحُفٍ مُكَرَّمَةٍ ۝ مُرْفُوعَةٍ
مُطَهَّرَةٍ ۝ بِأَيْدِي سَفَرَةٍ ۝
كِرَامٍ بَرَرَةٍ ۝

1. Alikunja uso Mtume na akageuka,

2. Kwa sababu alimjia kipofu!

3. Na nini kitakujuulisha pengine yeye atatakasika?

4. *Au atawaidhika, na mawaidha yamfae?*
5. *Ama ajionaye hana haja,*
6. *Wewe ndio unamshughulikia?*
7. *Na si juu yako kama hakutakasika.*
8. *Ama anayekujia kwa juhudi.*
9. *Naye anaogopa.*
10. *Ndio wewe unampuuza?*
11. *Sivyo hivyo! Huku ni kukumbushana.*
12. *Basi anayependa akumbuke.*
13. *Yamo katika kurasa zilizohishimiwa.*
14. *Zilizoinuliwa, zilizotakaswa.*
15. *Zimo mikononi mwa Malaika waandishi.*
16. *Watukufu, wema.*

Kukosolewa Mtume ﷺ kwa Kumkunja Uso Mtu Mnyonge: Ibn Umri Makhtum رضي الله عنه.

Wafasiri wengi wametaja kwamba Mtume ﷺ siku moja alikuwa akizungumza na mmoja au wengi wa Makureshi na alikuwa ameshaingia tamaa katika kusilimu kwa baadhi ya viongozi hao. Wakati akiwa katika mazungumzo, ghafla akatokezea Ibnu Umri Makhtum رضي الله عنه ambaye alikuwa ni miongoni mwa watu waliosilimu, akawa anamuuliza Mtume ﷺ kuhusu jambo na huku akishikilia hilo. Mtume ﷺ akataka muda huo apewe nafasi, kwa tamaa na kwa kutarajia kumuongoa kiongozi huyo wa Makureshi. Hivyo akakunja uso na akampa nyongo Ibnu Umri Makhtum رضي الله عنه, na akamuelekea kiongozi huyo. Hapo Akateremsha Allah تعالى:

عَبَسَ وَتَوَلَّى ۖ أَنْ جَاءَهُ الْأَعْمَىٰ ۚ وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّهٗ يَزْكَىٰ ۚ

***“Alikunja uso (Mtume) na akageuka, Kwa sababu alimjia kipofu!
Na nini kitakujuulisha pengine yeye atatakasika?”***

Maana yake: Upatikane kwake utakaso na usafi katika nafsi yake,

أَوْ يَذَّكَّرُ فَتَنْفَعَهُ الذِّكْرَىٰ ﴿١٠﴾

“Au atawaidhika, na mawaidha yamfae?”

Maana yake: Itapatikana kwake kukumbuka maonyo na kutakasika na mambo yaliyoharamishwa.

أَمَّا مَنْ أَسْتَفْتَىٰ ﴿١١﴾ فَأَنْتَ لَهُ تَصَدَّىٰ ﴿١٢﴾

“Ama ajionaye hana haja, Wewe ndio unamshughulikia?”

Kwa maana: Ama tajiri wewe ndiye unayeshughulika naye. Huenda akaongoka,

وَمَا عَلَيْكَ أَلَّا يَزُكَّىٰ ﴿١٣﴾

“Na si juu yako kama hakutakasika.”

Maana yake: Hukuwa wewe unadaiwa kwake iwapo haukupatikana kwake utakaso.

وَأَمَّا مَنْ جَاءَكَ يَسْعَىٰ ﴿١٤﴾ وَهُوَ يَخْشَىٰ ﴿١٥﴾

“Ama anayekujia kwa juhudi, naye anaogopa.”

Maana yake: 'Anakuhitaji wewe na anakujia ili aweze kuongozwa kwa yale unayoyasema.

فَأَنْتَ عَنْهُ تَلَهَّىٰ ﴿١٦﴾

“Ndio wewe unampuuza?”

Maana yake: Unajishughulisha. Na kutokea hapo Allah تعالیٰ Alimuamrisha Mtume Wake ﷺ maonyo yake yasiwe mahususi kwa watu fulani, bali afanye usawa baina ya mtukufu na mnyonge, fukara na tajiri, bwana au mtwana, wanamume na wanawake, wadogo na wakubwa.

Kisha Allah تعالیٰ Atamuongoza Anayemtaka kwenye njia iliyonyooka na Yake Yeye Hekima kubwa na hoja yenye kuvunja upinzani wote.

Amepokea Abuu Ya'ala رحمه الله تعالیٰ na Ibnu Jarir رحمه الله تعالیٰ kutoka kwa Aisha رضي الله عنها; Iliteremshwa;

عَبَسَ وَتَوَلَّى ﴿١﴾

“Alikunja uso (Mtume) na akageuka”

Kwa sababu ya Ummi Makhtum رضي الله عنه – kipofu aliyekwenda kwa Mtume ﷺ akawa anasema: Niongoze na hali ya kuwa mbele ya Mtume ﷺ kulikuwa na mtu mmoja miongoni mwa wakubwa wa Kishirikina. Amesema Aisha رضي الله عنها akawa Mtume ﷺ anampa mgongo huku akimuelekea na kumpa umuhimu mtu mwingine, na akasema;

«أَتَرَىٰ بِمَا أَقُولُ بِأَنسًا؟»

“Je unaona kwa haya ninayoyasema huku hayana uzito wowote?”

Akajibu: ‘Hapana.’ Katika hili ikateremka aya;

عَبَسَ وَتَوَلَّى ﴿٢﴾

“Alikunja kipaji na akageuka.”

Iliteremshwa.¹ Na amepokea At-Tirmidh Hadith hii na hakumtaja Aisha رضي الله عنها.² Nami nasema, Hadith hii ipo kama hivyo katika Muwatwa.³

Sifa za Qur’an

Na Kauli Yake Allah تعالى:

كَلَّا إِنَّهَا تَذْكِرَةٌ ﴿٣﴾

“Sivyo hivyo! Huku ni kukumbushana.”

Katika sura hii pana maelekezo au wasia wa kufanya usawa kati ya watu katika kufikisha Elimu kati ya Mtukufu wao na Mnyonge wao. Na amesema Qatada na As-Suddi kuhusu aya,

كَلَّا إِنَّهَا تَذْكِرَةٌ ﴿٤﴾

“Sivyo hivyo! Huku ni kukumbushana.” Anakusudia Qur’an,

¹ At-Tabari 24:217.

² Tuhfat Al-Ahwadh 9:250.

³ Al-Muwatta 1:203.

فَمَنْ شَاءَ ذَكَرْهُ ﴿٧٠﴾

"Atakayetaka atayakumbuka maonyo hayo."

Maana yake: Mwenye kutaka atakumbuka Allah تعالى katika mambo yake yote.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فِي صُحُفٍ مُّكْرَمَةٍ ﴿٧١﴾ مَرْفُوعَةٍ مُّطَهَّرَةٍ ﴿٧٢﴾

"Yamo kwenye kurasa zenye kutukuzwa. Zenye kunyanyuliwa zenye kutakaswa."

Maana yake: Sura hii au maonyo mawili yote hayo ni lazima, hali ni kwamba Qur'an yote imo katika kurasa zenye kutukuzwa. Maana zenye kuheshimiwa.

مَرْفُوعَةٍ

"Zilizowekwa juu sana."

Maana yake: Ipo katika hadhi na cheo cha juu,

مُطَهَّرَةٍ ﴿٧٣﴾

"Zenye kutakaswa."

Maana yake: Kutokuwa na uchafu, nyongeza au upungufu.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

بِأَيْدِي سَفَرَةٍ ﴿٧٤﴾

"Imo mikononi mwa wajumbe."

Amesema Ibnu Abbas, Mujahid, Adh-Dhahaak na Ibnu Zaid رضي الله عنهم hao ni malaika.¹

Na amesema Al-Bukhari, malaika husuluhisha baina yao pindi wanaposhuka na Wahyi wa Allah تعالى na kuufikisha huwa kama vile balozi, Mwakilishi ambaye husuluhisha baina ya watu.² Na Kauli Yake Allah تعالى:

¹ At-Tabari 24:221, na Ad-Durr Al-Manthur 8:414.

² Fat'hul Al-Bari 8:561.

كِرَامِ بَرَّةٍ ﴿١١﴾

"Watukufu wema." Maana yake: Umbile lao ni zuri tukufu, Tabia zao na matendo yao ni mema matakatifu yamekamiliika. Na kutoka hapa inatakikana kwa Mwenye kuichukua Qur'an awe mkweli na muongofu katika matendo yake, na maneno yake ili aige tabia ya Qur'an.

Amepokea Imamu Ahmad, kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kuwa amesema, Mtume ﷺ amesema.

«الَّذِي يقرأ القرآنَ وهو ماهرٌ به، مع السفرة الكرام البررة، والذي يقرؤه وهو عليه شاق، له أجران»

*"Yule ambaye anaisoma Qur'an na hali ya kuwa ni hodari nayo atakuwa pamoja na wajumbe wema watukufu; na yule ambaye anaisoma na hali ya kuwa hana uhodari nayo hivyo ana malipo mawili."*¹

Kundi la wapokeaji Hadithi limeithibitsha Hadithi hii.²

فَتِلَّ الْإِنْسَانُ مَا أَكْفَرَهُ ﴿١٧﴾ مِنْ أَيِّ شَيْءٍ خَلَقَهُ ﴿١٨﴾ مِنْ نُطْفَةٍ خَلَقَهُ فَقَدَّرَهُ ﴿١٩﴾
 ثُمَّ السَّبِيلَ يَسْرُهُ ﴿٢٠﴾ ثُمَّ أَمَاتَهُ فَأَقْبَرَهُ ﴿٢١﴾ ثُمَّ إِذَا شَاءَ أَنْشَرَهُ ﴿٢٢﴾ كَلَّا لَمَّا يَقْضِ
 مَا أَمَرَهُ ﴿٢٣﴾ فَلْيَنْظُرِ الْإِنْسَانُ إِلَى طَعَامِهِ ﴿٢٤﴾ أَنَا صَبَبْنَا الْمَاءَ صَبًّا ﴿٢٥﴾ ثُمَّ
 شَقَقْنَا الْأَرْضَ شَقًّا ﴿٢٦﴾ فَأَنْبَتْنَا فِيهَا حَبًّا ﴿٢٧﴾ وَعَيْنًا وَقَضْبًا ﴿٢٨﴾ وَزَيْتُونًا وَنَخْلًا
 ﴿٢٩﴾ وَحَدَائِقَ غُلْبًا ﴿٣٠﴾ وَفَيْكَةً وَأَبًّا ﴿٣١﴾ مَتَعًا لَكُمْ وَلَا تَعْمُرُونَ ﴿٣٢﴾

17. **Amelaaniwa mwanadamu ni ukafiri ulioje huo alionao?"**

18. **"Ni kutokana na kitu gani Amemuumba?"**

19. **"Ni kutokana na tone la manii Amemuumba na Akamkadiria"**

20. **"Kisha njia ya kutoka Akaifanya nyepesi"**

21. **"Kisha Atamfisha kisha Ataamrisha azikwe"**

¹ Ahmad 6:48.

² Fat'hul Al-Bari 8:560, Muslim 1:549, Abu Dawud 2:148, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:215.

22. *"Kisha Atakapotaka Atamfufua"*
23. *"Hapana sivyo hivyo bado hajayatekeleza yale aliyomuamrisha"*
24. *"Na akichunguze binadamu chakula chake"*
25. *"Hakika Sisi Tumeyamimina maji, kuyamimina kwa wingi sana"*
26. *"Kisha Tumepasua ardhi, kupasua kukubwa"*
27. *"Tukaotesha humo tembe za chakula"*
28. *"Na mizabibu na mboga"*
29. *"Na mizaituni na mitende"*
30. *"Na bustani yenye miti mingi"*
31. *"Na matunda na nyasi"*
32. *"Kwa ajili ya manufaa yenu na wanyama wenu."*

Jibu kwa Anayakanusha Uwepo wa Maisha Mengine Baada ya Kufa

Allah تعالى Anasema Akimkemea yule mwenye kukanusha kufufuliwa na kukusanywa miongoni mwa wanaadamu;

قُتِلَ الْإِنْسَانُ مَا أَكْفَرَهُ ﴿٧٧﴾

"Amelaaniwa mwanadamu, ni kukufuru kulikoje kwake huko?" Amesema Adh-Dhahak kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

قُتِلَ الْإِنْسَانُ

"Amelaaniwa mwanadamu". "Amelaaniwa."¹ Na kama hivyo amesema Abuu Malik na maneno haya yanahusu kila binadamu anayekadhibisha kutokana na wingi wa kukadhibisha kwake. Pasi na mashiko yoyote, bali ni kutokana na kuona tu kwamba jambo hilo haliwezekani na ukosefu wa Elimu. Ibnu Juraij amesema,

مَا أَكْفَرَهُ ﴿٧٧﴾

"ni kukufuru kulikoje huko?" Ni ukubwa ulioje wa kukufuru kwake. Na amesema Qatada:

¹ Al-Qurtubi 19:217 Adh-dhahaak hakumsikia Ibn Abbaas رضي الله عنهما.

مَا أَكْفَرُهُ ﴿٧٦﴾

“Ni kukufuru kulikoje huko?” Ni kulaaniwa kulikoje?¹

Kisha Ameweka wazi Allah تعالى; namna Alivyomuumba kutokana na kitu kinyonge na kwamba Yeye Anaweza Kumrejeshwa kama alivyokuwa mwanzo. Kwa hiyo Amesema Allah تعالى:

مَنْ أَيِّ شَيْءٍ خَلَقَهُ ﴿٧٧﴾ مِنْ نُطْفَةٍ خَلَقَهُ فَقَدَّرَهُ ﴿٧٨﴾

“Ni kutokana na kitu gani Amemuumba”? , ni kutokana na tone la manii Amemuumba na Amemkadiria.”

Maana yake: Ameukadiria muda wake, riziki yake, matendo yake, na ni nani miongoni mwao mwema na nani muovu.

ثُمَّ السَّبِيلَ يَسَّرَهُ ﴿٧٩﴾

“Kisha njia ya kutokea Akaifanya nyepesi” Amesema Awfi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما; kisha Amerahisisha kutoka kwake tumboni mwa mama yake.² Na kama hivyo amesema Ikrimah na Adh-Dhahak na Abu Saleh na Qatada na As- Ssudi na ameyakubali Ibn Jarir رحمه الله تعالى³ Ama Mujahid amesema kuwa; maneno haya ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٨٠﴾

“Kwa hakika Sisi Tumemuongoza njia ima ni mwenye kushukuru au ima mwenye kukufuru.” (76:3)

Maana: Tumembainishia na Tumemuwekea wazi na Tumemshilishia matendo yake. Na kama hivyo amesema Hasan na Ibnu Zaid.⁴ Haya ndiyo yaliyo na nguvu zaidi, na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi. Na Kauli Yake Allah تعالى:

ثُمَّ أَمَاتَهُ فَأَقْبَرَهُ ﴿٨١﴾

“Kisha Atamfisha na Ataamrisha azikwe.”

¹ Al-Baghawi 4:448

² At-Tabari 24:223 Al-Awfi dhaifu

³ Ad-Durr Al-Manthur 8:419, 223, 224

⁴ At-Tabari 24:224

Maana yake: Baada ya Kumuumba Atamfisha, na Atajaalia azikwe. Maana Atamfanya kuwa ni mkazi wa kaburini. Waarabu wanasema: nimemzika mtu pindi atakapolitawalia jambo hilo kwake. Na Kauli Yake Allah تعالى:

ثُمَّ إِذَا شَاءَ أَنْشَرَهُ ﴿٣٢﴾

“Kisha Atakapotaka Atamfufua.”

Maana yake: Atamfufua baada ya kufa kwake. Na kutokana na maana hiyo husemwa: kufufuliwa na kukusanywa,

وَمِنَ آيَاتِنَا أَنْ خَلَقْنَاكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ إِذَا أَنْتُمْ بَشَرٌ تَنْتَشِرُونَ ﴿٢٠﴾

“Na kutokana na alama za uwezo wake ni Kuwaumbeni kutokana na mchanga kisha ghafila nyinyi ni binadamu mnaozagaa katika ardhi.” (30:20)

وَأَنْظُرْ إِلَى الْعِظَامِ كَيْفَ نُنشِزُهَا ثُمَّ نَكْسُوهَا لَحْمًا

“Na itazame mifupa namna Tunavyoihuisha na kisha Tunaivika nyama.” (2:259)

Imekuja katika sahihi mbili kutoka kwa Al-'Amash kutoka kwa Abu Swaleh kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه,

«كُلُّ ابْنِ آدَمَ يَنَلُّ إِلَّا عَجَبَ الذَّنْبِ، مِنْهُ خُلِقَ، وَبِهِ يُرْكَبُ»

“Mwili wote wa Mwanadamu utaoza, isipokuwa Ajbu Adh-Dhanab, kutokana na huo ameumbwa kutokana na huo ataumbwa tena”¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

كَلَّا لَمَّا يَقْضِ مَا أَمَرَهُ ﴿٣١﴾

“Hapana sivyo hivyo, bado hajayatekeleza yale Aliyomuamrisha.”

Amesema Ibnu Jarir رحمه الله تعالى; Anasema Allah تعالى Sifa Zake Zimetukuka yamethibiti hayo hayakuwa mambo kama anavyoyasema huyu mwanadamu aliyekufuru. Kwamba yeye amekwisha kutekeleza haki ya Allah تعالى juu yake katika nafsi yake na mali yake.

¹ Fat'hul Al-Bari 8:414, na Muslim 4:2270.

لَمَّا يَقْضِ مَا أَمَرَهُ ﴿٣٢﴾

“Bado hajatekeleza yale Aliyomuamrisha.”

Anasema: Hakuyatekeleza yale mambo ambayo yaliyofaradhishwa juu yake kutoka kwa Mola Wake Aliyeshinda na Kutukuka.¹ Yale yanayonidhihirikia mimi katika maana ya maneno hayo na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi. Ni kwamba maana ya aya hii ifuatayo;

ثُمَّ إِذَا شَاءَ أَنْشَرَهُ ﴿٣٣﴾

“Kisha atakapotaka atamfufua.” Maana yake: Atamfufua.

كَلَّا لَمَّا يَقْضِ مَا أَمَرَهُ ﴿٣٤﴾

“Hapana sivyo hivyo, bado hajayatekeleza yale Aliyomuamrisha.”

Maana yake: Bado hajalitekeleza (Kuwafufua), mpaka muda ukapita na kudura kwa mwanadamu imalizike katika Aliowaandikia kuwa yatapatikana kwao na yatatoka kuja duniani na Allah تعالى Ameshaamrisha na Kulipanga hilo. Litakapokoma hilo mbele ya Allah تعالى Atawafufua viumbe na Atawarudisha kama Alivyowaumba mwanzo.

Kuotesha Tembe za Vyakula na Nyenginezo ni Uthibitisho wa Kuwepo Maisha Mengine baada ya Kufa.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَلْيَنْظُرِ الْإِنْسَانُ إِلَى طَعَامِهِ ﴿٣٥﴾

“Na akichunguze mwanadamu chakula chake Ndani yake.”

Na kutaja neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa waja Wake ndani yake kuna dalili ya kuishi mimea katika ardhi iliyokufa, kwa kuvihuisha viwiliwili baada ya kuwa vilikuwa ni mifupa iliyochakaa, na udongo uliotawanyika.

أَنَا صَبَبْنَا الْمَاءَ صَبًّا ﴿٣٦﴾

“Kwamba Sisi Tumeyamimina maji kwa wingi sana.”

Maana yake: Tumeyateremsha kutoka mawinguni maji hadi ardhini.

¹ At-Twabari 24:225.

ثُمَّ شَقَقْنَا الْأَرْضَ شَقًّا

“Kisha Tumeipasua ardhi kuipasua kukubwa sana.”

Maana yake: Tumeyaweka hayo maji yakaingia katika mipaka na kupenya hadi katika tembe ambayo imewekwa katika ardhi ikaota na ikapanda juu na ikaonekana katika uso wa ardhi.

فَأَنْبَتْنَا فِيهَا حَبًّا وَعَيْنًا وَقَضْبًا

“Tukaotesha katika hiyo ardhi tembe na mizabibu na mboga.”

Kwa hiyo “Habbu” ni kila kinachotajwa katika tembe na zabibu zinazojulikana; na “Al Qadhbu” ni majani ambayo hulishwa wanyama hali ya kuwa mabichi. Na huitwa Al Qat vilevile. Ameyasema hayo Ibn Abbas na Qatadah na Adh-Dhaahak na As-Sudiy رضي الله عنهم.¹ Na Hassan Al-Basri رحمه الله تعالى amesema, Al Qadhb ni majani yaliwayo na wanyama.

وَزَيْتُونًا

“Na mizaituni.”

Zaituni zinajulikana nazo ni nyeusi na maji yake ni meusi na mafuta yake huwashwa taa na hujipaka kwayo watu.

وَنَخْلًا

“Na mitende.”

Na Tende huliwa zikiwa Mbichi, Kavu na Mbivu. Huliwa katika hali ya kupikwa. Pia hukamuliwa na kufanywa siki. Matumizi ya tende yapo katika hali nyingi na mbalimbali.

وَحَدَائِقَ غُلْبًا

“Na bustani zenye miti mingi sana.”

Maana yake: Bustani. Amesema Hassan na Qatada kuwa Ghulb ni mitende mizito iliyo mizuri.² Na amesema Ibn Abbas na Mujahid رضي الله عنهما. Kila kilichosongamana na kujikusanya pamoja.³

¹ At-Tabari 24:226.

² At-Tabari 24:228, 221.

³ At-Tabari 24:227.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَفِيكِهِمْ وَأَبًا

"Na matunda na nyasi." Ama "fakiha" ni kila ambacho hustarehewa kwacho, katika matunda. Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما, "Al -Fakiha." Ni kila kinacholiwa na mwanadamu hali ya kuwa kibichi. Na "Abbu" ni kila kilichooteshwa na ardhi katika ambavyo vinaliwa na wanyama, wala haviliwi na watu.¹ Na katika upokezi mwengine, "Abbu" ni nyasi za wanyama.² Na amepokea Abu Ubaid Al Qasim bin Salam kutoka kwa Ibrahim At-Tiimi amesema aliulizwa Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه kuhusu Kauli Yake Allah تعالى:

وَفِيكِهِمْ وَأَبًا

"Na matunda na nyasi." Akasema; ni mbingu gani itakayonifunika na ardhi gani itakayonibeba iwapo nitasema katika kitabu cha Mwenyezi Mungu jambo ambalo silielewi?³ Ama aliyoyapokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Anas رضي الله عنه amesema; alisoma Umar bin Khattab رضي الله عنه:

عَبَسَ وَتَوَلَّى

"Alikunja uso na akampa nyongo."

Alipofikia katika aya hii,

وَفِيكِهِمْ وَأَبًا

"Na matunda na nyasi." Alisema; tumejua maana ya "Al -Fakiha" nini maana ya "Al -Abbu" akasema naapa kwa umri wako wewe Ibn Al - Khattab, hakika huku ni kujikalifisha. Haya ni mapokezi sahihi.⁴

Na amayapokea haya zaidi ya mtu mmoja kutoka kwa Anas رضي الله عنه na maelezo haya yanachukuliwa juu ya kuwa yeye alitaka kujua umbile lake, na namna yake na dhati yake, na kama si hivyo ni kwamba kila mwenye kuisoma aya hii anajuwa kwamba "Abbu" ni mmea katika mimea ya ardhi.

Kwa sababu ya Kusema Kwake Allah تعالى:

¹ At-Tabari 24:230, 231.

² Ad-Durr Al-Manthur 8:421.

³ Al-Baghawi 4:449.

⁴ At-Tabari 24:229.

فَأَنْبَتْنَا فِيهَا حَبًّا ﴿١٧﴾ وَعِنبًا وَقَضْبًا ﴿١٨﴾ وَزَيْتُونًا وَنَخْلًا ﴿١٩﴾ وَحَدَائِقَ غُلْبًا ﴿٢٠﴾
وَفَيْكِهِمَّ وَأَبًّا ﴿٢١﴾

“Tukaotesha katika ardhi tembe. Na mizabibu na mboga. Na mizaituni na mitende. Na bustani zenye miti mingi sana. Na Matunda na Nyasi.”

Na Kauli Yake Allah تعالى:

مَتْنَعًا لَكُمْ وَلَا تَعْمِلُوا ﴿٢٢﴾

“Kwa ajili ya manufaa yenu na wanyama wenu.”

Maana yake: Kwa ajili ya maisha yenu na wanyama wenu katika hii Dunia mpaka siku ya Qiyama.

* * *

فَإِذَا جَاءَتِ الصَّاحَّةُ ﴿٣٣﴾ يَوْمَ يَفِرُّ الْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ ﴿٣٤﴾
 وَأُمِّهِ وَأَبِيهِ ﴿٣٥﴾ وَصَلْحَتَيْهِ وَبَنِيهِ ﴿٣٦﴾ لِكُلِّ أَمْرٍ
 مِّنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ ﴿٣٧﴾ وَوَجْهُهُ يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرٌ ﴿٣٨﴾
 ضَاحِكَةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ ﴿٣٩﴾ وَوَجْهُهُ يَوْمَئِذٍ عَلِيمٌ ﴿٤٠﴾
 تَرَهَّقَهَا قَتْرَةٌ ﴿٤١﴾ أَوْلَتْكَ هُمُ الْكَافِرَةُ الْفَجْرَةَ ﴿٤٢﴾

فَإِذَا جَاءَتِ الصَّاحَّةُ ﴿٣٣﴾ يَوْمَ يَفِرُّ
 الْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ ﴿٣٤﴾ وَأُمِّهِ وَأَبِيهِ
 ﴿٣٥﴾ وَصَلْحَتَيْهِ وَبَنِيهِ ﴿٣٦﴾ لِكُلِّ
 أَمْرٍ مِّنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ ﴿٣٧﴾
 وَوَجْهُهُ يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرٌ ﴿٣٨﴾ ضَاحِكَةٌ
 مُّسْتَبْشِرَةٌ ﴿٣٩﴾ وَوَجْهُهُ يَوْمَئِذٍ عَلِيمٌ
 ﴿٤٠﴾ تَرَهَّقَهَا قَتْرَةٌ ﴿٤١﴾
 أَوْلَتْكَ هُمُ الْكَافِرَةُ الْفَجْرَةَ ﴿٤٢﴾

33. Basi utakapokuja ukelele.

34. Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye.

35. Na mamaye na babaye.

36. Na mkewe na wanawe.

37. Kila mtu miongoni mwao siku hiyo atakuwa na lake la kumtoshia.

38. Siku hiyo ziko nyuso zitazonawiri.

39. Zitacheka, zitachangamka.

40. Na nyuso siku hiyo zitakuwa na mavumbi.

41. Giza totoro litazifunika.

42. Hao ndio makafiri watenda maovu.

Siku ya Qiyama na Watu Kukimbia Jamaa Zao.

Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema, "As-Swakha" Ni jina katika majina ya siku ya kiyama, Allah تعالى Ameipa uzito siku hiyo na Amewatahadharisha nayo waja Wake".¹ Ibnu Jarir رحمه الله تعالى amesema, 'Huenda likawa hilo ni jina la kupulizia parapanda'.² Na Al-Baghawi رحمه الله تعالى amesema "As-Swakha" anaukusudia ukelele siku ya kiyama. Umeitwa ukelele kwa jina hilo, kwa sababu utayaumiza masikio. Maana: 'Utaendelea sana katika kuyasikilizisha mpaka utakapokaribia kuyafanya yawe maziwi."³

¹ At-Tabari 24:232.

² At-Tabari 24:231.

³ At-Tabari 24:449.

يَوْمَ يَفِرُّ الْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ ﴿٣٣﴾ وَأُمِّهِ وَأَبِيهِ ﴿٣٤﴾ وَصَلْحَتِهِ وَبَنِيهِ ﴿٣٥﴾

“Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye. Na mamaye na babaye. Na mkewe na wanawe.”

Kwa maana: Anawaona lakini anawakimbia, kwani vitisho ni vikubwa sana. Katika Hadithi sahihi kuhusu maombezi ni kuwa kila akifuatwa Mtume katika Mitume wakubwa wa “Ulili Azmi” (Mitume waliopewa sheria na kuvumilia sana matatizo) ili awaombe kwa Allah تعالى Atajibu kwa kusema, ‘Nafsi, nafsi, sitoomba leo hii isipokuwa kuiombea nafsi yangu tu. Hata Issa bin Maryam عليه السلام atasema: “Sitoweza kumuombea yeyote leo hii ila nafsi yangu, hata mama yangu Mariam aliyenizaa sitomuombea.”¹

Na ndipo Alipotremsha Allah تعالى Kauli Yake,

يَوْمَ يَفِرُّ الْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ ﴿٣٣﴾ وَأُمِّهِ وَأَبِيهِ ﴿٣٤﴾ وَصَلْحَتِهِ وَبَنِيهِ ﴿٣٥﴾

“Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye. Na mamaye na babaye. Na mkewe na wanawe.”

Qatadah anasema kuwa maana yake: ‘Ni mpendwa na mpendwa wake, ndugu kwa nduguye wa karibu zaidi na jamaa kwa jamaa yake wa karibu zaidi (yaani kila mmoja atamkimbia mwenzake). Kutokana na vitisho vikubwa vya siku hiyo.” Kauli Yake Allah تعالى,

لِكُلِّ أَمْرٍ مِّنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ ﴿٣٦﴾

“Atakuwa ana kila mtu katika wao siku hiyo jambo linalomtosha.”

Maana yake: “Atakuwa ni mwenye kushughulika na nafsi yake hivyo kumfikiria mwingine haitopatikana.” Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«تُحْشَرُونَ حَفَاةَ عُرَاةٍ مُّشَاةٍ عُرُلًا»

“Mtafufuliwa mkiwa pekupeku, uchi, mkitembea kwa miguu, na mkiwa na magovi yenye kuning’inia.”

¹ At-Tabari 24:231.

² At-Tabari 24:449.

³ Muslim 1:182.

Mke wake Mtume ﷺ akamuuliza, "Je, kama hali ni hiyo tutakuwa tunaangaliana?" Mtume ﷺ akajibu kwa kusoma aya hii,

«لِكُلِّ امْرِئٍ مِنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ - أَوْ قَالَ: - مَا أَشْغَلَهُ عَنِ النَّظَرِ»

"Atakuwa ana kila mtu katika wao siku hiyo jambo linalomtosha."
au alisema, "kuwa hakuna kitu kitakachomfanya aangalie kwani kila mmoja ameshughulishwa na ya kwake."¹

Imepokelewa kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema,

«تُحَسِّرُونَ حُفَاةَ عُرَاةٍ غُرُلًا»

"Mtafufuliwa mkiwa pekupeku, uchi,
na mkiwa na magovi."

Mwanamke mmoja akauliza, "Je mtu ataweza kuona uchi wa mwenzake?"
Mtume ﷺ akajibu,

«يَا فَلَانَةُ، لِكُلِّ امْرِئٍ مِنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ»

"Ewe, Mwanamke! atakuwa ana kila mtu katika wao siku hiyo jambo linalomtosha!"

At-Tirmidhi amesema, kuwa Hadithi hii ni Hasan Sahih.²

Nyuso za Watu wa Peponi na za Watu wa Motoni Siku ya Kiyama

Kauli Yake Allah تعالي:

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرَةٌ ﴿٣٨﴾ ضَاحِكَةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ ﴿٣٩﴾

"Siku hiyo ziko nyuso zitazonawiri. Zitacheka, zitachangamka."

Maana yake: Watu katika siku hiyo watakuwa katika makundi mawili; kundi lina nyuso zenye furaha na kuangaza, na kundi hili nyuso zao zitakuwa,

ضَاحِكَةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ ﴿٣٩﴾

"Zitacheka, zitachangamka."

¹ Al-Hakim 2:251. (Inafanana na Al-Bukhari na. 6162).

² Tuhfatul Ahwadhi 9:251.

Watu wenye kufarahi ndani ya moyo wao na tabasamu huonekana katika nyuso zao kwa furaha kuu waliyokuwa nayo; hawa ndio watu wa peponi.

وَوُجُوهٌُ يَوْمَئِذٍ عَلَيَّا غَيْرَةٌ ۖ تَرْهَقُهَا قَتَرَةٌ ﴿٥٠﴾

“Na nyuso zengine siku hiyo patakuwa na vumbi juu yake utazifunika weusi.”

Maana yake: “Vumbi huwafunika na kuwafanya weusi, waliochafuka kwa vumbi.” Yaani, nyuso zao hufunikwa kwa weusi wa vumbi. Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema,

تَرْهَقُهَا قَتَرَةٌ ﴿٥٠﴾

“Utazifunika weusi.”

Maana yake: Nyuso zao zitafunikwa na weusi.¹

Kauli Yake Allah تعالى،

أُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرَةُ الْفَجْرَةُ ﴿٥١﴾

“Hao ndio makafiri watenda maovu.”

Maana yake: “Makafiri katika mioyo yao na waovu katika matendo yao.” Kama katika Kauli Yake Allah تعالى،

وَلَا يَلِدُوا إِلَّا فَاكِرًا كَفَّارًا ﴿٥٢﴾

“Wala wao hawatazaa ila waovu makafiri.” (71:27)

Mwisho wa Tafsiri ya Suratu 'Abasa, shukrani ni kwa Allah تعالى kwa Neema Zake.

* * *

¹ Ad-Durr Al-Manthur 8:424.

Tafsiri ya Suratu Takwir Sura ya 81 Iliteremshwa Makkah

Yaliyokuja Kuhusu Sura hii.

Al-Imamu Ahmad amepokea kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما, kuwa Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ سَرَّهُ أَنْ يَنْظُرَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ كَأَنَّهُ رَأَى عَيْنٍ فَلْيَقْرَأْ: ﴿إِذَا الشَّمْسُ كُوِّرَتْ﴾ ۞ و
﴿إِذَا السَّمَاءُ انْفَطَرَتْ﴾ ۞ و ﴿إِذَا السَّمَاءُ انشَقَّتْ﴾ ۞»

*“Ambaye kunamhamasisha kuitazama siku ya Qiyama, kana kwamba anakiona kwa macho na azisome sura hizi: “Jua litakapokunjwa.” (81:1), “Mbingu itapochanika.” (82:1), “Itapochanika mbingu.” (84:1)”*¹

Na kama hivyo amepokea haya Al-Tirmidhi.²

* * *

¹ Ahmad 2:27.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 9:252.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ التَّكْوِيْنِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِذَا الشَّمْسُ كُوِّرَتْ ① وَإِذَا النُّجُومُ انْكَدَرَتْ ② وَإِذَا

الْجِبَالُ سُيِّرَتْ ③ وَإِذَا الْعِشَارُ عُطِّلَتْ ④ وَإِذَا

الْوُحُوشُ حُيِّرَتْ ⑤ وَإِذَا الْبِحَارُ سُجِّرَتْ ⑥ وَإِذَا

النُّفُوسُ زُوِّجَتْ ⑦ وَإِذَا الْمَوْءِدَةُ سُيِّلتْ ⑧ بِأَيِّ

ذَنْبٍ قُيِّلَتْ ⑨ وَإِذَا الصُّحُفُ نُثِرَتْ ⑩ وَإِذَا السَّمَاءُ

كُثِيطَتْ ⑪ وَإِذَا الْجَحِيمُ سُعِرَتْ ⑫ وَإِذَا الْجَنَّةُ أُزْلِفَتْ

عَلِمَتْ نَفْسٌ مَّا أَحْضَرَتْ ⑬ فَلَا أُقْسِمُ بِالْخُنُوسِ

⑭ الْجَوَارِ الْكُنَّسِ ⑮ وَاللَّيْلِ إِذَا عَسَسَ ⑯

وَالصُّبْحِ إِذَا تَنَفَّسَ ⑰ إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ⑱

ذِي قُوَّةٍ عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ ⑲ مُطَاعٍ ثَمَّ أَمِينٍ ⑳

وَمَا صَاحِبُكُم بِمَجْنُونٍ ㉑ وَلَقَدْ رَآهُ بِالْأَفْئِ الْيَمِينِ

⑳ وَمَا هُوَ عَلَى الْغَيْبِ بِضَنِينٍ ㉒ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ

شَيْطَانٍ رَّجِيمٍ ㉓ فَأَيْنَ تَذْهَبُونَ ㉔ إِنَّ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ

لِلْعَالَمِينَ ㉕ لِمَنْ شَاءَ مِنْكُمْ أَنْ يَسْتَقِيمَ ㉖ وَمَا

تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ㉗

إِذَا الشَّمْسُ كُوِّرَتْ ① وَإِذَا

النُّجُومُ انْكَدَرَتْ ② وَإِذَا الْجِبَالُ

سُيِّرَتْ ③ وَإِذَا الْعِشَارُ عُطِّلَتْ ④

وَإِذَا الْوُحُوشُ حُيِّرَتْ ⑤ وَإِذَا

الْبِحَارُ سُجِّرَتْ ⑥ وَإِذَا النُّفُوسُ

زُوِّجَتْ ⑦ وَإِذَا الْمَوْءِدَةُ سُيِّلتْ

⑧ بِأَيِّ ذَنْبٍ قُيِّلَتْ ⑨ وَإِذَا

الصُّحُفُ نُثِرَتْ ⑩ وَإِذَا السَّمَاءُ

كُثِيطَتْ ⑪ وَإِذَا الْجَحِيمُ سُعِرَتْ

⑫ وَإِذَا الْجَنَّةُ أُزْلِفَتْ ⑬ عَلِمَتْ

نَفْسٌ مَّا أَحْضَرَتْ ⑭

نَفْسٌ مَّا أَحْضَرَتْ ⑬

1. Jua litakapokunjwa, na kupoteza mwanga wake na nguvu zake.

2. Na nyota zitakapodondoshwa.

3. Na milima ikaondolewa.

4. Na ngamia wenye mimba pevu watakapoachwa wasi-shughulikiwe.

5. *Na wanyama wa mwituni wakakusanywa.*
6. *Na bahari zikawaka moto.*
7. *Na roho zikaunganishwa na kiwiliwili.*
8. *Na msichana aliyezikwa hai atapoulizwa.*
9. *Kwa kosa gani aliuliwa?.*
10. *Na madaftari yatakapoenezwa.*
11. *Na mbingu itapotanduliwa.*
12. *Na Jahannamu itapochochewa.*
13. *Na Pepo ikasogezwa.*
14. *Kila nafsi itajua ilichokihudhurisha.*

Yatakayotuka Siku ya Qiyama nayo ni Kukunjwa Jua

Amesema Ali bin Abi Twalha kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما

إِذَا أَلْشَّمْسُ كُوِّرَتْ ﴿١﴾

“Pindi jua litakapokunjwa”

Anakusudia litakapokuwa na kiza.¹ Na akasema Al-Awfi kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما, ‘litakapoondoka.’ Na amesema Qatadah, ‘litakapoondoka mwangaza wake.’² Amesema Said bin Jubair, “*litakapo kunjwakunjwa.*” litakapozamishwa.³ Na amesema Abu Swaleh, “*litakapokunjwakunjwa.*” Na “*Takwiir*” Ni kukikusanya kitu baadhi yake juu ya baadhi nyingine. Na katika matumizi ya neno, ‘*Takwiir*’, ni kukikunja kilemba na kuzikusanya nguo pamoja. Kwa hiyo maana ya Kauli Yake Allah تعالى,

كُوِّرَتْ ﴿٢﴾

“...*Kuwwirat.*” Litakusanywa baadhi yake kwenye baadhi kisha litafungwafungwa na litatupwa, litapofanywa hivyo utaondoka mwangaza wake. Amepokewa Bukhari kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema,

¹ At-Tabari 24:237.

² At-Tabari 24:238. Isnadi yake ni dhaifu.

³ At-Tabari 24:238.

«الشَّمْسُ وَالْقَمَرُ بِكَوْرَانِ يَوْمَ الْيَوْمِ»

“Jua na mwezi vitakunjwa siku ya Qiyama”¹

Hadithi hii ameipokea Bukhari peke yake na hili ni tamko lake.

Kuporomoka kwa Nyota

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذَا النُّجُومُ انْكَدَرَتْ ﴿٦٠﴾

“**Na nyota zitakapodondoshwa.**” Maana yake: Zitakapopukutika kama alivyosema Allah تعالى.

وَإِذَا الْكَوَاكِبُ انْتَبَرَتْ ﴿٦١﴾

“**Na pindi nyota zitakapopuputika.**” (82:2)

Na asili ya “*Al-Inkidaar*” Ni kumiminika kwa watu. Amesema Rabi bin Anas kutoka kwa Abu Al-Aliya nae kutoka kwa Ubay bin Ka’ab رضي الله عنه amesema, ‘Alama sita zitaonekana kabla ya siku ya Qiyama. Wakati watu watakapokuwa masokoni mwao.’ Ghafla mwangaza wa jua utaondoka na wakati wao wamo katika hali hiyo zitaanguka nyota na yataanguka majabali juu ya uso wa ardhi. Kwa hiyo itatilifika na itatetemeka na itachanganyika. Watafadhaika majini kuelekea kwa watu na watu nao watafadhaika wakielekea kwa majini; na watachanganyika wanyama na ndege na wanyama wa porini watazongana wenyewe kwa wenyewe.

وَإِذَا الْوُحُوشُ حُشِرَتْ ﴿٦٢﴾

“**Na wanyama wa mwituni wakakusanywa.**”

Amesema, ‘watakapochanganyika.’

وَإِذَا الْعِشَارُ عُطِّلَتْ ﴿٦٣﴾

“**Na ngamia wenye mimba pevu watakapochwa wasishughulikiwe.**”

Pasina mwenye kuwachinja. Amesema; watu watawatelekeza wamiliki wake.

وَإِذَا الْبِحَارُ سُجِّرَتْ ﴿٦٤﴾

“**Na bahari zikawaka moto.**”

¹ Fat’hul Al-Bari 6:343.

Amesema: watasema majini sisi tutawaleteeni habari. Amesema; wataenda baharini - ghafla wataikuta bahari ni moto unaowaka. Amesema wakati wao wakiwa katika hali hiyo ghafla itapasuka ardhi mpasuko mmoja tu kuelekea kwenye ardhi ya saba ya chini na pia itakwea kwenye Mbingu ya Saba ya Juu. Amesema wakati wao wakiwa katika hali hiyo, ghafla utawajia wao upepo mkali utawaua; ameyapokea hayo Ibnu Jariri رحمه الله تعالى¹ na hili ni tamko lake.

Kuondoshwa kwa Kuachwa Ngamia Wenye Mimba ya Miezi Kumi na Kukusanywa Wanyama.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذَا الْجِبَالُ سُيِّرَتْ ﴿٢٧﴾

“Na milima ikaondolewa.” Maana yake: Yatakapoondoka yakawa mbali na mahali pake na yatakapopeperushwa yakaiwacha ardhi ikiwa ni tambarare iliyo sawa sawa. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذَا الْعِشَارُ عُطِّلَتْ ﴿٢٨﴾

“Na ngamia wenye mimba pevu watakapoachwa wasishughulikiwe.”

Ikrimah na Mujahid wamesema maana yake ni, ‘Ngamia wenye mimba ya miezi kumi.’² Amesema Mujahid, ‘Watakapoachwa.’ Maana yake: Ni watakapotelekezwa.³ Ubayy bin Ka’ab, na Adh-Dhahak wamesema, ‘Watakapoachwa bila ya uangalizi na watu wake’. Ama Rabii bin Khuthaymi amesema kuwa ina maana ya, ‘hawakukamuliwa na hazikufungwa chuchu zake ili watoto wake wasiweze kunyonya, wameachwa na wenyewe.’⁴

Na akasema Adh-Dhahak kuwa, ‘Wameachwa hali ya kuwa hawana mchungaji.’⁵ Na maana katika maelezo yote haya yanakaribiana, na wanaokusudiwa katika ngamia ni wale ambao ni bora kwao na wenye mimba katika hao. Ambao imefikia mimba ya miezi kumi – na jina lake analoitwa nalo wakati huo kwa lugha ya kiarabu ni ‘ushraaa’ anapokuwa Ngamia mmoja.

¹ At-Tabari 24:237.

² At-Tabari 24:240.

³ At-Tabari 24:240.

⁴ At-Tabari 24:240.

⁵ At-Tabari 24:240.

Hataachwa kuwa anaitwa kwa jina hilo mpaka atakapozaa. Wameshughulika watu na ngamia hao katika kuwaangalia, kuwatunza na kunufaika nao baada ya kuwa ni watu wenye kupendezwa sana na ngamia hao. Wataacha kutokana na lile lililowapata miongoni mwa jambo kubwa sana lenye kufadhaisha, lenye kutisha nalo ni jambo la siku ya Qiyama na kufungamana kwa sababu zake na kutuka kwa mambo yake ya utangulizi. Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَإِذَا أَلْوَحُوشُ حَشِرَتْ ﴿٦٨﴾

“Na wanyama wa mwituni wakakusanywa.”

Maana yake: ‘Watakapojumuishwa’. Kama Alivyosema Allah تعالی:

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمَمٌ أَمْثَالُكُمْ ۚ مَا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ
مِنْ شَيْءٍ ۚ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ ﴿٦٩﴾

“Na hapana chochote chenye kutambaa katika ardhi wala ndege anayeruka kwa mbawa zake isipokuwa hivyo ni umma Mifano yenu hatukuacha katika kitabu kitu chochote. Kisha kwa Mola Wao Mlezi wanakusanywa.” (6:38)

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما vitakusanywa vitu vyote mpaka nzi. Ameyapokea haya Ibnu Abi Hatim رحمه الله تعالى.¹ Amesema Allah تعالی:

وَالطَّيْرَ مَحْشُورَةً ۚ

“Na ndege ni wenye kukusanywa.” (38:19) Maana yake: Wenye kujumuishwa.

Kuwashwa kwa Bahari

Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَإِذَا الْبِحَارُ سُجِّرَتْ ﴿٧٠﴾

“Na bahari zikawaka moto.” Amepokea Ibnu Jarir رحمه الله تعالى kutokana na Said bin Al-Musayyab amesema kuwa Ali رضي الله عنه alimuuliza siku moja mtu katika Mayahudi, ‘Iko wapi Jahannamu?’ Mtu Yule akajibu, ‘Iko baharini.’ Ali رضي الله عنه akasema naona kama vile si mkweli, kwani Bahari ni yenye kuwashwa moto.

¹ At-Tabari 24:240.

وَالْبَحْرِ الْمَسْجُورِ ﴿٦﴾

“Na bahari iliyojazwa.” (52:6) na

وَإِذَا الْبِحَارُ سُجِّرَتْ ﴿٧﴾

“Na bahari zikawaka moto.”¹

Na pindi bahari itakapowashwa moto yametangulia maelezo juu ya hilo katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَالْبَحْرِ الْمَسْجُورِ ﴿٦﴾

“Na bahari iliyojazwa.” (52:6)²

Kuchanganywa Nafsi

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذَا النُّفُوسُ رُوِّجَتْ ﴿٧﴾

“Na roho zikaunganishwa na kiwiliwili.” Maana yake: Pindi litakapokusanywa kila umbile kwenye mfano wake. Kama Kauli Yake Allah تعالى:

﴿ أَحْشُرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ

“Wakusanyeni wale waliyodhulumu na wenza wao.” (37:22) Amepokea Ibnu Abi Hatim رضي الله عنه kutoka kwa An-Numaan bin Bashir رحمه الله تعالى kwamba yeye amesema Mtume ﷺ, amesema;

﴿ وَإِذَا النُّفُوسُ رُوِّجَتْ ﴾ ﴿٧﴾ الضَّرَبَاءُ: كُلُّ رَجُلٍ مَعَ كُلِّ قَوْمٍ كَانُوا يَعْمَلُونَ عَمَلَهُ وَذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ يَقُولُ: ﴿وَكُنْتُمْ أَزْوَاجًا ثَلَاثَةً﴾ ﴿٧﴾ فَأَصْحَابُ الْيَمِينِ مَا أَصْحَابُ الْيَسْمِينِ ﴿٨﴾ وَأَصْحَابُ الْمَشْأَمِ مَا أَصْحَابُ الْمَشْأَمِ ﴿٩﴾ وَالسَّيِّئُونَ السَّيِّئُونَ ﴿١٠﴾ هُمْ الضَّرَبَاءُ»

“Na nafsi zikaunganishwa.” hao ni watu wa namna moja na watu ambao walikuwa wanatenda matendo yake na hilo ni kwa sababu ya kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema, “na mkawa ni Mbeya tatu. Watu wa upande wa kulia, ni wapi watu wa upande

¹ Al-Qurtubi 19:229.

² At-Tabari 24:242.

³ Angalia juzuu ya 8, Tafsiri ya Surat At-Tur (52:6).

wa kulia; na watu wa upande wa kushoto, ni wapi watu wa upande wa kushoto? Na wenye kutangulia wenye kutangulia” (56:7-10). Amesema hao ni watu wa namna moja.¹

Kuulizwa Mtoto Mwanamke Aliyezikwa Hali yu Hai

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذَا الْمَوْءُدَةُ سُئِلَتْ ﴿١﴾ بِأَيِّ ذَنْبٍ قُتِلَتْ ﴿٢﴾

“Na msichana aliyezikwa hai atapoulizwa kwa kosa gani aliuliwa?”

Na *“Mauudah”* Ni binti ambaye walikuwa watu wa Jahilia kabla ya Uislamu wanamfukia katika mchanga kwa kuwachukia watoto wa kike. Ama siku ya Qiyama ataulizwa ni kwa dhambi gani aliuliwa? Ili iwe ni kitisho kwa yule Muuaji wake, kwani atakapoulizwa mwenye kudhulumiwa unahisi ni hisia gani atakayokuwa nayo mwenye kudhulumu? Amesema Ali bin Abi Twalha kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما,

وَإِذَا الْمَوْءُدَةُ سُئِلَتْ ﴿٣﴾

“Na msichana aliyezikwa hai atapoulizwa.”

Maana yake: Atakapoulizwa. Na kama hivi amesema Abu Adh-Dhuha atakapouliza maana yake: ‘Atakapodai damu yake’.² Na yamepokewa kutokana na As-Sudiy na Qatadah na mfano wake.

Na zimekuja Hadithi nyingi zinazofungamana na mtoto mwanamke aliyezikwa na hali ya kuwa yu hai. Amepokea Al-Imamu Ahmad kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kutokana na Judhama binti Wahb, dada yake ‘Ukasha amesema, ‘Mtume ﷺ alifika kwa watu akawa anasema,

«لَقَدْ هَمَمْتُ أَنْ أَنْهَى عَنِ الْغِيَلَةِ فَنَظَرْتُ فِي الرُّومِ وَفَارِسَ، فَإِذَا هُمْ يُبْيِلُونَ
أَوْلَادَهُمْ، وَلَا يَضُرُّ أَوْلَادَهُمْ ذَلِكَ شَيْئًا»

“Kwa hakika nilikusudia kuwakataza kuwanyonyesha watoto wenu

¹ At-Tabari 24:245. Isnadi ya masimulizi haya si sahihi. Kabla ya masimulizi haya, At-Tabari ameandika Isnadi sahihi yenye sehemu kubwa ya maneno kutoka kwa ‘Umar, Allah awe radhi naye.

² At-Tabari 24:246.

na hali mama zao ni wajawazito, lakini nilipowatazama wafursi na Warumi nikawaona wao wanawanyonyesha watoto wao na hali ya kuwa mama zao ni wajawazito na hilo halikuwadhuru watoto chochote”.

Kisha wakamuuliza kuhusu kumwaga mbegu za uzazi nje ya mfuko wa kizazi akasema Mtume ﷺ:

«ذَلِكَ الرَّأْدُ الْخَنِيْ، وَهُوَ الْمَرْوَدَةُ سُبُلَتْ»

“Huko ni kumzika mtoto kulikojificha na hivyo ni mtoto aliyezikwa mzima atakapoulizwa.”¹

Imepokewa na Muslim na Ibnu Majah na Abu Dawud na Tirmidhi na An-Nasai.²

Kafara la kuwazika Mabinti na Hali Wakiwa Hai

Amesema Abdul-Razzaq ametueleza Israil kutoka kwa Simak bin Harb, kutoka kwa An-Nuuman bin Bashir kutoka kwa Umar bin Al-Khattawab رضي الله عنه kuhusu Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذَا الْمَوْءِدَةُ سُبُلَتْ ﴿٨١﴾

“Na msichana aliyezikwa hai atapoulizwa.”

Amesema alikuja Qais bin ‘Aasim رضي الله عنه kwa Mtume ﷺ akasema, ‘Ee Mjumbe wa Allah hakika mimi niliwazika mabinti wangu wakiwa wazima katika zama za Jahilia.’ Mtume ﷺ akamuambia,

«أَغْنِيَّ عَنْ كُلِّ وَاحِدَةٍ مِنْهُنَّ رَقَبَةٌ»

“Mwache huru mtumwa kwa kila mmoja katika wao.”

Akasema Qais رضي الله عنه, ‘Ewe Mjumbe wa Allah hakika mimi ni mwenye ngamia.’ Akasema:

«فَأَنْحَرُ عَنْ كُلِّ وَاحِدَةٍ مِنْهُنَّ بَدَنَةٌ»

“Mchinjie kila mmoja wao ngamia.”³

¹ Ahmad 6:434.

² Muslim 2:1066, 1067, Ibn Majah 1:648, Abu Dawud 3:211, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:249, na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:106.

³ Abdur-Razzaq 3:351.

Kufunuliwa kwa Madaftari ya Matendo

Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَإِذَا الصُّحُفُ نُشِرَتْ ﴿١١﴾

“Na madaftari yatakapoenezwa.” Amesema Adh-Dhahaak atakapopewa kila mtu daftari lake kwa mkono wake wa kulia au wa kushoto. Na amesema Qatadah: ‘Ee mwanadamu unajaza katika daftari hilo kisha litakunjwa kisha litakunjuliwa siku za Qiyama basi na ayachunguze mtu yale anayoyajaza katika daftari lake.’¹

Kuondolewa Mbingu, Kuwashwa Moto na Kusogezwa Pepo.

Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَإِذَا السَّمَاءُ كُشِطَتْ ﴿١٢﴾

“Na mbingu itapotanduliwa.” Amesema Mujahid - zitakapovutwa.² Na amesema As-Ssudiy - itakapofunuliwa. Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَإِذَا الْجَحِيمُ سُعِرَتْ ﴿١٣﴾

“Na Jahannamu itapochochewa.” Amesema As-Suddi - utakapowashwa. Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَإِذَا الْجَنَّةُ أُنزِلَتْ ﴿١٤﴾

“Na Pepo ikasogezwa.” Amesema Adh-Dhahak na Abu Maliki na Qatada na Rabi bin Khuthaim: Maana yake: itakaposogezwa kwa watu wake.

Kila Mmoja Anajua Siku ya Qiyama Yale Aliyoyahudhurisha

Na Kauli Yake Allah تعالی:

عَلِمَتْ نَفْسٌ مَّا أَحْضَرَتْ ﴿١٥﴾

“Kila nafsi itajua ilichokihudhurisha.”

Hili ndilo jibu. Maana Yake: Yatakapotuka mambo haya wakati huo, Itajua kila nafsi yale iliyoyatenda na yakahudhurishwa hayo kwa ajili yake. Kama Alivyosema Allah تعالی:

¹ At-Tabari 24:249.

² At-Tabari 24:249.

يَوْمَ تَجِدُ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ مِنْ خَيْرٍ مُّحَضَّرًا وَمَا عَمِلَتْ مِنْ سُوءٍ تَوَدُّ لَوْ أَنَّ بَيْنَهَا
وَبَيْنَهُ أَمَدًا بَعِيدًا^١

“Siku ambayo itakuta kila nafsi yale iliyoyatenda miongoni mwa kheri yamehudhurishwa na yale iliyoyatenda miongoni mwa uovu; itatamanisha kwamba pana kati yake na kati ya hayo matendo masafa ya mbali sana.” (3:30).

Na Amesema Allah تعالى:

يُنَبِّئُوا الْإِنْسَانَ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ

“Ataelezwa binadamu siku hiyo yale aliyoyatanguliza na aliyoyachelewesha” (75:13).

فَلَا أُقْسِمُ بِالْخُنُوسِ ﴿١﴾ أَجْوَارِ الْكُنُوسِ ﴿٢﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا عَسْعَسَ ﴿٣﴾ وَالصُّبْحِ إِذَا
تَنَفَّسَ ﴿٤﴾ إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿٥﴾ ذِي قُوَّةٍ عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ ﴿٦﴾ مُطَاعٍ
ثُمَّ أَمِينٍ ﴿٧﴾ وَمَا صَاحِبُكُمْ بِمَجْنُونٍ ﴿٨﴾ وَلَقَدْ رَآهُ بِالْأُفُقِ الْمُبِينِ ﴿٩﴾ وَمَا هُوَ عَلَى
الْغَيْبِ بِضَنِينٍ ﴿١٠﴾ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَيْطَانٍ رَجِيمٍ ﴿١١﴾ فَأَيْنَ تَذَهَبُونَ ﴿١٢﴾ إِنَّ هُوَ إِلَّا
ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿١٣﴾ لِمَنْ شَاءَ مِنْكُمْ أَنْ يَسْتَقِيمَ ﴿١٤﴾ وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ
الْعَالَمِينَ ﴿١٥﴾

15. Naapa kwa sayari zinaporejea nyuma,

16. Zinazokwenda, kisha zikajificha,

17. Na kwa usiku unapopungua,

18. Na kwa asubuhi inapopambazuka,

19. Kwamba hakika bila ya shaka hii ni kauli ya Mjumbe Mtukufu,

20. Mwenye nguvu na mwenye cheo kwa huyo Mwenye Kiti cha Enzi,

21. Anaye t'iiwa, tena Muaminifu.
22. Na wala huyu mwenzenu hana wazimu.
23. Na hakika yeye alimuona kwenye upeo wa macho uliosafi.
24. Wala yeye si bakhili kwa mambo ya ghaibu.
25. Wala hii si kauli ya Shetani maluuni.
26. Basi mnakwenda wapi?
27. Haikuwa hii ila ni ukumbusho kwa walimwengu wote.
28. Kwa yule miongoni mwenu anayetaka kwenda sawa.
29. Wala nyinyi hamtataka isipokuwa Atake Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.

Tafsiri ya Al-Khunnasi na Al-Kunnasi

Amepokea Muslim katika sahihi yake na An-Nasai katika tafsiri yake kwenye aya hii kutoka kwa Amri bin Huraithi رضي الله عنه kuwa amesema: "Nilisali nyuma ya Mtume ﷺ Sala ya Asubuhi, akasoma,

فَلَا أُقْسِمُ بِالْخُنَّسِ ﴿٥٠﴾ الْجَوَارِ الْكُنَّسِ ﴿٥١﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا عَسَسَ ﴿٥٢﴾ وَالصُّبْحِ إِذَا تَنَفَّسَ ﴿٥٣﴾

"Naapa kwa sayari zinaporejea nyuma. Zinazokwenda, kisha zikajificha. Na kwa usiku unapopungua. Na kwa asubuhi inapo pambazuka."¹

Ibnu Jarir رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Khalid bin 'Ar-ara, kuwa amesema, nilimsikia Ali رضي الله عنه amesema baada ya kuulizwa maana ya aya hii kuhusu;

فَلَا أُقْسِمُ بِالْخُنَّسِ ﴿٥٠﴾ الْجَوَارِ الْكُنَّسِ ﴿٥١﴾

"Naapa kwa sayari zinaporejea nyuma. Zinazokwenda. kisha zikajificha."

¹ Muslim 1:336, na An-Nasai katika Al-Kubra 6:507.

Alijibu kwa kusema, 'Hizo ni nyota zinarudi nyuma mchana na usiku.'¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَاللَّيْلِ إِذَا عَسَسَ ﴿٧﴾

"Na kwa usiku unapopungua"

Pana kauli mbili: Moja ya kauli hizo: Ni kuja kwake na kiza chake, amesema Mujahid: Umefunga kiza, na amesema Saiid bin Jubair: Pindi utakapoanza. Ama Al-Hassan al-Basry رحمه الله تعالى amesema, 'Utakapofunika watu.'² na vivyo hivyo amesema 'Atwiyya Al-Awfi'³ na Ali bin Abi Twalha na Al-Awfi kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما kuwa,

إِذَا عَسَسَ ﴿٧﴾

"Unapopungua."

Kutakapokuwa kunaondoka.⁴ Na kama hivyo amesema Qatadah, na Mujahid na Adh-Dhahak.⁵ Na kama hivyo amesema Zaid bin Aslam na mtoto wake AbduRrahman.

إِذَا عَسَسَ ﴿٧﴾

"Unapopungua."

Maana yake: Pindi utakapoondoka na ukaenda zake.¹

Na kwangu mimi ni kwamba kusudio la Kauli Yake:

إِذَا عَسَسَ ﴿٧﴾

"Unapopungua."

Utakapokuwa unakuja ijapokuwa kunafaa kulitumia neno 'As'asa kwa maana ya kuondoka vilevile, isipokuwa maana ya 'kuja' hapa ina muiano zaidi. Kana kwamba Allah تعالى Ameapa kwa usiku na kiza chake pindi unapokuja na kwa Alfajiri na mwangaza wake, pindi unapoangaza. Kama Alivyosema Allah تعالى:

¹ At-Tabari 24:251.

² At-Tabari 24:256.

³ At-Tabari 24:256.

⁴ At-Tabari 24:255.

⁵ At-Tabari 24:256.

⁶ At-Tabari 24:256.

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿١﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّىٰ ﴿٢﴾

“Naapa kwa usiku pindi unapofunika kila kitu. Na mchana pindi unapodhihiri” (92:1-2)

Na Amesema Allah تعالى:

وَالضُّحَىٰ ﴿١﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٢﴾

“Naapa kwa wakati wa Dhuha. Na usiku pindi unapofunika kwa kiza.” (93:1-2)

Na Amesema Allah تعالى:

فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا

“Mwenye kuipasha asubuhi na Ameufanya usiku kuwa ni wakati kwa matulizano.” (6:96)

Na zisizokuwa hizo miongoni mwa aya mbalimbali. Na wamesema wengi katika wanazuoni wa somo la kanuni na misingi ya kisharia *“Al-Usuul”*.

Hakika tamko *“As’asa”* linatumiwa kwa maana ya kuja na kuondoka kwa pamoja na juu ya maelezo hayo kunasihi kukusudiwa maana zote mbili na Allah تعالى Ndiye Anayejua zaidi.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَالصُّبْحِ إِذَا تَنَفَّسَ ﴿١﴾

“Na kwa asubuhi inapopambazuka”

Amesema Adh-Dhahaak. Pindi inapochomoza na amesema Qatadah: itakapoangaza na ikaja.¹

¹ At-Tabari 24:258.

Qur'ani Ameshuka nayo Jibril عليه السلام na Sio Matokeo ya Wendawazimu.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿٥١﴾

“Kwamba hakika bila ya shaka hii ni kauli ya Mjumbe mtukufu.”

Anakusudia kwamba hii Qur'ani ni kufikisha ujumbe mtukufu maana Malaika Mtukufu, Mwenye tabia Njema, mzuri wa mtazamo, naye, ni Jibril عليه السلام. Ameyasema haya Ibnu Abbas na As-sha'bi na Maymum bin Maharan na Al-Hassan na Qatadah na Al-Rabii bin Anas na Adh-Dhahak, na wengine رضي الله عنهم.¹

ذِي قُوَّةٍ

“Mwenye nguvu.”

Ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَى ﴿٥٢﴾ ذُو مِرَّةٍ

**“Amemfundisha mwenye nguvu kubwa sana. Mwenye Kutua...”.
(53:5-6)**

Mwenye nguvu mno. Maana mwenye umbo lenye Nguvu kubwa.

عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ ﴿٥٣﴾

“Na mwenye cheo kwa huyo Mwenye Kiti cha Enzi”

Maana yake: Ana cheo mbele ya Allah تعالى, Mwenye Kushinda, Mwenye Kutukuka, cheo cha juu,

مُطَاعٍ ثَمَّ

“Anayetiwa, huko tena...”.

Maana yake: Ana Hadhi, neno lake ni lenye kusikilizwa. Naye ni mwenye kutiwa katika hadhara za juu zaidi (za Malaika). Qatadah amesema:

¹ Al-Qurtubi 19:240 na Ad-Durr Al-Manthur 8:433.

مُطَاعِثٌ

“Anaye tiiwa, huko tena ...”.

Maana yake: Katika Mbingu. Anakusudia kwamba yeye si katika Malaika wasiojulikana, bali yeye ni katika mabwana watukufu, amependelewa, ana cheo na yeye ni mwenye kusikilizwa, ameteuliwa kubeba wadhifa huu mkubwa. Amesema hayo Qatadah. Na Kauli Yake Allah تعالى:

أَمِينٍ

“Tena muaminifu” Muaminifu. Hapa anasifiwa Jibril عليه السلام kwa uaminifu. Na hili ni jambo kubwa sana kwamba Mola Mwenye Kushinda na Utukufu Anamtakasa mja Wake na Mjumbe Wake - malaika Jibril عليه السلام. Kama alivyomtakasa Mjumbe wake wa kibinadamu Muhammad ﷺ kwa Kauli Yake Allah تعالى. **“Na hakuwa jamaa yenu ni mwenda wazimu.”** amesema Al-sha’bi na Maymun bin Malirani, na Abu Swaleh na tuliowataja ambao umetangulia utaji wao. Maana ya Kauli Yake Allah تعالى:

وَمَا صَاحِبُكُمْ بِمَجْنُونٍ

“Na wala huyu mwenzenu hana wazimu.”

Anamkusudia Muhammad ﷺ¹ na Kauli Yake Allah تعالى:

وَلَقَدْ رَءَاهُ بِالْأُفُقِ الْمُبِينِ

“Na hakika yeye alimuona kwenye upeo wa macho uliosafi.”

Anakusudia kwa hakika Muhammad ﷺ alimuona Jibril عليه السلام ambaye anamletea ujumbe kutoka kwa Allah عزوجل, juu ya sura ambayo Alimuumba Allah تعالى juu ya Sura hiyo akiwa ana mbawa mia sita.

بِالْأُفُقِ الْمُبِينِ

“Upeo wa macho ulio safi.” Maana yake: Zilizo wazi na huo ndiyo uonaji wa kwanza ambao ulikuwa huko Makkah na uonaji huo ndiyo uliotajwa katika Kauli Yake.

¹ Al-Twabari 24:259 na Ad-Durr Al-Manthur 8:434.

عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَى ﴿٥٠﴾ ذُو مِرَّةٍ فَاسْتَوَى ﴿٥١﴾ وَهُوَ بِالْأُفُقِ الْأَعْلَى ﴿٥٢﴾ ثُمَّ دَنَا
فَتَدَلَّى ﴿٥٣﴾ فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَى ﴿٥٤﴾ فَأَوْحَى إِلَى عَبْدِهِ مَا أَوْحَى ﴿٥٥﴾

“Amemfundisha mwenye nguvu kubwa, mwenye nguvu akalingana sawa. Na hali ya kuwa yeye yuko katika pambizo za mbingu za juu. Kisha akakaribia sana akawa kiasi cha pinde mbili au karibu zaidi kuliko hivyo. Akayafikisha kwa njia ya wahyi yale aliyoyafikisha.” (53:5-10)

Kama ilivyotangulia tafsiri ya maneno hayo na uthibitisho wake, na dalili juu ya hilo kwamba kusudio ya maelezo hayo ni Jibril عليه السلام. Na ilivyo wazi na Allah تعالى Anajua zaidi, ni kwamba sura hii ilishuka kabla ya ule usiku aliopelekwa Mtume ﷺ mbinguni. Kwa sababu haukutajwa ndani yake isipokuwa uonaji huu nao ni wa kwanza. Ama wa pili ni ule uliyotajwa katika Kauli ya Allah تعالى:

وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَى ﴿٥٦﴾ عِنْدَ سِدْرَةِ الْمُنْتَهَى ﴿٥٧﴾ عِنْدَهَا جَنَّةُ الْمَأْوَى ﴿٥٨﴾ إِذْ
يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَى ﴿٥٩﴾

“Na kwa hakika alimuona mara nyingine na mbele ya Sidrat-Al-Muntaha mbele zake inapatikana pepo ya ukazi. Wakati yanaufunika mkunazi yale yaliyoufunika uonaji huo.” (53:13-16)

Hakika si vingine uonaji huo umetajwa katika Surat An-Najm na imeshuka baada ya Suratu Al-Israa.

Hakuwa Mtume ﷺ ni Bakhili katika Kuufikisha Wahyi

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَمَا هُوَ عَلَى الْغَيْبِ بِضَبِينٍ ﴿٦٠﴾

“Wala yeye si bakhili kwa mambo ya ghaibu.”

Maana yake: Hakuwa Muhammad ﷺ kwa yale yaliyoteremshwa kwake, ni bakhili. Maana: Mwenye kutuhumiwa. Bali anaitoa kwa kila mmoja. Amesema Sufyan bin Uyayna, kwa maana hakuwa muongo na hakuwa muovu.¹

¹ At-Tabari 24:261.

Na amesema Qataadah: Ilikuwa Qur’ani ni ghaibu kitu kilichojificha kuwepo machoni pa watu Akaiteremsha Allah تعالى juu ya Muhammad ﷺ hakufanya ubakhili kwayo kwa watu, bali alieneza na akaifikisha na akaitoa kwa kila mwenye kuitaka.¹

Na kama hivyo amesema Ikrima na Ibni Zaid na wengine. Na ameridhia Ibnu Jarir رحمه الله تعالى maana ya Bakhili.²

Mimi nasema maana mbili zote ni sahihi zimepokelewa kutoka kwa Mtume ﷺ. Kama ilivyotangulia.

Qur’ani ni Ukumbusho kwa Walimwengu na si Wahyi wa Shetani Aliyelaaniwa

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَيْطَانٍ رَّجِيمٍ ﴿٢٦﴾

“Wala hii si kauli ya Shetani maluuni.”

Maana: Haikuwa hii Qur’an ni maneno ya shetani aliyewekwa mbali na rehema za Allah تعالى. Maana yake: Hawezi kuichukuwa wala haitaki na haitakikani iwe kwake yeye. Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَمَا تَزَلَتْ بِهِ الشَّيْطَانُ ﴿٢٧﴾ وَمَا يُنْفِئُ هُمْ وَمَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٢٨﴾ إِنَّهُمْ عَنِ السَّمْعِ لَمَعَزُولُونَ ﴿٢٩﴾

“Wala Mashet’ani hawakuteremka nayo. Wala haitakiwi kwao, na wala hawawezi.” (26:210-212)

Na Kauli ya Allah تعالى:

فَأَيْنَ تَذْهَبُونَ ﴿٣٠﴾

“Basi mnakwenda wapi?”

Maana yake: Zinaelekea wapi akili zenu katika kuikadhibisha Qur’an pamoja na uwazi wake, na kudhihiri kwake na kuibanisha kwake ni haki itokayo mbele

¹ At-Tabari 24:261.

² At-Tabari 24:260, 261, na Ad-Durr Al-Manthur 8:435.

ya Allah تعالى Mwenye Kushinda, Mwenye Kutukuka. Kama Alivyosema Asswidiq رضي الله عنه kwa ujumbe wa watu wa Bani Khanifa wakati walipokuja hali ya kuwa ni Waislamu na akaamrisha na wakamsomea kitu katika Qur'an ya Musaylimatul mzandiki ambayo iko katika ukomo wa uropokaji na uduni wa muundo wa maneno yake. Akasema Abubakar رضي الله عنه, 'Vipi nyie akili zenu zimesafiri kwenda wapi! Na hapa maneno haya hayakutoka kabisa kwa Allah تعالى."

فَأَيُّنَ تَذْهَبُونَ ﴿٨١﴾

"Basi mnakwenda wapi?"

Maana yake: Mnaelekea wapi mkikiacha kitabu cha Mwenyezi Mungu na kumtii Yeye. Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿٨٢﴾

"Haikuwa hii ila ni ukumbusho kwa walimwengu wote."

Maana yake: Qur'an hii ni ukumbusho kwa wanaadamu wote, hukumbushwa na kuonywa nayo,

لِمَنْ شَاءَ مِنْكُمْ أَنْ يَسْتَقِيمَ ﴿٨٣﴾

"Kwa yule miongoni mwenu anayetaka kwenda sawa."

Inamaanisha kuwa yeyote mwenye kutaka uongofu, basi ashikamane na Qur'an hii, kwani ndio uokovu na mwongozo wake. Hakuna uongofu kinyume na Qur'an.

وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٨٤﴾

"Wala nyinyi hamtataka isipokuwa Atake Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote."

Maana yake: Utashi hamjaachiwa nyinyi. Hivyo basi, yeyote anayetaka kuongoka ataongoka na anayetaka kupotea atapotea, bali yote haya ni kwa mujibu wa Utashi wa Allah تعالى na Yeye ni Bwana wa kila kiumbe.

Imepokewa na Sufiani Ath-Thawri رحمه الله تعالى kutoka kwa Sulayman bin Musa kuwa Aya hii ilipotremshwa,

لِمَنْ شَاءَ مِنْكُمْ أَنْ يَسْتَقِيمَ ﴿٨٣﴾

"Kwa yule miongoni mwenu anayetaka kwenda sawa."

Abu Jahl akasema: “Jambo liko juu yetu sisi, tukitaka tutanyooka, na tusipotaka hatutanyooka.” Hivyo, Allah تعالی Akateremsha Aya,

وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٨١﴾

“Wala nyinyi hamtataka isipokuwa Atake Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.”¹

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Al-Takwiir* na ni kwa Allah تعالی: tu Kusifiwa kwa Sifa Njema na Kuneemesha.

* * *

¹ At-Tabari 24:264. Hii Imepokewa na *Mursal*.

Tafsiri ya Suratul Infitwar

Sura ya 82

Iliteremshwa Makkah

Ubora wa *Suratul Infitar*

An-Nasai amepokea kutoka kwa Jabir رضي الله عنه amesema kuwa Alisimama Muadhi رضي الله عنه akasali Sala yake ya Isha ya mwisho akarefusha, akasema Mtume ﷺ,

«أَفْتَانُ أَنْتَ يَا مُعَاذُ؟ أَيْنَ كُنْتَ عَنِ سَبْحِ أَمْرِ رَبِّكَ الْأَعْلَى» ﴿وَالصَّحِينَ﴾ وَ ﴿إِذَا السَّمَاءُ
انْفَطَرَتْ﴾

“Ewe Muadhi unataka watu (waichukie Sala ya jamaa)? Kwanini usisome, ‘Sabbihisma Rabbiika-Al-aala’, ‘Waddhuha’ na ‘Idha Assamaun Fatwarat.’”¹

Na asili ya Hadithi hii imethibitishwa katika sahihi mbili² isipokuwa kutajwa kwa,

﴿إِذَا السَّمَاءُ انْفَطَرَتْ﴾

“Idh-Ssamaun Fatwarati”

Ni katika upokezi wa An-Nasaai peke yake. Na umetangulia katika upokezi wa Abdillah bin Umar رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ سَرَّهُ أَنْ يَنْظُرَ إِلَى الْقِيَامَةِ رَأْيَ عَيْنٍ فَلْيَقْرَأْ: ﴿إِذَا الشَّمْسُ كُوِّرَتْ﴾ وَ ﴿إِذَا السَّمَاءُ
انْفَطَرَتْ﴾ وَ ﴿إِذَا السَّمَاءُ انشَقَّتْ﴾»

“Yule ambaye kunamfurahisha kutizama Qiyama kama kwamba anakiona kwa macho, Na asome: ‘Idha Sshamsu kuwwirat’ na ‘Idha Assamaun – fatwarat’ na ‘Idha-Assamaun – Shaqqat’.”³

* * *

¹ An-Nasai *Al-Kubra* 6:508.

² *Fat’hul Al-Bari* 10:532, na Muslim 1:339.

³ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:252.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْاِنْفِطَارِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِذَا السَّمَاءُ أَنْفَطَرَتْ ﴿١﴾ وَإِذَا الْكُوَاكِبُ انْتَبَرَتْ ﴿٢﴾
 وَإِذَا الْبِحَارُ فُجِرَتْ ﴿٣﴾ وَإِذَا الْقُبُورُ بُعْثِرَتْ ﴿٤﴾ عَلِمْتَ
 نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ وَأَخَّرَتْ ﴿٥﴾ يَتَأْتِيَا الْإِنْسَانَ مِمَّا غَشَّى
 الْكَرِيمِ ﴿٦﴾ الَّذِي خَلَقَكَ فَسَوَّنَكَ فَعَدَلَكَ ﴿٧﴾
 فِي أَيِّ صُورَةٍ مَّا شَاءَ رَكَّبَكَ ﴿٨﴾ كَلَّا بَلْ تُكَذِّبُونَ
 بِالَّذِينَ ﴿٩﴾ وَإِنَّ عَلَيْكُمْ لَحَافِظِينَ ﴿١٠﴾ كِرَامًا كَاتِبِينَ ﴿١١﴾
 يَعْمُونَ مِمَّا تَفْعَلُونَ ﴿١٢﴾ إِنَّ الْأَبْرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ﴿١٣﴾ وَإِنَّ
 الْفُجَارَ لَفِي حَبِيمٍ ﴿١٤﴾ يَصَلُّونَهَا يَوْمَ الَّذِينَ ﴿١٥﴾ وَمَا هُمْ
 عَنْهَا بِغَائِبِينَ ﴿١٦﴾ وَمَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمَ الَّذِينَ ﴿١٧﴾ ثُمَّ مَا
 أَدْرَاكَ مَا يَوْمَ الَّذِينَ ﴿١٨﴾ يَوْمَ لَا تَمَلِكُ نَفْسٌ لِنَفْسٍ
 شَيْئًا ۗ وَالْأَمْرُ يَوْمَئِذٍ لِلَّهِ ﴿١٩﴾

إِذَا السَّمَاءُ أَنْفَطَرَتْ ﴿١﴾ وَإِذَا
 الْكُوَاكِبُ انْتَبَرَتْ ﴿٢﴾ وَإِذَا الْبِحَارُ
 فُجِرَتْ ﴿٣﴾ وَإِذَا الْقُبُورُ بُعْثِرَتْ ﴿٤﴾
 عَلِمْتَ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ وَأَخَّرَتْ ﴿٥﴾
 يَتَأْتِيَا الْإِنْسَانَ مِمَّا غَشَّى
 الْكَرِيمِ ﴿٦﴾ الَّذِي خَلَقَكَ
 فَسَوَّنَكَ فَعَدَلَكَ ﴿٧﴾ فِي أَيِّ صُورَةٍ
 مَّا شَاءَ رَكَّبَكَ ﴿٨﴾ كَلَّا بَلْ
 تُكَذِّبُونَ بِالَّذِينَ ﴿٩﴾ وَإِنَّ عَلَيْكُمْ
 لَحَافِظِينَ ﴿١٠﴾ كِرَامًا كَاتِبِينَ ﴿١١﴾
 يَعْمُونَ مِمَّا تَفْعَلُونَ ﴿١٢﴾

1. Mbingu zitakapopasuka .
2. Na nyota zitapotawanyika.
3. Na bahari zitakapopasuliwa.

4. Na makaburi yatapo fukuliwa.

5. Hapo kila nafsi itajua ilichotanguliza, na ilicho bakisha nyuma.

6. Ewe mwanaadamu! Nini kilichokughuri ukamuacha Mola Wako Mlezi Mtukufu?

7. Aliyekuumba, Akakuweka sawa, Akakunyooosha.

8. Katika sura yoyote Aliyoipenda Akakujenga.

9. Sivyoo hivyo! Bali nyinyi mnaikanusha Siku ya Malipo.

10. Na hakika bila ya shaka wapo walinzi juu yenu.

11. Waandishi wenye hishima.

12 Wanayajua mnayoyatenda.

Mambo Yatakayotokea Siku ya Kiyama

Anasema Allah تعالى:

إِذَا السَّمَاءُ أَنْفَطَرَتْ ﴿١﴾

“Mbingu zitakapopasuka.”

Maana yake: Kupasuka. Allah تعالى Amesema:

السَّمَاءُ مُنْفَطِرٌ بِهِ ۚ

“As-Samaau Munfatwirun bihi.” (73:18)

Halafu Anasema,

وَإِذَا الْكَوَاكِبُ انْتَثَرَتْ ﴿٢﴾

“Na nyota zitapotawanyika.”

Maana yake: Kuanguka,

وَإِذَا الْبِحَارُ فَجُورَتْ ﴿٣﴾

“Na bahari zitakapopasuliwa.” Amesema Ali bin Abi Twalha; kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما kuwa, ‘Atazipasua Allah تعالى baadhi yake katika baadhi’.¹ Na amesema Hassan “Atapasua Allah تعالى baadhi yake katika zingine yakaondoka maji yake”.² Na amesema Qatadah, yatachanganyika matamu yake kwa chumvi yake.³

وَإِذَا الْقُبُورُ بُعْثِرَتْ ﴿٤﴾

“Na makaburi yatapofukuliwa.”

¹ At-Tabari 24:267.

² At-Tabari 24:267.

³ At-Tabari 24:217.

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما: yatakapofukuliwa.¹ Na amesema As-Ssudi, yatatikisika, kutetemeka na kusababisha kutoka vilivyo ndani yake.

عَلِمَتْ نَفْسٌ مَا قَدَمَتْ وَأَخَّرَتْ ﴿٨٢﴾

“Hapo kila nafsi itajua ilichotanguliza, na ilichobakisha nyuma.”

Maana yake: Yatakapotimia haya ndio yatapatikana.

Hakutakikani kwa Mwanadamu Kumsahau Mwenyezi Mungu

Na Kauli Yake Allah تعالى:

يَتَأْتِيهَا الْإِنْسَانُ مَا عَرَّفَكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيمِ ﴿٨٣﴾

“Ewe mwanaadamu! Nini kilichokughuri ukamuacha Mola wako Mlezi Mtukufu?”

Maneno haya ni vitisho na karipio, sio kama wanavyoyadhania baadhi ya watu kuwa maneno haya ni maelekezo, kwa mwanadamu, au ni majibu ya kauli yake, wakati aliposema kuwa yeye ni mkarimu. Kiasi cha kusema msemaji wao: Umemhadaa Mwanadamu ukarimu wake, bali maana ya aya hii, ni ‘Jambo gani lililokuhadaa Ewe mwanadamu kwa Mola wako Aliye Mtukufu mpaka ukafanya ujasiri wa kumkabili Mola wako, hali ya kuwa umefanya maasi na mambo yasiyotakikana.’ Kama ilivyokuja katika Hadithi.

«يَوْمَ اللهُ تَعَالَى يَوْمَ الْقِيَامَةِ: يَا ابْنَ آدَمَ مَا عَرَّفَكَ بِي؟ يَا ابْنَ آدَمَ مَاذَا أَجَبْتَ الْمُرْسَلِينَ؟»

“Atasema Mwenyezi Mungu siku ya Qiyama, ‘Ewe Mwanadamu kitu gani kilikuhadaa ukaniacha mimi?’ Ewe mwanaadamu uliwajibu nini Mitume yetu tuliyoituma!”²

Na amesimulia Baghawiy kutoka kwa Kalb na Muqatil kwamba kwao wamesema: Aya hii ilimshukia Al-Aswad bin Shariq alimpinga Mtume ﷺ na hakuadhibiwa wakati uleule, na katika hali iliyokuwepo akateremsha Allah تعالى:

¹ At-Tabari 24:267.

² Tuhfat Al-Ashraf 7:70. Hii ni rejea tu ya Hadithi, hivyo usahihi wake haukuthibitishwa.

مَا عَرَكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيمِ ﴿٧﴾

“Nini kilichokughuri ukamuacha Mola Wako Mlezi Mtukufu?”¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

الَّذِي خَلَقَكَ فَسَوَّنَكَ فَعَدَلَكَ ﴿٧﴾

“Aliyekuumba, Akakuweka sawa, Akakunyoosha.”

Maana yake: Ni nini kilichokuhadaa kwa Mola Wako Mlezi Mtukufu

الَّذِي خَلَقَكَ فَسَوَّنَكَ فَعَدَلَكَ ﴿٧﴾

“Aliyekuumba, Akakuweka sawa, Akakunyoosha.”

Maana yake: Amekuumba sawasawa umekamilika, mwenye kunyooka na kulingana kimo chako, mwenye kunyooka katika umbile zuri na ubora wa mandhari.

Amepokea Al-Imamu Ahmad kutoka kwa Bushri bin Jihaashi Al-Qurashi kuwa Mtume ﷺ alitema mate siku moja katika kiganja chake kisha akaweka juu kidole chake kisha akasema,

«قَالَ اللهُ عَزَّ وَجَلَّ: يَا ابْنَ آدَمَ أَنَّى تُعْجِزُنِي وَقَدْ خَلَقْتُكَ مِنْ مِثْلِي هَذِهِ؟ حَتَّى إِذَا سَوَّيْتُكَ وَعَدَلْتُكَ مَسَّيْتَ بَيْنَ بُرْدَيْنِ، وَلِلْأَرْضِ مِنْكَ وَبَيْدٌ، فَجَمَعْتَ وَمَنَعْتَ حَتَّى إِذَا بَلَغْتَ التَّرَافِي قُلْتَ: أَنَصَدُّ وَأَنَّى أَوَانُ الصَّدَقَةِ؟»

“Mwenyezi Mungu Mwenye Kushinda na Kutukuka Amesema,; “Mwanadamu utanishinda vipi na hali Nimekuumba kutokana na mfano wa hiki?” Mpaka Nilipokuweka sawa na Nikakulinganisha ukaenda kati ya nguzo mbili na hali ya kuwa ardhi inapiga kelele kutokana nawe ukakusanya na ukazuia mpaka mauti yalipokujia. Hapo ndipo utakaposema, “Ninatoa sadaka, uko wapi tena wakati wa kutoa sadaka?”²

Kama hivi amepokea Ibnu Majah.³ Na Kauli Yake Allah تعالى

¹ Al-Baghawi 4:455. Hii Imepokewa na Mursal.

² Ahmad 4:210.

³ Ibn Majah 2:903.

﴿ فِي أَيِّ صُورَةٍ مَا شَاءَ رَكَّبَكَ ﴾

“Katika sura yoyote Aliyoipenda Akakujenga.”

Amesema Mujahid, katika kushabihiana na yeyote, Baba, Mama au Mjomba au Ammi.¹ Na imekuja katika sahihi mbili kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه kuwa mtu mmoja alilalamika, ‘Ewe Mjumbe wa Allah: Hakika mke wangu amezaa mtoto mweusi.’ Mtume ﷺ akamuuliza:

«هَلْ لَكَ مِنْ إِبِلٍ؟»

“Jee una ngamia.”

Akajibu, ‘ndiyo.’ Akamuuliza:

«فَمَا أَلْوَانُهَا»

“Rangi zao ni zipi?”

Akajibu, ‘mwekundu.’ Akamuuliza:

«فَهَلْ فِيهَا مِنْ أَوْزَقٍ»

“Jee pana wenye rangi nyeusi na za kijivu?”

Akajibu, ‘Ndiyo.’ Akamuuliza,

«فَأَنَّى آتَاهَا ذَلِكَ»

“Ni kutoka wapi wamejiwa na rangi hizo?”

Akajibu; ‘Huenda ni ambukizo kutoka katika mshipa wa asili.’ Hapo Mtume ﷺ akasema,

«وَهَذَا عَسَى أَنْ يَكُونَ نَزْعُهُ عِرْقٌ»

“Na hii huenda ikawa ni ambukizo la mshipa wa asili.”²

¹ At-Tabari 24:270

² Fat’hul Al-Bari 9:351, na Muslim 2:1137

Sababu za Mtu Kuhadaika na Kuzindushwa Malaika Kwamba Huandika Matendo ya Wanadamu

Na Kauli Yake Allah تعالى:

كَلَّا بَلْ تُكَذِّبُونَ بِالَّذِينَ ﴿١٠﴾

“Sivyo hivyo! Bali nyinyi mnaikanusha Siku ya Malipo.”

Maana yake: Hakika hapana jambo lolote linalowafanya nyinyi kutokumkubali Mola Wenu Mkarimu. Kutomkubali Yeye kumewapelekea kumkabili Mkarimu na kumuelekea kwa kufanya maasi. Na hivyo ni kukadhibisha ndani ya nyoyo zenu, juu ya marejeo ya siku ya malipo na hesabu. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِنَّ عَلَيْكُمْ لَحَافِظِينَ ﴿١١﴾ كِرَامًا كَاتِبِينَ ﴿١٢﴾ يَعْمُونَ مَا تَفْعَلُونَ ﴿١٣﴾

“Na hakika bila ya shaka wapo walenzi juu yenu, Waandishi wenye hishima. Wanayajua mnayo yatenda.”

Anakusudia kwamba juu yenu kuna malaika watukufu wenye kuwalinda basi msiwakabili kwa matendo maovu. Kwani wao wanaandika matendo yenu yote.

إِنَّ الْأَبْرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ﴿١٤﴾ وَإِنَّ الْفُجَّارَ لَفِي حَجِيمٍ ﴿١٥﴾ يَصْلَوْنَهَا يَوْمَ الَّذِينَ ﴿١٦﴾ وَمَا هُمْ عَنْهَا بِغَائِبِينَ ﴿١٧﴾ وَمَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمَ الَّذِينَ ﴿١٨﴾ يَوْمَ لَا تَمْلِكُ نَفْسٌ لِنَفْسٍ شَيْئًا ۗ وَالْأَمْرُ يَوْمَئِذٍ لِلَّهِ ﴿١٩﴾

13. Hakika wema bila ya shaka watakuwa katika neema,

14. Na hakika waovu bila ya shaka watakuwa Motoni;

15. Wataingia humo Siku ya Malipo.

16. Na hawatoacha kuwamo humo.

17. Na nini kitakachokujulisha Siku ya Malipo ni siku gani?

18. Tena nini kitakachokujulisha Siku ya Malipo ni siku gani?

19. Siku ambayo nafsi haitakuwa na madaraka yoyote juu ya nafsi; na amri yote siku hiyo ni ya Mwenyezi Mungu tu.

Malipo ya Watu Wema na Waovu

Allah تعالی Anaeleza kuhusu mwisho wa watu wema ni neema. Nao ni wale ambao waliomtii Allah تعالی: Mwenye Kushinda na Kutukuka, na hawakumkabili kwa kufanya maasi. Kisha ametaja mwisho wa watu waovu kuwa ni moto na adhabu ya kudumu.

Kwa sababu hiyo Allah تعالی Amesema:

يَصْلَوْنَهَا يَوْمَ الدِّينِ ﴿١١﴾

“Wataingia humo Siku ya Malipo.”

Maana yake: Siku ya hesabu na malipo. Nayo ni siku ya Kiyama.

وَمَا هُمْ عَنْهَا بِغَائِبِينَ ﴿١٢﴾

“Na hawatoacha kuwamo humo.”

Kwa maana: Kwamba hawatapotea na hiyo adhabu, hata kwa saa moja, na wala hawatafanyiwa tahafifu adhabu yake na wala hawatajibiwa maombi yao, ya kutaka kufa au kupumzika ijapokuwa siku moja.

Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَمَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمَ الدِّينِ ﴿١٣﴾

“Na nini kitakachokujulisha Siku ya Malipo ni siku gani?”

Ni kuitukuza siku ya Qiyama kisha akasisitiza kwa Kauli Yake Allah تعالی:

ثُمَّ مَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمَ الدِّينِ ﴿١٤﴾

“Tena nini kitakachokujulisha Siku ya Malipo ni siku gani?”

Maana yake: Imefasiriwa na aya nyingine:

يَوْمَ لَا تَمْلِكُ نَفْسٌ لِّنَفْسٍ شَيْعًا ﴿١٥﴾

“Hataweza mtu yeyote juu ya kumnufaisha mtu yeyote.”

Wala kumuokoa na yale ambayo yamo ndani yake isipokuwa Allah تعالی Atatoa idhini kwa Anayemtaka na Kumridhia. Na tunataja hapa Hadithi hii:

«يَا بَنِي هَاشِمٍ، أَنْقِذُوا أَنْفُسَكُمْ مِنَ النَّارِ لَا أَمَلِكُ لَكُمْ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا»

“Enyi Bani Hashim Ziokoeni Nafsi zenu na moto, kwa hakika mimi siwezi kuwasaidia na kukuokoeni na adhabu ya moto.”¹

Na hili tulilitaja hapo nyuma katika Surat Ash-Shuaraa, na hivyo Amesema Allah تعالى:

وَالْأَمْرُ يَوْمَئِذٍ لِلَّهِ

“Na Amri yote siku hiyo ni ya Mwenyezi Mungu tu.”

Kama vile Kauli Yake,

لِمَنِ الْمُلْكُ الْيَوْمَ لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ

“...Ufalme ni wa nani leo? Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja Mwenye Nguvu (za Kufanya Atakalo).” (40:16)

Na Kauli Yake,

الْمَلِكُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ لِلرَّحْمَنِ

“Ufalme wa haki siku hiyo utakuwa wa Arrahman, Mwingi wa Rehema...” (25:26)

Ni Kama Kauli Yake,

مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ

“Mwenye Kumiliki Siku ya Malipo.”

Qatadah amesema,

يَوْمَ لَا تَمْلِكُ نَفْسٌ لِنَفْسٍ شَيْئًا وَالْأَمْرُ يَوْمَئِذٍ لِلَّهِ

“Siku ambayo nafsi haitakuwa na madaraka yoyote juu ya nafsi; na amri yote siku hiyo ni ya Mwenyezi Mungu tu.”

Na Amri siku hiyo ni ya Allah تعالى. Hakuna yeyote atakayeshindana na Allah تعالى siku hiyo.

Huu ni Mwisho wa tafsiri ya Surat Al-Infitwaar. Na Kuhimidiwa ni kwa Allah تعالى. Na ni Yeye Anayestahiki Kusifiwa.

* * *

¹ Muslim 1:193.

Tafsiri ya Suratul Mutaffifin

Sura ya 83

Iliteremshwa Madinah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُوْرَةُ الْمُتَفَفِّفِيْنَ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَيْلٌ لِّلْمُتَفَفِّفِيْنَ ﴿١﴾ الَّذِيْنَ إِذَا أَكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ
 يَسْتَوْفُونَ ﴿٢﴾ وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿٣﴾ أَلَا
 يَظُنُّ أُولَئِكَ أَنَّهُمْ مَبْعُوثُونَ ﴿٤﴾ لِيَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٥﴾ يَوْمٍ
 يَقُومُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعَالَمِيْنَ ﴿٦﴾ كَلَّا إِنَّ كِتَابَ الْفَجَارِ لَفِي
 سَجِيْنٍ ﴿٧﴾ وَمَا أَدْرَاكَ مَا سَجِيْنٌ ﴿٨﴾ كِتَابٌ مَّرْقُومٌ ﴿٩﴾
 وَيْلٌ لِّيَوْمِيَوْمٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿١٠﴾ الَّذِيْنَ يُكَذِّبُوْنَ بِيَوْمِ
 الَّذِيْنَ وَعَدْنَا وَمَا يُكذِّبُ بِهِ إِلَّا كُلُّ مُعْتَدٍ أَثِمٍ ﴿١١﴾ إِذَا تَنَتَلَى
 عَلَيْهِ ءَايَاتُنَا قَالَ أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِيْنَ ﴿١٢﴾ كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى
 قُلُوبِهِمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٣﴾ كَلَّا إِنَّهُمْ عَنْ رَبِّهِمْ يَوْمِيَوْمٍ
 لَّخَجُوبُونَ ﴿١٤﴾ ثُمَّ إِنَّهُمْ لَصَالُوا الْجَحِيْمِ ﴿١٥﴾ ثُمَّ يُقَالُ
 هَذَا الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿١٦﴾

وَيْلٌ لِّلْمُتَفَفِّفِيْنَ ﴿١﴾ الَّذِيْنَ إِذَا
 أَكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ ﴿٢﴾
 وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿٣﴾
 أَلَا يَظُنُّ أُولَئِكَ أَنَّهُمْ مَبْعُوثُونَ ﴿٤﴾
 لِيَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٥﴾ يَوْمٍ يَقُومُ النَّاسُ
 لِرَبِّ الْعَالَمِيْنَ ﴿٦﴾

1. Ole wao hao wapunjao!
2. Ambao wanapojipimia kwa watu hudai watimiziwe.
3. Na wao wanapo wapimia watu kwa kipimo au mizani hupunguza.
4. Kwani hawadhani hao kwamba watafufuliwa
5. Katika Siku iliyu kuu.
6. Siku watakaposimama watu kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote?.

Kuongeza na Kupunguza katika Kupima kwa Pishi au Mizani ndio Sababu ya Adhabu Kali na Kupata Hasara.

An-Nasai na Ibnu Majah wamepokea kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما kuwa amesema: Alipofika Mtume ﷺ Madina aliwakuta watu wa Madina ni waovu mno kuliko watu wote katika kupunja, Akateremsha Allah تعالى:

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ ﴿١٧﴾

“Ole wao hao wapunjao!”

Wakapima vizuri baada ya hapo.¹ Na makusudiwa ya kupunguza hapa ni kupunguza katika pishi na mizani. Ima iwe mtu anataka kuongezewa pindi atakapopimiwa au kuwapunguzia watu pindi atakapowapimia watu wengine. Kwa sababu hiyo, Allah تعالى Amewaonya wenye kupunguza, wale ambao Amewakemea kuwa watapata hasara na kuangamia, na hiyo ndiyo adhabu kali. Kwa Kauli Yake Allah تعالى:

الَّذِينَ إِذَا أَكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ

“Ambao wanapojipimia kwa watu.”

Maana yake: Kwa watu,

يَسْتَوْفُونَ ﴿١٨﴾

“Hudai watimiziwe.”

Maana yake: Huchukua haki zao na zaidi ya hapo, lakini,

وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿١٩﴾

“Na wao wanapowapimia watu kwa kipimo au mizani hupunguza.”

Kwa hakika, Ameamrisha Allah تعالى kukamilisha pishi na mizani Aliposema,

وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كَلَّمْتُمْ وَزَنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٢٠﴾

“Na timizeni kipimo mpimapo. Na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na khatimaye ndio bora.” (17:35)

¹ An-Nasai katika Al-Kubraa: 6:508 na Ibn Majah: 2:748.

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَالْمِيزَانَ بِالْقِسْطِ ۗ لَا تَكْفُفْ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۗ

“...Na timizeni vipimo na mizani kwa uadilifu. Sisi hatumkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake...”(6:152)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَقِيمُوا آلُوزْنَ بِالْقِسْطِ وَلَا تُخْسِرُوا الْمِيزَانَ ﴿٥٩﴾

“Na wekeni mizani kwa haki, wala msipunje katika mizani.” (55:9)

Na Akawaangamiza Allah تعالى watu wa Shuaib عليه السلام, na Aliwateketeza kutokana na vile walivyokuwa wakiwapunguzia watu katika mizani na vipimo.

Kuhofishwa Wapunguzaji Vipimo kuwa Watasimama Mbele ya Mola Mlezi wa Viumbe Wote.

Kisha Amesema Allah تعالى Akiwaonya,

أَلَا يَظُنُّ أُولَئِكَ أَنَّهُمْ مَبْعُوثُونَ ﴿٦٠﴾ لِيَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٦١﴾

“Kwani hawadhani hao kwamba watafufuliwa katika Siku iliyo kuu.”

Maana yake: Hivi hawaogopi hao kufufuliwa na kusimama mbele ya Anayezijua siri na dhamira za watu, katika siku yenye vituko vikubwa, yenye fazaa nyingi, yenye misiba mikubwa. Atakayepata hasara katika siku hiyo ataingizwa motoni - moto ulio mkali sana.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

يَوْمَ يَقُومُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٢﴾

“Siku watakaposimama watu mbele ya Mola Mlezi wa walimwengu wote?”

Maana yake: Watasimama hali ya kuwa wako pekupeku, wako uchi, hawakutahiriwa, katika kisimamo kigumu finyu na dhiki, chenye tabu, juu ya muovu na mwenye makosa.

Na litawafinika wao amri ya Allah تعالى jambo ambalo nguvu na hisia zitashindwa kutokana nalo jambo hilo.

Amepokea Imamu Malik kutoka kwa Nafii kutoka kwa Ibni Umar رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«يَوْمَ يَقُومُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ، حَتَّى يَغِيبَ أَحَدُهُمْ فِي رَشْحِهِ إِلَى أَنْصَابِ أذُنَيْهِ»

"Siku watakayosimama watu mbele ya Bwana wa viumbe - mmoja wao atafunikwa na Jasho lake, mpaka nusu ya masikio yake."

Ameipokea Al-Bukhari kutokana na Hadithi ya Maliki na Abdallah bin Aun, wote wawili hao wamepokea kutoka kwa Nafii.¹ Na vile vile ameipokea Muslim kutokana na njia zote mbili.²

(Hadithi nyengine) Ameipokea Imamu Ahmad kutoka kwa Al-Miqdad anamkusudia Ibni Al-Aswad Al-Kindy رضي الله عنه amesema: Nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

«إِذَا كَانَ يَوْمُ الْقِيَامَةِ أَذْنَيْتِ الشَّمْسِ مِنَ الْعِبَادِ حَتَّى تَكُونَ قَدَرِ مِيلٍ أَوْ مِيلَيْنِ - قَالَ - فَتَضَهُرُهُمُ الشَّمْسُ فَيَكُونُونَ فِي الْعَرَقِ كَقَدْرِ أَعْمَالِهِمْ، مِنْهُمْ مَنْ يَأْخُذُهُ إِلَى عَقَبِيهِ، وَمِنْهُمْ مَنْ يَأْخُذُهُ إِلَى رُكْبَتَيْهِ، وَمِنْهُمْ مَنْ يَأْخُذُهُ إِلَى حَقْوَيْهِ، وَمِنْهُمْ مَنْ يُلْجِمُهُ الْجَنَامَا»

"Itapokuwa siku ya Qiyama litasogezwa karibu jua kwa waja mpaka liwe kiasi cha maili moja au maili mbili - amesema - jua litawayeyusha watakuwa katika jasho kwa kiasi cha matendo yao, miongoni mwao wapo watakozibwa na jasho mpaka visigino vyake viwili, kuna katika wao watakozibwa mpaka magotini mwake, na miongoni mwao kuna litakayemchukua mpaka kiunoni mwake, na kuna ambaye litamfika mdomoni mwake kabisa." (Muslim na Tirmidhi).³

¹ Fat'hul Al-Bari 8:565.

² Muslim 4:2195, 2196.

³ Ahmad 6:3, Muslim 2864 na Tuhfatul Al-Ahwadhi 8:89.

Na katika Sunna za Abu Dawuud kuwa Mtume ﷺ alikuwa akijilinda kwa Allah تعالى na dhiki ya kusimama siku ya Kiyama.¹

Na imepokewa kutokana na Ibni Mas'ud رضي الله عنه kuwa, katika siku ya kiyama watasimama kwa muda wa miaka arobaini hali ya kuwa wamenyanyua vichwa vyao kuvielekeza mbinguni, hawasemeshwi na mtu yeyote, jasho limewafika mdomoni mwao, mwema wao na maovu wao."² Ama kutoka kwa Ibni Umar رضي الله عنهما anasema. 'watasimama kwa muda wa miaka mia moja.' Amezipokea njia zote mbili Ibni Jarir رحمه الله تعالى.³

Na katika Sunan za Abu Dawuud, An-Nasaai na Ibnu Majah kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kwamba Mtume ﷺ alikuwa anakianza kisimamo cha usiku akitoa takbira mara kumi na anamsifu Allah تعالى mara kumi na anamtakasia mara kumi na anamtaka msamaha mara kumi na anasema:

«اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَاهْلِي وَارْزُقْنِي وَعَافِنِي»

"Allahumma ghfir liy Wa-Ahdiniy War-zuqniy Wa-Afini."

Kwa Maana: 'Ewe Mola Wangu Mlezi Nisamehe mimi, Niongoze, Niruzuku na Unipe uzima."

Kisha baada ya hapo anajilinda kwa Allah تعالى na dhiki ya kisimamo cha siku ya Kiyama.⁴

كَلَّا إِنَّ كِتَابَ الْفُجَارِ لَفِي سَعِيرٍ ﴿١٠﴾ وَمَا أَدْرَاكَ مَا سَعِيرٌ ﴿١١﴾ كِتَابٌ مَّرْقُومٌ ﴿١٢﴾
 وَيَلُّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٣﴾ الَّذِينَ يَكْذِبُونَ بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿١٤﴾ وَمَا يُكْذِبُ بِهِ إِلَّا كُلٌّ ﴿١٥﴾
 مُعْتَدٍ أَثِيمٍ ﴿١٦﴾ إِذَا تَتَلَّى عَلَيْهِ ءَايَاتُنَا قَالَ أَسْطِيرُ الْأُولِينَ ﴿١٧﴾ كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى
 قُلُوبِهِمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٨﴾ كَلَّا إِنَّهُمْ عَنْ رَبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَمَحْجُوبُونَ ﴿١٩﴾ ثُمَّ إِنَّهُمْ
 لَصَالُوا الْجَحِيمِ ﴿٢٠﴾ ثُمَّ يُقَالُ هَذَا الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿٢١﴾

¹ Abu Dawuud 1:487.

² At-Tabari 24:281. Isnadi yake ni dhaifu Shariik bin Abdullah ana hifadhi mбая.

³ At-Tabari 24:280.

⁴ Abu Dawuud 1:486, An-Nasaai 3:299 na Ibn Majah 1:431.

7. Hakika maandiko ya wakosefu bila ya shaka yamo katika Sijjin

8. Unajua nini Sijjin?

9. Kitabu kilichoandikwa.

10. Ole wao siku hiyo kwa wanaokadhibisha!

11. Ambao wanaikadhibisha Siku ya Malipo.

12. Wala haikadhibishi ila kila mwenye kuruka mipaka, mwenye dhambi.

13. Anaposomewa Aya zetu husema: Ni visa vya watu wa kale!

14. Hasha! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao hao waliokuwa wakiyachuma.

15. Hasha! Hakika hao siku hiyo bila ya shaka watazuiliwa kumuona Mola Wao Mlezi.

16. Kisha wataingia Motoni!

17. Kisha waambiwe: Haya ndiyo mliyokuwa mkiyakadhabisha."

Kumbukumbu za Watu Waovu na Yale Yatakayotokea Kwao

Anasema Allah تعالى kwa ukweli kabisa:

كَلَّا إِنَّ كِتَابَ الْفُجَارِ لَفِي سِجِّينَ ﴿١٠﴾

"Hakika maandiko ya wakosefu bila ya shaka yamo katika Sijjin."

Maana yake: Hakika mwisho wao na makazi yao ni katika "Sijjin" Kwa maana ya kuwa watakuwa katika dhiki. Kwa sababu hiyo ndio maana Allah تعالى jambo Lake Amelifanya kubwa. Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَمَا أَدْرَاكَ مَا سِجِّينٌ ﴿١١﴾

"Unajua nini Sijjin?"

Maana yake: Hilo ni jambo kubwa sana, ni jela ya kudumu na adhabu yenye kutia chungu. Kisha wamesema wasemaji hiyo Sijjin iko chini ya ardhi ya saba yametangulia maelezo yake katika Hadithi ya Baraa bin Aazib katika Hadithi yake ndefu:

«يَقُولُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ فِي رُوحِ الْكَافِرِ اكْتُبُوا كِتَابَهُ فِي سِجِّينَ . وَسِجِّينُ هِيَ تَحْتُ الْأَرْضِ السَّابِعَةِ»

“Anasema Mwenyezi Mungu Aliyeshinda na Kutukuka, kuhusu roho ya kafiri: yaandikeni maandiko yake katika “Sijjini” na hiyo Sijjin ipo chini ya ardhi ya saba.”¹

Na yalipokuwa marejeo ya makafiri ni katika mioto ya Jahannam na moto wa Jahannam nao uko chini ya walio chini. Kama Alivyosema Allah تعالى:

ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿٥﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٦﴾

“Kisha Tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini! Lakini wale walio amini na wakatenda mema, hao watapata ujira usio kwisha.” (95:5-6)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

كَلَّا إِنَّ كِتَابَ الْفُجَارِ لَفِي سِجِّينَ ﴿٥﴾ وَمَا أَدْرَاكَ مَا سِجِّينُ ﴿٦﴾

“Hasha! Hakika maandiko ya wakosefu bila ya shaka yamo katika Sijjin. Unajua nini Sijjin?”

Na hiyo inakusanya dhiki kama Alivyosema Allah تعالى,

وَإِذَا أُلْقُوا مِنْهَا مَكَانًا ضَيِّقًا مُقَرَّبِينَ دَعَوْا هُنَالِكَ ثُبُورًا ﴿١٣﴾

“Na watakapo tupwa humo mahali pa dhiki, hali wamefungwa, wataomba wafe.” (25:13)

Kauli Yake Allah تعالى,

كِتَابٌ مَّرْقُومٌ ﴿١٤﴾

“Kitabu kilichoandikwa.”

Hii sio tafsiri kwa Kauli Yake,

¹ Angalia, Atwawaal ya At-Twabaraniy 238.

وَمَا أَدْرَاكَ مَا سِجِّينٌ ﴿٨٣﴾

“Unajua nini Sijjin?”

Lakini Maana Yake: Ni tafsiri waliyoandikiwa katika matokeo watakyokuwa nayo katika *Sijjin* kila kitu kimeisha kamilika kuandikwa, hakuna kuongezeka wala kupunguzwa chochote kwa mtu. Ameyasema hayo Muhammad bin Ka’ab Al-Quradhy.¹ Kisha Allah تعالى Amesema:

وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٨٤﴾

“Ole wao siku hiyo kwa wanaokadhibisha!”

Maana yake: Pindi watakapokuwa katika siku ya Qiyama kwenye yale ambayo Amewakamia nayo Allah تعالى miongoni mwa *Sijjini* na adhabu yenye kudhalilisha. Kwa hakika yamekwisha tangulia maneno juu ya Kauli Yake: Adhabu kali “Wail” kwa kiasi kinachotosheleza na kwamba makusudio ya hilo, ni maangamivu kama ambavyo husemwa: ‘Maangamivu na adhabu kali ni kwa fulani’ na kama ilivyokuja katika *Musnadi* na *As-Sunan* katika upokezi wa Bahaz bin Hakiim bin Mu’awiya bin Haydah kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake amesema, amesema Mtume ﷺ ,

«وَيْلٌ لِلَّذِي يُحَدِّثُ فَيَكْذِبُ لِيُضْحِكَ النَّاسَ، وَيَيْلٌ لَهُ وَيَيْلٌ لَهُ»

“Adhabu kali ni ya yule ambaye anazungumza na anasema urongo, ili awachekesha watu, adhabu kali ni yake adhabu kali ni yake.”²

Kisha Amesema Allah تعالى: Akiwa Anawaelezea wenye kukadhibisha; waovu, makafiri:

الَّذِينَ يُكَذِّبُونَ بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿٨٥﴾

“Ambao wanaikadhibisha Siku ya Malipo.”

Maana yake: Hawasadikishi kutuka kwake na hawaamini kuwa kwake na wanaliona kuwa ni la mbali jambo lake.

¹ *Ad-Durarul Manthuur* 8:444.

² *An-Nasaai* katika *Al-Kubra* 6:509.

Amesema Allah تعالى:

﴿ وَمَا يُكَذِّبُ بِهِ إِلَّا كُلُّ مُعْتَدٍ أَثِيمٍ ﴾

“Wala haikadhibishi ila kila mwenye kuruka mipaka, mwenye dhambi.”

Maana yake: Mwenye kuvuka mpaka katika matendo yake miongoni mwa kufanya haramu na kuvuka mipaka katika kuyatumia yaliyoruhusiwa na katika maneno yake akizungumza anaongopa na akitoa ahadi hatekelezi na akigombana huzidisha sana katika ugomvi wake.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

﴿ إِذَا تَتْلَىٰ عَلَيْهِ ءَايَاتُنَا قَالَ أَسْطِيفُ الْأَوَّلِينَ ﴾

“Anaposomewa Aya Zetu husema: Ni visa vya watu wa kale!”

Maana yake: Atakaposikia maneno ya Allah تعالى kutoka kwa Mtume humkadhibisha, na humdhanika dhana mbaya na huitakidi kuwa hayo maneno yameundwa na yamekusanywa kutoka katika vitabu vya watu wa kale.

Kama Alivyosema Allah تعالى:

﴿ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ مَآذًا أَنْزَلَ رَبُّكُمْ قَالُوا أَسْطِيفُ الْأَوَّلِينَ ﴾

“Na wanapoambiwa: Kateremsha nini Mola wenu Mlezi? Husema: Hadithi za kubuni za watu wa kale!” (16:24)

Na Amesema Allah تعالى:

﴿ وَقَالُوا أَسْطِيفُ الْأَوَّلِينَ أَكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمَلَّىٰ عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴾

“Na wakasema: Hivi ni visa vya watu wa kale alivyoviandikisha, anavyosomewa asubuhi na jioni.” (25:5)

Kisha Akasema,

﴿ كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَىٰ قُلُوبِهِم مَّا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴾

“Hasha! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao hao waliokuwa wakiyachuma.”

Maana yake: Hayakuwa mambo kama walivyodai wala kama walivyosema: hakika hii Qur'an si simulizi za watu wa kale bali hiyo Qur'an ni maneno ya Allah تعالى na Wahyi Wake na uteremsho Wake kwa Mjumbe Wake ﷺ lakini nyoyo zimezibwa kuamini kwa yale yaliyo juu ya nyoyo hizi miongoni mwa madhambi na makosa. Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى:

كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى قُلُوبِهِمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٧﴾

“Hasha! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao yale waliyokuwa wakiyachuma.”

Na Ar-Rain huzizukia nyoyo za makafiri. Na Al-Ghaym, huzizukia nyoyo za watu wema na Al-Ghayn huzizukia nyoyo za waliokurubishwa.

Amepokea Ibnu Jarir رحمه الله تعالى na Tirmidhi na An-Nasai na Ibnu Majah kutokana na njia tofauti kutoka kwa Abu Hurairah عنه رضي الله عنهما kutoka kwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ الْعَبْدَ إِذَا أَدْنَبَ ذَنْبًا كَانَتْ نُكْتَةً سَوْدَاءَ فِي قَلْبِهِ، فَإِنْ تَابَ مِنْهَا صُفِيَ قَلْبُهُ، وَإِنْ زَادَ زَادَتْ، فَذَلِكَ قَوْلُ اللَّهِ تَعَالَى: ﴿كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى قُلُوبِهِمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ﴾»

*“Hakika mja atakapofanya dhambi hutokea tone jeusi katika moyo wake, akitubia madhambi hayo hukwatuliwa moyo wake na akizidisha madhambi litaongezeka lile tone jeusi. Basi hiyo ndiyo maana ya Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **“Hasha! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao yale waliyokuwa wakiyachuma”**”*

Na Tirmidhi akaitaja Hadithi hii kuwa ni Hassan Sahihi.

«إِنَّ الْعَبْدَ إِذَا أَخْطَأَ خَطِيئَةً نُكِبَتْ فِي قَلْبِهِ نُكْتَةٌ سَوْدَاءٌ، فَإِنْ هُوَ نَزَعَ وَاسْتَغْفَرَ وَتَابَ صُفِيَ قَلْبُهُ، فَإِنْ عَادَ زِيدَ فِيهَا حَتَّى تَعْلُو قَلْبُهُ فَهُوَ الرَّانُ الَّذِي قَالَ اللَّهُ تَعَالَى: ﴿كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى قُلُوبِهِمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ﴾»

“Pindi mja anapofanya kosa, doa jeusi hutiwa moyoni mwake, ikiwa atajiepusha nalo, moyo wake husafishwa. akiirudia tena dhambi, doa

¹ At-Twabari 24:287, Tuḥfatu Al-Aḥwadhī 9:253, An-Nasaai katika Al-Kubra 6:509 na Ibn Majah 2:1418.

huwa kubwa mpaka kuweza kuufunika moyo wote, na hiyo ndiyo Ran ambayo Allah Mtukufu Alisema, "Hasha! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao yale waliyokuwa wakiyachuma."

Na Kauli Yake Allah تعالى:

كَلَّا إِنَّهُمْ عَنْ رَبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّحَجُونَ

"Hasha! Hakika hao siku hiyo bila ya shaka watazuliwa na kumuona Mola wao Mlezi." (83:15)

Maana yake: Wana wao siku ya Qiyama mashukio yao na makaribisho yao yatakuwa *Sijjiini* kisha wao siku ya Qiyama pamoja na yote hayo watazuliwa kumuona Bwana wao na Muumba wao. Amesema Imamu Abu Abdillah Shafii. Na katika aya hii kuna dalili juu ya kwamba waumini watamuona siku hiyo Allah تعالى, Mwenye Kushinda, Mwenye Kutukuka. Na Kauli Yake Allah تعالى:

ثُمَّ إِنَّهُمْ لَصَالُوا الْجَحِيمِ

"Kisha wataingia Motoni!"

Maana yake: Kisha wao pamoja na kuzuiliwa kumuona Bwana wao Mwingi wa Rehema ni katika watu wa motoni.

ثُمَّ يُقَالُ هَذَا الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تُكَذِّبُونَ

"Kisha waambiwe: Haya ndiyo mliyokuwa mkiyakadhabisha."

Maana yake: Watambiwa maneno hayo kwa madhumuni ya kuwakebehi, kuwakaripia na kuwadharau.

* * *

كَلَّا إِنَّ كِتَابَ الْأَبْرَارِ لَفِي عِلِّيِّينَ ﴿١٨﴾ وَمَا أَدْرَاكَ مَا
 عِلِّيُّونَ ﴿١٩﴾ كِتَابٌ مَرْقُومٌ ﴿٢٠﴾ يَشْهَدُهُ الْمُقَرَّبُونَ ﴿٢١﴾ إِنَّ
 الْأَبْرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ﴿٢٢﴾ عَلَى الْأَرَآئِكِ يَنْظُرُونَ ﴿٢٣﴾
 تَعْرِفُ فِي وُجُوهِهِمْ نَضْرَةَ النَّعِيمِ ﴿٢٤﴾ يُسْقَوْنَ مِنْ رَحِيقٍ
 مَخْتُومٍ ﴿٢٥﴾ خِتْمُهُمْ مِسْكَ ﴿٢٦﴾ وَفِي ذَلِكَ فَلْيَتَنَافَسِ
 الْمُتَنَفِّسُونَ ﴿٢٧﴾ وَمَرَاجُئُهُمْ مِنْ تَسْنِيمٍ ﴿٢٨﴾ عَيْنًا يُشْرَبُ
 بِهَا الْمُقَرَّبُونَ ﴿٢٩﴾ إِنَّ الَّذِينَ أَجْرَمُوا كَانُوا مِنَ
 الَّذِينَ ءَامَنُوا يَضْحَكُونَ ﴿٣٠﴾ وَإِذَا مَرُّوا بِهِمْ يَتَغَامَزُونَ
 ﴿٣١﴾ وَإِذَا انْقَلَبُوا إِلَىٰ أَهْلِهِمْ انْقَلَبُوا فَكِهِينَ ﴿٣٢﴾ وَإِذَا
 رَأَوْهُمْ قَالُوا إِنَّ هَٰؤُلَاءِ لَضَالُّونَ ﴿٣٣﴾ وَمَا أُرْسِلُوا عَلَيْهِمْ
 حَافِظِينَ ﴿٣٤﴾ فَالْيَوْمَ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنَ الْكُفَّارِ يَضْحَكُونَ
 ﴿٣٥﴾ عَلَى الْأَرَآئِكِ يَنْظُرُونَ ﴿٣٦﴾ هَلْ تُؤْتَوْنَ الْكُفَّارُ مَا
 كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٣٧﴾

كَلَّا إِنَّ كِتَابَ الْأَبْرَارِ لَفِي عِلِّيِّينَ
 ﴿١٨﴾ وَمَا أَدْرَاكَ مَا عِلِّيُّونَ ﴿١٩﴾
 كِتَابٌ مَرْقُومٌ ﴿٢٠﴾ يَشْهَدُهُ الْمُقَرَّبُونَ
 ﴿٢١﴾ إِنَّ الْأَبْرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ﴿٢٢﴾
 ﴿٢٣﴾ عَلَى الْأَرَآئِكِ يَنْظُرُونَ ﴿٢٣﴾
 تَعْرِفُ ﴿٢٤﴾ فِي وُجُوهِهِمْ نَضْرَةَ النَّعِيمِ ﴿٢٤﴾
 يُسْقَوْنَ مِنْ رَحِيقٍ مَخْتُومٍ ﴿٢٥﴾
 خِتْمُهُمْ مِسْكَ ﴿٢٦﴾ وَفِي ذَلِكَ فَلْيَتَنَافَسِ
 الْمُتَنَفِّسُونَ ﴿٢٧﴾ وَمَرَاجُئُهُمْ مِنْ
 تَسْنِيمٍ ﴿٢٨﴾ عَيْنًا يُشْرَبُ بِهَا
 الْمُقَرَّبُونَ ﴿٢٩﴾

18. Hasha! Hakika maandiko ya watu wema bila ya shaka yamo katika l'liyyin.

19. Na nini kitakachokujavya nini l'liyyin?.

20. Kitabu kilichoandikwa.

21. Wanakishuhudia waliokaribishwa.

22. Hakika watu wema bila ya shaka watakuwa katika neema.

23. Wakae juu ya viti vya enzi wakiangalia.

24. Utatambua katika nyuso zao mng'aro wa neema.

25. Watanyweshwa kinywaji cha mvinyo kilichofungwa.

26. Mwisho wake ni miski. Na katika hayo washindanie wenye kushindana.

27. Na mchanganyiko wake ni Tasniim.

28. Chemchemi watakayoinywa waliokurubishwa.

Kitabu cha Kumbukumbu ya Watu Wema na Malipo Yao

Allah تعالى Anasema,

إِنَّ كِتَابَ الْأَبْرَارِ

“Hakika maandiko ya watu wema.” Nao ni kinyume na Waovu. Kwani wao,

لَفِي عِلِّيِّينَ

“Bila ya shaka yamo katika I’liyyin.” Maana yake: Mwisho wao ni kwenye I’liyyin. Nayo ni kinyume cha Sijjini. Imepokewa kutoka kwa Hilal bin Yasaf amesema, aliulizwa Ibnu Abbas na Ka’ab رضي الله عنهم kuhusu maana ya “Sijjin” na hali ya kuwa mimi nipo nao. Akasema: ‘hiyo Sijjini ni ardhi ya saba na hapo zipo roho za Makafiri’. Na alimuuliza kuhusu ‘I’liyyin. Akasema, ‘hiyo ni Mbingu ya saba na humo zimo roho za waumini.’¹ Na kama hivyo imesemwa na watu wengi, kwamba hiyo ni Mbingu ya Saba.² Na amesema Ali bin Twalha kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake,

كَلَّا إِنَّ كِتَابَ الْأَبْرَارِ لَفِي عِلِّيِّينَ

“Hakika maandiko ya watu wema bila ya shaka yamo katika I’liyyin”

Anakusudia peponi.³ Na amesema mwingine, I’liyyin iko kwenye Sidrat Al-Muntahaa.⁴ Na kauli yenye nguvu ni kwamba neno I’liyyin limechukuliwa kutoka katika neno ‘Uluwwu na kila kinapokuwa juu kitu chochote hutukuka na huwa kikubwa. Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى hali ya kulitukuza jambo Lake.

وَمَا أَدْرَاكَ مَا عِلِّيُّونَ

“Na nini kitakachokujavya nini I’liyyun.” Kisha akasema Allah تعالى hali ya kulitilia mkazo lile waliloandikiwa:

كِتَابٌ مَّرْقُومٌ ۝ يَشْهَدُهُ الْمُرْسَلُونَ ۝

“Kitabu kilichoandikwa. Wanakishuhudia waliokaribishwa.”

¹ At-Tabari 24:291.

² At-Tabari 24:290.

³ At-Tabari 24:292.

⁴ At-Tabari 24:292.

Nao, ni Malaika. Ameyasema hayo Qatadah.¹ Na amesema Al-Awfi kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما: watakishuhudia katika kila mbingu wakurubishwa wake.² Kisha Amesema Allah تعالى:

إِنَّ الْأَبْرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ﴿١٨﴾

“Hakika watu wema bila ya shaka watakuwa katika neema.” Maana yake: Siku ya Qiyama wao watakuwa katika neema zenye kudumu na pepo ambayo ndani yake mna ubora wenye kuenea.

عَلَىٰ الْأَرْيَافِ

“Wakiangalia.” Wanamtazama Allah تعالى, Mwenye Kushinda, Mwenye Kutukuka katika miliki Yake na Alichowapa Allah تعالى kutokana na kheri mbalimbali na fadhila ambazo haziishi na hazipotei.

عَلَىٰ الْأَرْيَافِ يَنْظُرُونَ ﴿١٩﴾

“Wakae juu ya viti vya enzi wakiangalia.” Ametaja kuhusu hawa kwamba wao wataruhusiwa kumtazama Allah تعالى, Mwenye Kushinda, Mwenye Kutukuka. Hii ni kinyume na hali ya wale watu waovu, kwani wao watakuwa,

كَلَّا إِنَّهُمْ عَنْ رَبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَمَحْجُوبُونَ ﴿٢٠﴾

“Hasha! Hakika hao siku hiyo bila ya shaka watazuiliwa na neema za Mola Wao Mlezi.” (83:15)

Ikatajwa hali ya watu wema kuwa watakuwa juu ya vitanda na magodoro yao wakimtazama Allah تعالى. Na Kauli Yake Allah تعالى:

تَعْرِفُ فِي وُجُوهِهِمْ نَضْرَةَ النَّعِيمِ ﴿٢١﴾

“Utatambua katika nyuso zao mng'aro wa neema.” Maana yake: Utajua pindi utakapowaangalia katika nyuso zao kunyinyirika kwa neema na sifa ya starehe na heshima na furaha na utulivu na uongozi katika yale ambayo wao wamo ndani yake miongoni mwa neema kubwa sana. Na Kauli Yake Allah تعالى:

يُسْقَوْنَ مِنْ رَحِيقٍ مَخْتُومٍ ﴿٢٢﴾

“Watanyweshwa kinywaji safi cha mvinyo kilichofungwa.”

¹ At-Tabari 24:294.

² At-Tabari 24:294.

Maana yake: Watanyweshwa Pombe kutoka peponi na *Al-Rahiiq* ni katika majina ya Pombe. Ameyasema hayo Ibnu Mas'ud na Ibnu Abbas na Mujahid na Al-Hassan na Qatadah na Ibnu Zaid رضي الله عنهم.¹

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Abuu Said Al-Khudri رضي الله عنه. kutoka kwa Mtume ﷺ amesema; "Muumini yeyote atakayemnyweshwa Muumini mwenzake Maji kutokana na kiu, Allah تعالى Atakwenda kumnyweshwa siku ya kiama Kinywaji safi kilichotiwa mihuri. Na Muumin yeyote atakayemlisha chakula Muumini mwenzake kutokana na njaa, Allah تعالى Atakwenda kumlisha matunda ya Peponi. Na Muumini yeyote atakayemvisha Muumini mwenzake aliyekosa nguo za kuvaa, Allah تعالى Atakwenda kumvisha nguo za Kijani za Peponi." Na amesema Ibnu Mas'ud رضي الله عنه katika Kauli Yake.

خَتْمُهُ مِسْكٌ

"Mwisho wake ni miski." Maana yake: Mchanganyiko wake ni miski.² Na amesema Al-Awfi kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما: Allah تعالى Ameifanya Pombe hiyo kuwa Kinywaji kizuri kwa ajili yao, na kitu cha mwisho kitakachowekwa ndani yake humo ni miski, itakayohitimishwa kwa miski.³ Na kama hivyo amesema Qatadah na Adh-Dhahak.⁴ Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَفِي ذَلِكَ فَلْيَتَنَفَّسْ أَلْمُتَنَفِّسُونَ ﴿٦١﴾

"Na katika hayo washindanie wenye kushindana."

Maana yake: Na katika mfano wa hali hii wajifaharishe wenye kujifaharisha, washindane kwa kufanya matendo mengi. Washindane kwenye mfano wake wenye kutaka kushindana. Kama Kauli Yake Allah تعالى:

لِمِثْلِ هَذَا فَلْيَعْمَلِ الْعَامِلُونَ ﴿٦٢﴾

"Kwa mfano wa haya nawatende watendao." (37:61)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

¹ At-Tabari 24:296.

² Ahmad 3:13. Isnadi yake ni dhaifu, Atwiya Al-Awfi ni dhaifu Mudallis, kama ilivyotangulia mara nyingi, angalia pia Sunan Tirmidhi 2449.

³ At-Tabari 24:297. Pia yupo Al-Awiyah Al-Awfi.

⁴ At-Tabari 24:297, 298.

وَمَزَّاجُهُ مِنْ تَسْنِيمٍ ﴿٢٨﴾

“Na mchanganyiko wake ni Tasniim.” Maana yake: Kichanganyio cha huu mvinyo ulivyosifiwa ni katika *tasniim*. Maana: ni katika kinywaji kinachoitwa *tasniim*. Na kinywaji hicho, ni kinywaji bora mno cha watu wa peponi na cha juu sana. Amesema hayo Abu Swaleh na Adh-Dhahak¹ na kwa sababu hiyo Amesema:

عَيْنًا يَشْرَبُ بِهَا الْمُقَرَّبُونَ ﴿٢٩﴾

“Chemchemi watakayoinywa waliokurubishwa.” (83:28)

Maana yake: Watainywa wenye kukurubishwa hali ya kuwa safi na itachanganywa kwa watu wa mkono wa kulia. Ameyasema hayo Ibnu Mas’ud na Ibni Abbas na Masruuq na Qatadah na wengineo رضي الله عنهم.²

إِنَّ الَّذِينَ أَجْرَمُوا كَانُوا مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا يَضْحَكُونَ ﴿٢٩﴾ وَإِذَا مَرُّوا بِهِمْ يَتَغَامَزُونَ ﴿٣٠﴾
 وَإِذَا انْقَلَبُوا إِلَىٰ أَهْلِهِمْ انْقَلَبُوا فَكِهِينَ ﴿٣١﴾ وَإِذَا رَأَوْهُمْ قَالُوا إِنَّ هَٰؤُلَاءِ لَضَالُّونَ ﴿٣٢﴾
 وَمَا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ حَفِظِينَ ﴿٣٣﴾ فَالْيَوْمَ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنَ الْكُفَّارِ يَضْحَكُونَ ﴿٣٤﴾
 عَلَىٰ الْأَرَابِكِ يُنظَرُونَ ﴿٣٥﴾ هَلْ نُؤِوبَ الْكُفَّارِ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٣٦﴾

29. Kwa hakika wale waliokuwa wakosefu walikuwa wakiwacheka walioamini.

30. Na wanapopita karibu yao wakikonyezana.

31. Na wanaporudi kwa watu wao hurudi nao wamefurahi.

32. Na wanapowaona husema: Hakika hawa ndio khasa waliopotea.

33. Na wao hawakutumwa wawe walinzi juu yao.

34. Basi leo walioamini ndio watawacheka makafiri,

35. Nao wako juu ya viti vya enzi wakiangalia.

36. Je! makafiri wamelipwa malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda?

¹ At-Tabari 24:301.

² At-Tabari 24:300, 301.

Uovu wa Wakosefu na Kuwacheza Shere Kwao Waumini

Anaeleza Allah تعالى kuhusu watu waovu, kwamba wao walikuwa duniani wanawacheza waumini: Maana: Wanawacheza shere na wanawadharau. Na pindi wanapowapitia waumini wanakonyezana. Maana: wanawadharau.

وَإِذَا أَنْقَلَبُوا إِلَىٰ أَهْلِهِمْ أَنْقَلَبُوا فَكِهِينَ ﴿١٨﴾

“Na wanaporudi kwa watu wao hurudi nao wamefurahi.”

Maana yake: Pindi wakirejea hawa waovu kuelekea majumbani mwao wanarejea kwenye majumba hayo hali ya kufurahi. Maana chochote wanachokitafuta hukipata. Lakini pamoja na hayo hawakuzishukuru neema za Allah تعالى juu yao, bali walishughulika na waumini wakiwadharau na wakiwahusudu.

وَإِذَا رَأَوْهُمْ قَالُوا إِنَّ هَٰؤُلَاءِ لَضَالُّونَ ﴿١٩﴾

“Na wanapowaona husema: Hakika hawa ndio khasa waliopotea.”

Maana yake: Kwa sababu ya kuwa kwao sio katika dini yao.

Amesema Allah تعالى:

وَمَا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ حَفِظِينَ ﴿٢٠﴾

“Na wao hawakutumwa wawe walinzi juu yao.”

Maana yake: Hawakutumwa hawa waovu kwa ajili ya kuwalinda hawa waumini, yale yanayotokana na wao miongoni mwa maneno yao na matendo yao. Na hawakukalifishwa kwao jukumu lolote kwa nini walijishughulisha nao na wakawaweka wao mbele ya macho yao? Kama Alivyosema Allah تعالى:

قَالَ أَحْسَبُوا فِيهَا وَلَا تُكَلِّمُونِ ﴿٢١﴾ إِنَّهُ كَانَ فَرِيقٌ مِّنْ عِبَادِي يَقُولُونَ رَبَّنَا ءَأَمَنَّا

فَأَغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ ﴿٢٢﴾ فَاتَّخَذْتُمُوهُمْ سِحْرِيًّا حَتَّىٰ أَنْسَوَكُم ذِكْرِي

وَكُنْتُمْ مِّنْهُمْ تَضْحَكُونَ ﴿٢٣﴾ إِنِّي جَزَيْتُهُمُ الْيَوْمَ بِمَا صَبَرُوا أَنَّهُمْ هُمُ الْفَٰرِغُونَ ﴿٢٤﴾

“Atasema Mwenyezi Mungu: Tokomeeni humo, wala msinisemeze. Bila ya shaka lilikuwapo kundi katika waja wangu likisema: Mola wetu Mlezi! Tumeamini; basi tusamehe na uturehemu, nawe

ndiwe Mbora wa wanaorehemu. Lakini nyinyi mliwakejeli hata wakakusahaulisheni kunikumbuka, na mlikuwa mkiwacheka. Hakika Mimi leo Nimewalipa kwa vile walivyo subiri. Bila ya shaka hao ndio wenye kufuzu.”

Na kwa sababu hiyo amesema hapa:

فَالْيَوْمَ

“Basi leo hii.” Anakusudia siku ya Qiyama,

الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنَ الْكُفَّارِ يَضْحَكُونَ ﴿١٨﴾

“Walioamini ndio watawacheka makafiri.”

Kwa Maana: kwa kukabili na kile walichokuwa wakifanya:

عَلَىٰ الْأَرْبَابِكِ يَنْظُرُونَ ﴿١٩﴾

“Nao wako juu ya viti vya enzi wakiangalia.” Maana yake: Wanamtazama Allah تعالی, Mwenye Kushinda, na Kutukuka ikiwa ni malipo ya vile walivyodai makafiri kwamba wao wamepotea na wala hawakupotea bali wao ni miongoni mwa wapenzi wa Allah تعالی waliokurubishwa Kwake. Watamuona Bwana Wao katika mahali pa Utukufu Wake.

Na Kauli Yake Allah تعالی:

هَلْ تُوْبَ الْكُفَّارُ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٢٠﴾

“Je! makafiri wamelipwa malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda?”

Maana yake: Je, wamelipwa makafiri juu ya yale waliyokuwa wanawakabili kwao waumini miongoni mwa kuwacheza shere na kuwadharau au hapana? Anakusudia kuwa wamelipwa malipo yaliyotimia na yaliyokamilika.

Tafsiri ya Suratul Inshiqaq Sura ya 84 Iliteremshwa Makkah

Kuna Sijda ya Kisomo katika *Suratul Inshiqaq*

Imepokewa kutoka kwa Abu Salama رضي الله عنه kwamba Abu Hurairah رضي الله عنه. Aliwasomea,

إِذَا السَّمَاءُ أَنْشَقَّتْ ﴿١﴾

“Itakapopasuka mbingu.”

Akasujudu, Alipomaliza aliwaeleza kwamba Mtume ﷺ alisujudu ndani yake. Imepokewa na Muslim na An-Nasai kutokana na njia ya Malik.¹

Na amepokea Bukhari kutoka kwa Abuu Rafi amesema: Nilisali pamoja na Abuu Huraira رضي الله عنه Sala ya Isha akasoma,

إِذَا السَّمَاءُ أَنْشَقَّتْ ﴿٢﴾

“Idhaa ssamaaun shaqqat”

Nikamuuliza akasema: ‘Nilisujudu nyuma ya Abuu Al-Qasim kwa hivyo nitaendelea kusujudu mpaka nitakapokufa.²

* * *

¹ Muslim 1:406 na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:510.

² *Fat’hul Al-Bari* 1:292.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْاِنْشِقَاقِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِذَا السَّمَاءُ انشَقَّتْ ۝ وَأَذْنَتْ لِرَبِّهَا ۝ وَإِذَا الْأَرْضُ مُدَّتْ ۝ وَأَذْنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ۝ وَتَخَلَّتْ ۝ وَوَقَّتْ ۝ كَذَّابًا فَمُلَقِيهِ ۝ فَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ ۝ فَسَوْفَ يُحَاسَبُ حِسَابًا يَسِيرًا ۝ وَيَنْقَلِبُ إِلَىٰ أَهْلِهِ ۝ مَسْرُورًا ۝ وَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ وَرَاءَ ظَهْرِهِ ۝ فَسَوْفَ يَدْعُوا ثُبُورًا ۝ وَيَصَلَّىٰ سَعِيرًا ۝ إِنَّهُ كَانَ فِي أَهْلِهِ مَسْرُورًا ۝ إِنَّهُ ظَنَّ أَن لَّنْ نَّحُورَ ۝ بَلَىٰ إِنَّ رَبَّهُ كَانَ بِهِ بَصِيرًا ۝ فَلَا أُقْسِمُ بِالسَّفَاقِ ۝ وَاللَّيْلِ ۝ وَمَا وَسَقِ ۝ وَالْقَمَرِ إِذَا اتَّسَقِ ۝ لَتَرْكَبُنَّ طَبَقًا عَن طَبَقِ ۝ فَمَا هُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ۝ وَإِذَا فُرِئَ عَلَيْهِمُ الْقُرْءَانُ لَا يَسْجُدُونَ ۝ بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا يُكَذِّبُونَ ۝ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يُوعُونَ ۝ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ۝ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ هُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ۝

إِذَا السَّمَاءُ انشَقَّتْ ۝ وَأَذْنَتْ لِرَبِّهَا ۝ وَحُقَّتْ ۝ وَإِذَا الْأَرْضُ مُدَّتْ ۝ وَأَذْنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ۝ وَتَخَلَّتْ ۝ وَأَذْنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ۝ يَتَأْتِيهَا الْإِنْسَانُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَذَّابًا فَمُلَقِيهِ ۝ فَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ ۝ فَسَوْفَ يُحَاسَبُ حِسَابًا يَسِيرًا ۝ وَيَنْقَلِبُ إِلَىٰ أَهْلِهِ مَسْرُورًا ۝ وَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ وَرَاءَ ظَهْرِهِ ۝ فَسَوْفَ يَدْعُوا ثُبُورًا ۝ وَيَصَلَّىٰ سَعِيرًا ۝ إِنَّهُ كَانَ فِي أَهْلِهِ مَسْرُورًا ۝ إِنَّهُ ظَنَّ أَن لَّنْ نَّحُورَ ۝ بَلَىٰ إِنَّ رَبَّهُ كَانَ بِهِ بَصِيرًا ۝

1. Itapopasuka mbingu.

2. Na ikamsikiliza Mola Wake Mlezi, na ikapaswa kumsikiliza.

3. Na ardhi itakapotanuliwa.

4. Na kuvitoa vilivyokuwa ndani yake, ikawa tupu.

5. *Na ikamsikiliza Mola Wake Mlezi, na ikapaswa kumsikiliza,*
6. *Ewe mtu! Hakika wewe unajikusuru kwa juhudi kumuendea Mola Wako Mlezi, basi utakutana Naye.*
7. *Ama atakayepewa daftari lake kwa mkono wa kulia,*
8. *Basi huyo atahisabiwa hisabu nyepesi,*
9. *Na arudi kwa watu wake na hali ya kuwa mwenye furaha.*
10. *Na ama atakayepewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake,*
11. *Basi huyo ataomba kuteketea.*
12. *Na ataingia Motoni.*
13. *Hakika alikuwa furahani (katika maasi) pamoja na jamaa zake.*
14. *Huyo hakika alidhani kuwa hatarejea tena.*
15. *Kwani? Hakika Mola Wake Mlezi Alikuwa Akimuona!”*

Kupasuka kwa Mbingu na Kutanuliwa Ardhi Siku ya Qiyama

Anasema Allah تعالى:

إِذَا السَّمَاءُ أَنْشَقَّتْ ﴿١﴾

“Itapo chanika mbingu”

Na hiyo ni siku ya Qiyama.

وَأُذِنَتْ لِرَبِّهَا

“Na ikamsikiliza Mola Wake Mlezi.” Maana yake: Itamsikiliza Mola Wake na kutii Amri Yake ya kuchanika na hilo litakuwa siku ya Qiyama,

وَحُفَّتْ ﴿٢﴾

“Na ikapaswa kumsikiliza.” Maana yake: Ikathibitishwa hivyo, kutii Amri ya Mola Wake Mlezi, kwa sababu Yeye Allah تعالى Ndiye Mkubwa Asiyepingwa wala Asiyeshindwa, bali kila kitu kimedhalilika Kwake. Kisha Amesema:

وَإِذَا الْأَرْضُ مُدَّتْ ﴿١﴾

“Na ardhi itakapotanuliwa.”

Itakapokunjuliwa na ikatandikwa na ikapanuliwa.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَلْقَتْ مَا فِيهَا وَتَخَلَّتْ ﴿٢﴾

“Na kuvitoa vilivyokuwa ndani yake, ikawa tupu”

Maana yake: Ikatupa vilivyo tumboni mwake miongoni mwa wafu na ikaepukana nao. Ameyasema hayo Mujahid na Said na Qatada.¹

وَأُذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ﴿٣﴾

“Na ikamsikiliza Mola Wake Mlezi, na ikapaswa kumsikiliza”

Kama ilivyotangulia.

Malipo ya Matendo ni Kweli

Na Kauli Yake:

يَتَأْتِيهَا الْإِنْسَانُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدْحًا

“Ewe mtu! Hakika wewe unajikusuru kwa juhudi kumuendea Mola Wako Mlezi.”

Maana yake: Hakika wewe unahangaika kuelekea kwa Mola Wako unahangaika sana na unatenda matendo mengi,

فَمُلَاقِيهِ ﴿٤﴾

“Basi utakutana naye.”

Kisha hakika Kwake utayakuta yale uliyoyatenda miongoni mwa Kheri au Shari.

Na yanalishuhudia hilo, yale aliyoyapokea Abu Dawud At-Twayaalis kutoka kwa Jabir رضي الله عنه amesema Mtume ﷺ,

¹ At-Tabari 24:310.

«قَالَ جِبْرِيلُ: يَا مُحَمَّدُ، عِشْ مَا شِئْتَ فَإِنَّكَ مَيِّتٌ، وَأَحْبِبْ [مَنْ] شِئْتَ فَإِنَّكَ مُفَارِقُهُ، وَاعْمَلْ مَا شِئْتَ فَإِنَّكَ مُلَاقِيهِ»

“Akasema Jibril, “Ee Muhammad Ishi muda utakao, hakika wewe utakufa, na mpende umtakea, hakika wewe utatengana naye, na fanya ulitakalo hakika wewe utakutana nalo”.¹

Na katika watu kuna wanaotafsiri Kauli Yake “**Mola Wako.**” Kwa Maana: Atakujazi juu ya matendo yako na Atakulipa juu ya mahangaiko yako na kila moja kati ya hizi kauli mbili zinakubalika. Amesema Al-Awfi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

يَتَأْتِيهَا آلَانَسْنُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَى رَبِّكَ كَدْحًا

“Ewe mtu! Hakika wewe unajikusuru kwa juhudi kumuendea Mola Wako Mlezi.”

Unaharakisha kwenda kwa Mola Wako Mlezi na wewe ni mwenye kufanya amali.²

Kuoneshwa na Majadiliano katika Siku ya Hesabu

Kisha Amesema Allah تعالى:

فَأَمَّا مَنْ أَوْفَىٰ كَتَبَهُ بِمِيزَانٍ ﴿٧﴾ فَسَوْفَ مُحَاسَبٌ حِسَابًا يَسِيرًا ﴿٨﴾

“Ama atakayepewa daftari lake kwa mkono wa kulia, basi huyo atahisabiwa hisabu nyepesi.” (84:7-8)

Maana yake: Nyepesi pasi na kufanya uzito wowote. Maana hapatafanywa uhakiki juu yake wa mambo yote madogo madogo katika matendo yake. Hakika yule atakayehesabiwa kwa uhakika wa kila jambo, kwa hakika ataangamia hapana budi.

Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Aisha رضي الله عنها amesema, Mtume ﷺ amesema,

¹ Musnad At-Tayalisi no. 242. Isnadi yake ni dhaifu.

² At-Tabari 24:312.

«مَنْ نُوقِشَ الْحِسَابَ عُذِّبَ»

“Atakayejadiliwa katika kuhesabiwa ataadhibiwa.”

Kisha Aisha رضي الله عنها akasema: Hivi hakuwa Amesema Allah تعالى:

﴿فَسَوْفَ تُحَاسَبُ حِسَابًا يَسِيرًا﴾

“Basi huyo atahisabiwa hisabu nyepesi.”

Amesema Mtume ﷺ,

«لَيْسَ ذَلِكَ بِالْحِسَابِ، وَلَكِنَّ ذَلِكَ الْغَرَضُ، مَنْ نُوقِشَ الْحِسَابَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عُذِّبَ»

“Hiyo sio hesabu lakini ni ile hali ya kuoneshwa matendo. Atakayejadiliwa katika kuhesabiwa ataadhibiwa.”¹

Na kama hivyo amepokea Bukhari, Muslim, Tirmidhi, An-Nasai na Ibnu Jarir تعالى: Na Kauli Yake Allah تعالى.² رحمه الله

﴿وَيَنْقَلِبُ إِلَىٰ أَهْلِهِ مَسْرُورًا﴾

“Na arudi kwa watu wake hali ya kuwa mwenye furaha.”

Maana yake: Na atarejea kwa watu wake peponi. Ameyasema hayo Qatadah na Adh-Dhahaak, *“na furaha.”* Maana: Hali ya kuwa ni mwenye furaha, hali ya kuona raha kwa yale Aliyompa Allah تعالى, Mwenye Kushinda, na Kutukuka.³

Na Kauli Yake Allah تعالى:

﴿وَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ وَرَأَىٰ ظَهْرَهُ﴾

“Na ama atakayepewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake.”

Maana yake: Kwa mkono wake wa kushoto, nyuma ya mgongo wake, utavutwa mkono wake kwa nyuma yake. Maana: Mkono wake uko nyuma yake. Na Kauli Yake Allah تعالى:

¹ Ahmad:6:47.

² Fat’hul Al-Bari 8:566, Muslim 4:2204, Tuḥfat Al-Aḥwadhī 9:256, An-Nasai katika Al-Kubra 6:510 na At-Tabari 24:313.

³ At-Tabari 24:315.

فَسَوْفَ يَدْعُوا ثُبُورًا ﴿١٠﴾

“Basi huyo ataomba kuteketea.”

Maana yake: Kwa kupata hasara na kuangamia.

وَيَصَلَّىٰ سَعِيرًا ﴿١١﴾ إِنَّهُ كَانَ فِي أَهْلِهِ مَسْرُورًا ﴿١٢﴾

“Na ataingia Motoni. Hakika alikuwa furahani kati ya jamaa zake.”

Maana yake: Hali akiwa na furaha, hakufikiria matokeo yake, wala hakuogopa kilichokuwa mbele yake. Furaha yake ndogo itafuatiwa na huzuni ndefu.

إِنَّهُ ظَنَّ أَنْ لَنْ نَحْضُرَ ﴿١٣﴾

“Huyo hakika alidhani kuwa hatarejea tena.”

Alikuwa anaamini kwamba yeye hatarejea kwa Allah تعالى na Hamrejeshi baada ya kufa kwake; ameyasema hayo Ibnu Abbas na Qatadah na wengine رضي الله عنهم¹. Na *Al-Haur* ni kurejea. Amesema Allah تعالى:

بَلَىٰ إِنَّ رَبَّهُ كَانَ بِهِم بَصِيرًا ﴿١٤﴾

“Kwani? Hakika Mola Wake Mlezi alikuwa akimuona!”

Maana: Anakusudia kwa nini Atamrejsha Allah تعالى Kama Alivyomuanzisha na Atamlipa juu ya matendo yake, mema yake na maovu yake. Hakika Yeye Allah تعالى ni Muoni sana. Maana yake: Mwingi wa Elimu, Mwingi wa Utambuzi.

فَلَا أُقْسِمُ بِالشَّفَقِ ﴿١٥﴾ وَاللَّيْلِ وَمَا وَسَقَ ﴿١٦﴾ وَالْقَمَرِ إِذَا اتَّسَقَ ﴿١٧﴾ لَتَرْكَبُنَّ طَبَقًا عَن طَبَقٍ ﴿١٨﴾ فَمَا هُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٩﴾ وَإِذَا قُرِئَ عَلَيْهِمُ الْقُرْآنُ لَا يَسْجُدُونَ ﴿٢٠﴾ بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا يُكْذِبُونَ ﴿٢١﴾ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يُوعُونَ ﴿٢٢﴾ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٢٣﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ هُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٢٤﴾

¹ At-Tabari 24:317.

16. *Basi ninaapa kwa wekundu wa jua linapokuchwa.*
17. *Na kwa usiku na unavyovikusanya.*
18. *Na kwa mwezi unapopevuka.*
19. *Mtasafiri hatua kwa hatua!*
20. *Basi wana nini hawaamini?.*
21. *Na wanapo somewa Qur'ani hawasujudu?.*
22. *Bali waliokufuru wanakanusha tu.*
23. *Na Mwenyezi Mungu Anajua wanayoyadhamiria.*
24. *Basi wabashirie adhabu chungu!.*
25. *Isipokuwa wale walioamini na wakatenda mema; hao watakuwa na ujira usio malizika.*

Kiapo Juu ya Kupanda Binadamu Kutoka Hali Moja hadi Nyingine.

Pamepokewa kutokana na Ali, Ibnu Abbas, 'Ubad bin Swaamit, Abu Huraira, Shaddad bin Ausi, Ibni Umar, Muhammad bin Ali bin Hussein, Makhoul, Bakr bin Abdillahi al-Muzani, Bukiir bin Ashajji, Malik, Ibn Abu Dhi-ib na Abdul-Azizi bin Abu Salama, Al-Majishoun رضي الله عنهم kwamba wao wamesema, '*Ash-Shafaq*': Ni wekundu.¹

Amepokea Abdul-Razzaq kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه, amesema: '*Ash-Shafaq*': Ni weupe.² Kwa hiyo '*Ash-Shafaq*' ni wekundu – wa pembizoni mwa mbingu, ima kabla ya kuchomoza jua kama alivyolisema hilo Mujahid;³ Au baada ya kuzama kwake kama linavyojulikana kwa watu wa lugha.

Amesema Khalil bin Ahmad: '*Ash-Shafaq*', ni wekundu tokea kuzama kwa jua mpaka wakati wa Isha ya mwisho. Utakapoondoka husemwa: yamepotea mawingu mekundu.⁴

¹ Al-Qurtubi 19:274.

² Abdr-Razzaq 3:358.

³ At-Tabari 24:318.

⁴ Al-Qurtubi 19:275.

Na amesema Al-Jawhari, *'Ash-Shafaq'*, ni mabaki ya mwangaza wa jua na wekundu wake, mwanzoni mwa usiku mpaka karibu kidogo na kiza kinene. Na kama hivyo amesema Ikrima- *'Ash-Shafaq'*: Ni ule umanjano unaokuwepo baina ya Magharibi na Isha.

Imekuja katika sahihi Muslim kutoka kwa Abdullahi bin Amri رضى الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba yeye amesema,

«رَقَّتِ الْمَغْرِبِ مَا لَمْ يَغِبِ الشَّفَقُ»

*“Wakati wa Magharibi ni muda wa kuwa hayajazama mawingu mekundu”.*¹

Katika maelezo yote haya, kuna dalili juu ya kwamba *'Ash-Shafaq'*: Maana yake: ni kama alivyosema Khalil na Al-Jawhari.

Amesema Ibnu Abbas na Mujahid na Hassan na Qatadah رضى الله عنهم,

وَمَا وَسَقَ

“Na unavyovikusanya.”

Na ulichokikusanya.² Amesema Qatadah na kilichokusanywa miongoni mwa nyota na wanyama.³ Na amesema Ikrimah

وَاللَّيْلِ وَمَا وَسَقَ

“Na kwa usiku na unavyovikusanya”

Anasema; Na kile ulichokikusanya miongoni mwa kiza, utakapokuja usiku huondoka kila kitu kuelekea kwenye mashukio yake.⁴ Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَالْقَمَرَ إِذَا آتَسَقَ

“Na kwa mwezi unapopevuka.”

¹ Muslim 1:426.

² At-Tabari 24:319.

³ At-Tabari 24:320.

⁴ At-Tabari 24:321.

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما, 'utakapokusanyika na ukastawi.'¹ Na amesema Hassan: 'utakapojiunganisha na kuwa kamili.'²

Na amesema Qatadah, 'Pindi utakapo kuwa duara.'³ Aya hii ina maana ya maneno hiyo. Pindi utakapokamilika mwangaza wake, na ukawa Mbalamwezi na Akaujaalia unakubaliana na usiku na yale Aliyoyakusanya. Na Kauli Yake Allah تعالى:

لَتَرْكَبَنَّ طَبَقًا عَن طَبَقٍ ﴿٨٤﴾

"Lazima Mtasafiri hatua kwa hatua!"

Amepokea Al-Bukhari kutoka kwa Mujahid amesema: Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما,

لَتَرْكَبَنَّ طَبَقًا عَن طَبَقٍ ﴿٨٤﴾

"Lazima Mtasafiri hatua kwa hatua!"

Maana yake: Hali baada ya hali. Ameyasema haya Mtume wenu ﷺ, kama hivi ameyapokea Bukhari kwa tamko hili.⁴ Na amesema Ikrimah,

طَبَقًا عَن طَبَقٍ ﴿٨٤﴾

"Hatua kwa hatua!"

Maana yake: Ni hali baada ya hali.⁵ Mwenye kuachishwa ziwa baada ya kuwa alikuwa ananyonya na mzee baada ya kuwa alikuwa kijana. Na amesema Hassan Basri رحمه الله تعالى,

طَبَقًا عَن طَبَقٍ ﴿٨٤﴾

"Hatua kwa hatua!"

Anasema: ni hali baada ya hali.⁶ Raha baada ya shida, shida baada ya raha, utajiri baada ya ufukara, ufukara baada ya utajiri, uzima baada ya ugonjwa na ugonjwa baada ya uzima.

¹ At-Tabari 24:321.

² At-Tabari 24:321.

³ At-Tabari 24:322.

⁴ Fat'hul Al-Bari 8:567.

⁵ At-Tabari 24:323.

⁶ At-Tabari 24:323.

Ubashiri wa Adhabu kwa Makafiri na Kutokuamini Kwao Tena, na Neema ni za Waumini Pekee.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

﴿فَمَا لَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ﴾ وَإِذَا قُرِئَ عَلَيْهِمُ الْقُرْآنُ لَا يَسْجُدُونَ ﴿١٥﴾

“Basi wana nini hawaamini? Na wanaposomewa Qur’ani hawasujudu?”

Maana yake: Ni jambo gani linalowazuia kumuamini Allah تعالى na Mtume Wake na siku ya mwisho. Na wana nini kwao pindi wanaposomewa aya za Allah تعالى na maneno Yake, nayo ni hii Qur’an hawasujudu kwa kuitukuza na kwa kuiheshimu na kwa kuikirimu. Na Kauli Yake Allah تعالى:

﴿بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا يَكْذِبُونَ﴾

“Bali waliokufuru wanakanusha tu.” Maana yake: miongoni mwa tabia zao ni kukadhibisha na kupinga na kwenda kinyume na haki,

﴿وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يُوعُونَ﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anajua wanayoyadhamiria.”

Amesema Mujahid na Qatadah wanayoyaficha vifuani mwao.¹

﴿فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ﴾

“Basi wabashirie adhabu chungu!”

Maana yake: Wape khabari Ee Muhammad ﷺ kwamba Allah تعالى Mwenye Kushinda na Kutukuka, Amewaandalia adhabu yenye kuumiza. Na Kauli Yake Allah تعالى:

﴿إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ﴾

“Isipokuwa wale walioamini na wakatenda mema.”

Huu ni mchujio usiofanana kihadhi. Kwa maana: Kilicho chujwa hakilingani hadhi yake na kilichosalia – maana wale walioamini kwa nyoyo zao na wakatenda matendo mema kwa viungo vyao.

¹ At-Tabari 24:327.

هُمَّ أَجْرٌ

“Hao watakuwa na ujira”

Maana yake: Katika nyumba ya akhera

عَبْرُ مَمْنُونٍ

“Usiomalizika”

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما maana yake: ujira usiopunguzwa.¹ Na amesema Mujahid na Adh-Dhahak: yasiyohesabiwa na pato.² Maana ya maneno yao ni kwamba malipo hayo si yenye kukatwa.

Kama Alivyosema Allah تعالى:

عَطَاءٌ غَيْرُ مَجْدُودٍ

“Hicho ni kipawa kisio na ukomo.” (11:108)

Na amesema As-Sudiy wamesema baadhi yao: yasiyopunguzwa.

Huu ni mwisho wa Tafsiri za *Suratu Al-Inshiqaq* na ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemeshwa. Na ni Kwake Yeye tu Kuwezesha na Kuinga.

* * *

¹ At-Twabari 24:327.

² At-Twabari 24:327.

Tafsiri ya Suratul Buruj

Sura ya 85

Iliteremshwa Makkah

سُورَةُ الْبُرُوجِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْبُرُوجِ ﴿١﴾ وَالْيَوْمِ الْوَعُودِ ﴿٢﴾ وَشَاهِدِ
 وَمَشْهُودِ ﴿٣﴾ قَتَلَ أَصْحَابَ الْأَخْضُدِ ﴿٤﴾ النَّارِ ذَاتِ
 الْوُقُودِ ﴿٥﴾ إِذْ هُمْ عَلَيْهَا قُعُودٌ ﴿٦﴾ وَهُمْ عَلَىٰ مَا يَفْعَلُونَ
 بِالْمُؤْمِنِينَ شُهُودٌ ﴿٧﴾ وَمَا نَقَمُوا مِنْهُمْ إِلَّا أَن يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ
 الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿٨﴾ الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ
 وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٩﴾ إِنَّ الَّذِينَ فَتَنُوا الْمُؤْمِنِينَ
 وَالْمُؤْمِنَاتِ لَمْ يَتُوبُوا فَلَهُمْ عَذَابٌ جَهَنَّمَ وَهُمْ عَذَابُ
 الْحَرِيقِ ﴿١٠﴾ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ هُمْ جَنَّاتُ
 تَجْرَىٰ مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْكَبِيرُ ﴿١١﴾ إِنَّ بَطْشَ
 رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿١٢﴾ إِنَّهُ هُوَ يُبْدِي وَيُعِيدُ ﴿١٣﴾ وَهُوَ
 الْغَفُورُ الْوَدُودُ ﴿١٤﴾ ذُو الْعَرْشِ الْحَمِيدُ ﴿١٥﴾ فَعَالٌ لِّمَا
 يُرِيدُ ﴿١٦﴾ هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْجُنُودِ ﴿١٧﴾ فِرْعَوْنَ وَثَمُودَ ﴿١٨﴾
 بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي تَكْذِيبٍ ﴿١٩﴾ وَاللَّهُ مِنْ وَرَائِهِمْ
 مُحِيطٌ ﴿٢٠﴾ بَلْ هُوَ قُرْءَانٌ مَّجِيدٌ ﴿٢١﴾ فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ ﴿٢٢﴾

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi
 wa Rehema, Mwenye
 Kurehemu.

وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْبُرُوجِ ﴿١﴾ وَالْيَوْمِ
 الْوَعُودِ ﴿٢﴾ وَشَاهِدِ وَمَشْهُودِ ﴿٣﴾
 قَتَلَ أَصْحَابَ الْأَخْضُدِ ﴿٤﴾ النَّارِ
 ذَاتِ الْوُقُودِ ﴿٥﴾ إِذْ هُمْ عَلَيْهَا قُعُودٌ
 ﴿٦﴾ وَهُمْ عَلَىٰ مَا يَفْعَلُونَ
 بِالْمُؤْمِنِينَ شُهُودٌ ﴿٧﴾ وَمَا نَقَمُوا
 مِنْهُمْ إِلَّا أَن يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ الْعَزِيزِ
 الْحَمِيدِ ﴿٨﴾ الَّذِي لَهُ مُلْكُ
 السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ
 شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٩﴾ إِنَّ الَّذِينَ فَتَنُوا
 الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ لَمْ يَتُوبُوا
 فَلَهُمْ عَذَابٌ جَهَنَّمَ وَهُمْ عَذَابُ
 الْحَرِيقِ ﴿١٠﴾

1. **Naapa kwa mbingu yenye Nyota kubwa!**
2. **Na kwa siku iliyoahidiwa!**
3. **Na kwa shahidi na kinachoshuhudiwa!**
4. **Wameangamizwa watu wa makhandaki**
5. **Yenye moto wenye kuni nyingi,**
6. **Walipokuwa wamekaa hapo,**
7. **Na wao ni mashahidi wa yale waliyokuwa wakiwafanyia Waumini.**
8. **Nao hawakuona baya lolote kwao ila kuwa wakimuamini Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Msifiwa,**
9. **Ambaye Anao Ufalme wa Mbingu na Ardhi; na Mwenyezi Mungu ni shaahidi wa kila kitu.**
10. **Hakika waliowafitini Waumini wanaume na Waumini wanawake, kisha hawakutubu, basi watapata adhabu ya Jahannamu na watapata adhabu ya kuungua."**

Tafsiri ya Al-Burouj

Anaapa Allah تعالى, kwa mbingu na Buruji zake, nazo ni nyota kuu kama Alivyosema Allah تعالى:

تَبَارَكَ الَّذِي جَعَلَ فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا وَجَعَلَ فِيهَا سِرَاجًا وَقَمَرًا مُنِيرًا ﴿٦١﴾

"Ametukuka Aliyezijaalia nyota mbinguni, na Akajaalia humo taa na mwezi unaong'ara." (25:61)

Amesema Ibnu Abbas na Mujahid na Adh-Dhahak na Hassan, Qatadah na As-Sudiy رضي الله عنهم kuwa Al Burouj, maana yake ni nyota.¹ Amesema Al-Minhal bin Amru,

وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْبُرُوجِ ﴿٦١﴾

"Naapa kwa mbingu yenye Buruji!" Zenye umbile zuri.² Na ameichagua Ibnu Jarir رحمه الله تعالى kwamba 'Burouj' ni mashukio ya jua na mwezi, nayo ni

¹ Al-Qurtubi 19:200

² Al-Qurtubi 19:283

mashukio kumi na mbili. Na jua linakwenda katika kila moja katika mashukio hayo, kwa muda wa mwezi. Na unakwenda mwezi katika kila moja katika mashukio hayo kwa muda wa siku mbili na theluthi ya siku. Kwa hiyo hayo ni mashukio ishirini na nane na hujificha mwezi katika usiku miwili.¹

Tafsiri ya Siku yenye Kuahidiwa na Shahidi na Mwenye Kushuhudiwa

Na Kauli Yake Allah تعالى:

﴿وَالْيَوْمِ التَّوَعُّودِ﴾ وَشَاهِدٍ وَمَشْهُودٍ ﴿﴾

“Na kwa siku iliyoahidiwa! Na kwa shahidi na kinachoshuhudiwa!”

Amepokea Ibnu Abi Hatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه amesema Mtume ﷺ,

﴿وَالْيَوْمِ التَّوَعُّودِ﴾ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ﴿وَشَاهِدٍ﴾ يَوْمَ الْجُمُعَةِ، وَمَا طَلَعَتْ شَمْسٌ وَلَا غَرَبَتْ عَلَى يَوْمٍ أَفْضَلَ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ، وَفِيهِ سَاعَةٌ لَا يُوَافِقُهَا عَبْدٌ مُسْلِمٌ يَسْأَلُ اللَّهَ فِيهَا خَيْرًا إِلَّا أَعْطَاهُ إِيَّاهُ، وَلَا يَسْتَعِيدُ فِيهَا مِنْ شَرٍّ إِلَّا أَعَادَهُ. ﴿وَمَشْهُودٍ﴾ يَوْمَ عَرَفَةَ

“Na kwa siku iliyoahidiwa!” maana yake ni siku ya Qiyama; **“Na kwa shahidi”** ni siku ya Ijumaa na halijachomoza jua na kuzama juu ya siku bora sana kuliko siku ya Ijumaa, na ndani yake mna saa haiwafiki mja Muislamu akimuomba Allah تعالى ndani yake kheri yoyote, isipokuwa Atampa kheri hiyo. Na hatataka hifadhi ndani yake na shari yoyote isipokuwa Atamkinga na shari hiyo; na **‘kinacho shuhudiwa!’** “Ni siku ya Arafa.”²

Na kama hivi ameipokea Hadithi hii Ibnu Khuzaima. Na imepokelewa hadithi hii kwa njia ya ‘Mawquuf’ kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه, na inashabihiana zaidi na njia hiyo.³

Na imepokewa kutoka kwa Abu Huraira, Ibni Abbas, Hassan bin Ali, Hassan Basry, Saiid bin Musayyab, Mujahid, krimah na Adh-Dhahak رضي الله عنهم wote wamesema, **“na kinacho shuhudiwa!”** Maana yake: Ni siku ya Qiyama.

¹ At-Tabari 24:332.

² At-Tabari 24:333, 334.

³ Ibnu Khuzayma 3:116.

Amesema Al-Baghawi wafasiri wengi wamesema: kwamba **“Shahidi”** ni siku ya Ijuma na **“Mash’hudi”** ni Siku ya Arafah.¹

Dhulma ya Watu wa Mahandaki Dhidi ya Waislamu

Na Kauli Yake Allah تعالى:

قَتَلَ أَصْحَابُ الْأَخْذُودِ ﴿١٠﴾

“Wameangamizwa watu wa makhandaki.”

Maana yake: Wamelaaniwa wenye mahandaki na wingi wa *Al-Ukhduud* ni *Al-Akhaadid* nayo ni mashimo katika ardhi.

Na ni habari kuhusiana na watu katika makafiri, waliwakusudia kwa ubaya wale walioamini miongoni mwao. Allah تعالى Mwenye Kushinda na Kutukuka Akawatenza nguvu. Watu wale, walitakiwa warejee kwenye dini yao wakawakatalia, wakawachimbia makaburi katika ardhi na humo wakawasha moto, na wakauandalia kuni, wakawasha kuni hizo, kisha wakawataka tena waiache dini yao, wakawakatalia wakawatupa ndani ya moto. Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى.

قَتَلَ أَصْحَابُ الْأَخْذُودِ ﴿١٠﴾ النَّارِ ذَاتِ الْوَقُودِ ﴿١١﴾ إِذْ هُمْ عَلَيْهَا قُعُودٌ ﴿١٢﴾ وَهُمْ عَلَىٰ مَا

يَفْعَلُونَ بِالْمُؤْمِنِينَ شُهُودٌ ﴿١٣﴾

“Wameangamizwa watu wa makhandaki yenye moto wenye kuni nyingi, Walipokuwa wamekaa hapo. Na wao ni mashahidi wa yale waliyokuwa wakiwafanyia Waumini.”

Maana yake: Wanayashuhudia yale wanayofanyiwa waumini hao. Amesema Allah تعالى:

وَمَا نَقَمُوا مِنْهُمْ إِلَّا أَنْ يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿١٤﴾

“Nao hawakuona baya lolote kwao ila kuwa wakimuamini Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Msifiwa.”

Maana yake: Hawakuwa kwao wana makosa yoyote isipokuwa kumuamini kwao Allah تعالى, Mwenye Kushinda ambaye hadhulumiwi, mwenye kukimbilia

¹ Al-Baghawi 4:466

Kwake, Mwenye Nguvu, Mwenye Kusifiwa kwa wema katika Maneno Yake na Vitendo Vyake, na Shari Zake, na Makadirio Yake. Japokuwa Amekadiria kwa waja Wake hawa haya yaliyowapata kutokana na mikono ya wanaomkufuru Yeye. Yeye Ndiye Mwenye Kushinda, Mwenye Kusifiwa ijapokuwa hujificha sababu ya hilo kwa watu wengi. Kisha Amesema Allah تعالى:

الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Ambaye Anao Ufalme wa mbingu na ardhi.”

Katika ukamilifu wa sifa ni kwamba Yeye Ndiye Mwenye Kuvimiliki vilivyomo mbinguni na ardhini na vilivyomo ndani yao na kati yao.

وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni shaahidi wa kila kitu.”

Maana yake: Hakifichiki Kwake kitu chochote katika mbingu zote na ardhi na hakijifichi Kwake chochote chenye kujificha.

Kisa cha Mchawi, Mtawa Kijana na Wale Waliotiwa katika Mahandaki

Amepokea Imamu Ahmad رحمه الله تعالى kutoka kwa Suhayb رضي الله عنه, kwamba Mtume ﷺ amesema:

«كَانَ فِيمَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ مَلِكٌ وَكَانَ لَهُ سَاجِرٌ، فَلَمَّا كَبِرَ السَّاجِرُ قَالَ لِلْمَلِكِ: إِنِّي قَدْ كَبِرَ سِنِّي وَحَضَرَ أَجْلِي، فَادْفَعْ إِلَيَّ غُلَامًا لِأَعْلَمَهُ السُّحْرَ، فَدَفَعَ إِلَيْهِ غُلَامًا فَكَانَ يُعَلِّمُهُ السُّحْرَ، وَكَانَ بَيْنَ السَّاجِرِ وَبَيْنَ الْمَلِكِ رَاهِبٌ فَأَتَى الْغُلَامُ عَلَى الرَّاهِبِ فَسَمِعَ مِنْ كَلَامِهِ فَأَعْجَبَهُ نَحْوُهُ وَكَلَامُهُ، وَكَانَ إِذَا أَتَى السَّاجِرَ ضَرَبَهُ وَقَالَ: مَا حَبَسَكَ؟ وَإِذَا أَتَى أَهْلَهُ ضَرَبُوهُ وَقَالُوا: مَا حَبَسَكَ؟ فَسَكَ ذَلِكَ إِلَى الرَّاهِبِ فَقَالَ: إِذَا أَرَادَ السَّاجِرُ أَنْ يَضْرِبَكَ فَقُلْ: حَبَسَنِي أَهْلِي، وَإِذَا أَرَادَ أَهْلُكَ أَنْ يَضْرِبُوكَ فَقُلْ: حَبَسَنِي السَّاجِرُ، قَالَ: فَبَيْنَمَا هُوَ ذَاتَ يَوْمٍ إِذْ أَتَى عَلَى دَابَّةٍ فَطَيَعَةَ عَظِيمَةً قَدْ حَبَسَتِ النَّاسَ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ أَنْ يَجُوزُوا. فَقَالَ: التَّيْمَ أَغْلَمَ أَمْرُ الرَّاهِبِ أَحَبُّ إِلَيَّ اللَّهُ أَمْ أَمْرُ السَّاجِرِ؟ قَالَ: فَأَخَذَ حَجْرًا فَقَالَ: اللَّهُمَّ إِنْ كَانَ أَمْرُ الرَّاهِبِ أَحَبَّ إِلَيْكَ وَأَرْضِي مِنْ أَمْرِ السَّاجِرِ فَاقْتُلْ هَذِهِ الدَّابَّةَ حَتَّى يَجُوزَ النَّاسُ، وَرَمَاهَا فَقَتَلَهَا وَمَضَى النَّاسُ.»

“Alikuwapo katika watu waliokuwa kabla yenu Mfalme ambaye alikuwa na mchawi. Mchawi yule alipokuwa mtu mzima sana alimuambia mfalme, “Hakika mimi nimeshakuwa mtu mzima na kifo kinaninyemelea. Hivyo nitafutie kijana nimfundishe uchawi. Mfalme akampelekea kijana akawa anamfundisha uchawi na alikuwa baina ya mchawi na Mfalme kuna mtawa wa kinaswara. Kijana yule akaenda kwa yule mtawa na akasikiliza mafundisho yake ukamvutia ufasaha wake na maneno yake. Na akawa anapomuendea mchawi anampiga na kumuambia ni jambo gani lililokucheleweshwa? Na akiwa anakwenda kwa watu wake humpiga na kumuambia ni jambo gani lililokucheleweshwa? Yule kijana akaeleza hali yake (ya kupigwa na yule Mchawi) kwa yule Mtawa. Akamuambia hakika mchawi akikupiga sema wamenichelewesha watu wangu, na wakitaka watu wako kukupiga sema amenichelewesha mchawi. Siku moja katika ada yake ghafla akiwa anakwenda kwa yule mtawa alitokea mnyama mkubwa sana njiani amewazuia watu hawawezi kupita. Kwa kutokea jambo lile akasema leo nitaelewa jambo la mtawa je, linapendeza sana kwa Mwenyezi Mungu au jambo la mchawi ndilo lenye kupendeza?. Amesema, ‘Mara kijana yule akachukua jiwe akasema, ‘Ee Mola Wangu wa haki likiwa jambo la mtawa linapendeza sana kwako na linaridhiwa sana kuliko jambo la mchawi basi muue mnyama huyo ili watu waweze kupita.’ Akamtupia jiwe mnyama yule na akamuua na watu wakapita.

فَأَخْبَرَ الرَّاهِبَ بِذَلِكَ فَقَالَ: أَيُّ بَنِي، أَنْتَ أَفْضَلُ مِنِّي وَإِنَّكَ سَتَبْتَلَى، فَإِنْ ابْتَلَيْتَ
فَلَا تَدُلُّ عَلَيَّ، فَكَانَ الْعَلَامُ يُبْرِئُ الْأَكْمَةَ وَالْأَبْرَصَ وَسَائِرَ الْأَدْوَاءِ وَيُنْفِيهِمْ،
وَكَانَ لِلْمَلِكِ جَلِيسٌ فَعَمِيَ فَسَمِعَ بِهِ فَأَتَاهُ بِهَدَايَا كَثِيرَةٍ فَقَالَ: اشْفِنِي وَلَكَ مَا هُنَا
أَجْمَعُ، فَقَالَ: مَا أَنَا أَشْفِي أَحَدًا، إِنَّمَا يَشْفِي اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ، فَإِنْ آمَنْتَ بِهِ دَعَوْتُ
اللَّهَ فَشَفَاكَ، فَأَمَّنَّ فَدَعَا اللَّهَ فَشَفَاهُ.

Kijana akamueleza yule mtawa habari ile akasema: ‘Ewe kijana changu wewe ni mbora kuliko mimi na utapata majaribio.’ Utakapopatwa na majaribio usiwafahamishe watu kuhusu mimi. Ikawa kazi ya kijana yule kuwaponesha vipofu na wenye mbalanga na baki ya magonjwa.

Mfalme alikuwa ana rafiki katika baraza lake aliyepofuka, akasikia kuhusu habari za kijana yule akamuendea na zawadi nyingi sana, akamuambia niponyeshe na utapata vitu vyote nilivyonavyo. Yule kijana akasema: 'Sikuwa mimi ninamponya mtu yoyote, hakika hapana jambo lolote nifanyalo isipokuwa mwenye kulifanya ni Mwenyezi Mungu, Mwenye Kushinda na Utukufu, ukimuamini, nitamuomba na Atakuponyesha. Yule bwana akaamini –na Yule kijana akamuomba Mwenyezi Mungu na akapona.

ثُمَّ أَتَى الْمَلِكَ فَجَلَسَ مِنْهُ نَحْوَ مَا كَانَ يَجْلِسُ فَقَالَ لَهُ الْمَلِكُ: يَا فُلَانُ، مَنْ رَدَّ عَلَيْكَ بَصْرَكَ؟ فَقَالَ: رَبِّي. فَقَالَ: أَنَا؟ قَالَ: لَا، رَبِّي وَرَبُّكَ اللَّهُ، قَالَ: وَلَكَ رَبٌّ غَيْرِي؟ قَالَ: نَعَمْ رَبِّي وَرَبُّكَ اللَّهُ، فَلَمْ يَزَلْ يُعَذِّبُهُ حَتَّى دَلَّ عَلَى الْغُلَامِ، فَبَعَثَ إِلَيْهِ فَقَالَ: أَيُّ بَنِي بَلْعٍ مِنْ سِحْرِكَ أَنْ تُبْرِيءَ الْأَكْمَةَ وَالْأَبْرَصَ وَهَذِهِ الْأَدْوَاءُ؟ قَالَ: مَا أَشْفِي أَحَدًا إِنَّمَا يَشْفِي اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ، قَالَ: أَنَا؟ قَالَ: لَا. قَالَ: أَرَأَيْتَ رَبٌّ غَيْرِي؟ قَالَ: رَبِّي وَرَبُّكَ اللَّهُ، فَأَخَذَهُ أَيْضًا بِالْعَذَابِ فَلَمْ يَزَلْ بِهِ حَتَّى دَلَّ عَلَى الرَّاهِبِ فَأَتَى بِالرَّاهِبِ فَقَالَ: ارْجِعْ عَنْ دِينِكَ فَأَبِي، فَوَضَعَ الْبِنشَارَ فِي مَفْرَقِ رَأْسِهِ حَتَّى وَقَعَ شِقْمَاهُ، وَقَالَ لِلْأَعْمَى: ارْجِعْ عَنْ دِينِكَ، فَأَبِي، فَوَضَعَ الْبِنشَارَ فِي مَفْرَقِ رَأْسِهِ حَتَّى وَقَعَ شِقْمَاهُ إِلَى الْأَرْضِ. وَقَالَ لِلْغُلَامِ: ارْجِعْ عَنْ دِينِكَ، فَأَبِي، فَبَعَثَ بِهِ مَعَ نَفَرٍ إِلَى جَبَلٍ كَذَا وَكَذَا وَقَالَ: إِذَا بَلَغْتُمْ ذُرْوَتَهُ فَإِنْ رَجَعَ عَنْ دِينِهِ وَإِلَّا فَذَهَبُوهُ، فَذَهَبُوا بِهِ فَلَمَّا عَلَوْا بِهِ الْجَبَلَ قَالَ: اللَّهُمَّ اكْفِنِيهِمْ بِمَا شِئْتَ، فَزَجَفَ بِهِمُ الْجَبَلَ فَذَهَبُوا أَجْمَعُونَ، وَجَاءَ الْغُلَامُ يَتَلَمَّسُ حَتَّى دَخَلَ عَلَى الْمَلِكِ فَقَالَ: مَا فَعَلَ أَصْحَابُكَ؟ فَقَالَ: كَفَّانِيهِمُ اللَّهُ تَعَالَى، فَبَعَثَ بِهِ مَعَ نَفَرٍ فِي فُرْقُورٍ فَقَالَ: إِذَا لَجَجْتُمْ بِهِ الْبَحْرَ فَإِنْ رَجَعَ عَنْ دِينِهِ، وَإِلَّا فَعَرِّقُوهُ فِي الْبَحْرِ، فَلَجَجُوا بِهِ الْبَحْرَ فَقَالَ الْغُلَامُ: اللَّهُمَّ اكْفِنِيهِمْ بِمَا شِئْتَ، فَعَرِّقُوا أَجْمَعُونَ.

Kisha akamuendea Mfalme akakaa kwake palepale alipokuwa anakaa, Mfalme akamuuliza, "Ee fulani ni nani aliyekurudishia kuona kwako?" Akasema: "Ni Bwana Wangu." Akasema: "mimi?" Akasema: 'Hapana Bwana Wangu na Bwana Wako ni Mwenyezi Mungu.' Mfalme akasema, "Jee wewe una Bwana asiyekuwa mimi?" Akasema: "Ndiyo Bwana Wangu na Bwana Wako ni Mwenyezi Mungu." Mfalme akawa anamtesa hadi akajulishwa kuhusu kijana yule, Mfalme akapeleka ujumbe kwa yule kijana

akasema, 'Ee kijana changu, umefikia katika uchawi wako kiasi cha kuwa unawaponyesha vipofu, na wenye mbalanga? na magonjwa mengine haya?' Yule kijana akasema, 'Mimi simponyeshi mtu yeyote hakika hapana jambo lolote bali anayeponyeshi ni Mwenyezi Mungu Mwenye Kushinda na Kutukuka.' Mfalme akasema: "Ni Mimi?' Kijana akamjibu: 'Hapana' Mfalme akamuuliza, 'Hivi wewe una Bwana mwengine asiye kuwa mimi?' Kijana akamjibu: 'Bwana Wangu na Bwana Wako ni Mwenyezi Mungu.' Mfalme akamuadhibu kijana yule kwa adhabu mbali mbali kiasi cha yule kijana kutoa siri ya yule Mtawa. Mfalme akaamuru kukamatwa kwa mtawa na kupelekwa kwake na akamtaka aache dini yake. Mtawa yule akakataa kuacha dini yake. Mfalme akaamrisha kuwekwa msumeno na kukatwa pande zake mbili za kiwiliwili na akakatwa kichwa chake, mpaka zikaanguka pande zake mbili. Mfalme akamgeukia yule kipofu na kumuamrisha kurejea katika dini yake naye akakataa. Akauweka msumeno katika mgawanyiko wa kichwa chake, mpaka zikaanguka pande zake mbili chini na akamuambia yule kijana rejea uiache dini yako – akakataa akampeleka pamoja na kundi la watu kwenye jabali fulani na akasema: 'Mtakapofikia kileleni kwake iwapo atarejea na akaiacha dini yake – hapo muacheni na kama hatorejea na hataiacha dini yake hapo mporomosheni.' Wakaenda naye walipofika naye jabalini akasema: 'Ee Mola Wangu wa haki nitosheleze na wao kwa lile Ulitakalo, likatetemeka jabali wakaporomoka wote'. Akaja yule kijana akitafutatafuta mpaka akaingia kwa Mfalme. Mfalme akauliza; 'Wamefanya nini wenzio?' Akamjibu, 'Amenitosha mimi Allah Taala.' Mfalme akaamrisha apelekwe pamoja na watu katika jahazi, akasema; 'Mtakapoingia baharini na huyo kijana iwapo atarejea na kuiacha dini yake muacheni na kama hakurejea katika dini yake mzamisheni baharini.' Wakaingia naye baharini akasema yule kijana, "Ewe Mola Wangu wa haki nitosheleze na hawa kwa lile Unalolitaka." Wakazama majini wote.

وَجَاءَ الْعُلَامُ حَتَّى دَخَلَ عَلَى الْمَلِكِ فَقَالَ: مَا فَعَلَ أَصْحَابُكَ؟ فَقَالَ: كَفَّابِهِمُ اللَّهُ تَعَالَى ثُمَّ قَالَ لِلْمَلِكِ: إِنَّكَ لَسْتَ بِقَاتِلِي حَتَّى تَفْعَلَ مَا أَمْرُكَ بِهِ، فَإِنْ أَنْتَ فَعَلْتَ مَا أَمْرُكَ بِهِ قَتَلْتَنِي، وَإِلَّا فَإِنَّكَ لَا تَسْتَطِيعُ قَتْلِي، قَالَ: وَمَا هُوَ؟ قَالَ: تَجْمَعُ النَّاسَ فِي صَعِيدٍ وَاحِدٍ ثُمَّ تَصْلُبُنِي عَلَى جِذْعٍ وَتَأْخُذُ سَهْمًا مِنْ كِتَابَتِي، ثُمَّ قُلْ: بِاسْمِ اللَّهِ

رَبِّ الْعَلَامِ. فَإِنَّكَ إِذَا فَعَلْتَ ذَلِكَ قَتَلْتَنِي. فَفَعَلَ وَوَضَعَ السَّهْمَ فِي كَيْدِ قَوْمِهِ ثُمَّ رَمَاهُ وَقَالَ: بِاسْمِ اللَّهِ رَبِّ الْعَلَامِ، فَوَقَعَ السَّهْمُ فِي صُدْغِهِ، فَوَضَعَ الْعَلَامُ يَدَهُ عَلَى مَوْضِعِ السَّهْمِ وَمَاتَ، فَقَالَ النَّاسُ: أَمَّا بِرَبِّ الْعَلَامِ. فَقِيلَ لِلْمَلِكِ: أَرَأَيْتَ مَا كُنْتَ تَحْذَرُ؟ فَقَدْ رَأَى نَزْلَ بَيْتِكَ، قَدْ آمَنَ النَّاسُ كُلُّهُمْ، فَأَمَرَ بِأَفْوَاهِ السُّكَّكِ، فَخُدَّتْ فِيهَا الْأَخَادِيدُ وَأُضْرِمَتْ فِيهَا النَّيْرَانُ، وَقَالَ: مَنْ رَجَعَ عَنِّي فِدْعُوهُ، وَإِلَّا نَأْفِجُوهُ فِيهَا، قَالَ: فَكَانُوا يَتَمَادُونَ فِيهَا وَيَتَدَفَعُونَ، فَجَاءَتْ امْرَأَةٌ بَابِنِ لَهَا تَرْضِعُهُ، فَكَانَتْ تَقَاعَسَتْ أَنْ تَقَعَ فِي النَّارِ فَقَالَ الصَّيِّ: اضْرِبِي يَا أُمَّةُ فَإِنَّكَ عَلَى الْحَقِّ

Akaja kijana mpaka akaingia kwa Mfalme. Mfalme akauliza, "Wamefanya nini wenzi?" Akasema: "Amenitoshana nao Allah Taala." Kisha yule kijana akamuambia Mfalme, "Kwa hakika wewe hutaweza kuniua mpaka ufanye lile nitakalokuamrisha? Iwapo wewe utalifanya hilo hapo utaweza kuniua na kama hukufanya basi wewe hutaweza kuniua." Mfalme akauliza, "Ni jambo gani hilo?" Yule kijana akajibu, "Kusanya watu katika uwanja mmoja, kisha unifunge katika shina la mti na uchukue mshale wangu katika mkoba wake kisha sema, "Kwa Jina la Allah, Bwana wa Kijana huyu", hakika wewe utakapofanya hivyo utaniua. Mfalme akafanya kama alivyoambiwa, akaweka mshale katikati ya upinde wake kisha akamfyatulia na akasema, "kwa Jina la Allah Bwana wa kijana huyu." Ukapiga mshale sehemu iliyo kati ya shavu na sikio, akaweka kijana mkono wake juu ya mahali pa mshale na akafa. Watu wote wakasema: "Tumemuamini Bwana wa kijana." Akaambiwa Mfalme: "Jee umeliona lile ulilokuwa unalitahadhari nalo? Kwa hakika tunaapa kwa Allah limekwisha kukushukia. Kwa hakika watu wote wameamini." Akaamrisha katika maingilio ya njia zote yakachimbwa mahandaki na ukawashwa katika mahandaki hayo moto na akasema, "Atakayerejea na kuiacha dini yake huyo muacheni, na kama hakurejea mtumbukize ndani ya moto." Wakawa watu wanaongezeka kwa idadi na wanashindana kuingia motoni. Akaja mwanamke na mtoto wake hali ya kuwa anamnyonyesha, kana kwamba alisita kuingia motoni akasema yule mtoto: 'Vumilia Ee mama yangu kwa hakika wewe uko juu ya haki.'

¹ Ahmad 6:17.

Kama hivi amekipokea kisa hiki Muslim mwishoni mwa sahihi yake.¹

Na amekileta bin Ishaq رحمه الله تعالى kisa hiki katika sira kwa utaratibu mwingine unaotofautiana na huu tulioueleza.

Kisha baada ya hapo Ibn Ishaq رحمه الله تعالى akabainisha kuwa watu wa Najraan baada ya kuuliwa kijana juu ya dini yake ya kinaswara, amesema, akawaelekea Dhu An-Nawaas, na Jeshi lake akawalingania kwenye Uyahudi na akawakhiyarisha kati ya kuukubali Uyahudi na kati ya kuuliwa. Wakachagua kuuliwa, akachimba mahandaki akawachoma moto na kuwaua kwa upanga na akakatakata viungo vyao mpaka akawaua miongoni mwao kiasi cha watu elfu ishirini (20,000).

Kwa sababu ya Dhu An-Nawaas na Jeshi lake, Aliteremsha Allah تعالى, Mwenye Kushinda na Mtukufu – juu ya Mtume Wake:

فُتِلَ أَصْحَابُ الْأُخْدُودِ ﴿٤١﴾ النَّارِ ذَاتِ الْوُقُودِ ﴿٤٢﴾ إِذْ هُمْ عَلَيْهَا قُعُودٌ ﴿٤٣﴾ وَهُمْ عَلَىٰ مَا
يَفْعَلُونَ بِالْمُؤْمِنِينَ شُهُودٌ ﴿٤٤﴾ وَمَا نَقَمُوا مِنْهُمْ إِلَّا أَن يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿٤٥﴾
الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٤٦﴾

“Wameangamizwa watu wa makhandaki yenye moto wenye kuni nyingi. Walipokuwa wamekaa hapo. Na wao ni mashahidi wa yale waliyokuwa wakiwafanyia Waumini. Nao hawakuona baya lolote kwao ila kuwa wakimuamini Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Msifiwa. Ambaye Anao Ufalme wa mbingu na ardhi; na Mwenyezi Mungu ni shahidi wa kila kitu.” (85:4-9)

Kama hivi ametaja Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى katika sira, kwamba ambaye aliwaua watu wa mahandakini alikuwa ni Dhu-An-Nawaas, na jina lake ni Zurah na aliitwa hivi katika zama za utawala wake Yusuf عليه السلام na yeye ni mtoto wa Tubaan Asad Abu Karb. Na yeye ndiye *Tabba* ambaye aliipiga vita Madina na akaivalisha Al-Kaaba.² Na baadhi ya watu katika Yemen waliingia Uyahudi kupitia kwake. Ameitaja Khabari hii Ibnu Ishaq رحمه الله تعالى kwa upana wake.

¹ Muslim 4:2299.

² Ibn Hishaam 1:36.

Dhu An-Nawaas Aliwaua katika asubuhi moja ndani ya mahandaki watu elfu ishirini (20,000), na hakuokoka katika wao isipokuwa mtu mmoja ambaye alikuwa anaitwa Daus Dhou Thaalaban alikimbia hali ya kupanda farasi na wakamfukuza kwa nyuma yake na hawakumpata hadi akaenda kwa Kaisari Mfalme wa Sham. Akamuandikia Najashi mfalme wa Uhabeshi, akapeleka pamoja naye Jeshi la Manaswara wa Habeshi, akiwa mbele yao Aryat na Abraha na wakaiokoa Yemen, kutoka mikononi mwa Mayahudi. Na akaenda Dhu An-Nawaas hali ya kukimbia akaingia baharini akazama. Ufalme wa Habeshi uliendelea kuwa mikononi mwa Manaswara kwa muda wa miaka sabini.

Kisha akaiokoa Saif bin Dhi Yazin Al-Himyari kutoka mikononi mwa Manaswara wakati alipoomba msaada wa jeshi kutoka kwa Kisra Mfalme wa Fursi, akapeleka Wanajeshi na wafungwa karibu ya watu mia saba (700) waliyoikomboa Yemen na kwa sababu hiyo ufalme ukarejea kwa Himyar.

Tutataja sehemu ya khabari hiyo Apendapo Allah تعالى katika tafsiri ya Surat Fyl. Anasema:

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَابِ الْفِيلِ ﴿١﴾

“Kwani hukuona jinsi Mola Wako Mlezi Alivyowatenda wale wenye tembo?”(105:1)

Malipo ya Watu wa Mahandaki

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ فَتَنُوا الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ

“Hakika waliowafitini Waumini wanaume na Waumini wanawake.”

Maana: Waliwachoma moto. Ameyasema hayo Ibnu Abbas, Mujahid, Qatadah, Adh-Dhahak na Ibnu Abza رضي الله عنهم¹

ثُمَّ لَمْ يَتُوبُوا

“Kisha hawakutubu.” Maana yake: Wasiepukane na yale waliyoyafanya na wakajuta juu ya yale waliyoyatanguliza.

¹ At-Tabari 24:343, 344.

فَلَهُمْ عَذَابٌ جَهَنَّمُ وَهُمْ عَذَابُ الْحَرِيقِ ﴿١١﴾

“Basi watapata adhabu ya Jahannamu na watapata adhabu ya kuungua.”

Na hilo ni kwa sababu ya kuwa malipo yanakuwa ni katika jinsi ya matendo. Amesema Hassan Basry, ‘Utazameni ukarimu huu wamewaua wapenzi wake, na hali ya kuwa Yeye bado Anawaita kwenye kutubia na kutaka msamaha.

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ هُمْ جَنَّاتُ تَجْرَى مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ؕ ذَلِكَ الْفَوْزُ
الْكَبِيرُ ﴿١٢﴾ إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿١٣﴾ إِنَّهُ هُوَ يُتَدَبَّرُ وَيُعِيدُ ﴿١٤﴾ وَهُوَ الْغَفُورُ
الْوَدُودُ ﴿١٥﴾ ذُو الْعَرْشِ الْمَجِيدُ ﴿١٦﴾ فَعَالٌ لِّمَا يُرِيدُ ﴿١٧﴾ هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْجُنُودِ
﴿١٨﴾ فِرْعَوْنَ وَثَمُودَ ﴿١٩﴾ بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي تَكْذِيبٍ ﴿٢٠﴾ وَاللَّهُ مِنْ وَرَائِهِمْ مُحِيطٌ ﴿٢١﴾
بَلْ هُوَ قُرْءَانٌ مَجِيدٌ ﴿٢٢﴾ فِي لَوْحٍ مَحْفُوظٍ ﴿٢٣﴾

11. Hakika walioamini na wakatenda mema watapata Bustani zenye mito ipitayo kati yake. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

12. Hakika kutesa kwa Mola Wako Mlezi ni kukali.

13. Yeye Ndiye Anayanzisha na Ndiye Anayerejeza tena.

14. Naye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Mapenzi.

15. Mwenye Kiti cha Enzi, Mtukufu.

16. Atendaye Ayatakayo.

17. Je! Zimekuwasilia khabari za majeshi?

18. Ya Firauni na Thamudi?

19. Lakini waliokufuru wamo katika kukadhibisha.

20. Na Mwenyezi Mungu nyuma yao Amewazunguka.

21. Bali hii ni Qur’ani Tukufu

22. Katika Ubao Uliohifadhiwa.”

Malipo ya Watu Wema na Mateso Makali kwa Makafiri Maadui wa Allah

تعالى.

Anaeleza Allah تعالى kuhusu waja Wake waumini kwamba,

هَمْ جَنَّتْ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Watapata Bustani zenye mito ipitayo kati yake.”

Kinyume na yale Aliyowaandalia maadui zake, miongoni mwa moto na maji ya moto. Na kwa sababu hiyo Amesema:

ذَلِكَ الْفَوْزُ الْكَبِيرُ ﴿١٠﴾

“Huko ndiko kufuzu kukubwa”. Kisha Allah تعالى Akasema tena,

إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿١١﴾

“Hakika kutesa kwa Mola Wako Mlezi ni kukali”.

Maana yake: Hakika makamato na mateso Yake kwa maadui Zake, wale waliowakadhibisha wajumbe Wake na wakayapa mgongo maamrishi Yake, kwa hakika mateso hayo ni makubwa yenye nguvu mno. Kwani Yeye Allah تعالى ni Mwenye Nguvu Kubwa sana Ambaye Alitakalo linakuwa, kama Alivyolitaka, kwa mpepeso wa jicho au chini ya hapo. Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى,

إِنَّهُ هُوَ يُبَدِّلُ وَيُعِيدُ ﴿١٢﴾

“Yeye Ndiye Anayanzisha na Ndiye Anaye rejeza tena.”

Maana yake: Kutokana na Nguvu Zake na Uwezo Wake uliokamilika Analianza umbile, na Analirejesha kama Alivyolianza. Kama Alivyolianza pasi na kuwepo mwenye kumkataza wala mwenye kumzuia,

وَهُوَ الْغَفُورُ الْوَدُودُ ﴿١٣﴾

“Naye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Mapenzi.” Maana yake: Anasamehe makosa ya mwenye kutubia Kwake na akanyenyekoa mbele Yake, japokuwa makosa yanatokana na kitu chochote kitakachokuwa. Ama *Al-Waduud* amelielezea Ibnu Abbas رضي الله عنهما kwa kusema kuwa maana yake ni: Mwingi wa upendo.¹¹ At-Tabari 24:346.

ذُو الْعَرْشِ

“Mwenye Kiti cha Enzi” Maana yake: Mwenye Arshi Tukufu ambayo iko juu ya viumbe wote.

الْمَجِيدُ

“Mtukufu” Katika neno hili *Al-Majiid* hapa pana tafsiri mbili na zote ni sahihi. Kwa maana ya sifa ya Mwenyezi Mungu au kwa maana ya sifa ya Arshi Yake Allah تعالى.

فَعَالٌ لِّمَا يُرِيدُ

“Atendaye Ayatakayo.”

Maana yake: Wakati wowote Atakapotaka Kufanya kitu hapana mwenye kuipinga hukumu Yake, na haulizwi lile Alifanyalo, kwa sababu ya Ukubwa Wake na Kutenza Nguvu Kwake, na Hekima Yake na Uadilifu Wake. Kama tulivyopokea kutoka kwa Abubakar As-Siddiq رضي الله عنه kwamba yeye aliambiwa na hali ya kuwa yuko katika ugonjwa wa kufa, “Je, mganga amekuchunguza?” Akasema: “Ndiyo.” Wakasema: “Amekuambia nini?” ‘Akasema: “Ameniambia, hakika Mimi Ninafanya lile Nilitakalo.”¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

هَلْ أَتَتْكَ حَدِيثُ الْجُنُودِ ۖ فِرْعَوْنَ وَثَمُودَ

“Je! Zimekuwasilia khabari za majeshi? Ya Firauni na Thamudi?”

Maana yake: Je yamekufikia yaliyowashukia miongoni mwa adhabu na Akawateremshia miongoni mwa mateso ambayo hakuyarudisha kuyaepusha na wao mtu yeyote?. Na huu ni uthibitisho wa Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ

“Hakika kutesa kwa Mola Wako Mlezi ni kukali.”

Maana yake: Atakapomkamata dhalimu Humkamata makamato yenye kuumiza na makali sana. Makamato ya Mwenye Kushinda, Mwenye Uweza. Na Kauli Yake Allah تعالى:

¹ Al-Qurtubi 19:297.

بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي تَكْذِيبٍ ﴿٨٥﴾

“Lakini waliokufuru wamo katika kukadhibisha.”

Maana yake: Wao wamo katika shaka, wasiwasi, ukafiri na upingaji,

وَاللَّهُ مِنْ وَرَائِهِم مَّحِيطٌ ﴿٨٦﴾

“Na Mwenyezi Mungu nyuma yao Amewazunguka.”

Maana yake: Yeye ni Mwenye Uwezo juu yao, Mwenye Kuwatenza Nguvu, hawamkimbii na hawamshindi.

بَلْ هُوَ قُرْآنٌ مَّجِيدٌ ﴿٨٧﴾

“Bali hii ni Qur’ani Tukufu.”

Maana yake: Kubwa na Tukufu mno

فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ ﴿٨٨﴾

“Katika Ubao Ulihifadhiwa.”

Maana yake: Hiyo Qur’an iko katika ulimwengu wa juu, imehifadhiwa dhidi ya kuongezwa, kupunguzwa, kupotoshwa na kubadilishwa.

* * *

Tafsiri ya Suratu Tariq Sura ya 86 Iliteremshwa Makkah

Ubora wa *Suratu At-Tariq*

Ampokea Annasai kutoka kwa Jabir رضي الله عنه amesema; Alisali Muadhhi رضي الله عنه Sala ya Magharibi akasoma sura ya *Baqarah* na *An-Nisaa* akasema Mtume ﷺ,

«أَفْتَانُ أَنْتَ يَا مُعَاذُ، مَا كَانَ يَكْفِيكَ أَنْ تَقْرَأَ بِالسَّمَاءِ وَالطَّارِقِ وَالشَّمْسِ وَصُحَاهَا
وَنُحُومَهَا؟»

“Je umekuwa ni mfitinishaji ewe Muadh, ilikuwa inatosha kusoma; wassamai watwariq, wasshamsi wa Dhuhaha na mfano wake.”¹

* * *

¹ An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:512.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الطَّارِقِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالسَّمَاءِ وَالطَّارِقِ ﴿١﴾ وَمَا أَدْرَاكَ ﴿٢﴾
 مَا الطَّارِقِ ﴿٣﴾ النَّجْمُ الثَّاقِبُ ﴿٤﴾
 إِنَّ كُلَّ نَفْسٍ لَّمَّا عَلَيْهَا حَافِظٌ ﴿٥﴾
 فَلْيَنْظُرِ الْإِنْسَانُ مِمَّ خُلِقَ ﴿٦﴾ خُلِقَ مِنْ مَّاءٍ دَافِقٍ ﴿٧﴾
 تَخْرُجُ مِنْ بَيْنِ الصُّلْبِ وَالتَّرَائِبِ ﴿٨﴾ إِنَّهُ عَلَى رَجْعِهِ
 لِقَادِرٌ ﴿٩﴾ يَوْمَ تُبْلَى السَّرَائِرُ ﴿١٠﴾ فَمَا لَهُ مِنْ قُوَّةٍ وَلَا
 نَاصِرٍ ﴿١١﴾ وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الرَّجْعِ ﴿١٢﴾ وَالْأَرْضِ ذَاتِ
 الصَّدَعِ ﴿١٣﴾ إِنَّهُ لَقَوْلٌ فَضْلٌ ﴿١٤﴾ وَمَا هُوَ بِأَهْوَىٰ ﴿١٥﴾
 إِيَّاهُمْ يَكِيدُونَ كَيْدًا ﴿١٦﴾ وَأَكِيدُ كَيْدًا ﴿١٧﴾ فَمَهْلٍ
 الْكَافِرِينَ أَمْهَلُهُمْ رُوَيْدًا ﴿١٨﴾

وَالسَّمَاءِ وَالطَّارِقِ ﴿١﴾ وَمَا أَدْرَاكَ
 مَا الطَّارِقِ ﴿٣﴾ النَّجْمُ الثَّاقِبُ ﴿٤﴾
 إِنَّ كُلَّ نَفْسٍ لَّمَّا عَلَيْهَا حَافِظٌ ﴿٥﴾
 فَلْيَنْظُرِ الْإِنْسَانُ مِمَّ خُلِقَ ﴿٦﴾ خُلِقَ
 مِنْ مَّاءٍ دَافِقٍ ﴿٧﴾ تَخْرُجُ مِنْ بَيْنِ
 الصُّلْبِ وَالتَّرَائِبِ ﴿٨﴾ إِنَّهُ عَلَى
 رَجْعِهِ لِقَادِرٌ ﴿٩﴾ يَوْمَ تُبْلَى
 السَّرَائِرُ ﴿١٠﴾ فَمَا لَهُ مِنْ قُوَّةٍ وَلَا
 نَاصِرٍ ﴿١١﴾

1. Naapa kwa mbingu na kinachokuja usiku!
2. Na nini kitakacho kujuulisha ni nini hicho kinachokuja usiku?

3. Ni Nyota yenye mwanga mkali.
4. Hapana nafsi ila inayo mwangalizi.
5. Hebu na ajitazame mwanaadamu ameumbwa kwa kitu gani?
6. Ameumbwa kwa maji yatokayo kwa kuchupa,
7. Yatokayo baina ya mifupa ya mgongo na mbavu.
8. Hakika Yeye Ana Uweza wa Kumrudisha.
9. Siku zitakapodhihirishwa siri.
10. Basi hatakuwa na nguvu wala msaidizi.

Kiapo Juu ya Kuwa Mwanadamu ni Mwenye Kuzungukwa na Utaratibu wa Allah تعالى.

Allah تعالى Anaapa kwa msingi wa vile ambavyo Amevifanya ndani yake miongoni mwa nyota zenye mwangaza.

Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى:

وَالسَّمَاءِ وَالطَّارِقِ ﴿١﴾

“Naapa kwa mbingu na kinachokuja usiku!”

Kisha Amesema:

وَمَا أَدْرَبكَ مَا الطَّارِقُ ﴿٢﴾

“Na nini kitakachokujuulisha ni nini hicho kinachokuja usiku?”

Kisha Allah تعالى Anaielezea kwa Kusema:

النَّجْمُ الثَّاقِبُ ﴿٣﴾

“Ni nyota yenye mwanga mkali.”

Amesema Qatada na wengine; hakika hakuna jambo jingine imeitwa nyota kuwa inakuja usiku, hakika si vingine inaonekana usiku na inajificha mchana.¹ Yanayapa nguvu maelezo haya yaliyokuja katika Hadith sahihi kwamba Mtume ﷺ amekataza mtu kumgongea ahli wake usiku. Kwa maana; kuwaendea ghafla usiku².

Na Kauli Yake Allah تعالى:

النَّاقِبُ ﴿٤﴾

“Yenye mwanga mkali.”

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما, yenye kuangaza.³ Na amesema Ikrimah; hiyo ni yenye kuangaza na yenye kuwaunguza Mashetani.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

¹ At-Tabari 24:351.

² Fat’hul Al-Bari 9:251.

³ At-Tabari 24:352.

إِنَّ كُلَّ نَفْسٍ لَّمَّا عَلَيْهَا حَافِظٌ ﴿٨٦﴾

“Hapana nafsi ila inayo mwangalizi.”

Maana yake: Kila nafsi pana juu yake kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu chenye kuihifadhi, kinachokilinda na madhara mbalimbali. Kama Alivyosema Allah تعالى:

لَهُد مُعَقِّبَتٌ مِّنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ يَحْفَظُونَهُ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ ﴿٨٦﴾

“Kila mtu analo kundi la malaika mbele yake na nyuma yake linamlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu...” (13:11)

Namna ya Kuumbwa Mwanadamu ni Dalili Juu ya Uwezo wa Mwenyezi Mungu wa Kumrejsha Tena.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَلْيَنْظُرِ الْإِنْسَانُ مِمَّ خُلِقَ ﴿٨٧﴾

“Hebu na ajitazame mwanaadamu ameumbwa kwa kitu gani?”

Huu ni uzinduzi kwa mwanadamu juu ya udhaifu wa asili yake ambayo ameumbwa kutokana nayo. Na ni muongozo kwake kwenye kukiri kuwa atarejeshwa kwenye maisha ya akhera. Kwa sababu Mwenye Kuweza Kuumba kwa mara ya kwanza ni Muweza wa Kurudisha kwa njia bora zaidi. Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ ﴿٨٧﴾

“Yeye Ndiye Anayeanzisha Uumbaji, kisha Ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi kwake...” (30:27)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

خُلِقَ مِنْ مَّاءٍ دَافِقٍ ﴿٨٨﴾

“Ameumbwa kwa maji yatokayo kwa kuchupa.”

Anakusudia manii yanatoka kwa kuruka kwa mwanamume na mwanamke. Huzalika kutokana na wawili hao mtoto. Kwa Amri ya Allah تعالى, Mwenye Kushinda na Kutukuka. Na kwa sababu hiyo Amesema;

مُخْرَجٌ مِنْ بَيْنِ أَلْصُلْبِ وَالْتَّرَائِبِ ﴿٧﴾

“Yatokayo baina ya mifupa ya mgongo na mbavu.”

Anakusudia mgongo wa mwanaume na mifupa ya kifua cha mwanamke - nacho ni kifua chake. Na amesema Shabib bin Bishr kutoka kwa Ikrimah kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

مُخْرَجٌ مِنْ بَيْنِ أَلْصُلْبِ وَالْتَّرَائِبِ ﴿٧﴾

“Yatokayo baina ya mifupa ya mgongo na mbavu.”

Mgongo wa mwanaume na mifupa ya kifua cha mwanamke yakiwa ya manjano mepesi, hawi mtoto isipokuwa kutokana na wawili hao.¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّهُ عَلَىٰ رَجْعِهِ لَقَادِرٌ ﴿٨﴾

“Hakika Yeye Ana Uweza wa Kumrudisha.”

Hakika Yeye juu ya Kumrejisha mtu huyu aliyeumbwa kutokana na maji yenye kutoka kwa kuruka. Maana; Kumrudisha na Kumfufua kwa ajili ya nyumba ya akhera ni Mwenye Kuweza hilo. Kwa sababu Mwenye Kuweza Kuumba kwa mara ya kwanza, Ataweza Kuumba kwa mara ya pili, na Ameutaja Allah تعالى ushahidi huo sehemu nyingi sana katika Qur'an.

Siku ya Qiyama Hatakuwa Binadamu na Uwezo wala Nusra

Na kwa sababu hiyo Allah تعالى Anasema:

يَوْمَ تُبْلَى السَّرَائِرُ ﴿٩﴾

“Siku zitakapodhihirishwa siri.”

Maana yake: Siku ya Qiyama zitadhihirishwa ndani yake siri. Maana: Zitadhihiri na zitaonekana, na itabaki siri kuwa ni dhahiri na kilichofichwa kuwa wazi. Na imethibiti katika sahihi mbili, kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema;

¹ Ad-Durr Al-Manthur 8:475.

«يُرْفَعُ لِكُلِّ غَادِرٍ لِرَاءِ عِنْدَ اسْتِثْبَاتِهِ يُقَالُ: هَذِهِ غَدْرَةُ فُلَانٍ بِنِ فُلَانٍ»

*"Itanyanyuliwa bendera matakoni kwa kila mwenye khiana na patasemwa hii ni khiana ya fulani bin fulani."*¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَمَا لَهُ

"...Basi hatakuwa..."

Maana yake: Mwanadamu siku ya Qiyama.

مِنْ قُوَّةٍ

"...na nguvu..."

Maana yake: kutokana na yeye mwenyewe.

وَلَا نَاصِرٍ

"wala msaidizi."

Maana yake: kutoka nje yake. Maana: hawezi kuiokoa nafsi yake, na adhabu ya Allah تعالى na Hawezi kumfanyia jambo hilo mtu yeyote.

وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الرَّجْعِ ۝ وَالْأَرْضِ ذَاتِ الصَّدْعِ ۝ إِنَّهُ لَقَوْلٌ فَضْلٌ ۝ وَمَا هُوَ بِأَهْزَلٍ ۝ إِنَّهُمْ يَكِيدُونَ كَيْدًا ۝ وَأَكِيدُ كَيْدًا ۝ فَمَهْلِكُ الْكَافِرِينَ أَهْمَهُمْ ۝ رُوَيْدًا ۝

11. Naapa kwa mbingu yenye marejeo!

12. Na kwa ardhi inayopasuka!

13. Hakika hii ni kauli ya kupambanua.

14. Wala si mzaha.

15. Hakika wao wanapanga mpango.

16. Na Mimi Napanga mpango.

17. Basi wape muhula makafiri - wape muhula pole pole.

¹ Al-Bukhari no. 6177, 6178, na Muslim 3:1359.

Kiapo Juu ya Kuwa Qur'an ni Ukweli na Kufeli kwa Wapinzani Wake.

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما. "Al-Raju" ni mvua.¹ Imepokewa kutoka kwake kuwa "Al-Raju" Ni mawingu ambayo ndani yake yana mvua. Na imepokewa tena kutoka kwake,

وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الرَّجْعِ ﴿١١﴾

"Naapa kwa mbingu yenye marejeo!"

Zinanyesha kisha zinanyesha. Na amesema Qatada: Yanarejesha rizki ya waja kila mwaka na lau si hivyo wangeangamia wao na wanyama wao.²

وَالْأَرْضِ ذَاتِ الصَّدْعِ ﴿١٢﴾

"Na kwa ardhi inayopasuka!"

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما, Huko ni kupasuka kwa Ardhi kwa ajili ya kuota mimea.³

Na kama hivyo amesema Said Ibn Jubair, Ikrimah, Abu Malik, Adh-Dhahak, Hassan, Qatada na Suddiy na wengine.⁴

إِنَّهُ لَقَوْلٌ فَصْلٌ ﴿١٣﴾

"Hakika hii ni kauli ya kupambanua."

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما ni maneno ya kweli.⁵ Na kama hivyo amesema Qatadah na amesema mwengine, "Ni hukumu adilifu."

وَمَا هُوَ بِأَهْزَلٍ ﴿١٤﴾

"Wala si mzaha."

Kisha Ameeleza kuhusu makafiri kwamba wao wanakadhibisha hiyo Qur'an na wanawazuia watu na njia Yake. Kwa hiyo Amesema;

¹ At-Tabari 24:360.

² At-Tabari 24:360.

³ At-Tabari 24:361.

⁴ Ad-Durr Al-Manthur 8:477.

⁵ At-Tabari 24:362.

إِنَّهُمْ يَكِيدُونَ كَيْدًا ﴿١٦﴾

“Hakika wao wanapanga mpango.”

Maana yake: Wanawafanyia vituko watu katika kuwalingania watu kinyume na vilivyomo ndani ya Qur’an.

فَمَهْلِكُ الْكَافِرِينَ ﴿١٧﴾

“Basi wape muhula makafiri.”

Maana yake: Wape muda na usiwafanyie haraka.

أَمْهَلُهُمْ رُؤْيَا ﴿١٨﴾

“Wape muhula pole pole.”

Maana yake: Muda mchache. Maana yake: Punde hivi utaona ni yapi yale nitakayowateremshia miongoni mwa adhabu, mateso na maangamizi,

نُمتِعُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿١٩﴾

“Tunawastarehesha kwa uchache, kisha Tutawasukuma kwenye adhabu ngumu.” (31:24)

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu At-Twariq* na shukrani ni kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye Kuneemesha.

* * *

Tafsiri ya Suratul A'la¹ Sura ya 87 Iliteremshwa Makkah

Ubora wa Suratul A'la

Sura hii imeshuka Makka. Imeshuka kabla ya Hijra. Na dalili juu ya hilo ni yale yaliyopokelewa na Bukhari kutoka kwa Baraa bin Aazib رضي الله عنه, amesema; mtu wa kwanza aliyefika kwetu katika masahaba wa Mtume ﷺ ni Mus'ab bin Umair na Ibn Umri Makhtoum رضي الله عنهما. Wakawa wanatusomea Qur'an kisha akaja Ammar, Bilal na Saad رضي الله عنهم, kisha akaja Mtume ﷺ. Sikuwaona watu wa Madina wamefurahi kwa jambo kama kufurahishwa kwao kutokana na kuja kwa Mtume ﷺ, mpaka nikawaona watoto wadogo wanasema, huyu Mtume ﷺ amekuja. Na hakuja mpaka nimesoma,

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴿١﴾

"Litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye juu kabisa."

Pamoja na sura nyingine mfano wake.²

Na imethibiti katika sahihi mbili kwamba Mtume ﷺ alimuambia Mu'adh رضي الله عنه,

«مَلَأَ صَالِيَتُ بِـ ﴿سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى﴾ ﴿وَالسَّمِيعِ وَخَصْمَهَا﴾ ﴿وَأَتَيْلِ إِذَا يَتَنُ﴾»

*"Kwa nini usingesali kwa Sabbihisma Rabbika Al-A'laa, Wash-Shamsi wadhuhaha, Wallayli idhaa Yaghshaa."*³

Ampokea Imam Ahmad kutoka kwa An-Nuuman bin Bashir kwamba Mtume ﷺ alisoma katika Idd mbili,

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴿١﴾ — — هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَاشِيَةِ ﴿٢﴾

"Litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye juu kabisa,"(87:1) "Je! Imekufikia khabari ya msiba wa kufudikiza?" (88:1)

¹ Fat'hul Al-Bari 8:569.

² Fat'hul Al-Bari 2:234, na Muslim 1:340.

Na ikifika siku ya Ijumaa¹ husoma zote mbili, ameyapokea hayo Muslim katika sahihi yake, Abu Daud, At-Tirmidhi na An-Nasai. Na ameyapokea hayo Ibn Majah na tamko ni la Muslim na watu wa Sunna. Mtume ﷺ alikuwa akisoma katika Iddi mbili na siku za Ijumaa,

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴿١﴾ — — هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَدَشِيَةِ ﴿٢﴾

"Litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye juu kabisa." (87:1) "Je! Imekufikia khabari ya msiba wa kufudikiza?" (88:1)

Na huenda yakakusanyika mawili hayo katika siku moja huzisoma sura zote mbili. Na Amepokea Imam Ahmad katika kitabu chake Musnad kutokana na Hadith ya Ubay bin Kaab, na Abdillahi bin Abbas, na Abdurahman bin Abzaa رضي الله عنهم na Aisha رضي الله عنها Mama wa Waumini kwamba Mtume ﷺ alikuwa akisoma katika wistir,

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴿١﴾ — — قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ ﴿٢﴾ — قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴿٣﴾

"Litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye juu kabisa." (87:1) , "Sema: Enyi makafiri! Sema." (109:1), "Yeye Mwenyezi Mungu ni wa Pekee." (112:1)

Ameongeza Aishah رضي الله عنها pia husoma *Muawidha* mbili. Yaani sura za kujikinga na mambo mabaya, (*Suratu Al-Falaq* na *An-Nas*).²

* * *

¹ Ahmad 4:271.

² Ahmad kutoka kwa Ubayy 5:123, Ibn Abbas 1:299, Ibn Abza 3:406, na Aishah 6:227.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْاَعْلَىٰ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَىٰ ﴿١﴾ الَّذِي خَلَقَ فَسَوَّىٰ ﴿٢﴾
 وَالَّذِي قَدَّرَ فَهَدَىٰ ﴿٣﴾ وَالَّذِي أَخْرَجَ الْمَرْعَىٰ ﴿٤﴾
 فَجَعَلَهُ غُثَاءً أَحْوَىٰ ﴿٥﴾ سَنُقْرِئُكَ فَلَا تَنسَىٰ ﴿٦﴾ إِلَّا
 مَا شَاءَ اللَّهُ ۗ إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ وَمَا يَخْفَىٰ ﴿٧﴾ وَنُيَسِّرُكَ
 لِلْيُسْرَىٰ ﴿٨﴾ فَذَكِّرْ ۚ إِن نَّفَعَتِ الذِّكْرَىٰ ﴿٩﴾ سَيَذَكِّرْ مَنْ
 يَخْشَىٰ ﴿١٠﴾ وَيَتَجَنَّبُهَا الْأَشْقَىٰ ﴿١١﴾ الَّذِي يَصْلَى النَّارَ
 الْكُبْرَىٰ ﴿١٢﴾ ثُمَّ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ ﴿١٣﴾ قَدْ أَفْلَحَ
 مَنْ تَزَكَّىٰ ﴿١٤﴾ وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّىٰ ﴿١٥﴾ بَلْ تُؤَظُّرُونَ
 الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿١٦﴾ وَالْآخِرَةَ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ﴿١٧﴾ إِنَّ هَذَا
 لَفِي الصُّحُفِ الْأُولَىٰ ﴿١٨﴾ صُحُفِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ ﴿١٩﴾

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَىٰ ﴿١﴾ الَّذِي
 خَلَقَ فَسَوَّىٰ ﴿٢﴾ وَالَّذِي قَدَّرَ
 فَهَدَىٰ ﴿٣﴾ وَالَّذِي أَخْرَجَ الْمَرْعَىٰ
 فَجَعَلَهُ غُثَاءً أَحْوَىٰ ﴿٤﴾
 سَنُقْرِئُكَ فَلَا تَنسَىٰ ﴿٥﴾ إِلَّا مَا
 شَاءَ اللَّهُ ۗ إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ وَمَا
 يَخْفَىٰ ﴿٦﴾ وَنُيَسِّرُكَ لِلْيُسْرَىٰ ﴿٧﴾
 فَذَكِّرْ ۚ إِن نَّفَعَتِ الذِّكْرَىٰ ﴿٨﴾
 سَيَذَكِّرْ مَنْ يَخْشَىٰ ﴿٩﴾ وَيَتَجَنَّبُهَا
 الْأَشْقَىٰ ﴿١٠﴾ الَّذِي يَصْلَى النَّارَ
 الْكُبْرَىٰ ﴿١١﴾ ثُمَّ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا
 يَحْيَىٰ ﴿١٢﴾

1. Litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye juu kabisa.
2. Aliyeumba, na Akaweka sawa.
3. Na Ambaye Amekadiria na Akaongoa.
4. Na Aliyeotesha malisho.
5. Kisha Akayafanya makavu, meusi.
6. Tutakusomesha wala hutasahau.

7. Ila Akipenda Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye Anayajua yaliyodhaahiri na yaliyofichikana.

8. Na Tutakusahilishia yawe mepesi.

9. Basi kumbusha, kama kukumbusha kunafaa.

10. Atakumbuka mwenye kuogopa.

11. Na atajitenga mbali nayo mpotovu,

12. Ambaye atauingia Moto mkubwa.

13. Tena humo hatakufa wala hawi hai.

Amri ya Kusabbih na Majibu Yake.

Amesema Imam Ahmad kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kwamba Mtume ﷺ alikuwa pindi akisoma:

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴿١﴾

"Litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye juu kabisa."

Husema,

«سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَى»

"Subhana Rabbiyal A'ala"¹ "Ametakasika Mola Wangu Mtukufu"

Na amepokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Abi Ishak Al Hamdan kwamba Ibn Abbas رضي الله عنهما alipokuwa akisoma,

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴿١﴾

"Litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye juu kabisa."

Anasema, 'Subhana Rabbiyal A'ala.' Kwa maana: Ametakasika Mola Wangu Mtukufu. Na pindi akisoma,

لَا أُقْسِمُ بِيَوْمِ الْقِيَامَةِ ﴿١﴾

"Ninaapa kwa Siku ya Kiyama!" (75:1)

¹ Ahmad 1:232, Isnadi yake ni dhaifu.

Akifika mwisho wake,

أَلَيْسَ ذَلِكَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَن نُّجِئَ الْمَوْتَىٰ ﴿٤٠﴾

"Je! Huyu hakuwa ni Muweza wa Kufufua wafu?" (75:40)

Husema "Subhanaka wabalaa".¹ Kwa maana: Ametakasika na Unaweza Kufanya hivyo. Na amesema Qatada,

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَىٰ ﴿٤١﴾

"Litakase Jina la Mola Wako Mlezi Aliye juu kabisa."

Tunajua kwamba Mtume ﷺ alipokuwa anaisoma sura hiyo husema,

«سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَىٰ»

"Subhana Rabbiyal A'ala"² "Ametakasika Mola Wangu Mtukufu."

Kuumba, Kukadiria na Kuotesha Mimea

Na Kauli Yake Allah تعالى:

الَّذِي خَلَقَ فَسَوَّىٰ ﴿٤٢﴾

"Aliyeumba, na Akaweka sawa."

Maana yake: Amewaumba viumbe na Amekifanya sawa kila kiumbe katika uzuri wa umbo.

وَالَّذِي قَدَّرَ فَهَدَىٰ ﴿٤٣﴾

"Na ambaye Amekadiria na Akaongoa."

Amesema Mujahid, Amemuongoza mwanadamu kwa uovu na wema, na Amewaongoza wanyama kwenye malisho yao.³

Na aya hii ni kama Kauli Yake Allah تعالى Akimuelezea Musa عليه السلام kwamba yeye alimuambia Firaun,

¹ At-Tabari 24:367.

² At-Tabari 24:368.

³ At-Tabari 24:369.

رَبُّنَا الَّذِي أَعْطَى كُلَّ شَيْءٍ حَلْقَهُ ثُمَّ هَدَى ﴿٥٠﴾

“...Mola Wetu Mlezi ni Yule Aliyekipa kila kitu umbo lake, kisha Akakiongoa.” (20:50)

Maana yake: Amekadiria makadirio makubwa na Akawaongoza viumbe kwenye makadirio hayo. Kama ilivyothibiti katika Hadithi ya Muslim kutoka kwa Abdillahi bin Amri رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ اللَّهَ قَدَّرَ مَقَادِيرَ الْخَلَائِقِ قَبْلَ أَنْ يَخْلُقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِخَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ وَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ»

“Hakika Mwenyezi Mungu Alikadiria makadirio ya viumbe kabla Hajaumba mbingu na Ardhi kwa muda wa miaka Elfu khamsini na ilikuwa Arshi yake ipo juu ya maji.”²

Juu ya Kauli ya Allah تعالى:

وَالَّذِي أَخْرَجَ الْمَرْعَى ﴿٥١﴾

“Na Aliyeotesha malisho.”

Maana yake: Katika namna zote za mimea,

فَجَعَلَهُ غُثَاءً أَحْوَى ﴿٥٢﴾

“Kisha Akayafanya makavu, meusi.” Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما, yenye kukatika katika yenye kubadilika.³ Na imepokewa kutoka kwa Mujahid na Qatada na Ibn Zaid mfano wake.⁴

Mtume ﷺ Hasahau Wahy ila Atakapotaka Allah تعالى

Allah تعالى Amesema:

سَنُقْرَأُكَ

“Tutakusomesha,..” Maana yake: Muhammad ﷺ.

¹ Muslim 4:2044.

² At-Tabari 24:369.

³ At-Tabari 24:369, 370.

﴿ فَلَا تَنْسَى ﴾

“Wala hutasahu.” Na haya ni maelezo kutoka kwa Allah تعالى na ni ahadi kutoka Kwake, kwamba Yeye Atamsomesha usomaji ambao hatasahu.

﴿ إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ ﴾

“Ila Akipenda Mwenyezi Mungu.” Na pamesemwa kwamba kusudio la kauli Yake;

﴿ فَلَا تَنْسَى ﴾

“Wala hutasahu.” Na amesema Qatadah رضي الله عنه; alikuwa Mtume ﷺ hasahau kitu chochote isipokuwa kile Alichokitaka Allah تعالى:

﴿ إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ وَمَا يَخْفَى ﴾

“Hakika Yeye Anayajua yaliyodhaahiri na yaliyofichikana.”

Maana yake: Anayajua yale wanayoyadhihirisha waja na yale wanayoyaficha miongoni mwa maneno yao. Hakijifichi Kwake katika hayo kitu chochote.

﴿ وَنُيَسِّرُكَ لِلْيُسْرَى ﴾

“Na Tutakusahilishia yawe mepesi.” Maana yake: Tutakurahisishia matendo ya kheri na maneno yake. Na Tutakuwekea sheria nyepesi iliyonyooka, yenye uadilifu, hapana kupinda pinda ndani yake, wala hapana ugumu wala uzito.

Amri ya Kukumbusha

Kisha, Allah تعالى Anasema:

﴿ فَذَكِّرْ إِنْ نَفَعَتِ الذِّكْرَى ﴾

“Basi kumbusha, kama kukumbusha kunafaa.” Maana yake: Onya yatakapofaa maonyo.

Hapa tunapata jambo la kufanya adabu katika kueneza elimu, kwa hiyo asiweke mbele ya wasiokuwa watu wake, kama alivyosema Amiri Muuminina Ali رضي الله عنه, ‘Hukuwa wewe unawazungumzia watu maneno ambayo hayafikii akilini mwa watu, bali baadhi yake ni mtihani kwa baadhi yao. Na amesema, ‘wazungumzie watu yale wanayoyajua. Je, mnapenda watu wamkadhibishe

Allah تعالى na Mtume Wake?."1 Na Kauli Yake Allah تعالى:

سَيَذَكَّرُ مَنْ تَحْشَى ﴿١﴾

"Atakumbuka mwenye kuogopa." Maana yake: Ataonyeka kwa yale unayoyafikisha ewe Muhammad ﷺ katika moyo wake anayemuogopa Allah تعالى na anajuwa kwamba yeye atakutana Naye.

وَيَتَجَنَّبُهَا الْأَشْقَى ﴿٢﴾ الَّذِي يَصْلَى النَّارَ الْكُبْرَى ﴿٣﴾ ثُمَّ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَى ﴿٤﴾

"Na atajitenga mbali nayo mpotovu. Ambaye atauingia Moto mkubwa. Tena humo hatakufa wala hawi hai."

Maana yake: Hatakufa akapumzika, na hatakuwa nao uhai utakaomnufaisha, bali uhai wenye madhara kwake. Kwani sababu yake atahisi kile anachoadhibiwa kwacho, miongoni mwa adhabu na namna za mateso. Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Abu Said رضي الله عنه amesema, amesema Mtume ﷺ,

«أَمَا أَهْلُ النَّارِ الَّذِينَ هُمْ أَهْلُهَا لَا يَمُوتُونَ وَلَا يَحْيُونَ، وَأَمَا أَنَا سُرُّ يُرِيدُ اللَّهُ بِهِمُ الرَّحْمَةَ فَيُجِيبُهُمْ فِي النَّارِ فَيَدْخُلُ عَلَيْهِمُ الشَّفَعَاءُ فَيَأْخُذُ الرَّجُلُ الضَّارَةَ فَيُنْتِهِمُ - أَوْ قَالَ: يَنْتَبِثُونَ فِي نَهْرِ الْحَيَاةِ، أَوْ قَالَ: الْحَيَاةِ، أَوْ قَالَ: النَّهْرِ الْحَيَّةِ - فَيَنْتَبِثُونَ نَبَاتِ الْحَبَّةِ فِي حَمِيلِ السَّبِيلِ»

"Ama watu wa motoni ambao wanastahili kuwa humo hawatakufa na hawatakuwa wazima. Na ama watu ambao Atawatakia Allah تعالى rehemata Atawafisha katika moto huo. Humo motoni wataingia kwao waombeaji, atalichukua kundi la watu - atawaotesha, au alisema, 'wataota katika mto wa uhai' au alisema, 'katika mto wa maisha' au alisema, 'wanyama', au alisema, 'mto wa peponi' - wataota watu kama zinavyoota mbegu katika takataka za mafuriko."

Mtume ﷺ Amesema,

«أَمَا تَرَوْنَ الشَّجَرَةَ تَكُونُ خَضْرَاءَ، ثُمَّ تَكُونُ صَفْرَاءَ، ثُمَّ تَكُونُ خَضْرَاءَ؟»

"Hivi hamuoni mti unakuwa wa kijani kisha unakuwa wa manjano kisha unakuwa wa kijani."

¹ Al-Bukhari kitabu cha elimu 127 kutoka kwa Ali na Muslim. Al-Muqaddimah kwa hadithi ya Ibn Mas'ud mfano wake.

Wakasema baadhi yao ni kana kwamba Mtume ﷺ alikuwa viungani.¹

Na amepokea Ahmad vilevile kutoka kwa Abi Saiid Khudhri رضى الله عنه amesema, amesema Mtume ﷺ,

«أَنَا أَهْلُ النَّارِ الَّذِينَ هُمْ أَهْلُهَا فَإِنَّهُمْ لَا يَمُوتُونَ فِيهَا وَلَا يَحْيُونَ، وَلَكِنْ أَنَا سَ -
 أَوْ كَمَا قَالَ - نُصِيبُهُمُ النَّارُ بِذُنُوبِهِمْ - أَوْ قَالَ: يَخْطَأِيَانَهُمْ - فَيُيْتِيهِمْ إِمَانَةٌ حَتَّى إِذَا
 صَارُوا فَحَمًا أُذِنَ فِي الشَّفَاعَةِ، فَجِيءَ بِهِمْ ضَبَائِرُ ضَبَائِرٍ فَبُتُوا عَلَى أَنَّهَا الْجَنَّةُ
 فَيَقَالُ: يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ أَفِيضُوا عَلَيْهِمْ، فَيَتَّبِعُونَ نَبَاتَ الْجَنَّةِ تَكُونُ فِي حِمْلِ السَّيْلِ»

“Ama watu wa motoni ambao watastahili kuwa humo, hakika wao hawatakufa humo na hawatakuwa hai, isipokuwa kuna watu au, kama alivyosema, ‘utawapata moto kwa sababu ya madhambi yao’ au alisema, ‘kwa makosa yao atawafisha ufishaji mmoja tu, mpaka watakapokuwa mkaa, patatolewa ruhusa ya kuombewa, wataletwa hali ya kuwa makundi makundi, watakusanywa katika mito ya peponi patasemwa, ‘enyi watu wa peponi wamiminieni, wataota kama inavyoota tembe inayokuwa katika takataka za mafuriko.”

Amesema, akasema mtu mmoja katika wao wakati huo; kana kwamba Mtume ﷺ alikuwa viungani.² Imepokewa pia na Muslim.³

فَدَأْفَلَحَ مَنْ تَرَكَى ۝ وَذَكَرَ أَسْمَرَ رَبِّيهِ فَصَلَّى ۝ بَلْ تُؤْثِرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ۝
 وَالْآخِرَةَ خَيْرٌ وَأَتَقَى ۝ إِنَّ هَذَا لَفِي الصُّحُفِ الْأُولَى ۝ صُحُفِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى ۝

14. Hakika amekwisha fanikiwa aliyejitakasa.

15. Na akakumbuka Jina la Mola Wake Mlezi, na akasali.

16. Lakini nyinyi mnakhiari maisha ya dunia!

17. Na Akhera ni bora na yenye kudumu zaidi.

18. Hakika haya yamo katika Vitabu vya mwanzo.

19. Vitabu vya Ibrahimu na Musa.

¹ Ahmad 3:5.

² Ahmad 3:11.

³ Muslim 1:172.

Ubainifu wa Watu wa Mafanikio

Allah تعالی Anasema:

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ تَزَكَّى ﴿١﴾

“Hakika amekwisha fanikiwa aliye jitakasa.”

Maana: Aliyeitakasa nafsi yake na tabia mbovu na akayafuatilia yale Aliyoyateremsha Allah تعالی juu ya Mjumbe Wake.

وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّى ﴿٢﴾

“Na akakumbuka Jina la Mola Wake Mlezi, na akasali.”

Maana yake: Akasimamisha Sala katika nyakati zake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu, na kwa kuyatii maamrisha na kutekeleza sheria Zake. Imepokelewa kutoka kwa Amiri wa Waumini, Umar bin Abdil Aziz رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى, kuwa yeye alikuwa anawaamrisha watu kutoa sadaka ya *fitr*¹ na akiisoma aya hii,

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ تَزَكَّى ﴿١﴾ وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّى ﴿٢﴾

“Hakika amekwisha fanikiwa aliyejitakasa. Na akakumbuka Jina la Mola Wake Mlezi, na akasali.”

Na amesema Abu Ahwas, atakaponijia mmoja wenu mwenye kuomba na hali ya kuwa yeye anataka kusali na atangulize mbele ya Sala yake sadaka. Kwani Allah تعالی Anasema,

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ تَزَكَّى ﴿١﴾ وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّى ﴿٢﴾

“Hakika amekwishafanikiwa aliyejitakasa. Na akakumbuka Jina la Mola Wake Mlezi, na akasali.”

Qatadah amesema kuhusu Aya hii,

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ تَزَكَّى ﴿١﴾ وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّى ﴿٢﴾

“Hakika amekwisha fanikiwa aliyejitakasa. Na akakumbuka Jina la Mola Wake Mlezi, na akasali.”

Akaisafisha mali yake na akamridhisha Bwana wake.²

¹ At-Tabari 24:374.

² At-Twabari 24/374.

Dunia Haina Thamani kwa Kulinganisha na Akhera.

Kisha Allah تعالیٰ Anasema:

بَلْ تُؤْتِرُونَ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا ﴿١٦﴾

“Lakini nyinyi mnakhiari maisha ya dunia!” Maana yake: Mnayatanguliza juu ya mambo ya akhera na mnayapa kipaumbele mambo ambayo ndani yake kuna manufaa na maslahi yenu katika maisha yenu na kusahau marejeo yenu.

وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ﴿١٧﴾

“Na Akhera ni bora na yenye kudumu zaidi.” Maana yake: Malipo ya Allah تعالیٰ katika nyumba ya akhera ni bora kuliko Duniani, na ni yenye kubaki kwani Dunia ni duni na yenye kumalizika na akhera ni bora na yenye kubaki. Vipi mwenye akili anakipa kipaumbele kile kinachoondoka juu ya kinachobaki? Na anashughulika na kinachoondoka punde hivi, na anaacha kushughulika na nyumba ya kukaa milele.

Amepokea Imam Ahmad رحمه الله تعالى kutoka kwa Abu Mussa Al-Ash-'Ary رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ أَحَبَّ دُنْيَاهُ أَضْرَّ بِآخِرَتِهِ، وَمَنْ أَحَبَّ آخِرَتَهُ أَضْرَّ بِدُنْيَاهُ، فَاتَّبِرُوا مَا بَقِيَ عَلَىٰ مَا بَقِيَ»

“Mwenye kuipenda Dunia atataabika katika akhera yake, na mwenye kuipenda akhera yake, atataabika katika dunia yake, kwa hivyo chagueni cha kudumu juu ya chenye kuisha.”

Amepwekeka nayo Ahmad.¹

Vitabu vya Ibrahim عليه السلام na Musa عليه السلام.

Kisha Allah تعالیٰ Anasema:

إِنَّ هٰذَا لَفِي الصُّحُفِ الْأُولَىٰ ﴿١٨﴾ صُحُفِ إِبْرٰهِيْمَ وَمُوسَىٰ ﴿١٩﴾

“Hakika haya yamo katika Vitabu vya mwanzo. Vitabu vya Ibrahimu na Musa.”

¹ Ahmad 4:412. Hadithi hii ina udhaifu katika mlolongo wa mapokezi.

Ni kama Kauli Yake Allah تعالى،

أَمْ لَمْ يُنَبِّأْ بِمَا فِي صُحُفِ مُوسَى ﴿٣٦﴾ وَإِبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّى ﴿٣٧﴾ أَلَا تَرَىٰ وَازِرَةً وَّرَدًّا ﴿٣٨﴾
 أُخْرَىٰ ﴿٣٩﴾ وَأَنْ لَّيْسَ لِلْإِنْسَانِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ﴿٤٠﴾ وَأَنَّ سَعْيَهُ سَوْفَ يُرَىٰ ﴿٤١﴾ ثُمَّ يُجْزَاهُ الْجَزَاءَ الْأَوْفَىٰ ﴿٤٢﴾ وَأَنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ أَلْمُتَبَىٰ ﴿٤٣﴾

“Au hakuambiwa yaliyomo katika Vitabu vya Musa?. Na vya Ibrahimu aliyetimiza ahadi?. Ya kwamba hakika nafsi iliyobeba madhambi haibebi madhambi ya mwengine?. Na ya kwamba hatapata mtu ila aliyoyafanya mwenyewe?. Na kwamba vitendo vyake vitaonekana?. Kisha ndio atalipwa malipo yake kwa ukamilifu. Na kwamba kwa Mola Wako Mlezi ndio mwisho.”
 (53:36-42)

Katika *Suratu An-Najmi*, zisome aya hizi mpaka mwisho. Amesema Abu Aliya kisa cha sura hii kimo katika vitabu vya mwanzo,¹ Na Ibnu Jarir رحمه الله تعالى amesema makusudio ya Kauli Yake,

إِنَّ هَذَا

“Hakika haya...” Hurejea, katika Kauli Yake.

فَدَأْفَلَحَ مَنْ تَزَكَّىٰ ﴿١٤﴾ وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّىٰ ﴿١٥﴾ بَلْ تُؤَوتُونَ الدُّنْيَا ﴿١٦﴾
 وَالْآخِرَةَ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ﴿١٧﴾

“Hakika amekwishafanikiwa aliyejitakasa. Na akakumbuka Jina la Mola Wake Mlezi, na akasali. Lakini nyinyi mnakhiari maisha ya dunia! Na Akhera ni bora na yenye kudumu zaidi.” (87:14-17)

Kisha Amesema,

إِنَّ هَذَا

“Hakika haya...”

Maana yake: Madhumuni ya maneno haya.

¹ At-Tabari 24:376.

لَيْفَى الصُّحُفِ الْأُولَى ﴿١﴾ صُحُفِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى ﴿٢﴾

“Yamo katika Vitabu vya mwanzo. Vitabu vya Ibrahimu na Musa.”¹

Na mtazamo huu ambao amechagua ni mzuri na wenye nguvu. Na imepokewa kutoka kwa Qatada na Ibn Zaid² mfano wake. Na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Huu ni mwisho wa tafsiri ya *Suratu Sabbih* na ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha na Kwake tu kuomba, kuwezesha na kulingwa.

* * *

¹ At-Tabari 24:377.

² At-Tabari 24:376.

Tafsiri ya Suratul Ghashiyah

Sura ya 88

Iliteremshwa Makkah

Kusomwa kwa *Suratul Aala* na *Al Ghashiya* katika Sala ya Ijumaa.

Imetangulia kusemwa huko nyuma, kutoka kwa An-Nuumani bin Bashir رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alikuwa anasoma *Sabbihisma Rabbika Al A'ala* na *al-Ghashiya* katika Sala ya Idd na Sala ya Ijumaa.¹

Na amepokea Imam Ahmad kwamba Adh-Dhahak bin Qais alimuuliza An-Nuumani bin Bashir رضي الله عنه, 'ni sura gani alikuwa anasoma Mtume ﷺ katika Sala ya Ijumaa pamoja na *Suratul jumaa*?' akasema; "*Hal'ata-ka Hadithu al-Ghashiyat.*"²

Na ameyapokea hayo Abu Dawud na An-Nasai. Aidha ameipokea Muslim na Ibn Majah.³



¹ Muslim 2:598.

² Al-Muwatta 1:111.

³ Abu Daud 1:679, An-Nasai 3:112, Muslim 2:598 na Ibn Majah 1:355.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْغَاشِيَةِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَاشِيَةِ ۝ وَجُوهُ يَوْمٍ خَشِيعَةً ۝
 عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ۝ تَصَلَّى نَارًا حَامِيَةً ۝ تُسْقَى مِنْ عَيْنٍ
 ءَآيِنَةٍ ۝ لَيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ إِلَّا مِنْ ضَرِيحٍ ۝ لَا يُسْمِنُ
 وَلَا يُغْنِي مِنْ جُوعٍ ۝ وَجُوهُ يَوْمٍ نَاعِمَةٌ ۝ لِسْعِيهَا
 رَاضِيَةٌ ۝ فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ۝ لَا تَسْمَعُ فِيهَا لَغِيَةً ۝
 فِيهَا عَيْنٌ جَارِيَةٌ ۝ فِيهَا سُرُرٌ مَرْفُوعَةٌ ۝ وَأَكْوَابٌ
 مَوْضُوعَةٌ ۝ وَنَمَارِقُ مَصْفُوفَةٌ ۝ وَزَلَّالٌ مَبْنُوثَةٌ ۝
 أَفَلَا يَنْظُرُونَ إِلَى الْإِبِلِ كَيْفَ خُلِقَتْ ۝ وَإِلَى السَّمَاءِ
 كَيْفَ رُفِعَتْ ۝ وَإِلَى الْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ ۝ وَإِلَى
 الْأَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ ۝ فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ ۝
 لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ۝ إِلَّا مَنْ تَوَلَّى وَكَفَرَ ۝
 فَيُعَذِّبُهُ اللَّهُ الْعَذَابَ الْأَكْبَرَ ۝ إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ۝ ثُمَّ
 إِنَّ عَلَيْنَا جِسْمَهُمْ ۝

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَاشِيَةِ ۝
 وَجُوهُ يَوْمٍ خَشِيعَةً ۝ عَامِلَةٌ
 نَّاصِبَةٌ ۝ تَصَلَّى نَارًا حَامِيَةً ۝
 تُسْقَى مِنْ عَيْنٍ ءَآيِنَةٍ ۝ لَيْسَ لَهُمْ
 طَعَامٌ إِلَّا مِنْ ضَرِيحٍ ۝ لَا يُسْمِنُ
 وَلَا يُغْنِي مِنْ جُوعٍ ۝

1. Je! Imekufikia khabari ya msiba wa kufudikiza?

2. Siku hiyo nyuso zitainama.

3. Zikifanya kazi, nazo taabani.

4. Ziingie katika Moto unaowaka.

5. Zikinyweshwa kutoka chemchemi inayochemka.

6. Hawatakuwa na chakula isipokuwa kichungu chenye miba.

7. Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa.

Qiyama na Hali ya Watu wa Motoni Itakavyokuwa

Al-Ghashiya ni katika majina ya siku ya Qiyama, amesema hayo Ibnu Abbas na Qatada na Ibnu Zaid رضي الله عنهم.¹ Kwa sababu hicho Qiyama kitawafunika watu na kitaenea.

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ خَاشِعَةٌ ﴿١٠﴾

“Siku hiyo nyuso zitainama...” Maana yake: Zitakuwa dhalili, ameyasema hayo Qatadah.² Na amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما zitadhalilika na hayatazifaa matendo yake.

عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿١١﴾

“Zikifanya kazi, nazo taabani.” Maana yake: Zimetenda matendo mengi na zimetaabika ndani yake na zitaingia motoni siku ya Qiyama, moto ulio mkali sana. Amepokea Hafidh Abu Bakr al-Barqan رحمه الله تعالى kutoka kwa Abuu Imran Aljawn amesema; alipita Umar bin Khattab رضي الله عنه katika nyumba ya Ibada ya Mwana wachuoni wa kiyahudi. Amesema; akamuita, ‘Eee!! Mtaalamu!’ Akachungulia, akasema; akawa Umar رضي الله عنه anamtazama analia, akaulizwa. “Eee!! Amirul Muuminina ni jambo gani linalokuliza kwa huyu!?” Akasema, “nimekumbuka Kauli ya Allah تعالى katika Kitabu Chake;

عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿١١﴾ تَصَلَّىٰ نَارًا حَامِيَةً ﴿١٢﴾

“Zikifanya kazi, nazo taabani. Ziingie katika Moto unao waka.”

Hilo ndilo liloniliza.³ Na amesema Bukhari, amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما,

عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿١١﴾

“Zikifanya kazi, nazo taabani.” Manaswara.⁴ Na imepokewa kutoka kwa Sudi, zitatumika Duniani kwa kufanya maasia, zitataabika motoni kwa adhabu na kuangamia. Amesema Ibnu Abbas na Hassan na Qatada رضي الله عنهم,

تَصَلَّىٰ نَارًا حَامِيَةً ﴿١٢﴾

“Ziingie katika Moto unao waka.” Mkali wenye joto kali.

¹ At-Tabari 24:381.

² At-Tabari 24:382

³ Abdur-Razzaq 2:299, na Al-Hakim 2:522. Isnadi yake imekatika kwani Abu Imran Al-Juwayni hakudiriki zama za Umar.

⁴ Fat’hul Al-Bari 8:570.

تُسْقَىٰ مِنْ عَيْنٍ ءَانِيَةٍ ﴿١٠﴾

“Zikinyweshwa kutoka chemchem inayochemka.”

Maana yake: Limefikia mwisho joto lake na kuchemka kwake, ameyasema hayo Ibnu Abbas na Mujahid, Hassan na Suddi رضي الله عنهم.¹ Na Kauli Yake Allah تعالى:

لَيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ إِلَّا مِنْ ضَرِيعٍ ﴿١١﴾

“Hawatakuwa na chakula isipokuwa kichungu chenye miba.”

Ali bin Abi Twalha amesema, akipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa hiyo miti ni iliyo ndani ya moto.² Na amesema Ibnu Abbas na Mujahid na Ikrimah na Abuu Al-Jawzaa na Qatadah رضي الله عنهم kuwa Maqurayshi wanauita wakati wa vuli, ‘Ash-Shabraq’, na wakati wa kaskazi “Al-dharii”. Amesema Ikrimah; na huo ni mti wenye miba umeambatana na ardhi.³ Na amesema Bukhari; amesema Mujahid, “al-Dharii” ni mmea unaoitwa ‘Asshibriq’ wanauita watu wa Hijjaz ‘al-Dharii’ pindi unapokauka na ni mmea wenye sumu.⁴

Na amesema Maamar kutoka kwa Qatadah,

لَيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ إِلَّا مِنْ ضَرِيعٍ ﴿١٢﴾

“Hawatakuwa na chakula isipokuwa kichungu chenye miba.”

Huo ni ‘Asshibriq’ utakapokauka huitwa “al-Dharii”.⁵ Na amesema Saiid kutoka kwa Qatadah,

لَيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ إِلَّا مِنْ ضَرِيعٍ ﴿١٣﴾

“Hawatakuwa na chakula isipokuwa kichungu chenye miba.”

Katika chakula kibaya mno na kiovu chake na kichafu kupita kiasi.⁶ Na Kauli Yake Allah تعالى:

¹ At-Tabari 24:383.

² At-Tabari 24:385.

³ At-Tabari 24:384.

⁴ Fat’hul Al-Bari 8:570.

⁵ At-Tabari 24:384.

⁶ At-Tabari 24:384.

لَا يُسْمِنُ وَلَا يُغْنِي مِنْ جُوعٍ ﴿٧﴾

“Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa.”

Anakusudia hakina faida wala hakiondoshi lilokusudiwa.

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاعِمَةٌ ﴿٨﴾ لِّسَعْيِهَا رَاضِيَةٌ ﴿٩﴾ فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ﴿١٠﴾ لَا تَسْمَعُ فِيهَا لَنِيَّةً ﴿١١﴾
فِيهَا عَيْنٌ جَارِيَةٌ ﴿١٢﴾ فِيهَا سُرُرٌ مَّرْفُوعَةٌ ﴿١٣﴾ وَأَكْوَابٌ مَوْضُوعَةٌ ﴿١٤﴾ وَنَمَارِقُ ﴿١٥﴾
مَصْفُوفَةٌ ﴿١٦﴾ وَزَرَابِيُّ مَبْثُوثَةٌ ﴿١٧﴾

8. Siku hiyo nyuso zao zitakuwa kunjufu.

9. Zitakuwa radhi kwa juhudi yao.

10. Katika Bustani ya juu.

11. Hawatasikia humo upuuzi.

12. Humo imo chemchemi inayomiminika.

13. Humo vimo viti vilivyo nyanyuliwa.

14. Na Bilauri zilizopangwa.

15. Na matakia safusafu.

16. Na mazulia yaliyota ndikwa.

Hali ya Watu wa Peponi Siku ya Qiyama.

Alipotaja Allah تعالی hali ya watu waovu amefuatisha kwa kutaja hali ya watu wema kwa kusema,

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ

“Siku hiyo nyuso nyengine...” Maana yake: Siku ya Qiyama,

نَّاعِمَةٌ ﴿٨﴾

“Zitakuwa kunjufu.” Maana yake: Zitaonekana neema katika nyuso hizo, na hakika hapana jambo jingine, nyuso hizo zimepata neema hiyo kwa sababu ya matendo yake. Na amesema Sufyan,

لَسَعِيهَا رَاضِيَةٌ ﴿١٥﴾

“Zitakuwa radhi kwa juhudi yao.”

Zimeyaridhia matendo yake. Na Kauli Yake Allah تعالى,

فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ﴿١٦﴾

“Katika Bustani ya juu.”

Maana yake: Nzuri zilizo na hadhi ya juu katika vyumba hali ya kuwa na amani.

لَا تَسْمَعُ فِيهَا لَٰغِيَةً ﴿١٧﴾

“Hawatasikia humo upuuzi.”

Maana yake: Hazitasikia humo peponi maneno ya kiupuuzi. Kama Alivyosema Allah تعالى,

لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا إِلَّا سَلَامًا ۗ

“Humo hawatasikia upuuzi,¹ ila Salama tu...” (19:62)

Na Kauli Yake Allah تعالى;

لَا لَغْوٌ فِيهَا وَلَا تَأْتِيهِمُ ۙ

“...Hakutakuwa na maneno ya upuuzi wala dhambi.” (52:23)

Allah تعالى Amesema,

لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا تَأْتِيهِمُ ۙ ﴿١٨﴾ إِلَّا قِيلًا سَلَامًا سَلَامًا ﴿١٩﴾

“Humo hawatasikia porojo wala maneno ya dhambi, isipokuwa maneno ya Salama, Salama.” (56:25-26)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

فِيهَا عَيْنٌ جَارِيَةٌ ﴿٢٠﴾

“Humo imo chemchem inayomiminika.”

Maana yake: Zenye kwenda. Kwa maana ndani yake kuna chemchem nyingi zenye kupita. Amepokea Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Abi Hurairah رضي الله عنه amesema; amesema Mtume ﷺ,

«أَنْهَارُ الْجَنَّةِ نَفَّجْرٌ مِنْ تَحْتِ نِلاَلٍ - أَوْ مِنْ تَحْتِ جِبَالٍ - الْمِسْكِ»

“Mito ya peponi inapasuka kutoka katika vichuguu au kutoka chini ya majabali ya Miski.”¹

فِيهَا سُرُرٌ مَرْفُوعَةٌ ﴿٣٧﴾

“Humo vimo viti vilivyonyanyuliwa.”

Maana yake: Viko juu vimesimama vyenye magodoro mengi vimenyanyuka kimo chake juu yao. Wapo wanawake wa peponi Hurul’Ain. Wamesema akitaka mpenzi wa Allah تعالى kukaa juu ya viti hivyo, vitashuka kwa ajili yake.

وَأَكْوَابٌ مَوْضُوعَةٌ ﴿٣٨﴾

“Na bilauri zilizo pangwa.”

Anakusudia vyombo vya kunywa vimetayarishwa kwa mwenye kuvitaka.

وَمَنَارِقُ مَصْفُوفَةٌ ﴿٣٩﴾

“Na matakia safu safu.”

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما “Nama-riqu” ni mito.² Na kama hivyo amesema Ikrimah na Qatada na Adh-Dhahak na Suddi na Ath-Thauri na wengine. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَزَرَالِي مَبْنُوتَةٌ ﴿٤٠﴾

“Na mazulia yaliyotandikwa.”

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما “Alzarabiya” ni mabusati na kama hivyo amesema Adh-Dhahaak na wengine na maana ya Mabthutha yaliyotandazwa hapa na pale kwa mwenye kutaka kukaa juu yake.

أَفَلَا يَنْظُرُونَ إِلَى الْإِبِلِ كَيْفَ خُلِقَتْ ﴿٤١﴾ وَإِلَى السَّمَاءِ كَيْفَ رُفِعَتْ ﴿٤٢﴾ وَإِلَى

الْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ ﴿٤٣﴾ وَإِلَى الْأَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ ﴿٤٤﴾ فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ

¹ Ibn Hibban no. 2622. Angalia Mawarida Adh-dhmaan.

² At-Tabari 24:387.

لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيْطِرٍ ﴿١٧﴾ إِلَّا مَنْ تَوَلَّىٰ وَكُفِرَ ﴿١٨﴾ فَيُعَذِّبُهُ اللَّهُ الْعَذَابَ الْأَكْبَرَ ﴿١٩﴾
 إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ﴿٢٠﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُمْ ﴿٢١﴾

17. Je! Hawamtazami ngamia jinsi alivyoumbwa?
18. Na mbingu jinsi ilivyoinuliwa?
19. Na milima jinsi ilivyokitwa imara?
20. Na ardhi jinsi ilivyotandazwa?
21. Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji.
22. Wewe si mwenye kuwatawalia.
23. Lakini anaye rudi nyuma na kukataa,
24. Basi Mwenyezi Mungu Atamuadhibu kwa adhabu iliyo kubwa kabisa!
25. Hakika ni Kwetu Sisi ndio marejeo yao.
26. Kisha hakika ni juu Yetu Sisi hisabu yao!

Mahimizo Juu ya Kuchunguza Kuumbwa kwa Ngamia, Mbingu, Majabali na Ardhi.

Anasema Allah تعالى Akiwaamrisha waja Wake kutazama kwa mazingatio katika uumbaji wa viumbe Vyake vyenye kufahamisha juu ya uwezo Wake na utukufu Wake.

أَفَلَا يَنْظُرُونَ إِلَىٰ الْإِبْرَٰئِيلَ كَيْفَ خُلِقَتْ ﴿٧٦﴾

“Je! Hawamtazami ngamia jinsi alivyoumbwa?”

Kwani hao ngamia ni umbile la ajabu, na muundo wake unastaajibisha zaidi kwani hao ngamia wapo katika upeo wa nguvu na uimara. Na ngamia hao pamoja na hayo wanalainika kwa kuchukua mzigo mzito na wananyenyekea kwa kiongozi aliye mnyonge. Na wanaliwa na panapatwa manufaa kwa manyoya yake na yananywewa maziwa yake. Na yamesemwa yote hayo, kwa kuzingatia kuwa aghlabu Waarabu Ngamia alikuwa ni sehemu kubwa ya wanyama wao. Na alikuwa Kadhi Shurayhi akisema, “tutoke ili tuwachunguze ngamia namna walivyoumbwa; na mbingu namna zilivyonyanyuliwa.” Maana:

Alivyozinyanyua Allah تعالى Mwenye Kushinda na Utukufu kutoka ardhini humo unyanyuaji mkubwa sana. Kama Alivyosema Allah تعالى،

أَفَلَمْ يَنْظُرُوا إِلَى السَّمَاءِ فَوْقَهُمْ كَيْفَ بَنَيْنَاهَا وَزَيَّنَّاهَا وَمَا هِيَ مِنْ فُرُوجٍ ﴿٦﴾

“Je! Hawaangalii mbingu zilizo juu yao! Vipi Tulivyozijenga, na Tukazipamba. Wala hazina nyufa.”(50:6)

Allah تعالى Akasema،

وَأِلَى الْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ ﴿٧﴾

“Na milima jinsi ilivyokitwa imara?”

Maana yake: Yamefanywa ni yenye kusimamishwa. Hakika hayo majabali yamejikita na yamedhibiti kwa ajili ardhi isije ikayumba pamoja na watu, na Amejaalia ndani yake miongoni mwa manufaa mbalimbali na madini tofauti،

وَأِلَى الْأَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ ﴿٨﴾

“Na ardhi jinsi ilivyotandazwa?”

Maana yake: Namna ilivyotandikwa ikanyooshwa na ikafanywa ni tandiko. Amezinduliwa bedui ili achukue dalili kutokana na alivyoviona miongoni mwa ngamia wake anayempanda, na mbingu ambazo ziko juu ya kichwa chake na majabali ambayo yako mbali yake na ardhi ambayo ipo chini yake. Achukue dalili juu ya uwezo wa Muumba wa vitu hivyo na Mtengenezaji Wake kwamba huyo ni Bwana Mkubwa Mwenye Kumiliki na Kufanya Atakavyo na kwamba Yeye ni Mola ambaye Anastahiki Kuabudiwa Yeye tu.

Kisa cha Dhwimaam Bin Tha'alabah.

Kama hivi aliapa Dhwimaam katika kumuuliza kwake Mtume ﷺ kama isemavyo Hadithi aliyopokea Imaam Ahmad kutoka kwa Thabit kutoka kwa Anas amesema: 'Tulikuwa tumezuiliwa kumuuliza Mtume ﷺ kuhusu kitu chochote.' Na ilikuwa tukifurahishwa sana pindi anapokuja bedui kutoka Jangwani mwenye weledi na kumuuliza Mtume ﷺ na hali sisi tunasikia. Akaja mtu mmoja katika watu wa viungani akasema, 'Ewe! Muhamad kwa hakika ametujia mjumbe wako akidai kwamba wewe unadai kwamba Allah تعالى Amekutuma.' Akasema:

«صَدَقَ»

"Amesema kweli," Akauliza, "Ni nani aliyeumba Mbingu?" Akamjibu, "Mwenyezi Mungu." Akauliza, "Ni nani aliyeumba ardhi?" Akamjibu "Mwenyezi Mungu." Akauliza tena, "Ni nani aliyesimamisha haya majabali na akayafanya katika hayo majabali yale aliyoyafanya?" Akamjibu, "Naapa kwa Yule ambaye Ameziumba mbingu na ardhi na Akayasimamisha majabali." Akauliza, "Hivi ni Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekupeleka?" Akamjibu

«نَعَمْ»

"Ndiyo." Akauliza, "Na amedai Mjumbe wako kwamba ni wajibu juu yetu Sala tano katika mchana wetu na usiku wetu?" Akamjibu;

«صَدَقَ»

"Amesema kweli." Akasema, "Naapa kwa Yule Aliyekutuma. Hivi Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuamrisha mambo haya?" Akamjibu,

«نَعَمْ»

"Ndiyo." Akauliza, "Na amedai Mjumbe Wako kwamba ni wajibu juu yetu Zaka ya mali yetu?" Akamjibu;

«صَدَقَ»

"Amesema kweli." Akasema: "Naapa kwa Yule Aliyekupeleka! Je Mwenyezi Mungu Amekuamrisha mambo haya?" Akamjibu, 'Ndiyo.'" Akasema, "Amedai mjumbe wako kwamba ni wajibu wetu Funga za Mwezi wa Ramadhani katika mwaka wetu?" Akamjibu,

«نَعَمْ»

"Ndiyo amesema kweli." Akasema, "Naapa kwa Yule Aliyekupeleka! Hivi Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuamrisha mambo haya?" Akamjibu, 'Ndiyo.'" Akasema, "Na amedai mjumbe wako kwamba pana juu yetu kuikusudia Kaaba kwa mwenye kuweza njia ya kuiendea?" Akasema;

«صَدَقَ»

"Amesema kweli."

Akasema; "Naapa kwa Yule Aliyekutuma kwa ukweli! Sitaongeza juu ya hayo kitu chochote na sitapunguza katika mambo hayo kitu chochote." Akasema Mtume ﷺ,

«إِنْ صَدَقَ لَيَدْخُلَنَّ الْجَنَّةَ»

*"Iwapo atakuwa mkweli kwa hakika ataingia peponi."*¹

Ameipokea Bukhari, Muslim, Abu Dawuud, At-Tirmidh, An-Nasai na Ibnu Majah.²

Kazi ya Mtume ni Kufikisha Ujumbe Tu.

Na Kauli Yake Allah تعالى،

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ ﴿١٠﴾ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ﴿١١﴾

"Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawalia."

Maana yake: 'Onya Eeeh!! Muhammad kwa yale uliyopelekwa kwayo kwao.'

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلَاغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿١٢﴾

"Juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu Yetu ni hisabu." (13:40)

Na kwa sababu hiyo Amesema;

لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ﴿١٣﴾

"Wewe si mwenye kuwatawalia."

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما na Mujahid na wasiokuwa hao; hukuwa juu yao shupavu.³ Maana: hukuwa unaumba imani katika nyoyo zao. Na amesema Ibn Zaid, hukuwa yule ambaye unawalazimisha kuamini.⁴ Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Jabir رضي الله عنه amesema Mtume ﷺ،

«أَمِرْتُ أَنْ أَقَاتِلَ النَّاسَ حَتَّى يَقُولُوا: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، فَإِذَا قَالُوا عَصَمُوا مِنِّي دِمَاءَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ إِلَّا بِحَقِّهَا، وَحِسَابُهُمْ عَلَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

¹ Ahmad 3:143.

² Al-Bukhari no.63, Muslim 1:41, Abu Daud no.486, Al-Tirmidhi no.619, An-Nasai katika Al-kubra no.2401, 2402 Ibn Majah no.1402.

³ At-Tabari 24:390.

⁴ At-Tabari 24:390.

"Nimeamrisha kupigana na watu mpaka waseme hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, watakaposema maneno hayo watazihifadhi kwangu damu zao na mali zao; isipokuwa kwa haki yao na hesabu yao ni juu ya Mwenyezi Mungu Mwenye Kushinda Mwenye Utukufu."

Kisha akasoma,

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ ﴿١٠﴾ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ﴿١١﴾

"Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawalia."¹

Na kama hivyo amepokea Muslim katika mlango wa Iman na Tirmidhi na An-Nasai katika mlango wa tafsiri katika sunna zao.² Na hadithi hii imethibitishwa katika sahihi mbili.³

Makemeo kwa Mwenye Kuipa Mgongo Haki.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِلَّا مَنْ تَوَلَّىٰ وَكَفَرَ ﴿١٢﴾

"Lakini anayerudi nyuma na kukataa."

Maana yake: Amekataa kufanya kazi kwa viungo vyake, na akakufuru haki kwa moyo wake na ulimi wake. Aya hii ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

فَلَا صَدَقَ وَلَا صَلَّىٰ ﴿١٣﴾ وَلٰكِنْ كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿١٤﴾

"Kwa sababu hakusadiki, wala hakusali. Bali alikanusha, na akageuka." (75:31-32)

Na kwa sababu hiyo Amesema,

فَيُعَذِّبُهُ اللَّهُ الْعَذَابَ الْأَكْبَرَ ﴿١٥﴾

"Basi Mwenyezi Mungu Atamuadhibu kwa adhabu iliyo kubwa kabisa!"

¹ Ahmad 3:300.

² Muslim 1:53, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:265, na An-Nasai katika Al-Kubra 6:514.

³ Fat'hul Al-Bari 1:95, kutoka kwa Ibn Umar, na Muslim 1:52.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ﴿٨٨﴾

“Hakika ni Kwetu Sisi ndio marejeo yao.”

Maana yake: Marejeo yao na mageuko yao.

ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُمْ ﴿٨٩﴾

“Kisha hakika ni juu Yetu Sisi hisabu yao!”

Maana yake: Sisi Tutawahesabu juu ya matendo yao na Tutawalipa kutokana na matendo hayo. Yakiwa mazuri, malipo nayo yatakuwa mazuri, na yakiwa mabaya malipo nayo yatakuwa mabaya.

Huu ni mwisho wa tafsiri ya *Suratu Ghashiya* na sifa zote njema na shukrani ni Zake Allah تعالى.

* * *

Tafsiri ya Suratul Fajr

Sura ya 89

Iliteremshwa Makkah

Kusomwa *Suratul Fajr* katika Sala.

Amepokea An-Nasai kutoka kwa Jabir رضي الله عنه amesema: Muadh رضي الله عنه alisalisha Sala, akaja mtu akasali nyuma yake. Muadh رضي الله عنه akairefusha Sala ile na yule mtu akaondoka akasali peke yake. Ilipomfikia Muadh habari ya mtu yule. Muadh رضي الله عنه akasema, 'Mtu huyo ni mnafiki.' Likatajwa hilo kwa Mtume ﷺ. Akamuuliza yule kijana. Akasema, 'Eeh!! Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, nilikuja nisali jamaa, Muadhi رضي الله عنه akairefusha juu yangu Sala, nikaondoka nikasali upande mwengine wa msikiti nikaenda kumlisha majani Ngamia wangu." Akasema Mtume ﷺ,

«أَفَتَأْتُونَ يَا مُعَاذُ؟ أَيْنَ أَنْتَ مِنْ سَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَىٰ ﴿١﴾ وَأَسْتَمِينِ وَحُصْنَهَا ﴿٢﴾ وَالنَّجْرِ ﴿٣﴾
«وَأَتَيْلِ إِنَّا يَتَسَنَّى ﴿٤﴾»

"Je ni mwenye fitina wewe Muadh? (Kwa maana unataka kuwafitinisha watu na Mungu wao!) uko wapi wewe na "Sabihisma Rabbika al 'Iaa," "Wash-Shamsi wadhuhaaha," "Walfajri," "Wallayl idhaa yaghshaa."¹

* * *

¹ An-Nasai katika Al-Kubra 6:55.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْفَجْرِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالْفَجْرِ ۝ وَلَيَالٍ عَشْرٍ ۝ وَالشَّفْعِ وَالْوَتْرِ ۝
وَاللَّيْلِ إِذَا يَسْرِ ۝ هَلْ فِي ذَلِكَ قَسَمٌ لِّذِي حِجْرِ ۝ أَلَمْ
تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ۝ إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ۝ الَّتِي لَمْ
يَخْلُقْ مِثْلَهَا فِي الْبَلَدِ ۝ وَتَمُودَ ۝ الَّذِينَ جَاءُوا الصَّخَرَ
بِالْوَادِ ۝ وَفِرْعَوْنَ ذِي الْأَوْتَادِ ۝ الَّذِينَ طَعَفُوا فِي
الْبَلَدِ ۝ فَأَكْتَرُوا فِيهَا الْفَسَادَ ۝ فَصَبَّ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ
سَوْطَ عَذَابٍ ۝ إِنَّ رَبَّكَ لَبِالْمِرْصَادِ ۝ فَأَمَّا
الْإِنْسَانُ إِذَا مَا ابْتَلَاهُ رَبُّهُ فَأَكْرَمَهُ وَنَعَّمَهُ فَيَقُولُ رَبِّي
أَكْرَمَنِي ۝ وَأَمَّا إِذَا مَا ابْتَلَاهُ فَقَدَرَ عَلَيْهِ رِزْقَهُ فَيَقُولُ
رَبِّي أَهْنَنِي ۝ كَلَّا بَلْ لَا تَكْرُمُونَ الْيَتِيمَ ۝ وَلَا
تَحْتَضِرُونَ عَلَىٰ طَعَامِ الْمَسْكِينِ ۝ وَتَأْكُلُونَ
الَّذَاتِ أَكْلًا لَّمًّا ۝ وَتُحِبُّونَ أَمْوَالَ حُبًّا جَمًّا ۝

وَالْفَجْرِ ۝ وَلَيَالٍ عَشْرٍ ۝ وَالشَّفْعِ وَالْوَتْرِ ۝
وَاللَّيْلِ إِذَا يَسْرِ ۝ هَلْ فِي ذَلِكَ قَسَمٌ لِّذِي حِجْرِ ۝
أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ۝ إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ۝
الَّتِي لَمْ يَخْلُقْ مِثْلَهَا فِي الْبَلَدِ ۝ وَتَمُودَ ۝ الَّذِينَ
جَاءُوا الصَّخَرَ بِالْوَادِ ۝ وَفِرْعَوْنَ ذِي الْأَوْتَادِ ۝
الَّذِينَ طَعَفُوا فِي الْبَلَدِ ۝ فَأَكْتَرُوا فِيهَا
الْفَسَادَ ۝ فَصَبَّ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ سَوْطَ عَذَابٍ ۝
إِنَّ رَبَّكَ لَبِالْمِرْصَادِ ۝

1. Naapa kwa Alfajiri.

2. Na kwa masiku kumi.

3. Na kwa viwili viwili na kimoja kimoja.

4. Na kwa usiku unapopita.

5. Je! Hapana katika haya Dalili zilizowazi kwa mwenye akili?.

6. Kwani hukuona jinsi Mola Wako Mlezi Alivyowafanya kina A'di?.

7. Wa Iram, wenye majumba marefu?.

8. *Ambao haukuumbwa mfano wake katika nchi?*
9. *Na Thamudi waliochonga majabali huko bondeni?*
10. *Na Firauni mwenye vigingi?*
11. *Ambao walifanya jeuri katika nchi?*
12. *Wakakithirisha humo ufidadi?*
13. *Basi Mola Wako Mlezi Aliwapiga mjeledi wa adhabu.*
14. *Hakika Mola Wako Mlezi Yupo kwenye mavizio Anawavizia.*

Tafsiri ya Sura ya *Al-Fajr* na Yaliyo Baada Yake.

Ama *Al-Fajr* inajulikana nayo ni Asubuhi, ameyesema hayo Ali, Ibn Abbas, Ikrimah, Mujahid na Suddi رضي الله عنهم.¹

Na imepokewa kutoka kwa Masrouq na Muhamad bin Kaab, Muradi wa '*Al-Fajr*' ni '*Al-Fajr*' ya siku ya kuchinja tu, na hitimisho la siku kumi.²

Na siku kumi hizo ni zile za mwezi *Dhulhijja* (mfungo tatu). Kama alivyosema Ibn Abbas, Ibn Zubair na Mujahid na wengine رضي الله عنهم, katika wafasiri waliotangulia na waliokuja nyuma.³

Na imethibiti katika sahihi Bukhari kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kwa njia ya '*marfuu*', yaani kuiegemeza Hadithi moja kwa moja kwa Mtume ﷺ,

«مَا مِنْ أَيَّامٍ الْعَمَلُ الصَّالِحُ أَحَبُّ إِلَى اللَّهِ فِيهِنَّ مِنْ هَذِهِ الْأَيَّامِ»

"Hapana katika siku kutenda matendo mema kunapendeza sana kwa Mwenyezi Mungu kuliko kutenda katika siku hizi."

Anakusudia siku kumi za mwezi wa *Dhulhijja* (mfungo tatu). Wakauliza, "Wala kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu?" Mtume ﷺ akasema,

¹ At-Tabari 24:395, na Al-Baghawi 4:481.

² Al-Qurtubi 20:39.

³ At-Tabari 24:396.

«وَلَا الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، إِلَّا رَجُلًا خَرَجَ بِتَمْسِهِ وَمَالِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْجِعْ مِنْ ذَلِكَ
بِشَيْءٍ»

“Wala jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, isipokuwa mtu aliyetoka yeye mwenyewe na mali yake, kisha asirejee na chochote.”¹

Imepokewa Hadithi na Imamu Ahmad kutoka kwa Jabir kutoka kwa Mtume amesema: “Hakika siku kumi ni za *Adh’haa*. Na “*Witri*” ni siku ya Arafa. Na “*Shaf’u*” ni siku ya kuchinja.” Aidha Hadithi hii imepokewa na Imamu Annasai. Na Isnadi ya Hadithi hii wapokezi wake hawatiliwi shaka sana. Kwangu mimi ni kwamba matini ya Hadithi hii ina walakini kidogo. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَالشَّفَعِ وَالْوَتْرِ ﴿٢٠﴾

“Na kwa viwili viwili na kimoja kimoja.”

Imetangulia katika Hadithi kwamba “*Al-Watr*” Ni siku ya Arafa kwa kuwa ni siku ya tisa na kwamba “*Ash-Shaf’i*” ni siku za kuchinja kwa kuwa kwake ni siku ya kumi.² Ameyasema hayo Ibn Abbas, Ikrimah na Adh-Dhahaak vilevile.³ Na katika tafsiri ya matamko mawili hayo pana kauli nyingi sana.

Tafsiri ya *Allayl* (Usiku).

Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَاللَّيْلِ إِذَا يَسْرَ ﴿٢١﴾

“Na kwa usiku unapopita.” Amesema Al-’Awfi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, maana utakapokwenda⁴ na amesema Abdallah bin Zubair رضي الله عنه,

وَاللَّيْلِ إِذَا يَسْرَ ﴿٢١﴾

“Na kwa usiku unapopita.” Kuwa, mpaka utapoondoa baadhi yake baadhi nyingine.⁵ Na amesema Mujahid, Abuu Al-’Aaliya, Qatada, na Malik kutoka kwa Zaid bin Aslam na Ibn Zaid,

¹ *Fat’hul Al-Bari* 2:530 na Ahmad 2/224.

² Ahmad 3/327.

³ At-Tabari 24:397,398.

⁴ At-Tabari 24:401.

⁵ At-Tabari 24:401.

وَأَلَيْلٍ إِذَا يَسَّرٌ ﴿١٠﴾

“Na kwa usiku unapopita.” Utakapokwenda.¹

Na Kauli Yake Allah تعالى،

هَلْ فِي ذَلِكَ قَسَمٌ لِّذِي حِجْرٍ ﴿١١﴾

“Je! Hapana katika haya kiapo kwa mwenye akili?”

Maana yake: Kwa mwenye akili? Na dini? Imeitwa akili kwa tamko la “Hijri” kwa sababu inamzuia mwanadamu kufanya mambo yasiyofanana naye katika matendo na maneno. Na katika maana ya *Hijr* ya al-Kaaba,² kwa sababu inamzuia mwenye kuizunguka na kuambatana na ukuta wa upande wa Sham. Na katika matumizi yake ni *Hijri-Al Yamamah* na husemwa; “*Hajara Alhakim Alaa fulani*” kwa maana, mtawala amemzuia fulani, pindi anapotoa amri ya kutotumia mali yake.

وَيَقُولُونَ حِجْرًا مَّحْجُورًا ﴿١٢﴾

“Na watasema (siku hiyo) Mungu Atuepushie mbali adhabu hii iliyotukabili.” (25:22)³

Yote haya ni ya namna moja na maana zenye kukaribiana. Na kiapo hiki ni cha nyakati za ibada, miongoni mwa Hijja na Sala nyingine ambazo zinazomkurubisha mja kwa Allah تعالى. Wanajikurubisha Kwake waja Wake wachamungu wenye kumtii, wanaomuogopa, wanyenyekavu Kwake na wenye kudhalilika kwa Dhati Yake Tukufu.

Kutajwa Kuangamizwa kwa Aadi.

Alipowataja hawa na kuabudu kwao na kutii kwao amesema baada ya hayo,

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿١٣﴾

“Kwani hukuona jinsi Mola Wako Mlezi Alivyo wafanya kina A’di?”

Na hawa walikuwa ni wenye kuasi wenye kushupaa, wenye kutoka katika utii wa Allah تعالى wenye kuwakadhibisha Mitume Wake, wenye kuvipinga vitabu

¹ At-Tabari 24:401.

² Eneo lililo upande wa kaskazini mwa Ka’bah.

³ Maana yake, ameacha kabisa.

Vyake. Ametaja Allah تعالى namna Alivyowaangamiza na Akawateketeza Akawafanya ni simulizi na mazingatio kwa watu wengine. Amesema;

إِرْمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٧﴾ أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٦﴾

**“Kwani hukuona jinsi Mola Wako Mlezi Alivyowafanya kina A’di?
Wa Iram, wenye majumba marefu?”**

Na hawa ni Aadi wa mwanzo, ambao ni watoto wa Aad Bin Iram Bin Busmi Ausi bin Sam bin Nuh amesema hayo Ibn Is-haqa.¹ Na hao ndio wale ambao Allah تعالى Alimpeleka kwao Mjumbe Wake Huud عليه السلام wakamkadhibisha na wakampinga, akamuokoa yeye Allah تعالى mbele yao na wale waliomuamini pamoja naye, katika wao. Na Akawaangamiza kwa upepo wenye kelele ulio na nguvu.

سَخَّرَهَا عَلَيْهِمْ سَبْعَ لَيَالٍ وَثَمَنِيَةَ أَيَّامٍ حُسُومًا فَتَرَى الْقَوْمَ فِيهَا صَرْعَى كَأَنَّهُمْ أُعِجَازُ
نَخْلٍ خَاوِيَةٍ ﴿٦﴾ فَهَلْ تَرَى لَهُم مِّنْ بَاقِيَةٍ ﴿٧﴾

**“...Aliowapelekea siku saba, na siku nane, mfululizo bila ya kusita.
Utaona watu wamepinduka kama kwamba ni magogo ya mitende
yaliowazi ndani. Basi je! Unamuona mmoja wao aliye baki?” (69:7-8)**

Allah تعالى Amekitaja kisa chao katika Qur’an sehemu nyingi sana, ili waumini wapate kuzingatia kutokana na kisa chao. Na Kauli Yake Allah تعالى,

إِرْمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٧﴾

“Wa Iram, wenye majumba marefu?”

Maneno haya yameunganishwa na maneno yaliyotangulia, kwa madhumuni ya kuongeza kuwatolea taarifa zaidi. Kauli Yake Allah تعالى,

ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٧﴾

“Wenye majumba marefu?”

¹ At-Tabari 24:404.

Kwa sababu wao walikuwa wanaishi katika nyumba za nyasi, ambazo hunyanyuliwa kwa nguzo zenye nguvu na kwa hakika walikuwa ni watu wenye nguvu sana kwa maumbile katika zama zao na wana nguvu sana katika makamato. Na kwa sababu hiyo aliwakumbusha Hud عليه السلام neema hiyo. Na waitumie neema hiyo katika kumtii Bwana wao, Ambaye Amewaumba wao. Amesema;

وَأذْكُرُوا إِذْ جَعَلْنَا خُلَفَاءَ مِنْ بَعْدِ قَوْمِ نُوحٍ وَزَادْنَاكُمْ فِي الْخَلْقِ بَصِطَةً ۖ فَادْكُرُوا
ءَالَآءَ اللَّهِ لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُونَ ﴿٦٩﴾

“Na kumbukeni Alivyokufanyeni mshike pahala pa kaumu ya Nuhu, na Akakuzidisheni katika umbo. Basi zikumbukeni neema za Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa.” (7:69)

Allah تعالى Amesema tena,

فَأَمَّا عَادٌ فَاسْتَكْبَرُوا فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَقَالُوا مَنْ أَشَدُّ مِنَّا قُوَّةً أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ
الَّذِي خَلَقَهُمْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُمْ قُوَّةً ۖ

“Ama kina A’di walijivuna katika nchi bila ya haki, na wakasema: Nani aliye kuwa na nguvu kushinda sisi? Kwani wao hawakuona kwamba Mwenyezi Mungu Aliyewaumba ni Mwenye Nguvu Kushinda wao?” (41:15)

Na Amesema Allah تعالى,

الَّتِي لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِي الْبَلَدِ ﴿٨٩﴾

“Ambao haukuumbwa mfano wake katika nchi?”

Na amesema hamna kabila ambalo liloumbwa mfano wao katika miji yao, kutokana na nguvu zao na ukakamavu wao na ukubwa wa maumbile yao. Amesema Mujahid “Iram” ni Umma wa zamani anakusudia ‘Ad; Amesema Qatadah bin Di’ama na As-Suddi; Hakika “Iram” ni nyumba ya mamlaka ya ‘Ad’ na hii ni kauli nzuri, bora na yenye nguvu.

Na Kauli Yake Allah تعالى,

الَّتِي لَمْ تُخْلَقْ مِثْلَهَا فِي الْبَلَدِ ﴿٨٩﴾

“Ambao haukuumbwa mfano wake katika nchi?”

Ibn Zaid ameirejesha amesema ni nguzo, kutokana na urefu wake. Na amesema, walijenga nguzo huko *Ahqaaf*, hazikuumbwa mfano wake katika miji.¹ Ama Qatada na Ibn Jariir wao wamesema ni kabila la ‘Ad. Maana, halikuumbwa mfano wa kabila hilo katika miji. Kwa maana katika zama zao.² Na kauli hii ndiyo sahihi.

Kauli ya Ibn Zaid na waliyokwenda mwendo wake, kauli hiyo ni dhaifu. Kwa sababu lau maana yangukuwa hayo, angesema; ambazo hazikujengwa mfano wake katika miji.

Na hakika si vingine Allah تعالى Amesema;

لَمْ تُخْلَقْ مِثْلَهَا فِي الْبَلَدِ ﴿٩٠﴾

“Ambao haukuumbwa mfano wake katika nchi?”

Na Kauli Yake Allah تعالى;

وَتَمُودَ الَّذِينَ جَابُوا الصَّخَرَ بِالْوَادِ ﴿٩١﴾

“Na Thamudi waliochonga majabali huko bondeni?”

Maana yake: Walikata mawe katika jangwa. Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما, wanayachonga na wanayatoboa.³ Na kama hivyo amesema Mujahid, Qatada, Adh-Dhahak na Ibn Zaid⁴.

Na Amesema Allah تعالى,

وَتَنْحِتُونَ مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا فَرِهِينَ ﴿٩٢﴾

“Na mnachonga milimani majumba kwa ustadi.”(26:149)

¹ At-Tabari 24:406.

² At-Tabari 24:406.

³ At-Tabari 24:408.

⁴ At-Tabari 24:408.

Kutajwa kwa Firauni.

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَفِرْعَوْنَ ذِي الْأَوْتَادِ ﴿١٠٠﴾

“Na Firauni mwenye vigingi?”

Anasema Al-'Awfi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما “Al-Awtad” ni majeshi ambayo hulitia nguvu jambo lake.¹

Na pamesemwa: alikuwa Firauni anagongomea mikono yao na miguu yao katika vigingi vya chuma, anawafunga katika vigingi hivyo.

Na kama hivyo amesema Mujahid, alikuwa anawagongomea watu katika vigingi.²

Na kama hivyo amesema Said bin Jubair na As-Sudiy.³

Na Kauli Yake Allah تعالى،

الَّذِينَ طَغَوْا فِي الْبَلَدِ ﴿١٠١﴾ فَأَكْثَرُوا فِيهَا الْفَسَادَ ﴿١٠٢﴾

“Ambao walifanya jeuri katika nchi?. Wakakithirisha humo ufisadi?”

Maana yake: Waliasi na wakafanya katika ardhi ufisadi mkubwa sana na maudhi kwa watu.

فَصَبَّ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ سَوْطَ عَذَابٍ ﴿١٠٣﴾

“Basi Mola Wako Mlezi Aliwapiga mjeledi wa adhabu.”

Maana yake: Aliteremsha juu yao adhabu kutoka mbinguni na Akawateremshia mateso ambayo hayaepukiki kwa watu madhalimu.

¹ At-Tabari 24:409.

² At-Tabari 24:409.

³ At-Tabari 24:409.

⁴ At-Tabari 24:411.

Bwana Yumo katika Uangalizi.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّ رَبَّكَ لَبِالْمِرْصَادِ ﴿١٥﴾

“Hakika Mola Wako Mlezi Yupo kwenye mavizio Anawavizia.”

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما: Anasikia na Anaona.⁴ Maana: Anawaangalia viumbe Wake katika yale wanayotenda na Anamlipa kila mmoja kutokana na matendo yake katika dunia, na huko akhera watarejeshwa viumbe wote Kwake. Atahukumu kwa uadilifu Wake na Atamlipa kila mmoja yale anayostahiki na Yeye Ametakasika Yuko mbali na dhuluma.

فَأَمَّا الْإِنْسَانُ إِذَا مَا ابْتَلَاهُ رَبُّهُ فَأَكْرَمَهُ وَنَعَّمَهُ فَيَقُولُ رَبِّي أَكْرَمَنِ ﴿١٥﴾ وَأَمَّا إِذَا مَا ابْتَلَاهُ فَقَدَرَ عَلَيْهِ رِزْقَهُ فَيَقُولُ رَبِّي أَهْنَنِ ﴿١٦﴾ كَلَّا بَلْ لَا تَكْرُمُونَ الْيَتِيمَ ﴿١٧﴾ وَلَا تَحْضُونَ عَلَىٰ طَعَامِ الْمَسْكِينِ ﴿١٨﴾ وَتَأْكُلُونَ التُّرَاثَ أَكْلًا لَّمًّا ﴿١٩﴾ وَتُحِبُّونَ الْمَالَ حُبًّا جَمًّا ﴿٢٠﴾

15. Ama mtu anapajaribiwa na Mola Wake Mlezi, Akamkirimu na Akamne emesha, husema: Mola Wangu Mlezi Amenikirimu!

16. Na ama Anapomjaribu Akampunguzia riziki yake, husema: Mola Wangu Mlezi Amenitia unyonge!

17. Sivyoo hivyo! Bali nyinyi hamuwakirimu mayatima,

18. Wala hamhimizani kulisha masikini;

19. Na mnakula urithi kwa ulaji wa pupa,

20. Na mnapenda mali pendo la kupita kiasi.

Utajiri na Ufakiri ni Majaribio na Wala si Kutukuzwa au Kudhalilishwa kwa Mja na Mwenyezi Mungu.

Allah تعالى Amesema Akipinga hali ya mwanadamu pindi Allah تعالى, Anapompa nafasi nzuri katika rizki ili Amjaribu katika hilo, huitakidi kwamba hilo kutoka kwa Allah تعالى ni kutukuzwa yeye. Na si hivyo bali hayo ni majaribio kama Alivyosema Allah تعالى,

أَحْسِبُونَ أَنَّمَا نُثَمِّرُهُمْ بِهِ مِنْ مَّالٍ وَبَيْنَ ۞ نُسَارِعُ لَهُمْ فِي الْخَيْرَاتِ بَلْ لَا يَشْعُرُونَ ۞

“Je! Wanadhani ya kuwa kwa vile Tunavyowapa mali na watoto. Ndio Tunawahimizia kheri? Lakini wenyewe hawatambui.” (23:55-56)

Ni hivyo hivyo katika upande mwengine, pindi Atakapomjaribu na Kuifanya ngumu riziki yake, huitakidi kwamba hilo ni kudhalilishwa na Yeye. Amesema Allah تعالى,

كَلَّا

“Sivyo hivyo!” Maana yake: Halikuwa jambo kama alivyodai, si katika hili wala katika hili. Kwani Allah تعالى Anampa mali Anayempenda na Asiyempenda na Humnyima Anayempenda na Asiyempenda. Hakika hapana jambo jengine muhimu katika hali zote mbili isipokuwa kumtii Allah تعالى. Atakapokuwa tajiri amshukuru Allah تعالى juu ya hilo, na atakapokuwa ni fakiri na asubiri.

Miongoni mwa Maovu Ayafanyayo Mja katika Mali.

بَلْ لَا تُكْرِمُونَ الْيَتِيمَ ۞

“Bali nyinyi hamuwakirimu mayatima.”

Amepokea Abuu Dawuud kutoka kwa Sahil anamkusudia Ibn Said kwamba Mtume ﷺ amesema;

«أَنَا وَكَافِلُ الْيَتِيمِ كَهَاتَيْنِ فِي الْجَنَّةِ»

“Mimi na mlezi wa yatima tutakuwa kama vidole hivi peponi.” Akakutanisha kati ya vidole vyake viwili, kidole cha kati na kidole cha shahada.¹

¹ Abu Dawud 5:356. sawa na Muslim no. 2983.

وَلَا تَحْتَضِرُوا عَلَىٰ طَعَامِ الْمَسْكِينِ ﴿١٦﴾

“Wala hamhimizani kulisha masikini.”

Anakusudia hawaamrishi kuwafanyia wema mafakiri na masikini na hawahimizani wao kwa wao katika hilo.

وَتَأْكُلُونَ التَّرَاثَ

“Na mnakula urithi.”

Anakusudia mirathi.

أَكَلًا لَّمَّا ﴿١٧﴾

“Ulaji wa pupa.”

Maana yake: Kutoka upande wowote hajali limepatikana hilo katika halali au katika haramu.

وَتُحِبُّونَ الْمَالَ حُبًّا جَمًّا ﴿١٨﴾

“Na mnayapenda mali pendo la kupita kiasi.”

Maana yake: Mnayapenda sana. Baadhi yao wamesema, kupenda kupita mpaka.

* * *

كَلَّا إِذَا دُكَّتِ الْأَرْضُ دَكًّا دَكًّا ﴿٢١﴾ وَجَاءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ
 صَفًّا صَفًّا ﴿٢٢﴾ وَجِئَءَ يَوْمَئِذٍ بِجَهَنَّمَ ۚ يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ
 الْإِنْسَانُ وَأَنَّى لَهُ الذِّكْرَى ﴿٢٣﴾ يَقُولُ يَلِيَّتَنِي قَدَمْتُ
 لِحَيَاتِي ﴿٢٤﴾ فَيَوْمَئِذٍ لَا يُعَذِّبُ عَذَابُهُ أَحَدًا ﴿٢٥﴾ وَلَا
 يُوثِقُ وَثَاقَهُ أَحَدًا ﴿٢٦﴾ يَتَأْتِيهَا النَّفْسُ الْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾
 أَرْجِعِي إِلَىٰ رَبِّكَ رَاضِيَةً مُّرْضِيَةً ﴿٢٨﴾ فَأَدْخُلِي فِي عِبْدِي
 ﴿٢٩﴾ وَأَدْخُلِي جَنَّتِي ﴿٣٠﴾

كَلَّا إِذَا دُكَّتِ الْأَرْضُ دَكًّا دَكًّا ﴿٢١﴾ وَجَاءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا ﴿٢٢﴾
 وَجِئَءَ يَوْمَئِذٍ بِجَهَنَّمَ ۚ يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ وَأَنَّى لَهُ الذِّكْرَى ﴿٢٣﴾
 يَقُولُ يَلِيَّتَنِي قَدَمْتُ لِحَيَاتِي ﴿٢٤﴾ فَيَوْمَئِذٍ لَا يُعَذِّبُ عَذَابُهُ
 أَحَدًا ﴿٢٥﴾ وَلَا يُوثِقُ وَثَاقَهُ أَحَدًا ﴿٢٦﴾ يَتَأْتِيهَا النَّفْسُ الْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾

أَرْجِعِي إِلَىٰ رَبِّكَ رَاضِيَةً مُّرْضِيَةً ﴿٢٨﴾ فَأَدْخُلِي فِي عِبْدِي ﴿٢٩﴾ وَأَدْخُلِي جَنَّتِي ﴿٣٠﴾

21. Sivyoy hivyo! Itakapovunjwa ardhi vipande vipande,
22. Na Akaja Mola Wako Mlezi na Malaika waliojipanga mistari,
23. Na ikaletwa Jahannamu siku hiyo, siku hiyo mtu atakumbuka! Lakini kukumbuka huko kutamfaa nini?
24. Atasema: Laiti ningelijitangulizia kwa uhai wangu!
25. Basi siku hiyo hataadhibu yeyote namna ya Kuadhibu kwake.
26. Wala hatafunga yeyote kama Kufunga kwake.
27. Ewe nafsi iliyotua!
28. Rejea kwa Mola Wako Mlezi umeridhika, na umemridhisha.
29. Basi ingia miongoni mwa waja Wangu,
30. Na ingia katika Pepo Yangu.

Siku ya Qiyama Atalipwa Kila Mtu kwa Yale Aliyoyatenda Miongoni mwa Kheri au Shari.

Anaeleza Allah تعالى kuhusu yale yatakayotokea siku ya Qiyama, miongoni mwa vituko vikubwa sana. Amesema Allah تعالى;

كَلَّا

“Sivyo hivyo!”

Maana yake: Limethibiti jambo la Kiyama.

كَلَّا إِذَا دُكَّتِ الْأَرْضُ دَكًّا دَكًّا

“Sivyo hivyo, itakapovunjwa ardhi vipande vipande...”

Maana yake: Itakapotandikwa na kusawazishwa ardhi na majabali na viumbe kusimama mbele ya Mola wao,

وَجَاءَ رَبُّكَ

“Na Akaja Mola Wako Mlezi.”

Anakusudia kwa ajili ya kupambanua hukumu kati ya viumbe Wake, na itatokea baada ya kutaka uombezi, kwa Mtukufu wa watoto wa Adam, Muhammad ﷺ. Kwa ujumla ni kwamba baada ya kuomba Mitume watano waliopewa majukumu *Ulul-Azm* – mmoja baada ya mwengine. Kila mmoja wao atasema; ‘sikuwa nahusika na jambo hilo.’ Mpaka itamfikia zamu Mtume Muhammad ﷺ, atasema Mtume ﷺ: “Mimi hasa ndio nastahili kufanya jambo hilo.” Mtume ﷺ atakwenda ataomba mbele ya Allah تعالى Ahukumu kati ya waja Wake, Allah تعالى Atakubali maombi yake katika hilo.¹

Maombezi hayo ndiyo mwanzo wa maombezi yote na maombezi hayo yana hadhi kubwa, “*Al-Maqamu Al-Mahmoud*” kama yalivyotangulia maelezo yake katika *Sura Subhan*. Atakuja Bwana Aliyetukuka kwa ajili ya kupambanua hukumu kama Atakavyo, na malaika watakuja mbele Yake hali ya kupanga safu. Na Kauli Yake Allah تعالى,

¹ Ahmad 1:282.

وَجِئْنَا يَوْمَئِذٍ بِجَهَنَّمَ

“Na ikaletwa Jahannamu siku hiyo.”

Amepokea Imam Muslim Ibn Hajjaj katika sahihi yake kutoka kwa Abdillahi Ibn Mas'ud رضي الله عنه amesema, amesema Mtume ﷺ,

«يُؤْتَى بِجَهَنَّمَ يَوْمَئِذٍ لَهَا سَبْعُونَ أَلْفَ زِمَامٍ مَعَ كُلِّ زِمَامٍ سَبْعُونَ أَلْفَ مَلَكٍ يَجُرُّونَهَا»

“Utaletwa moto wa Jahannam siku hiyo ukiwa na hatamu sabini elfu kila hatamu moja ina upana - malaika elfu sabini wanaikokota Jahannam.”¹

Na kama hivi ameipokea At-Tirmidhi.² Na Kauli Yake Allah تعالى،

يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ

“Siku hiyo mtu atakumbuka!”

Maana yake: Matendo yake na yale aliyoyatanguliza katika zama zake za kale na za sasa,

وَأَنَّى لَهُ الذِّكْرَىٰ

“Lakini kukumbuka huko kutamfaa nini?”

Maana yake: Vipi kutamfaa kukumbuka.

يَقُولُ يَلْبِئْتَنِي قَدَّمْتُ لِحَيَاتِي

“Atasema: Laiti ningelijitangulizia kwa uhai wangu!”

Kwa maana: Atajuta juu ya yale aliyotenda huko nyuma kwake miongoni mwa maasia akiwa ni mwenye kuasi. Na atatamani lau angekuwa ameongeza katika kumtii Allah تعالى iwapo alikuwa ni mtiifu.

Kama alivyopokea Imam Ahmad bin Hambal, kutoka kwa Muhammad bin Abu Umairah na alikuwa katika Masahaba wa Mtume ﷺ amesema, “Lau kwamba mja alimtii Allah تعالى tokea siku aliyozaliwa mpaka atakapokufa hali ya kuwa

¹ Muslim 4:2184.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 7:294.

ni mkongwe, katika kumtii Allah تعالى, angeuona mchache utiifu huo siku ya Kiyama na angetamani kwamba arudishwe tena duniani ili aongeze thawabu na malipo.”¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَيَوْمَئِذٍ لَا يُعَذِّبُ عَذَابُهُ أَحَدًا ﴿٢١﴾

“Basi siku hiyo hataadhibu yeyote namna ya kuadhibu kwake.”

Maana yake: Hapana mtu yeyote mkali wa adhabu kama Allah تعالى kwa wale waliomuasi.

وَلَا يُوثِقُ وَثَاقَهُ أَحَدًا ﴿٢٢﴾

“Wala hatafunga yeyote kama kufunga Kwake.”

Maana yake: Hapana mtu yeyote mkali wa kukamata na kufunga kuliko mazabania² kwa wale waliomkufuru Bwana Wao Mwenye Kushinda na Kutukuka. Na haya ni kwa watu waovu katika viumbe na madhalimu. Ama nafsi iliyo safi, yenye kutulizana, iliyotua na iliyothibiti yenye kwenda pamoja na ukweli, itaambiwa;

يَتَأْتِيهَا النَّفْسُ الْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٣﴾ أَرْجِعِي إِلَىٰ رَبِّكِ

“Ewe nafsi iliyo tua!. Rejea kwa Mola Wako Mlezi.”

Maana yake: Kwenye ukaribu Wake na malipo Yake na yale Aliyowaandalia waja Wake peponi.

رَاضِيَةً

“Umeridhika...”

Maana yake: Katika nafsi,

مَرْضِيَّةً ﴿٢٤﴾

“Na umemridhisha.”

Maana yake: Imemridhia Allah تعالى Naye Ameiridhia na Ameiridhisha.

¹ Ahmad 4:185.

² Hawa ni malaika wa adhabu motoni. Angalia surat Al-Alaq.

فَادْخُلِي فِي عِبَادِي ﴿٢١﴾

“Basi ingia miongoni mwa waja Wangu.”

Maana yake: Katika ujumla wao,

وَأَدْخُلِي جَنَّتِي ﴿٢٢﴾

“Na ingia katika Pepo Yangu.”

Maneno haya itaambiwa nafsi wakati wa kufikiwa na mauti na pia katika siku ya Kiyama. Kama ambavyo malaika watampa habari njema muumini wakati wa kufikwa na mauti, na wakati wa kusimama kwake kutoka katika kaburi lake basi ni kama hivyo hapa.

Amepokea Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake Allah تعالى:

يَتَأْتِيهَا النَّفْسُ الْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٣﴾ أَرْجِعِي إِلَىٰ رَبِّكَ رَاضِيَةً مُّرَضِيَةً ﴿٢٤﴾

“Ewe nafsi iliyo tua! Rejea kwa Mola Wako Mlezi umeridhika, na umemridhisha”

Amesema: Abubakr رضي الله عنه akiwa amekaa akasema; ‘Eee!! Mjumbe wa Allah! Ni uzuri ulioje wa maneno haya!!’ Akasema,

«أَمَا إِنَّهُ سَيَقَالُ لَكَ هَذَا»

“Ama hakika utaambiwa maneno haya.”¹

Huu ni mwisho wa *Suratu Al-Fajr* na kila sifa njema zote na Utukufu Anastahiki Allah تعالى.

* * *

¹ Ibn Abi Hatim, Ibn Marda wayhi, na Ad-Dhiyaa Al-Maqdasi katika *Al-Mukhtarah*. Angalia *Ad-Durr Al-Manthur* 8:513.

Tafsiri ya Suratul Balad

Sura ya 90

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْبَلَدِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

لَا أُقْسِمُ بِهَذَا الْبَلَدِ ۝ وَأَنْتَ حِلٌّ بِهَذَا الْبَلَدِ ۝
 وَوَالِدٍ وَمَا وَلَدَ ۝ لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي كَبَدٍ ۝
 أَمْحَسِبُ أَنْ لَنْ يَقْدِرَ عَلَيْهِ أَحَدٌ ۝ يَقُولُ أَهْلَكْتُ مَالًا
 لُبَدًا ۝ أَمْحَسِبُ أَنْ لَمْ يَرَهُ أَحَدٌ ۝ أَلَمْ نَجْعَلْ لَهُ
 عَيْنَيْنِ ۝ وَلِسَانًا وَشَفَتَيْنِ ۝ وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ ۝
 فَلَا اقْتَحَمَ الْعَقَبَةَ ۝ وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْعَقَبَةُ ۝
 فَكُّ رَقَبَةٍ ۝ أَوْ إِطْعَمٌ فِي يَوْمٍ ذِي مَسْغَبٍ ۝ يَتِيمًا
 ذَا مَقْرَبَةٍ ۝ أَوْ مَسْكِينًا ذَا مَقْرَبَةٍ ۝ ثُمَّ كَانَ مِنَ
 الَّذِينَ ءَامَنُوا وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا بِالْمَرْحَمَةِ ۝
 أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّيْمَةِ ۝ وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِنَا هُمْ
 أَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ ۝ عَلَيْهِمْ نَارٌ مُؤَصَّدَةٌ ۝

لَا أُقْسِمُ بِهَذَا الْبَلَدِ ۝ وَأَنْتَ
 حِلٌّ بِهَذَا الْبَلَدِ ۝ وَوَالِدٍ وَمَا
 وَلَدَ ۝ لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي
 كَبَدٍ ۝ أَمْحَسِبُ أَنْ لَنْ يَقْدِرَ
 عَلَيْهِ أَحَدٌ ۝ يَقُولُ أَهْلَكْتُ
 مَالًا لُبَدًا ۝ أَمْحَسِبُ أَنْ لَمْ
 يَرَهُ أَحَدٌ ۝ أَلَمْ نَجْعَلْ لَهُ
 عَيْنَيْنِ ۝ وَلِسَانًا وَشَفَتَيْنِ ۝
 وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ ۝

1. Naapa kwa Mji huu!
2. Nawe unaukaa Mji huu.
3. Na Naapa kwa mzazi na alichokizaa.
4. Hakika Tumemuumba mtu katika taabu.

5. Ati anadhani hapana yeyote atayemuweza?

6. Anasema: Nimeteketeza chungu ya mali.

7. Ati anadhani ya kuwa hapana yeyote anayemuona?

8. Kwani hatukumpa macho mawili?

9. Na ulimi, na midomo miwili?

10. Na Tukambainishia njia zote mbili?

Kiapo kwa Utukufu wa Makkah Juu ya Kuumbwa kwa Mwanadamu katika Taabu.

Hiki ni kiapo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Aliyetakata na Kutukuka, Akiuapia mji wa Makkah, "*Ummul Quraa*" mama wa miji yote duniani, katika hali ya uhalali wa mkazi wake humo, ili Azindue juu ya ukubwa wa cheo chake katika hali ya kuwa watu wake wamo katika kutukuza mji huo. Amesema Khusaif kutoka kwa Mujahid.

لَا أُقْسِمُ بِهَذَا الْبَلَدِ

"Naapa kwa Mji huu!"

"La" ina maana,¹ Jibu kwao, makafiri wa Makka, Ninaapa kwa mji huu. Na amesema Shabib bin Bishir kutoka kwa Ikrimah kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

لَا أُقْسِمُ بِهَذَا الْبَلَدِ

"Naapa kwa Mji huu!"

Anakusudia mji wa Makkah.

وَأَنْتَ حِلٌّ بِهَذَا الْبَلَدِ

"Nawe unaukaa Mji huu."

Amesema; "Ee!! Muhammad! ni halali kwako kutetea mji huu."²

Na kama hivyo amesema Said Ibn Jubair, Abu Swaleh, 'Atiyah na Adh-Dhahak na Qatada na As-Sudiy na Ibn Zaid.³ Na amesema Hassan Basry. Alihalalisha

¹ *Ad-Durr Al-Manthur* 8:517.

² *Al-Qurtubi* 20:60, na *Ad-Durr Al-Manthur* 8:518.

³ *Al-Qurtubi* 20:60 na *Ad-Durr Al-Manthur* 8:518.

Allah تعالى kwake Makkah kwa muda wa saa moja ya mchana.¹ Maana hiyo waliyoisema imethibiti katika Hadithi sahihi ya Mtume ﷺ, amesema:

«إِنَّ هَذَا الْبَلَدَ حَرَمَهُ اللَّهُ يَوْمَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ، فَهُوَ حَرَامٌ بِحُرْمَةِ اللَّهِ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا يُعْضَدُ شَجَرُهُ وَلَا يُخْتَلَى خَلَاهُ، وَإِنَّمَا أَحَلَّتْ لِي سَاعَةٌ مِنْ نَهَارِي، وَقَدْ عَادَتْ حُرْمَتُهَا التَّيْمَ كَحُرْمَتِهَا بِالْأَمْسِ، أَلَا فَلْيَبْلُغِ الشَّاهِدُ الْغَائِبَ»

“Kwa hakika mji huu alikutuza Mwenyezi Mungu siku Aliyounda mbingu na ardhi, kwa hiyo mji huu ni mtukufu kwa utukufu wa Mwenyezi Mungu mpaka siku ya Qiyama, hautakatwa mti wake, na hautang’olewa mmea wake, hakika si vingine ulihalalishwa kwangu kwa muda wa saa moja tu ya mchana, na umerejea utukufu wake leo kama ulivyokuwa hapo jana, zindukeni! Na afikishiwe ujumbe huu aliyepo na asiyekuwepo.”²

Na katika tamko jengine;

«فَإِنْ أَحَدٌ تَرَحَّصَ بِقِتَالِ رَسُولِ اللَّهِ فَقُولُوا: إِنَّ اللَّهَ أَدِنَ لِرَسُولِهِ وَلَمْ يَأْذَنْ لَكُمْ»

“Iwapo mtu yeyote atachukua ruhusa ya kupigana ndani ya Makkah, kwa sababu ya kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipigana semeni; Hakika Mwenyezi Mungu Alimruhusu Mjumbe Wake na hakuwaruhusu nyinyi.”³

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَوَالِدٍ وَمَا وَلَدَ ﴿١٠٠﴾

“Na Naapa kwa mzazi na alichokizaa.”

Na amesema Mujahid, Abu Swaleh, Qatada, Adh-Dhahak, Sufyan Ath-Thawri, Sa’id bin Jubair, As-Sudiy, Al-Hassan Al-Basri, Khusayf, Shurahbil bin Sa’d na wengine, Anakusudia kwa Mzazi ni Adam عليه السلام na alichokizaa ni watoto wake.⁴ Na haya maelezo ya Mujahid na wenzake ni mazuri na yenye nguvu.

¹ Ad-Durr Al-Manthur 8:518.

² Fat’hul Al-Bari 4:56.

³ Fat’hul Al-Bari 1:238.

⁴ Al-Qurtubi 20:61, Ad-Durr Al-Manthur 8:519, na At-Tabari 24:432.

Kwa sababu Allah تعالى wakati Alipoapa kwa *Ummul Quraa* nayo ni makazi, Ameapa baada ya hapo kwa mkazi naye ni Adam عليه السلام Baba wa watu wote na watoto wake. Amesema Abuu Imran Al-Jawni huyo ni Ibrahim عليه السلام na watoto wake, na ameyapokea hayo Ibn Jarir¹ رحمه الله تعالى na Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى, na ameyafadhilisha hayo Ibn Jarir رحمه الله تعالى, kwamba inajumuisha kila mzazi na mtoto wake, na hayo yanawezekana.² Na Kauli Yake Allah تعالى,

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي كَبَدٍ ﴿١٠﴾

“Hakika Tumemuumba mtu katika taabu.”

Na amesema Ibn Abu Najih na Juraiji na ‘Atwaa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, amesema kuhusiana na neno “*Fi Kabad*” kuwa ni katika shida ya uumbaji, je hamuoni? Na akataja kuzaliwa kwake na kuota kwa meno yake.³ Amesema Mujahid kuwa,

فِي كَبَدٍ ﴿١٠﴾

“...katika taabu...”

Ni hali ya tone la manii, kisha pande la damu kisha pande la nyama. Anasumbuka katika hatua za kuumbwa. Amesema Mujahid. Aya hii ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا ۗ

“Mama yake amechukua mimba yake kwa taabu, na akamzaa kwa taabu.” (46:15)

Na amemnyonyesha kwa taabu na maisha yake ni ya taabu, kwa hiyo yeye anasumbuana na hayo. Na amesema Saiid bin Jubair رحمه الله تعالى:

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي كَبَدٍ ﴿١٠﴾

“Hakika Tumemuumba mtu katika taabu.” Katika matatizo na kutafuta sababu za kuishi. Na amesema Ikrimah; katika shida na uwezo.⁴

¹ At-Tabari 24:433.

² At-Tabari 24:433.

³ At-Tabari 24:434.

⁴ *Ad-Durr Al-Manthur* 8:520.

Na amesema Qatada katika taabu.¹ Na kutokana na Al-Hassan, 'Anapambana na madhila ya dunia na shida ya akhera.'

Mwanadamu Amezungukwa na Allah تعالی na Neema Zake.

Na Kauli Yake Allah تعالی:

أَحْسَبُ أَنْ لَنْ يَقْدِرَ عَلَيْهِ أَحَدٌ ﴿١٠﴾

"Ati anadhani hapana yeyote atayemuweza?"

Amesema Hassan Basry; Anakusudia,

أَحْسَبُ أَنْ لَنْ يَقْدِرَ عَلَيْهِ أَحَدٌ ﴿١٠﴾

"Ati anadhani hapana yeyote atayemuweza?"

'Kuyachukua mali yake, Na amesema Qatada:

أَحْسَبُ أَنْ لَنْ يَقْدِرَ عَلَيْهِ أَحَدٌ ﴿١٠﴾

"Ati anadhani hapana yeyote atayemuweza?"

Amesema, mwanadamu anadhani kuwa hatoulizwa kuhusu mali hii ni kutoka wapi ameichuma na katika jambo gani ameitumia?²

Na Kauli Yake Allah تعالی,

يَقُولُ أَهْلَكْتُ مَالًا لُبَدًا ﴿١١﴾

"Anasema: Nimeteketeza chungu ya mali."

Maana yake: Anasema mwanadamu nimetumia mali mengi sana. Ameyasema hayo Mujahid, Hassan, Qatada, As-Sudiy na wengine.³

أَحْسَبُ أَنْ لَمْ يَرَهُ أَحَدٌ ﴿١٢﴾

"Ati anadhani ya kuwa hapana yeyote anayemuona?"

¹ At-Tabari 24:433.

² At-Tabari 24:436.

³ At-Tabari 24:436.

Amesema Mujahid, maana; anadhani hakumuona Allah تعالى Mwenye Kushinda na Kutukuka. Na kama hivyo wamesema wanawazuoni wengine waliotangulia.

Na Kauli Yake Allah تعالى,

أَلَمْ يَجْعَلْ لَهُ عَيْنَيْنِ ﴿١٠﴾

“Kwani hatukumpa macho mawili?”

Maana yake: Anaona kutokana nayo?

وَلِسَانًا

“Na ulimi,..”

Maana yake: Anatamka kwa huo ulimi na anayaeleza yaliyo moyoni mwake.

وَشَفْتَيْنِ ﴿١١﴾

“...na midomo miwili?”

Na anajisaidia kwa midomo hiyo katika kuzungumza na kula chakula, na kuupamba uso wake na mdomo wake.

Kupambanua kati ya Kheri na Shari ni Neema.

وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ ﴿١٢﴾

“Na Tukambainishia njia zote mbili?”

Njia mbili. Amesema Sufyan Thaury رحمه الله تعالى kutoka kwa ‘Asim kutoka kwa Zirr kutoka kwa Abdillah Ibn Mas’ud رضي الله عنه,

وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ ﴿١٢﴾

“Na Tukambainishia njia zote mbili?”

Amesema ya kheri na shari.² Na kama hivyo imepokelewa kutoka kwa Ali, Ibn Abbas, Mujahid, Ikrimah, Abu Wail, Abu Swaleh, Muhammad bin Kaab, Adh-Dhahak na Atwaa Khurafani, pamoja na watu wengine رضي الله عنهم.¹

¹ At-Tabari 24:437.

² At-Tabari 24:437, 438. na Ad-Durr Al-Manthuri 8:521, 522.

Na mfano wa aya hii ni kama Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ نُطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿١﴾ إِنَّا هَدَيْنَاهُ
السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٢﴾

“Hakika Sisi Tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika, Tumfanyie mtihani. Kwa hivyo Tukamfanya mwenye kusikia, mwenye kuona.” “Hakika Sisi Tumembainishia Njia. Ama ni mwenye kushukuru, au mwenye kukufuru.” (76:2-3)

فَلَا أَقْتَحَمَ الْعَقَبَةَ ﴿٣﴾ وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْعَقَبَةُ ﴿٤﴾ فَكَّ رَقَبَةَ ﴿٥﴾ أَوْ إِطْعَمْتُ فِي يَوْمٍ
ذِي مَسْغَبَةٍ ﴿٦﴾ يَتِيمًا ذَا مَقْرَبَةٍ ﴿٧﴾ أَوْ مَسْكِينًا ذَا مَتْرَبَةٍ ﴿٨﴾ ثُمَّ كَانَ مِنَ الَّذِينَ
ءَامَنُوا وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا بِالرِّحْمَةِ ﴿٩﴾ أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْيَمِينِ ﴿١٠﴾ وَالَّذِينَ
كَفَرُوا بِعَاقِبَتِنَا هُمْ أَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ ﴿١١﴾ عَلَيْهِمْ نَارٌ مُؤَصَّدَةٌ ﴿١٢﴾

11. Lakini hakujitoma kwenye njia ya vikwazo vya milimani.
12. Na nini kitakujuywa ni nini njia ya vikwazo vya milimani?
13. Kumkomboa mtumwa;
14. Au kumlisha siku ya njaa
15. Yatima aliye jamaa,
16. Au masikini aliye vumbini.
17. Tena awe miongoni mwa walioamini na wakausiana kusubiri na akausiana kuhurumiana.
18. Hao ndio watu wa kheri wa kuliani.
19. Lakini waliozikataa Ishara Zetu, hao ndio watu wa shari wa kushotoni.
20. Juu yao utakuwa Moto uliofungiwa kila upande.

Kuhimiza Juu ya Kuifuata Njia ya Kheri

Amesema Ibn Zaid,

فَلَا أَقْتَحَمَ الْعَقَبَةَ ﴿١﴾

“Lakini hakujitoma kwenye njia ya vikwazo vya milimani.”

Maana yake: Kwa nini asipite njia ambayo ndani yake pana kheri na uokovu Kisha ameweka wazi kwa Kusema Allah تعالى;

وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْعَقَبَةُ ﴿٢﴾ فَكُ رَقَبَةٍ ﴿٣﴾ أَوْ إِبْرَاهِيمَ

**“Na nini kitakujavya ni nini njia ya vikwazo vya milimani?
Kumkomboa mtumwa, au kumlisha...”¹**

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Said bin Murjanah kwamba yeye amemsikia Abu Hurairah عنه رضي الله akisema, amesema Mtume ﷺ,

«مَنْ أَعْتَقَ رَقَبَةً مُؤْمِنَةً أَعْتَقَ اللَّهُ بِكُلِّ إِرْبٍ - أَيِ عَضْوٍ - مِنْهَا إِرْبًا مِنْهُ مِنَ النَّارِ حَتَّى
إِنَّهُ لَيَغْتِقُ بِالْيَدِ الْيَدَ، وَبِالرَّجْلِ الرَّجْلَ، وَبِالْفَرْجِ الْفَرْجَ»

“Mwenye kumuacha huru mtumwa muumini - Atakiacha huru Mwenyezi Mungu, kila kiungo - kwa mtumwa huyo - kiungo chake na moto - mpaka Mwenyezi Mungu Atauacha huru mkono kwa mkono, na mguu kwa mguu na tupu kwa tupu.”

Aliuliza Ali bin Hussein, “Wewe umeyasikia haya kutoka kwa Abu Hurairah عنه رضي الله Akasema Ali bin Hussein عنه رضي الله kwa kijana wake ambaye ni mchangamfu katika vijana wake, “Hebu mwiite Mutrifu.” Aliposimama mbele yake alisema, “Nenda zako wewe upo huru kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu.”¹ Na ameyapokea hayo Bukhari na Muslim, At-Tirmidhiy na Annasai kutokana na njia ya Saiid bin Marjanah.² Amepokea Ahmad kutoka kwa Abuu Umaamah kutoka kwa Amri bin Abbas عنه رضي الله, ya kuwa Mtume ﷺ amesema,

¹ At-Tabari 24:440.

² Ahmad 2:422.

³ Fat’hul Al-Bari 5:174 na 11608, na Muslim 2:1147, Tuhfat Al-Ahwadhi 5:144, na An-Nasai katika Al-Kubra 3:168.

«مَنْ بَنَى مَسْجِدًا يُذَكِّرَ اللَّهُ فِيهِ بَنَى اللَّهُ لَهُ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ وَمَنْ أَعْتَقَ نَفْسًا مُسْلِمَةً كَانَتْ فِدْيَتُهُ مِنْ جَهَنَّمَ وَمَنْ شَابَ شَيْبَةً فِي الْإِسْلَامِ كَانَتْ لَهُ نُورًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

“Mwenye kujenga msikiti ili Allah Atajwe ndani yake, Allah Atamjengea mtu huyo nyumba Peponi, na mwenye kumuacha huru Muislamu, itakuwa ndiyo fidia yake dhidi ya Jahanamu, na mwenye kuota mvi huku angali katika Uislamu, zitakuwa mvi hizo nuru kwa ajili yake Siku ya Kiyama.”³

Amesema Sulami nilimuambia tuzungumzie Hadithi uliyoisikia toka kwa Mtume ﷺ hamna ndani yake upungufu wala dhana akasema; nimemsikia akisema,

«مَنْ وُلِدَ لَهُ ثَلَاثَةٌ أَوْلَادٍ فِي الْإِسْلَامِ فَمَاتُوا قَبْلَ أَنْ يَبْلُغُوا الْحِنْتَ أَدْخَلَهُ اللَّهُ الْجَنَّةَ بِفَضْلِ رَحْمَتِهِ إِيَّاهُمْ، وَمَنْ شَابَ شَيْبَةً فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَانَتْ لَهُ نُورًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَمَنْ رَمَى بِسَهْمٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بَلَغَ بِهِ الْعُدْرَ أَصَابَ أَوْ أَخْطَأَ كَانَ لَهُ عِنَقٌ رَقِيَّةً، وَمَنْ أَعْتَقَ رَقَبَةً مُؤْمِنَةً أَعْتَقَ اللَّهُ بِكُلِّ عَضْوٍ مِنْهُ عَضْوًا مِنْهُ مِنَ النَّارِ، وَمَنْ أَنْفَقَ زَوْجِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَإِنَّ لِلْجَنَّةِ ثَمَانِيَةَ أَبْوَابٍ يُدْخِلُهُ اللَّهُ مِنْ أَيِّ بَابٍ شَاءَ مِنْهَا»

“Yule ambaye wamezaliwa kwake watoto watatu katika Uislamu wakafa kabla hawajabalehe Allah تعالی Atamuingiza yeye peponi kutokana na ubora wa rehema yake kwao. Na mwenye kupata mvi moja katika njia ya Allah تعالی, itakuwa mvi hiyo ni nuru kwake siku ya Kiyama, na mwenye kutupa mshale katika njia ya Allah تعالی ukamfikia adui, ulimpata au ulimkosa utakuwa hilo kwake ni kama kumuacha huru mtumwa. Na mwenye kumuacha huru mtu aliye muumini atakiacha huru Allah تعالی kila kiungo cha mtumwa huyo, kiungo chake na moto. Na mwenye kutoa aina mbili za vitu katika njia ya Allah تعالی, Hakika pepo ina milango minane atamuingiza Allah تعالی katika mlango wowote anaoutaka¹ katika milango hiyo.”¹

¹ Ahmad 4:386.

Imepokewa hadithi hii kutokana na njia nyingi na mapokezi hayo ni mazuri na yenye nguvu, na ni kwa Allah تعالی tu kusifiwa.

Na Kauli Yake Allah تعالی:

أَوْ إِطْعَمٌ فِي يَوْمٍ ذِي مَسْغَبَةٍ ﴿١٠﴾

“Au kumlisha siku ya njaa.”

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما; Yenye Njaa.¹ Na kama hivyo amesema Ikrimah, Mujahid, Adh-Dhahak, Qatada na wengine² Neno “Assaghub” ni njaa.

Na Kauli Yake Allah تعالی:

يَتِيمًا

“Yatima.”

Maana yake: Akamlisha katika siku kama hiyo Yatima.

ذَا مَقْرَبَةٍ ﴿١١﴾

“Aliye jamaa.”

Maana yake: Mwenye udugu naye, amesema hayo Ibn Abbas, Ikrimah, Hassan, Adh-Dhahak na As-Sudiy رضي الله عنهم.² Kama ilivyokuja katika Hadithi ambayo ameipokea Imam Ahmad kutoka kwa Salman bin Amir رضي الله عنه amesema; alimsikia Mtume ﷺ akisema;

«الصَّدَقَةُ عَلَى الْمِسْكِينِ صَدَقَةٌ وَعَلَى ذِي الرَّجْمِ اثْنَانِ: صَدَقَةٌ وَصِلَةٌ»

“Kutoa sadaka kwa maskini ni sadaka tu, na kutoa kwa ndugu ni sadaka mbili, ni sadaka na kuunga udugu.”³

Na ameipokea Hadith hiyo Atirmidhiy na Annasai⁴ na hii ni isnad sahihi. Na Kauli Yake Allah تعالی,

¹ At-Tabari 24:442

² Al-Tabari 24:442, 443.

³ Ad-Durr Al-Manthur 8:525.

⁴ Ahmad 4:214.

⁵ Tuhfat Al-Ahwadhi 3:324, na An-Nasai 5:92.

أَوْ مَسْكِينًا ذَا مَتْرَبَةٍ ﴿١٧﴾

“Au masikini aliye vumbini.”

Maana yake: Fukara sana aliyetopea. Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما, ni yule aliyetupwa njiani ambaye hana nyumba na kitu chochote kinachomkinga na mchanga.¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

ثُمَّ كَانَ مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا

“Tena awe miongoni mwa walioamini.”

Maana yake: Kisha yeye pamoja na kuwa na sifa hizo nzuri zilizo wazi ni muumini kwa moyo wake, anataka malipo ya kufanya hivyo kutoka kwa Allah تعالى, Mwenye Kushinda na Utukufu. Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَىٰ لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ كَانَ سَعْيُهُمْ مَشْكُورًا ﴿١٨﴾

“Anayeitaka Akhera, na akazifanyia juhudi a’ mali zake, naye ni Muumini, basi hao juhudi yao itakuwa ni ya kushukuriwa.” (17:19)

Na Amesema Allah تعالى,

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ

“Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini.” (16:97)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا بِالْبِرِّحِمَةِ ﴿١٩﴾

“...na wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana.”

Maana yake: Akawa ni katika waumini wenye kutenda matendo mema, wenye kuusia kusubiri juu ya maudhi ya watu na juu ya kuwahurumia, kama yalivyokuja nayo katika Hadithi,

¹ At-Tabari 24:444.

«الرَّاحِمُونَ يَرْحَمُهُمُ الرَّحْمَنُ، اِرْحَمُوا مَنْ فِي الْأَرْضِ يَرْحَمْكُمْ مَنْ فِي السَّمَاءِ»

“Wenye kuwahurumia watu Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma Atawarehemu wao. Wahurumieni waliyo katika ardhi watawahurumieni waliyo mbinguni.”¹

Na imekuja katika Hadith nyingine,

«لَا يَرْحَمُ اللَّهُ مَنْ لَا يَرْحَمُ النَّاسَ»

“Hatamhurumia Mwenyezi Mungu yule asiyewahurumia watu.”²

Na Amesema Abu Dawuud kutoka kwa Abdillahi bin Amri رضي الله عنه aliyepokea hadithi hii kuwa amesema;

«مَنْ لَمْ يَرْحَمْ صَغِيرَنَا وَيَعْرِفْ حَقَّ كَبِيرَنَا فَلَيْسَ مِنَّا»

“Ambaye hakuhurumia mdogo wetu na hakujua haki ya mkubwa wetu huyo si katika sisi.”³

Na Kauli Yake Allah تعالى:

أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْمَيْمَةِ ﴿٢٤﴾

“**Hao ndio watu wa kheri wa kuliani.**” Maana yake: Wenye kusifika na sifa hizo ni katika watu wa kuume.

Watu wa Upande wa Kushoto na Malipo Yao.

Kisha Amesema Allah تعالى:

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِعَاقِبَتِنَا هُمْ أَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ ﴿٢٥﴾

“**Lakini waliozikataa Ishara Zetu, hao ndio watu wa shari wa kushotoni.**”

Maana yake: Watu wa kushoto.

¹ Abu Dawud 5:231.

² Muslim 4:1809.

³ Abu-Daud 5:231.

عَلَيْهِمْ نَارٌ مُّؤَصَّدَةٌ ﴿٩٠﴾

“Juu yao utakuwa Moto ulio fungwiwa kila upande.”

Maana yake: Mwenye kufungwiwa juu yao hapana namna kwao ya kuepuka moto huo, na hawana namna yoyote kwao ya kutoka humo motoni. Amesema Abuu Huraira, Ibn Abbas, Ikrimah, Saiid bin Jubair, Mujahid, Muhamad bin Kaab Quradh, Attiya, ‘Awfi, Hassan, Qatada na As-Suddi.

مُؤَصَّدَةٌ ﴿٩١﴾

“...fungwiwa kila upande.”

Maana yake: ‘Mwenye kufungwa.’¹ Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما, wenye kufungwa milango yake,

مُؤَصَّدَةٌ ﴿٩٢﴾

“...Uliofungwiwa kila upande.”²

Na amesema Adh-Dhahak, ‘(Wenye kukomewa) Ukuta usiokuwa na milango.’ Na amesema Qatada,

مُؤَصَّدَةٌ ﴿٩٣﴾

“...Uliofungwiwa kila upande.”

Wenye kufungwa hapana mwangaza ndani yake na hapana sehemu ya kupenya wala kutoka humo motoni milele.³

Huu ni mwisho wa tafsiri ya *Suratu Al Balad* ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹ At-Tabari 24:447, na *Ad-Durr Al-Manthur* 8:526.

² *Ad-Durr Al-Manthur* 8:526.

³ At-Tabari 24:447.

Tafsiri ya Suratu Ash-Shams

Sura ya 91

Iliteremshwa Makkah

Kusomwa kwa *Washamsi* katika Sala ya Isha.

Imetangulia Hadith ya Jabir رضي الله عنه ambayo ipo katika sahihi ya Bukhari na Muslim kwamba Mtume ﷺ alisema kumuambia Muadh رضي الله عنه,

«خَلَا صَلَّيْتَ بِـ ﴿سَبِّحْ أَسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى﴾ ﴿وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا﴾ ﴿وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَى﴾؟»

“Kwa nini usingesali kwa kusoma ‘Sabihisma Rabika Al aala’ ‘Washamsi wa Dhuhaha’ ‘Wallayli Idhaa Yagshaa?’”¹

* * *

¹ Fat’hul Al-Bari 2:234, na Muslim 1:340.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا ﴿١﴾ وَالْقَمَرِ إِذَا
تَلَّهَا ﴿٢﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا جَلَّهَا ﴿٣﴾
وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَاهَا ﴿٤﴾ وَالسَّمَاءِ وَمَا
بَنَدَهَا ﴿٥﴾ وَالْأَرْضِ وَمَا طَحَنَهَا ﴿٦﴾
وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّاهَا ﴿٧﴾ فَأَلْهَمَهَا
فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا ﴿٨﴾ قَدْ أَفْلَحَ مَنْ
زَكَّاهَا ﴿٩﴾ وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّاهَا ﴿١٠﴾
إِذْ أَنْبَعَتْ أَشْقَاهَا ﴿١١﴾ فَقَالَ هُمْ رَسُولُ اللَّهِ نَاقَةَ اللَّهِ
وَسُقَيْنَهَا ﴿١٢﴾ فَكَذَّبُوهُ فَعَقَرُوهَا فَدَمْدَمَ عَلَيْهِمْ رَبُّهُمْ
بِذُنُوبِهِمْ فَسَوَّاهَا ﴿١٣﴾ وَلَا يَخَافُ عُقْبَاهَا ﴿١٤﴾

وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا ﴿١﴾ وَالْقَمَرِ إِذَا
تَلَّهَا ﴿٢﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا جَلَّهَا ﴿٣﴾
وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَاهَا ﴿٤﴾ وَالسَّمَاءِ وَمَا
بَنَدَهَا ﴿٥﴾ وَالْأَرْضِ وَمَا طَحَنَهَا ﴿٦﴾
وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّاهَا ﴿٧﴾ فَأَلْهَمَهَا
فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا ﴿٨﴾ قَدْ أَفْلَحَ مَنْ
زَكَّاهَا ﴿٩﴾ وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّاهَا ﴿١٠﴾

1. Naapa kwa jua na
mwangaza wake!

2. Na kwa mwezi unapoli-
fuatia!

3. Na kwa mchana unapoli-
dhihirisha!

4. Na kwa usiku unapolifunika!

5. Na kwa mbingu na kwa Aliyeijenga!

6. Na kwa ardhi na kwa Aliyeitandaza!

7. Na kwa nafsi na kwa Aliyeitengeneza!

8. Kisha Akaifahamisha uovu wake na wema wake,

9. Hakika amefanikiwa aliyeitakasa,

10. Na hakika amekhasiri aliyeviza.

Kuapa kwa Allah تعالیٰ kwa Viumbe Vyake Juu ya Kufuzu kwa Mwenye Kuitakasa Nafsi Yake na Kupata Hasara kwa Mwenye Kuizamisha katika Mambo Maovu.

Amesema Mujahid;

وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا ﴿١﴾

“Naapa kwa jua na mwangaza wake!”

Maana yake: Na mwangaza wake.¹ Na amesema Qatada,

وَضُحَاهَا ﴿٢﴾

“Na mwangaza wake!”

Mchana wote.² Amesema Ibn Jarir رحمه الله تعالى; na usawa ni kusemwa; ‘Ameliapia Allah تعالیٰ jua na mchana wake kwa sababu mwangaza wa jua ndiyo wenye kuonekana mchana.’

وَالْقَمَرِ إِذَا تَلَّهَا ﴿٣﴾

“Na kwa mwezi unapolifuatia!”

Amesema Mujahid: Utakapolifuatia Jua.³ Na amesema Aufi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.

وَالْقَمَرِ إِذَا تَلَّهَا ﴿٤﴾

“Na kwa mwezi unapolifuatia!”

Amesema unalifuatia mchana.⁴ Na amesema Qatada. Pindi utakapolifuatia usiku wa mwezi mwandamo, litakapozama jua unaona mwezi mwandamo.⁵ Na Kauli Yake Allah تعالیٰ,

وَالنَّهَارِ إِذَا جَلَّهَا ﴿٥﴾

“Na kwa mchana unapolidhihirisha!”

Amesema Mujahid, utakapoangaza.⁶

¹ At-Tabari 24:451.

² At-Tabari 24:451.

³ At-Tabari 24:452. Isnadi yake ni dhaifu.

⁴ At-Tabari 24:452. Isnadi yake ni dhaifu.

⁵ At-Tabari 24:452. Isnadi yake ni dhaifu.

⁶ At-Tabari 24:529.

Na kwa sababu hiyo amesema Mujahid,

وَالنَّهَارِ إِذَا جَلَّتْهَا ﴿٢٠﴾

“Na kwa mchana unapolidhihirisha.”

Na wamesema katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّى ﴿٢١﴾

“Na kwa mchana unapolidhihirisha.”

Na wamesema katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿٢٢﴾

“Na kwa usiku unapolifunika!” (92:2)

Anakusudia pindi unapofunika jua wakati linapozama na pambizo zote zinakuwa kiza. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَالسَّمَاءِ وَمَا بَنَدَهَا ﴿٢٣﴾

“Na kwa mbingu na kwa Aliyejenga!”

Hapa kuna tafsiri mbili unaweza kusema: Naapa kwa mbingu na ujenzi wake. Au Naapa kwa mbingu na Aliyejenga. Na hii ni kauli ya Mujahid.¹ Na maana zote mbili zinakubalika, na kujenga ni kunyanyua. Kama Kauli Yake Allah تعالى:

وَالسَّمَاءِ بَنَيْنَهَا بِأَيْدِي ﴿٢٤﴾

“Na mbingu Tumezijenga kwa nguvu,..”(51:47)

Maana yake: Kwa Nguvu. Ni kama ilivyo katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَالسَّمَاءِ بَنَيْنَهَا بِأَيْدِي وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ ﴿٢٥﴾ وَالْأَرْضَ فَرَشْنَاهَا فَنِعْمَ الْمَبْهُدُونَ ﴿٢٦﴾

“Na mbingu Tumezifanya kwa Nguvu na Uweza na hakika Sisi bila ya shaka ndio Twenye Uweza wa Kuzitanua. Na ardhi Tumeitandaza; basi watandazaji wazuri namna gani Sisi!” (51:47-48)

¹ At-Tabari 24:453.

Hii ni sawa na Kauli Yake Allah تعالى:

وَالْأَرْضِ وَمَا طَحْنَهَا ﴿١٠﴾

“Na kwa ardhi na kwa Aliyeitandaza!”

Amesema Mujahid ‘Twahaha’ Ameitandika.¹ Na amesema Al Aafi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa,

وَمَا طَحْنَهَا ﴿١١﴾

“Na Aliyeitandaza.”

Maana yake: Alivyoviumba ndani yake.² Amesema Ali bin Abi Twalha kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

طَحْنَهَا ﴿١٢﴾

“Aliyezitandaza.”

Ameigawa.³ Na amesema Mujahid, Qatada, Adh- Adhahak, Ssudiy, Athaury, Abu Swaleh na ibn Zaid, ‘Twahaha’ Ameitandika.⁴

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّاهَا ﴿١٣﴾

“Na kwa nafsi na kwa Aliyeitengeneza!”

Maana yake: Ameumba hali ya kuwa sawa imenyooka juu ya umbile lililo sawasawa. Kama Alivyosema Allah تعالى:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ

“Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu Alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika Uumbaji wa Mwenyezi Mungu....” (30:30)

¹ At-tabari 24:454.

² At-Tabari 24:453.

³ At-Tabari 24:454.

⁴ At-Tabari 24:454, na Ad-Durr Al-Manthur 8:529, 530.

Na amesema Mtume ﷺ,

«كُلُّ مَوْلُودٍ يُوَلَّدُ عَلَى الْفِطْرَةِ فَأَبَوَاهُ يُهَرِّدَانِهِ أَوْ يُصَرِّغَانِهِ أَوْ يُمَجِّسَانِهِ، كَمَا تُوَلَّدُ
الْبَيْهَمَةُ بِبَيْمَةِ جُمُعَاءَ، هَلْ نُجَسُونَ فِيهَا مِنْ جَدْعَاءَ؟»

“Kila mwenye kuzaliwa, anazaliwa juu ya umbile la Uislamu. Wazazi wake humfanya awe Myahudi au Mnaswara au Mmajusi. Kama anavyozaliwa mnyama anazaliwa akiwa mnyama aliyetimia viungo vyake vyote, je mnahisi katika hao wanyama yupo anayezaliwa hali ya kuwa amekatwa viungo vyake?”

Wameithibitisha hadithi hii Bukhari na Muslim katika upokezi wa Abu Hurairah رضي الله عنه.¹ Na katika sahihi ya Muslim katika upokezi wa ‘Iyadhi bin Himar Mujashi رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ amesema,

«يَقُولُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: إِنِّي خَلَقْتُ عَبَادِي حُنَفَاءَ فَجَاءَتْهُمْ الشَّيَاطِينُ فَأَجْتَالَنَّهُمْ عَنْ
دِينِهِمْ»

“Allah تعالى Anasema, ‘Hakika! Mimi Nimewaumba waja Wangu kuwa Hunafaa (wampwekeshao Mungu), lakini mashetani wakawajia na wakawapotosha kutoka katika dini yao.”

Na Kauli Yake Allah تعالى،

﴿فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا﴾

“Kisha Akaifahamisha uovu wake na wema wake.”

Ameiongoza kwenye uovu wake na uchamungu wake. Maana: Ameibanishia kwa ajili yake kwa wale Aliowakadiria. Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما،

﴿فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا﴾

“Kisha Akaifahamisha uovu wake na wema wake.”

‘Akaifahamisha.’² ‘Ameibanishia kheri na shari’ na kama hivyo amesema Mujahid, Qatadah, Adh-Dhahak na Thaury.³

¹ Fat’hul Al-Bari 3:290, na Muslim 4:2048.

² Muslim 4:2197.

³ At-Tabari 24:454.

Na amesema Saiid Ibn Jubair, 'Ameifundisha kheri na shari.' Na amesema Ibn Zaid; 'Amejaalia ndani yake uovu wake na uzuri wake.'¹

Na amepokea Ibn Jarir رَحْمَةً اللهُ تَعَالَى kutoka kwa Abi Al A sswad Al-Adily, amesema; alimuambia Imran bin Huswain alipoyaona yale wanayoyatenda watu na wanataabika ndani yake, 'jee ni kitu ambacho kimehukumiwa juu yao na kimepitishwa kutokana na makadirio yaliyotangulia, au ni jambo lililoandikwa baada ya kufikiwa na ujumbe unaotoka kwa Mtume ﷺ kutakapokuwa na hoja dhidi yao?' Nikasema, "Bali kitu kimeshahukumiwa juu yao." Akauliza: 'Jee itakuwa hilo ni dhulma?' Akasema; "Nikafadhaika kutokana naye fadhaa kubwa sana."

Amesema: nikamuambia, "Hapana kitu chochote isipokuwa Amekiumba Naye ni Mmiliki Wake haulizwi kuhusu kile Anachokifanya na wao ndio watakaoulizwa." Akasema; 'Akunyooshee wewe Allah تَعَالَى, hakika si jambo jingine nimekuuliza ili nijaribu akili yako, hakika mtu mmoja katika kabila la Muzayna au Juhaina alimuendea Mtume ﷺ akasema, 'Eee!! Mtume ﷺ; Je Unayaonaje yale wanayofanya watu wanataabika ndani yake? Je ni jambo ambalo limehukumiwa juu yao na limepita juu yao kutokana na makadirio yaliyokwishatangulia, au ni jambo katika mambo wanayoyaelekea katika yale ambayo amewajia nayo mjumbe wao na ikatiliwa mkazo hoja kwa jambo hilo juu yao?' Akasema;

«بَلْ سَنِيَةٌ قَدْ قُضِيَ عَلَيْهِمْ»

"Bali hilo ni jambo limehukumiwa juu yao."

Akauliza; 'Basi ni kwanini watu wanatenda matendo?' Akasema:

«مَنْ كَانَ اللهُ خَلْقَهُ لِإِخْدَى الْمَرْتَلِينَ يُهَيْئُ لَهَا، وَتَصْدِيقُ ذَلِكَ فِي كِتَابِ اللهِ تَعَالَى :
﴿وَتَقْرَأُ وَمَا سَوَّاهَا ۚ قَالَتْ لَهَا جُورًا وَتَقْوَاهَا﴾»

"Yule atakayekuwa Amemuumba Yeye Allah تَعَالَى kwa moja ya daraja mbili, Atamuandaa kwa daraja hilo, na ukweli wa hilo, umo katika kitabu cha Allah تَعَالَى, 'Na kwa nafsi na kwa Aliyeitengeneza! Kisha Akaifahamisha uovu wake na wema wake.'"²

¹ At-Tabari 24:455.

² At-Tabari 24:455.

Ameipokea Ahmad na Muslim.¹

Na Kauli Yake تعالى,

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ زَكَّاهَا ﴿١﴾ وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّاهَا ﴿٢﴾

“Hakika amefanikiwa aliyeitakasa. Na hakika amekhasiri aliyeiviza.”

Inawezekana yakawa maana yake ni, ‘amefuzu yule aliyeitakasa nafsi yake.’ Maana: Kwa kumtii Allah تعالى. Kama alivyosema Qatada, ‘ameitakasa na tabia mbaya na chafu.’ Na imepokewa mfano wa hayo kutoka kwa Mujahid, Ikrimah, Saiid na Ibn Jubair.

وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّاهَا ﴿٢﴾

“Na hakika amekhasiri aliyeiviza.”

Maana yake: Aliyeifanya duni, aliyeiweka chini kwa kuiweka mbali na uongofu, mpaka ikatenda maasi na ikaacha kumtii Allah تعالى Mwenye Kushinda Mwenye Kutukuka.

Na yawezekana maana yakawa, ‘amefuzu yule ambaye Allah تعالى Ameitakasa nafsi yake na amepata hasara yule ambaye Allah تعالى Ameifanya duni nafsi yake.’ Kama alivyosema Ausi na Ali bin Abi Twalha kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.² Na amepokea Twabaran kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, amesema; alikuwa Mtume ﷺ pindi anapoisikia aya hii,

وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّاهَا ﴿٧﴾ فَأَهْمَهَا جُورَهَا وَتَقْوَاهَا ﴿٨﴾

“Na kwa nafsi na kwa Aliyeitengeneza!. Kisha Akaifahamisha uovu wake na wema wake.”

Hutulia kidogo kisha anasema;

«اللَّهُمَّ آتِ نَفْسِي تَقْوَاهَا، أَنْتَ وَلِيُّهَا وَمَوْلَاهَا، وَخَيْرُ مَنْ زَكَّاهَا»

“Eee!! Mola Wangu ipe nafsi yangu uchaji wake, Wewe ndiye Msimamizi Wake na Mtawala Wake, na Mbora wa Aliyeitakasa.”

¹ Ahmad 4:438, na Muslim 4:2041.

² At-Tabari 24:457.

Hadith nyengine ameipokea Imam Ahmad kutoka kwa Zayd bin Arqam رضي الله عنه amesema; alikuwa Mtume ﷺ akisema;

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْعَجْزِ وَالْكَسَلِ، وَالْهَرَمِ وَالْجُبْنِ وَالْبُخْلِ وَعَذَابِ الْقَبْرِ.
اللَّهُمَّ آتِ نَفْسِي تَقْوَاهَا، وَزَكَّاهَا أَنْتَ خَيْرُ مَنْ زَكَّاهَا، أَنْتَ وَلِيُّهَا وَمَوْلَاهَا. اللَّهُمَّ
إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ قَلْبٍ لَا يَخْشَعُ، وَمِنْ نَفْسٍ لَا تَشْبَعُ، وَعِلْمٍ لَا يَنْفَعُ، وَدَعْوَةٍ لَا
يُسْتَجَابُ لَهَا»

"Eee! Mola Wangu hakika mimi najilinda Kwako kutokana na kushindwa na uvivu, na ukongwe na uwoga na ubakhili na adhabu ya kaburi, Eee!! Mola Wangu ipe nafsi yangu uchaji wake, na Wewe Ndiye Mbora wa Mwenye Kuitakasa, Wewe Ndiye Msimamizi Wake na Mtawala Wake,¹ Eee!! Mola Wangu najilinda Kwako na moyo usionyenyekaa na nafsi isiyotosheka na elimu isiyo na manufaa na maombi yasiyojibiwa."

Amesema Zayd رضي الله عنه; alikuwa Mtume ﷺ akitufundisha maneno hayo na sisi tunaku fundisheni maneno hayo.² Ameipokea Muslim.³

كَذَّبَتْ ثَمُودُ بِطَغْوَاهَا ﴿١١﴾ إِذْ أُنْبِئَتْ أَشْقَاهَا ﴿١٢﴾ فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ نَاقَةَ اللَّهِ
وَسُقَيْنَهَا ﴿١٣﴾ فَكَذَّبُوهُ فَعَقَرُوهَا فَدَمْدَمَ عَلَيْهِمْ رَبُّهُم بِذُنُوبِهِمْ فَسَوَّاهَا ﴿١٤﴾ وَلَا يَخَافُ
عُقُبَهَا ﴿١٥﴾

11. Kina Thamudi wali kadhibisha kwa sababu ya upotofu wao,
12. Aliposimama muovu wao mkubwa,
13. Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu alipowaambia: Huyu ni ngamia wa Mwenyezi Mungu, muacheni anywe maji fungu lake.
14. Lakini walimkadhibisha na wakamchinja ngamia, kwa hivyo Mola wao Mlezi Aliwaangamiza kwa sababu ya dhambi zao na Akawafuta kabisa.
15. Wala Yeye haogopi matokeo yake.

¹ At-Tabarani 11:106.

² Ahmad 4:371.

³ At-Tabari 24:458.

Kukadhibisha kwa Thamud na Kuangamiizwa Kwao.

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Thamud, kwamba wao walimkadhibisha Mtume wao kwa sababu ya uwovu na upotevu wao, ameyasema hayo Mujahid, Qatada na wengineo.¹ Likawafuatishia hilo kukadhibisha katika nyoyo zao kwa yale aliyokuja nayo kwao Mjumbe wao miongoni mwa uongofu na yakini.

﴿إِذْ أَنْبَعَتْ أَشْقَاهَا﴾

“Aliposimama muovu wao mkubwa.”

Maana yake: Muovu wa kabila hilo naye ni Qudaru bin Salif ambaye alimkata miguu ngamia, naye ni Uhaimiri Thamud, naye ndiye yule aliyesema Allah تعالى kuhusu yeye,

﴿فَتَادَوْا صَاحِبَهُمْ فَتَعَاطَى فَعَقَرَ﴾

“Basi wakamuita mtu wao akaja akamchinja.” (54:29)

Na alikuwa mtu huyu ni mwenye hadhi na utukufu kwa watu wake, mwenye nasaba kubwa, kiongozi mwenye kutiiwa. Kama alivyopokea Imam Ahmad kutoka kwa Abdillahi bin Zamah رضي الله عنه, amesema; alikhutubia Mtume ﷺ na akamtaja ngamia na yule aliyemkata miguu Ngamia huyo, akasema;

﴿إِذْ أَنْبَعَتْ أَشْقَاهَا﴾ أَنْبَعَتْ لَهَا رَجُلٌ عَارِمٌ عَزِيزٌ مَنِيْعٌ فِي رَهْطِهِ مِثْلُ أَبِي زَمْعَةَ

“Basi wakamuita muovu wao mkubwa; mtu aliyekuwa shupavu, mwenye ubora kwa watu, mwenye nguvu katika kundi lake, kama vile Abu Zam’ah.”¹

Hadithi hii imeandikwa na Bukhari katika mlango wa tafsiri na Muslim katika mlango wa sifa za moto, na At-Tirmidh na An-Nasai katika mlango wa tafsiri katika “Sunan zao” za vitabu vya Hadithi.²

¹ Ahmad 4:17.

² Fat’hul Al-Bari 8:575, Muslim 4:2191, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:268, na An-Nasai katika Al-Kubra 6:515.

Kisa cha Ngamia wa Swaleh.

Kauli Yake Allah تعالى،

فَقَالَ هُمْ رَسُولُ اللَّهِ

“Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu alipowaambia...”

نَاقَةَ اللَّهِ

“...huyu ni ngamia wa Mwenyezi Mungu,..”

Anamkusudia Swaleh عليه السلام. Maana yake: Mtahadharini Ngamia wa Allah تعالى kumgusa kwa ubaya wowote.

وَسُقَيْنَهَا

“Muacheni anywe maji fungu lake.”

Maana yake: Msimfanyie uadui katika kinywaji chake, kwani yeye ana haki kunywa siku moja na mna haki nyinyi ya kunywa siku moja yenye kujulikana. Amesema Allah تعالى،

فَكَذَّبُوهُ فَعَقَرُوهَا

“Lakini walimkadhibisha na wakamchinja ngamia,..”

Maana yake: Walimkadhibisha katika lile ambalo alilowajia nalo, likawafuatishia hilo kumkata miguu ngamia ambaye Alimtoa Allah تعالى katika jiwe hali ya kuwa ni ishara na hoja juu yao,

فَدَمَدَمَ عَلَيْهِمْ رَبُّهُمْ بِذُنُوبِهِمْ

“...kwa hivyo Mola wao Mlezi Aliwaangamiza kwa sababu ya dhambi zao na Akawafuta kabisa.”

Maana yake: Allah تعالى Alighadhibika juu yao Akawaangamiza.

فَسَوَّاهَا

“...na Akawafuta kabisa.” Maana yake: Akaifanya adhabu yenye kuwashukia juu ya usawa.

¹ Fat'hul Al-Bari 8:575, Muslim 4:2191, Tuhtat Al-Ahwadhi 9:268, na An-Nasai katika Al-Kubra 6:515.

Amesema Qatada رضي الله عنه; imetufikia kwamba Uhaimiri wa Thamud hakumkata ngamia miguu mpaka, walipomfuata wadogo wao na wakubwa wao na wanaume wao na wanawake wao. Waliposhirikiana watu wote katika kumkata miguu, Aliimimina Allah تعالى adhabu juu yao Akaifanya sawa.¹

Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَلَا يَخَافُ

“Wala Yeye haogopi.”

Na pamesomwa.

(فَلَا يَخَافُ)

“Hivyo, haogopi...”

عُقِبَهَا

“Matokeo yake.”

Maana yake: Haiogopwi, (mwisho wake). Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما, Haogopi Mwenyezi Mungu lawama toka kwa yeyote.²

Na kama hivyo amesema Mujahid, Hassan na Bakri bin Abdillahi Muzani na wengine.³

Huu ni mwisho wa tafsiri ya *Suratu Ash-Shams* na ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹ At-Tabari 24:460.

² At-Tabari 24:416.

³ At-Tabari 24:461.

Tafsiri ya Suratul Layl Sura ya 92 Iliteremshwa Makkah

Usomaji wa Suratul Layl katika Sala ya 'Ishaa Imetangulia Kauli yake Mtume

ﷺ kwa Muadh رضي الله عنه,

«فَهَلَّا صَلَّيْتَ بِرَبِّكَ الْأَعْلَىٰ ﴿١﴾ وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا ﴿٢﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا يَنشَقُّ ﴿٣﴾»

"Kwa nini usingesali kwa kusoma 'sabi hisma rabbika Al aala' 'wasshamsi wa dhuhaha' wallayl idhaa yaghshaa"¹

* * *

¹ Fat'hul Al-Bari 2:234 na Muslim 1:340.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُوْرَةُ اللَّيْلِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَى ﴿١﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّى ﴿٢﴾ وَمَا خَلَقَ
 الذَّكَرَ وَالْأُنثَى ﴿٣﴾ إِنَّ سَعْيَكُمْ لَشَتَّى ﴿٤﴾ فَأَمَّا مَنْ
 أَعْطَى وَاتَّقَى ﴿٥﴾ وَصَدَقَ بِالْحُسْنَى ﴿٦﴾ فَسَنِيبُهُ
 لِلْعُسْرَى ﴿٧﴾ وَأَمَّا مَنْ بَخِلَ وَاسْتَغْنَى ﴿٨﴾ وَكَذَّبَ
 بِالْحُسْنَى ﴿٩﴾ فَسَنِيبُهُ لِلْعُسْرَى ﴿١٠﴾ وَمَا يُغْنِي عَنْهُ
 مَالُهُ إِذَا تَرَدَّى ﴿١١﴾ إِنَّ عَلَيْنَا لَلْهُدَى ﴿١٢﴾ وَإِنَّ لَنَا
 لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَى ﴿١٣﴾ فَأَنْذَرْتُمْ كُرْهًا نَارًا تَلْفَطْنَ ﴿١٤﴾ لَّا
 يَصْلِيهَا إِلَّا الْأَشْقَى ﴿١٥﴾ الَّذِي كَذَّبَ وَتَوَلَّى ﴿١٦﴾
 وَسَيُجَنَّبُهَا الْأَتْقَى ﴿١٧﴾ الَّذِي يُؤْتِي مَالَهُ يَتَزَكَّى ﴿١٨﴾
 وَمَا لِأَحَدٍ عِنْدَهُ مِنْ نِعْمَةٍ تُجْزَى ﴿١٩﴾ إِلَّا أَتْبَعَاءَ وَجْهِ
 رَبِّهِ الْأَعْلَى ﴿٢٠﴾ وَلَسَوْفَ يَرْضَى ﴿٢١﴾

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَى ﴿١﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا
 تَجَلَّى ﴿٢﴾ وَمَا خَلَقَ الذَّكَرَ وَالْأُنثَى
 ﴿٣﴾ إِنَّ سَعْيَكُمْ لَشَتَّى ﴿٤﴾ فَأَمَّا
 مَنْ أَعْطَى وَاتَّقَى ﴿٥﴾ وَصَدَقَ
 بِالْحُسْنَى ﴿٦﴾ فَسَنِيبُهُ لِلْعُسْرَى
 ﴿٧﴾ وَأَمَّا مَنْ بَخِلَ وَاسْتَغْنَى ﴿٨﴾
 وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَى ﴿٩﴾ فَسَنِيبُهُ
 لِلْعُسْرَى ﴿١٠﴾ وَمَا يُغْنِي عَنْهُ
 مَالُهُ إِذَا تَرَدَّى ﴿١١﴾

1. Naapa kwa usiku unapofunika!
2. Na mchana unapodhihiri!
3. Na kwa Aliyeumba dume na jike!
4. Hakika juhudi na amali zenu ni zenye kutofautiana.

5. Ama mwenye kutoa na akamchamngu.

6. Na akaliwafiki lilio jema.

7. Tutamfanyia yeye yawe mepesi.

8. Na ama mwenye kufanya ubakhili, na asiwe na haja ya wenzake.

9. *Na akakanusha lilio jema.*

10. *Tutamfanyia yeye yawe mazito!*

11. *Na mali yake yatamfaa nini atapokuwa anadidimia?*

Kiapo Juu ya Kutofautiana kwa Watu Katika Juhudi Zao na Kutanabahisha Juu ya Matokeo Tofauti ya Juhudi Hizo.

Allah تعالیٰ Ameapa,

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ

“Naapa kwa usiku unapofunika!” Maana yake: Unapovifunika viumbe kwa kiza chake.

وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّىٰ

“Na mchana unapodhihiri!” Maana yake: Kwa mwangaza wake na kwa kuangaza kwake.

وَمَا خَلَقَ الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ

“Na kwa Aliyeumba dume na jike!” Maneno hayo ni kama Kauli Yake Allah تعالیٰ:

وَخَلَقْنَاكُمْ أَزْوَاجًا

“Na Tukakuumbeni kwa jozi?” (78:8)

Na ni Kama Kauli Yake Allah تعالیٰ,

وَمِنْ كُلِّ شَيْءٍ خَلَقْنَا زَوْجَيْنِ

“Na katika kila kitu Tumeumba kwa jozi ili mzingatie.” (51:49)

Na kulipokuwa Tukiviapia hivi vitu vyenye kutofautiana imekuwa chenye kuapiwa pia ni chenye kutofautiana vilevile. Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالیٰ:

إِنَّ سَعْيَكُمْ لَشَتَّىٰ

“Hakika juhudi na amali zenu ni zenye kutofautiana.”

Maana yake: Matendo ya waja ambayo wameyachuma ni yenye kutofautiana vilevile; na ni yenye kupingana kwani kuna mwenye kufanya kheri na kuna mwenye kufanya shari. Amesema Allah تعالیٰ,

فَأَمَّا مَنْ أُعْطِيَ وَاتَّقَى ﴿٦﴾

“Ama mwenye kutoa na akamcha mungu.” Maana yake: Atakayetoa kile alichomrisha kukitoa na akamcha Allah تعالى katika mambo hayo,

وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَى ﴿٦﴾

“Na akaliwafiki lilio jema.” Maana yake: Akasadikisha malipo juu ya matendo hayo, amesema hayo Qatada¹ na amesema Khusayfu Said.

Na Kauli Yake Allah تعالى,

فَسَنِّيْبِرُهُ لِلْيُسْرَى ﴿٧﴾

“Tutamfanyia yeye yawe mepesi.” Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, Anakusudia kheri.² Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى;

وَأَمَّا مَنْ يَخِلْ

“Na ama mwenye kufanya ubakhili,..” Maana: Kwa kile alichonacho.

وَأَسْتَفْتَى ﴿٧﴾

“Na asiwe na haja ya wenzake.” Amesema Ikrimah kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما ina maana; atakayefanya ubakhili kwa mali yake na akajitosha na Bwana Wake Mwenye Kushinda Mwenye Kutukuka.³ Ameyapokea hayo Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى

وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَى ﴿٧﴾

“Na akakanusha lilio jema.” Maana yake: Malipo katika nyumba ya akhera.

فَسَنِّيْبِرُهُ لِلْعُسْرَى ﴿٨﴾

“Tutamfanyia yeye yawe mazito!” Maana yake: Kwa njia ya shari kama Alivyosema Allah تعالى,

وَنُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَرَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَنَنذُرُهُمْ فِي طَغْيِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٨﴾

“Nasi Twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza, Tunawaacha katika maasi yao wakitangatanga.” (6:110)

¹ At-Tabari 24:470.

² Ad-Durr Al-Manthur 8:535.

³ At-Tabari 24:472.

Na aya katika maudhui hii ziko nyingi sana zinafahamisha juu ya kuwa Allah تعالی Mwenye Kushinda na Kutukuka Atamlipa mwenye kukusudia kheri kwa Kumuezesha, na mwenye kukusudia shari kwa Kumnyima, na yote hayo ni kwa makadirio yaliyokadiriwa. Aidha hadithi zenye kufahamisha juu ya maana hiyo ni nyingi.

Upokezi wa Abubakr Swiddiq رضي الله عنه.

Ameipokea Imam Ahmad kutoka kwa Abubakr رضي الله عنه amesema nilimuuliza Mtume ﷺ, 'Je tunatenda juu ya yale yaliyokwishamalizwa au juu ya yale yaliyoanza?' Akasema,

«بَلِّ عَلَى أَمْرٍ قَدْ فُرِغَ مِنْهُ»

"Bali juu ya jambo lilomalizwa katika hilo."

Nikauliza; 'Basi ni kwa nini kutenda?' 'Mtume ﷺ akasema,

«كُلُّ مُبَسَّرٍ لِمَا خُلِقَ لَهُ»

"Kila mmoja amerahisishwa kwa lile aliloumbiwa." ¹

Upokezi wa Ali رضي الله عنه,

Imamu Bukhari pia amenukuu masimulizi sawa na haya kutoka kwa 'Ali bin Abu Twalib رضي الله عنه ambapo amesema: "Tulikuwa mazikoni katika makaburi ya Al-Baqi Al-Gharqad, alipokuja Mtume ﷺ na akaketi. Nasi tukaja na kuketi kwa kumzunguka. Naye alikuwa ameshika fimbo. Aliinamisha kichwa na akawa anakwangua chini kwa fimbo yake, akasema,

«مَا بَيْنَكُمْ مِنْ أَحَدٍ - أَوْ مَا مِنْ نَفْسٍ مَنُوقَسَةٍ - إِلَّا كُتِبَ مَكَانُهَا مِنَ الْجَنَّةِ وَالنَّارِ،
وَأَلَّا قَدْ كُتِبَتْ شَقِيَّةٌ أَوْ سَعِيدَةٌ»

"Hapana yeyote miongoni mwenu, au hakuna nafsi yoyote iliyoumbwa, isipokuwea sehemu yake Peponi au Motoni imeandikwa, na imeandikwa kuwa ni mbaya au ya furaha."

Mtu mmoja akauliza, "Ewe Mtume! Je, tutegemee kilichoandikwa na tuache kufanya amali? Kwani kila mmoja wetu ambaye ni mtu wa furaha, basi atakuwa

¹ Ahmad 1:5. sawa. Isnadi yake ni dhaifu.

ni mtu wa furaha, na atakayekuwa miongoni mwa watu wa mabaya, basi atakuwa katika watu wa mabaya." Mtume ﷺ akamjibu,

وَأَمَّا أَهْلُ السَّعَادَةِ فَيَسْرُونَ لِعَمَلِ أَهْلِ السَّعَادَةِ، وَأَمَّا أَهْلُ الشَّقَاءِ فَيَسْرُونَ إِلَى
عَمَلِ أَهْلِ الشَّقَاءِ، ثُمَّ قَرَأَ:

"Watu ambao ni wa wema watarahisishiwa kufanya amali za watu wa wema, na watu wa mabaya watarahisishiwa kutenda amali za watu wabaya." Kisha akasoma Aya ifuatayo:

فَأَمَّا مَنْ أَعْطَى وَاتَّقَى ۝ وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَى ۝ فَسَنِيَرُهُ لِلْيُسْرَى ۝ وَأَمَّا مَنْ
خَبِلَ وَأَسْتَعْفَى ۝ وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَى ۝ فَسَنِيَرُهُ لِلْعُسْرَى ۝

"Ama mwenye kutoa na akamchamungu, na akaliwafiki lilio jema, Tutamsahilishia yawe mepesi. Na ama mwenye kufanya ubakhili, na asiwe na haja ya wenzake, na akakanusha lilio jema, Tutamsahilishia yawe mazito!"¹

Wameisimulia Hadithi wapokezi² wengine.

Upokezi wa Abdillah Bin Umar رضي الله عنه.

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما amesema: Umar رضي الله عنه amesema; 'Ewe!! Mtume, Jee unayaonaje yale tunayoyatenda jee ni katika mambo ambayo tayari yamekamiliwa au yanayoanzwa kuzushwa upya?' Akasema

«فِيمَا قَدْ فُرِغَ مِنْهُ، فَاعْمَلْ يَا ابْنَ الْخَطَّابِ، فَإِنَّ كُلَّ مَيْسِرٍ، أَمَا مَنْ كَانَ مِنْ أَهْلِ
السَّعَادَةِ فَإِنَّهُ يَعْمَلُ لِلْسَّعَادَةِ، وَأَمَّا مَنْ كَانَ مِنْ أَهْلِ الشَّقَاءِ فَإِنَّهُ يَعْمَلُ لِلشَّقَاءِ»

"Katika yaliyokwisha kumaliziwa. Kwa hiyo ewe Ibn Khattab kwani hakika kila mmoja amerahisishiwa, ama atakapokuwa ni katika watu wema hakika yeye atatenda matendo ya watu wema, ama atakapokuwa ni katika watu waovu; hakika yeye atatenda matendo ya watu waovu."³

¹ Fat'hul Al-Bari 8:579.

² Muslim no. 2039, 2040, Abu Dawud 5:68, Tuhfat Al-Ahwadhi 6:340, na 9:270, An-Nasai katika Al-Kubra 6:516, 517, na Ibn Majah 1:30.

³ Ahmad 2:52.

Amepokea Atirmidhy katika *Al Qadar* na amesema ni Hassan Sahihi:¹

Hadithi Nyingine kutoka kwa Jabir رضي الله عنه.

Amepokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Jabir bin Abdillahi رضي الله عنه kwamba yeye amesema; 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu jee tunatenda kwa jambo ambalo tayari limeshakamilishwa au jambo tunalolianza upya?' Akasema Mtume ﷺ, "Mnatenda kwa jambo lilokuwa limeshakamilishwa."

«الْأَمْرُ قَدْ فُرِغَ مِنْهُ»

"Ni jambo lililokwishamalizwa."

Akasema Suraqa; 'Kama ndio hivyo basi ni kwa sababu gani tunatenda?' Akasema Mtume ﷺ,

«كُلُّ غَامِلٍ مُبْتَرٌ لِعَمَلِهِ»

*"Kila mtendaji amerahisishiwa kwa matendo yake."*²

Ameipokea Muslim.³

Amepokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Amir bin Abdillahi bin Zubair amesema; alikuwa Abubakr رضي الله عنه anawaacha huru watumwa kwa sababu ya Uislamu pale Makkah, akawa anawaacha huru vikongwe na wanawake pindi wanapoinjia katika Uislamu. Baba yake akamuambia: 'Ewe kijana wangu ninakuona unawaacha huru watu wanyonge, lau wewe ungewaacha huru wanaume wenye nguvu wangesimama pamoja na wewe na wangekusaidia na wangekulinda na matatizo na shari mbalimbali.' Akasema, 'Ewe!! Baba yangu hakika si vingine nadhani; alisema; ninayataka yale yaliyo kwa Allah تعالى.' Amesema; 'wakawazungumzia watu wa nyumbani kwangu kwamba aya hii iliteremshwa kwa Abubakr رضي الله عنه,

فَأَمَّا مَنْ أَعْطَىٰ وَاتَّقَىٰ ﴿١﴾ وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَىٰ ﴿٢﴾ فَسَنِّيَرُهُدٍ لِّلْيُسْرَىٰ ﴿٣﴾

"Ama mwenye kutoa na akamchamungu, na akaliwafiki lilio jema, Tutamsahilishia yawe mepesi."⁴

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 6:339.

² At-Tabari 24:475.

³ Muslim 4:2041.

⁴ At-Tabari 24:473.

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّى ﴿١٢﴾

“Na mali yake yatamfaa nini atapokuwa anadidimia?”

Amesema Mujahid, atakapokufa.¹ Na amesema Abu Swaleh na Malik kutoka kwa Zaid bin Aslam: ‘atakapoporomoka katika moto.’²

إِنَّ عَلَيْنَا لَلْهُدَىٰ ﴿١٢﴾ وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَىٰ ﴿١٣﴾ فَأَنْذَرْتُكُمْ نَارًا تَلَظَىٰ ﴿١٤﴾ لَا يَصْلَاهَا إِلَّا الْأَشْقَى ﴿١٥﴾ الَّذِي كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿١٦﴾ وَسَيَجْزِيهَا الْآتَىٰ ﴿١٧﴾ الَّذِي يُؤْتِي مَالَهُ يَتَزَكَّىٰ ﴿١٨﴾ وَمَا لِأَحَدٍ عِنْدَهُ مِنْ نِعْمَةٍ تُجْزَىٰ ﴿١٩﴾ إِلَّا ابْتِغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِ الْأَعْلَىٰ ﴿٢٠﴾ وَلَسَوْفَ يَرْضَىٰ ﴿٢١﴾

12. Hakika ni juu Yetu kuonesha uwongofu.

13. Na hakika ni Yetu Sisi Akhera na dunia.

14. Basi Nakuonyeni na Moto unaowaka!

15. Hatauingia ila muovu kabisa!

16. Anayekadhibisha na kuipa mgongo.

17. Na mchamungu ataepushwa nao,

18. Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa.

19. Na wala si kwa kuwa yupo yeyote aliyemfanyia hisani ndio anamlipa.

20. Ila ni kutaka radhi ya Mola Wake Mlezi Aliye Juu Kabisa.

21. Naye atakuja ridhika!

¹ At-Tabari 24:476.

² At-Tabari 24:476, na Al-Qurtubi 20/85.

Uongofu na Mambo Mengine Vimo Mikononi mwa Allah تعالی. Na Allah تعالی Anatoa Onyo Kuhusu Jahannam.

Amesema Qatada,

إِنَّ عَلَيْنَا لَلْهُدَىٰ

“Hakika ni juu Yetu Kuonesha uwongofu.”

Maana yake: ‘Tunabainisha halali na haramu.’¹ Wengine wamesema kuwa inamaanisha kwa kufuata njia ya uongofu atafika kwa Allah تعالی. Na ameifanya aya hiyo kama Kauli Yake Allah تعالی,

وَعَلَىٰ اللَّهِ فَصْدُ السَّبِيلِ

“Na ni juu ya Mwenyezi Mungu kuelekeza Njia.” (16:9)

Ameyasema hayo Ibn Jarir رحمه الله تعالی.² Na Kauli Yake Allah تعالی,

وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَىٰ

“Na hakika ni Yetu Sisi Akhera na dunia.”

Maana yake: Vyote hivyo ni Miliki Yetu na Mimi Ndiye Ninayefanya Nitakavyo katika dunia na akhera. Na Kauli Yake Allah تعالی.

فَأَنْذَرْتُكُمْ نَارًا تَلَظَّىٰ

“Basi Nakuonyeni na Moto unao waka!”

Mujahid amesema: Ina maana; wenye kuwaka.³ Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Simak bin Harb nilimsikia An- Nuuman bin Bashir رضي الله عنه akitoa khutuba akisema nimemsikia Mtume ﷺ akiwa anahutubia akisema,

«أَنْذَرْتُكُمْ النَّارَ»

“Ninawakhofisheni na moto.” Mpaka lau kwamba mtu aliyekua sokoni angemsikia mahali alipokuwa amesema. Alizungumza maneno haya mpaka kilianguka miguuni pake kishali kilichokuwa begani mwake.⁴ Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Aby Ishaq nimemsikia An-Nuumani bin Bashir akitoa khutba akiwa anasema; nilimsikia Mtume ﷺ akiwa anasema:

¹ At-Tabari 24:477.

² At-Tabari 24:477.

³ At-Tabari 24:477.

⁴ Ahmad 4:272.

«إِنَّ أَهْوَنَ أَهْلِ النَّارِ عَذَابًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ رَجُلٌ تَوَضَّعَ فِي أَحْمَصِ قَدَمَيْهِ جَمْرَتَانِ يَغْلِي
مِنْهُمَا دِمَاعُهُ»

“Hakika mwepesi wa watu wa motoni kwa adhabu siku ya kiyama, ni mtu ambaye yatawekwa katika nyayo za miguu yake, makaa mawili, utachemka kutokana na makaa hayo ubongo wake.”¹

Ameipokea Bukhari.² Na amepokea Muslim kutoka kwa Abi Ishaqa kutoka kwa An-Numan bin Bashir رضي الله عنه amesema. Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ أَهْوَنَ أَهْلِ النَّارِ عَذَابًا مَنْ لَهُ نَعْلَانِ وَشِرَاكَانِ مِنْ نَارٍ يَغْلِي مِنْهُمَا دِمَاعُهُ كَمَا
يَغْلِي الْمُرْجُلُ، مَا يَرَى أَنَّ أَحَدًا أَشَدُّ مِنْهُ عَذَابًا، وَإِنَّهُ لَأَهْوَنُهُمْ عَذَابًا»

“Hakika mwepesi wa watu wa motoni kwa adhabu, ni yule mwenye viatu viwili na kamba mbili za viatu vya moto, utachemka kutokana na viwili hivi, ubongo wake, kama kinavyochemka chungu, hataona kuwa kuna mtu yoyote mwenye adhabu kubwa kuliko yeye na hakika yeye, ni mwepesi kwa watu wote kwa adhabu.”³

Na Kauli Yake Allah تعالى:

لَا يَصْلَحَنَّ إِلَّا الْأَشَقَى ﴿٥٠﴾

“Hatauingia ila muovu kabisa.” Maana yake: Muovu. Kisha Akamuweka wazi kwa Kusema;

الَّذِي كَذَّبَ

“Anayekadhibisha.” Kwa moyo wake,

وَتَوَلَّى ﴿٥١﴾

“Na kuipa mgongo.” Maana yake: Kutenda kwa viungo vyake.

Ameipokea Imam Ahmad kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه amesema; amesema Mtume ﷺ,

«كُلُّ أُمَّتِي يَدْخُلُ الْجَنَّةَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِلَّا مَنْ أَبَى»

“Umati wangu wote wataingia peponi isipokuwa yule atakayekataa.”

¹ Ahmad 4/274.

²Fat’hul Bari 424.

³Muslim 1/196.

Wakasema, 'Ni nani atakayekataa Ewe Mtume?' Akasema,

مَنْ أَطَاعَنِي دَخَلَ الْجَنَّةَ، وَمَنْ عَصَانِي فَقَدْ أَبَىٰ

*"Atakayenitii mimi ataingia peponi na atakayeniasi kwa hakika huyo amekataa."*¹

Ameipokea Bukhari.²

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَسَيُجَنَّبُهَا الْأَتْقَى

"Na mchamungu ataepushwa nao."

Maana yake: Ataepushwa na moto mtu mchaji aliyesafika. Kisha akamfasiri kwa kusema:

الَّذِي يُؤْتِي مَالَهُ يَتَزَكَّىٰ

"Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa."

Maana yake: anatoa mali yake katika kumtii Mola Wake, na anaitakasa nafsi yake na mali yake na kile Alichompa Allah تعالى miongoni mwa Dini na dunia.

وَمَا لِأَحَدٍ عِنْدَهُ مِنْ نِعْمَةٍ تُجْزَىٰ

"Na wala si kwa kuwa yupo yeyote aliyemfanyia hisani ndio anamlipa."

Maana yake: Hakukuwa kutoa kwake mali yake, ni katika kulipana na yule aliyempa huo wema. Kwa hiyo akawa anatoa mali yake katika kumlipa huyo aliyemfanyia wema. La hasha hafanyi hayo kwa sababu hiyo, hapana jambo jingine linalomsukuma kufanya hivyo.

إِلَّا ابْتِغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِ الْأَعْلَىٰ

"Ila ni kutaka radhi ya Mola Wake Mlezi Aliye juu kabisa."

Maana yake: Kwa kutamani katika kutoa kwake huko kumuona Mola Wake katika nyumba ya akhera, katika mabustani ya pepo. Allah تعالى Amesema,.

¹ Ahmad 2:361.

² Fat'hul Al-Bari 13:263.

وَلَسَوْفَ يَرْضَىٰ ﴿١١﴾

“Naye atakuja ridhika!”

Punde hivi ataridhia huyo aliyesifika na sifa hizi.

Sababu ya Kushuka Aya Hizi na Ubora wa Abubakar رضي الله عنه.

Wafasiri wengi wametaja kwamba aya hizi zimeshuka kwa Abubakar رضي الله عنه. Mpaka baadhi yao wamesimulia “*Ijmai*” makubaliano ya Wafasiri juu ya sababu hiyo. Hapana shaka kwamba yeye anahusika na jambo hilo, na umma wote. Kwani andiko limekuja kwa kujumuisha watu wote.

Nalo ni Kauli Yake Allah تعالى،

وَسَيُجَنَّبُهَا الْأَتْقَى ﴿١٧﴾ الَّذِي يُؤْتِي مَالَهُ يَتَزَكَّى ﴿١٨﴾ وَمَا لِأَحَدٍ عِنْدَهُ مِنْ نِعْمَةٍ تُجْزَىٰ ﴿١٩﴾

“Na mchamungu ataepushwa nao. Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa. Na wala si kwa kuwa yupo yeyote aliyemfanyia hisani ndio anamlipa.”

Isipokuwa ni kwamba Abubakar رضي الله عنه ni mtangulizwa mbele na amewashinda watu wengi katika sifa zote njema. Kwani yeye alikuwa mkweli, alikuwa mchaji, alikuwa mkarimu, mtoaji mali zake katika kumtii Allah تعالى na katika kumnusuru Mjumbe Wake ﷺ.

Ni Dirham na Dinar ngapi alizozitoa kwa kutaka Dhati ya Bwana Wake Mtukufu? Na hakuhitaji kwa mtu yeyote miongoni mwa watu aliyowaacha huru kumlipa kwa sababu ya kufanya hivyo? Isipokuwa ni kwamba ubora na wema wake ulikuwa juu zaidi ya wengi watukufu na viongozi wa Makkah.

Na kwa sababu hiyo amesema Ur’wa Ibn Masoud na yeye ni mtukufu wa kabila la Thakif, siku za mkataba wa Hudaibiya – Alimuambia Abubakar رضي الله عنه, ‘ama naapa kwa Allah تعالى lau kama si msaada wako ulionisaidia ambao bado sijakulipa ningekuitikia.’

Na alikuwa Abubakar رضي الله عنه amemshambulia kwa maneno. Ikiwa hii ndio hali yake kwa mabwana wa waarabu na viongozi wao wa makabila; vipi itakuwa hali kwa watu wengine. Na kwa sababu hiyo, Allah تعالى Amesema,

وَمَا لِأَحَدٍ عِنْدَهُ مِنْ نِعْمَةٍ تُجْزَىٰ إِلَّا أَتْبَغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِ الْأَعْلَىٰ ﴿٧٦﴾ وَلَسَوْفَ يَرْضَىٰ ﴿٧٧﴾

“Na wala si kwa kuwa yupo yeyote aliyemfanyia hisani ndio anamlipa. Ila ni kutaka radhi ya Mola Wake Mlezi Aliye juu kabisa. Naye atakuja ridhika!”

Na Imekuja katika sahihi mbili kwamba Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ أَنْفَقَ زَوْجَيْنِ فِي سَبِيلِ اللَّهِ دَعَتْهُ خَزَنَةُ الْجَنَّةِ يَاعْبُدَ اللَّهَ، هَذَا خَيْرٌ»

“Mwenye kutoa jozi mbili katika njia ya Mwenyezi Mungu watamuita walinzi wa peponi mja wa Mwenyezi Mungu - hii ni kheri,”

Abubakar رضي الله عنه akasema, “Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu pana udharura wowote kwa yule atakayeitwa katika mlango mmoja wa pepo, kama hakuitwa katika milango mingine, kwa kuwa lengo la kuingia peponi limeshapatikana?” Mtume ﷺ akasema,

«نَعَمْ ، وَأَزْجُو أَنْ تَكُونَ مِنْهُمْ»

“Ndio na ninatarajia kuwa wewe utakuwa miongoni mwao.”¹

Ufafanuzi wa swali la Abubakar رضي الله عنه ni kwamba alimuuliza Mtume ﷺ, ‘wakati mwingine kufuatana na matendo ya mtu, huenda akaitwa kuingia peponi kupitia milango mingi, je iwapo ataingia kupitia mlango mmoja, si itakuwa inatosheleza, na wala hakuna haja ya kuitikia maombi ya kila mlango?’ Hapo ndio Mtume ﷺ akasema, ‘ndio’. Kwa kuwa lengo la kuingia peponi limeshapatikana hakuna haja ya kuuitikia kila mlango.

Huu ni mwisho wa tafsiri ya *Suratu Al-Layl*. Na ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹Fat’hul Al-Bari 7:23 na Muslim 2:712

Tafsiri ya Suratu Dhuha Sura ya 93 Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الدُّهُحِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالضُّحَىٰ ﴿١﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٢﴾ مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ﴿٣﴾
وَلَلْآخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَىٰ ﴿٤﴾ وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ﴿٥﴾
أَلَمْ يَجِدَكَ يَتِيمًا فَفَآوَىٰ ﴿٦﴾ وَوَجَدَكَ ضَالًّا فَهَدَىٰ ﴿٧﴾
وَوَجَدَكَ عَابِلًا فَأَغْنَىٰ ﴿٨﴾ فَأَمَّا الْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ ﴿٩﴾ وَأَمَّا السَّائِلَ فَلَا تَنْهَرْ ﴿١٠﴾
وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ﴿١١﴾

وَالضُّحَىٰ ﴿١﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٢﴾ مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ﴿٣﴾
وَلَلْآخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَىٰ ﴿٤﴾ وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ﴿٥﴾
أَلَمْ يَجِدَكَ يَتِيمًا فَفَآوَىٰ ﴿٦﴾ وَوَجَدَكَ ضَالًّا فَهَدَىٰ ﴿٧﴾
وَوَجَدَكَ عَابِلًا فَأَغْنَىٰ ﴿٨﴾ فَأَمَّا الْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ ﴿٩﴾ وَأَمَّا السَّائِلَ
فَلَا تَنْهَرْ ﴿١٠﴾ وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ﴿١١﴾

1. Naapa kwa mchana!
2. Na kwa usiku unapo tanda!
3. Mola Wako Mlezi Haku kuacha, wala Hakukasirika nawe.
4. Na bila ya shaka Akhera ni bora kwako kuliko ulimwengu.
5. Na Mola Wako Mlezi Atakupa mpaka uridhike.
6. Kwani Hakukukuta yatima Akakupa makaazi?
7. Na Akakukuta umepotea Akakuongoa?

8. Akakukuta mhitaji Akakutosheleza?

9. Basi yatima usimuonee!

10. Na anayeomba au kuuliza usimkaripie!

11. Na neema za Mola Wako Mlezi zisimulie.

Sababu ya Kushuka Surat Adh-Dhuhaa.

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Junayb amesema: aliumwa Mtume ﷺ hakusimama kwa muda wa usiku mmoja au usiku miwili akaja mwanamke mmoja akasema, 'Muhamad simuoni shetani wako isipokuwa amekuacha.' Akateremsha Allah تعالى Mwenye Kushinda na Kutukuka,

وَالضُّحَىٰ ۝ وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ۝ مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ۝

"Naapa kwa mchana! Na kwa usiku unapotanda! Mola Wako Mlezi Hakukuacha, wala Hakukasirika nawe."¹

Ameipokea Bukhari, Muslim, Atirmidhiy, Annasai, Ibn Abi Hatim na Ibn Jabir² kutoka kwa Jundabi ambaye ni Ibn Abdallah Bajali Al-Aqali.

Na katika upokezi mwingine wa kutoka kwa Al-Aswaa bin Qais amesema nilimsikia Jundabi akisema alichelewa Jibril عليه السلام kuja kwa Mtume ﷺ wakasema washirikina; 'Muhammad ameachana na Mola Wake Mlezi.'

Hivyo, Akateremsha Allah تعالى.

وَالضُّحَىٰ ۝ وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ۝ مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ۝

"Naapa kwa mchana! Na kwa usiku unapotanda! Mola Wako Mlezi Hakukuacha, wala Hakukasirika nawe."³

¹ Ahmad 4:312.

² Fat'h ul Al-Bari 3:11, na 8:580, 581, 619, na Muslim 3:1421, 1422, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:272, An-Nasai katika Al-kubra 6:517, na At-Tabari 24:485, 486.

³ At-Tabari 24:486.

وَالضُّحَىٰ ﴿١﴾ وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٢﴾

“Naapa kwa mchana! Na kwa usiku unapotanda!”

Aufi amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, ilipotaremka kwa Mtume ﷺ Qur'an, alichelewa Jibril عليه السلام kushuka nayo siku kadhaa, jambo hilo likaleta simanzi kwa Mtume ﷺ.

Hivyo wakasema washirikina; ‘Amemuacha Mola Wake na Amemchukia.’ Akateremsha Allah تعالى,

مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ﴿٣﴾

“Mola Wako Mlezi Hakukuacha, wala Hakukasirika nawe.”¹

Na hiki ni kiapo kutoka Kwake Allah تعالى kwa wakati wa *Dhuhaa* na yale yaliyofanywa ndani yake miongoni mwa mwangaza,

وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٤﴾

“Na kwa usiku unapotanda!”

Maana yake: Unapotulizana na ukafunga kiza na ukawa mweusi sana. Ameyasema hayo Mujahid, Qatada, Adh-Dhahak, Ibn Zaid na wengine.

Na hiyo ni dalili ya wazi juu ya kuwepo kwa Muumba wa haya. Kama Alivyosema Allah تعالى,

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿٥﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَافَىٰ ﴿٦﴾

“Naapa kwa mchana! Na kwa usiku unapotanda!”

Kisha Amesema Allah تعالى,

فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا ۚ ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٧﴾

“Ndiye Anayepambazua mwangaza wa asubuhi; na Ameufanya usiku kuwa mapumziko na utulivu, na jua na mwezi kwenda kwa hisabu. Hayo ndiyo makadirio ya Aliyetukuka Mwenye Nguvu, Mwenye Ujuzi.” (6:96)

¹ At-Tabari 24:484, na Al-Qurtubi 20:91.

مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ

“Mola wako Mlezi Hakukuacha.” Maana yake: Hakukuacha

وَمَا قَلَىٰ

“Wala Hakukasirika nawe.” Maana yake: Hakukuchukia.

Akhera ni Bora Kuliko Dunia.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَلَلْآخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَىٰ

“Na bila ya shaka Akhera ni bora kwako kuliko ulimwengu.”

Maana yake: Kwa hakika nyumba ya Akhera ni bora kwako kuliko nyumba hii na kwa sababu hiyo alikuwa Mtume ﷺ ni mpaji kuliko watu wote katika Dunia na mkubwa wao zaidi katika kuitupa Dunia kama ambavyo hilo linaeleweka kwa dhamira katika sira yake Mtume ﷺ. Na alipokhiyarishwa Mtume ﷺ mwishoni mwa umri wake kati ya kukaa muda mrefu hapa duniani mpaka mwisho wake kisha kwenda peponi na kati ya kwenda kwa Allah تعالى Mwenye Kushinda na Kutukuka alichagua yaliyo kwa Allah تعالى dhidi ya hii Dunia duni.

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Abdillah naye ni Ibn Masoud رضي الله عنه amesema; alilala Mtume ﷺ juu ya mkeka ukaweka alama katika ubavu wake, alipoamka nikawa ninaufuta ubavu wake na nikasema, ‘Ewe!! Mtume ﷺ huturuhusu ili tukutandikie juu ya mkeka kitu? “Akasema Mtume ﷺ

«مَالِي وَلِلدُّنْيَا، إِنَّمَا مَتَلِي وَمَنْ لُّ الدُّنْيَا كَرَايِبٍ ظَلَّ تَحْتَ شَجَرَةٍ ثُمَّ رَاحَ وَتَرَكَهَا»

“Nani mimi na Dunia, hakika mfano wangu na mfano wa Dunia ni kama msafiri aliyejipumzisha chini ya mti kisha akaenda zake na akauacha.”¹

Ameyapokea hayo Atirmidhy na Ibn Maja, katika Hadith ya Masoud رضي الله عنه na amesema Atirmidhy, Hassan sahih.²

¹ Ahmad 1:391.

² Tuhfat Al-ahwadhi 7:48, na Ibn Majah 2:1376.

Neema Nyingi za Akhera Zinamngojea Mtume ﷺ.

Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ

“Na Mola Wako Mlezi Atakupa mpaka uridhike.”

Maana yake: Katika nyumba ya akhera Atampa mpaka Amridhishe kwa umma wake. Na katika yale Aliyomuandalia miongoni mwa utukufu. Na katika jumla ya mambo atakayopewa ni mto wa *Al-Kauthar* king’o zake kubwa za lulu, zenye mivungu, na udongo wake ni miski yenye harufu nzuri sana kama yatakavyokuja maelezo yake.

Na amepokea Imam Abuu Amr, Al Awzai kutoka kwa Abdillah bin Abbas رحمه الله عنه amesema; “Yalioneshwa kwa Mtume ﷺ mambo yaliyofunguliwa juu ya umma wake baada yake, hazina kwa hazina za mali akafurahi kwa hilo Mtume ﷺ.”

وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ

“Na Mola Wako Mlezi Atakupa mpaka uridhike.”

Akampa huko peponi maelfu ya Makasri katika kila kasri pana yale “yanayotakikana” kwake, miongoni mwa wake na watumishi. Ameyapokea hayo Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى kutokana na njia yake na upokezi huu ni sahihi kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.¹

Kutaja Baadhi ya Neema za Allah تعالی Juu ya Mtume ﷺ.

Allah تعالی Akaanza Kuhesabu Neema Zake juu ya mja Wake na Mjumbe Wake Muhammad ﷺ. Allah تعالی Amesema;

أَلَمْ تَجِدْكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ

“Kwani Hakukukuta yatima Akakupa makaazi?”

Na hilo ni kwa sababu ya kuwa Baba yake alikufa hali ya kuwa yeye ni mimba tumboni mwa mama yake. Kisha akafa mama yake Amina bint Walib, akiwa

¹ At-Tabari 24:487.

Mtume ﷺ na umri wa miaka sita. Kisha akawa katika ulezi wa babu yake Abdil Mutalib mpaka alipokufa na hali ya kuwa umri wa Mtume ﷺ ni miaka minane.

Hivyo akamlea ami yake Abu Twalib, hakuacha kuwa anamuhifadhi na anamnusuru, na akakinyanyua cheo chake na anamtukuza na anamkinga na maudhi ya watu wake hata baada ya Allah ﷻ Kumpa Utume akiwa na umri wa miaka arobaini. Hayo yote yalifanyika na hali ya kuwa Abu Twalib yuko katika dini ya watu wake katika kuabudu masanamu.

Na yote hayo ni kwa makadirio ya Allah ﷻ na uzuri wa mpango Wake. Mpaka alipokufa Abu Twalib na kabla ya kuhama kwa muda mfupi hapo ndipo walipomfanyia maovu wajinga wa Maqurayshi na wapumbavu wao. Akamchagulia Allah ﷻ kuhama kutoka baina yao kwenda kwenye mji wa Al-Answar, miongoni mwa makabila ya Ausi na Khazraji. Kama Alivyozipitisha Allah ﷻ Taratibu Zake juu ya utaratibu uliyotimia na ukamilifu sana. Alipofika kwao walimhifadhi na walimnusuru na walimlinda na wakapigana mbele yake (Allah ﷻ Awaridhie wote). Na yote hayo yanatokana na Ulinzi wa Allah ﷻ Kwake, na Uangalizi Wake.

Na Kauli Yake Allah ﷻ,

وَوَجَدَكَ ضَالًّا فَهَدَىٰ ﴿٥٢﴾

“Na Akakukuta umepotea Akakuongoa?”

Kama Allah ﷻ Alivyosema,

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا ۗ مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا آلِ كَتَابٍ وَلَا الْإِيمَانُ وَلَٰكِن جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِّنْ عِبَادِنَا ۗ

“Na namna hivi Tumekufunulia Qur’ani kwa Amri Yetu. Ulikuwa hujui Kitabu ni nini, wala Imani. Lakini Tumekifanya kuwa ni Nuru ambayo kwayo Tunamuongoa Tumtakaye katika waja Wetu...”
(42:52)

Na Kauli Yake Allah ﷻ,

وَوَجَدَكَ عَابِلًا فَأَغَىٰ ﴿٥٣﴾

“Akakukuta mhitaji Akakutosheleza?”

Maana yake: Ulikuwa fukara, mwenye wategemezi au mwenye familia (inayokutegemea) Akakutosheleza Allah تعالى na wala hakuna mwingine. Akakukusanyia daraja mbili, fakiri, mwenye kusubiri na tajiri mwenye kushukuru Rehema za Allah na Amani Zake ziwe juu yako. Na imekuja katika sahihi mbili kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه amesema; amesema Mtume ﷺ,

«لَيْسَ الْغِنَىٰ عَنْ كَثْرَةِ الْعَرَضِ، وَلَكِنَّ الْغِنَىٰ غِنَى النَّفْسِ»

“Haukuwa utajiri ni kutokana na kuwa na rasilimali nyingi isipokuwa utajiri ni utajiri wa nafsi.”¹

Na imekuja katika sahihi ya Muslim kutoka kwa Abdillah bin Amri رضي الله عنه amesema; amesema Mtume ﷺ,

«قَدْ أَفْلَحَ مَنْ أَسْلَمَ وَرَزَقَ كَفَافًا وَتَمَّعَهُ اللَّهُ بِمَا آتَاهُ»

“Kwa hakika amefaulu yule aliyejisalimisha (katika kufuata mafunzo ya Uislamu) na akaruzukiwa kile kinachomtosheleza kwa siku yake na Mwenyezi Mungu Akamkinaisha kwa kile Alichompa.”²

Vipi Tutazitukuza Neema Hizi

Kisha Allah تعالى Amesema,

فَأَمَّا الْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ ﴿١٠﴾

“Basi yatima usimuonee!” Kama wewe ulivyokuwa yatima Akakuhifadhi Allah تعالى, usimuonee yatima. Maana: Usimdhalilise na usimkaripie na kumfanya mnyonge, lakini mfanyie wema na upole. Amesema Qatadah رضي الله عنه: ‘kuwa kwa yatima kama vile baba mwenye huruma.’³

وَأَمَّا السَّائِلَ فَلَا تَنْهَرْ ﴿١١﴾

“Na anayeomba au kuuliza usimkaripie!” Maana yake: Kama ulivyokuwa umekosa muongozo Allah تعالى Akakuongoza, usimkaripie mwenye kuuliza katika elimu, mwenye kutaka maelekezo. Amesema ibn Ishaqa رحمه الله تعالى,

¹ Fat’hul Al-Bari 11:276, na Muslim 2:726 kwa Isnadi hii na nyingine pia.

² Muslim 2:730.

³ Al-Qurtubi 20:100.

وَأَمَّا السَّائِلَ فَلَا تَنْهَرْ ﴿١٠﴾

“Na anayeomba au kuuliza usimkaripie!”

Maana yake: Usiwe m-babe wala mwenye kiburi wala muovu wala mwenye tabia mbaya kwa wanyonge katika waja wa Allah تعالى. Na amesema Qatada anakusudia, ‘mjibu maskini kwa kumuonea huruma na kwa upole.’¹

وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ﴿١١﴾

“Na neema za Mola Wako Mlezi zisimulie.”

Maana yake: Kama ulivyokuwa ni mwenye familia na fukara, Akakutosheleza Allah تعالى, basi zungumzia neema ya Allah تعالى kwako.

Na amepokea Abu Dawud kutoka kwa Abuu Hurairah عنه رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ amesema;

«لَا يَشْكُرُ اللَّهُ مَنْ لَا يَشْكُرُ النَّاسَ»

*“Hamshukuru Mwenyezi Mungu ambaye hawashukuru watu.”*²

Ameipokea Atirmidhy na amesema; ni hadith sahihi.³

Na amepokea Abuu Dawud kutoka kwa Jabir عنه رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ amesema;

«مَنْ أُبْلِيَ بِلَاءٍ فَذَكَرَهُ فَقَدْ شَكَرَهُ، وَمَنْ كَتَمَهُ فَقَدْ كَفَرَهُ»

*“Mwenye kupewa majaribu yoyote akayataja, atakuwa amemshukuru Allah, na mwenye kuyaficha kwa hakika amemkufuru”*⁴

Hadithi hii ameipokea Abu Dawud peke yake.

Huu ndio mwisho wa *Suratu Adh-Dhuhaa*. Na ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹ Al-Baghawi 4:500.

² Abu Dawud 5:157.

³ Tuhfat Al-Ahwadhi 6:87.

⁴ Abu Dawud 5:159.

Tafsiri ya Suratu Ash-Sharh

Sura ya 94

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُوْرَةُ الشَّرْحِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ﴿١﴾ وَوَضَعْنَا عَنكَ وِزْرَكَ ﴿٢﴾
 أَلَّذِي أَنْقَضَ ظَهْرَكَ ﴿٣﴾ وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ ﴿٤﴾ فَإِنَّ مَعَ
 الْعُسْرَ يُسْرًا ﴿٥﴾ إِنَّ مَعَ الْعُسْرَ يُسْرًا ﴿٦﴾ فَإِذَا فَرَغْتَ
 فَانصَبْ ﴿٧﴾ وَإِلَىٰ رَبِّكَ فَارْغَبْ ﴿٨﴾

أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ﴿١﴾
 وَوَضَعْنَا عَنكَ وِزْرَكَ ﴿٢﴾ أَلَّذِي
 أَنْقَضَ ظَهْرَكَ ﴿٣﴾ وَرَفَعْنَا لَكَ
 ذِكْرَكَ ﴿٤﴾ فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٥﴾
 إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٦﴾ فَإِذَا فَرَغْتَ
 فَانصَبْ ﴿٧﴾ وَإِلَىٰ رَبِّكَ فَارْغَبْ ﴿٨﴾

1. Hatukukunjulia kifua chako?
2. Na Tukakuondolea mzigo wako,
3. Uliovunja mgongo wako?
4. Na Tukakunyanyulia utajo wako?
5. Basi kwa hakika pamoja na uzito upo wepesi,
6. Hakika pamoja na uzito upo wepesi.
7. Na ukipata faragha, fanya juhudi.
8. Na Mola Wako Mlezi ndio mshughulikie.

Maana ya Kukunjuliwa Kifua.

Allah تعالى Anasema,

أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ﴿١﴾

“Hatukukunjulia kifua chako?”

Anakusudia hakika sisi Tumekunjua kifua chako. Maana yake: Tumekitia Nuru na Tumekifanya kipokezi na kikunjufu. Kama ilivyo Kauli Yake Allah تعالى,

فَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ ۗ

“Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu Anataka kumuongoza humfungulia kifua chake Uislamu...” (6:125)

Na kama Alivyokikunjua kifua chake, hivyo Ameifanya sheria Yake kuwa ni pana, kunjufu, nyepesi, hamna ubaya ndani yake, wala ugumu wala dhiki.

Kubainisha Neema za Allah تعالى Juu ya Mtume Wake ﷺ.

Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَوَضَعْنَا عَنَّا وِزْرَكَ ﴿١﴾

“Na Tukakuondolea mzigo wako.”

Ni kwa maana,

لِيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ

“Ili Mwenyezi Mungu Akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo.” (48:2)

الَّذِي أَنْقَضَ ظَهْرَكَ ﴿٢﴾

“Uliovunja mgongo wako?”

“Al-Inqadh” ni sauti, hilo wamelisema wengi waliotangulia katika Kauli Yake Allah تعالى.

الَّذِي أَنْقَضَ ظَهْرَكَ ﴿٢﴾

“Uliovunja mgongo wako?” Maana yake: Ambao umekupa uzito kuubeba.

Maana ya Kunyanyuliwa Utajo wa Mtume ﷺ.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ ﴿١﴾

“Na Tukakunyanyulia utajo wako?”

Amesema Mujahid, ‘Sitajwi isipokuwa unatajwa pamoja Nami, kwa kauli hii - ‘Nashuhudia kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى, na ninashuhudia Muhammad ﷺ kuwa ni Mjumbe wa Allah.’¹

Na amesema Qatada: Allah تعالى Ameunyanyua Utajo Wake Duniani na akhera, hapana mwenye kukhutubia, wala mwenye kutamka shahada, wala mwenye kusali isipokuwa husema, “Nashuhudia kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى na kwamba Muhammad ﷺ ni Mjumbe wake.”²

Wepesi Baada ya Uzito.

Na Kauli Yake Allah تعالى,

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٢﴾ إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٣﴾

“Basi kwa hakika pamoja na uzito upo wepesi. Hakika pamoja na uzito upo wepesi.”

Allah تعالى Ameeleza kwamba pamoja na uzito unapatikana wepesi kisha Akaitilia mkazo habari hii.

Amri ya Kuleta Dhikri Ikipatikana Faragha

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَإِذَا فَرَغْتَ فَانصَبْ ﴿٤﴾ وَإِلَىٰ رَبِّكَ فَارْغَبْ ﴿٥﴾

“Na ukipata faragha, fanya juhudi. Na Mola Wako Mlezi ndio mshughulikie.”

¹ At-Tabari 24:494.

² At-Tabari 24:494.

Maana yake: Utapomaliza mambo ya Dunia na shughuli zake na ukakuta mafungamano yake, taabika katika kufanya ibada na simama na iendee hali ya kuwa mchangamfu usiozongwa na mawazo. Na mtakasie nia na utashi Mola wako. Hili linawiana na kauli ya Mtume ﷺ katika hadithi sahihi,

«لَا صَلَاةَ بِحَضْرَةِ الطَّعَامِ، وَلَا هُرْ يُدَاوِعُهُ الْأَخْبَانِ»

“Hapana Sala katika hadhara ya chakula wala wakati mtu anasukumana na hadathi mbili.”²

Na kauli yake Mtume ﷺ,

«إِذَا أُقِيمَتِ الصَّلَاةُ وَحَضَرَ الْعِشَاءُ فَأَبْدَأُوا بِالْعِشَاءِ»

“Na itakapokimiwa Sala na kipo juu chakula cha usiku anzeni kula chakula cha usiku.”²

Amesema Mujahid katika aya hii kuna mafundisho: ‘Pindi utakapomaliza mambo ya Dunia simama kwenye Sala, taabika kwa ajili ya Bwana Wako.’³

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Alam Nashrah*. Allah تعالیٰ tu ni wa Kusifiwa, Naye ni Mwenye Kuneemesha.

* * *

¹ Muslim 1:393.

² *Fat’h Al-Bari* 9:498.

³ At-Tabari 24:497.

Tafsiri ya Suratu Tin

Sura ya 95

Iliteremshwa Makkah

Kusomwa kwa *Suratu Wattini* katika Sala Ndani ya Safari

Amesema Malik na Shuba kutoka kwa Addiy bin Thabit kutoka kwa Albaraa bin Azib رضي الله عنه: alikuwa Mtume ﷺ akisoma katika safari yake katika moja ya rakaa mbili *Surat At-Tin*, sijamsikiapo mtu yoyote mzuri sana kwa sauti au kisomo kuliko yeye, kundi la wapokeaji wa Hadithi limethibitisha Hadithi hii.¹



¹ *Fat'hul Al-Bari* 8:583, *Muslim* 1:339, *Abu Dawud* 2:19, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 2:226, *An-Nasai* katika *Al-Kubra* 6:518 na *Ibn Majah* 1:273.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ التِّينِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالَّتَيْنِ وَالزَّيْتُونَ ﴿١﴾ وَطُورِ سِينِينَ ﴿٢﴾ وَهَذَا الْبَلَدِ الْأَمِينِ ﴿٣﴾ لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٤﴾ ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿٥﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٦﴾ فَمَا يُكَذِّبُكَ بَعْدُ بِالذِّكْرِ ﴿٧﴾ أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَحْكَمَ الْحَاكِمِينَ ﴿٨﴾

وَالَّتَيْنِ وَالزَّيْتُونَ ﴿١﴾ وَطُورِ سِينِينَ ﴿٢﴾ وَهَذَا الْبَلَدِ الْأَمِينِ ﴿٣﴾ لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٤﴾ ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿٥﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٦﴾ فَمَا يُكَذِّبُكَ بَعْدُ بِالذِّكْرِ ﴿٧﴾ أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَحْكَمَ الْحَاكِمِينَ ﴿٨﴾

1. Naapa kwa tini na zaituni!
2. Na kwa Mlima wa Sinai!
3. Na kwa mji huu wenye amani!
4. Bila ya shaka Tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa.
5. Kisha Tukamrudisha kuwa chini kuliko waliochini!
6. Lakini wale walioamini na wakatenda mema, hao watapata ujira usiokwisha.
7. Basi ni lipi likupatalo litakalokukukadhibishia kutokea siku ya malipo?
8. Kwani Mwenyezi Mungu si Muadilifu kuliko mahakimu wote?

Tafsiri ya Attini na Yaliyo Baada Yake

Maana ya *Atiini*: Kama ambavyo ameeleza Auafi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kwamba *Atiin* ni msikiti wa Nuhu عليه السلام ambao uko juu ya Al Juudiy. Na amesema Mujahid; *Atiin* ni tini yenu hii,¹

وَالزَّيْتُونَ

“Zaituni!”

Amesema Kaab Al'ahbar na Qatada Ibn Zaid na wengine, huo ni msikiti wa *Baytul Muqaddas*. Na amesema Mujahid na Ikrimah; ni hii Zaytuni ambayo mnaikamua.²

وَطُورِ سَيْنِينَ

“Na kwa Mlima wa Sinai!”

Amesema Kaab al'Ahbar na wengineo; ni jabali ambalo Alizungumza Allah تعالى na Musa عليه السلام.³

وَهَذَا الْبَلَدِ الْأَمِينِ

“Na kwa mji huu wenye amani!”

Anakusudia Makkah. Ameyasema hayo Ibn Abbas na Mujahid na Ikrimah na Al-Hassan na Ibrahim Anakhai na Ibn Zaid na Kaab Al'ahbar رضي الله عنهم⁴ na wala hawakutofautiana katika hilo. Na wamesema baadhi ya Maimamu, “hizi ni sehemu tatu ambazo Alipeleka Allah تعالى kila moja katika sehemu hizo Mtume miongoni mwa “*Ulul Azmi*” wenye sheria kubwa.”

Mahali pa Kwanza ni *Tiin* na *Azaytun* napo ni *Baytul Muqaddas* alimpeleka Allah تعالى hapo Issa Ibn Maryam عليه السلام. (Mahali pa Pili) ni “*Turisinin*” napo ni *Tur-Saynaa*, mahali ambapo Allah تعالى Alimsemesha Musa bin Imran عليه السلام. Mahali pa Tatu ni Makkah, Mji wenye Amani, ambao atakayeuingia amepata salama. Na huo ndio mji ambao alipelekwa Muhammad ﷺ.

¹ At-Tabari 24:502.

² At-Tabari 24:501.

³ At-Tabari 24:503.

⁴ At-Tabari 24:505, 506.

Wamesema kwamba mwishoni mwa Taurat zimetajwa sehemu hizi tatu. Alikuwa Allah تعالى kutoka *Tur-Saynaa*, anakusudia ile ambayo Alimsemesha juu yake Mussa bin Imran عليه السلام na Akatoa mwangaza kutoka *Sair*, analikusudia Jabal la *Baytul Muqaddas* ambapo Alimpeleka Allah تعالى hapo Issa عليه السلام na Akatangaza kutoka katika majabali ya parani Anakusudia majabali ya Makkah ambayo Alimpeleka Allah تعالى katika majabali hayo Muhammad ﷺ. Basi Akawataja kwa Kuwaelezea juu ya utaratibu wa kupatikana kwao, kufuatana na utaratibu wao katika zama, na kwa sababu hiyo Ameapa kwa kilicho kitukufu, kisha kitukufu zaidi, kisha kitukufu kuliko vyote.

Kuanguka kwa Mwanadamu Chini Zaidi ya Aliye Chini Pamoja na Kuwa Ameumbwa katika Umbile Zuri na Matokeo ya Hilo.

Na Kauli Yake Allah تعالى,

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿١﴾

“Bila ya shaka Tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa.”

Hili ndilo lililoapiwa, nalo ni kwamba Yeye Allah تعالى Amemuumba mwanadamu katika uzuri mno wa sura na umbile, mwenye kusimama kimo, mwenye kuwiana viungo vyake,

ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿٢﴾

“Kisha Tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini!”

Vikiwa viungo hivyo ni vizuri kisha Tutamrudisha hali ya kuwa chini sana ya waliyo chini. Maana yake: kwenda motoni. Ameyasema hayo Mujahid na Abu Aliya na Al Hassan na wasiokuwa hao.¹ Kisha baada ya uzuri huu na mvuto, mwisho wao ni motoni, kwa kuwa hakumtii Allah تعالى na akawakataa Mitume wake. Na kwa sababu hiyo Amesema,

إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Isipokuwa wale walioamini na wakatenda mema,”

Na wamesema baadhi yao;

¹ At-Tabari 24:110, 509.

ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿١﴾

“Kisha Tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini!”

Maana yake: Kwenye uduni wa umri. Yamepokewa haya kutoka kwa Ibn Abbas hatarejeshwa kwenye uduni wa umri.”¹ Na amechagua hayo Ibn Jarir² رحمه الله تعالى. Ingekuwa ndiyo kusudio wasingepewa waumini katika jambo, hilo, kwa sababu ukongwe huwapata baadhi yao. Na hakika si vingine maana sahihi ni hayo tuliyoataja ni kama Kauli Yake Allah تعالى،

وَالْعَصْرِ ﴿١﴾ إِنَّ الْإِنْسَانَ لَفِي خُسْرٍ ﴿٢﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Naapa kwa Zama!. Hakika binaadamu wote wapo katika khasara, Ila wale walioamini, na wakatenda mema,...” (103:1-3)

Na Kauli Yake تعالى،

فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿١﴾

“...hao watapata ujira usiokwisha.”

Maana yake: Yasiyokatika. Kama ilivyotangulia. Kisha Amesema:

فَمَا يُكَذِّبُكَ

“Basi ni lipi likupatalo litakalokukukadhibisha...?”

Ewe Mwana wa Adamu!’

بَعْدُ بِالَّذِينَ ﴿١﴾

“...kutokea siku ya malipo.”

Maana yake: ‘Ewe!! Mwanadamu (baada ya hayo) unakadhibisha malipo?’ Maana: Malipo siku ya Kiyama, hakika umejua Uumbaji wa kwanza, na umekwishamjua Mwenye Kuweza Kuumba mara ya kwanza, Yeye Anajua Kurejeshwa Alichokiumba kwa namna ile ile ya kwanza. Ni kitu gani kinachokufanya na kinachokuchukua juu ya kukadhibisha marejeo na hali ya

¹ At-Tabari 24:508.

² At-Tabari 24:511.

kuwa umeyajuwa hayo? Na Kauli Yake Allah تعالى.

أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَحْكَمَ الْحَاكِمِينَ ﴿٥﴾

“Kwani Mwenyezi Mungu si Muadilifu kuliko mahakimu wote?”

Maana: Ama Yeye ni Hakimu wa mahakimu wote ambaye Hafanyi ujeuri na Hamdhulumu mtu yoyote, na katika Uadilifu Wake ni Kukisimamisha Kiyama ili Amchukulie haki mwenye kudhulumiwa duniani kutoka kwa aliyemdhulumu. Na tumekwisha kutanguliza katika Hadithi ya Abu Huraira رضي الله عنه. Hadithi iliyo maarufu “Atakaposoma mmoja wenu *Wattiin wazaitun*.” Akafika, mwisho wa sura na aseme, ***Balaa Wa ‘ana alaa Dhalika Mina Ssha-hidina***.¹ Maana: ‘Kwanini? na mimi juu ya hilo ni katika wenye kushuhudia.’

Huu ni mwisho wa tafsiri ya *Suratu Wattiin Wazaitun*. Na ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹ Abuu Dawud 1 / 550.

Tafsiri ya Suratul 'Alaq

Sura ya 96

Iliteremshwa Makkah

Ndiyo Kitu cha Kwanza Kushuka katika Qur'an.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْعَلَقِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ﴿١﴾ خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ﴿٢﴾
 أَقْرَأْ ﴿٣﴾ وَرَبُّكَ الْأَكْرَمُ ﴿٤﴾ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ﴿٥﴾
 عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ﴿٦﴾ كَلَّا إِنَّ الْإِنْسَانَ لَبِئْسَ أَفْئِسَ ﴿٧﴾
 أَنْ رَآهُ اسْتَغْفَى ﴿٨﴾ إِنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ أَلْحَبَىٰ ﴿٩﴾ أَرَأَيْتَ إِذْ
 أَلْفَىٰ يَنْهَىٰ ﴿١٠﴾ عَبْدًا إِذَا صَلَّىٰ ﴿١١﴾ أَرَأَيْتَ إِنْ كَانَ
 عَلَىٰ الْهُدَىٰ ﴿١٢﴾ أَوْ أَمَرَ بِالتَّقْوَىٰ ﴿١٣﴾ أَرَأَيْتَ إِنْ كَذَّبَ
 وَتَوَلَّىٰ ﴿١٤﴾ أَلَمْ يَعْلَمْ بِأَنَّ اللَّهَ يَرَىٰ ﴿١٥﴾ كَلَّا لَئِنْ لَمْ يَنْهَ
 لَنْسَفَعْنَا بِالْناصِيَةِ ﴿١٦﴾ نَاصِيَةٍ كَذِبَةٍ خَاطِئَةٍ ﴿١٧﴾ فَلْيَدْعُ
 نَادِيَهُ ﴿١٨﴾ سَدِّعُ الزَّبَانِيَةَ ﴿١٩﴾ كَلَّا لَا تَطِعَهُ وَأَسْجُدْ
 وَاقْتَرِبْ ﴿٢٠﴾

أَقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ﴿١﴾
 خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ﴿٢﴾ أَقْرَأْ ﴿٣﴾
 وَرَبُّكَ الْأَكْرَمُ ﴿٤﴾ الَّذِي عَلَّمَ
 بِالْقَلَمِ ﴿٥﴾ عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ
 يَعْلَمْ ﴿٦﴾

1. Soma kwa Jina la Mola Wako Mlezi Aliyeumba,
2. Amemuumba binaadamu kwa tone la damu,
3. Soma! Na Mola Wako Mlezi ni Karimu kushinda wote!
4. Ambaye Amefundisha kwa kalamu.
5. Kamfundisha mtu aliyokuwa hayajui.

Kuanza kwa Utume wa Muhammad ﷺ na Kitu cha Mwanzo Kilichoshuka katika Qur'an.

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Aisha رضي الله عنها amesema: Kitu cha kwanza alichianza kwacho Mtume ﷺ katika Wahyi ni ndoto za kweli usingizini, alikuwa haoti ndoto yoyote isipokuwa huja mfano wa mwangaza wa Asubuhi. Kisha kukapendezwa kwake yeye kujitenga, akawa analiendea Jabal Hiraa anafanya lbada humo masiku yenye kuhesabika na alikuwa anajiandaa kwa sababu hiyo. Kisha anarejea kwa mama Khadija anajiandaa mfano wake, mpaka wahyi ukamjia ghafla na hali ya kuwa yeye yumo katika pango hilo. Akaamriwa; "Soma." Akajibu Mtume ﷺ,

«قُلْتُ: مَا أَنَا بِقَارِيءٍ»

"Nikasema Sikuwa ni mwenye kusoma."

Amesema: 'Akanikamata, akanibana, mpaka ikafikia mwisho wa uwezo wangu (wa kustahamili) kisha akaniachia akasema; "Soma" Nikasema, 'Sikuwa ni mwenye kusoma.' Akanibana mara ya pili mpaka akafikia mwisho wa uwezo wangu (wa kustahamili), kisha akaniachia akasema; "Soma" Nikasema. 'Sikuwa ni mwenye kusoma' Akanibana mara ya tatu mpaka akafikia mwisho wa uwezo wangu (wa kustahamili), kisha akaniachia, kisha akasema:

«أَقْرَأُ بِأَسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ»

"Soma kwa Jina la Mola Wako Mlezi Aliyeumba." Mpaka,

«مَا لَمْ يَعْلَمْ»

"...mtu aliyokuwa hayajui."

Maana yake: Yale ambayo hakuwa akiyajuwa. Amesema; akarejea na aya hizo na hali ya kuwa anatetemeka moyo wake na viungo vyake, mpaka akaingia kwa Khadija akasema,

«زَمَلُونِي زَمَلُونِي»

"Nifunikeni Nifunikeneni"

Wakamfunika mpaka ikamuo ndokea khofu, akasema, 'Ewe!! Khadija unaniamini mimi?' Akamueleza ile khabari na akasema;

«قَدْ خَشِيتُ عَلَى نَفْسِي»

"Ninaigopea nafsi yangu."

Akamuambia, 'Hapana! Furahi, naapa Mwenyezi Mungu Hatakdhalilisha milele, hakika wewe unaunga udugu na ni mkweli katika mazungumzo, na umeuchukua uzito na unamkirimu mgeni na unasaidia juu ya matatizo ya kweli.' Kisha Khadija رضي الله عنها akaondoka naye mpaka kwa Waraqa bin Naufal bin Asad bin Abdil Uzza bin Qusway, naye ni mtoto wa ami wa Khadija, ndugu wa baba yeke, na alikuwa ni mtu aliyefuata dini ya kinaswara wakati wa Jahiliya. Na alikuwa anaandika maandishi ya kiarabu, na aliandika injili kwa lugha ya kiarabu. Alichotaka Allah تعالى Anaandika na alikuwa ni mzee mkubwa wa makamo aliyepofuka macho, Akasema Khadija kumuambia; 'Ewe!!mtoto wa Ami yangu; sikia kutoka kwa mtoto wa ndugu yako' Akasema Waraqa; 'Ewe mtoto wa ndugu yangu, unaona nini?' Akamueleza Mtume ﷺ yale aliyoyaona. Akasema Waraqa; 'Huyo ndiye Mjumbe¹ Aliyeteremshwa kwa Musa عليه السلام, natamani katika wakati huo ningekuwa kijana, natamani ningekuwa mzima watakapokufukuza watu wako." Akauliza Mtume ﷺ,

«أَوْ مُخْرِجِيْ هُمْ؟»

"Hivi hao watanitoa?"

Akasema Waraqa, 'Ndiyo, hakuja mtu yoyote kabisa kwa hili ambalo umekuja nalo isipokuwa hufanyiwa uadui, iwapo itanikuta siku yako nitakusaidia msaada mkubwa sana."

Kisha hakuishi muda mrefu Waraqa akafariki. Wahyi ukakatika kwa muda² mpaka akahuzunika Mtume ﷺ katika yaliyotufikia. Alihuzunika huzuni kubwa sana. Mara nyingi asubuhi na mapema sana hutoka ili ajirushe katika vilele vya jabali, na kila anapofika katika vilele vya Jabali humdhihirikia Jibril عليه السلام humuambia; 'Ewe!! Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.'" Kwa ukweli hapo hutulia hamasa yake na hutulizana nafsi yake na hurejea katika hali ya kawaida.

¹ Mtunzaji wa siri, yaani Jibril.

² Kutoka sehemu hii hadi mwisho wa masimulizi yametolewa na Az-Zuhri kama alivyosimulia Ma'mar na imeelezwa kwa kirefu na Ibn Hajar katika Fat'hul Al-Bari Na. 6982.

Kukirefuka juu yake kukatika kwa Wahyi hutoka mapema kwa kutaka kufanya mfano wa hivyo, akifika katika kilele cha jabali Jibril عليه السلام humdhihirikia humuambia mfano wa yale maneno aliyomuambia mwanzo.¹

Na Hadith hii imetolewa katika sahihi mbili kupitia Hadithi ya Zuhri.²

Na kwa hakika tumeizungumzia hadithi hii kwa upande wa upokezi wake na matamshi yake na maana yake mwanzoni mwa sherehe yetu kwa ukamilifu, basi atakayeyataka maelezo hayo basi yapo huko yakiwa yamehaririwa. Ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.

Kwa hiyo kitu cha kwanza kushuka katika Qur'an ni aya hizi tukufu zenye kubarikiwa, na aya hizo ndio rehema ya kwanza ambayo Amewarehemu Allah تعالى waja Wake na ni Neema ambayo Amewaneemesha juu yao.

Utukufu wa Mwanadamu na Ubora Wake ni kwa Elimu.

Kutoka aya za mwanzo za sura hii, pana uzinduzi juu ya kuanza Kuumbwa kwa mwanadamu kutokana na pande la damu, na miongoni mwa ukarimu wa Allah تعالى kwamba Amemfundisha mwanadamu yale ambayo hakuwa akiyajua.

Kwa hiyo utukufu na ubora wa mwanadamu ni kwa elimu na hiyo elimu ndio kiasi ambacho amepambanuka kwacho baba wa watu wote Adamu juu ya malaika.

Na elimu mara inakuwa katika akili na mara nyingine inakuwa katika ulimi, na mara nyingine kuandika kwa vidole.

Kwa hiyo elimu ni ya akili, kutamka na kuandika, ambako hulazimiana kwa namna zote mbili.

Kwa sababu hiyo Amesema,

أَقْرَأُ وَرَبُّكَ الْأَكْرَمُ ﴿٦﴾ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ﴿٧﴾ عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ﴿٨﴾

“Soma! Na Mola Wako Mlezi ni Karimu kushinda wote!. Ambaye Amefundisha kwa kalamu. Kamfundisha mtu aliyokuwa hayajui.”

¹ Ahmad 6:232.

² Fat'hul Al-Bari 12:368, na Muslim 1:139.

Na imekuja *athar*: 'Idhibiti elimu kwa kuandika.'¹ Na imekuja katika *athar* vilevile, 'mwenye kuyafanyia kazi yale aliyoyajua atamrithisha yeye Allah تعالى kujua yale ambayo hakuwa akiyajua.'²

كَلَّا إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنَّاظٍ ﴿١﴾ أَنْ رَّأَاهُ اسْتَغْفَىٰ ﴿٢﴾ إِنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ أَلْحَبَىٰ ﴿٣﴾ أَرَأَيْتَ الَّذِي يَنْهَىٰ ﴿٤﴾ عَبْدًا إِذَا صَلَّىٰ ﴿٥﴾ أَرَأَيْتَ إِنْ كَانَ عَلَىٰ أَهْدَىٰ ﴿٦﴾ أَوْ أَمَرَ بِالتَّقْوَىٰ ﴿٧﴾ أَرَأَيْتَ إِنْ كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿٨﴾ أَلَمْ يَعْلَم بِأَنَّ اللَّهَ يَرَىٰ ﴿٩﴾ كَلَّا لَئِنْ لَمْ يَنْتَه لِنَسْفَعًا بِالنَّاصِيَةِ ﴿١٠﴾ نَاصِيَةٍ كَذِبَةٍ خَاطِئَةٍ ﴿١١﴾ فَلْيَدْعُ نَادِيَهُ ﴿١٢﴾ سَدَّعَ الزَّيْنِيَةَ ﴿١٣﴾ كَلَّا لَا تَطِعَهُ وَأَسْجُدْ وَقْتَرَبْ ﴿١٤﴾

6. Kwani! Hakika mtu bila ya shaka huwa jeuri.

7. Akijiona katajirika.

8. Hakika kwa Mola Wako Mlezi ndio marejeo.

9. Umemuona yule anayemkataza

10. Mja anaposali?

11. Umeona kama yeye yuko juu ya uwongofu?

12. Au anaamrisha uchamungu?

13. Umeona kama yeye akikanusha na anarudi nyuma?

14. Je, Hajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anaona?

15. Kwani! Kama haachi, Tutamkokota kwa shungi la nywele!

16. Shungi la nywele la muongo, lenye makosa!

17. Basi na awaite wenzake!

18. Nasi Tutawaita Mazabania!

19. Hasha! Usimt'ii! Nawe sujudu na ujongee!

¹ Hadithi hii si sahihi. Angalia Al-Hakim 1:106. Pia imenasibishwa katika usemi wa 'Umar kupitia isnadi dhaifu kupitia kwa Ibn Abu Shaybah (26418) na wengine.

² Hadithi hii si sahihi, pia huwa wanaisimulia kuwa ilisemwa na Nabii 'Isa iliandikwa na Abu Nu'aym katika Al-Hilyah 10:14-15. Angalia Adh-Dhwa'ifah Na. 422.

Makamio Juu ya Kuvuka Mipaka kwa Mwanadamu kwa sababu ya Mali.

Allah تعالی Ameeleza kuhusu mwanadamu kwamba yeye ni mwenye furaha na majivuno na kuvuka mipaka, pindi aonapo nafsi yake imejitosha na imekuwa nyingi mali yake. Kisha Amemtisha na Kumkamia na Amemuonya kwa Kusema:

إِنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ أَلْرُجْعَىٰ ﴿١٠﴾

"Hakika kwa Mola Wako Mlezi ndio marejeo."

Maana: Ni kwa Allah تعالی tu marejeo na Kuhesabiwa. Na kila mtu ataulizwa kuhusu mali yake imetoka wapi na vipi ameikusanya na vipi ameitumia?

Kumsema Vibaya Abu Jahal na Karipio Kali la Kumuadhibu.

Kisha Allah تعالی Amesema,

أَرَأَيْتَ الَّذِي يَنْهَىٰ ﴿١١﴾ عَبْدًا إِذَا صَلَّىٰ ﴿١٢﴾

"Umemuona yule anayemkataza Mja anaposali?"

Aya hizi zilimshukia Abu-Jahali (Allah تعالی Amlaani) alimtisha Mtume ﷺ alipokuwa anasali mbele ya Alkaaba, akumuonya Allah تعالی kwa maneno ambayo ni mazuri kwanza kwa kusema,

أَرَأَيْتَ إِنْ كَانَ عَلَىٰ أَهْدَىٰ ﴿١٣﴾

"Umeona kama yeye yuko juu ya uwongofu?"

Maana yake: Ni nini dhana yako iwapo atakuwa huyu unayemkataza yupo juu ya njia iliyonyooka katika kitendo chake (au akiamrisha kumcha Allah تعالی) kwa maneno yake. Na wewe unamkemea na unamkamia juu ya Sala yake. Na kwa sababu hiyo Amesema;

أَوْ أَمَرَ بِالْتَّقْوَىٰ ﴿١٤﴾

"Au anaamrisha uchamungu?"

Maana yake: Hivi hakujua huyu mkatazaji wa mtu aliyeongoka kwamba Allah تعالی Anamuona na Anasikia maneno yake na Atamlipa juu ya matendo yake malipo yaliyokamilika. Kisha Amesema Allah تعالی hali ya Kumkamia na hali ya Kumtisha,

أَلَمْ يَعْلَم بِأَنَّ اللَّهَ يَرَىٰ

“Hajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anaona?”

Maana yake: Asiporejea kuacha yale ambayo yeye yumo ndani yake miongoni mwa ugomvi na ukaidi. Kisha Allah تعالى Amesema,

كَلَّا لَئِن لَّمْ يَنْتَهُ

“Kwani! Kama haachi...”

لَتَسْفَعَا بِالنَّاصِيَةِ

“Tutamkokota kwa shungi la nywele!”

Maana: Tutaupakaza utosi wake rangi nyeusi siku ya Qiyama. Kisha Amesema:

نَاصِيَةٍ كَذِبَةٍ خَاطِئَةٍ

“Shungi la nywele la muongo, lenye makosa!”

Maana yake: Abu Jahal ni muongo. Maneno yake yana makosa katika matendo yake,

فَلْيَدْعُ نَادِيَهُ

“Basi na awaite wenzake”

Maana: Watu wake na jamaa zake. Maana: Na awaite atake nusra kwao.

سَنَدْعُ الزَّبَانِيَةَ

“Nasi Tutawaita Mazabania!”

Na hao ni malaika wa adhabu ili ajue nani atakaeshinda ni kundi lake au kundi letu? Amepokea Al-Bukhari kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema: Alisema Abu Jahl: Naapa, iwapo nitamuona Muhammad anasali kwenye Al-Ka'aba nitamkanyaga shingo yake. Ikamfikia habari hiyo Mtume ﷺ naye akasema;

«لَئِن فَعَلْ لَأَخَذْتَهُ الْمَلَائِكَةُ»

“Naapa kwa hakika iwapo atalifanya hilo malaika watamkamata.”¹

¹ Fat'hul Al-Bari 8:595.

Hadithi hiyo pia iliandikwa na An-Nasai katika vitabu vyao.¹ Kadhalika ameipokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى.² Ahmad, Atirmidhy, An-Nasai na Ibn Jarir رحمه الله تعالى wameipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema: Kwa maneno yafuatayo: Mtume ﷺ alikuwa anasali kwenye *Maqam Ibrahim*, Abu Jahl bin Hisham akampitia akasema; 'Eee!! Muhammad sikukukataza kufanya kitendo hiki?' Na akamtishia kwa maneno mazito na Mtume ﷺ akakasirika na kumkaripia. Abu Jahal akasema, 'Ewe!! Muhammad ni kwa jambo gani unanitisha? Ama naapa kwa Mwenyezi Mungu mimi ni mwingi wa ndugu na jamaa katika bonde hili.' Akateremsha Allah تعالى،

فَلْيَدْعُ نَادِيَهُ ﴿١٧﴾ سَدَّعُ الزَّيْنَبِيَّةَ ﴿١٨﴾

"Basi na awaite wenzake!. Nasi Tutawaita Mazabania!" (96:17-18)

Na amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما, 'lau angeliwaita watu wa baraza lake wangemkamata malaika wa adhabu palepale.' Na amesema Atirmidhy hadithi hii ni Hassan Sahihi.³ Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameandika kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه amesema; amesema Abu Jahl; 'Jee ameutia vumbi uso wake mbele yenu" Wakasema, 'ndio'. Akasema, 'Naapa kwa Al Uzza kwa hakika iwapo nitamuona anasali kama hivyo nitaikanyaga shingo yake na nitaugaragaza uso wake katika mchanga.' Akamuendea Mtume ﷺ hali ya kuwa anasali kwa madhumuni ya kuikanyaga shingo yake. Amesema hakukuwashitua kwake isipokuwa ni pale walipomuona anarudi nyuma na anajikinga kwa mikono yake. Akasema; Akaulizwa, 'Una jambo gani?' Akasema; kati yangu na 'kati yake pana handaki la moto na vitisho vikubwa sana na mbawa nyingi." Amesema: Akasema Mtume ﷺ،

«لَوْ دَنَا مِنِّي لَأَخْطَفْتَهُ الْمَلَائِكَةُ عُضْوًا عُضْوًا»

"Lau angenikaribia Malaika wangemnyakua kiungo kimoja kimoja."

Amesema; Allah تعالى Aliteremsha Ayah lakini sijui kama inahusu Hadithi ya Abu Huraira رضي الله عنه au laa. Amesema Allah تعالى:

¹ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:277, na An-Nasai in *Al-Kubra* 6:518.

² At-Tabari 12:649.

³ Ahmad 1:329, At-Tirmidhi 3349, An-Nasai katika *Al-Kubra* 11684, na At-Tabari 12:648.

كَلَّا إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنَّا

“Kwani! Hakika mtu bila ya shaka huwa jeuri”

Mpaka mwisho wa Surat¹ na amepokea Ahmad bin Hanbal na Muslim na Annasai na Atirmidhy.²

Kufundishwa kwa Mtume ﷺ

Na Kauli Yake Allah تعالى،

كَلَّا لَا تُطِيعُهُ

“Hasha! Usimt'ii!”

Anakusudia, “Eee Muhammad usimtii katika lile analokukataza nalo, miongoni mwa kudumu na ibada na wingi wake na usali wakati wowote unaotaka na usimjali kwani Allah تعالى Ndio Muhifadhi Wako Atakunusuru na Yeye Atakulinda na shari za watu.”

وَأَسْجُدْ وَاقْتَرِبْ ﴿١٧﴾

“Nawe sujudu na ujongee!”

Kama ilivyothibiti katika hadith sahihi kutoka kwa Muslim kutoka kwa Abuu Saleh kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه na kwamba Mtume ﷺ amesema;

«أَقْرَبُ مَا يَكُونُ الْعَبْدُ مِنْ رَبِّهِ وَهُوَ سَاجِدٌ، فَأَكْثِرُوا الدُّعَاءَ»

“Ukaribu sana anaokuwa mja na bwana wake ni pale anapokuwa amesujudu; kwa hiyo ongezeni maombi kwa wingi.”³

Na imetangulia vilevile kwamba Mtume ﷺ alikuwa anasujudu katika,

إِذَا السَّمَاءُ أَنْشَقَّتْ ﴿٨٤﴾

“Itapo chanika mbingu.” (84:1) na,

¹ At-Tabari 12:649.

² Ahmad 2:370, Muslim 2797, na An-Nasai katika *Al-Kubra* 11683.

³ Muslim 1:350.

أَقْرَأْ بِأَسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ

“Soma kwa Jina la Mola Wako Mlezi Aliyeumba...”(96:1)¹

Huu ni mwisho wa tafsiri ya *Surat Iqraa*. Na ni kwa Allah تعالى tu, Kusifiwa na Kuneemesha. Na Kwake tu kutaka kuwezesha na kulindwa.

* * *

¹ Muslim 1:406.

Tafsiri ya Suratul Qadr Sura ya 97 Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْقَدْرِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ ۝ وَمَا أَدْرَاكَ مَا لَيْلَةُ الْقَدْرِ ۝ تَنْزِيلُ الْمَلَائِكَةِ وَالرُّوحِ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ مِنْ كُلِّ أَمْرٍ ۝ سَلَّمَ هِيَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ الْفَجْرِ ۝

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ ۝ وَمَا
أَدْرَاكَ مَا لَيْلَةُ الْقَدْرِ ۝ لَيْلَةُ
الْقَدْرِ حَمْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ ۝ تَنْزِيلُ
الْمَلَائِكَةِ وَالرُّوحِ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ مِنْ
كُلِّ أَمْرٍ ۝ سَلَّمَ هِيَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ
الْفَجْرِ ۝

1. Hakika Sisi Tumeiteremsha Qur'ani katika Laylatul Qadri, Usiku wa Cheo Kitukufu.
2. Na nini kitachokujuulisha nini Laylatul Qadri?
3. Laylatul Qadri ni bora kuliko miezi elfu.
4. Huteremka Malaika na Roho (katika usiku huo) kwa Idhini ya Mola Wao Mlezi kwa kila jambo.
5. Amani usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajiri.

Ubora wa Usiku wa Cheo.

Anaeleza Allah تعالى, Kwamba Yeye Ameiteremsha Qur'an katika usiku wa cheo. Na huo ndio usiku uliobarikiwa ambao Amesema Allah تعالى Mwenye Kushinda na Kutukuka.

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ مُبَرَّكَةٍ ۚ إِنَّا كُنَّا مُنذِرِينَ ﴿٣﴾

“Hakika Tumekiteremsha katika usiku uliobarikiwa. Hakika Sisi ni Waonyaji.” (44:3)

Nao ni usiku wa cheo na usiku huo upo katika mwezi wa Ramadhani kama Anavyosema Allah تعالى,

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ

“Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur’ani...” (2:185)

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine, “Aliteremsha Allah تعالى Qur’an kwa pamoja kutoka katika ubao uliohifadhiwa mpaka Baytul Izza katika mbingu ya Dunia, kisha ikateremka hali ya kupambanuliwa kufuatana na matukio katika muda wa miaka ishirini na mitatu (23) kwa Mtume ﷺ.”

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَمَا أَدْرَاكَ مَا لَيْلَةُ الْقَدْرِ ﴿١﴾ لَيْلَةُ الْقَدْرِ خَيْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ ﴿٢﴾

“Na nini kitachokujulisha nini Laylatul Qadri?. Laylatul Qadri ni bora kuliko miezi elfu.”¹

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه amesema; Ilipokuja Ramadhani alisema Mtume ﷺ;

«قَدْ جَاءَكُمْ شَهْرُ رَمَضَانَ، شَهْرُ مَبَارَكٍ، افْتَرَضَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ صِيَامَهُ، تَفْتَحُ فِيهِ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ، وَتُغْلَقُ فِيهِ أَبْوَابُ الْجَحِيمِ، وَتُغْلَقُ فِيهِ الشَّيَاطِينُ، فِيهِ لَيْلَةٌ خَيْرٌ مِنْ أَلْفِ شَهْرٍ، مَنْ حُرِمَ خَيْرَهَا فَقَدْ حُرِمَ»

¹ At-Tabari 24:531, 532, na Al-Qurtubi 20:130.

“Kwa hakika umekujieni mwezi wa Ramadhani, mwezi wenye kubarikiwa Amefaradhisha Mwenyezi Mungu juu yenu kuufunga, hufunguliwa ndani yake milango ya pepo na hufungwa ndani yake milango ya moto, na hufungwa pingu ndani yake Mashetani, ndani yake mna usiku mbora kuliko miezi elfu, atakayezuiliwa na kheri yake hiyo amezuiwa na kheri kubwa.”¹ Ameipokea Annasai.²

Na ulipokuwa usiku wa cheo unalingana ibada yake na ibada ya miezi elfu, imethibiti katika hadith ya Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema;

«مَنْ قَامَ لَيْلَةَ الْقَدْرِ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ»

“Mwenye kusimama usiku wa cheo kwa kumuamini Mwenyezi Mungu na kutaka malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu atasamehewa katika yaliyotangulia katika madhambi yake.”³

Kushuka kwa Malaika na Kuhukumiwa Kila Jambo la Kheri katika Usiku wa Cheo.

Na Kauli Yake Allah تعالى،

تَنْزِلُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ ﴿١٠٠﴾

“Huteremka Malaika na Roho (katika usiku huo) kwa Idhini ya Mola Wao Mlezi kwa kila jambo.”

Maana yake: Kunakuwa kwingi kushuka kwa malaika katika usiku huu kwa sababu ya wingi wa baraka zake. Na Malaika wanashuka pamoja na kushusha baraka na rahma, kama wanavyoshuka wakati wa kusoma Qur’an. Na wanavizunguka vikundi vya kumtaja Allah تعالى na wanaziweka chini mbawa zao kwa mwenye kutafuta elimu kwa ukweli kwa ajili ya kumtukuza.

¹ Ahmad 2:230. (Kuna ushahidi wa Hadithi hii katika vitabu vya *Sunan* kutokana na Hadithi ya Anas bin Malik رضي الله عنه.)

² An-Nasai 4:129.

³ *Fat’hul Al-Bari* 4:294, na Muslim 1:523.

Ama Roho imesemwa hapa kuwa ni Jibril عليه السلام kwa hiyo maneno hapa yamekuja katika mbinu ya kilugha. Maana: ametajwa pekee Jibril عليه السلام licha ya kuwa ni katika Malaika. Imefanywa hivyo kutokana na utukufu wake.

Na Kauli Yake Allah تعالى،

مِنْ كُلِّ أَمْرٍ ﴿٤﴾

“...kwa kila jambo...”

Amesema Mujahid: Usiku huo ni amani ya kila jambo. Na amesema Saiid Bin Mansour: Ametuzungumzia Issa bin Yunus, ametuzungumzia Aamesh kutoka kwa Mujahid katika Kauli Yake،

سَلَّمَ هِيَ

“Amani usiku huo..”

Amesema usiku huo ni wenye kusalimika, hauwezi shetani kufanya uovu ndani ya usiku huo au kufanya maudhi. Na amesema Qatada na wengine: Huhukumiwa mwanadamu ndani yake mambo na hukadiriwa ajali na rizki.

Kama Alivyosema Allah تعالى؛

فِيهَا يُفْرَقُ كُلُّ أَمْرٍ حَكِيمٍ ﴿٥﴾

“Katika usiku huu hubainishwa kila jambo la hikima.” (44:4)

Na Kauli Yake تعالى،

سَلَّمَ هِيَ حَتَّىٰ مَطَلَعِ الْفَجْرِ ﴿٦﴾

“Amani usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajiri.”

Amesema Saiid bin Mansour, amesema ametuzungumzia Hushaym kutoka kwa Shuaib katika Kauli Yake Allah تعالى،

مِنْ كُلِّ أَمْرٍ ﴿٦﴾ سَلَّمَ هِيَ حَتَّىٰ مَطَلَعِ الْفَجْرِ ﴿٧﴾

“Huteremka Malaika na Roho (katika usiku huo) kwa idhini ya Mola Wao Mlezi kwa kila jambo. Amani usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajiri.”

Amesema wanatoa salamu Malaika katika usiku wa cheo kwa watu wa misikiti mpaka kuchomoza kwa Alfajiri.

Na amesema Qatada na Ibn Zaid Katika Kauli Yake تعالى،

سَلَّمُ هِيَ

“Amani usiku huo...”

Anakusudia kwamba usiku huo wote kuwa ni kheri na hapana ndani yake shari yoyote mpaka kuchomoza kwa Alfajiri.

Kuuainisha Usiku wa Cheo na Alama Zake

Yanatilia nguvu jambo hili Hadithi iliyopokewa na Imam Ahmad kutoka kwa Ubada bin Swamit رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«لَيْلَةُ الْقَدْرِ فِي الْعَشْرِ الْبَوَاقِي، مَنْ قَامَهُنَّ ابْتِغَاءَ جَسَبِيَهِنَّ فَإِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ وَمَا تَأَخَّرَ، وَهِيَ لَيْلَةٌ رُبَّ: تِسْعٍ أَوْ سَبْعٍ أَوْ خَامِسَةٍ أَوْ ثَالِثَةٍ أَوْ آخِرِ لَيْلَةٍ»

“Usiku wa cheo unapatikana katika siku kumi za mwisho, mwenye kusimama katika siku hizo, kwa kutaka malipo yake kwa hakika Mwenyezi Mungu Atamsamehe yaliyotangulia katika madhambi yake na yaliyokuja nyuma, na huo ni usiku wa witri, usiku wa tisa au wa saba au wa tano au wa tatu au usiku wa mwisho.”

Na amesema Mtume ﷺ،

«إِنَّ أَمَارَةَ لَيْلَةِ الْقَدْرِ أَنَّهَا صَافِيَةٌ بَلْجَةٌ، كَأَنَّ فِيهَا قَمَرًا سَاطِعًا، سَاكِتَةٌ سَاجِدَةٌ، لَا يَزْدُ فِيهَا وَلَا حَرٌّ، وَلَا يَحِلُّ لِكُوكَبٍ يُرْمَى بِهِ فِيهَا حَتَّى يُضِيحَ، وَإِنَّ أَمَارَتَهَا أَنَّ الشَّمْسَ صَبِيحَتَهَا تَخْرُجُ مُسْتَوِيَةً لَيْسَ لَهَا شُعَاعٌ، مِثْلَ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ، وَلَا يَحِلُّ لِلشَّيْطَانِ أَنْ يَخْرُجَ مَعَهَا يَوْمَئِذٍ»

“Kwa hakika alama ya usiku wa cheo ni kwamba usiku wake unakuwa safi wenye mwanangaza, kana kwamba ndani yake pana mwezi wenye kuangaza, usiku huo ni mtulivu sana, hapana baridi ndani yake wala joto, kimondo hakiruhusiwi kutupwa katika usiku

huo mpaka asubuhi, na kwa hakika alama yake ni kwamba jua katika asubuhi linachomoza hali ya kuwa sawasawa halina mionzi mfano wa usiku wa mbalamwezi, wala shetani haruhusiwi kutoka pamoja nalo (jua) katika siku hiyo.”¹

Hadithi hii Isnadi yake ni Hasani. Matini yake pana tatizo la nyongeza ya maneno na katika baadhi ya matamshi kuna utata na ukakasi.

Ametarujumi Abu Dawuud katika suna yake kwa kusema, “Mlango wa kuweka Wazi kwamba Usiku wa Cheo Unapatikana katika Ramadhan Yote” Kisha amepokea kutoka kwa Abdillahi bin Umar رضي الله عنه amesema aliulizwa Mtume ﷺ hali ya kuwa mimi ninasikia kuhusu usiku wa cheo akasema,

«هِيَ فِي كُلِّ رَمَضَانَ»

“Usiku huo unapatikana katika Ramadhan yote.”²

Wapokezi wa Hadithi hii wote ni wa kweli. Isipokuwa Abu Dawuud, amesema; amepokea hadith hii Shuhba na Sufyan kutoka kwa Abuu Is’haq wakaifanya *Mawquuf*. Na imepokewa kutoka kwa Abuu Saiid Khudhry رضي الله عنه amesema, “Alikaa Itikafu Mtume ﷺ katika kumi la kwanza katika mwezi wa Ramadhan, na sisi tukakaa itikafu pamoja naye. Jibril عليه السلام akamjia akamuambia hakika kile unachokitafuta kiko mbele yako, akakaa itikafu kumi la pili, tukakaa itikafu pamoja naye. Jibril عليه السلام akamjia akamuambia ambacho unakitafuta kiko mbele yako. Kisha akasimama Mtume ﷺ hali ya kuhutubia asubuhi ya mwezi ishirini katika mwezi wa Ramadhan akasema;

«مَنْ تَمَانَ اعْتَكَفَ مَعِيَ فَلْيَرْجِعْ فَإِنِّي رَأَيْتُ لَيْلَةَ الْقَدْرِ، وَإِنِّي أَنْسِيْتُهَا، وَإِنَّهَا فِي الْعَشْرِ الْأَوَّخِرِ فِي وَتْرٍ، وَإِنِّي رَأَيْتُ كَأَنِّي أَسْجُدُ فِي طِينٍ وَمَاءٍ»

“Ambaye amekuwa amekaa itikaf pamoja nami na arejee kwa hakika mimi nimeuona usiku wa cheo, na hakika mimi nimesahaulishwa usiku huo na unapatikana katika kumi la mwisho katika witr na hakika mimi nimeona kana kwamba ninasujudu katika udongo na maji.”

¹ Ahmad 5:324. (ni katika mapokezi ya Mursal).

² Abu Dawud 2:111.

Na ilikuwa sakafu ya juu ya msikiti ni matawi ya mtende na hatuoni mbinguni kitu chochote, kikaja kipande cha wingu tukanyeshewa na mvua. Mtume ﷺ akasali pamoja nasi, nikaona athari ya udongo na maji katika bapa la uso wa Mtume ﷺ ikiwa ni uthibitisho wa ndoto yake na katika tamko katika asubuhi ya siku ya ishirini na moja, wameitoa katika sahihi mbili.¹

Shafii رحمه الله تعالى amesema hadithi hii upokezi wake ni sahihi zaidi. Na pamesemwa ni usiku wa mwezi ishirini na tatu kutokana na hadithi ya Abdullah bin Unaisi رضي الله عنه katika sahihi ya Muslim.² Na limesemwa unakuwa usiku wa ishirini na tano kutokana na alivyoyapokea Bukhari kutoka kwa Abdallah bin Abbas رضي الله عنهما kwamba Mtume ﷺ amesema;

«التَّمِسُّونَا فِي الْعَشْرِ الْأَوَاخِرِ مِنْ رَمَضَانَ فِي تَاسِعَةِ تَبَقَى، فِي سَابِعَةِ تَبَقَى، فِي خَامِسَةِ تَبَقَى»

“Utafuteni usiku huo katika siku kumi za mwisho katika mwezi wa Ramadhan, katika siku ya tisa zinazobaki, katika siku ya saba zinazobaki, katika siku ya tano zinazobaki.”³

Wamefasiri watu wengi kuwa siku hizo ni *witr* na maelezo yao ni dhahiri zaidi na nimeshauri zaidi, na imesemwa kwamba usiku huo, umo katika shufwa kama ilivyopokelewa na Muslim katika sahihi yake kutoka kwa Abu Said رضي الله عنه kwamba yeye amechukulia hivyo.⁴

Na imesemwa kwamba ni usiku wa ishirini na saba. Kutokana na Hadithi ya Muslim katika sahihi yake kutoka kwa Ka'ab رضي الله عنه, kutoka kwa Mtume ﷺ: ‘Kuwa ni usiku wa ishirini na saba.’

Na amepokea imamu Ahmad kutoka kwa Zirr nimemuuliza Ubayy bin Kaab رضي الله عنه nikasema; ‘Ewe!! Abal Mundhir hakika ndugu yako Ibnu Masuudi رضي الله عنه anasema; Mwenye kusali Sala za usiku kwa mwaka mzima ataupata

¹ *Fat'hul Al-Bari* 4:329, 318, na Muslim 2:824.

² Muslim 2:827.

³ *Fat'hul Al-Bari* 4:306.

⁴ Muslim 2:826 - 827.

usiku wa cheo.’ Akasema Allah تعالى Amrehemu, ‘kwa hakika amejua kwamba usiku huo umo katika Mwezi wa Ramadhani na huo ni usiku wa ishirini na saba. ‘ Kisha akaapa nikasema; ‘Vipi mnalijuwa hilo?’ Akasema, ‘kwa alama au kwa kielezo ambacho tumeelezwa ni kwamba, ‘Jua linachomoza siku hiyo likiwa halina mionzi.”¹ Ameipokea Muslim.²

Na panasemwa kwamba usiku huo unakuwa katika usiku wa mwezi ishirini na tisa. Na amepokea Imamu Ahmad Bin Hanbal, kutoka kwa Ubayy Bin Swamiti رضي الله عنه, kwamba yeye alimuuliza Mtume ﷺ kuhusu usiku wa cheo akasema Mtume ﷺ,

«فِي رَمَضَانَ فَاتَمِسُوهَا فِي الْعَشْرِ الْأَوَاخِرِ، فَإِنَّهَا فِي وَثْرِ إِحْدَى وَعِشْرِينَ، أَوْ ثَلَاثَ وَعِشْرِينَ، أَوْ خَمْسَ وَعِشْرِينَ، أَوْ سَبْعَ وَعِشْرِينَ، أَوْ تِسْعَ وَعِشْرِينَ، أَوْ فِي آخِرِ لَيْلَةٍ»

“Utafuteni katika Ramadhani katika kumi la mwisho, kwani huo upo katika witiri ya ishirini na moja, au ishirini na tatu, au ishirini na tano, au ishirini na saba, au ishirini na tisa au usiku wake wa mwisho.”³

Imamu Ahmad pia ameandika kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema kuhusu usiku wa cheo,

«إِنَّهَا لَيْلَةٌ سَابِعَةٌ أَوْ تَاسِعَةٌ وَعِشْرِينَ، وَإِنَّ الْمَلَائِكَةَ تِلْكَ اللَّيْلَةَ فِي الْأَرْضِ أَكْثَرَ مِنْ عَدَدِ الْحَصَى،»

“Ni usiku wa ishirini na saba au ishirini na tisa, na Malaika usiku huo katika ardhi ni wengi sana kuliko idadi ya changarawe.”⁴

Ameipokea peke yake hadithi hii Ahmad, na upokezi wake hauna matatizo yoyote.

Na amepokea Attirmidhy kutoka kwa Abi Qilaba kwamba yeye amesema: “Usiku wa cheo una hamahama katika siku kumi za mwisho.” Na hizo ndizo

¹ Ahmad 5:130.

² Muslim 2:828.

³ Ahmad 5:318.

⁴ Ahmad 2:519.

ambazo amezisimulia Abuu Qilaba. Pia amezisema juu yake Malik, Atthaury, Ahmad bin Hanbal, Is'haq bin Raahawaini, Abu Thaury, Al Muzani na Abubakar bin Khuzaima na wengineo, Allah تعالى Awarehemu. Na pia zimezungumziwa kutoka kwa Shafii ameyanukuu kutoka kwa Al-Qadh, nayo yanafanana sana. Na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Maombi ya Usiku wa Cheo.

Na jambo lenye kusuniwa ni kuzidisha katika kuomba katika nyakati zote katika mwezi wa Ramadhan. Kila mtu afanye wingi sana kuomba katika kumi la mwisho katika mwezi wa Ramadhan, kisha katika witr zote aombe zaidi. Na inasuniwa kuzidisha kuomba Dua hii.

“Eee!! Mola wangu wa haki hakika wewe ni msamehevu sana unapenda kusamehe kwa hiyo nisamehe.”

Kutokana na Hadithi iliyonukuliwa na Imam Ahmad kwamba Aisha رضي الله عنها amesema; ‘Ewe!! Mtume iwapo nitaupata usiku wa cheo ni jambo gani niombe?’ Akasema;

«قُولِي: اللَّهُمَّ إِنَّكَ عَفُوٌّ تُحِبُّ الْعَفْوَ فَاعْفُ عَنِّي»

“Sema; Ewe!! Mola Wangu wa haki hakika Wewe ni Msamehevu sana Unapenda Kusamehe nisamehe.”¹

Na amepokea Attirmidhy na Annasai na Ibnu Majah na amesema Attirmidhy; Hadithi hii daraja lake ni Hasan sahihi.² Na ameithibitisha Hakim katika kitabu chake Mustadrak, na amesema: Hii ni hadithi sahihi juu ya sharti ya Bukhari na Muslim.³ Na amepokea An-Nasai vilevile.⁴

Huu ni mwisho wa tafsir ya *Suratu Laylatul Qadr*, na kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.



¹ Ahmad 6:182.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:495, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:218, na Ibn Majah 2:1265.

³ Al-Hakim 1:530.

⁴ An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:219.

Tafsiri ya Suratu Lam Yakun (Al-Bayyinah)¹ Sura ya 98 Iliteremshwa Madinah

Mtume ﷺ Kumsomea Sura hii Ubayy رضي الله عنه.

Amepokea Imam Ahmad kwamba Anas bin Malik رضي الله عنه amesema; amesema Mtume ﷺ kumuambia Ubayy bin Kaab رضي الله عنه,

«إِنَّ اللَّهَ أَمَرَنِي أَنْ أَقْرَأَ عَلَيْكَ ﴿لَمْ يَكُنِ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ﴾»

'Hakika Mwenyezi Mungu Ameniamrisha nikusomee.' ***"Hawakuwa waliokufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu,.."***

Ubayy رضي الله عنه akasema; "Na Amenitaja kwako?" Akasema;

«نَعَمْ»

"Ndiyo"

Akalia.² Ameipokea Bukhari na Muslim, na Attirmidh na Anas رضي الله عنهم kutokana na hadithi ya Shuaiba رضي الله عنه.³

* * *

¹ Sura hii pia inajulikana kama Al-Bayyinah.

² Ahmad 3:130.

³ *Fat'hul Al-Bari* 8:597, *Muslim* 1:550, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 10:294, na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:520.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْبَيِّنَاتِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

لَمْ يَكُنِ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ مُنْفِكِينَ
 حَتَّى تَأْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ ۖ رَسُولٌ مِّنَ اللَّهِ يَتْلُوا صُحُفًا مُّطَهَّرَةً
 ۖ فِيهَا كُتُبٌ قَيِّمَةٌ ۖ وَمَا تَفَرَّقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ
 إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنَةُ ۖ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا
 اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا
 الزَّكَاةَ ۚ وَذَلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ ۖ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ
 الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ فِي نَارِ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ أُولَئِكَ
 هُمْ شُرَكَاءُ الْبَرِيَّةِ ۖ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
 أُولَئِكَ هُمْ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ ۖ

لَمْ يَكُنِ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ
 الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ مُنْفِكِينَ حَتَّى
 تَأْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ ۖ رَسُولٌ مِّنَ اللَّهِ
 يَتْلُوا صُحُفًا مُّطَهَّرَةً ۖ فِيهَا كُتُبٌ
 قَيِّمَةٌ ۖ وَمَا تَفَرَّقَ الَّذِينَ أُوتُوا
 الْكِتَابَ إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمْ
 الْبَيِّنَةُ ۖ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا
 اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ
 وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ ۚ
 وَذَلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ ۖ

1. Wale waliokufuru miongoni mwa Watu wa

Kitabu na washirikina hawataacha walionayo mpaka iwajie bayana.

2. Yaani Mtume aliyetoka kwa Mwenyezi Mungu anayewasomea kurasa zilizotakasika.

3. Ndani yake mna maandiko yaliyonyooka.

4. Wala hawakufarikiana waliopewa Kitabu ila baada ya kuwajia hoja zilizo wazi.

5. Nao hawakuamrisha kitu ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu, na washike Swala, na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Dini madhubuti.

Kutaja Hali ya Makafiri Miongoni mwa Watu wa Kitabu na Washirikina

Ama watu wa Kitabu, hao ni mayahudi na manaswara. Na washirikina ni wale wanaoabudu masanamu katika Waarabu na Waajemi. Amesema Mujahid;

مُنْفَكِينَ

“Hawakuwa ni weye kuachana.”

Anakusudia wenye kukoma mpaka itakapo wadhihirikia haki² na kama hivyo amesema Qatada;¹

حَتَّى تَأْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ ﴿١﴾

“Mpaka itakapowajia hoja iliyowazi.”

Maana yake: Hii Qur’an na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى;

لَمْ يَكُنِ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ مُنْفَكِينَ حَتَّى تَأْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ ﴿١﴾

“Hawakuwa waliokufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu na washirikina waache walionayo mpaka iwajie bayana.”

Kisha Ameifasiri hoja hiyo,

رَسُولٌ مِنَ اللَّهِ يَتْلُو صُحُفًا مُطَهَّرَةً ﴿٢﴾

“Mtume aliyetoka kwa Mwenyezi Mungu anayewasomea kurasa zilizotakasika.”

Anamkusudia Muhammad ﷺ na kile anachokisoma ni Qur’an tukufu ambayo imeandikwa huko mbinguni katika nyaraka zenye kutakaswa. Kama Kauli Yake,

فِي صُحُفٍ مُكْرَمَةٍ ﴿٣﴾ مَرْفُوعَةٍ مُطَهَّرَةٍ ﴿٤﴾ بِأَيْدِي سَفَرَةٍ ﴿٥﴾ كِرَامٍ بَرَرَةٍ ﴿٦﴾

“Yamo katika kurasa zilizohishimiwa. Zilizoinuliwa, zilizotakaswa. Zimo mikononi mwa Malaika waandishi. Watukufu, wema.”

¹ At-Tabari 24:539.

² At-Tabari 24:539.

Na Kauli Yake Allah تعالى،

فِيهَا كُتِبَ قِيَمَةٌ ﴿١٠٥﴾

“Ndani yake mna maandiko yaliyonyooka.”

Amesema Ibnu Jariir رحمه الله تعالى: maana katika nyaraka zilizotakaswa pana maandishi kutoka kwa Allah تعالى، yenye unyoofu, yalio sawasawa yenye kunyooka. Hamna ndani yake makosa yoyote kwa sababu maandishi hayo yanatoka kwa Allah تعالى Mwenye Kushinda Mwenye Utukufu.¹

Kulitokea Kotofautiana Baada ya Kuja Elimu.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَمَا تَفَرَّقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنَةُ ﴿١٠٦﴾

“Wala hawakufarikiana waliopewa Kitabu ila baada ya kuwajia hoja zilizo wazi.”

Kama Kauli Yake Allah تعالى،

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ تَفَرَّقُوا وَاخْتَلَفُوا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنَةُ ؕ وَأُولَٰئِكَ هُمُ عَدَاؤُ

عَظِيمٌ ﴿١٠٧﴾

“Wala msiwe kama wale waliofarikiana na kukhitalifiana baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi. Na hao ndio watakaokuwa na adhabu kubwa.” (3:105)

Anawakusudia kwa maneno hayo watu wa vitabu vilivyoteremshwa kwa umma zilizokuwa kabla yetu. Baada ya kuwa Allah تعالى Amewasimamishia hoja na ubainifu walifarakana na wakatofautiana na katika lile Alilotaka Allah تعالى katika vitabu vyao. Haikuwa ni tofauti ndogo bali ni nyingi sana.

Kama ilivyokuja katika Hadithi iliyopokelewa kwa njia nyingi sana.

¹ At-Tabari 24:540.

«إِنَّ الْيَهُودَ اخْتَلَفُوا عَلَى إِحْدَى وَسَبْعِينَ فِرْقَةً، وَإِنَّ النَّصَارَى اخْتَلَفُوا عَلَى اثْنَتَيْنِ وَسَبْعِينَ فِرْقَةً، وَسَنَفَتِرُقُ هَذِهِ الْأُمَّةُ عَلَى ثَلَاثٍ وَسَبْعِينَ فِرْقَةً، كُلُّهَا فِي النَّارِ إِلَّا وَاحِدَةً»

“Kwa hakika Mayahudi walifarakana juu ya vikundi sabini. Na moja wa Manaswara walifarakana vikundi sabini na viwili, na utafarakana umma huu makundi sabini na tatu, makundi yote yatakuwa motoni isipokuwa moja.”

Wakasema: ‘Ni akina nani hao? Ee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?’ Akasema:

«مَا أَنَا عَلَيْهِ وَأَصْحَابِي»

“Lile ambalo mimi na masahaba wangu tuko juu yake.”¹

Lengo la Amri ya Allah تعالى ni Kumtakasia Dini

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَمَا أُمْرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

“Nao hawakuamrisha kitu ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Dini.”

Kama Kauli Yake nyingine,

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢١﴾

“Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.”
(21:25)

Na kwa hiyo Amesema,

حُنْفَاءُ

“Wawe waongofu.”

Maana: Hali ya kujiepusha na shirki na kuelekea kwenye Tauhidi. Kama Kauli Yake,

¹ Qurtubi 4:159 na 160.

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ^ط

“Na kwa hakika kwa kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani.” (16:36)

Yametangulia maelezo ya maana halisi ya *Al-Hanif*, katika *Surat Al-An'aam*. Kwa kiasi cha kutosheleza na hakuna haja ya kuyafafanua tena hapa.¹

وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ

“Na washike Sala.”

Na hiyo ni katika ibada tukufu kabisa za kiwiliwili na,

وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ^ك

“Na watoe Zaka.”

Zaka ni kuwafanyia wema Mafukara wenye haja,

وَذَلِكَ دِينُ الْقِيَمَةِ ﴿٨﴾

“Na hiyo ndiyo Dini madhubuti.”

Maana yake: Mila iliyonyooka iliyo sawasawa au umma ulionyooka unaolingania usawa na uadilifu.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ فِي نَارِ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا أُولَئِكَ هُمْ شَرُّ الْبَرِيَّةِ ﴿٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَئِكَ هُمْ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ ﴿٧﴾ جَزَاءُ هُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنَّاتُ عَدْنٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا^ط رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ذَلِكَ لِمَنْ حَشِيَ رَبَّهُ ﴿٨﴾

6. “Hakika waliokufuru miongoni mwa Watu wa Kitabu na washirikina wataingia katika Moto wa Jahannamu wadumu milele humo. Hao ndio viumbe waovu kabisa.

7. Hakika walioamini na wakatenda mema, hao ndio bora wa viumbe.

8. Malipo yao kwa Mola Wao Mlezi ni Bustani za daima, zipitazo mito kati yake. Wakae humo milele. Mwenyezi Mungu Yu radhi nao, na wao waradhi Naye. Hayo ni kwa anayemuogopa Mola Wake Mlezi.”

Kutajwa Viumbe Waovu na Wema Pamoja na Malipo Yao

Allah تعالى Anaeleza kuhusu marejeo ya waovu miongoni mwa makafiri wa watu wa kitabu na mushirikina, wenye kwenda kinyume na vitabu vya Allah تعالى Vilivyoteremshwa na Mitume wa Allah تعالى waliopelekwa kwao. Kwamba wao siku ya Qiyama watakuwa katika moto wa Jahanam – hali ya kuishi humo milele. Maana: Watakaa, hawatabadilishiwa humo na hawataondoka.

أُولَئِكَ هُمْ شَرُّ الْبَرِيَّةِ ﴿٩٨﴾

“Hao ndio viumbe waovu kabisa.”

Maana yake: Shari ya viumbe ambao Amewaumba Allah تعالى. Kisha Allah تعالى Anaelezea kuhusu hali za watu wema ambao wameamini kwa nyoyo zao, na wanatenda matendo mema kwa miili yao kwamba wao ni viumbe bora. Abu Hurairah رضي الله عنه na kundi miongoni mwa wanazuoni wametolea ushahidi aya hii juu ya kufanywa bora waumini miongoni mwa watu kuliko Malaika. Kwa Kauli Yake تعالى:

أُولَئِكَ هُمْ شَرُّ الْبَرِيَّةِ ﴿٩٩﴾

“Hao ndio bora wa viumbe.”

Kisha baada ya hapo Allah تعالى Akasema,

جَزَاءُ هُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ

“Malipo yao kwa Mola Wao Mlezi.”

Maana yake: Malipo yao ni siku ya Qiyama.

جَنَّتُ عَدْنٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ط

“Ni Bustani za daima, zipitazo mito kati yake. Wakae humo milele.”

Maana yake: Pasi na kupambanuka wala kukoma wala kumalizika.

رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ

“Mwenyezi Mungu Yu radhi nao.”

Na daraja ya radhi yake kwao liko juu kuliko yale yote ambayo wamepewa miongoni mwa neema zenye kudumu.

وَرَضُوا عَنْهُ

“Na wao wa radhi Naye.”

Katika yale Aliyowapa miongoni mwa neema zenye kuenea. Kisha baada ya hapo Allah تعالى Akasema,

ذَلِكَ لِمَنْ حَشِيَ رَبَّهُ

“Hayo ni kwa anayemuogopa Mola Wake Mlezi.”

Maana yake: Malipo haya yanapatikana kwa mwenye kumcha Allah تعالى na akamcha kwa ukweli wake na akamuabudu kana kwamba anamuona, na anajua kwamba iwapo hamuoni hakika Yeye Anamuona. Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Hurairah عنه رضي الله عنه amesema: amesema Mtume ﷺ,

«أَلَا أُخْبِرُكُمْ بِخَيْرِ الْبَرِيَّةِ؟»

“Hivi si wapi Khabari kuhusu viumbe bora?”

Masahaba wakajibu tueleze. Mtume ﷺ akasema,

«رَجُلٌ آخَذَ بِعَنَانٍ فَرَسِهِ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، كُلَّمَا كَانَتْ هَيْعَةً اسْتَوَى عَلَيْهِ. أَلَا أُخْبِرُكُمْ بِخَيْرِ الْبَرِيَّةِ؟»

“Huyo ni mtu aliyekamata hatamu ya farasi wake katika njia za Mwenyezi Mungu kila inapopatikana sauti ya fazaa anampanda farasi huyo, hivi si waelezi anayemfuatia huyo kwa ubora?”

Wakasema tuelezee: Mtume ﷺ akasema:

«رَجُلٌ فِي ثَلَاثَةِ مِائَةٍ مِنَ الْبَرِيَّةِ، يُقِيمُ الصَّلَاةَ وَيُؤْتِي الزَّكَاةَ. أَلَا أُخْبِرُكُمْ بِشَرِّ الْبَرِيَّةِ؟»

“Huyo ni mtu aliye katika kundi la mbuzi wake anasimamisha Sala na anatoa Zaka. Hivi nisiwaeleze kuhusu muovu wa viumbe?”

Masahaba wakasema, 'Tuelezee ewe Mtume.' Mtume ﷺ akasema,

«الَّذِي يُسْأَلُ بِاللهِ وَلَا يُعْطَى بِهِ»

"Ni yule mtu ambaye anaombwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu lakini hatoi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu".¹

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Lamyakun*, ni kwa Allah تعالى Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹ Ahmad 2:396.

Tafsiri ya Suratu Idha Zulzilati

Sura ya 99

Iliteremshwa Makkah

Ubora wa Suratu Az-Zalzalah

Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Abdillah bin Amri رضي الله عنه amesema: Alikwenda mtu mmoja kwa Mtume ﷺ akasema: Nisomee ewe Mtume ﷺ akamuambia:

«اقْرَأْ ثَلَاثًا مِنْ ذَوَاتِ الرَّءِ»

“Soma Sura tatu, katika sura zenye kuanzia na Alif Lam Raa.”

Mtu yule akasema kumuambia Mtume ﷺ, ‘Mimi ni mtu mzima sasa, moyo wangu umekuwa mgumu na ulimi wangu umekuwa mzito.’ Mtume ﷺ akamuambia,

«فَأَقْرَأْ مِنْ ذَوَاتِ حَمِّ»

“Soma katika sura zilizoanza na Haamim.”

Akasema yule mtu mfano wa maneno yake ya mwanzo. Mtume ﷺ akamuambia,

«اقْرَأْ ثَلَاثًا مِنَ الْمُسَبِّحَاتِ»

“Soma sura tatu zenye kuanza na Sabbaha”

Akasema mfano wa maneno yake ya kwanza. Bwana yule akamuambia Mtume ﷺ, “Ewe Mtume nisomeshe sura yenye kukusanya.” Mtume ﷺ akamsomesha,

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا

“Itakapotetemeshwa ardhi kwa mtetemeko wake!”

Mpaka alipomaliza. Bwana yule akasema, ‘Naapa kwa yule aliyekupeleka kwa ukweli hali ya kuwa Mtume, sitaongeza juu ya sura hii milele.’ Kisha akaenda zake, akasema Mtume ﷺ,

«أَفْلَحَ الرَّوْثِيُّ، أَفْلَحَ الرَّوْثِيُّ»

“Kamefuzu kale kamtu, kamefuzu kale kamtu.”

Kisha akasema:

«عَلَيْ بِهِ»

“Nileteeni mtu huyo” Akamjia akamuambia,

«أَمْرٌ بِبَيِّنَاتٍ لِّأَنَّ اللَّهَ جَعَلَهُ عَيْدًا لِّهَذِهِ الْأُمَّةِ»

“Mwenyezi Mungu Ameniamrisha katika siku ya Al-Adhhaa kuwa ni sikuukuu ya Iddi kwa Umma huu.”

Mtu yule akasema, “Jee unaonaje kama sikumpata isipokuwa ngamia mwenye kutoa maziwa jee nimchinje Ngamia huyo?” Mtume ﷺ Akamjibu,

«لَا، وَلَكِنَّكَ تَأْخُذُ مِنْ شَعْرِكَ وَتَقْلَمُ أَظْفَارَكَ وَتَقْصُرُ شَارِبَكَ وَتَخْلِقُ عَانَتَكَ فَمَاذَا تَمَامُ أَضْحِيَّتِكَ عِنْدَ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

“Hapana, isipokuwa ni kwamba wewe punguza nywele zako, kata kucha zako, na upunguze masharubu yako, na kunyoa kinena chako. Kwa kufanya hivyo ni ukamilifu wa kuchinja kwako mbele ya Mwenyezi Mungu, Mwenye Kushinda, Mwenye Utukufu”¹

Ameithibitisha Abu Dawuud na An-Nasai.²

* * *

¹ Ahmad 2:169.

² Abu Dawuud 2:119 na An-Nasai katika Al-Kubra 5:16.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الزَّلْزَلَةِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ① وَأَخْرَجَتِ الْأَرْضُ أَثْقَالَهَا ②
 وَقَالَ الْإِنْسَانُ مَا هَٰذَا ③ يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا ④
 بِأَنَّ رَبَّكَ أَوْحَىٰ لَهَا ⑤ يَوْمَئِذٍ يَصُدُّ النَّاسُ ⑥
 أَسْتَأْتًا لِّيَوْمِ أَعْمَلْتُمْ ⑦ فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا ⑧
 يَرَهُ ⑨ وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ⑩

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ①
 وَأَخْرَجَتِ الْأَرْضُ أَثْقَالَهَا ②
 وَقَالَ الْإِنْسَانُ مَا هَٰذَا ③ يَوْمَئِذٍ
 تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا ④ بِأَنَّ رَبَّكَ
 أَوْحَىٰ لَهَا ⑤ يَوْمَئِذٍ يَصُدُّ النَّاسُ
 أَسْتَأْتًا لِّيَوْمِ أَعْمَلْتُمْ ⑦ فَمَنْ
 يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ⑧
 وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ⑩

1. Itakapotetemeshwa ardhi kwa mtetemeko wake!
2. Na itakapotoa ardhi mizigo yake!
3. Na mtu akasema: Ina nini?
4. Siku hiyo itahadithia khabari zake.
5. Kwa sababu Mola Wake Mlezi Ameifunulia!
6. Siku hiyo watu watatoka kwa mfarakano vikundi kwa vikundi wakaoneshwe vitendo vyao!
7. Basi anayetenda chembe ya wema, mfano wa mdudu chungu atauona!
8. Na anayetenda chembe ya uovu mfano wa mdudu chungu atauona!"

Siku ya Qiyama na Mambo Yatakuwa ndani Yake, Hali ya Ardhi na ya Watu.

Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema:

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ﴿١﴾

“Itakapotetemeshwa ardhi kwa mtetemeko wake!”

Maana yake: Ikatikisika kwa chini yake.¹

وَأَخْرَجَتِ الْأَرْضُ أَثْقَالَهَا ﴿٢﴾

“Na itakapo toa ardhi mizigo yake!”

Anakusudia ikavitupa vilivyo ndani yake miongoni mwa wafu. Ameyasema hayo zaidi ya mmoja katika wanawazuoni waliotangulia.

Na aya hii ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ آتِفُوقًا رَبِّكُمْ ؕ إِنَّ زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيمٌ ﴿١﴾

“Enyi watu! Mcheni Mola Wenu Mlezi. Hakika tetemeko la Saa (ya Kiyama) ni jambo kuu.” (22:1)

Na Kama Kauli Yake تعالى:

وَإِذَا الْأَرْضُ مُدَّتْ ﴿١﴾ وَأَلْقَتْ مَا فِيهَا وَتَخَلَّتْ ﴿٢﴾

“Na ardhi itakapotanuliwa, na kuvitoa vilivyokuwa ndani yake, ikawa tupu,...”. (84:3-4)

Muslim amepokea katika sahihi yake kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه Mtume ﷺ amesema,

«تُلْقِي الْأَرْضُ أَوْلَادَ كَبِدِمَا أَثْقَالَ الْأَسْطُورَانِ مِنَ الذَّمْبِ وَالْفِضَّةِ، فَيَجِيءُ الْقَائِلُ قَيُّوْلُ فِي هَذَا قَتَلْتُ، وَيَجِيءُ الْقَاطِعُ قَيُّوْلُ فِي هَذَا قَطَعْتُ رَجِيْمِي، وَيَجِيءُ السَّارِقُ قَيُّوْلُ: فِي هَذَا قَطَعْتُ يَدِي، ثُمَّ يَدْعُوْنَهُ فَلَا يَأْخُذُوْنَ مِنْهُ شَيْئًا»

¹ Adurr Al-Manthuur 8:592.

*"Itatapika. Ardhi itatoa vitu mfano wa sahani za dhahabu na fedha. Kisha atakuja muuaji na atasema, 'Katika jambo hili nimemuua huyu.' Na atakuja mvunja udugu nae atasema, 'Kwa ajili hii nilikata udugu.' Kisha atakuja mwizi nae atasema, 'Kwa ajili hii nilikatwa mkono.' Kisha wataomba na wasipate kitu.'*¹

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

وَقَالَ الْإِنْسَانُ مَا لَهَا ﴿١٠٠﴾

"Na mtu akasema: Ina nini?"

Maana yake: Atalikana jambo la ardhi baada ya kuwa ilikuwa imetulizana, imethibiti na hali ya kuwa yeye ametulizana juu ya mgongo wake. Kwa maana: Imebadilika hali, kwa hiyo imekuwa inatikusika, inatetemeka, inafuata maagizo ya Allah تعالیٰ. Ameandalia hiyo ardhi tetemeko ambalo mwanadamu hawezi kulikwepa, kisha ikavitupa vilivyo ndani yake miongoni mwa wafu wa mwanzo na wa mwisho. Na wakati huo watu watakhofu na kubabaika juu ya jambo la ardhi na kubadilika, Ardhi ikawa siyo ardhi, na mbingu ikabadilika na wakadhihiri watu kwa Allah تعالیٰ Aliye Mmoja Mwenye Kutenza Nguvu.

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا ﴿١٠١﴾

"Siku hiyo itahadithia khabari zake".

Maana yake: Itayazungumzia mambo yaliyotendeka juu yake kwa wenye kutenda. Amepokea Al-Imamu Ahmad na Tirmidhi na Abu Abdul Rahman An-Nasai. Na tamko ni lake kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema kuhusu Aya hii,

يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا ﴿١٠١﴾

"Siku hiyo itahadithia khabari zake". Amesema,

«أَتَدْرُونَ مَا أَخْبَارُهَا؟»

"Je mnajua ni zipi khabari zake?"

¹ Muslim Na. 1013.

Wakasema: Allah تعالى na Mjumbe Wake wanajua mno. Mtume ﷺ akasema,

«فَإِنَّ أَخْبَارَهَا أَنْ تَشْهَدَ عَلَى كُلِّ عَبْدٍ وَأَمَةٍ بِمَا عَمِلَ عَلَى ظَهْرِهَا أَنْ تَقُولَ: عَمِلَ
كَذًا وَكَذًا يَوْمَ كَذَا وَكَذَا، فَهَذِهِ أَخْبَارُهَا»

“Kwa Hakika khabari zake ni kushuhudia juu ya kila mja na mjakazi kwa yale aliyoyatenda. Juu ya mgongo wake, kwa hiyo itasema: Amefanya hivi na vile katika siku hii na ile, hizi ndizo khabari zake.”

Kisha amesema Tirmidhi hii ni hadithi Hassan Sahih *Gharib*.¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

بِأَنَّ رَّبِّكَ أَوْحَىٰ لَهَا ﴿٦﴾

“Kwa sababu Mola Wake Mlezi Ameifunulia!”

Amesema Bukhari *Awaha laha* na *Awaha- Ilayha*, *Wawaaha laha*, *Wawaha Ilayha*, zote hizo maana yake ni moja. Na kama hivyo amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما, *Awhalahaa* maana yake ni: *Awah Ilayha*.

Na dhahiri ni kwamba tamko la *Awaha* na *Waha*, yamedhamini. Maana yake: ‘Ameiruhusu’. Na amesema Shubayb bin Bishri kutoka kwa Ikrima na kutoka kwa Ibni Abbas رضي الله عنهما,

يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا ﴿٧﴾

“Siku hiyo itahadithia khabari zake”.

Amesema amemuambia Bwana wake: ‘Sema’, ‘itasema’.² Na amesema Mujahid: ‘*Awaha-lahaa* maana ameiamrisha.’³ Na amesema Al-Qurtubi: ‘***Ameiamrisha***’ ni kupasuka ili waweze kutoka. Na Kauli Yake Allah تعالى:

يَوْمَئِذٍ يَصْدُرُ النَّاسُ أَشْتَاتًا

“Siku hiyo watu watatoka kwa mfarakano wakaoneshwe vitendo vyaol!”

¹ Ahmad 2:374, *Tuhfatul Ahwadhi* 9:285 na An-Nasaai katika *Al-Kubra* 11693.

² *Adurr Al-Manthuur* 8:592.

³ At-Tabari 24:548.

Maana yake: Watarejea wakitoka mahali pa kuhesabiwa wakiwa aina mbali mbali. Maana: Aina nyingi za watu; muovu na mwema, mwenye kuamrisha kwenda peponi, na mwenye kuamrisha kwenda motoni. Na amesema Assudy: 'Ashta-tan.' Maana yake: Makundi.¹ Na Kauli Yake Allah تعالى:

لِيُرَوْا أَعْمَلَهُمْ ﴿١٠﴾

“Wakaoneshwe vitendo vyao!”

Maana yake: Ili wajue na walipwe kwa yale waliyoyatenda duniani miongoni mwa kheri na shari.

Malipo ya Kila Chembe katika Matendo

Na kwa sababu hiyo Amesema:

فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿١١﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿١٢﴾

“Basi anayetenda chembe ya wema, atauona! Na anayetenda chembe ya uovu atauona!”

Amepokea Bukhari kutokana na Abu Hurairah رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema,

«الْخَيْلُ لثَلَاثَةِ، لِرَجُلٍ أَجْرًا، وَلِرَجُلٍ سِتْرًا، وَعَلَى رَجُلٍ وَزْرًا. فَأَمَّا الَّذِي لَهُ أَجْرٌ فَرَجُلٌ رَبَطَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَأَطَالَ طِيلَهَا فِي مَرْجٍ أَوْ رَوْضَةٍ، فَمَا أَصَابَتْ فِي طِيلِهَا ذَلِكَ فِي الْمَرْجِ وَالرَّوْضَةِ كَانَ لَهُ حَسَنَاتٍ، وَلَوْ أَنَّهَا قَطَعَتْ طِيلَهَا فَاسْتَنْتَّ شَرَفًا أَوْ شَرَفَيْنِ كَانَتْ آثَارُهَا وَأَزْوَائُهَا حَسَنَاتٍ لَهُ، وَلَوْ أَنَّهَا مَرَّتْ بِنَهْرٍ فَشَرِبَتْ مِنْهُ - وَلَمْ يُرِدْ أَنْ يَسْقِيَ بِهِ - كَانَ ذَلِكَ حَسَنَاتٍ لَهُ، وَهِيَ لِذَلِكَ الرَّجُلِ أَجْرًا. وَرَجُلٌ رَبَطَهَا تَعْنِيًا وَتَعَمُّمًا وَلَمْ يَنْسَ حَقَّ اللَّهِ فِي رِقَابِهَا وَلَا ظَهْرِهَا فَبَيَّ لَهَا سِتْرًا، وَرَجُلٌ رَبَطَهَا فَخْرًا وَرِيَاءً وَنَوَاءً فَهِيَ عَلَى ذَلِكَ وَزْرًا»

“Farasi ni kwa mambo matatu: Kwa mtu ni malipo na kwa mtu ni sitara, na kwa mtu ni madhambi. Ama yule ambaye kwake ni malipo, ni mtu amemfanya katika njia ya Mwenyezi Mungu akairefusha

¹ Adurr Al-Manthuur 8:593.

kamba yake katika nyasi au bustani, yale atakayoyapata katika kamba yake hiyo katika nyasi au bustani, yatakuwa hayo ni mema yake. Na lau kwamba farasi huyo alikata kamba yake na akaupanda mlima mmoja au miwili zitakuwa nyayo zake na mavi yake ni mema yake. Na lau kwamba yeye alipita katika mto akanywa katika mto huo, (na wala asikusudie kuyanyweshwa watu maji hayo) yatakuwa hayo ni katika mema yake, na farasi huyo kwa mtu huyo ni malipo. Na mtu aliyemfunga kwa kujitoshia na kwa kujilinda na kuomba na hakusahau hadhi ya Mwenyezi Mungu katika shingo na migongo ya farasi huyo kwake ni sitara. Na mtu amemfunga farasi huyo kujifakharisha na kujionesha na kwa kujikweza, farasi huyo kwa hayo atakuwa kwake ni madhambi.”

Akaulizwa Mtume ﷺ kuhusu Punda akasema,

«مَا أَنْزَلَ اللَّهُ فِيهَا شَيْئًا إِلَّا هَذِهِ الْآيَةُ الْفَادَةُ الْجَامِعَةَ ﴿قَمَنَ يَسْمَلُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ﴾
 ﴿يَسْرُورًا﴾ وَمَنْ يَسْمَلُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٨﴾»

“Haikuteremshwa na Mwenyezi Mungu kuhusu hao punda kitu chochote isipokuwa aya hii pekee yenye kukusanya” **“Basi anayetenda chembe ya wema, mithili ya mdudu chungu atauona! Na anayetenda chembe ya uovu mithili ya mdudu chungu atauona!”**¹ Imepokelewa na Muslim.²

Na imekuja katika sahihi ya Bukhari kutoka kwa Adiy hali ya kuwa Hadithi hii imenyanyuliwa mpaka kwa Mtume ﷺ,

«اتَّقُوا النَّارَ وَلَوْ بِشِقِّ تَمْرَةٍ، وَلَوْ بِكَلِمَةٍ طَيِّبَةٍ»

“Jikingeni na moto, ijapokuwa kwa kutoa upande wa tende na ijapokuwa kwa kuzungumza maneno mazuri”.³

Na kwa upokezi wake vilevile katika sahihi.

¹ Fat'hul Al-Bari 8:598.

² Muslim 2:680.

³ Fat'hul Al-Bari 3:332.

«لَا تَحْفِرَنَّ مِنَ الْمَعْرُوفِ شَيْئًا وَلَوْ أَنْ تُفْرَغَ مِنْ دَلْوِكَ فِي إِيَاءِ الْمُسْتَقِيِّ، وَلَوْ أَنْ تُلْقَى أَخَاكَ وَوَجْهَكَ إِلَيْهِ مُنْبَسِطًا»

“Usidharau miongoni mwa wema kitu chochote ijapokuwa kumimina kutoka katika ndoo yako kwa mwenye kuomba maji katika chombo chake na japo utakutana na ndugu yako na hali ya kuwa uso wako kwake ni wenye kukunjuka”.¹

Na imekuja katika sahihi vilevile.

«يَا مَعْشَرَ نِسَاءِ الْمُؤْمِنَاتِ، لَا تَحْفِرَنَّ جَارَةً لِحَارَتِهَا وَلَوْ فِرْسَنَ شَاةٍ»

“Enyi kongamano la wanawake waumini asimdharau jirani, Jirani yake, ijapokuwa kumpa kwato la mbuzi.”²

Anakusudia kwato lake na imekuja katika Hadithi nyingine,

«رُدُّوا السَّائِلَ وَلَوْ بِظَلْفٍ مُحْرَقٍ»

“Mrudisheni (mpeni) mwenye kuomba ijapokuwa kwa kwato lililochomwa”.³

Na imepokelewa kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kwamba alitoa sadaka zabibu moja na akasema: ‘Kuna kiasi gani cha uzito wa mdudu chungu katika zabibu hii?’⁴ Kadhalika Imamu Ahmad amepokea kutoka kwa Auf bin Al-Harithi bin Tufail kwamba Aisha رضي الله عنها alimueleza kuwa Mtume ﷺ alikuwa akisema:

«يَا عَائِشَةُ، إِيَّاكَ وَمُحَقَّرَاتِ الذُّنُوبِ، فَإِنَّ لَهَا مِنَ اللَّهِ طَالِبًا»

“Ewe Aisha: Tahadhari na madhambi yanayodharauliwa kwani madhambi hayo yataomba kwa Mwenyezi Mungu.”

Ameipokea An-Nasaai na Ibn Majah.⁵

¹ Muslim 4:2026.

² Fat’h ul Al-Bari 10:459.

³ Ahmad 5:381.

⁴ Al-Muwatwa 2:997.

⁵ Ahmad 6:151, Ibn Majah 4243.

Kadhalika pamepokewa na Imam Ahmad kutoka kwa Abdullah bin Masuud رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِيَّاكُمْ وَمُحَقَّرَاتِ الذُّنُوبِ، فَإِنَّهُنَّ يَجْتَمِعْنَ عَلَى الرَّجُلِ حَتَّى يُهْلِكُنَّهُ»

“Ewe Aisha: Tahadhari na madhambi yanayodharauliwa kwani madhambi hayo yatakusanyika kwa mtu mpaka yamuangamize.”

Na kwa hakika Mtume ﷺ aliwapigia wanawake mfano wa watu waliofanya kambi katika ardhi ya Jangwa, akaja mtengenezaji wao wa chakula akawa mtu anaondoka analeta ujiti na mtu mwingine anaondoka analeta ujiti mpaka wakakusanya – Mzigo mkubwa na wakawasha moto na wakakiivisha kile walichokiweka ndani ya moto huo.¹

Huu ni mwisho wa tafsiri ya *Idhaa Zulzilati*. Allah تعالى ni wa Kuhimidiwa na Kwake tunatarajia neema.

* * *

¹ Ahmad 1:402.

Tafsiri ya Suratul 'Adiyat
Sura ya 100
Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

<p>سُورَةُ الْعَادِيَاتِ</p> <p>بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ</p> <p>وَالْعَادِيَاتِ ضَبْحًا ① فَالْمُورِيَاتِ قَدْحًا ② فَالْغِيْرَاتِ ضَبْحًا ③ فَاتَّزْنَ بِهٖ نَقْعًا ④ فَوَسَطْنَ بِهِ جَمْعًا ⑤ إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهٖ لَكَنُودٌ ⑥ وَإِنَّهٗ عَلَىٰ ذَٰلِكَ لَشَهِيدٌ ⑦ وَإِنَّهٗ لِحُبِّ الْخَيْرِ لَشَدِيدٌ ⑧ * أَفَلَا يَعْلَمُ إِذَا بُعْثِرَ ⑨ مَا فِي الْقُبُورِ ⑩ وَحُصِّلَ مَا فِي الصُّدُورِ ⑪ إِنَّ رَبَّهُم ⑫ بِهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّخَبِيرٌ ⑬</p>
--

وَالْعَادِيَاتِ ضَبْحًا ①
 فَالْمُورِيَاتِ قَدْحًا ②
 فَالْغِيْرَاتِ ضَبْحًا ③
 فَاتَّزْنَ بِهٖ نَقْعًا ④
 فَوَسَطْنَ بِهِ جَمْعًا ⑤
 إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهٖ لَكَنُودٌ ⑥
 وَإِنَّهٗ عَلَىٰ ذَٰلِكَ لَشَهِيدٌ ⑦
 وَإِنَّهٗ لِحُبِّ الْخَيْرِ لَشَدِيدٌ ⑧
 * أَفَلَا يَعْلَمُ إِذَا بُعْثِرَ مَا فِي الْقُبُورِ ⑨
 وَحُصِّلَ مَا فِي الصُّدُورِ ⑩
 إِنَّ رَبَّهُم ⑫
 بِهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّخَبِيرٌ ⑬

1. Naapa kwa farasi wendao mbio wakihema,
2. Na wakitoa moto kwa kupiga kwato zao chini,
3. Wakishambulia wakati wa asubuhi,
4. Huku wakitimua vumbi,
5. Na wakijitoma kati ya kundi,
6. Hakika mwanaadamu ni mtovu wa fadhila kwa Mola Wake Mlezi!
7. Na hakika yeye mwenyewe bila ya shaka ni shahidi wa hayo!

8. Naye hakika bila ya shaka ana nguvu za kupenda mali!

9. Kwani hajui watakapofufuliwa waliomo makaburini?

10. Na yakakusanywa yaliomo vifuani?

11. Kuwa hakika Mola Wao Mlezi siku hiyo bila ya shaka Atakuwa na khabari zao wote!

Kuapiwa Farasi wa Vita Juu ya Ukanushi wa Mwanadamu na Pupa Yake

Allah تعالی Anaapia kwa farasi pindi wanapopelekwa mbio katika Njia Yake, wakakimbia na wakahama uhamaji wenye kusababisha kutoa sauti ambayo inasikiwa kutokana na farasi wakati wanapokimbia.

فَالْمُورِيَّتِ قَدَّحًا

“Na wakitoo moto kwa kupiga kwato zao chini.”

Anakusudia kusigana kwato na mawe huwaka kutokana nayo moto.

فَالْغَيْرَاتِ صُبْحًا

“Wakishambulia wakati wa asubuhi.”

Anakusudia kushambulia wakati wa asubuhi. Kama alivyokuwa Mtume ﷺ anashambulia wakati wa asubuhi. Na anasikiliza adhana akisikia adhana hashambulii na kama hakisikia anashambulia.

Na Kauli Yake Allah تعالی:

فَأُتْرِنَ بِهِ نَقْعًا

“Huku wakitimua vumbi.”

Anakusudia vumbi la mahali pa mashambulizi ya farasi.

فَوْسَطْنَ بِهِ جَمْعًا

“Na wakijitoma kati ya kundi.”

Maana yake: Wakaingilia katika mahali hapo wote, wakiwa ni kundi.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَالْمَغِيرَاتِ صُبْحًا ﴿٦٠﴾

“Wakishambulia wakati wa asubuhi.”

Amesema Ibnu Abbas na Mujahid na Qatada رضي الله عنهم: anakusudia kushambulia farasi wakati wa asubuhi katika Njia ya Allah تعالى.¹ Na Kauli Yake:

فَأَثَرُنَ بِمَاءِ نَقْعًا ﴿٦١﴾

“Huku wakitimua vumbi.”

Hapo ni mahali ambapo wameingia na wakatifua vumbi. Na Kauli Yake Allah تعالى,

فَوْسَطِنَ بِمَاءِ حَمَّاءَ ﴿٦٢﴾

“Na wakijitoma kati ya kundi.”

Amesema Al-'Awfi: Kutokana na Ibni Abbas, 'Atwaa, Ikrima, Qatada na Adh-Dhahak رضي الله عنهم anakusudia kundi la makafiri katika maadui.²

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّ الْأَنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنُودٌ ﴿٦٣﴾

“Hakika mwanaadamu ni mtovu wa fadhila kwa Mola Wake Mlezi!”

Hili ndilo lililoapiwa kwa maana yeye Neema za Mola wake anazikanusha, Amesema Ibnu Abbas, Mujahid, Ibrahim, An-Nakhai. Abu Jawzaa, Abu Aliya, Abu Dhuhaa, Said bin Jubair na Muhammad bin Qaisi, Adh-Dhahak, Hassan, Qatada, Al-Rabii bin Anas na Ibni Zaid رضي الله عنهم kuwa *Al-Kanuud*: Maana yake: Ni mwingi wa kukufuru.³ Amesema Hassan *Al-Kanuud*: Ni yule anayehesabu misiba na anasahau neema za Allah تعالى juu yake.⁴ Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَنَّهُ عَلَىٰ ذٰلِكَ لَشَهِيدٌ ﴿٦٤﴾

“Na hakika yeye mwenyewe bila ya shaka ni shahidi wa hayo!”

¹ At-Tabari 24:562.

² At-Tabari 24:564 na 565.

³ At-Tabari 24:566.

⁴ At-Tabari 24:566.

Amesema Qatada na Sufyani Tthauri 'hakika Allah تعالى juu ya hayo ni mwenye kushuhudia.¹ Na inawezekana mwanadamu ni mwenye kushuhudia hayo. Muhammad bin Ka'ab Al-Quradhy anasema: Hakika mwanadamu juu ya kuwa kwake ni mwenye kukanusha anashuhudia. Maana: Kwa ulimi wa hali yake. Maana: Linaonekana hilo kwa uwazi katika maneno yake, na matendo yake. Kama Allah تعالى Alivyosema,

مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِينَ أَنْ يَعْمُرُوا مَسْجِدَ اللَّهِ شَاهِدِينَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ بِالْكَفْرِ

“Haiwi kwa makafiri ndio waamirisha misikiti ya Mwenyezi Mungu, hali wanajishuhudishia wenyewe ukafiri...”

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأِنَّهُ لِحُبِّ الْخَيْرِ لَشَدِيدٌ

“Naye hakika bila ya shaka ana nguvu za kupenda mali!”

Maana yake: Hakika yeye kwa kupenda kheri nayo ni mali anayapenda sana. Ndani ya neno *Lashadid* pana maana mbili yaliyowagawanya wanazuoni: Moja yao; ina maana ya: kwamba yeye anayapenda sana mali. Ya pili ni kuwa yeye anapupa sana na ni bakhili kutokana na kuyapenda kwake mali. Na njia zote hizo ni sahihi.

Kukhofisha Kutokana na Siku ya Qiyama

Kisha Allah تعالى Akasema Akiwataka watu waipende nyongo dunia na waipende akhera, na hali ya kuwa mwangalifu juu ya yale yatakayokuwa baada ya hali hiyo, na yale atakayokutana nayo mwanadamu miongoni mwa vituko mbali mbali.

• أَفَلَا يَعْلَمُ إِذَا بُعِثَ مَا فِي الْقُبُورِ

“Kwani hajui watakapofufuliwa waliomo makaburini?”

Maana yake: Vikatolewa, vilivyo ndani yake miongoni mwa wafu.

وَحُصِّلَ مَا فِي الصُّدُورِ

“Na yakakusanywa yaliomo vifuani?”

¹ At-Tabari 24:576.

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما na wengineo anakusudia, 'kubainishwa na yakadhihirishwa¹ yale waliyokuwa wanayaficha katika nafsi zao.'

إِنَّ رَبَّهُمْ بِهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّخَبِيرٌ ﴿١٠٠﴾

"Kuwa hakika Mola Wao Mlezi siku hiyo bila ya shaka atakuwa na khabari zao wote!"

Maana yake: Anayajuwa yote waliyokuwa wanayatenda na kuyafanya na Atawalipa juu yake malipo kamili, na hatadhulumu kiasi cha uzito wa sisimizi.

Huu ni mwisho wa tafsiri ya Surat Al-'Adiyat. Na ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹ At-Tabari 24:569.

Tafsiri ya Suratul Qari'a
Sura ya 101
Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

<p style="font-size: 1.2em; margin: 0;">سُورَةُ الْقَارِعَةِ</p> <p style="margin: 10px 0 0 0;">بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ</p> <p style="margin: 0 0 10px 0;">الْقَارِعَةُ ﴿١﴾ مَا الْقَارِعَةُ ﴿٢﴾ وَمَا أَذْرَكَ مَا الْقَارِعَةُ ﴿٣﴾</p> <p style="margin: 0 0 10px 0;">يَوْمَ يَكُونُ النَّاسُ كَالْفَرَاشِ الْمَبْثُوثِ ﴿٤﴾</p> <p style="margin: 0 0 10px 0;">وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ الْمَنْفُوشِ ﴿٥﴾ فَأَمَّا مَنْ</p> <p style="margin: 0 0 10px 0;">ثَقَلَتْ مَوَازِينُهُ ﴿٦﴾ فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَاضِيَةٍ ﴿٧﴾ وَأَمَّا مَنْ</p> <p style="margin: 0 0 10px 0;">خَفَّتْ مَوَازِينُهُ ﴿٨﴾ فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ ﴿٩﴾ وَمَا أَذْرَكَ مَا</p> <p style="margin: 0 0 10px 0;">هِيَ ﴿١٠﴾ نَارٌ حَامِيَةٌ ﴿١١﴾</p>
--

الْقَارِعَةُ ﴿١﴾ مَا الْقَارِعَةُ ﴿٢﴾ وَمَا أَذْرَكَ مَا الْقَارِعَةُ ﴿٣﴾ يَوْمَ يَكُونُ النَّاسُ كَالْفَرَاشِ الْمَبْثُوثِ ﴿٤﴾ وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ الْمَنْفُوشِ ﴿٥﴾ فَأَمَّا مَنْ ثَقَلَتْ مَوَازِينُهُ ﴿٦﴾ فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَاضِيَةٍ ﴿٧﴾ وَأَمَّا مَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ ﴿٨﴾ فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ ﴿٩﴾ وَمَا أَذْرَكَ مَا هِيَ ﴿١٠﴾ نَارٌ حَامِيَةٌ ﴿١١﴾

1. Qiyama.
2. Nini Qiyama?
3. Na nini kitachokujulisha nini Qiyama?
4. Siku ambayo watu watakuwa kama panzi waliotawanyika.
5. Na milima itakuwa kama sufi iliyochambuliwa!
6. Basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito,
7. Huyo atakuwa katika maisha ya kupendeza.

8. Na yule ambaye mizani yake itakuwa khafifu.

9. Huyo maskani yake yatakuwa Moto wa Hawiya!

10. Na nini kitacho kujulisha nini hiyo?

11. Ni Moto mkali!"

Al-Qaari'a ni katika majina ya siku ya Qiyama kama vile Al-Haqqa, At-Twamma, As-Swakha na Al-Ghashiya na yasiyokuwa hayo. Kisha Amesema Allah تعالى hali ya Kulitukuza jambo lake na hali ya Kutishia kutokana na hali yake:

وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْقَارِعَةُ ﴿١﴾

"Na nini kitachokujulisha nini Qiyama?"

Kisha Amelifasiri hilo kwa Kauli Yake,

يَوْمَ يَكُونُ النَّاسُ كَالْفَرَاشِ الْمَبْثُوثِ ﴿٢﴾

"Siku ambayo watu watakuwa kama panzi waliotawanyika."

Maana yake: Katika kuzagaa kwao na kutawanyika kwao. Na kwenda kwao na kuja kwao kutokana na kukwama kwao katika siku hiyo. Watakuwa kana kwamba wao ni vipepeo wenye kutawanywa.

Kama Alivyosema Allah تعالى katika aya nyingine.

كَأَنَّهُمْ جَرَادٌ مُّنتَشِرٌ ﴿٧﴾

"... kama nzige waliotawanyika,...". (54:7)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ الْمَنْفُوشِ ﴿٨﴾

"Na milima itakuwa kama sufi iliyochambuliwa!"

Anakusudia kuwa yamekuwa ni kama sufi iliyochambuliwa ambayo imeanza kupeperuka na kukatikakatika.

Amesema Mujahidi na Ikrima na Saiid bin Jubair na Hassan na Qatadah na Atwaa Khurasani na Adh-Dhahak na As-Sudi.

كَأَعْيُنِ

"Kama sufi."

Maana yake: Sufi.¹ Kisha Ameeleza Allah تعالى kitakachotokea katika matendo ya watendaji. Na kitachotokea katika kutukuzwa au kudhalilishwa kulingana na matendo ya watendaji. Akasema:

فَأَمَّا مَنْ ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ ﴿٥﴾

"Basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito"

Maana yake: Yamekuwa mazito mema yake kuliko maovu yake.

فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَاضِيَةٍ ﴿٦﴾

"Huyo atakuwa katika maisha ya kupendeza."

Anakusudia atakuwa peponi.

وَأَمَّا مَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ ﴿٧﴾

"Na yule ambaye mizani yake itakuwa khafifu."

Maana yake: Yamekuwa mazito maovu yake kuliko mema yake. Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ ﴿٨﴾

"Huyo maskani yake yatakuwa Moto wa Hawiya!"

Pamesemwa: Maana yake: Ataanguka na ataporomoka kwa utosi wa kichwa chake katika moto wa Jahannam. Na amelielezea hilo kwa neno: "Ummuhu" – anakusudia ubongo wake. Yamepokewa mfano wa haya kutoka kwa Ibnu Abbas na Ikrima na Abu Saleh na Qatada رضي الله عنهم.² Na amesema Qatada: Ataporomoka katika moto juu ya kichwa chake.³ Na kama hivyo amesema – Abu Saleh: wataporomoka ndani ya moto juu ya vichwa vyao.⁴

¹ At-Twabari 24:574.

² At-Twabari 24:575 na 576 na Al-Qurtubi 20:167.

³ At-Twabari 24:576.

⁴ At-Twabari 24:575.

Na pamesemwa: 'Ummuhu' Maana yake: Ambaye atarejea Kwake na atakuwa huko akhera katika 'Haawiya'. Nalo ni jina katika majina ya moto. Amesema Ibnu Jabir: Hakika hapana jambo jengine pamesemwa ya kuwa *Haawiya* ni mama yake. Kwa sababu yeye hana marejeo mengine zaidi ya huo moto.¹ Na amesema Ibnu Zaid: *Al-Haawiya* ni moto. Ndiyo mama yake na marejeo yake ambayo atarejea kwenye marejeo hayo. Na Amesema:

وَمَا أُوْنَهُمُ النَّارُ

"Na makazi yao ni motoni." (3:151)²

Amesema Ibnu Abi Hatim رحمه الله تعالى, imepokewa kutoka kwa Qatada kwamba yeye amesema: huo ni moto nao ndiyo makazi yao.³ Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى Akifasiri maana ya *Haawiya*:

وَمَا أَدْرَاكَ مَا هِيَةٌ

"Na nini kitacho kujuilisha nini hiyo?"

Na Kauli Yake Allah تعالى:

نَارٌ حَامِيَةٌ

"Ni Moto mkali!"

Maana yake: Mkali sana, wenye joto kali sana, miali yenye nguvu sana na unawaka sana. Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«نَارُ بَنِي آدَمَ الَّتِي تُوقَدُونَ، جُزْءٌ مِنْ سَبْعِينَ جُزْءًا مِنْ نَارِ جَهَنَّمَ»

"Moto wa wanadamu ambao mnauwasha ni sehemu moja tu katika sehemu sabini za moto wa Jahannam."

Wakasema: 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa hakika kama ni hivyo basi unatosha.' Mtume ﷺ akasema:

¹ At-Twabari 24:575.

² At-Twabari 24:576.

³ At-Twabari 24:575.

«إِنَّهَا فَضَّلَتْ عَلَيْهَا بِتِسْعَةِ وَسِتِّينَ جُزْءًا»

"Hakika moto huo umezidishwa juu yake kwa mafungu sitini na tisa"

Ameipokea Bukhari na Muslim.¹ Na katika baadhi ya matamshi yake,

«إِنَّهَا فَضَّلَتْ عَلَيْهَا بِتِسْعَةِ وَسِتِّينَ جُزْءًا، كُلُّهُنَّ مِثْلُ حَرِّهَا»

"Hakika huo moto umezidishwa juu yake kwa mafungu sitini na tisa na yote ni mfano wa joto lake."

Na imekuja katika Hadithi ya Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba yeye amesema,

«إِنَّ أَهْوَنَ أَهْلِ النَّارِ عَذَابًا مَنْ لَهُ نَعْلَانِ، يُغْلِي مِنْهُمَا دِمَاعُهُ»

*"Hakika Mwepesi sana wa watu wa motoni kwa adhabu ni yule ambaye ana viatu viwili, unachemka kutokana navyo ubongo wake."*²

Na imethibitika katika sahihi mbili kwamba Mtume ﷺ amesema:

«اشْتَكَّتِ النَّارُ إِلَى رَبِّهَا فَقَالَتْ: يَا رَبِّ أَكَلَّ بَعْضِي بَعْضًا، فَأُذِنَ لَهَا بِتَمْسِينِ: تَنْفَسِي فِي الشُّتَاءِ، وَتَنْفَسِي فِي الصَّيْفِ، فَأَشَدُّ مَا تَجِدُونَ فِي الشُّتَاءِ مِنْ بَرْدِهَا، وَأَشَدُّ مَا تَجِدُونَ فِي الصَّيْفِ مِنْ حَرِّهَا»

*"Ulishitaki moto kwa Mola Wake ukasema: Ewe Mola Wangu imekula baadhi yangu kuila baadhi. Akauruhusu kupumua pumzi mbili – Pumzi wakati wa kusi na pumzi wakati wa Kaskazi. Kwa hiyo ule ukali mnaoupata katika wakati wa kusi ni kutokana na baridi yake na ukali mnaoupata wakati wa Kaskazi unatokana na joto lake."*³

Na katika sahihi mbili.

¹ Fat'hul Al-Bari 6:380, Muslim 4:2184.

² Ahmad 2:432 na 3:13.

³ Fat'hul Al-Bari 6:380 na Muslim 1:431.

«إِذَا اشْتَدَّ الْحَرُّ فَأَبْرِدُوا عَنِ الصَّلَاةِ، فَإِنَّ شِدَّةَ الْحَرِّ مِنْ فَيْحِ جَهَنَّمَ»

"Itakaposhitadi joto lipunguzeni kwa Sala, kwani kushitadi kwa joto ni mvuke wa Jahanamu."¹

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Al-Qaari'a*. Na ni kwa Allah تعالى Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹ *Fat'hul Al-Bari* 2:20 na *Muslim* 1:430.

Tafsiri ya Suratu Takathur

Sura ya 102

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ التَّكْوِيْنِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَلْهَنَكُمْ التَّكَاثُرَ ① حَتَّى زُرْتُمُ الْمَقَابِرَ ② كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ③
 تَعْلَمُونَ ④ ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ⑤ كَلَّا لَوْ تَعْلَمُونَ
 عِلْمَ الْيَقِينِ ⑥ لَتَرَوُنَّ الْجَحِيمَ ⑦ ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا
 عَيْنَ الْيَقِينِ ⑧ ثُمَّ لَتَسْتَسْلِفْنَ ⑨ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ ⑩

أَلْهَنَكُمْ التَّكَاثُرَ ① حَتَّى زُرْتُمُ
 الْمَقَابِرَ ② كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ
 ③ ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ④
 كَلَّا لَوْ تَعْلَمُونَ عِلْمَ الْيَقِينِ ⑤
 لَتَرَوُنَّ الْجَحِيمَ ⑥ ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا
 عَيْنَ الْيَقِينِ ⑦ ثُمَّ لَتَسْتَسْلِفْنَ
 ⑧ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ ⑨

1. Kumekushughulisheni kutafuta wingi, wa mali.
2. Mpaka mmeingia makaburini!
3. Sivyo hivyo! Punde kidogo Mtakuja jua!
4. Tena sivyo hivyo! Mtakuja jua!
5. Sivyo hivyo! Lau mngelijua kwa ujuzi wa yakini,
6. Basi bila ya shaka mtauona moto!
7. Tena, bila ya shaka, mtauona kwa jicho la yakini.
8. Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya matumizi ya neema mlizopewa."

Matokeo ya Kuipenda Dunia ni Kughafilika na Akhera

Allah تعالى Anasema, kumewashughulisha kuipenda dunia, na neema zake na pambo lake kuliko kuitafuta akhera na kuipenda kwake na nyie mmeendelea na hilo mpaka kimewajieni kifo na mmeingia makaburini na mkawa katika watu wake.

Katika sahihi Bukhari katika mlango wa "Al-Riqaaq". Kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه naye kutoka kwa Ubay bin Ka'ab رضي الله عنه amesema, 'Tulikuwa tunayaona haya katika Qurani Tukufu hadi iliposhuka,

أَلْهَيْكُمْ التَّكَاثُرُ ﴿١﴾

"Kumekushughulisheni kutafuta wingi wa mali"

Anayakusudia maneno haya:

«لَوْ كَانَ لِابْنِ آدَمَ وَادٍ مِنْ ذَهَبٍ»

"Lau mwanadamu angekuwa na jangwa la dhahabu".¹

Na amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Abdillah bin Shikhir رضي الله عنه amesema: Nilisikia kwa Mtume ﷺ na hali ya kuwa anasema:

«أَلْهَيْكُمْ التَّكَاثُرُ ﴿١﴾ يَقُولُ ابْنُ آدَمَ: مَالِي مَالِي، وَهَلْ لَكَ مِنْ مَالِكَ

إِلَّا مَا أَكَلْتَ فَأَنْبَيْتَ، أَوْ لَبَسْتَ فَأَبْنَيْتَ، أَوْ تَصَدَّقْتَ فَأَمْضَيْتَ؟»

"Kumekushughulisheni kutafuta wingi wa mali" Anasema mwanadamu mali yangu, mali yangu, huna wewe katika mali yako isipokuwa ile uliyoila na ukaimaliza au uliyoivaa ukaichakaza au uliyoitoa sadaka ukalipitisha hilo."²

Muslim na At-Tirmidhi na An-Nasai wameipokea.³

Kadhhalika Muslim amepokea kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema,

¹ Fat'hul Al-Bari 11:258.

² Ahmad 4:24.

³ Muslim 4:2273, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:286 na An-Nasaai katika Al-Kubra 6:521.

«يَقُولُ الْعَبْدُ: مَالِي مَالِي، وَإِنَّمَا لَهُ مِنْ مَالِهِ ثَلَاثٌ: مَا أَكَلَ فَأَنْفَى، أَوْ لَيْسَ فَأَبْلَى،
أَوْ نَصَدَّقَ فَأَمْضَى، وَمَا سِوَى ذَلِكَ فَذَاهِبٌ وَتَارِكُهُ لِلنَّاسِ»

“Anasema Mja: mali yangu, mali yangu hakika si vinginevyo ana yeye katika mali yake vitu vitatu; alichokila akakimaliza au alichokivaa akakichakaza au alichokitoa sadaka akakipitisha na yasiyokuwa hayo yeye ni mwenye kuondoka na atawaachia watu.”¹

Muslim ameipokea peke yake.

Na amepokea Bukhari kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema,

«يَتَّبِعُ الْمَيِّتَ ثَلَاثَةً، فَيَرْجِعُ اثْنَانِ وَيَبْقَى مَعَهُ وَاحِدٌ: يَتَّبِعُهُ أَهْلُهُ وَمَالُهُ وَعَمَلُهُ، فَيَرْجِعُ
أَهْلُهُ وَمَالُهُ، وَيَبْقَى عَمَلُهُ»

“Vinamfuata maiti vitu vitatu, vinarudi viwili kinabaki pamoja naye kimoja. Humfuatia watu wake, mali yake, na matendo yake, wanarudi watu wake na mali yake na matendo yake yanabakia.”²

Na kama hivyo amepokea Muslim na Tirmidhi na An-Nasai.³

Na amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«يَهْرَمُ ابْنُ آدَمَ وَيَبْقَى مِنْهُ اثْنَتَانِ: الْجِرْصُ وَالْأَمَلُ»

“Anazeeka mwanadamu na hubakia kwake vitu viwili – tamaa na matumaini.”⁴

Wameitoa katika sahihi mbili.⁵

¹ Muslim 4:2273.

² Fat'hul Al-Bari 11:369.

³ Muslim 4:2273, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 7:50 na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:631.

⁴ Ahmad 3:115.

⁵ Bukhari 6421 na Muslim 1047.

Karipio la Kuuona Moto na Kuulizwa Juu ya Neema

Na Kauli Yake تعالیٰ:

كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿١﴾ ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٢﴾

“Sivyo hivyo! Punde kidogo Mtakuja jua! Tena sivyo hivyo! Punde kidogo Mtakuja jua!”

Hassan Basry رحمه الله تعالیٰ Amesema: Hayo ni makamio baada ya makamio.¹ Ama Adh-Dhahak akifasiri aya hii amesema,

كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿١﴾

“Sivyo hivyo! Punde kidogo Mtakuja jua!”

Anakusudia: ‘Enyi makafiri,

ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٢﴾

“Tena sivyo hivyo! Punde kidogo Mtakuja jua!”

Anakusudia: “Enyi waumini.”² Na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

كَلَّا لَوْ تَعْلَمُونَ عِلْمَ الْيَقِينِ ﴿١﴾

“Sivyo hivyo! Lau mngelijua kwa ujuzi wa yakini.”

Maana: Lau mngejua ukweli, kusingewapumbazisha kujifakharisha kwa wingi wa mali na kuitafuta nyumba ya akhera mpaka mmekuwa katika makaburi.

Kisha amesema:

لَتَرْوَبْنَ الْجَحِيمَ ﴿١﴾ ثُمَّ لَتَرْوَبُنَّهَا عَيْنَ الْيَقِينِ ﴿٢﴾

“Basi bila ya shaka mtauona moto! Tena, bila ya shaka, mtauona kwa jicho la yakini.”

Hii ni Tafsiri ya makaripio yaliyotangulia nayo ni Kauli Yake تعالیٰ:

¹ Al-Baghwiyy 4:520.

² At-Tabari 24:581.

كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿١﴾ ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٢﴾

“Sivyo hivyo! Punde kidogo Mtakuja jua! Tena sivyo hivyo ! Punde kidogo Mtakuja jua!”

Amewakemea kwa hali hii, nayo ni kuona watu wa motoni - Moto. Moto ambao ukitoa sauti ya kuwaka kwake. Mara moja tu atapomoka - kwa magoti yake kila malaika mwenye kukurubishwa au Mtume ﷺ aliyepeleka - kutokana na tisho na ukubwa na kuuona waziwazi moto huo na vituko vyake. Maelezo hayo yapo katika *Athar* iliyopokewa kuhusiana na hilo. Na Kauli Yake Allah تعالى،

ثُمَّ لَتُسْأَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ ﴿٣﴾

“Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema mlizopewa.”

Maana yake: Kisha mtaulizwa siku hiyo kuhusu kuzishukuru neema ambazo Amezineemesha Allah تعالى kwenu, miongoni mwa afya, amani, rizki, na yasiyokuwa hayo. Ni jambo gani linaloonesha kukubali neema Zake kama sio Kumshukuru na Kumtii.

Ibnu Jarir رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Husaini bin Ali As-Swaddai, naye kutoka kwa Al-Walid bin Kisan, naye kutoka kwa Abuu Hazim, naye kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه kuwa amesema: Wakati Abubakar na Umar رضي الله عنهما, wamekaa, ghafla Mtume ﷺ akatokezea na kuwauliza kwa kusema:

«مَا أَجَلَسَكُمَا هُنَا؟»

“Ni jambo gani liliwafanya mkae hapa.”

Abubakar na Umar رضي الله عنهما wakasema: ‘Tunaapa kwa Yule Aliyekupeleka kwa haki, haikututoa majumbani mwetu isipokuwa njaa tu.’ Nae Mtume ﷺ akasema vilevile:

«وَالَّذِي بَعَنِي بِالْحَقِّ مَا أَخْرَجَنِي غَيْرُهُ»

“Naapa kwa Yule Aliyenipeleka kwa haki haikunitoa mimi jambo jingine isipokuwa hilo hilo.”

Wakaondoka mara wakaiendea nyumba ya mtu katika Answare. Mwanamke aliwapokea na akawakaribisha. Mtume ﷺ akamuuliza:

«أَيْنَ فُلَانٌ؟»

“Yuko wapi fulani?”

Mwanamke yule akajibu, ‘Amekwenda kututafutia maji, punde bwana yule akarudi huku amebeba kiriba chake cha maji. Akasema: ‘Karibuni! hakuna watu waliotembelewa na mtu bora zaidi kuliko nilivyotembelewa leo mimi na Mtume ﷺ.’ Akakitundika kiriba chake katika shina la jani la mtende – akaondoka akawaleta kole la tende.’ Mtume ﷺ akasema

«أَلَا كُنْتَ اجْتَنَيْتَ؟»

“Kwa nini usingezichuma?”

Akasema: ‘Nimependa mchague wenyewe kwa macho yenu.’ Kisha akachukua kisu. Mtume ﷺ akamuambia:

«إِيَّاكَ وَالْحُلُوبَ»

“Tahadhari na (kuchinja) mnyama anayenyonyesha.”

Akawachinja siku hiyo wakala. Mtume ﷺ akamuambia,

«لَتَسْأَلُنَّ عَنْ هَذَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ، أَخْرَجَكُم مِّنْ بُيُوتِكُمْ الْجُوعُ، فَلَمْ تَرْجِعُوا حَتَّى
أَصَبْتُمْ هَذَا، فَهَذَا مِنَ النَّعِيمِ»

“Mtaulizwa siku ya Qiyama kuhusu jambo hili imewatoa kutoka majumbani kwenu njaa hamkurejea mpaka mmeipata neema hii na kwa kweli hii ni katika neema.”¹ Na ameipokea Muslim.²

Na imethibiti katika sahihi ya Bukhari na Sunan Tirmidhi na An-Nasai na Ibnu Majah kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema, amesema Mtume ﷺ,

«بِعَمَّتَانِ مَغْبُورٍ فِيهِمَا كَثِيرٌ مِنَ النَّاسِ: الصُّحَّةُ وَالْفَرَاغُ»

“Neema mbili wamepunjwa katika neema hizo watu wengi: uzima na nafasi.”³

¹ At-Tabari 24:583.

² Muslim 3:1609.

³ Fat’hul Al-Bari 11:233; Tuhfat Al-Ahwadhi 6:589; Tuhfat Al-Ashraaf 4:465; Ibn Majah 2:1396.

Na maana ya maneno hayo: Kwamba wao wameacha wajibu wao katika kuzishukuru neema mbili hizo, hawasimamii wajibu wao juu ya neema hizo. Na yule asiyesimamia haki yake basi maana yake ni kuwa amepunjwa.

Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه, kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

«يَقُولُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ - قَالَ عَفَانُ: يَوْمَ الْقِيَامَةِ - يَا ابْنَ آدَمَ، حَمَلْتَنِي عَلَى الْخَيْلِ وَالْإِبِلِ، وَرَزَوَجْتَنِي النِّسَاءَ، وَجَعَلْتَنِي تَرْبِيعٌ وَتَرْأَسٌ، فَأَيْنَ شُكْرُ ذَلِكَ؟»

“Atasema Mwenyezi Mungu, Mwenye Kushinda, Mwenye Kutukuka – Anasema Msamehevu, (Siku ya Qiyama) Ewe mwanadamu: Nimekuchukua juu ya farasi na ngamia na Nimekuozesha wanawake na Nimekufanya ustarehe. Je, iko wapi shukurani yako juu ya neema hizo?”¹

Ameipokea peke yake na kwa njia hii.

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu At-Takaathur*. Ni kwa Allah تعالی tu Kusifiwa na Kuneemesha.



¹ Ahmad 2:492. Pia angalia Muslim na. 7438.

Tafsiri ya Suratul 'Asr

Sura ya 103

Iliteremshwa Makkah

Kujua kwa Amri bin Al-Aswi Muujiza wa Qur'ani Kutokana na Sura Hii.

Wametaja kwamba Amri bin Al-'Aswi alikwenda kwa Musaylimah Al-Kaddhab pale baada ya kupewa Utume Mtume Muhammad ﷺ na kabla ya kusilimu kwa Amri.

Musaylimah akamuuliza Amri; 'Kitu gani kimeteremshwa juu ya Swahiba yenu kwa muda huu?' Amri Akajibu kwa kusema: 'Kwa hakika imeteremshwa juu yake Sura fupi yenye maana nyingi.' Musaylimah akauliza: 'Ni Sura gani hiyo?' Akasema:

وَالْعَصْرِ ۝١
 إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكْفُورٌ ۝٢
 إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَّصُوا
 بِالصَّبْرِ ۝٣

- 1. Naapa kwa Zama za Alasiri!**
- 2. Hakika wanadamu wote wamo katika khasara,**
- 3. Ila wale walio amini, na wakatenda wema, na wakausiana haki, na wakausiana kusubiri**

Musaylimah akafikiria kwa muda mfupi kisha akasema hakika imeteremshwa juu yangu mfano wake. Amri akamuambia, 'Ni ipi sura hiyo?' Akasema: "Ewe Wabr hakika sijambo jengine wewe ni masikio mawili na kifua, na sehemu yako yote iliyobaki ni mashimo na vitobo." Kisha akasema unaonaje Ewe Amir? Amri akamuambia, 'Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika wewe unajua kwamba mimi ninaelewa kwamba wewe unadanganya.'¹

Kwa hakika nimemuona Abubakr Al-Kharaitwi amepokea katika kitabu chake

¹ Imetajwa vile vile katika kitabu, *Al-Bidaayatu Waa-Nihaayatu* 6:330 zamzam, wa mfano wake na Al-Haafidh katika kitabu *Al-Iswaabah* 3:225.

kinachojulikana kwa jina la (*Masaawi-Al-Akhlaq*) – misingi ya tabia mbaya – katika Juzuu ya Pili ya kitabu hicho – amepokea kitu – katika habari hii au karibu ya habari hii.

Na *Al-Wabr* ni mdudu anayefanana na paka, kikubwa kwa mdudu huyo ni masikio yake na kifua chake na sehemu iliyosalia haipendezi. Kwa hiyo alikusudia Musaylimah kuunda kutokana na upanuzi huu maneno ambayo yatapingana na Qur'ani.

Lakini jaribio lake hilo halikupata faida kwa wenye kuabudu masanamu katika zama hizo.

Twabarani amepokea kutoka kwa Abdillah bin Hafsi Abu Madina, amesema: Walikuwa watu wawili katika masahaba wa Mtume ﷺ, pindi wanapokutana hawaachani, isipokuwa atamsomea mmoja wao mwingine Suratul Asri mpaka mwisho wake.

Kisha baada ya hapo ndio humsalimia mmoja wao mwengine.¹

Na amesema Imam Shaafiy رحمه الله تعالى: Lau watu wangeifikiria sura hii kwa kina ingewatosha.



¹ *Al-Mu'ujam Al-Awsat* 5098 (Majma' Al-Bahrain).

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

<p>سُورَةُ الْاَسْرِ</p>
<p>بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ</p> <p>وَالْعَصْرِ ﴿١﴾ إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنُفٍ ﴿٢﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ ﴿٣﴾ وَتَوَّصَّوْا بِالصَّبْرِ ﴿٤﴾</p>

وَالْعَصْرِ ﴿١﴾ إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنُفٍ ﴿٢﴾
 ﴿٣﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا
 الصَّالِحَاتِ ﴿٣﴾ وَتَوَّصَّوْا
 بِالْحَقِّ ﴿٤﴾ وَتَوَّصَّوْا
 بِالصَّبْرِ ﴿٤﴾

1. Naapa kwa Zama za Alasiri!

2. Hakika wanadamu wote wapo katika khasara,

3. Ila wale walioamini, na wakatenda mema, na wakausiana haki, na wakausiana kusubiri."

Al-'Asr: Ni zama ambazo ndani yake harakati za wanadamu za kheri au za shari zinatokea na kuendelea.

Na amesema Maliki: Kutoka kwa Zaid bin Aslam: Muda huo ni jioni. Na kauli mashuhuri ni ile ya kwanza. Ameiapia Allah تعالیٰ kwa hilo juu ya kwamba mwanadamu yu katika hasara maana, "Katika hasara na maangamivu."

إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

"Ila wale walioamini, na wakatenda mema."

Amewatoa katika kundi la khasara wale ambao wameamini kwa nyoyo zao na wakatenda matendo mema kwa viungo vyao.

وَتَوَّصَّوْا بِالْحَقِّ

"Na wakausiana kwa haki."

Kushikamana na haki ni kutekeleza Twa'a na kuacha mambo yaliyoharamishwa.

وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ ﴿٣﴾

“Na wakausiana kusubiri.”

Maana yake: Juu ya misiba na makadirio, na maudhi ya wale wanaowaudhi wenye kuamrisha mema na wanaokataza maovu.

Huu ni mwisho wa *Tafsiri ya Suratu Al-Asr* na ni kwa Allah تعالیٰ Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

Tafsiri ya Suratul Humazah

Sura ya 104

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْهُمَزَةِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ۝
 الَّذِي جَمَعَ مَالًا وَعَدَّدَهُ ۝
 يَحْسَبُ أَنَّ مَالَهُ أَخْلَدَهُ ۝
 كَلَّا ۖ لَيُبَدَّنُ فِي
 الْحُطْمَةِ ۝
 وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْحُطْمَةُ ۝
 النَّارُ الَّتِي
 الْمَوْقِدَةُ ۝
 الَّتِي تَطَّلِعُ عَلَى الْأَفْئِدَةِ ۝
 إِنَّهَا عَلَيْهِمْ
 مُؤَصَّدَةٌ ۝
 فِي عَمَدٍ مُّمَدَّدَةٍ ۝

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ۝
 الَّذِي جَمَعَ مَالًا وَعَدَّدَهُ ۝
 يَحْسَبُ أَنَّ مَالَهُ أَخْلَدَهُ ۝
 كَلَّا ۖ لَيُبَدَّنُ فِي
 الْحُطْمَةِ ۝
 وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْحُطْمَةُ ۝
 النَّارُ الَّتِي
 الْمَوْقِدَةُ ۝
 الَّتِي تَطَّلِعُ عَلَى الْأَفْئِدَةِ ۝
 إِنَّهَا عَلَيْهِمْ
 مُؤَصَّدَةٌ ۝
 فِي عَمَدٍ مُّمَدَّدَةٍ ۝

1. Ole wake kila safihi, msengenyaji!
2. Aliyekusanya mali na kuyahisabu.
3. Anadhani ya kuwa mali yake yatambakisha milele!
4. Hasha! Atavurumishwa katika H'ut'ama.
5. Na nani atakujuvya ni nini H'ut'ama?
6. Moto wa Mwenyezi Mungu uliowashwa.
7. Ambao unapanda nyoyoni.
8. Hakika huo utafungiwa nao
9. Kwenye nguzo zilionyooshwa."

Al-Hammaza: Ni yule anayewauchi sana watu kwa maneno. Na *Allammazi*: Ni kwa vitendo. Yule anayetia kasoro watu kwa vitendo na kukusudia. Anawadharau watu na anawaona kuwa wana upungufu. Umetangulia ufafanuzi wa hilo katika Kauli Yake Allah تعالی:

هَمَّازٌ مَّشَاءٌ بِنَمِيمٍ ﴿١٠﴾

“Mtapitapi, apitaye akifitini.” (68:11)

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما: *Humaza, Lamzi* mwenye kutia ila, mwenye kutia aibu.¹ Na amesema Mujahid: *Al-Hummaza* ni kwa mkono na jicho; na *Al-Lamzi* ni kwa ulimi. Na Allah تعالی Amesema:

الَّذِي جَمَعَ مَالًا وَعَدَّدَهُ ﴿١١﴾

“Aliyekusanya mali na kuyahisabu.”

Maana yake: Ameyakusanya baadhi yake juu ya baadhi na akaidhibiti hesabu yake. Kama Kauli Yake Allah تعالی:

وَجَمَعَ فَأَوْعَى ﴿١٢﴾

“Na akakusanya mali, kisha akayahifadhi.” (70:18)

Ameyasema hayo Asudiy na Ibnu Jarir.² Na amesema Muhammad bin Kaab katika Kauli Yake:

جَمَعَ مَالًا وَعَدَّدَهُ ﴿١٣﴾

“Aliyekusanya mali na kuyahisabu.”

Yamempumbazisha mali yake wakati wa mchana kwa kufanya hili na lile, na unapofika usiku hulala kana kwamba yeye ni mzoga wenye uvundo.

Na Kauli Yake Allah تعالی:

تَحَسَّبُ أَنْ مَالَهُ أَخْلَدَهُ ﴿١٤﴾

“Anadhani ya kuwa mali yake yatambakisha milele!”

¹ At-Tabari 24:596.

² At-Tabari 24:598 na Al-Qurtubi 20:138.

Maana yake: Mtu anadhani kwamba kukusanya kwake mali kutamueka milele katika nyumba hii.

كَلَّا ط

“Hasha!”

Maana yake: Mambo hayatakuwa hivyo kama alivyodhani na sio kama alivyofikiri. Kisha Amesema Allah تعالى:

لِيُبَدَنَّ فِي الْخَطْمَةِ ﴿١﴾

“Hasha! Atavurumishwa katika H’ut’ama.”

Maana yake: Kwa hakika atatupwa huyu aliyekusanya mali na akazihesabu hesabu katika *Hutwama*; na *Hutwama* ni wasifu katika majina ya moto. Kwa sababu moto huo unawavunjavunja walio ndani yake.

Na kwa sababu hiyo amesema:

وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْخَطْمَةُ ﴿٢﴾ نَارُ اللَّهِ الْمَوْقَدَةُ ﴿٣﴾ الَّتِي تَطَّلُعُ عَلَى الْأَعْيُنِ ﴿٤﴾

“Na nani atakujuvya ni nini H’ut’ama? Moto wa Mwenyezi Mungu uliowashwa ambao unapanda nyoyoni”.

Amesema Thabiti Bunani: Utawachoma mpaka kwenye nyoyo zao na hali ya kuwa wako hai. Kisha amesema: Kwa hakika imewafikia kwao adhabu – kisha akalia. Amesema Muhammad bin Kaab, moto utakula kila kitu katika mwili wake mpaka utafika kwenye moyo wake kuelekea koo lake, utarejea mwilini mwake.¹

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّا عَلَيْهِمْ مُّؤَصَّدَةٌ ﴿٥﴾

“Hakika huo utafungiwa nao.”

Maana yake: Umezibwa kama ilivyotangulia katika *Surat Al-Balad*. Na Kauli Yake Allah تعالى:

¹ Al-Qurtubi 20:185.

﴿ فِي عَمَلٍ مُّمدَّدَةٍ ﴾

“Kwenye nguzo zilionyoshwa.”

Amesema 'Atwiyya Al-Awfi: Nguzo za chuma. Na amesema Asudiy. Ya moto. Na amesema Al-Awfi kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما: Atawaingiza katika maguzo marefu yatakayorefushwa juu yao, nao watafungwa minyororo shingoni mwao na watafungiwa milango (ya Jahannamu) juu yao.¹

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Waylu-li-kulli humazatin lumaza*. Na ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹ At-Tabari 24:600.

Tafsiri ya Suratul Fiyl
Sura ya 105
Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْفِيلِ	
بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ	
أَلَمْ تَجْعَلْ	أَلَمْ تَجْعَلْ
كَيْدَهُمْ فِي	كَيْدَهُمْ فِي
تَضَلِيلٍ	تَضَلِيلٍ
وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا	وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا
أَبَابِيلَ	أَبَابِيلَ
تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّنْ	تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّنْ
سِجِّيلٍ	سِجِّيلٍ
فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ	فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ
مَّأْكُولٍ	مَّأْكُولٍ

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَابِ
 الْفِيلِ ﴿١﴾ أَلَمْ تَجْعَلْ كَيْدَهُمْ فِي
 تَضَلِيلٍ ﴿٢﴾ وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا
 أَبَابِيلَ ﴿٣﴾ تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّنْ
 سِجِّيلٍ ﴿٤﴾ فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ
 مَّأْكُولٍ ﴿٥﴾

1. Kwani hukuona jinsi Mola Wako Mlezi Alivyowatenda wale wenye tembo?
2. Kwani Hakujaalia vitimbi vyao kuharibika?
3. Na Akawapelekea ndege makundi kwa makundi,
4. Wakiwatupia mawe ya udongo wa Motoni,
5. Akawafanya kama majani yaliyoliwa!

Hizi ni katika neema ambazo Amewaneemesha nazo Allah تعالی Makureishi katika lile Alilowaokoa nalo miongoni mwa watu wa ndovu, ambao walikuwa wameazimia kuivunja Al-Ka'aba na kufuta athari yake katika Ulimwengu. Allah تعالی Akawaangamiza na Akawadhalilisha na Akayarudisha patupu waliyoazimia na Akapoteza matendo yao Akawarudisha kwa ubaya na kurudi patupu. Hawa watu wa ndovu walikuwa ni watu waliokuwa wanafuata dini ya

Kinaswara, na ilikuwa dini yao wakati huo ilikaribiana na Dini ya kweli (Uislamu) kuliko ushirikina wa Makureishi.

Isipokuwa ni kwamba yalikuwa hayo ni katika mlango wa maandalizi ya kupelekwa Mtume ﷺ, kwani mnamo mwaka huo alizaliwa Mtume na hiyo ndio kauli iliyo mashuhuri sana. Ni kama vile kutokana na Kudura Yake Allah تعالى Anasema: Kuwaambia Makuraishi: Enyi Makureishi hatukuwanusuru dhidi ya wahabeshi kwa sababu ya ubora wenu juu yao isipokuwa ni kwa kuikinga nyumba kongwe ambayo Tutaitukuza na Tutaifanya kuwa ni bora na Tutaipa heshima kwa Kumpeleka Mtume ﷺ asiyeandika wala kusoma maandishi akiwa ni mwisho wa Mitume.

Kisa cha Watu wa Ndovu kwa Ufupi

Kisa hiki cha watu wa ndovu kwa ufupi na kwa mukhtasari. Kimetangulia katika kisa cha watu wa mahandaki kwamba Dhu Nawasi alikuwa ni Mfalme wa mwisho katika wafalme wa Himyar, na alikuwa anamshirikisha Mwenyezi Mungu, na yeye ndiye aliyewaua watu wa mahandaki ambao walikuwa ni manaswara. Watu hawa waliouawa katika mahandaki walikuwa wanakaribia elfu ishirini, na hakuweza kuponyoka katika wao isipokuwa Daws Dhu Thaalaban kwani aliondoka akaomba msaada kwa Kaisar Mfalme wa Sham na alikuwa Mnaswara mwenzake. Naye akamuandikia kwenda kwa Najashi Mfalme wa Uhabeshi, kwa sababu ya kuwa yuko karibu sana na wao, akawapeleka pamoja naye viongozi wawili Aryat na Abraha bin Swabah Aba Yaksuum katika jeshi kubwa.

Wakaingia Yemen wakaenda huku na huko katika miji hiyo na kuwapiga na hivyo Mfalme wa Himyar Dhu Nawasi akaangamia kwa kuzama katika maji ya bahari. Uhabeshi ikajitenga na ufalme wa Yemen na wakawa juu yao hawa viongozi wawili. Aryat na Abraha wakatofautiana katika jambo lao wakavutana na wakagombana, kisha baadae wakapatana, mmoja wao akamshauri mwenzake kwa kumuambia, 'Kwa hakika hapana haja ya kugongana majeshi yetu. Isipokuwa tupigane na yeyote atakayemuua mwenzake basi huyo atajitenga na Ufalme.' Baada ya makubaliano wakapigana. Aryat akamshambulia Abraha akampiga kwa upanga na kumjeruhi pua na mdomo wake na akampasua uso wake, Atouda mtumwa wa Abraha akafanya mashambulizi juu ya Aryat, akamuua, na akarejea Abraha hali ya kuwa ni

majeruhi, akayatibu majeraha yake na akapona, akaamua kukaa na jeshi la Uhabeshi huko Yemen.

An-Najashi akamuandikia Abraha akimlaumu juu ya mambo aliyoyafanya na akamtisha na akaapa kwamba atakapokanyaga nchi yake ataukata utosi wake. Abraha akapeleka ujumbe kwake akimtaka awe mpole kwake na amfanyie ulaini. Akampelekea zawadi pamoja na mjumbe wake, zawadi ile ilikuwa na vitu vya thamani na vyombo vya ngozi ambavyo ndani yake mlikuwa na udongo wa Yemen na akakata nywele za utosi wake akavipeleka – vitu hivyo pamoja na mjumbe huyo na akasema katika barua yake: Akanyage mfalme juu ya vyombo hivi vya ngozi vyenye udongo wa Yemen. Ili atekeleze kiapo chake na hizi (nywele za) Utosu wangu nimekuletea, yalipofika kwake hayo yalimfurahisha Najashi sana na alimridhia akamthibitisha katika kazi yake.

Abraha akapeleka ujumbe kwa An-Najashi akimuambia kwamba hakika mimi nitakujengea kanisa katika ardhi ya Yemen, halijajengwa hapo kabla yako kanisa kubwa sana katika mji wa Sanaa. Kanisa refu sana, zimepambwa pande zake Waarabu waliloliita Al-Qulayyis, kwa sababu ya urefu wake. Kwa sababu mwenye kulitazama inakaribia kuanguka kofia yake kutoka kichwani kwake kutokana na urefu wa jengo lake. Kwa mpango wake huo Abraha Al-Ashram aliazimia kuwaondoa Waarabu katika Hija yao na kuwaelekeza kwenye Kanisa hilo ili wahiji kama wanavyohiji kwenye Al-Kaaba huko Makkah.

Abraha akalitangaza jambo hilo katika mamlaka yake na Waarabu wa Kabila la 'Adnan na Qahtwan walichukizwa sana na tendo hilo. Wakakasirika Makureishi kwa ghadhabu kubwa mno mpaka walilikusudia baadhi yao, mmoja katika hao akafanya kila njia akaweza kuingia ndani ya Kanisa hilo wakati wa usiku akajisaidia humo na akarejea alikotoka. Waangalizi wa kanisa hilo walipoona uchafu huo walipeleka taarifa za jambo hilo kwa Mfalme wao Abraha, wakamuambia hakika hapana jambo jingine wamelifanya jambo hili baadhi ya Makureishi wakiwa wamekasirika, kwa sababu umejenga jengo linalofanana na nyumba yao. Abraha akaapa kwamba atakwenda kwenye nyumba ya Makkah na ataibomoa jiwe baada ya jiwe.

Muqatil bin Sulaiman Ametaja kwamba vijana wa Kikureishi waliingia humo wakawasha moto humo, na siku hiyo ilikuwa na upepo mkali sana. Kanisa likaungua na likaanguka chini. Akajiandaa Abraha. Na kwa sababu hiyo akaenda akiwa pamoja na jeshi kubwa sana lenye nguvu ili mtu yeyote asiweze

kulizulia. Huku akifuatana na ndovu mkubwa sana hapajakuwepo mfano wake, ndovu huyo akiitwa Mahmud.

Mfalme wa Uhabeshi An-Najashi alimpa jukumu hilo, na inasemekana kuwa walikuwa pamoja naye idadi ya ndovu wanane vilevile au walikuwa kumi na wawili mbali na wale wanane. Allah تعالی Ndiye Mjuzi wa hayo. Lengo la kufuatana na ndovu huyo mkubwa ni kuweza kuibomoa Al-Kaaba kupitia kwa ndovu huyo kwa kufunga mnyororo katika nguzo za Al-Kaaba na kufungia shingoni mwa ndovu, kisha atakemewa ili auangushe ukuta kwa mara moja.

Waarabu Waliposikia habari hiyo (kwani jambo hilo walilionga kuwa ni kubwa sana) waliona kuwa ni haki juu yao kupambana ili kuihami nyumba hiyo na kumrudisha anayeikusudia kwa ubaya. Akamtokea mtu mmoja katika watukufu wa watu wa Yemen na wafalme wao, ambaye anaitwa Dhu Nafar akawaita watu wake na waliomuitika katika baki ya Waarabu kwenye kupigana vita dhidi ya Abraha na kupigania nyumba ya Mwenyezi Mungu na lile analolitaka miongoni mwa kuivunja na kuibomoa wakamuitika na wakampiga vita Abraha.

Abraha akawashinda kwa sababu ya lile Alilolitaka Allah تعالی, Mwenye Kushinda na Kutukuka, miongoni mwa kuitukuza Nyumba Yake Tukufu na kuiadhimisha, na Dhu Nafar akatekwa, akafuatana naye. Kisha akaenda upande wake mpaka alipokuwa katika ardhi ya Khatham, akazuiwa na Nufail bin Habib Al-Khatham pamoja na watu wake akiwemo katika hao Shahrana na Nahisi wakapigana naye, Abraha akawashinda akamteka Nufail bin Habib na akataka kumuua. Kisha akamsamehe akafuatana naye ili amfahamishe miji ya Hijazi.

Alipokaribia katika ardhi ya Taif walimtokea watu wake Thaqif wakamfanyia upole na ulaini kwa kuogopea juu ya mahali pao pa ibada walipopaita Al-Lata. Akawa mwema kwao na wakampeleka pamoja naye Aba Righal akiwa ni muongozaji wa Safari, alipokomelea Abraha mahali paitwapo Al-Mughhammas na hapo ni mahali palipo karibu na Makkah akafanya kambi hapo, na likafanya mashambulizi jeshi lake juu ya mifugo yao. Katika mifugo ile ilikuwemo ngamia mia mbili wa Abdul Muttwalib na alikuwa yule aliyewavamia na kuwashambulia wanyama hao ni kwa amri ya Abraha kiongozi wa safu ya mbele ya jeshi, na alikuwa anaitwa Al-Aswad bin Maqsoud, wakamtukana baadhi ya Waarabu kama ambavyo amehadithia.

Abraha akampeleka Hunatwa Al-Humayri huko Makkah akamuamrisha amletee mtukufu wa Makureishi amueleze kwamba Mfalme hakuja kuwapiga vita isipokuwa pale mtakapomzuia na nyumba, akaja Hunatwa akafahamishwa kwa Abdul Muttwalib bin Hashim na yakamfikia aliyoyasema Abraha. Abdul Muttwalib akasema kumjibu, “Naapa kwa Allah تعالی Mtukufu sisi hatutaki kupigana naye na hatuna uwezo wa hilo. Hii ni nyumba ya Allah تعالی na nyumba ya Mola wake Ibrahim عليه السلام, iwapo atamzuia nayo hiyo ni Nyumba yake na Patukufu Pake, hivyo ndivyo na iwapo atamuachia kati yake na Nyumba Yake, naapa kwa Allah تعالی sisi hatuna uwezo wa kumzuia.” Baada ya hapo akamuambia Hunatwa basi twende kwake pamoja. Akaenda naye.

Abraha alipomuona alimtukuza. Abdul Muttwalib alikuwa ni mtu mwenye mwili mkubwa, mzuri wa mtazamo. Abraha aliteremka kutoka kitandani kwake akakaa naye juu ya busati akamuambia Mfasiri wake, ‘muambiye,’ nini haja yako? Akasema kumuambia mfasiri, ‘hakika haja yangu ni kuwa nataka kwa mfalme anirejeshee ngamia wangu mia mbili ambao amewachukua.’ Abraha akasema kumuambia Mfasiri wake, ‘Muambie kwa hakika ulikuwa umenivutia wakati nilipokuona na nikakuamkia uliponisemesha, nakushangaa kwa sasa unazungumza kuhusu Ngamia wako mia mbili na unaaacha kuzungumzia nyumba ambayo ndiyo dini yako, na dini ya wazazi wako? ambayo nimekuja kuibomoa? Huzungumzi nami kuhusu nyumba hiyo?’

Abdul Muttwalib akamuambia, ‘Hakika mimi ni Bwana wa ngamia na nyumba nayo ina Bwana ambaye Anaikinga na Kuilinda’ Abraha akasema, ‘Haiwezekani Anizuie nami’. Abdul Muttwalib akasema, ‘Basi kama ni hivyo ni juu yako na Mola wa nyumba hii.’ Inasemekana kadhalika kuwa, Abdul Muttwalib alikwenda na ujumbe wa kundi la watu Watukufu, wa kiarabu, wakatoa pendekezo kwa Abraha achukuwe thuluthi za mali ya Tihama kwa sharti asivunje Nyumba. Abraha akawakatalia ombi hilo. Baada ya hapo Abraha akamrudishia Abdul Muttwalib ngamia wake kisha Abdul Muttwalib akarejea kwa Makureishi na akawaamrisha watoke na kwenda nje ya Makkah ili kujikinga katika vilele vya majabali na majeshi ya Abraha.

Kisha Abdul Muttwalib pamoja na kundi la Makureishi akasimama katika kikuku cha mlango wa Al-Kaaba na wakamuomba Mwenyezi Mungu Awanusuru juu ya Abraha na askari wake. Abdul Muttwalib akaomba huku amekamata kikuku cha Mlango wa Al-Kaaba:

“Hakuna lililo muhimu kwa mtu yeyote kwa sasa kuliko kulinda mifugo yake na mali yake. Kwa hiyo, Ewe Mola Wangu! Linda mali yako. Misalaba yao na nguvu zao hazitazishinda nguvu Zako itakapowadia asubuhi.”

Ibnu Ishaqa رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى (mwanachuoni wa siira) amesema kuwa, kisha baada ya kusema maneno hayo wakatoka kuelekea kwenye vilele vya majabali.

Muqatil bin Sulaiman ametaja kuwa wao waliacha mbele ya Al-Kaaba ngamia mia moja, wamefungwa alama shingoni mwao huenda baadhi ya askari watahughulishwa na ngamia hao pasi na haki ili Allah تَعَالَى Awaadhibu.

Abraha alipoamka asubuhi ili ajiandae kuelekea Makkah na kuingia katika mji huo alimuandaa ndovu wake aliyekuwa akiitwa Mahmuud pamoja na jeshi lake. Walipomuelekeza ndovu yule upande wa Makkah akawa hataki kwenda. Akaja Nufail bin Habib mpaka akasimama ubavuni mwake kisha akalikamata sikio lake akasema, “Piga magoti Ewe Mahmuud au rejea ulipotoka. Kwani hakika wewe upo katika mji wa Allah Taala kisha akaliachia sikio lake.” Ndovu yule akapiga magoti, Nufail bin Habib akaondoka pale kwa haraka mpaka akapanda juu ya Jabali. Jeshi la Abraha wakampiga ndovu ili asimame lakini akakataa wakaamua kumpiga kichwani kwa shoka na wakaziingiza fimbo zenye ncha katika sehemu zilizo laini kwa ndovu yule wakamtoa damu kwa fimbo hizo ili asimame lakini akakataa, wakamuelekeza hali ya kurejea Yemen akasimama hali ya kuwa anakwenda haraka na wapolimuelekeza upande wa Sham akafanya hivyo hivyo, wakamuelekeza Mashariki akafanya mfano wa hivyo na wakamuelekeza Makkah akapiga magoti kugoma kwenda.

Allah تَعَالَى Akawapelekea ndege kutoka baharini mfano wa kunguru kila ndege alikuwa na mawe matatu anayoyachukua: Jiwe moja liko mdomoni mwake na mawili yako miguuni mwake, mfano wa fiwi na adesi na halimpatu mtu yeyote katika mawe hayo isipokuwa mtu huyo huangamia. Pamoja na kuwa hawakupatwa wote lakini wakatoka hali ya kukimbia wakishindania njia wakimuulizia Nufail ili awaongoze njia. Wakati hayo yakijiri Nufail alikuwa kileleni mwa jabali pamoja na Makureishi na Waarabu wa Hijazi wakiangalia kinachoendelea kwa Allah تَعَالَى kuwateremshia watu wa ndovu mateso. Nufail akasema: Wapi pakujificha? Na Allah تَعَالَى anawasaka. Na Abraha ameshindwa, na Allah تَعَالَى Hawezi kushindwa.

Ibnu Ishaqa Nufail رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى katika tukio hilo amesema,

“Hivi hukutusalimu Ewe Rudaina tumewatuliza macho pamoja na asubuhi. Ee Rudaina lau ungeona na hutaona.

Ubavuni mwa jangwa Al-Muhasswab yale tuliyoyaona, ungenipa udhuru na ukayasifu mambo yangu.

Na usisikitike juu yake ya yale yaliyopita baina yetu.

Nimemshukuru Mwenyezi Mungu wakati nilipowaona ndege. Na nikayaogopa mawe yanayorushwa kwetu.

Watu wote walikuwa wanamuulizia Nufail. Kana kwamba pana juu yangu kwa Wahabeshi deni.”

Na amesema ‘Atwa bin Yasar na wengine, “Siyo kila mmoja wao ilimpata adhabu katika muda ule miongoni mwao, kuna waliyoangamia haraka na kuna katika wao ambaye ilikuwa kiungo chake kinaanguka kimoja baada ya kimoja. Na hali ya kuwa wao wanakimbia na alikuwa Abraha ni katika wale ambao vilianguka viungo vyao hadi akafa katika miji ya kabila la Khatham.”

Na amesema Ibnu Ishaq رحمه الله تعالى: wakatoka na hali ya kuwa wanaanguka na kuangamia njiani. Abraha aliumia sana katika mwili wake na wakatoka naye hali ya kuwa kidole chake kinaoza kimoja baada ya kingine mpaka wakafika naye Sanaa na hali ya kuwa yeye ni mfano wa kifaranga cha ndege, hakufa mpaka kilipopasuka kifua chake kikaachana na moyo wake kama walivyodai.’

Amesema Ibnu Ishaq رحمه الله تعالى: Wakati Allah تعالى Alipompeleka – Muhammad ﷺ lilikuwa katika mambo ambayo yalihesabiwa kuwa ni katika neema na fadhila za Allah تعالى juu ya Makureishi ni kule Kuwarejisha Wahabeshi na Shari zao na Kuihifadhi nyumba ya Allah تعالى. Allah تعالى Anasema Akielezea tukio hili la kihistoria kwa Kukumbusha,

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَابِ الْفِيلِ ﴿١﴾ أَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ فِي تَضْلِيلٍ ﴿٢﴾ وَأَرْسَلَ

عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ﴿٣﴾ تَزْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّن سِجِّيلٍ ﴿٤﴾ فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍ ﴿٥﴾

“Kwani hukuona jinsi Mola Wako Mlezi Alivyowatenda wale wenye tembo? Kwani Hakujaalia vitimbi vyao kuharibika? Na Akawapelekea ndege makundi kwa makundi. Wakiwatupia mawe ya udongo wa Motoni. Akawafanya kama majani yaliyoliwa!”

لَا يَلْفُ قَرِيْشٍ ﴿١﴾ ۚ اِلَيْهِمْ رِحْلَةُ الشِّتَاءِ وَالصَّيْفِ ﴿٢﴾ ۚ فَلْيَعْبُدُوْا رَبَّ هٰذَا الْاَبْتِ ﴿٣﴾
 الَّذِيْ اَطْعَمَهُمْ مِّنْ جُوْعٍ وَّءَامَنَهُمْ مِّنْ خَوْفٍ ﴿٤﴾

“Kwa walivyo zoea Makureshi. Kuzoea kwao safari za siku za baridi na siku za joto. Basi na wamuabudu Mola Mlezi wa Nyumba hii. Ambaye Anawalisha wasipate njaa, na Anawalinda na khofu.”
(106:1-4)

Maana yake: Asije akabadilisha kitu chochote katika hali yao ambayo walikuwa nayo kwa lile ambalo Amewatakiwa kwalo Allah ﷻ miongoni mwa kheri; lau wangekuwa wamelikubali hilo.

Amesema Ibnu Hisham رحمه الله تعالى: *Al-Ababil*: Ni makundi na Waarabu hawakuwa na neno hilo umoja wake. Amenieleza Yunus An-Nahawi na Abu Ubaida kuwa kwamba *Assijil*: ni ukali na ugumu. Amesema: Wametaja baadhi ya wafasiri kwamba hayo ni matamko mawili kwa lugha ya Kifursi. Waarabu wameyatohoa matamko mawili hayo kuwa tamko moja, hakika hapana jambo lolote asili yake katika lugha ya Kifursi ni *Sanj* na *Jilli*. Anakusudia kwa maana neno *Sanj*: ni Jiwe na “*Al-Jilli*” kwa maana ya Udongo. Anasema: Mawe ya jinsi mbili hizo nazo ni jiwe na udongo. Amesema na ‘*Asfu* ni majani ya mimea ambayo hayakuchumwa - umoja wa *Al-Asfu* ni *Asfah*.¹

Na amesema Hammad Ibni Salama kutoka kwa ‘Aswim kutoka kwa Zirri, kutoka kwa Abdillah na Abu Salama bin Abdul-Rrahman,

طَيْرًا اَبَابِيْلَ ﴿١﴾

“Ndege makundi kwa makundi.”

Amesema, maana yake makundi, na akasema Ibnu Abbas na adh-Dhahaak: kuwa ndege hawa wana kawaida ya kufuatana fuatana. Ama Hassan al-Basri na Qatadah wamesema kuwa maana ya “*Al-Ababil*” ni wengi. Na amesema Mujahid- “*Ababil*” mbali mbali wenye kufuatana wenye kukusanyika. Na kwa Waarabu amesema Ibnu Zaid: “*Al-Ababil*” wenye kutofautiana wanakuja kutoka hapa na kutoka pale, waliwajia kutoka kila mahali.²

¹ Ibnu Hishaam 1:51-56.

² At-Tabari 24:605, 606.

Na amesema Al-Kisai رحمه الله تعالى, "Nimewasikia baadhi ya wataalamu wa somo la Nahau (kanuni ya lugha ya kiarabu) wakisema umoja wa "Al-Ababil" ni "Ibil". Na amepokea Ibnu Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Ishaq bin Abdullah bin Al-Harithi Ibni Nawfal رحمه الله تعالى, kwamba yeye Amesema katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ﴿١﴾

"Na Akawapelekea ndege makundi kwa makundi."

Hayo ni makundi kama ngamia wenye kukusanyika.¹ Na imepokewa kutokana na Ibnu Abbas رضي الله عنهما:

وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ﴿٢﴾

"Na Akawapelekea ndege makundi kwa makundi."

Amesema wana midomo kama midomo ya ndege na viganja kama viganja vya mbwa.²

Imepokewa kutokana na Ikrima katika Kauli Yake Allah تعالى:

طَيْرًا أَبَابِيلَ ﴿٣﴾

"Ndege makundi kwa makundi."

Amesema: Walikuwa Ndege wa kijani waliotoka baharini wana vichwa kama vichwa vya wanyama wakali.³ Imepokewa kutoka kwa Ubaid bin Umair:

طَيْرًا أَبَابِيلَ ﴿٤﴾

"Ndege makundi kwa makundi."

Hao ni Ndege weusi wa baharini midomoni mwao na makuchani⁴ mwao pana mawe na haya ni mapokezi yaliyo sahihi.

¹ At-Tabari 24:606.

² At-Tabari 24:607.

³ At-Tabari 24:607.

³ At-Tabari 24:607.

Imepokewa kutoka kwa Ubaid bin Umair amesema: Alipotaka Allah تعالیٰ Kuwaangamiza watu wa ndovu Aliwaleta ndege walioumbwa kutoka baharini, mfano wa mwewe. Kila ndege katika hao amebeba mawe matatu yaliyokatwa, mawe mawili miguuni mwake na jiwe moja mdomoni mwake. Amesema wakaja mpaka wakapanga msitari juu ya vichwa vyao kisha wakapiga kelele na wakavitupa vilivyo miguuni mwao na midomoni mwao. Jiwe lolote linalotupwa kichwani kwa mtu yeyote, jiwe lile linaingia kwa mtu huyo na hutokea katika sehemu zake za haja kubwa. Na halitoki juu ya kitu chochote katika mwili wake isipokuwa hutoka kwa upande wake mwingine. Na Aliupeleka Allah تعالیٰ upepo mkali sana akayapiga yale mawe ukayaongezea ugumu wakaangamizwa wote.

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

جَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍ ﴿١﴾

“Akawafanya kama majani yaliyoliwa!”

Amesema Said bin Jubair: Anakusudia: maganda ambayo watu wa kawaida wanayaita *Habbaur* na katika upokezi wa Said majani ya ngano.¹

Na kutoka naye vile vile *Al-Asf*: Maganda. *Al-Ma'koul* ni Shairi hukakwa kwa ajili ya wanyama. Na kama hivyo amesema Hassan Basri. Na imepokewa kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما *Al-Asfu*: Ni ganda ambalo liko juu ya tembe kama vile kifuniko juu ya ngano.²

Na amesema Ibnu Zaid: *Al-Asf* ni majani ya mimea na majani ya mboga yatakapoliwa na wanyama wakiyanya yakawa ni kinyesi.³ Na maana ni kwamba Allah تعالیٰ Aliwaangamiza na Akawahilikisha na Akavirejesha vitimbi na hasira yao. Hawakupata kheri yoyote. Aliwaangamiza wote, hakurejea katika wao mwenye kutoa khabari isipokuwa na hali ya kuwa ana majeraha. Kama lilivyopita hilo kwa Mfalme wao Abraha kwani, Mfalme wao kilipasuka kifua chake na kuachana na moyo wake, wakati alipofika katika mji wake Sanaa. Akawaeleza watu wake yale yaliyowapitia kisha akafa.

¹ *Adurr Al-Manthuur* 8:633.

² *Al-Baghwi* 4:529.

³ *At-Tabari* 24:699.

Akatawala baada yake, mtoto wake Yaksoum, kisha akatawala baada yake nduguye Abraha, aliyekuwa akiitwa Masrouq bin Abraha, kisha akatoka Seif bin Dhi Yazin Al-Himyar kwenda kwa Kisra akamuomba msaada dhidi ya Uhabeshi. Akawapeleka pamoja naye jeshi lake wakapigana pamoja naye. Allah تعالى Akawarejeshea ufalme wao na yale yaliyokuwa kwa wazazi wao, miongoni mwa ufalme na ukamuendea ujumbe wa Waarabu kumpa pongezi.¹

Na tumetanguliza kutaja katika *Surati Al-Fat'h* kwamba Mtume ﷺ alipokaribia siku ya mkataba wa Hudaibiya juu ya mlima ambao wanashukia katika mlima huo Makureishi alipiga magoti ngamia wake. Basi watu wakajaribu kumfanya ainuke lakini alikataa. Watu wakasema Al-Qaswa amekuwa mkaidi. Mtume ﷺ akasema:

«مَا خَلَّاتِ الْقُضْوَاءُ، وَمَا ذَاكَ لَهَا يَخْلُقِي، وَلَكِنْ حَبَسَهَا حَابِسُ الْفَيْلِ»

“Al-Qas-waai’ (Ngamia wa Mtume ﷺ) Hiyo siyo tabia yake isipokuwa Amemzuia Yule Aliyemzuia ndovu.”

Kisha Akasema,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَا يَسْأَلُنِي الْيَوْمَ خُطَّةٌ يُعْظُمُونَ فِيهَا حُرْمَاتِ اللَّهِ إِلَّا أَجَبْتُهُمْ
إِنَّهَا»

“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Wao (Makuraishi) hawataniuliza juu ya jambo lolote (kuhusu mkataba) ambamo kuna mambo matukufu ya Mwenyezi Mungu, isipokuwa nitawajibu.”

Halafu akamkemelea akasimama.² Na Hadithi hii ni katika Hadith alizozipokea Al-Bukhari peke yake na imekuja katika sahihi mbili kwamba Mtume ﷺ amesema siku ya ufunguzi wa Makkah,

«إِنَّ اللَّهَ حَسَنَ عَنِ مَكَّةَ الْفَيْلِ، وَسَلَطَ عَلَيْهَا رَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنِينَ، وَإِنَّهُ قَدْ عَادَتْ
حُرْمَتُهَا الْيَوْمَ كَحُرْمَتِهَا بِالْأَمْسِ، أَلَا فَلْيَبْلُغِ الشَّاهِدُ الْغَائِبَ»

¹ Angalia maelezo ya kutosha katika Siira ya Ibnu Hishaam 1:96-103.

¹ *Fat'hul Al-Bari* 5:388.

"Hakika Mwenyezi Mungu Aliwazuia ndovu Makkah na Akaukabidhi mikononi mwa Mjumbe wake na waumini na hakika umerudi utukufu wake leo, kama ulivyokuwa utukufu wake hapo jana. Zindukeni! naafikishe aliyekuwepo kwa asiyekuwepo."¹

Huu ni mwisho wa *Tafsiri ya Surat Al-Fil*. Na ni kwa Allah تعالی tu Kusifiwa na Kuneemesha.



¹ *Fat'hul Al-Bari* 1:248 na *Muslim* 2:988.

Tafsiri ya Suratu Quraysh

Sura ya 106

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

<p>سُوْرَةُ الْقُرَيْشِ</p> <p>بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ</p> <p>لَا يَلْفُ قُرَيْشٍ ۝ إِذْ لَفِهِمْ رِحْلَةَ الشِّتَاءِ وَالصَّيْفِ ۝ فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ الَّذِي أَطْعَمَهُمْ مِنْ جُوعٍ وَءَامَنَّهُمْ مِنْ خَوْفٍ ۝</p>

لَا يَلْفُ قُرَيْشٍ ۝ إِذْ لَفِهِمْ رِحْلَةَ
 الشِّتَاءِ وَالصَّيْفِ ۝ فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ
 هَذَا الْبَيْتِ ۝ الَّذِي أَطْعَمَهُمْ
 مِنْ جُوعٍ وَءَامَنَّهُمْ مِنْ خَوْفٍ ۝

1. Kwa walivyo zoea MaKureshi.
2. Kuzoea kwao safari za siku za baridi na siku za joto.

3. Basi na wamuabudu Mola Mlezi wa Nyumba hii.

4. Ambaye Anawalisha wasipate njaa, na Anawalinda na khofu.

Sura hi iimetenganishwa na ile iliyo kabla yake katika Msahafu wa Al-Imamu –Msahafu ambao uliandikwa wakati wa Khalifa Uthman bin ‘Affani رضي الله عنه – waliandika katika sura mbili hizo msitari (*Bismillahir-Rahmanir Rahiim*) ijapokuwa pana uhusiano kati ya sura mbili hizo. Kama alivyoliweka wazi hilo. Muhammad bin Ishaq na Abdur Rahman bin Zaid bin Aslam kuwa maana yake ni: ‘Tumewazuia ndovu Makkah na Tumewaangamiza watu wake’.

لَا يَلْفُ قُرَيْشٍ ۝

“Kwa walivyo zoea Makureshi.”

Maana yake: Kwa sababu ya kuungana kwao na kukusanyika kwao katika mji wao hali ya kuwa wamo katika amani. Na pamesemwa: Makusudi ya maneno

hayo ni yale waliyokuwa wanayazoea miongoni mwa msafara katika wakati wa kusi kuelekea Yemeni na katika kipindi cha kaskazi wakielekea Sham, kwa mambo ya biashara na mengine. Kisha wanarejea mjini kwao hali ya kuwa wamo katika amani katika safari zao. Kwa sababu ya Utukufu wao mbele za watu, kwa sababu wao ni wakazi wa Haramu ya Mwenyezi Mungu – mahali ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Aempatukuza – Kwa hiyo yule anayewajua anawaheshimu. Mwenye kuhusishwa na wao na akaenda pamoja nao hupata amani kwa sababu yao. Na hii ndiyo hali yao katika safari zao, katika kaskazi yao na kusi yao. Ama katika hali ya ukazi wao katika mji wa Makkah ni kama Alivyosema Allah تعالى:

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا جَعَلْنَا حَرَمًا ءَامِنًا وَتُتَخَطَّفُ النَّاسُ مِنْ حَوْلِهِمْ

“Je! Hawaoni ya kwamba Tumeifanya nchi takatifu ina amani, na hali watu wengine wananyakuliwa kote kwa majirani zao?” (29:67)

Na Ndivyo Allah تعالى Alivyosema katika Kauli Yake,

لَا يَلْفُ قُرَيْشٍ ۖ إِيَّاهُمْ

“Kwa walivyo zoea Makureshi Kuzoea kwao?”

Analifasiri hilo walilolizoea: Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى:

إِيَّاهُمْ رِحْلَةَ الشِّتَاءِ وَالصَّيْفِ ۚ

“Kuzoea kwao safari za siku za baridi na siku za joto.”

Amesema Ibnu Jariir رحمه الله تعالى kwamba Lamu, ya “*Liyilafi*” – Ni kustaajabu kana kwamba Anasema: Staajabuni kuzoea kwa Makureishi na Kuneemesha Kwangu juu yao katika hilo. Amesema, na hilo linatokana na kukubaliana Waislamu wote juu ya kwamba hizo ni sura mbili zenye kutengana na zenye kujitegemea.

Kisha Amewaongoza kwenye kuishukuru neema hii kubwa kwa kusema: Kama Alivyosema Allah تعالى:

فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ هَذَا الْبَيْتِ ۚ

“Basi nawamuabudu Mola Mlezi wa Nyumba hii.”

Kwa maana basi na wamuabudu Yeye Pekee wasimshirikishe Allah تعالى kama vile Alivyowajaalia Haram yenye usalama na Nyumba Tukufu.

Kama Alivyosema Allah تعالى,

إِنَّمَا أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ رَبَّ هُدَيْتَنِي الْبَلَدَةَ الَّتِي حَرَّمَهَا وَلَهُ كُلُّ شَيْءٍ وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ
مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿١﴾

“Ama mimi nimeamrisha nimuabudu Mola Mlezi wa mji huu Aliyeufanya ni mtakatifu; na ni Vyake Yeye tu vitu vyote. Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waislamu, wenye kunyenyekea.” (27:91)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

الَّذِي أَطَعَهُمْ مِنْ جُوعٍ

“Ambaye Anawalisha wasipate njaa.”

Maana yake: Yeye Ndiye Bwana wa Nyumba hii na Yeye Ndiye Aliyewalisha kutokana na njaa.

وَأَمَّنَّهُمْ مِنْ خَوْفٍ ﴿٢﴾

“Na Anawalinda na khofu.”

Maana yake: Amewafanyia wema kwa amani na wampwekeshe kwa kumuabudu Yeye Peke Yake akiwa hana mshirika na wasiabudu kinyume chake sanamu lolote wala mshirika yoyote. Na kwa sababu hiyo yule atakayeliitikia jambo hili Atamkusanyia Allah تعالى kati ya amani ya dunia na akhera na atakayeasi basi atanyang'anywa hayo mawili kwake.

Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا قَرْيَةً كَانَتْ ءَامِنَةً مُطْمَئِنَّةً يَأْتِيهَا رِزْقُهَا رَغَدًا مِنْ كُلِّ مَكَانٍ

فَكَفَرَتْ بِأَنْعَمِ اللَّهِ فَأَذَاقَهَا اللَّهُ لِبَاسَ الْجُوعِ وَالْخَوْفِ بِمَا كَانُوا يَصْنَعُونَ ﴿٣﴾

وَلَقَدْ جَاءَهُمْ رَسُولٌ مِنْهُمْ فَكَذَّبُوهُ فَأَخَذَهُمُ الْعَذَابُ وَهُمْ ظَالِمُونَ ﴿٤﴾

“Na Mwenyezi Mungu Amepiga mfano wa mji uliokuwa na amani na utulivu, riziki yake ikiufikia kwa nafasi kutoka kila mahali. Lakini ukazikufuru neema za Mwenyezi Mungu; kwa hivyo Mwenyezi Mungu Akauvika vazi la njaa na khofu kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyafanya. Na alikwisha wajia Mjumbe miongoni mwao wenyewe. Lakini wakamkanusha; basi iliwafika adhabu hali ya kuwa wamedhulumu.” (16:112-113)

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Liilafi Qureishi*. Na ni kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu Kusifiwa na Kuneemesha.



Tafsiri ya Suratul Ma'un

Sura ya 107

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْمَاعُونِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَرَأَيْتَ الَّذِي يُكَذِّبُ بِالذِّينِ ۚ فَذَلِكَ الَّذِي

يَدْعُ الْيَتِيمَ ۚ وَلَا تَحْضُ عَلَىٰ طَعَامِ الْمَسْكِينِ ۚ

فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ ۚ الَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ

۝ الَّذِينَ هُمْ يُرَاءُونَ ۚ وَيَمْنَعُونَ الْمَاعُونَ ۝

أَرَأَيْتَ الَّذِي يُكَذِّبُ بِالذِّينِ ۚ ①

فَذَلِكَ الَّذِي يَدْعُ الْيَتِيمَ ②

وَلَا تَحْضُ عَلَىٰ طَعَامِ الْمَسْكِينِ ③

فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ ④ الَّذِينَ هُمْ

عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ⑤ الَّذِينَ

هُم يُرَاءُونَ ⑥ وَيَمْنَعُونَ

الْمَاعُونَ ⑦

1. Je! Umemuona anayekadhibisha Malipo?
2. Huyu ndiye anayemsukuma yatima.
3. Wala hahimizi kumlisha masikini.
4. Basi, ole wao wanaosali.
5. Ambao wanapuuzza Sala zao;
6. Ambao wanajionesha,
7. Nao huku wanazuia msaada.

Sifa za Wenye Kukanusha Qiyama

Allah تعالى Anasema: “Jee umemjua Ewe Muhammad yule anayekadhibisha Dini?” Nayo ni marejeo ya akhera na malipo,

فَذٰلِكَ الَّذِي يَدْعُ الْيَتِيْمَ ﴿١٧﴾

“Huyo ndiye anayemsukuma yatima.”

Maana yake: Ni yule anayemtenza nguvu yatima na anaidhulumu haki yake na hampi chakula na hamfanyii wema.

وَلَا يَخْضُ عَلٰى طَعَامِ الْمَسْكِيْنِ ﴿١٨﴾

“Wala hahimizi kumlisha masikini.”

Kama Alivyosema Allah تعالى:

كَلَّا ۗ بَلْ لَا تَكْرُمُوْنَ الْيَتِيْمَ ﴿١٧﴾ وَلَا تَخْضُوْنَ عَلٰى طَعَامِ الْمَسْكِيْنِ ﴿١٨﴾

“Sivyo hivyo! Bali nyinyi hamuwakirimu mayatima. Wala hamhimizani kulisha masikini.” (89:17-18)

Anamkusudia fukara ambaye hana chochote cha kumtoshelezea mahitaji yake na tosha yake. Kisha Amesema Allah تعالى:

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّيْنَ ﴿١٩﴾ الَّذِيْنَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُوْنَ ﴿٢٠﴾

“Basi, ole wao wanaosali ambao wanapuuza Sala zao.”

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما na wengine, anawakusudia wanafiki ambao wanasali katika hali ya kuonekana na hawasali katika hali ya siri.¹

Na kwa sababu hiyo Amesema:

لِّلْمُصَلِّيْنَ ﴿١٩﴾

“Wanao sali.”

Wale ambao ni katika watu wa Sala na wamelazimiana nayo. Kisha wao na hiyo Sala wanasahau, ama kutoitenda kabisa kama alivyosema Ibnu Abbas

¹ At-Tabari 24:632.

رضي الله عنهما. Au inaweza kumaanisha kutoitenda katika wakati uliopangwa kwa Sala hiyo kisheria, kwa hiyo anatoka kwenye wakati wake kabisa kama alivyosema Masrouq na Abu Duhaa.¹

Amesema Atwaa bin Dinar: Sifa Njema ni za Allah تعالى Ambaye Amesema:

عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٦﴾

“Ambao wanapuuza Sala zao.”

Na hakusema wanaosahau ndani ya Sala zao.²

Ama wanaitoa kwenye wakati wake wa kwanza, kwa hiyo wanaichelewesha mpaka mwisho wa wakati wake, siku zote au mara nyingi. Ama wanaichelewesha kuitekeleza kwa nguzo zake na sharti zake kwa njia iliyoamrisha. Ama kukosa unyenyekevu ndani yake na kuyazingatia maana yake. Kwa ujumla tamko linayakusanya yote hayo. Isipokuwa ni kwamba mwenye kusifika na kitu chochote katika hayo atakuwa na sehemu katika aya hii na mwenye kusifika na yote kwa hakika limekamilika fungu lake katika mambo hayo na umekamilika kwake unafiki wake kimatendo. Kama ilivyothibitika katika sahihi mbili kwamba Mtume ﷺ amesema,

«تِلْكَ صَلَاةُ الْمُنَافِقِ، تِلْكَ صَلَاةُ الْمُنَافِقِ، تِلْكَ صَلَاةُ الْمُنَافِقِ، يَجْلِسُ يَرْقُبُ
الشَّمْسَ، حَتَّى إِذَا كَانَتْ بَيْنَ نَرْنِيهِ الشَّيْطَانِ قَامَ فَتَقَرَّ أَرْبَعًا، لَا يَذْكُرُ اللَّهَ فِيهَا إِلَّا
قَلِيلًا»

“Hiyo ni Sala ya mtu mnafiki, hiyo ni Sala ya mtu mnafiki, Hiyo ni Sala ya mtu mnafiki, anakaa akiliangalia jua mpaka litakapokuwa kati ya pembe mbili za shetani husimama akadonoa mara nne hamtaji ndani ya Sala hiyo Allah تعالى isipokuwa kidogo sana.”³

Na huu ni mwisho wa Sala ya Al-Asri ambayo ndiyo Sala ya kati kama iliyothibitika andiko kwa aya iliyo wazi mpaka mwisho wa wakati wake. Nao ni wakati wa karaha kisha akasimama kwenye hizo Sala akadonoa donoa kama

¹ At-Tabari 24:631.

² Al-Qurtubi 20:212.

³ Fat'hul Al-Bari 6:386 na Muslim 1:434.

anavyodonoa kunguru hakutulizana na hakunyenyekaa ndani yake. Vile vile na kwa sababu hiyo amesema,

«لَا يَذْكُرُ اللَّهُ فِيهَا إِلَّا قَلِيلًا،»

“Hamtaji ndani yake Mwenyezi Mungu isipokuwa kidogo sana.”

Na hakika si jingine huenda kumempeleka kwenye Sala hiyo kuwaonesha watu si kutaka radhi ya Allah تعالى na Dhati Yake, kwa hiyo yeye anakuwa kana kwamba hkusali kabisa. Amesema Allah تعالى:

إِنَّ الْمُتَفِقِينَ لِيُخَدِعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِيعُهُمْ وَإِذَا قَامُوا إِلَى الصَّلَاةِ قَامُوا كَسَالَى يُرَاءُونَ

النَّاسَ وَلَا يَذْكُرُونَ اللَّهَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٤٢﴾

“Hakika wanaafiki wanamkhadaa Mwenyezi Mungu, na hali ni Yeye ndiye Mwenye kuwakhadaa wao. Na wanapoinuka kusali huinuka kwa unyong’onyo, wanajionesha kwa watu tu, wala hawamdhukuru Mwenyezi Mungu ila kidogo tu.” (4:142)

Na Akasema hapa hapa Allah تعالى:

الَّذِينَ هُمْ يُرَاءُونَ ﴿١٤٣﴾

“Ambao wanajionesha.”

Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Amri bin Murra amesema: Tulikuwa tumekaa mbele ya Abu Ubaida wakaitaja *Riyaa*. Mtu mmoja anayeitwa Abu Yaziid akasema, nilimsikia Abdullah bin Amri رضي الله عنه akiwa anasema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ سَمِعَ النَّاسَ بِعَمَلِهِ، سَمِعَ اللَّهُ بِهِ سَامِعَ خَلْقِهِ، وَحَقَّرَهُ وَصَغَّرَهُ،»

“Mwenye kuwasikilizisha watu matendo yake Atamsikilizisha Mwenyezi Mungu matendo hayo msikiaji katika viumbe wake na ataidharau kisha na ataifanya ndogo sana.”¹

¹ Ahmad 2:212.

Na katika yanayofungamana na Kauli Yake Allah تعالى،

الَّذِينَ هُمْ يُرْءَاوْنَ ﴿١﴾

“Ambao wanajionesha.”

Ni kwamba mwenye kufanya matendo kwa ajili ya Allah تعالى watu wakalionga hilo likawafurahisha, hilo kwa hakika halihesabiwi kuwa ni kuwaonesha watu.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَيَمْتَعُونَ الْمَاعُونَ ﴿٢﴾

“Nao huku wanazuia msaada.”

Maana yake: Hawakufanya vyema kumuabudu Mola Wao na hawakuwatendea wema viumbe Wake. Mpaka umefikia ubaya wao hawawaazimi watu vitu ambavyo watu wananufaika navyo na hupata msaada kutokana na vitu hivyo pamoja na kubaki dhati yake na kurejea kitu hicho kwao. Watu hawa kwa tabia zao hizo ndio hao hao ambao huzuia Zaka na namna za ibada mbali mbali zenye kukurubisha kwa Allah تعالى.

Amesema Al-Mas'udi kutoka kwa Salama Ibnu Kuhail kutoka kwa Abu Al-Ubiydaini kwamba aliulizwa Ibnu Mas'ud رضي الله عنه kuhusu *Al-Ma'un*, akasema, 'hicho ni kile wanachopeana watu na kuazimana, miongoni mwa vitu hivyo ni kama shoka, chungu, ndoo, na mifano ya hayo.¹

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya Sura hii na kwa Allah tu Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹ At-Tabari 24:639.

Tafsiri ya Suratul Kawthar Sura ya 108

**Iliteremshwa Madinah na Imesemwa
Vile Vile Kuwa Iliteremshwa Makkah**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْكَوْثَرِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ ﴿١﴾ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ ﴿٢﴾ إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ ﴿٣﴾

إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ ﴿١﴾ فَصَلِّ
لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ ﴿٢﴾ إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ
الْأَبْتَرُ ﴿٣﴾

1. Hakika Tumekupa kheri nyingi.

2. Basi sali na uchinje kwa ajili ya Mola Wako Mlezi.

3. Hakika anayekuchukia ndiye aliye mpungufu.

Amepokea Muslim, Abu Dawud na An-Nasai kutoka kwa Anas,¹ na tamko ni la Muslim amesema: wakati Mtume ﷺ yuko mbele yetu msikitini, ghafla alisinzia usinziaji wa mara moja kisha akanyanyua kichwa chake hali ya kuwa anatabasamu tukasema: ‘Ni jambo gani ambalo limekuchekesha Ewe Mtume?’ Akasema:

«لَقَدْ أَنْزَلْتُ عَلَيَّ آيَاتًا سُوْرَةً»

“Kwa hakika imeteremshwa kwangu punde hivi sasa sura.” Akasema:

إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ ﴿١﴾ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ ﴿٢﴾ إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ ﴿٣﴾

“Hakika Tumekupa kheri nyingi. Basi sali na uchinje kwa ajili ya Mola Wako Mlezi. Hakika anayekuchukia ndiye aliye mpungufu.”

¹ Muslim 1:300, Abu Dawud 5:110, na An-Nasai katika Al-Kubra 6:533

Kisha Akasema:

«أَتَذَرُونَ مَا الْكَوْثُرُ؟»

“Jee mnajuwa nini Al-Kauthar.”

Tukasema: ‘Allah تعالى na Mtume wake ﷺ wanajua.’ Akasema:

«فَإِنَّهُ نَهَرٌ وَعَدْنِيهِ رَبِّي عَزَّ وَجَلَّ، عَلَيْهِ خَيْرٌ كَثِيرٌ، هُوَ حَوْضٌ تَرُدُّ عَلَيْهِ أُمَّتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ، آيَتُهُ عَدَدُ النُّجُومِ فِي السَّمَاءِ، نِيْحْتَلِجُ الْعَبْدُ مِنْهُمْ فَأَقُولُ: رَبِّ إِنَّهُ مِنْ أُمَّتِي، فَيَقُولُ: إِنَّكَ لَا تَدْرِي مَا أَخَذْتُ بِغَدَاكَ»

“*Hakika Kauthar ni mto ambao Ameniahidi Mola Wangu Mwenye Kushinda na Kutukuka, juu yake kuna kheri nyingi sana, mto huo ni birika ambalo watakunywa katika birika hilo ummati wangu, siku ya Kiyama. Vyombo vyake, idadi yake ni kama idadi ya nyota za Mbinguni, atavutwa mja katika wao, nitasema, ‘Ewe Bwana Wangu hakika huyo ni katika Umati wangu. Allah Atasema: **Hakika wewe hujui yaliyozushwa baada yako.**”¹*

Ahmad amepokea Hadithi ikiwa na njia tatu za mapokezi kutokana na Muhammad bin Fudhail kutoka kwa Mukhtaar bin Fulful nae kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه.² Na amepokea Imam Ahmad, vile vile kutoka kwa Anas رضي الله عنه amesema: Amesema Mtume ﷺ

«دَخَلْتُ الْجَنَّةَ فَإِذَا أَنَا بِنَهْرٍ حَافَتَاهُ خِيَامُ اللَّوْزِ، فَضَرَبْتُ بِيَدِي إِلَى مَا يَجْرِي فِيهِ الْمَاءِ، فَإِذَا مِنْكَ أَدْفَرٌ، قُلْتُ: مَا هَذَا يَا جِبْرِيْلُ؟ قَالَ: هَذَا الْكَوْثُرُ الَّذِي أُعْطَاكَ اللهُ عَزَّ وَجَلَّ»

“*Niliingia peponi, ghafla nikawa kwenye mto, kingo zake mbili ni mahema ya lulu, nikapiga kwa mkono wangu zile sehemu ambazo yanapita ndani yake maji, ghafla nikaona miski yenye harufu nzuri sana nikauliza: ‘Ni nini hiki Ewe Jibril?’ Jibril akanijibu: ‘Hii ndiyo Kawthar ambayo Mwenyezi Mungu, Mwenye Kushinda na Kutukuka, Amekupatia.’³*

Bukhari amepokea katika sahihi yake. Na Muslim amepokea kutoka kwa Anas bin Malik amesema wakati alipopandishwa Mtume ﷺ mbinguni, alisema:

¹ Muslim 1:300.

² Ahmad 3:102.

³ Ahmad 3:103.

«أَتَيْتُ عَلَى نَهْرٍ حَافَتَاهُ قَبَابُ اللَّوْلُؤِ الْمُجَوَّبِ فَقُلْتُ: مَا هَذَا يَا جِبْرِيلُ؟ قَالَ: هَذَا الْكَوْثَرُ»

“Niliuendea mto, kingo zake mbili ni za lulu yenye uwazi, nikauliza: ‘Ni kitu gani hiki Ewe Jabril?’ Akanijibu: ‘Hii ndiyo Kawthar.’”

Na hilo ni tamko la Bukhari, Allah تعالى Amrehemu.

Ahmad amepokea kutoka kwa Anas رضي الله عنه kwamba mtu mmoja aliuliza: ‘Ee, Mtume! Ni nini Kawthar?’ Mtume ﷺ akasema:

«هُوَ نَهْرٌ فِي الْجَنَّةِ أُعْطِيَهُ رَبِّي، لَهُوَ أَشَدُّ بَيَاضًا مِنَ اللَّبَنِ، وَأَخْلَى مِنَ الْعَسَلِ، فِيهِ طُيُورٌ أُعْتِقَتْهَا كَأَعْتَابِي الْجُزُرِ»

“Huo ni mto ulio peponi, Amenipa mto huo Mola Wangu, kwa hakika mto huo ni mweupe sana kuliko maziwa na matamu sana kuliko asali, ndani yake mna ndege, shingo zao ni kama shingo za ngamia.”

Umar رضي الله عنه akasema, ‘Ee Mtume ﷺ, hakika Ndege hao wamo katika neema kubwa sana, na wamo katika starehe sana.’ Mtume ﷺ akamjibu akisema,

«أَكَلَهَا أَنْعَمُ مِنْهَا يَا عُمَرُ»

*“Walaji wake watakuwa katika neema zaidi kuliko hiyo Ee Umar.”*²

Al-Bukhari amepokea kutoka kwa Said bin Jubair naye kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما kwamba yeye amesema katika maana ya *Kawthar* kuwa, hiyo ni kheri ambayo Allah تعالى Alimpa Mtume ﷺ. Amesema Abu Bishr: nilimuambia Said bin Jubair: ‘Hakika kuna watu wanaodai kwamba hiyo *Kawthar* ni mto ulio peponi.’ Akasema Said: ‘Mto ulio peponi ni katika kheri ambazo Amempa Allah تعالى.’³ Na ameipokea vilevile kutoka kwa Said bin Jubair kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema: ‘*Al-Kawthar* ni kheri nyingi.’⁴ Na tafsiri hii inauenea mto na mambo mengine kwa sababu tamko *Al-Kawthar* linatokana na neno “*Kathra*” nazo ni kheri nyingi.

¹ Al-Bukhari Na. 4946.

² Ahmad 3:220.

³ *Fath Al-Bari* 8:603.

⁴ At-Tabari 24:648.

Imamu Ahmad amepokea kutoka kwa Ibnu Umar رضي الله عنهما, amesema, amesema Mtume ﷺ,

«الْكَوْثَرُ نَهْرٌ فِي الْجَنَّةِ حَافَتَاهُ مِنْ ذَهَبٍ، وَالْمَاءُ يَجْرِي عَلَى اللُّؤْلُؤِ، وَمَاؤُهُ أَشَدُّ
بَيَاضًا مِنَ اللَّبَنِ، وَأَخْلَى مِنَ الْعَسَلِ»

“Al-Kawthar ni mto ulio peponi kingo zake mbili ni za dhahabu na maji yanapita juu ya lulu na maji yake ni meupe sana kuliko maziwa na matamu sana kuliko asali.”¹

Na kama hivyo amepokea Tirmidhi, Ibnu Majah, Ibnu Abi Hatim na Ibnu Jarir. Na Tirmidhi amesema kuwa Hadithi hii daraja yake ni Hassan Sahihi.²

Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ ﴿١﴾

“Basi sali na uchinje kwa ajili ya Mola Wako Mlezi.”

Maana kama Tulivyokupa kheri nyingi duniani na akhera na katika kheri hizo ni mto ambao imetangulia sifa yake. Kwa hivyo Mtakasiye Mola Wako Swala yako ya faradhi na ya suna na kuchinja kwako na umuabudu Yeye hali ya kuwa Peke Yake hana mshirika. Na chinja kwa Jina Lake Peke Yake, hali ya kuwa hana mshirika. Kama Alivyosema:

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾ لَا شَرِيكَ لَهُ وَبِذَلِكَ
أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ ﴿٢﴾

“Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote. Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyoamrisha, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu.” (6:162-163)

Amesema hayo Ibnu Abbas, Atwaa, Mujahid, Ikrima na Al-Hassan رضي الله عنهم anakusudia kwa maneno hayo kuwachinja ngamia na mfano wake.³ Na kama hivyo amesema Qatadah, Muhammad bin Kaab Al-Quradhi, Adh-Dhahak, Rabii,

¹ Ahmad 2:67

² Tuhfat Al-Ahwadhi 9:294, Ibnu Majah 2:1450 na At-Tabari 24:650.

³ At-Tabari 24:653.

'Atwaa Al-Khurasani, Al-Hakam, Ismail bin Abi Khalid na wengine katika wafasiri waliotangulia (*Salaf*).¹ Na haya yanatofautiana na yale waliyokuwa juu yake washirikina miongoni mwa kumsujudia asiyekuwa Allah تعالی na kuchinja juu ya lisilokuwa Jina lake. Kama Alivyosema Allah تعالی:

وَلَا تَأْكُلُوا مِمَّا لَمْ يُذَكَّرْ أَسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَإِنَّهُ لَفِسْقٌ

“Wala msile katika wale wasiosomewa Jina la Mwenyezi Mungu. Kwani huo ni upotofu.” (6:121)

Adui wa Mtume ﷺ ndiye mwenye kukatikiwa na kheri zote

Kauli Yake Allah تعالی :

إِنَّ شَانِعَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ

“Hakika anayekuchukia ndiye aliye mpungufu.”

Maana yake: Hakika mwenye kukuchukia wewe Ewe Muhammad na mwenye kukichukia kile ulichokuja nacho miongoni mwa ukweli na uongofu na hoja iliyo wazi na nuru yenye kuangaza, huyo ndiye mwenye kunyimwa kila kitu, aliye mchache, mnyonge, mwenye kukatika utajo wake.

Amesema Ibnu Abbas, Mujahid, Said bin Jubair na Qatadah: Aya hii ilishuka kumhusu Al-'Aas bin Wail رضي الله عنهم.² Na amesema Muhammad bin Ishaq kutoka kwa Yazid bin Ruwman amesema: alikuwa Al-'Asw bin Wail pindi anapotajwa Mtume ﷺ anasema: “Muacheni kwani huyo ni mtu aliyekatikiwa na kheri zote, hana mbele yoyote, atakapokufa, utakatika utajo wake.” Ndipo Allah تعالی Akaiteremsha Sura hii.³

Na amesema Shammar bin Atiyya: Ilishuka kwa Uqba bin Abi Muayti.⁴ Na amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما vile vile na Ikrima amesema kuwa aya hii ilimshukia Ka'ab bin Ashraf na kundi katika Makureishi.⁵

Na amepokea Bazzar kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema: Alifika

¹ At-Tabari 24:654.

² At-Tabari 24:656 na 657.

³ Ibnu Hishaam 2:7 Ibn Is'haq ameipokea.

⁴ At-Tabari 24:657.

⁵ At-Tabari 24:657.

Ka'ab bin Al-Ashraf Makkah, Makureishi wakamuambia: 'Wewe ndiye mtukufu wao, hivi humtazami huyu mtu ambaye anajitenga na watu wake? Anayedai kwamba yeye ni mbora kuliko sisi, na ilhali sisi ndiyo wasimamizi wa mahujaji na tunaiangalia Al-Ka'aba, na tunawapa maji Mahujaji.' Ka'ab akasema: 'Nyinyi ni wa bora kuliko yeye.' Akasema ndipo hapo iliposhuka:

إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ ﴿١﴾

"Hakika anayekuchukia ndiye aliye mpungufu."

Kama hivyo amepokea Al-Bazzar na huo ni upokezi ulio sahihi.¹

Na kumepokewa kutoka kwa 'Atwaa amesema: Ilishuka kwa Abu Lahab wakati alipokufa mtoto wa Mtume ﷺ. Abu Lahab akaenda kwa Washirikina akasema: amekatwa Muhammad usiku huu. Akateremsha Allah تعالی katika jambo hilo:

إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ ﴿٢﴾

"Hakika anayekuchukia ndiye aliye mpungufu." Na amesema Sudi: walikuwa Waarabu. Pindi wanapokufa watoto wanamume wa mtu husema: Amekatwa. Kwani alipokufa mtoto mwanamume wa Mtume ﷺ wakasema: 'Limemfika la kumfika Muhammad.' Akateremsha Allah تعالی:

إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ ﴿٣﴾

"Hakika anayekuchukia ndiye aliyempungufu." Walidhani kutokana na ujinga wao, kwamba watakapokufa watoto wake utakatika utajo wake na sivyo hivyo. Tena sivyo hivyo, bali Allah تعالی Aliubakisha utajo wake juu ya vichwa vya mashahidi na Ameiwajibisha sheria zake juu ya Shingo za waja, yenye kuendelea na kubaki daima milele mpaka siku ya kukusanywa na kurejea. Rehma za Allah تعالی na Amani Yake ziwe juu yake siku zote – mpaka siku ya Qiyama.

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Al-Kawthar*. Na ni kwa Allah تعالی tu Kusifiwa na Kuneemesha.

* * *

¹ *Kashful Astaar* 3:83.

Tafsiri ya Suratul Kafirun

Sura ya 109

Iliteremshwa Makkah

Imethibiti katika Hadithi iliyo katika sahihi Muslim kutoka kwa Jabir رضي الله عنه, "kwamba Mtume ﷺ alisoma sura hii, na

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾

"Qul-huwallahu Ahad." (112:1).

Katika rakaa mbili za *Twawafu*,¹ Na imekuja katika sahihi Muslim, katika Hadithi ya Abu Huraira رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ alizisoma sura mbili hizo katika rakaa mbili za *Al-Fajri*.² Na amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Ibnu Umar رضي الله عنهما, kwamba Mtume ﷺ alisoma katika rakaa mbili kabla ya Sala ya *Al-Fajri* na rakaa mbili baada ya *Al-Magharibi* mara zaidi ya ishirini au zaidi ya kumi.

قُلْ يَتَّيِبُهَا لَكُمْ فَارُوا بَ ﴿٢﴾

"Qul-yaa-Ayyuhal-Kafiruun." na

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾

"Qul-Huwallahu Ahad." (112:1)³

Na amepokea Ahmad vile vile kutoka kwa Ibnu Umar رضي الله عنهما, amesema; "Nilimuona Mtume ﷺ kiasi cha mara ishirini na nne au ishirini na tano akisoma kabla ya *Al-Fajri* na rakaa mbili kabla ya Maghrib,

قُلْ يَتَّيِبُهَا لَكُمْ فَارُوا بَ ﴿٢﴾

"Qul-Yaa Ayyuhal kafiruun." na,

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾

"Qul Huwallahu Ahad". (112:1)⁴

¹ Muslim 2:888 katika Hadithi ndefu.

² Muslim 1:502.

³ Ahmad 2:24 na 58.

⁴ Ahmad 2:99.

Katika hadithi nyingine kama hiyo iliyopokelewa na Imamu Ahmad kutoka kwa Ibnu Umar رضي الله عنهما kuwa amesema, "Nilimuona Mtume ﷺ kiasi cha mwezi akisoma kabla ya *Al-Fajri*.

قُلْ يَتَّيِبُهَا لَكُمْ فَارُوا

"Qul-Yaa Ayuuhal Kafiruun." na,

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ

"Qul Huwallahu Ahad."¹

Na kama hivyo amepokea At-Tirmidhi, Ibnu Majah na An-Nasai ameithibitisha, na amesema At-Tirmidhi; Hadithi hii ni Hasan.²

Na imetangulia katika Hadithi kwamba sura hii inalingana na robo ya Qur-ani, na '*Idhaa Zulzilal*' inalingana na robo ya Qur-ani kadhalika.

* * *

¹ Ahmad 2:94.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 2:470, Ibn Majah:1:363 na An-Nasaai 2:170.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

<p>سُورَةُ الْكَافِرُونَ</p>	
<p>بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ</p>	
<p>قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ ﴿١﴾</p>	<p>لَا أَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٢﴾</p>
<p>وَلَا أَنَا عَابِدٌ مَّا عَبَدْتُمْ ﴿٣﴾</p>	<p>وَلَا أَنَا عَابِدٌ مَّا عَبَدْتُمْ ﴿٤﴾</p>
<p>وَلَا أَتُنَمُّ عِبَادُونَ مَّا أَعْبُدُ ﴿٥﴾</p>	<p>وَلَا أَتُنَمُّ عِبَادُونَ مَّا أَعْبُدُ ﴿٦﴾</p>
<p>لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِيَ دِينِ ﴿٧﴾</p>	<p>لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِيَ دِينِ ﴿٨﴾</p>

قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ ﴿١﴾ لَا
 أَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٢﴾ وَلَا أَتُنَمُّ
 عِبَادُونَ مَّا أَعْبُدُ ﴿٣﴾ وَلَا أَنَا عَابِدٌ
 مَّا عَبَدْتُمْ ﴿٤﴾ وَلَا أَتُنَمُّ عِبَادُونَ مَّا
 أَعْبُدُ ﴿٥﴾ لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِيَ دِينِ ﴿٦﴾

1. Sema: Enyi makafiri!
2. Siabudu mnachokiabudu.
3. Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu.
4. Wala sitaabudu mnachoabudu.
5. Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu.
6. Nyinyi mna dini yenu, nami nina Dini yangu.

Kuepukana na Shirki.

Hii ni sura ya kuepukana na matendo ambayo wanayatenda washirikina; nayo inaamrisha kufanya ikhlasi. Ndani yake kuna Kauli Yake Allah تعالیٰ,

قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ ﴿١﴾

“Sema: Enyi makafiri!”

Kauli hiyo inakusanya kila kafiri aliye juu ya uso wa ardhi. Isipokuwa ni kuwa hapa waliokusudiwa kwa maneno haya ni makafiri wa Kikuraishi. Na imesemwa; “Hakika wao kutokana na ujinga wao walimuita Mtume ﷺ kwenye kuabudu masanamu yao kwa muda wa mwaka mmoja, nao wamuabudu Mungu

wake kwa muda wa mwaka mmoja, Akaiteremsha Allah تعالى sura hii, na Akamuamrisha Mjumbe wake ﷺ katika sura hii ajiepushe na dini yao moja kwa moja,

لَا أُعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ﴿١﴾

“Siabudu mnachokiabudu.”

Anakusudia masanamu na vile vilivyoshirikishwa na Allah تعالى,

وَلَا أَنْتُمْ عِبُدُونَ مَا أُعْبُدُ ﴿٢﴾

“Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu.”

Naye ni Allah تعالى Peke Yake hali ya kuwa hana mshirika, na neno ‘Maa’ hapa lina maana ya ‘Man’. Kisha Amesema;

وَلَا أَنَا عَابِدٌ مَا عَبَدْتُمْ ﴿٣﴾ وَلَا أَنْتُمْ عِبُدُونَ مَا أُعْبُدُ ﴿٤﴾

“Wala sitaabudu mnachoabudu. Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu.”

Maana yake: Wala siabudu Ibada yenu. Maana sifuati wala siigi na hakika si kinyume na hivyo ninamuabudu Allah تعالى juu ya njia ambayo Anaipenda na Anayoiridhia. Na kwa sababu hiyo Amesema,

وَلَا أَنْتُمْ عِبُدُونَ مَا أُعْبُدُ ﴿٥﴾

“Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu.”

Maana yake: hamfuati maamrishi ya Allah تعالى na sheria Zake katika ibada yao, bali ni kwamba mmelizua jambo kutokana na nafsi zenu. Kama Alivyosema,

إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَمَا تَهْوَى الْأَنْفُسُ ۗ وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنْ رَبِّهِمْ الْهُدَىٰ ﴿٦﴾

“...Hawafuati ila dhana tu na kipendacho nafsi. Na kwa yakini uwongofu ulikwisha wafikia kutoka kwa Mola Wao Mlezi.” (53:23)

Hivyo: Akajiepusha na wao katika mambo yote ambayo wao wamo ndani yake, kwani mwenye kuabudu hapana budi awe na cha kuabudiwa ambacho anakiabudu na ibada anayoifuata. Kwani Mtume ﷺ pamoja na wafuasi wake

wanamuabudu Allah تعالى kwa kile Alichokiamrisha ndio maana kalima ya Uislamu, “*Laa ilaha illa Llah Muhammada Rasuulullah*, kwa maana hakuna kinachoabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى na hakuna njia isipokuwa aliyokuja nacho Mtume ﷺ. Na washirikina wanaabudu asiyekuwa Allah تعالى ibada ambayo Allah تعالى hakuidhinisha na ndio Mtume ﷺ akawajibu kama alivyoelekezwa na Mola wake,

لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِيَ دِينِ ﴿١﴾

“Nyinyi mna dini yenu, nami nina Dini yangu.”

Au Kama Allah تعالى Alivyosema,

وَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ لِي عَمَلِي وَلَكُمْ عَمَلُكُمْ أَنْتُمْ بَرِيئُونَ مِمَّا أَعْمَلُ وَأَنَا بَرِيءٌ مِمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٤١﴾

“Na wakikukanusha wewe, sema: Mimi nina a’ mali yangu, na nyinyi mna a’ mali yenu. Nyinyi hamna jukumu kwa niyatendayo, wala mimi sina jukumu kwa myatendayo.” (10:41). Na,

لَنَا أَعْمَلُنَا وَلَكُمْ أَعْمَلُكُمْ

“Sisi tuna jukumu kwa vitendo vyetu, na nyinyi mna jukumu kwa vitendo vyenu.” (28:58)

Na Al-Bukhari amesema kuwa imesemwa,

لَكُمْ دِينُكُمْ

“Nyinyi mna dini yenu.” Maana yake: Ukafiri

وَلِيَ دِينِ ﴿١﴾

“Nami nina Dini yangu.” Maana yake: Uislamu,”

Hii ndio mwisho wa *Suratu Qul Yaa-Ayuhal Kafirun*.

* * *

¹ Fat’h Al-Bari 8:604.

Tafsiri ya Suratu An-Nasr Sura ya 110 Iliteremshwa Madinah

Ubora wa *Suratu An-Nasr*

Imetangulia kwamba sura hii inalingana na robo ya Qur'an na *Idhaa Zulzilati*, inalingana na robo ya Qur'an.

Amepokea An-Nasai kutoka kwa Abdullah bin Abdullah bin 'Utba amesema, aliniambia Ibnu Abbas رضي الله عنهما – ewe Ibnu Utba; 'Jee unajua sura ya mwisho katika Qur'an iliyoshuka?' Nikasema, 'Ndiyo.'

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿١﴾

***"Idhaa Ja-a Nasrullahi Walfathu."* (110:1)**


Akasema umesema kweli.¹

* * *

¹ An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:525.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.



إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿١﴾
 وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ
 اللَّهِ أَفْوَاجًا ﴿٢﴾ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ
 وَأَسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ﴿٣﴾

1. Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi.

2. Na ukaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi.

3. Zitakase Sifa za Mola Wako Mlezi, na umuombe msamaha; hakika Yeye Ndiye Anayepokea toba.

Sura Hii Inaelezea Ukomo wa Muda wa Mtume ﷺ.

Ampokea Bukhari kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema alikuwa Umar رضي الله عنه akiniingiza pamoja na Masheikh wa Badri ikawa kana kwamba baadhi yao wamekasirika katika nafsi zao, wakasema, “Kwa nini anamuingiza huyu pamoja nasi? Na hali ya kuwa sisi tuna watoto mfano wake?” Akasema Umar رضي الله عنه, ‘hakika huyu ni katika wale ambao kwa hakika mmemjua.’

Akawaita siku moja, akaniingiza pamoja na wao sikuona kwamba yeye aliniita kwao siku hiyo isipokuwa awaoneshe kitu, akasema, ‘mnasemaje katika Kauli Yake Allah تعالى,

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿١﴾

“Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi.”

Wakasema baadhi yao, “Tumeamrisha tumsifu Allah تعالى na tumtake msamaha pindi tutakaponusuriwa na tukapata ushindi.” Wakanyamaza baadhi yao hawakusema kitu chochote.

Umar رضي الله عنه akaniambia, “Ni hivyo hivyo unasema ewe Ibnu Abbas?” Nikasema, “hapana.” Akasema, “unasema nini?” Nikasema, “hiyo ni ajali (utabiri wa kifo cha Mtume) ya Mtume ﷺ nimejua kutoka kwake.” Kisha akasoma,

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿١﴾

“Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi.”

Hiyo ni alama ya ajali yako. Kwa hivyo basi,

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَأَسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ﴿٢﴾

“Zitakase Sifa za Mola Wako Mlezi, na umuombe msamaha; hakika Yeye Ndiye Anayepokea toba.”

Akasema Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه; “Sijui kutokana na sura hii isipokuwa haya unayoyasema.”¹ Bukhari amepokea peke yake.

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema; iliposhuka,

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿١﴾

“Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi.”

Alisema Mtume ﷺ,

«نُعِيْتُ إِلَى نَفْسِي»

“Imetangaziwa kifo nafsi yangu.”

Kwa hakika yeye atafishwa mwaka huo.² Ahmad amepokea peke yake.

Na amepokea Bukhari kutoka kwa Aisha رضي الله عنها amesema, “Alikuwa Mtume ﷺ katika rukuu yake na sujudu yake husema, na katika mwisho wa uhai huzidisha kwa kusema,

«سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَبِحَمْدِكَ اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي»

“Subhaabanaka Allahumma Rabbana Wabihamdika Allahumma Ighfir lili.”³

¹ Fat’hul Al-Bari 8:60 na Ibn Majah 1:287.

² Ahmad 1:217.

³ Fat’h Al-Bari 8:605.

Kwa maana, “Kutakasika ni Kwako na kwa Kuhimidiwa ni Kwako ee Mola Wangu nisamehe.” Kundi nzima lilipokea Hadithi hii isipokuwa At-Tirmidhi.¹

Imam Ahmad amepokea kutoka kwa Masrouq kuwa amesema, Aisha رضي الله عنها amesema, “Mtume ﷺ alikuwa akikithirisha kila mara kusoma,

«سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ، أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ»

“Kutakasika na Kuhimidiwa ni Kwako, Ee Mola Wangu nisamehe na natubia Kwako.”

Kadhalika amesema,

«إِنَّ رَبِّي تَمَّانٌ أَخْبَرَنِي أَنِّي سَأَرَى عَلَامَةً فِي أُمَّتِي، وَأَمْرَنِي إِذَا رَأَيْتَهَا أَنْ أَسْبِغَ بِحَمْلِهِ وَأَسْتَغْفِرَهُ، إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا، فَقَدْ رَأَيْتَهَا: ﴿إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ﴾¹ وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا ﴿تَسْبِغَ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَأَسْتَغْفِرُهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا﴾²»

*“Kwa hakika Mwenyezi Mungu Alishaniambia kuwa nitaona alama katika Ummat wangu, na Akaniamrisha pindi nitakapouona nimitakasie Kwake na nimuombe maghufira kwa hakika Yeye ni Mwingi wa Kusamehe, na kweli hilo nimeliona: **“Itakapokuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi. Na ukaona watu wanaingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi, Zitakase sifa za Mola Wako Mlezi, na umuombe msamaha; hakika Yeye Ndiye Anayepokea toba.”***² Na kadhalika amepokea Muslim.³

Na makusudio ya ufunguzi hapa ni ufunguzi wa Makka hiyo ni kauli moja. Kwani makabila ya waarabu yalikuwa yanachelewa kusilimu walingojee kufunguliwa kwa Makka na walikuwa wakisema; “Akiwashinda watu wake basi yeye ni Mtume.” Alipomfungulia Allah تعالى Makka waliingia katika Dini ya Allah, hali ya kuwa makundi makundi, haikupita miaka miwili, mpaka kikajaa kisiwa cha wArabu kwa imani na Uislamu na hii ni neema ya Allah تعالى tu.

¹ Muslim 1:350, Abu Dawud 1:546, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:525 na Ibn Majah 1:287.

² Ahmad 6:35.

³ Muslim 1:351.

Na amepokea Bukhari katika sahihi yake kutoka kwa Amri bin Salama amesema; "Alipoifungua Allah تعالى Makkah watu wote walifanya haraka kuingia katika Uislamu kwa kumfuata Mtume ﷺ. Makabila yaliokuwa yanachelewa kuingia katika Uislamu yakingojea kufunguliwa kwa Makkah, na wakati huo walikuwa wakisema; "Muacheni na watu wake akiwashinda basi yeye ni Mtume ﷺ."¹

Mwenye kutaka kusoma zaidi kuhusu kisa cha ufunguzi wa Makkah basi asome katika kitabu chetu kinachoitwa "As-Siira" mwenye kutaka maelezo hayo na akirejee kitabu hicho. Na ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.

Na amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Ammar, amezungumzia jirani wa Jabir bin Abdillahi amesema; "Nilifika kutoka safarini akanijia Jabir bin Abdallah akanisalimia nikawa ninamzungumzia kuhusu kutengana kwa watu na yale waliyoyazua, akawa Jabir رضي الله عنه analia kisha akasema nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«إِنَّ النَّاسَ دَخَلُوا فِي دِينِ اللَّهِ أَفْوَاجًا، وَسَيَخْرُجُونَ مِنْهُ أَفْوَاجًا»

*"Hakika watu wameingia katika Dini ya Mwenyezi Mungu hali ya kuwa makundi makundi na watatoka humo hali ya kuwa makundi makundi."*²

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Suratu An-Nasri*. Na ni kwa Allah تعالى tu Kusifiwa na Kuneemesha.



¹ Fat'h Al-Bari 7:616.

² Ahmad 3:343.

Tafsiri ya Suratu Tabbat¹

Sura ya 111

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

<p>سُورَةُ التَّبَاتِ</p> <p>بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ</p> <p>تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ ① مَا أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ ② سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ هَبٍ ③ وَامْرَأَتُهُ حَمَّالَةَ الْحَطَبِ ④ فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍ ⑤</p>
--

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ ① مَا
 أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ ②
 سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ هَبٍ ③
 وَامْرَأَتُهُ حَمَّالَةَ الْحَطَبِ ④ فِي
 جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍ ⑤

1. Imeangamia mikono ya Abu Lahab, na yeye pia ameangamia.
2. Hayatamfaa mali yake, wala alivyovichuma.
3. Atauingia Moto wenye mwako.
4. Na mkewe, mchukuzi wa kuni.
5. Shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa.

Sababu ya Kushuka Sura na Upingaji wa Abu Lahb kwa Mtume ﷺ.

Ampokea Bukhari kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ alitoka kwenda Al-Batha akapanda juu ya jabali akaita kwa kusema;

«يَا صَبَّاحَاهُ»

“Ee, kumekucha.”

¹ This is known also as Surat Al-Masad

Wakakusanyika kwake makuraishi. Akawaambia;

«أَرَأَيْتُمْ إِنْ حَدَّثْتُمْ أَنَّ الْعَدُوَّ مُصَبِّحُكُمْ، أَوْ مُمْسِكُكُمْ أَكُنْتُمْ تُصَدِّقُونِي؟»

“Jee mnaonaje iwapo nitawaeleza kwamba adui atawajieni asubuhi, au atawajieni jioni, Jee mtakuwa ni wenye kunisadikisha?”

Wakasema; “Ndiyo.” Akasema,

«فَإِنِّي نَذِيرٌ لَكُمْ بَيْنَ يَدَيْ عَذَابٍ شَدِيدٍ»

“Hakika mimi ni mkhofishaji kwenu kuhusu adhabu kali.”

Akasema Abu Lahabi; “Kwa ajili ya hili umetukusanya? Kuangamia ni kwako.” Akateremsha Allah تعالى،

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ

“Imeangamia mikono ya Abu Lahab, na yeye pia ameangamia.”

Mpaka mwisho wa sura.¹ Na katika mapokezi mengine, akasimama na hali anaipukusa mikono yake na huku anasema; “Maangamivu ni yako siku zote, ni kwa ajili ya hili umetukusanya?” Akateremsha Allah تعالى،

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ

“Imeangamia mikono ya Abu Lahab, na yeye pia ameangamia.”

Yale maangamivu ya kwanza ni maapizo kwake na maangamivu ya pili ni taarifa juu ya kuangamia kwake. Abu Lahab huyu ni mmoja wa Ami zake Mtume ﷺ na jina lake ni Abdul-Uzza bin Abdul-Muttwalib na lakabu yake ni Abu ‘Utaybah, na aliitwa kwa jina la Abu Lahab kutokana na kuangaza kwa uso na alikuwa mwingi wa maudhi kwa Mtume ﷺ na kumbughudhi, kumdharau na kumfanya duni yeye na Dini yake.

Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Az-Zinad amesema; “alinieleza mtu mmoja ambaye anaitwa Rabia bin ‘Abbad katika Bani Al-Diil na alikuwa kafiri akasilimu, amesema; “Nilimuona Mtume ﷺ wakati wa Jahiliya (kabla ya Uislamu) katika soko la Dhi Al-Majazi na hali ya kuwa anasema;

¹ Fat’h Al-Bari 8:609.

«بَا أَيُّهَا النَّاسُ، قُولُوا: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ تَتْلِحُوا»

“Enyi watu semeni hapana Mola Apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, mtafaulu.”

Na hali ya kuwa watu wamekusanyika kwake, na hali ya kuwa nyuma yake kuna mtu ambaye uso wake unang’aa mwenye makengeza ana misokoto miwili ya nywele na hali ya kuwa anasema; “Huyo ni muongo ameacha dini yake.” Alikuwa anamfuata popote anapokwenda. Nikauliza kuhusu mtu huyo wakasema; “Huyu ni Ammi yake Abu Lahb.”¹ Maelezo haya yamepokewa kutoka kwa Suraiji, kutoka kwa Ibn Abu Az-Zunad kutoka kwa baba yake ameyataja haya amesema Abu Az-Zunad; “Nilisema kumuambia Rabia kuwa wakati huo nilikuwa mdogo.’ Rabia naye akasema; “Ama mimi naapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa wakati huo nilikuwa naelewa mambo, nilikuwa ninabeba kiriba cha maji.”² Ahmad amepokea peke yake Hadithi hii. Na Kauli Yake Allah تعالى،

مَا أَعْطَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ ﴿١١١﴾

“Hayatamfaa mali yake, wala alivyovichuma.”

Amesema Ibnu Abbas رضي الله عنهما na wengine,

﴿١١١﴾ وَمَا كَسَبَ ﴿١١١﴾

“Wala alivyovichuma.”

Anawakusudia watoto wake.³ Imepokewa hivyo hivyo kutoka kwa Aisha رضي الله عنها, Mujahid, ‘Atwaa, Al-Hassani na Ibn Sirrin.⁴

Na kumetajwa kutoka kwa Ibnu Mas’ud رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ wakati alipowataka watu wake waingie kwenye imani alisema Abu Lahabi: ‘Yakiwa yale aliyosema mtoto wa ndugu yangu ni kweli hakika mimi nitaikomboa nafsi yangu siku ya kiyama kutokana na adhabu yenye kuumiza kwa mali yangu na watoto wangu.” Akateremsha Allah تعالى،

¹ Ahmad 4:341.

² Ahmad 4:341.

³ At-Tabari 24:677.

⁴ At-Tabari 24:677.

مَا أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ ۖ

“Hayatamfaa mali yake, wala alivyovichuma.”

Na Kauli Yake Allah تعالى،

سَيَصِلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ۖ

“Ataungia Moto wenye mwako.”

Maana yake: Wenye miali na cheche za kuunguza sana.

Kutajwa kwa Hatima ya Ummu Jamil Mke wa Abu Lahb

وَأَمْرًا تُهْرَحْمَالَةَ ۖ

“Na mkewe, mchukuzi wa kuni.”

Lakabu ya mke wake lilikuwa ni Ummu Jamil katika mabibi wa Kikuraishi, na jina lake lilikuwa ni Arwaa bint Harb bin Umayya, naye ni dada wa Abu Sufyani na alikuwa na msaada mkubwa kwa mume wake katika ukafiri wake, kukanusha kwake na kupinga kwake. Kwa sababu hiyo atakuwa siku ya kiyama ni msaada juu yake katika kuadhibiwa kwake katika moto wa jahanam. Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى،

حَمَّالَةَ ٱلْحَطَبِ ۖ فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍ ۖ

“...mchukuzi wa kuni. Shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa.”

Anakusudia anachukua kuni na anatupa kwa mume wake ili azidi juu ya ile hali ambayo yuko juu yake. Na yeye ametayarishwa kwa ajili hiyo.

فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍ ۖ

“Shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa.”

Na yeye Mwenyewe amejiandaa kwa hilo. Amesema Mujahid na Urwaa, katika usumba wa moto.¹

¹ Ad-Durr Manthur 8:667.

Amesema Al-Awfi kutoka kwa Ibnu Abbas, 'Atwiyya al-Jadaly, adh-Dhahak na Ibnu Zaid: "Alikuwa anaweka miba katika njia ya Mtume ﷺ." Amesema Al-Jawhar: *Al-Masad*: ni ndifu, usumba. Na *Al-Masad* vile vile: "ni kamba ya ndifu, usumba au pongoo na huwa kutokana na ngozi ya ngamia au manyoya yake." Na amesema Mujahid,

فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍ ﴿١﴾

"Shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa."

Maana yake: kongwa la chuma. Hivi huoni kuwa waarabu wanaita ringi kwa jina la *Masad*?¹

Kisa cha Maudhi ya Mke wa Abu Lahab kwa Mtume ﷺ.

Amesema Ibnu Abu Hatim رحمه الله تعالى: ametuzungumzia baba yangu na Abu Zar'a wamesema: ametuzungumzia Abdallah bin Zubair Humaid, ametuzungumzia Sufyani, ametuzungumzia Walid Ibnu Kathiir kutoka kwa Ibn Tadrus kutoka kwa Asmaa bint Abubakri رضي الله عنها amesema: iliposhuka

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ

"Imeangamia mikono ya Abu Lahab..."

Alikuja mwenye chongo, Ummu Jamil bint Harb, na hali ya kuwa anapiga kelele na mkononi mwake kuna jiwe na hali ya kuwa anasema, 'Mwenye kusifiwa kwa ubaya tumemkataa, na dini yake tumeichukia na amri yake tumeiasi.'

Aliyasema hayo na hali ya kuwa Mtume ﷺ amekaa msikitini. Pamoja naye, Abubakri رضي الله عنه, pindi Abubakri رضي الله عنه alipomuona Ummu Jamiil alimuambia Mtume ﷺ: "Ee Mtume kwa hakika amekuja na ninaogopea juu yako kuwa atakuona." Akasema Mtume ﷺ,

«إِنَّهَا لَن تَرَانِي»

"Hakika yeye hataniona."

Akasoma Qur'an akajikinga kwayo. Kama Alivyosema Allah تعالى:

¹ At-Twabari 24:681.

وَإِذَا قُرَأْتَ الْقُرْآنَ جَعَلْنَا بَيْنَكَ وَبَيْنَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ حِجَابًا مَّسْتُورًا ﴿١٧﴾

“Na unapo soma Qur’ani Tunaweka baina yako na wale wasioiamini Akhera pazia linalowafunika.” (17:45)

Akaja mpaka akasimama kwa Abubakar رضي الله عنه na hakuweza kumuona Mtume ﷺ. Ummu Jamil akamuambia Abubakar رضي الله عنه: “Ee Abubakar hakika mimi nimepewa habari kwamba swahiba wako amenitukana.” Abubakar رضي الله عنه akajibu kwa kusema, ‘Hapana naapa kwa Bwana wa Al-Ka’aba hakukutukana.” Akaenda zake hali ya kuwa anasema, “Wamekwishajua Makuraishi kwamba mimi ni binti wa bwana wao.”

Amesema Al-Waliid katika mazungumzo yake au mtu mwingine, akajikwaa Ummu Jamil alipokuwa akitufu katika Al-Ka’aba. Akasema: “Ameangamia mwenye kusifiwa kwa ubaya.” Akasema Ummu Hakiim binti Abdul Mutwalib: “Hakika mimi ni mwanamke mwenye kujichunga na mambo maovu kwa hiyo sizungumzi, na ni mwerevu sina haja ya kufundishwa na sote ni katika watoto wa Ami mmoja. Na Makuraishi baada ya yote hayo wanaelewa.”¹

Huu ndio mwisho wa sura hii.

* * *

¹ Fat’hul Al-Bari 8:610.

Tafsiri ya Suratu Ikhlas

Sura ya 112

Iliteremshwa Makkah

Kutajwa Sababu ya Kushuka Kwake na Ubora Wake

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Ubay bin Ka'ab رضى الله عنه kuwa washirikina walimuambia Mtume ﷺ; "Tueleze nasaba ya Bwana Wako." Allah تعالى Akateremsha,

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ۝ اللَّهُ الصَّمَدُ ۝ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ۝ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا

أَحَدٌ ۝

1. Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni Mmoja.

2. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa.

3. Hakuzaa wala Hakuzaliwa.

4. Wala Hana anayelingana Naye kwa utukufu hata mmoja.¹

Na kama hivyo amepokea Tirmidhi. Na Ibnu Jarir رحمه الله تعالى na Tirmidhi wameongeza kwa kusema,

الصَّمَدُ ۝

"Asswamad" Ambaye Hakuzaa wala Hakuzaliwa, kwa sababu kinachozaliwa hufa na hapana kitakacho kufa isipokuwa kitarithiwa na hakika Allah تعالى Mwenye Kushinda na Kutukuka Hafi na Harithiwi.

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ ۝

"Wala hana anayefanana Naye hata mmoja."

Hakuna anayefanana Naye wala anayelingana Naye, na Hakuwa mfano wa kitu chochote.² Ameyapokea hayo Ibn Abi Hatim na Tirmidhi, wameitaja hali ya kuwa Hadithi hii ni *Mursal*. Kisha amesema Tirmidhi Hadithi hii ni sahihi zaidi.³

¹ Ahmad 5:133.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:299 na At-Tabari 24:691.

³ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:301.

Hadithi Nyingine katika Ubora Wake

Amepokea Bukhari kutoka kwa Amra binti Abdul Rahman aliyekuwa katika ulezi wa Aisha رضي الله عنها, mke wa Mtume ﷺ, kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kwamba Mtume ﷺ alimpeleka mtu akiwa kiongozi wa kikosi cha vita na alikuwa anawasomea wenzake katika Sala zao na anamalizia kwa,

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾

“**Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa Pekee.**” Waliporejea walilipeleka jambo hilo kwa Mtume ﷺ akasema,

«سَلُّوهُ لِأَيِّ شَيْءٍ يَضَعُ ذَلِكَ؟»

“Muulizeni kwa nini alifanya hivyo.” Wakamuuliza naye akawajibu, “Kwa sababu sura hiyo ni Sifa ya Allah تعالى na mimi ninapenda kuisoma.” Akasema Mtume ﷺ,

«أَخْبِرُوهُ أَنَّ اللَّهَ تَعَالَى يُحِبُّهُ»

“Mpeni habari kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu Anampenda.”

Hivi ndivyo ilivyopokelewa katika kitabu, ‘At-Tawhiid.’¹ Na amepokea Muslim na An-Nasai vile vile.²

Hadithi nyingine ameipokea Bukhari katika kitabu *Asswalat* kutoka kwa Anas رضي الله عنه kuwa mtu mmoja katika Answare alikuwa anasalisha katika msikiti wa Qubaa akawa kila anapoianza sura ambayo anawasomea katika Sala huanza kwa, “**Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa Pekee.**” mpaka aimalize.

Kisha alikuwa anasoma sura nyingine pamoja nayo na alikuwa anafanya hivyo katika kila rakaa, wenzake wakamsemesha juu ya hilo wakamuambia, “Hakika wewe unaanza kwa sura hii kisha unaona kuwa haikutoshi mpaka usome sura nyingine, ama uisome hiyo peke yake na ama uiache na usome nyingine.”

Akasema, “Sikuwa mvivu mwenye kuiacha. Mkipenda niwe Imamu wenu kwa utaratibu huo nitafanya na mkichukia nitaacha kuwa Imamu wenu.” Walikuwa wanamuona kuwa yeye ni mbora wao na walichukia kuwepo kwa Imamu mwingine. Walipomfikia Mtume ﷺ walimueleza habari ile kisha akamuuliza yule bwana,

¹ *Fat’hul Al-Bari* 13:360.

² Muslim 1:558 na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:177.

«يَا فُلَانُ، مَا يَمْنَعُكَ أَنْ تَفْعَلَ مَا يَأْمُرُكَ بِهِ أَصْحَابُكَ، وَمَا حَمَلَكَ عَلَى لُزُومِ هَذِهِ السُّورَةِ فِي كُلِّ رَكْعَةٍ؟»

“Ee Fulani ni jambo gani linalokuzuia kufanya vile wanavyokuamrisha wenzako? Ni jambo gani lilokufanya ushikamane na sura hii katika kila raka?”

Bwana yule akasema; “Hakika mimi ninaipenda sura hii.” Akasema;

«حُبُّكَ إِنَّمَا أَذْخَلَكَ الْجَنَّةَ»

“Kuipenda kwako sura hii kunakuingiza peponi.”

Kama hivyo ameipokea Bukhari na akaifanya kuwa ni ‘*Mu’alaq*’ kwa kuainisha ‘*Majzuum*’.¹

Hadithi kuwa Sura Hii Inalingana na Thuluthi ya Qur’ani

Amepokea Bukhari kutoka kwa Abu Said رضي الله عنه kuwa mtu mmoja alimsikia mtu anasoma;

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ

“Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa Pekee.”

Hali ya kuwa anairudia rudia, alipopambazukiwa alikwenda kwa Mtume ﷺ na akalitaja hilo kwa Mtume ﷺ kana kwamba yule mtu aliona sura hiyo ni ndogo sana. Akasema Mtume ﷺ,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ إِنَّهَا لَتَتَدَبَّرُ ثُمَّ الْقُرْآنَ»

“Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu imo katika Uwezo Wake, hakika sura hii inalingana na theluthi ya Qur’ani.”²

Ameipokea Hadithi hii Abu Dawuud na Nasai³

Hadithi nyingine ameipokea Bukhari kutoka kwa Abu Said رضي الله عنه kuwa amesema, Mtume ﷺ amesema kuwaambia Masahaba wake,

¹ *Fat’hul Al-Bari* 2:298.

² *Fat’hul Al-Bari*:8:676.

³ Abu Dawuud 2:152 na An-Nasai katika *Al-Kubra* 5:16.

«أَيَعْجِزُ أَحَدُكُمْ أَنْ يَتْرَأَ تِلْكَ الْقُرْآنِ فِي لَيْلَةٍ؟»

"Hivi anashindwa mmoja wenu kusoma theluthi ya Qur'ani katika usiku mmoja?"

Likawa gumu hilo juu yao. Wakauliza: "Ni nani kati yetu anaweza hilo?" Mtume ﷺ akasema:

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ۝ اللَّهُ الصَّمَدُ ۝ تِلْكَ الْقُرْآنِ ۝

*"Qul Huwa Ilahu Ahad, Allaahu Sswamadu." Ni theluthi ya Qur'ani."*¹

Ameipokea Bukhari peke yake.

Hadithi Nyingine: Katika Kuisoma Sura Hii Kunawajibisha Pepo

Ameipokea Imamu Malik bin Anas kutoka kwa Ubaid bin Hunain amesema: "Nimemsikia Abu Hurairah رضى الله عنه akisema, "Nilikuja pamoja na Mtume ﷺ akamsikia mtu anasoma, "Qul Huwa Ilahu Ahad." Mtume ﷺ akasema,

«وَجَبَتْ»

"Imepasa." Nikamuuliza, "Ni kitu gani ambacho kimepasa?" Akanijibu,

«الْجَنَّةُ»

*"Pepo."*²

Na ameipokea Tirmidhi na Nasai katika Hadithi ya Malik amesema Tirmidhi Hadithi hii ni *Hasani Sahihi Gharibu* hatuijui isipokuwa katika Hadithi ya Malik³ na imetangulia hadithi isemayo:

«حُبُّكَ إِيَّاهَا أَدْخَلَكَ الْجَنَّةَ»

"Kuipenda kwako sura hii kumekuingiza peponi."

Na tayari imekwishabainishwa huko nyuma.⁴

¹ Fat'hul Al-Bari 8:676.

² Al-Muwattwa 1:208.

³ Tuhfat Al-Ahwadhi 8:209 na An-Nasai katika Al-Kubra 6:177.

⁴ Fat'hul Al-Bari 2:298.

Hadithi Nyingine katika Kukariri Kusomo Kwake

Amepokea Abdillahi bin Imamu Ahmad kutoka kwa Muadhi bin Abdillahi bin Khubaib kutoka kwa baba yake kuwa amesema: “Tulipatwa na kiza. Tukamngojea Mtume ﷺ. Akasali nasi akatoka akaukamata mkono wangu akaniambia,

قُلْ

“*Qul*” Nikanyamaza. Akasema,

قُلْ

“*Qul*” Nikasema, “Niseme nini?” Akasema,

﴿قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ وَالْمَعْرُودَتَيْنِ جِبْنَ نُنْمِي وَجِبْنَ نُضْبِحُ ثَلَاثًا، تَكْفِكَ كُلَّ يَوْمٍ مَرَّتَيْنِ﴾

“*Qul Huwa Ilahu Ahad.*” na *Muawidhatayn*, “*Surat Nnasi na Surat Al-falaq.*” Wakati wa jioni na jua linapokupambazukia mara tatu. Itakutosha kila siku mara mbili.”¹

Ameipokea Hadithi hii pia Abu Dawuud, Tirmidhi na Nasai. Amesema Tirmidhi hii ni *Hasani Sahihi Gharib*.² Ameipokea Nasai katika njia nyingine na tamko lake,

﴿يَكْفِكَ كُلَّ شَيْءٍ﴾

“Itakutosha kila kitu.”³

Hadithi Nyingine: Katika Maombi Ambayo Imekusanya Sura Hii katika Majina.

Amepokea Nasai wakati wa kuifasiri sura hii kutoka kwa Abdillahi bin Buraida kutoka kwa baba yake kwamba yeye aliingia pamoja na Mtume ﷺ msikitini. Ghafla mtu mmoja akawa anasali na huku anaomba akiwa anasema: “Ewe Mola Wangu wa haki hakika mimi ninakuomba kwa kuwa mimi ninashuhudia kuwa hapana Mola Apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe Uliye Mpweke Mwenye Kukuabudiwa katika mambo yote, Ambaye Hakuzaa wala

¹ Ahmad 5:312.

² Abuu Dawuud 5:320, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 10:28 na An-Nasai 8:250.

³ An-Nasai 8:251.

Hakuzaliwa na hakuna Kwake mwenye kufanana Naye yeyote.” Mtume ﷺ akasema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَقَدْ سَأَلَهُ بِاسْمِهِ الْأَعْظَمِ ، الَّذِي إِذَا سُئِلَ بِهِ أُعْطِيَ ، وَإِذَا دُعِيَ بِهِ أَجَابَ»

“Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu imo Mikononi Mwake kwa hakika amemuomba kwa Jina Lake Kubwa na Tukufu Ambalo Akiombwa Kwalo Hutoa na Akiitwa Kwalo Anaitika”¹

Wameithibitisha baki ya watu wa *sunnan*.² Na amesema Tirmidhi kwamba Hadithi hii ni *Hasani Gharib*.

Hadithi Nyingine katika Kutaka Kuponywa kwa Sura Tatu.

Amepokea Bukhari kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kwamba Mtume ﷺ alikuwa pindi anaposhuka kwenye tandiko lake kila usiku hokusanya vitanga vyake viwili kisha hupuliza katika vitanga hivyo na husoma katika vitanga hivyo, “*Qul-huwallahu ahad*” “*Qul-audhu Birabbil Falaq*” na “*Qul-audhu Birabbil nas*” kisha hupaka kwa vitanga hivyo sehemu atakayoiweza mwilini mwake. Huanza kwa vitanga viwili hivyo juu ya kichwa chake, uso wake na sehemu ya mbele ya mwili wake, hufanya hivyo mara tatu.”³ Na kama hivyo wamepokea watu wa *sunna*.⁴



¹ An-Nasai katika *Al-Kubra Tuhfat Al-Ashraaf* 2:90.

² Abu Dawuud 1493, At-Tirmidhi 3475 na Ibn Majah 3857.

³ *Fat'hul Al-Bari* 8:679.

⁴ Abu Dawuud 5:303, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:347, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:198 na Ibn Majah 2:1275.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

<p>سُورَةُ الْاِخْلَاصِ</p>
<p>بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ</p>
<p>قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ۝ اللَّهُ الصَّمَدُ ۝ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ۝ لَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ ۝</p>

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ۝ اللَّهُ الصَّمَدُ

۝ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ۝ وَلَمْ

يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ ۝

1. Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni mmoja.

2. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa.

3. Hakuzaa wala hakuzaliwa.

4. Wala Hana anayelingana Naye kwa utukufu hata mmoja.

Umetangulia utajo wa sababu ya kushuka kwake. Na amesema Ikrima waliposema mayahudi: “Sisi tunamuabudu Uzairi mtoto wa Allah تعالى,” wakasema Manaswara, ‘Sisi tanamuabudu Masihi mtoto wa Allah .” na wakasema Majusi: “Sisi tunaliabudia jua na mwezi”, na wakasema washirikina: “Sisi tunayaabudu masanamu.” Allah تعالى Akateremsha juu ya Mtume wake

ﷻ

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ۝

“Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni mmoja.”

Anakusudia, huyo Allah تعالى Ndiye Aliye Mmoja, Aliye Mpweke Hana mfano, Hana msaidizi, Hana mwenza na Hana aliyefanana Naye na wala anayelingana Naye. Na halitamki tamko hili yeyote katika kuthibitisha isipokuwa juu ya Allah تعالى Mwenye Kushinda na Kutukuka kwa sababu Yeye Ndiye Aliyekamilika sana katika Sifa Zake na Matendo Yake. Na Kauli Yake Allah تعالى:

اللَّهُ الصَّمَدُ ۝

“Mwenyezi Mungu Mkusudiwa.”

Amesema Ikrimah kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: “Anakusudia ambaye

wanakusudia Kwake viumbe katika mahitaji yao na maombi yao.” Amesema Ali bin Abu Twalha kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما: “Yeye Ndiye Bwana Ambaye Umekamilika Ubwana Wake, na Mtukufu Ambaye Amekamilika katika Utukufu Wake, na Mkubwa Ambaye Amekamilika katika Ukubwa Wake, na Mpole Ambaye Amekamilika katika Upole Wake, na Mjuzi Ambaye Amekamilika katika Elimu Yake. Na Yeye Ndiye Ambaye Amekamilika katika sifa zote za Utukufu na Ubwana. Naye ni Allah تعالى, Kutakasika ni Kwake na sifa za upungufu. Hizi ndizo Sifa Zake hapatakikani kusifiwa kwa sifa hizo mtu yeyote, hapana anayefanana Naye na hapana mfano Wake kitu chochote. Kutakasika ni Kwake Allah تعالى Aliye Mmoja Mwenye Kutenza nguvu.”¹ Amesema Al-‘Aamashi kutoka kwa Shaqiq kutoka kwa Abu Walid,

الصَّمَدُ

“Mwenyezi Mungu Mkusudiwa.”

Ni Bwana Ambaye Umefikia Ukomo Ubwana Wake.²

Mwenyezi Mungu Ametakasika na Ubaba, Utoto, Uswahiba na Ukufu

Na Kauli Yake Allah تعالى,

لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ۝ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ ۝

“Hakuzaa wala Hakuzaliwa. Wala Hana anayefanana Naye hata mmoja.”

Maana yake: Yeye Hana mtoto wala mzazi na Hana mke. Amesema Mujahid

وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ ۝

“Wala Hana anayelingana Naye kwa utukufu hata mmoja.”

Aya inakusudia kuwa Hana swahiba wake, na hii ni kama Alivyosema Allah تعالى,

¹ At-Tabari 24:692.

¹ At-Tabari 24:692.

بَدِيعُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَنَّى يَكُونُ لَهُ وَلَدٌ وَلَمْ تَكُنْ لَهُ صَاحِبَةٌ ۖ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ ۗ

“Yeye Ndiye Muumbaji wa mbingu na ardhi bila ya ruwaza. Itakuwaje Awe na mwana Naye hakuwa na mke? Naye Ndiye Aliyeumba kila kitu. Naye ni Mwenye Kujua kila kitu.” (6:101)

Maana yake: Yeye Ndiye Mwenye Kumiliki kila kitu na Aliyeviumba; sasa vipi Atakuwa katika viumbe Vyake anayefanana Naye, anayeshindana Naye au jamaa anayekaribiana Naye. Ametukuka, Ametakasika na Aameepukana na Sifa zenye upungufu. Allah تعالى Amesema,

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ۗ لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا إِدًّا ۝ تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْأَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا ۝ أَنْ دَعَوْا لِلرَّحْمَنِ وَلَدًا ۗ وَمَا يُبْنِي لِلرَّحْمَنِ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا ۗ ۝ إِنَّ كُلُّ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتَى الرَّحْمَنِ عَبْدًا ۗ لَقَدْ أَحْصَاهُمْ وَعَدَّهُمْ عَدًّا ۗ وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ۗ

“Na wao ati husema kuwa (Arrahmani) Mwingi wa Rehema ana mwana! Hakika mmeleta jambo la kuchusha mno! Zinakaribia mbingu kutatuka kwa hilo, na ardhi kupasuka, na milima kuanguka vipande vipande. Kwa kudai kwao kuwa (Arrahmani) Mwingi wa Rehema ana mwana. Wala hahitajii (Arrahmani) Mwingi wa Rehema kuwa na mwana. Hapana yeyote aliomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa (Arrahmani) Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa Wake. Yeye hakika Amewadhibiti na Amewahisabu sawa sawa. Na kila mmoja katika wao atamfikia Siku ya Kiyama peke yake.” (19:88-95)

Na Allah تعالى Amesema,

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ بَلْ عِبَادٌ مُّكْرَمُونَ ۗ ۝ لَا يَسْبِقُونَهُ ۗ بِالْقَوْلِ ۗ وَهُمْ بِأَمْرِهِ يَعْمَلُونَ ۗ

“Na wanasema: Arrahman, Mwingi wa Rehema, ana mwana!

Subhanahu, Ametakasika na hayo! Bali hao (wanao waita wana) ni watumwa waliotukuzwa. Hawamtangulii kwa neno, nao wanafanya amri Zake.” (21:26-27)

Na tena Allah تعالى Akasema,

وَجَعَلُوا بَيْنَهُ وَبَيْنَ الْجَنَّةِ نَسَبًا ۗ وَلَقَدْ عَلِمَتِ الْجِنَّةُ إِنَّهُمْ لَمُحْضَرُونَ ﴿٣٧﴾ سُبْحَانَ اللَّهِ
عَمَّا يَصِفُونَ ﴿٣٨﴾

“Na wameweka makhusiano ya nasaba baina yake na majini; na majini wamekwisha jua bila ya shaka kuwa wao watahu dhurishwa.” (37:158-159)

Na imepokewa katika sahihi ya Bukhari

«لَا أَحَدٌ أَضْبِرُ عَلَىٰ أَدَىٰ سَمْعِهِ مِنَ اللَّهِ، يَجْعَلُونَ لَهُ وَلَدًا، وَهُوَ يَرْزُقُهُمْ وَيَعَايِهِمْ»

“Hapana yeyote mwenye subira sana juu ya maudhi ambayo ameyasikia kuliko Allah تعالى, wanamzushia eti ana mtoto na hali Yeye Anawapa riziki na Anawaondolea matatizo yao.”¹

Na amepokea Bukhari kutoka kwa Abu Hurairah رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ amesema,

«قَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: كَذَّبَنِي ابْنُ آدَمَ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ ذَلِكَ، وَسَمَّعَنِي وَلَمْ يَكُنْ لَهُ ذَلِكَ، فَأَمَّا تَكْذِيبُهُ إِيَّايَ فَقَوْلُهُ: لَنْ يُعِيدَنِي كَمَا بَدَأَنِي، وَلَيْسَ أَوَّلُ الْخَلْقِ بِأَهْوَنَ عَلَيَّ مِنْ إِعَادَتِهِ، وَأَمَّا سَمُّهُ إِيَّايَ فَقَوْلُهُ: اتَّخَذَ اللَّهُ وَلَدًا، وَأَنَا الْأَحَدُ الصَّمَدُ، لَمْ أَلِدْ وَلَمْ أُولَدْ، وَلَمْ يَكُنْ لِي كُفْوًا أَحَدٌ»

“Amesema Mwenyezi Mungu, Mwenye Kushinda na Kutukuka, Amenikadhibisha mwanadamu na hana haki ya kufanya hivyo, na Amenitukana na hakuwa na haki ya kufanya hivyo. Ama Kunikadhibisha kwake Mimi ni kauli yake: ‘Hawezi kunirudisha kama Alivyonianzisha, na hali haikuwa Umbaji wake wa kwanza ni rahisi

¹ Fat’hul Al-Bari 13:372.

*kuliko kumrejeshā alivyokuwa. Ama kunitukana ni kauli yake,
'Mwenyezi Mungu ana mtoto. Na Mimi ni wa Pekee, Mkusudiwa,
Sikuzaliwa na wala Sikuzaa na wala Sikufanana na yeyote.'*¹

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya Suratu *Al-Ikhlās*. Na ni Kwake Allah تعالی tu Kusifiwa na Kuneemesha.



¹ *Fat'h Al-Bari* 8:611 na 612.

Tafsiri ya Sura Mbili Al-Mu'awwidhatayni Suratul Falaq na An-Nas Sura ya 113-114 Ziliteremshwa Madinah

Msimamo wa Ibni Masu'di رضي الله عنه Kuhusu *Al-Mu'awwidhatayni*

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Zirr bin Hubaishi amesema: Nilimuambia Ubay bin Ka'ab رضي الله عنه. Hakika Ibnu Masu'd رضي الله عنه haandiki *Al-Mu'awwidhatayn* katika msahafu wake, akasema: Ninashuhudia kwamba Mtume ﷺ alimueleza kwamba Jibril عليه السلام alimuambia: Sema:

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴿١﴾

“Sema: Najikinga kwa Mola Mlezi wa mapambazuko.” (113:1)

Nikasema, akasema:

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿١﴾

“Sema: Ninajikinga kwa Mola Mlezi wa wanaadamu.” (114:1)

Akasema, “Kwa hiyo sisi tunasema kama alivyosema Mtume ﷺ.”¹

Ubora wa Al-Mu'awwidhatayn

Amepokea Muslim katika sahihi yake kutoka kwa 'Uqba bin Aamir رضي الله عنه, amesema: Amesema Mtume ﷺ,

وَأَلَمْ تَرَ آيَاتِ أَنْزَلْتُ هَذِهِ اللَّيْلَةَ لَمْ يَرِ مِثْلُهُنَّ قَطُّ:

“Hivi hukuziona aya ambazo zimeteremshwa usiku huu sijaona mfano wao kabisa: Nazo ni:

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴿١﴾

“Qul-Audhu-Birabil Falaq.” (113:1) Na,

¹ Ahmad 5:129.

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿١﴾

“Qul-Audhu-Birabil Nasi.”(114:1)¹

Ameipokea Imamu Ahmad na Tirmidhi. Daraja ya Hadithi hii ni Hassan Sahihi.²

Njia nyengine

Ameipokea Imamu Ahmad kutoka kwa ‘Uqba bin Aamir رضي الله عنه amesema: Wakati mimi ninamuongoza Mtume ﷺ katika njia moja katika njia za majabalini, ghafla aliniambia,

«يَا عُقْبَةُ أَلَا تَرَكَبُ؟»

“Ee Uqba hivi hupandi?” Akasema, ‘nikaogopa yasije yakawa ni maasia – akasema: Mtume ﷺ akateremka nikapanda muda mfupi kisha akapanda. Kisha akasema:

«يَا عُقْبَةُ، أَلَا أَعْلَمُكَ سُورَتَيْنِ مِنْ خَيْرِ سُورَتَيْنِ قَرَأَ بِهِمَا النَّاسُ؟»

“Ee ‘Uqba nikufundishe sura mbili zilizo bora katika sura mbili ambazo wanazisoma watu.”

Nikasema: ‘Kwanini (usinifundishe)? Ewe Mtume ﷺ.” Akanisomea,

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴿١﴾

“Qul-Audhu-Birabbi-l-falaq.” na,

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿١﴾

“Qul-Audhu-Birabii-Nnasi.”

Kisha ikasimamishwa Sala na Mtume ﷺ akatangulia kusalisha kwa sura hizi na baada ya Sala akaniuliza,

«كَيْفَ رَأَيْتَ يَا عُقْبَةُ، أَفَرَأَى بِهِمَا كُلَّمَا نَسْتُ وَكُلَّمَا قُمْتُ»

“Unaonaje Ewe Uqba kuwa unazisoma sura hizo kila unapolala na kila unaposimama.”³ Ameipokea An-Nasai na Abu Dawud.⁴

¹ Muslim 1:558.

² Ahmad 4:144, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:303 na An-Nasaai 8:254.

³ Ahmad 4:144.

⁴ Abu Dawuud 2:152 na An-Nasaai 8:253, 203.

Njia nyengine

Amepokea An-Nasai kutoka kwa Uqba bin 'Aamir رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ النَّاسَ لَمْ يَتَعَوَّدُوا بِمِثْلِ هَذَيْنِ:

"Hakika watu hawajajilinda kwa mfano wa sura mbili hizi:

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴿١﴾

"Qul-Audhu-Birabbi-Ifalaq." (113:1) na

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿٢﴾

"Qul-Audhu-Birabbi-Nasi." (114:1)¹

Njia nyengine

Amepokea An-Nasai kutoka kwa Uqba bin Aamir رضي الله عنه amesema: Nilikuwa ninakwenda pamoja na Mtume ﷺ akasema:

«يَا عُقَيْبَةُ قُلْ»

"Ee Uqba-sema." Nikasema, 'Kitu gani niseme?' Akaninyamazia kisha akasema,

قُلْ

"Sema." Nikasema: 'Niseme nini Ee Mtume ﷺ.' Akasema:

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴿١﴾

"Qul-Audhu-Birabbi-I-Falaq." (113:1)

Nikaisoma mpaka nikafika mwisho wake, kisha akasema:

قُلْ

"Sema." Nikasema, 'Niseme nini? Ee Mtume?' Akasema:

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿٢﴾

"Qul-Audhu-Birrabbi-Nasi" (114:1)

¹ Al-Kunaa ya Ad-Dawlaan 1:106.

Nikaisoma mpaka nikafika mwisho wake, kisha akasema Mtume ﷺ wakati huo,

«مَا سَأَلَ سَائِلٌ بِمِثْلِهَا، وَلَا اسْتَعَاذَ مُسْتَعِيزٌ بِمِثْلِهَا»

“Hajaombapo muombaji yeyote kwa mfano wa sura hiyo na hakujilinda mwenye kujilinda yoyote hifadhi yeyote kwa mfano wake.”¹

Hadithi nyengine

Amepokea An-Nasai kutoka kwa Ibnu Aabisi-al-Juhani رضى الله عنه kwamba Mtume ﷺ alimuambia,

«يَا ابْنَ عَابِسٍ أَلَا أَدُلُّكَ - أَوْ أَلَا أُخْبِرُكَ - بِأَفْضَلِ مَا يَتَعَوَّذُ بِهِ الْمُتَعَوِّذُونَ؟»

“Ewe Ibnu Aabisi – hivi nisikufahamishe au hivi nisikueleze kitu bora zaidi ambacho wanajilinda nacho wenye kujilinda.”

Akasema: ‘Nijulishe Ee Mjumbe wa Allah.’ Mtume ﷺ akasema: ‘sema’

«قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ» وَ«قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ» هَاتَانِ السُّورَتَانِ»

“Qul-Audhu-Birabbi-I-Falaq” na “Qul-Audhu-Birabil Nnasi” hizi sura mbili.²

Na amepokea Imamu Malik kutoka kwa Aisha رضى الله عنها kwamba Mtume ﷺ alikuwa anapoumwa hujisomea *Al-Mu’awwidhatayn* na hujipulizia na yalipozidi maumivu yake nilikuwa ninamsomea *Mu’awwidhatayn* na ninafuta kwa mkono wake juu yake kwa kutaraji baraka yake.³ Na ameipokea Bukhari na Abu Dawud na an- Nasai, na Ibni Majah.⁴

Na imepokewa kutoka kwa Abi Said رضى الله عنه kwamba Mtume ﷺ alikuwa anajilinda kutokana na macho ya majini na macho ya watu. Ziliposhuka hizi Sura mbili (*Al-Muawwidhatayn*) alishikamana nazo na akaziacha zisizokuwa hizo. Ameipokea Tirmidhi, Ibn Majah, na An-Nasai. Na amesema At-Tirmidhi kuwa hadithi hii ni Hassan Sahihi.⁵

¹ An-Nasaai 8:253.

² An-Nasaai 8:251.

³ Al-Muwatwa 2:942.

⁴ *Fat’h Al-Bari* 8:679, Muslim 4:1723, Abu Dawud 4:220, An-Nasaai katika *Al-Kubra* 4:867 na 367 na Ibn Majah 2:1166.

⁵ At-Tabari 24:700.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْفَلَقِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴿١﴾ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ ﴿٢﴾ وَمِنْ شَرِّ
عَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ﴿٣﴾ وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ ﴿٤﴾
وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ﴿٥﴾

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴿١﴾ مِنْ شَرِّ مَا

خَلَقَ ﴿٢﴾ وَمِنْ شَرِّ عَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ

﴿٣﴾ وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ

﴿٤﴾ وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ﴿٥﴾

1. Sema: Najikinga kwa Mola Mlezi wa mapambazuko.

2. Na shari ya Alivyoviumba,

3. Na shari ya giza la usiku liingiapo.

4. Na shari ya wanaopulizia mafundoni.

5. Na shari ya hasidi anapo husudu.

Amepokea Ibnu Abi Hatim رحمه الله تعالى, kutoka kwa Jabir رضي الله عنه amesema: "Al-Falaq" Ni asubuhi.¹ Na amesema al-Awfi kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما kuwa maana ya "Al-Falaq" ni asubuhi.² Na imepokewa kutoka kwa Mujahid, Said bin Jubair, Abdillah bin Muhammad bin Uqayl, Hassan, Qatadah, Muhammad bin Kaab Quradhy, Ibnu Zayd na Malik kutoka kwa Zayd bin Aslam mfano wa hayo.³ Amesema Al-Quradhy, Ibnu Zaid, na Ibnu Jarir nayo ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

فَالِقِ الْإِصْبَاحِ

"Ndiye Anayepambazua mwangaza wa asubuhi..." (6:96)²

Na Kauli Yake Allah تعالى,

¹ At-Tabari 24:701.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:218, An-Nasaai 8:271 na Ibn Majah 2:1161.

³ At-Tabari 24:700, 701.

مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ ﴿١﴾

“Na shari ya Alivyoviumba.”

Maana yake: Na shari ya viumbe wote. Na amesema Thabiti Al-Banani na Hassan Al-Basry رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, kuwa maana yake ni Jahanamu na Ibilisi na watoto wake ni katika Alivyoviumba.

وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ﴿٢﴾

“Na shari ya giza la usiku liingiapo.”

Amesema Mujahid: Kiza cha usiku kitakapofunga ni kuzama kwa jua. Ameyapokea hayo Bukhari kutokana naye.¹ Na kama hivyo amepokea Ibnu Abi Najihi kutokana naye.

Na kama hivyo amesema Ibnu Abbas, Muhammad bin Ka'ab al-Quradhy, Adh-Dhahak, Khuswaifi, Hassan na Qatadah رَضِيَ اللهُ عَنْهُمْ kwamba huo ni usiku utakapokuja na kiza chake.² Az-Zuhury رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى Amesema :

وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ﴿٣﴾

“Na shari ya giza la usiku liingiapo.”

Jua litakapozama. Amesema Abu-Mahzam kutoka kwa Abu Huraira رَضِيَ اللهُ عَنْهُ,

وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ﴿٤﴾

“Na shari ya giza la usiku liingiapo.”

Kuwa maana yake ni nyota.³ Amesema Ibnu Zaid Waarabu walikuwa wanasema: “Al-Ghasiqu” ni kuanguka kwa nyota za Thurayya na amesema na yalikuwa maradhi na ugonjwa wa Tauni, kukithiri wakati wa kuanguka kwa nyota hiyo, na yanaondoka wakati wa kuchomoza kwake.⁴

Amesema Ibnu Jarir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى na wamesema wengine kuwa huo ni mwezi. Mimi nasema, ‘Na mategemeo ya kauli hii ni yale aliyoyapokea Imamu Ahmad

¹ Fat’hul Al-Bari 8:613.

² At-Tabari 12:748, 749.

³ At-Tabari 12:149.

⁴ At-Tabari 12:149.

kutoka kwa Harithi bin Abi Salama amesema: Amesema Aisha رضي الله عنها, "Mtume ﷺ aliukamata mkono wangu, akanionesha Mwezi wakati kulipochomoza akasema:

«تَعَوَّذِي بِاللَّهِ مِنْ شَرِّ هَذَا الْعَاسِي إِذَا وَقَبَ»

*"Jilinde kwa Allah تعالى na shari ya huu usiku pindi unapofunga kiza."*¹

Na ameipokea Tirmidhi na Nasai katika vitabu vya tafsiri katika Sunani zao.² Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ ﴿٦﴾

"Na shari ya wanaopulizia mafundoni."

Amesema Mujahid na Ikrima na Hasan na Qatadah na adh-Dhahak anakusudia, 'wachawi.'³ Amesema Mujahid watakapozingua na wakapulizia katika mafundo. Na katika Hadithi nyengine Malaika Jibril عليه السلام alikuja kwa Mtume ﷺ akasema: 'Umeumwa Ee Muhammad, akasema,

«نَعَمْ»

"Ndiyo"

Akasema "Kwa Jina la Allah تعالى ninakuinga kwa kila ugonjwa unaokuudhi na kutokana na shari ya kila mwenye husuda na mwenye jicho baya, Allah تعالى Atakuponya."⁴

Kuweka Wazi Kurogwa kwa Mtume ﷺ

Amepokea Bukhari katika kitabu cha *At-Twib* katika sahihi yake kutoka kwa Aisha رضي الله عنها amesema: 'Alikuwa Mtume ﷺ amerogwa kiasi cha kuwa anaona kuwa anawaendea wanawake na wala hawaendei.' Akasema Sufiyani kuwa, 'huu ndio uchawi mkali zaidi.' Alipokuwa hivi akasema,

¹ Ahmad 6:61.

² At-Tirmidhi 3366.

³ At-Twabari:12:750 na 751.

⁴ Muslim 21:86.

«يَا عَائِشَةُ، أَعْلِمْتِ أَنْ اللَّهَ قَدْ أَفْتَانِي فِيمَا اسْتَفْتَيْتُهُ فِيهِ؟ أَتَانِي رَجُلَانِ قَعَدَا أَحَدُهُمَا عِنْدَ رَأْسِي وَالْآخَرُ عِنْدَ رِجْلِي، فَقَالَ الَّذِي عِنْدَ رَأْسِي لِلْآخَرِ: مَا بَالَ الرَّجُلِ؟ قَالَ: مَطْبُوبٌ، قَالَ: وَمَنْ طَبَّهُ، قَالَ: لَيْدُ بْنُ أَعْصَمٍ: رَجُلٌ مِنْ بَنِي زُرَيْقٍ حَلِيفٌ لِيَهُودَ، كَانَ مُتَافِقًا، قَالَ: وَفِيمَ؟ قَالَ: فِي مُشْطٍ وَمُشَاطَةٍ، قَالَ: وَأَيْنَ؟ قَالَ: فِي جُفِّ طَلْعَةِ ذَكَرٍ، تَحْتَ رَاغُوفَةٍ فِي بَيْتِ ذَرَوَانَ»

“Ee Aisha: Jee unajua kwamba Mwenyezi Mungu, Amenijibu lile nililomuuliza: wamenijia watu wawili akakaa mmoja wao kichwani kwangu na mwengine mbele ya miguu yangu, akasema yule aliye kichwani kwangu, kumuambia yule mwengine, “Ana nini huyu mtu?” Akasema, “Amerogwa.” Akauliza, “Ni nani aliyemroga?” Akasema, “Labid bin Aaswam mtu mmoja katika Bani Zuraiq aliyepiana na Mayahudi kunusuriana, alikuwa mnafiki.” Akauliza katika kitu gani?” Akamjibu, “Katika shanuo na nywele zilizoanguka kutokana na kuchanwa.” Wa kwanza akasema, “(Kiko) wapi?” Wa pili akajibu, “Kwenye gome kavu la mtende dume chini ya Jiwe lililo katika kisima cha Dharwan.”

Akasema: Akakiendea kisima mpaka akalitoa akasema:

«هَذِهِ الْبُئْرُ الَّتِي أَرَبْتُهَا، وَكَأَنَّ مَاءَهَا تُفَاعَةُ الْجَنَاءِ، وَكَأَنَّ نَحْلَهَا رُؤُوسُ الشَّيَاطِينِ»

“Hiki ndicho kisima nilichooneshwa kana kwamba maji yake ni mbambiko wa hina na kana kwamba mtende wake ni vichwa vya mashetani.”

Amesema: “Akautoa.” Amesema: Nikasema: “Hivi kwanini hukujifanyia dawa?”

Akasema:

«أَمَّا اللَّهُ فَقَدْ شَفَانِي، وَأَكْرَهُ أَنْ أُبَيَّرَ عَلَى أَحَدٍ مِنَ النَّاسِ شَرًّا»

“Ama Mwenyezi Mungu Amekwisha kuniponya. Kwa hiyo ninachukia kueneza shari kwa yeyote katika watu.”¹

* * *

¹ Fat’hul Al-Bari 10:243.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

<p>سُورَةُ النَّاسِ</p> <p>بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ</p> <p>قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ مَلِكِ إِلَهِهِ النَّاسِ مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ الَّذِي يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ</p>
--

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ مَلِكِ
 النَّاسِ إِلَهِهِ النَّاسِ مِنْ
 شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ الَّذِي
 يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ
 مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ

1. Sema: *Ninajikinga kwa Bwana Mlezi wa wanaadamu,*
2. *Mfalme wa wanaadamu,*
3. *Mungu wa wanaadamu,*
4. *Na shari ya wasiwasi wa Shetani, mwenye kurudi nyuma,*
5. *Anayetia wasiwasi katika vifua vya watu,*
6. *Kutokana na majini na wanaadamu.*

Hizi ni sifa tatu katika sifa za Bwana, Mwenye Kushinda na Kutukuka: Ubwana. Ufalme na Uungu. Kwa hiyo yeye ni Bwana wa kila kitu na Mfalme Wake na Mola Wake. Basi vitu vyote ni viumbe Vyake, vimetenzwa nguvu na kudhalilishwa Kwake na ni watumwa Wake. Kwa hiyo Amemuamrisha mwenye kujilinda ajilinde, kwa Mwenye Kusifika na sifa hizi, kutokana na shari ya mwenye kutia wasiwasi, mwenye kurejea nyuma. Naye ni shetani mwenye kuwakilishwa kwa mwanadamu. Kwa sababu hapana mwanadamu yeyote miongoni mwa wanadamu isipokuwa ana rafiki anayempambia maovu, wala hapunguzi juhudi katika kumharibia. Na mwenye kukingwa ni yule aliyekingwa na Allah تعالی.

Na imethibitika katika Hadithi sahihi kwamba:

«مَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا قَدْ وُكِّلَ بِهِ قَرِينٌ»

“Kila mmoja katika nyinyi amesalitwa shetani anayemshawishi vibaya.”

Wakasema: ‘Na wewe Ewe Mtume ﷺ; Akasema:

«تَعَمُّ، إِلَّا أَنْ اللَّهَ أَعَانَنِي عَلَيْهِ فَأَسْلَمَ، فَلَا يَأْمُرُنِي إِلَّا بِخَيْرٍ»

“Ndiyo isipokuwa ni kwamba Mwenyezi Mungu Amenisaidia juu yake, amesilimu, kwa hiyo hanishawishi isipokuwa kheri.”¹

Na imethibiti katika sahihi ya Bukhari na Muslim kutoka kwa Anas رضي الله عنه katika kisa cha ziara ya Swafiyah رضي الله عنها kumzuru Mtume ﷺ akiwa amekaa Itikafu na alipotoka kumrudisha nyumbani kwake wakakutana na watu wawili katika Anwar, pindi walipomuona Mtume ﷺ walikaza mwendo. Mtume ﷺ akawaambia,

«عَلَى رَسَلِكُنَا، إِنَّهَا صَفِيَّةُ بِنْتُ حُيَيٍّ»

“Nendeni taratibu hakika huyu ni Swafiyah bint Huyay.”

Wakasema, ‘Subhaanallah, Ee Mtume ﷺ.’ Mtume ﷺ akawaambia,

«إِنَّ الشَّيْطَانَ يَجْرِي مِنْ ابْنِ آدَمَ مَجْرَى الدَّمِ، وَإِنِّي خَشِيتُ أَنْ يَفْدِفَ فِي قُلُوبِكُنَا شَيْئًا، أَوْ قَالَ: شَرًّا»

“Hakika shetani anapita kwa mwanadamu mapito ya damu na kwa hakika mimi nimeogopea kutia katika nyoyo zenu kitu au alisema kuingiza shari.”²

Na amesema Said bin Jubair رضي الله عنهما kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake:

«مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ ①»

“Wasiwasi wa Shetani, mwenye kurudi nyuma.”

Amesema shetani amekaa juu ya moyo wa mwanadamu pindi akisahau na akaghafilika anamtia wasiwasi na pindi akimtaja Allah تعالى hurudi nyuma.³

¹ Muslim 4:2167.

² Fat’hul Al-Bari 4:326.

³ At-Tabari 24:709. Isnadi yake ni dhaifu.

Na kama hivi amesema – Mujahid na Qatadah.¹

Na amesema Al-Muutamir bin Sulaiman, kutoka kwa Baba yake: Nimeambiwa kwamba shetani mwenye kutia wasiwasi hupulizia katika moyo wa mwanadamu wakati wa huzuni na wakati wa furaha. Pindi atakapomtaja Allah تعالی hurejea nyuma.² Amesema Au fi kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake Allah تعالی:

الْوَسْوَاسِ

“...Wasiwasi...”

Amesema: ‘Huyo ni shetani anaamrisha, anapotiiwa Allah تعالی hurejea nyuma.’³ Na Kauli Yake Allah تعالی:

الَّذِي يُوسِّسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ

“Anayetia wasiwasi katika vifua vya watu.”

Jee lina husika hilo na wanadamu tu kama linavyoonekana hilo katika aya? Au linawaenea wanadamu na majini? Ndani yake kuna kauli mbili: Watakuwa wameingia katika tamko la (watu) kwa kuwapa kipaumbele watu.

Ibnu Jarir رحمه الله تعالی amesema: ‘Limetumiwa kwao neno wanaume, katika majini hapana jambo la ajabu kutumiwa neno (watu) kwa hao majini.’⁴

Na Kauli Yake Allah تعالی:

مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ

“Kutokana na majini na wanaadamu.”

Ni ufafanuzi wa Kauli Yake:

الَّذِي يُوسِّسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ

“Anayetia wasiwasi katika vifua vya watu.”

Kisha Akaweka wazi kwa Kusema:

¹ At-Tabari 24:710.

² At-Tabari 24:710.

³ At-Tabari 24:710.

⁴ At-Tabari 24:711.

مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ﴿١﴾

“Kutokana na majini na wanaadamu.”

Maneno haya yanaipa nguvu kauli ya pili. Na ikasemwa: Kauli Yake:

مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ﴿٢﴾

“Kutokana na majini na wanaadamu.”

Ni tafsiri ya yule mwenye kutia wasiwasi katika nyoyo za watu katika mashetani wa watu na majini. Kama Alivyosema Allah تعالى،

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيْطَانِ الْإِنْسِ وَالْجِنِّ يُوحِي بَعْضُهُمْ إِلَى بَعْضٍ زُخْرَفَ
الْقَوْلِ غُرُورًا

“Na kadhaalika Tumemfanyia kila Nabii maadui mashetani wa kiwatu, na kijini, wakifundishana wao kwa wao maneno ya kupamba-pamba, kwa udanganyifu. Na Angelipenda Mola Wako Mlezi wasingelifanya hayo. Basi waache na wanayoyazua.”(6:112).

Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Ibnu Abbas رضي الله عنهما kuwa amesema: alikuja mtu mmoja kwa Mtume ﷺ akasema, ‘Ee Mtume! Hakika mimi huizungumzia nafsi yangu jambo, kwa hakika kuporomoka kutoka mbinguni kunapendeza sana kwangu kuliko yale ninayoizungumzia nafsi yangu.’ Akasema, Mtume ﷺ akasema,

«الله أكبر، الله أكبر الحمد لله الذي رد كيده إلى الوسوسة»

“Allahu Akbar. Allahu Akbar, Sifa Njema ni za Mwenyezi Mungu Ambaye Amekirudisha kitimbi chake kwenye wasiwasi”.¹

Na ameipokea Abu Dawuud na An-Nasai.²

Huu ni mwisho wa Tafsiri. Na Sifa Njema ni za Allah تعالى tu, na ni Mwenye Kuneemesha, Bwana wa Ulimwengu wote.

* * *

¹ Ahmad 1:235.

² Abu Dawud 5:336, na An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:171.